
# AFRIKA

# BARA LA WATAKATIFU

## MARTIROLOJIA YA WATAKATIFU WA AFRIKA




**Kitabu hiki kimetungwa na**
**Padri Etienne Sion, M.afr.**

Kipigo chapa cha Mtandao
2020
Juzuu la 3

Agape Publications
P.O.Box 76021 Dar-es-Salaam
Simu : + 255 767 342068
e-mail : kungwecentre@gmail.com
kungwecentre@outlook.com

**Septemba 1**

Huko Uswisi, Wakatoliki wanamkumbuka siku ya leo Mt. **Verena**.
Huko Italia, Wakatoliki wanawakumbuka Wat. **Prisko na Kanio**, maaskofu**, Kastrensi,** Padri, na **mapadre wenzake 10**. Wote walilazimishwa na Waharabu kupanda katika meli mbovu kutoka nchi ya Aljeria. Wakafika pwani ya Italia na kuwahudumia Wakristo huko.[1]
Pia kumbukumbu ya maaskofu **Serbonio**, **Regulo**, **Feliksi** na **wenzao, kwa jumla 220**, waliohamishwa Italia na Waharabu kwa amri ya Mfalme Thrasamund, Mfuasi wa Ario.[2]
Huko Afrika ya Kaskazini, Wakatoliki wanawakumbuka Wat. **Tasio, Dubitato, Valensio, Donati**, wafiadini.
Pia kumbukumbu za: Wat. **Feliksi** na **wenzake 11,** walizaliwa Adrumetum, Byzacena (siku hizi Tunisia Kusini). Baada ya kuteswa vibaya kwa ajili ya imani yao katika mji wao, walihamishwa Benevento, Italia na huko wakauawa mwaka 258, wakati wa dhiki ya Kaizari Valeriani, au pengine wakati wa Dioklesiani.[3]
Huko Palestina, kumbukumbu ya Mt. **Yoshua**, Jemadari wa Waebrania.
Huko Sudan ya Kusini, Mhashama **Maria Teresa Scandola** (*Maria Giuseppa*), Sista wa Comboni, 1903.
Huko Soroti, Uganda, Wakatoliki wanawakumbuka **Laurenti Oyuru**, Padri wa Jimbo, Paroko wa Parokia ya Ocero, na **watu 25**, waliouawa na askari wa *Lord's Resistance Army*, mwaka 2003.

Huko Misri, Wakoptiki wanawakumbuka pia Mt. **Verena** na **Makari II**, Patriarka, askofu wa 69 wa Aleksandria.[4]
Huko Ethiopia, Wakristu wanawakumbuka **Musa** na dada yake **Sara**, wafiadini.[5]

---

[1] *Roman Martyrology*, ed. 1956. Wanaotajwa pamoja na Kastrensi: Tamaro, Rosio, Heraklio, Sekundino, Adjutori, Marko, Augusto, Elpidio na Vindomio,
[2] *Roman Martyrology*, ed. 1942
[3] *Les petits Bollandistes*. Wanaotajwa pamoja na Feleksi katika martirolojia ya Mt. Hieronimo: Donati, Aronsio, Honorati, Fortunati, Saviniano, Septimino, Januari, Feliksi, Vitalis, Satorio, na Reposito.
Kuhusu Yoshua rejea tarehe 20 Juni maisha yake.
[4] *Coptic Synaxarium, 4 Tute.*
[5] *Ethiopian Synaxarium: Nehasse 26.*

Huko Afrika ya Kusini, Waanglikana (*Church of South Africa*) wanamkumbuka **Robert Gray**, Askofu wa kwanza wa Cape Town, 1872.

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake! Amina.

## Mt. Verena, Karne la IV.



Verena anaheshimiwa kuwa Mtakatifu katika Kanisa Katoliki na Kanisa la Koptiki Misri. Kimapokeo tunaambiwa kwamba Verena alizaliwa karne la III, katika kijiji cha Garagous, Misri na kulelewa katika nchi ya Theba,[6] katika familia ya kikristo. Alikabidhiwa kwa askofu Cherimon. Akamfundisha dini ya ki-kristo na kumbatiza. Kadiri ya mapokeo Verena aliwasindikiza askari wa Jeshi la Theba, yaani Jeshi la Warumi kutoka mkoa wa Theba, Misri, walipokwenda Rhaetia, Uswisi. Alikuwa ndugu wa Mt. Viktori, askari wa Jeshi hilo. Ndugu wa askari waliruhusiwa kuwasindikiza ili waweze kuwatunza wakijeruhiwa.
Watakatifu Morisi na Viktori na wengi wa Jeshi la Theba walipouawa[7] kwa sababu ya imani yao katika Yesu Kristo, aliendelea kuishi Uswisi kama mkaa pweke. Kwanza alifanya makazi yake Solothurn, lakini baadaye aliishi pangoni, karibu ya mji wa Zurich, siku hizi. Kama mkaa pweke, Verena alifunga na kusali daima. Kwa mikono yake Bwana Yesu alifanya miujiza mingi. Aliwajalia kuwaangalia hasa wasichana wadogo, kwa ki-roho na hata ki-mwili, akisaidiwa na kazi yake ya unesi.
Kwa sababu ya sifa yake, Gavana akaamuru afungwe gerezani. Humo Mt. Morisi akamtokea kumfariji na kumpatia nguvu. Hatimaye,

---

[6] Thebe siku hizi ni Luxor, mkoa wa Upper Egypt.
[7] Tazama habari zao tarehe 22 mwezi wa 9.

alifunguliwa na kuendelea kutenda miujiza. Kwa sababu ya juhudi zake, watu wengi walioongoka na kuwa Wakristo. Aliendelea kuwahudumia maskini na kuwalisha. Zaidi ya hayo, alifurahia kuwatunza wagonjwa, hasa wale wenye ukoma. Alikuwa akiwaosha majeraha yao na kuwapaka mafuta, bila kujali kuambukizwa. Akafariki Uswisi.

Mnamo mwaka 1986, wakilishi wa Kanisa la Mt. Verena, Uswisi, walipeleka vipande vya masalia yake huko Misri. Kanisa la Koptiki la kwanza kwa jina la Mt. Morisi na Mt. Verena, lilijengwa Kairo na kuwekwa wakfu na Patriarka Shenouda III, tarehe 2, mwezi Februari, mwaka 1994.

Mt. Verena, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

## **Mhashama Maria Teresa Scandola, 1903**.



Maria Teresa Scandola alizaliwa huko Italia, [8] tarehe 26 Januari, 1849. Akapewa jina la utani Marietta. Baba yake alifariki Marietta alipokuwa na umri wa miaka sita. Familia iliishi katika umaskini bila kupotea imani na hasa matumaini. Kwa neema ya Mungu mama mmoja Teresa Vinco alimsaidia Marietta kusoma. Kila siku baada ya shule alifanya kazi ya kutunza mbuzi wachache. Alipoanza kazi kama msichana wa nyumbani, mvulana akamshambulia. Akanusurika, lakini akawa mgonjwa sana. Wakati wote walingoja kifo chake, lakini akapona mara. Ilikuwa sikukuu ya Bikira Maria Mkingiwa dhambi ya asili.

Mwaka 1871 akakutana na Danieli Comboni, aliyekuwa ameanzisha Taasisi ya Mama wa Afrika (*Institute of the Pious Mothers of Africa*), akajiunga huko Verona. Tarehe 19 Machi, 1877, akaweka nadhiri zake na kuitwa Sista Maria Ciuseppa.

Tarehe 12 Desemba 1877, alikuwa mmojawapo wa masista watano kutoka Verona kwenda Afrika. Tarehe 31 Machi 1877 baada ya safari ndefu na ya kuchosha, wakafika Berber, Sudan Kaskazini, kituo chao cha kwanza. Kutoka Berber Marietta akasafiri kwenda Al-Ubayyid, na

[8] Bosco Chiesanuova

pamoja na Sista Teresa Grigolini, kwenda hata Kharthoun. Huko Sista Maria Giuseppa, bila kuhesabu uchovu, alianza kazi ya kuwatunza watoto na wasichana. Akawa alama ya Upendo wa Mungu kati ya watu. Danieli Comboni akaandika habari zake: "Sista Maria Giuseppa ni sista mtakatifu kweli".

Mwaka 1888, Sista Maria Giuseppa, pamoja na Padri Kasimiro Giacomelli na bruda Petro Santoni, akaenda Gezira, kisiwa katika mto Nile. Huko Padri Antonio M. Roveggio alianzisha kijiji kwa wale waliokombolewa kutoka utumwa. Sista Maria Giuseppa akawa msaidizi wake mkuu. Akawatunza wote, akahakikisha kwamba wote wasome, watunzwe, na hasa warudishiwe heshima yao. Akasimamia nyumba ya wasichana wadogo wa Africa (*Little black girls*), akawafundisha kuwa mama na wake wema.

Mwezi wa Julai 1891 akachaguliwa kuwa Mama Mkuu wa *Pious Mothers of Africa*. Akajiona hastahili kupokea kazi hiyo. Akaendelea na kazi yake katika vituo vya misioni: baada ya Berber, Al-Ubayyid, Khartoum, Shellal, Gezira, Kairo na Aswan, aliomba kwenda Lul, mpakani mwa Sudan. Njiani alisimama huko Khartoum kumwomba Bwana ili misioni ijengwe upya tena baada ya jeshi la Mahdi kulibomoa. Akafika Lul, tarehe 21 Juni, 1903. Akajaa na furaha kuwepo moyoni mwa Afrika. Akaanza kujifunza lugha. Na misioni ikajengwa pole pole upya. Padri Giuseppe Beduschi, kijana, akaugua vibaya hata tumaini la kupona halikuwepo. Sista Maria Giuseppa aliposikia habari hiyo akamwambia asihangaike, kwa sababu wakati wa kwenda kwa Mungu ulikuwa wakati wake na siyo wakati wa Padri kijana. Kwa hiyo, akiwa na afya nzuri, alimwomba Mungu kumchukua yeye na kumjalia Padri afya yake tena. Bwana akasikia ombi lake. Mara Padri Beduschi akapona, na Sista Maria Giuseppa akafariki siku chache baadaye, tarehe 1 Septemba 1903. Akawa na umri wa miaka 54, na aliishi Afrika miaka 26.

Mhashama Sista Maria Giuseppa, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.[9]

---

[9] Rejea *Servans of the Gospel, witnesses in the footsteps of Saint Daniele Comboni in Sudan and South Sudan*, Paulines Publications Africa, 2014, uk.69-74.

**Septemba 2**

Sisi Wakatoliki tunamkumbuka leo Mt. **Yusto**, askofu na mtawa, mtu mtakatifu aliyejaliwa roho ya unabii. Akastaafu kutoka uaskofu na kwenda kuishi kama mtawa huko jangwani mwa Misri, pamoja na msomaji wake **Viatori**. Alipoishi miaka michache akaenda kwa Bwana wake kupokea taji la haki. Mwili wake na masalia ya msomaji wake Viatori, yalipelekwa Lioni, Ufaransa, tarehe 2, mwezi wa Septemba.[10]
Huko Misri, kumbukumbu ya Wat. **Thedoto** na **Theofano**, mashahidi.

Huko Ethiopia, Wakristu wanawakumbuka Mashahidi Abba **Benyamini** na **Eudoksia** wa mji Sabersir, Misri. Waorthodoksi Tewahedo pia wanawakumbuka **Viktori**, Mkristo wa Aleksandria, na mama yake **Sara**.[11]

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake! Amina.

## Mt. Yusto, Askofu na Mtawa, 390

Yusto alizaliwa Ufaransa, alikuwa shemasi tu, alipoteuliwa kuwa askofu wa mji wa Lioni (*Lyon*), Ufaransa. Alipokwisha pakwa mafuta matakatifu ya daraja ya uaskofu, alianza kulisimamia kundi lake kwa bidii. Watu walimsifu na kumpenda kwa wema wake na hekima yake kubwa, na hasa kwa huruma yake kwa maskini. Alikaa Lioni miaka mingi kwa amani na watu wake wote.
Siku moja, palikuwa na mwanamume mmoja aliyekuwa amepoteza akili baada ya kuugua homa kali. Alitokea njiani, akapiga upanga kuume na kushoto, akiwaumiza watu wengine. Watu walimzunguka kutaka kumzuia na kumkamata. Akapasua katikati, akakimbilia kanisani, akaingia humo, kisha akaufunga mlango nyuma yake. Kanisa si mahali haramu, wala siyo halali kuingiliwa ovyo kwa sababu ya kumkamata

[10] *Martyrologium Romanum,* ed. 2001.
[11] *The Ethiopian Rite Missal, Abba Emmanuel & Abba Brendan Cogavin, 2002, uk 328. Ethiopian Syxanarium, Nehasse 27.*

mtu ye yote. Walimfuata, wakakusanyika mbele ya kanisa kwa kelele na vishindo, wakiwa tayari kumwulia mbali.

Askofu aliposikia vishindo vya watu, alijiingiza kati yao, akijaribu kuwatuliza. Hawakumsikiliza. Kwa hasira, walisema wataichoma moto kanisa, kama askofu asipokubali kumtoa mtu huyo. Askofu akafanya shauri na mzee mmoja, mtu mkubwa wa mji, akapatana naye kwamba atamletea yule mwendawazimu, afungwe chumbani pasipo kudhuriwa. Basi, askofu akiamini maneno walioagana akaingia kanisani; punde akatoka na yule kichaa. Lakini maskini, alipofikia kizingitini, hakupata nafasi ya kukingwa na mdhamini wake, akakamatwa mara, akakokotwa njiani, wakamsukuma, na kumpiga mpaka wakamwua.

Askofu aliona uchungu sana kwa sababu mtu alikuwa ameuawa baada ya kuamini maneno ya mdhamini wake; hasa, kwa sababu imevunjwa sheria iliyokatazwa kumtoa mtu aliyekimbilia kanisani. Ijapokuwa kweli alidanganyika, kwamba mwenye maagano naye hakuyatimiza maagano, askofu alijipatiliza uuaji huo, akakusudia kujitenga na dunia, akae utawani kujitesa hata mwisho wake.

Basi, alipokwisha waza hayo moyoni mwake mbele ya Mungu, pasipo kumwambia mtu nia yake, aliondoka kwa siri, akaenda zake hata bandari ya Marsilia (*Marseille*), Ufaransa, akapanda katika merikebu iliyokuwa tayari kung'oa nanga. Alivuka hata akafika Misri. Alishuka akafululiza barani, hata akafika mbugani kwenye nyumba ya watawa. Akaenda kubisha hodi kwenye monasteri ya Shete.[12] Hakutaja jina lake wala hakusema kwamba yeye ni askofu. Akaomba ruhusa ya kutawa ki-monaki. Alipokewa, akakaa miaka kadha akizoea na kazi na sala za wenzake.

Hata siku moja akaja mhajiri mmoja kutoka Ulaya. Alipokwisha kuingizwa kati ya wamonaki waliokaa kitako sebuleni, mara alimtambua Yusto, ndiye askofu wake, kwani naye mwenyewe alikuwa mzaliwa wa Lioni, mji wake. Akamwangukia, akiomba baraka yake. Abate na wamonaki wengine walihamanika sana, wakamwomba mgeni awape habari. Alipowajulisha, wote walimwangukia mtakatifu Yusto wakamwomba radhi kwani hawakumjua kuwa ni askofu. Tangu siku hiyo walimwangalia kwa heshima na kumtukuza; mwenyewe

[12] Shete, au Scete, ni Wadi El Natrun ya siku hizi.

hakukubali kupunguza mazoezi aliyokuwa nayo kwanza. Alifanya kazi, alisali, alifunga pamoja na wamonaki wenzake. Alikaa hivyo maisha yake mpaka akawa mzee, akafa katika monasteri.

Askofu Yusto alisindikizwa na Viatori, msomaji na Katekista wa Kanisa Kuu la Lioni. Na yeye akafariki wiki chache baada ya kifo cha Yusto.

Sikukuu ya mtakatifu Yusto, askofu na mtawa, na Viatori, msomaji, ni tarehe 14 Oktoba. Tarehe 2 Septemba wanakumbuka pia walipoyahamisha masalia yake toka Misri na kupelekwa katika jimbo lake la Lioni.[13]

Watakatifu Yusto na Viatori, mtuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

## Abba Benyamini na Eudoksia, mashahidi

Wazazi wa Benyamini na dada yake Eudoksia walikuwa Wakristo wa mji wa Sabersir, Misri. Wazazi wao waliwalea watoto hao wawili kwa upendo katika dini ya ki-kristo na kuwawezesha kuishi kama wanavyostahili Wakristo kweli. Walionyesha ukarimu mkubwa kwa wahiji na wageni; waliishi katika usafi wa moyo; walijitoa kwa Mungu na kupiga vita vya kiroho.

Mtakatifu huyu Benyamini alitamani kufa shahidi kwa ajili ya Jina la Kristo. Basi akamwendea Gavana wa mji wa Setuf na akamkiri Yesu Kristo mbele yake. Gavana akamtesa sana na kumtia gerezani. Wazazi na dada yake walimtembelea, na walipomwona jinsi alivyoteseka walilia machozi na kuhuzunika sana. Lakini yeye aliwatia moyo na kuwaambia: “Maisha ya hapa ulimwenguni si kitu, na siku zinapita haraka, lakini maisha ya milele hayakomi”. Dada yake aliposikia maneno hayo, akamjibu: “Kaka yangu, Mungu aishivyo, tangu leo sitakuacha. Kifo utakachokufa nitakufa mimi pamoja nawe”.

Mara akakiri imani yake mbele ya Gavana. Gavana akamshika na akawaamuru askari kumtia katika mahali pa giza pamoja na kaka yake. Wakafanya hivyo. Wakakaa humo siku ishirini, bila kula wala kunywa. Baadaye askari wakawachukua, wakafunga mawe mazito shingoni mwao na kuwatupa mtoni. Lakini Malaika wa Bwana akashuka, akawaondolea mawe kutoka shingoni mwao. Wakapata nguvu,

[13] Kutoka *Maisha ya Watakatifu*, T.M.P. Book Department, Tabora, chapa 1996, uk. 306-307.

wakachukuliwa na mkondo wa maji mpaka wakafika bandari ya Batra. Bikira mmoja akawakuta, akawasaidia kutoka majini. Mara wakamwendea Gavana na kuilaani miungu ya uongo. Gavana akawatesa tena vibaya sana kwa muda wa siku nyingi. Mwishowe alipochoka kuwatesa akaamuru wakatwe vichwa. Basi watakatifu wakavishwa taji la kifodini na kuingia ufalme wa mbinguni.

Kanisa likajengwa katika mji wa Sabersir, kwa heshima yao. Miili yao ikazikwa pale pale kanisani. Miujiza mingi ikatendeka, hasa miujiza ya uponyaji wa magonjwa.

Mashahidi Benyamini na Eudoksia, mtuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

**Septemba 3**

Huko Afrika ya kuaskazini, kumbukumbu ya Mt. **Yohane**, shahidi pamoja na **Andrea** na mwenzao.[14]
Huko Ngaoundéré, Kameroun, Wakatoliki wanamkumbuka **Ivo Plumey**, Padri na Monsignori, aliyeuawa mwaka 1991.
Huko Aljeria, Wakatoliki wanawakumbuka Wenyeheri **Anjela Maria** (*Jeanne Littlejohn*) na **Bibiana** (*Denise Leckerq*) masista wa Shirika la Mama wa Mitume (*Our Lady of The Apostles*) waliouawa Belcourt, tarehe 3 mwezi wa 9, 1995.

Huko Misri, Wakoptiki wanawakumbuka Mt. **Abnodio** wa Ethiopia; **Besinta**, Shahidi na **Aristio**, Askofu huko Misri.[15]
Huko Ethiopia, Wakristu wanawakumbuka Watakatifu **Abrahamu, Isaka** na **Yakobo**.[16]

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake! Amina.

## Wenyeheri Anjela Maria na Bibiana, 1995

Jeni Littlejohn alizaliwa Tunis, nchi ya Tunisia, tarehe 22 Novemba 1933. Mwaka 1957 alijiunga na Shirika la Mama wa Mitume. Akapewa jina la Sr. Anjela Maria. Akaweka nadhiri za kwanza mwaka 1959. Akatumwa Bouzarea, Aljeria, mahali ambapo masista waliendesha nyumba ya yatima na shule ya bweni kwa wasichana, akiwa anawaangalia watoto wadogo na kufundisha kazi ya tarizi. Mwaka 1964, Shule ya Sanaa ya Aljeria ilipofunguliwa huko Belcourt, akaenda huko kama Mwalimu wa tarizi. Akabaki kule hadi kifo chake.
Sista Anjela Maria alikuwa na tabia nzuri. Alikuwa mvumilivu, wazi na karibu na wasichana. Alitaka kuwaingiza moyoni mwao upendo wa sanaa na kazi iliyofanywa vizuri. Alizungumza nao kwa lugha yao.

[14] Dictionary of Saints
[15] *Coptic Synaxarium, 6 Tute.*
[16] *The Ethiopian Rite Missal, Abba Emmanuel & Abba Brendan Cogavin, 2002, uk 329. Ethiopian Syxanarium, Nehasse 28.*

Alipenda sana nchi ya Aljeria, wakazi wake, wito wake, akishiriki furaha na mateso yao. Kazi yake ilitimizwa katika amani na urahisi.
Dionisia Leclecq alizaliwa tarehe 8 Januari 1930 huko Ufaransa. Akajiunga na Shirika la Masista ya Mama ya Mitume na kuitwa Sista Bibiana. Baada ya nadhiri zake za kwanza, mwaka 1961, alitumwa kwenda Aljeria kwa wadi ya uzazi huko Konstantini. Akiwa mwangalifu kwa mahitaji ya wengine, Sista Bibiana alichanuka katika kazi ya kuwatunza watoto wachanga na mama yao. Mwaka 1964, katika mji wa Aljeria, alikabidhiwa kuendesha chuo cha kushona na kutarizi kwa vijana ambao hawakusoma. Masista walikuwa wanapokea wasichana kutoka ujirani walipowatembelea familia zao. Kwa njia hiyo Sista Bibiana akatambua umaskini wa ki-mwili na ki-roho wa wanawake wa nchi hiyo. Akawashuhudia Yesu Kristo kwa ‘ukimya wa maneno‘ na matendo ya maisha yake.
Mwaka 1994, hali ya nchi ilipochafuka, ilimbidi kuamua kwa maisha yake: kuondoka au kubaki. Jibu lake lilikuwa wazi: “Ni watu wenyewe walioomba masista, tena wameomba tubaki. Ninahuzunika sana, ninajisikia siwezi kitu mbele ya mateso mengi, lakini najua kwamba Mungu anawapenda watu hawa na ninamtumaini Mama yetu wa Afrika. Yesu alisema: ‘Baba atawapa yote unayoomba kwa jina langu ...‘ Mwanga wake unanisaidia kutambua maajabu yaliyofichika ndani yao: kushikamana, kusaidiana, ujasiri kupita nguvu ya binadamu. Ndiye Roho Mtakatifu anayefanya kazi ndani yao. Neno la Mungu linanisaidia kuwa mwonzi wa tumaini kati yao. Nachagua kubaki.“
Padri Bonamour, Paroko, alipowakumbusha masista hatari ya kuuawa na kuwaonya kuwa tayari, walimjibu: “Tupo tayari“. Siku ya Jumapili, tarehe 3 Septemba 1995, walipoondoka kutoka kanisani baada ya kuhudhuria misa, wakati wa jioni, Sista Bibiana alishirikisha hofu yake na Sista Anjela Maria. Huyu akamjibu: “Inatubidi tusiwe na hofu. Lazima tuishi vizuri wakati huu, mambo mengine hayatuhusu“. Dakika 10 baadaye, njiani kwenda nyumbani mwao, Sista Anjela Maria na mwenzake Sista Bibiana wakauawa.
Wenyeheri Anjela na Bibiana, mtuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

**Septemba 4**

Sisi Wakatoliki tunamkumbuka Mt. **Musa**, nabii aliyewaongoza Waebrania kutoka Misri na kuingia katika nchi ya ahadi.[17]

Huko Misri, Wakoptiki wanawakumbuka siku ya leo Wt. **Agato, Petro, Amoni, Amona** na mama yao **Rebeka**, mashahidi; Mt. **Severiano**, askofu wa Gabla; Pia wanamkumbuka Mt. **Dioskoro**, Patriarka, askofu wa 25 wa Aleksandria.[18]
Waorthodoksi wanawakumbuka **Musa**, nabii wa A.K. na pia Mt. **Petronio**, mtawa mfuasi wa Pakomi, 349.[19]
Huko Ethiopia, Wakristu wanawakumbuka Mt. **Atanasi**, askofu, aliyekufa shahidi pamoja na wenzi wake, **Garsome** na **Theodoto**. Pia wanaadhimisha uhamisho wa mwili wa Aba Yohane mfupi katika monasteri ya Shete, mwaka 804 B.K..[20]
Huko Gabon na Ufaransa, kumbukumbu ya Mtu wa Mungu wa Kanisa la Kiluteri, **Alberti Schweitzer**, 1965.

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake! Amina.

## Mt. Musa, Nabii wa A.K.

Musa kwa Waisraeli ndiye Nabii mkuu aliyetumwa na Mungu kuwaokoa na utumwa wa Wamisri. Ni jitu la ki-roho katika A.K. Zamani ya Yesu, Wayahudi walimwangalia kama mwalimu wao mkuu kwa sababu ndiye aliyewaongoza Waisraeli kutoka utumwa wa Wamisri, aliyepewa amri za Mungu, aliyeongea na Mungu uso kwa uso: "*Sisi tuwajua ya kuwa Mungu alisema na Musa*" Yoh 9:29. Habari zake zimeandikwa katika vitabu vinne vya A.K.

---

[17] *Martyrologium Romanum,* ed. 2001.
[18] *Coptic Synaxarium, 7 Tute.*
[19] *Estearn Orthodox Liturgical Calendar*
[20] *The Ethiopian Rite Missal, Abba Emmanuel & Abba Brendan Cogavin, 2002, uk 329. Ethiopian Synaxarium, Nehasse 29.*

Aliishi maisha yake yote katika Afrika, Misri, isipokuwa muda mfupi kabla ya kufa kwake. Mungu mwenyewe akamzika bondeni, katika nchi ya Maobu, nje ya Misri na hadi leo kaburi lake halijulikani (Kum 34:5-6). Kadiri ya pokeo moja la Wayahudi Musa, kama Eliya, akapalizwa mbinguni.

Kuzaliwa kwake Musa kunajulikana: "*Mtu mmoja wa nyumba ya Lawi akaondoka akaoa binti mmoja wa Lawi. Yule mwanamke akachukua mimba akazaa mwana, na alipoona ya kuwa ni mtoto mzuri akamficha miezi mitatu. Na alipokuwa hawezi kumficha tena, akampatia kisafina cha manyasi akakipaka sifa na lami, akamtia mtoto ndani yake, akakiweka katika majani kando ya mto. Umbu lake mtoto akasimama mbali ili ajue yatakaompata. Basi binti Farao akashuka aoge mtoni, na vijakazi wake wakatembea kando ya mto; naye akakiona kile kisafina katika majani, akamtuma kijakazi wake kwenda kukileta. Akakifungua, akamwona mtoto, na tazama, mtoto yule analia. Basi akamhurumia, akasema, 'Huyu ni mmojawapo wa watoto wa Waebrania.' Basi umbu lake mtoto akamwambia binti Farao, 'Je, niende nikamwite mlezi katika wanawake wa Kiebrania, aje kwako, akunyonyeshee mtoto huyu?' Binti Farao akamwambia, 'Haya! enenda.' Yule kijana akaenda akamwita mama yake yule mtoto. Binti Farao akamwambia, 'Mchukue mtoto huyu, ukaninyonyeshee, nami nitakupa mshahara wako.' Yule mwanamke akamtwaa mtoto, akamnyonyesha. Mtoto akakua, naye akamleta kwa binti Farao, akawa mwanawe. Akamwita jina lake Musa, akasema, 'Ni kwa sababu nalimtoa majini.*'" Kut 2:1-10.

Binti Farao, kwa jina Termuthe, akampenda Musa, mwana wake wa kupanga. Siku moja, anayetusimulia Mwanahistoria Yosefu, binti Farao akampeleka Musa kwa baba yake. Farao akamchukua Musa mikononi mwake, na akistaajabia uzuri wake, akamwekea taji lake, ambalo lilikuwa mungu wake, juu ya kichwa chake. Mtoto Musa akalichukua na kulitupa chini ya miguu yake. Farao akakasirika. Akakusanya waganga wake na kuwauliza mtoto huyu atakuwaje. Wakamsimulia kuzaliwa kwake na kumwambia: "Huyu ataharibu ufalme wako, atakuwa mtawala wa Waebrania." Kwa hiyo Farao akaamua auawe. Lakini



wengine wakamtetea wakisema kwamba tendo hilo lilikuwa tendo la kitoto. Wakamshauri Farao kumweka mtoto katika jaribio. Wakafanya hivyo. Wakaweka mbele ya mtoto sahani moja iliyojaa makaa ya moto, na sahani nyingine iliyojaa matunda. Wakamsihi ale. Mtoto akachukua makaa ya moto na kuyapeleka kinywani mwake. Akaungua ulimi wake. Tangu siku ile Musa alikuwa na kigugumizi. Binti Termuthe akampokonya Musa kutoka mikononi mwa Farao na kumwokoa. Musa akanusurika kifo kwa mara ya pili.

Musa akakua, akajifunza lugha ya Kimisri, kusoma na kuandika, utamaduni wao. Akawa mmoja wa Wamisri. Lakini hakusahau kwamba yeye ni Mwebrania. Siku moja alipowaendea ndugu zake, akatazama mizigo yao. "*Akamwona Mmisri anampiga Mwebrania, mmojawapo wa ndugu zake. Basi akatazama huko na huko, na alipoona ya kuwa hapana mtu, akampiga Mmisri yule, akamficha ndani ya mchanga. Akatoka siku ya pili, na tazama, wawili wa Waebrania walikuwa wakipigana. Akamwambia yule aliyemdhulumu mwenzake, 'Mbona unampiga mwenzako?' Yule akasema, 'Ni nani aliyekuweka wewe kuwa mkuu wetu, na mwamuzi juu yetu? Je, wataka kuniua mimi kama ulivyomwua yule Mmisri?' Musa akaogopa, akasema, 'Kumbe! Jambo lile limejulikana.' Basi Farao alipopata habari, akataka kumwua Musa; lakini Musa akakimbia mbele ya Farao, akakaa katika nchi ya Midiani*." Kut 2:11-15. Kwa mara ya tatu akaepa hatari ya kifo!

Katika nchi ya Midiani Musa akaoa Sipora binti mmoja wa Yethro, kuhani wa Midiani. Akakaa huko akichunga kondoo za mkwewe. Akiwa katika kazi hiyo alikutana na Mungu wa baba zake Ibrahimu, Isaka na Yakobo. Sasa Mungu akaingia wazi katika maisha ya Musa, akaanza uhusiano naye wa karibu sana. Akamwita kushiriki naye katika kazi ya kuwaokoa Waisraeli kutoka utumwa wa Wamisri. Ilimbidi Musa arudi Misri kutimiza mapenzi ya Mungu.

Kazi yake haikuwa rahisi, lakini alizidi kuhusiana na Mungu. Alizungumza na Mungu kama mtu anavyozungumza na rafiki yake, uso kwa uso, (Kut 33:11/Hes 12:6-8). Alikaa na Mungu mara nyingi, tena kwa muda mrefu, yaani alikuwa katika uwepo wa Mungu kwa muda mrefu. (Kut 33:8-10). Kwa hiyo kwa mkono wa Musa Mungu alifanya miujiza mikubwa. Akawavusha Waisraeli bahari ya Shamu na "*Israeli akaiona ile kazi kubwa aliyoifanya Bwana juu ya Wamisri, ndipo hao*

*watu wakamcha Bwana, wakamwamini Bwana, na Musa mtumishi wake.*" Kut 14:31. Musa akawaongoza Waisraeli hadi nchi ya Kanaani kwa njia ya jangwa. Kwa miaka 40 wakazunguka huko na huko wakitayarishwa na Mungu kuingia nchi ya ahadi kwa nguvu ya imani.
Musa hakuruhusiwa kuingia nchi ya Kanaani kwa sababu ya kosa fulani. Inawezekana kwamba alikuwa na mashaka wakati Waisraeli walipofika Masa na Meriba, wakikosa maji ya kunywa. Mungu akamwambia Musa: "*'Tazama, nitasimama mbele yako huko, juu ya lile jabali katika Horebu; nawe utalipiga jabali, na maji yatatoka, watu wapate kunywa.' Musa akafanya hivyo mbele ya wazee wa Israeli*." Kut 17:6. Kadiri ya pokeo fulani, kuliko kupiga jabali mara tatu, Musa akalipiga mara moja kwa mashaka!
"*Musa akapanda kutoka uwanda wa Moabu mpaka mlima Nebo, hata kilele cha Pisga kukabili Yeriko. Bwana akamwonyesha nchi yote … 'Hiyo ndiyo nchi niliyowaapia Ibrahimu, na Isaka, na Yakobo, nikisema, 'Nitawapa wazao wako.' Basi nimekuonyesha kwa macho yako, lakini hutavuka huko. Basi Musa, mtumishi wa Bwana, akafa huko, katika nchi ya Moabu, kwa neno la Bwana. Akamzika bondeni, katika nchi ya Moabu, kukabili Beth-peori; lakini hapana mtu ajuaye kaburi lake hata leo. Musa alikuwa mtu wa miaka mia na ishirini alipokufa; jicho lake halikupofuka, wala nguvu za mwili wake hazikupunguka*." Kum 34:1-7.
Mt. Musa, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

## Wat. Agato, Petro, Yohane, Amnoni, Amona na Rebeka, mashahidi.

Wote walifariki mashahidi. Walikuwa wa Kemola, mkoa wa Kusi, Misri. Bwana Yesu Kristo aliwatokea na kuwafunulia yatakayowatokea, ya kwamba watapokea taji la kifodini huko Shoubra, karibu na mji mkuu wa Aleksandria, miili yao itapelekwa Nakraha, mkoa wa El-Behairah. Watakatifu walifurahi. Wakaamka mapema na kuwagawia maskini mali yao. Agato, kaka mkubwa, alikuwa mtu mashuhuri katika mji na alipendwa na watu wote. Rebeka, mama yao, aliwaimarisha na kuwatia moyo ili wavumilie mateso kwa jina la Bwana Yesu Kristo.

Wakafika mji Kusi na kukiri imani yao kwa Yesu Kristo, mbele ya Gavana Dionisi. Aliwatesa sana, kuanzia na mama yao aliyevumilia mateso kwa furaha. Baadaye aliwatesa waana watano. Alipochoka kuwatesa, alishauriwa kuwatuma mjini Aleksandria ili wasiwashawishi watu kwa kuwa walipendwa na wote. Kwa sababu yao wengi waliongoka na kumwamini Yesu Kristo na kupokea taji la kifodini.

Walipowekwa mbele ya Armenio, Gavana wa Aleksandria, aliyekuwa mjini Shoubra, aliwatesa sana, tena kwa ukatili. Akakatakata miili yao, akawatupa katika bwela, akawabana juu ya magurudumu na akawasulubisha vichwa chini. Kutokana na mateso hayo yote Bwana Yesu akawaponya na kuwahuisha upya. Gavana na watu wote wakaona haya.

Mwishowe Gavana akaamuru wakatwe vichwa na miili yao itupwe baharini. Wakakatwa vichwa na miili yao ikawekwa juu ya mashua ili itupwe baharini. Mungu akamtuma malaika wake kwa mtu tajiri wa mji wa Nakraha na kumwambia kuichukua miili yao. Mtu huyu akafurahi. Akafika mahali miili ya watakatifu ilipowekwa, akawahonga askari kwa fedha nyingi na kuichukua miili yao. Akaipeleka kanisani. Ndipo akasikia sauti: “Hapa ndio mahali pa penye haki”. Miili ilibaki katika kanisa hilo mpaka mwisho wa dhiki. Baadaye wakajenga kanisa kubwa kwa heshima yao. Miujiza na maajabu mengi yakafanyika kwa njia ya masalia yao. Hatimaye waliihamisha miili yao mji wa Sonbat, ambapo kanisa lilijengwa na kujulikana kwa jina la “Watano na mama yao”, au kwa jina la “*El-Sitt Refka*”, maana yake “Mama Rebeka”. Wakristo wengi wanahiji kule kubarikiwa na Watakatifu hawa.[21]

Watakatifu mashahidi, mtuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

## Mtu wa Mungu Alberti Schweitzer, 1965

Alberti Schweitzer alizaliwa Ufaransa. Mama yake aliitwa Adela Schillinger na baba yake Aloisi Theofilo Schweitzer. Alilelewa katika kijiji cha Gunsbach, wakati ule kilikuwa chini ya utawala wa Wajerumani kabla ya kurudi kuwa chini ya utawala wa Wafaransa baada ya Vita vya Pili vya Dunia. Baba yake, aliyekuwa mchungaji wa

---

[21] *Coptic Synaxarium, 7 Tute.*

kanisa la Kilutheri, akamfundisha kucheza muziki. Jengo la kanisa la Gunsbach lilitumiwa na Walutheri na Wakatoliki kwa zamu. Jambo hilo limemfundisha stahamala ya msimamo wa wale wenye dini nyingine na kuchapisha moyoni mwa Alberto hamu ya kutafuta daima umoja wa Wakristo.

Lugha yake ya kuzaliwa ilikuwa lahaja ya Kijerumani iliyozungumzwa katika mkoa wa *Alsace*. Akafuata shule ya Sekondari huko Mulhouse na kuhitimu mwaka 1893. Kwa miaka minane, alijifunza muziki chini ya Eugenio Munch, mpiga kinanda wa kanisa la Kiprotestanti wa mji ule. Na mwaka 1893 alicheza muziki chini ya Charles Marie Widor, mpiga kinanda katika kanisa katoliki la Saint Sulpice, Paris.

Kuanzia mwaka 1893 hadi 1899 akajifunza teolojia huko mji Strasbourg katika chuo cha Kaiser Wilhelm. Ilimbidi kujiunga na Jeshi kwa mwaka mmoja. Aliandika tasnifu yake kuhusu Falsafa ya Kant,[22] huko *La Sorbonne*. Na huko aliendelea kuhusiana na Charles Marie Widor na kujifunza kwake. Akahitimu, akawa Profesa huko Chuo cha Tübingen, Ujerumani, mwaka 1899. Sifa yake kama mwanamuziki bora ikavuma katika Ulaya wote. Mwaka 1905 akaandika kitabu kuhusu J. S. Bach[23] kwa lugha ya Kifaransa. Watu wengi waliomba kitabu hiki kitafsiriwe kwa lugha ya Kijerumani. Alikataa, bali, kinyume chake, alikiandika upya kwa lugha ya Kijerumani. Kikachapishwa kwa majuzuu mawili. Pia aliandika kitabu cha teolojia “Kutafuta Yesu wa Historia,“[24], ambacho kilikuwa muhimu katika teolojia ya zamani yake.

Mwaka 1899 Schweitzer akawa shemasi katika Kanisa la Kilutheri Mt. Nikolas, mjini Strasbourg. Mwaka uliofuata alipadirishwa, na mwaka 1903 akachaguliwa kuwa Mkuu wa Chuo cha Mt. Tomaso.

Alipokuwa na umri ya thelathini, Schweitzer aliitikia wito wa Shirika la ki-injili la ki-misionari la Paris [25]lililotafuta daktari kufanya kazi katika misioni. Shirika hilo halikupokea jibu lake, kwa sababu waliona alikuwa na msimamo tofauti kuhusu teolojia. Haidhuru, Schweitzer akaacha cheo chake cha Mkuu wa Chuo na kuanza kujifunza tena kwa miaka mitatu ili kuhitimu kama Daktari ya ki-mwili. Alipanga kueneza

---

[22] *The Religious Philosophy of Kant*
[23] *J.S. Bach, musician et Poet*
[24] *The Quest of the Historical Jesus*
[25] *The Society of the Evangelist Missions of Paris*

Injili kwa njia ya kazi yake kuponya miili ya watu, kuliko kuhubiri tu Neno la Mungu. Akaamini kwamba utumishi wake wa namna hiyo utakubaliwa katika kila Kanisa. Akamaliza masomo yake mwaka 1911. Mwezi Juni 1912 akamwoa Helena Bresslau.

Akakubaliwa na Shirika la ki-injili la ki-misionari la Paris. Mwaka 1913, yeye na mke wake na mtoto wake Peter, waondoka kwenda Afrika kukaa Lambaréné, kando la mto Ogooué, nchi ambayo sasa ni Gabon. Akaanzisha hospitali, iitwayo leo Hospitali ya Alberti Schweitzer. Kwa miezi tisa ya mwanzo, yeye na mke wake, wakahudumia wagonjwa 2.000, wenye magonjwa ya tropiki ya kila aina. Mke wake Helena alikuwa mtaalamu wa unusukaputi (*anaesthetis*).

Mwanzoni walifanya kazi katika kibanda na wodi zilijengwa jinsi zilivyojengwa nyumba za wenyeji, lakini pole pole walianza kujenga hospitali kwa matofali. Na mwaka ule walizaidiwa na msaada wa mwenyeji Galoa, aliyezungumza lugha ya Kifaransa.

Vita vya Kwanza vya Dunia vilipotokea Alberti na mke wake Helena waliendelea kazi yao bila kuwa na ruhusa kutoka nje ya maeneo yao. Mwaka 1917, Alberti akiwa mdhaifu sana kwa sababu ya ukosefu wa damu (*anemia*) na miaka minne ya kazi ngumu, yeye na mke wake wakapelekwa Ufaransa na kufungwa. Lakini mwisho wa mwaka 1918 Alberti akapata tena uraia wa Ufaransa na kuwa huru. Huko Strasbourg alifanya kazi kama daktari. Mwaka 1920 alipopona alitafuta hella kujenga hospitali yake kwa kucheza muziki. Aliandika vitabu viwili muhimu kwake: "Kuanguka na kusimama tena Ustaarabu (wa Ulimwengu)", pia "Ustaarabu (wa Ulimwengu) na Elimuadili"[26].

Mwaka 1924 akarudi Lambarene, bila mke wake. Majengo yote yalikuwa yamebomoka. Akaanza pamoja na wasaidizi wake kutoka Ulaya, kuwahudumia wagonjwa na kujenga hospitali. Baada ya miaka miwili hospitali mpya ikajengwa. Karibu kazi yote ilifanywa na msaada wa wenyeji. Maeneo yakafanana na kijiji. Madaktari wakaongezeka. Kwa hiyo, mwaka 1927 akarudi Ufaransa akiacha nyuma yake hospitali inayofanya kazi. Mwaka 1935 akarudi tena Lambarene na kufanya kazi huko muda wote hadi mwisho wa Vita vya Pili vya Dunia. Miaka

---

[26] *"The decay and restoration of Civilization"*, na *"Civilization and Ethics"*.

mitatu baada ya Vita akaweza kurudi Ulaya na kusafiri huko na huko, hata Marekani, kadiri ya uwezo wake.
Mwaka 1952 akazawadiwa '*The Nobel Peace Prize*'. Akaunga mkono na Alberti Einstein na wengine waliotaka ulimwengu huru kwa kupinga matumizi ya silaha ya nyuklia. Akatangaza hewani 'Adhimio ya dhamira' akisema: "Mwisho wa majaribio ya silaha ya kinyuklia utakuwa mwanzo wa matumaini wateswao ulimwenguni wanayongojea".
Alberti Schweitzer alifariki tarehe 4 Septemba 1965 katika hospitali yake, huko Lambaréné. Kaburi lake limeonyeshwa na msalaba aliotengeneza yeye mwenyewe.
Mawazo yake yakajulikana, siyo katika Ulaya tu hadi ulimwenguni pote. Lakini hakukosa kupata wapinzani wa kazi yake na mawazo yake. Wengine walimwona kama Kaka mkubwa akiwaangalia Waafrika kama wadogo wake. Kwa yoyote alieneza Injili ya Yesu kwa maneno yake na kwa matendo yake. Aliangalia kazi yake ya mmisionari katika Afrika kuwa jibu lake la wito wa Yesu: "*Utakuwa mvuvi wa watu*" Lk 5:10, na pia kufanya toba kwa ajili ya madhambi ya wakoloni kutoka Ulaya.
Mtu wa Mungu Alberti Scheitzer, utuombee Mungu atujalie amani ulimwenguni mwetu na atukuzwe daima na milele. Amina.

**Septemba 5**

Sisi Wakatoliki tunamkumbuka Mt. **Teresa wa Kalkuta**, aliyetembelea Tanzania na nchi nyingine za Afrika.
Huko Aleksandria, Misri, Wakatoliki wanawakumbuka Mt. **Rais** (au *Herais*) wa Tamma, bikira na mfiadini, 308; Wat. **Nimfido** na **Saturnino** wafiadini; Na mahali pengine Misri, kumbukumbu za Wat. **Taurino**, **Nemorati, Saturnino** (mwingine) na **Arapolinio,** wafiadini, Misri.[27]
Huko Ethiopia kumbukumbu ya Mt**. Dimadio,** Mwungama-dini.[28]

Wakoptiki wanamkumbuka Mt. **Dimide**, Shahidi.[29]
Huko Ethiopia, Wakristu wanamkumbuka Mt. Abba **Musa**, askofu wa Pelusium (Farma).[30]
Waorthodoksi wanamkumbuka Mt. **Rais**, bikira na mfiadini.[31]

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake! Amina.

## Mt. Dimide, Shahidi

Leo Wakoptiki wanamkumbuka Mt. Dimide. Alikuwa mwenyeji wa Tharch, jimbo la Dantua. Alipenda Kanisa, na kufuatana na maneno ya Yesu, aliwasaidia maskini na kuwatembelea wagonjwa. Siku moja mtu wa nuru akamtokea na kumwamuru aende kupokea taji la ushahidi na kuzawadiwa thawabu kutoka mbinguni. Mtakatifu akafurahi sana. Akamwacha baba yake, akatoka mjini na akamwomba Bwana neema ya kuvumilia mateso yote kwa jina lake.
Akafika katika mji Atribi na kumkiri Bwana Yesu kuwa Kristo. Akateswa vibaya sana. Baadaye akatumwa Aleksandria, kwa Gavana Lusiani. Alipokuwa katika meli, Bwana Yesu akamtokea, akamfariji na

[27] *Acta Sanctorum.* Rjea maisha ya Rais, au Herais wa Tamma, tarehe 23 Septemba.
[28] Dictionary of Saints
[29] *Coptic Synaxarium, 8 Tute.*
[30] *The Ethiopian Rite Missal, Abba Emmanuel & Abba Brendan Cogavin, 2002, uk 330. Ethiopian Synaxarium, Nehasse 30.*
[31] *Estearn Orthodox Liturgical Calendar*

kumtia moyo, akimwahidia kupumzika katika uzima wa milele. Akafurahi sana. Gavana Lusiani akamtesa kwa njia mbalimbali na mwishoni akaamuru akatwe kichwa. Watu wa mji wake wakafika kuchukua mwili wake na kumheshimu sana.[32]
Mt. Dimide, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

## Mt. Teresa wa Kalkuta, 1997

Mama Teresa anajulikana sana katika bara ya Afrika. Mwaka 1968 alianzisha nyumba hapa Tanzania. Katika Afrika ya Kusini akaanza kazi mwaka 1988 katika Kayelitsha kiunga cha mji Cape Town, n.k. Sasa Masista Wamisionari wa Upendo wanafanya kazi katika nchi nyingi za Afrika. Mara kadhaa Mama Teresa aliwatembelea masista wake katika Tanzania. Nchi ya Tanzania ilibarikiwa kila wakati alipokanyaga ardhi yetu.
Wakristo wengi wanamfahamu kwa jina, wamesikia habari zake, lakini wachache wanajua maisha yake. Angela (*Anjezë*), aliyejulikana kwa jina la Mama Teresa, alizaliwa, tarehe 26 Agosti 1910, katika mji wa Skopje, sasa mji mkuu wa Makedonia, zamani chini ya utawala wa Uturuki. Akabatizwa siku moja baada ya kuzaliwa kwake. Kwa Mama Teresa tarehe 27 Agosti ilikuwa siku ya kweli kuzaliwa kwake. Baba yake alifariki Anjela akiwa na umri wa miaka 8. Sikukuu ya Bikira Maria kupalizwa mbinguni, mwaka 1928, akisali katika Sakrario ya Mama Mweusi ya Vitina-Letnice, alihakikishwa rohoni mwake kwamba Mungu anamwita kuishi maisha ya utawa. Akaingia katika shirika la Masista wa Loreto. Baada ya kuishi katika Makedonia kwa muda wa miaka 18, alienda Ireland kujifunza Kiingereza na baadaye, alihamia India alipoishi miaka mingi hadi kifo chake. Akaweka nadhiri zake za kwanza mwaka 1931 na akaitwa Sista Teresa kwa heshima ya Mt. Terezia wa Lisieux, somo wa wamisionari. Kwa sababu sista mmoja alikwisha kuitwa Sista Terezia, akachagua kuitwa Teresa, matamshi ya lugha ya Kihispania. Akaweka nadhiri za maisha mwaka 1937.
Kwa muda wa miaka 20 alifundisha katika shule ya Loreto huko Entally, Mashariki ya mji Kalkuta. Ingawa alifurahi kufundisha, rohoni alihangaika akiona umaskini wa watu walioishi katika mji Kalkuta.

[32] *Synaxarium Arabic-Jacobite*

Mwaka 1946, tarehe 10 Sepemba, akasikia moyoni, kama alivyoita yeye mwenyewe wito katika wito wake, “Lazima niondoke kutoka konventi na kuwasaidia maskini kwa kuishi miongoni mwao. Ilikuwa amri. Kutotimiza amri hiyo kungekuwa kuvunja imani“. Akaanza kazi yake ya mmisionari miongoni mwa maskini mwaka 1948. Akapata uraia wa India, akajifunza unesi katika Hospitali ya Familia Takatifu kwa muda wa miezi michache na kuanza kutembelea wakazi wa mtaa na kuwakimu. Alianza kwanza shule kabla ya kuwashughulikia wenye njaa. Mwanzoni mwa mwaka 1949 alisaidiwa na akina mama wengine. Kwa pamoja mwaka 1950 alianzisha Shirika la Wamisionari wa Upendo lililokua kwa kasi hadi kufikia, mwaka 2012, masista 4,500 wanaofanya kazi katika nchi 133 za dunia. Mwaka 1963 alianzisha Shirika la Mabruda wa Upendo, na mwaka 1976 tawi la maisha ya kitaamuli pamoja na Walei wamisionari waliomsaidia katika kazi yake mahali popote.
Masista wanawashughulikia hasa maskini, kwa kuwatunza wale walioathirika na ukimwi, ukoma, kifua kikuu; kuwalisha wasioweza; kuwalea watoto yatima, n.k. Wanaweka nadhiri tatu za Usafi wa moyo, ufukura na utii. Wanazidisha nadhiri ya nne: “Kuwatumikia bila malipo maskini miongoni mwa maskini“.
Kwa miaka Mama Teresa alishawishiwa vibaya sana. Aliandika: “Bwana alitaka niwe sista huru nikivaa umaskini wa msalaba. Leo nilijifunza. Umaskini wa maskini bila shaka ni mgumu kwao. Ninapotafuta nyumba natembeatembea hadi mikono na miguu yangu inaniuma. Nilifikiri, jinsi gani wanavyoumia kimwili na kiroho, wakitafuta nyumba, chakula na afya. Ndipo, wazo la raha ya Loreto limekuja kunishawishi. ‘Sema neno tu na yote yatakuwa yako tena‘. Mshawishi aliendelea kuniambia. Lakini kwa uhuru kabisa, Mungu wangu na kwa upendo kwa ajili yako, nataka kubaki na kutenda yoyote ambayo ni mapenzi yako kwangu. Sikuruhusu hata chozi moja lianguke chini.“
Upendo wake ulienda kwa watu wote bila kuangalia rangi, ukabila na hali ya maisha. Alizoea kusema: “Kwa damu mimi ni Mwalbania, kwa uraia mimi ni Mhindi, kwa imani mini ni Mkatoliki, tena sista. Kuhusu wito wangu mimi ni mali ya ulimwengu. Kuhusu moyo wangu, mimi ni mali kabisa ya moyo wa Yesu.“ Alikuwa mwanamke aliyejazwa na

mwanga wa Kristo, akiwaka na upendo kwa Kristo na kuwa na hamu tu ya ‘kuzimisha kiu Yake kwa kumpenda na kuwapenda roho za watu.“
Wengi walimsifu sana kwa kazi yake ya upendo. Alipewa tuzo nyingi. Mwaka 1962 alipewa Tuzo la Amani la Ramon Magsaysay na 1979 Tuzo la Amani la Nobel. Lakini alishutumwa na wengine kwa msimamo wako wa kupinga kutoa mimba na hali mbaya ya nyumba za kutunza watu waliokuwa mahututi.
Akafariki tarehe 5 Septemba mwaka 1997, akiwa na umri wa miaka 87. Alitangazwa kuwa mwenyeheri tarehe 19 Oktoba 2003 na Baba Mtakatifu Yohane Paulo II na tarehe 4 Septemba 2016 Baba Mtakatifu Fransiso alimtangaza kuwa Mtakatifu.
Mtakatifu Teresa, utuombee na Mungu atukuzwe ndani mwetu kwa matendo ya huruma. Amina.

**Septemba 6**

Sisi Wakatoliki tunawakumbuka Wat. **Fausto,** padri, na **wenzake 12**, waliouawa wakati wa Kaizari Desio, Valerio akiwa Gavana wa Aleksandria, Misri, mwaka 250.
Pia tunawakumbuka Maaskofu Wat. **Donasiani** na **wenzake 5**, mashahidi, Tunisia, mwaka 484.[33]
Huko Uturuki, Wakatoliki wanamkumbuka Mt. **Onesifori** wa Kirene, mfuasi wa Paulo.[34]
Huko Ethiopia, kumbukumbu ya **Yassai,** Mtakatifu, Mfalme Ethiopia, 6 Septemba.[35]
Huko Kenya, Wakatoliki wanamkumbuka Mtumishi wa Mungu **Morisi Mikaeli Otunga**, Askofu Mkuu wa Nairobi, 2003.

Huko Misri, Wakoptiki wanamkumbuka Mt. **Pisora**, mfiadini, askofu wa Masil.
Waorthodoksi wanawakumbuka **Siriaki**, **Abibo** na **Dionisi** wa Aleksandria na **wenzao 11**, mashahidi, 250. Pia kumbukumbu ya Mt. **Daudi** wa Hermopolis, Misri, mkaa pweke.[36]
Pia kumbukumbu ya Mt. **Yohane wa XIV**, Patriarka wa 96 wa Aleksandria. Huko Ethiopia, Waamini wa Kanisa la Orthodoksi Tewahedo wanamkumbuka padri **Besoi**, shahidi, ndugu wa Mt. Abba Hori. Pia wanawakumbuka Wat. **Pakomi** na **Serapio**.[37]

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake! Amina.

## Wat. Donasiani na wenzake, 484

---

[33] *Martyrologium Romanum,* ed. 2001 na *Acta Sanctorum*. Wanaotajwa pamoja na Padri Fausto: Abibo shemasi, Dionisi alikuwa msomaji, Androniko, askari mmoja, Andropelagia, Siriaki, ambaye alikuwa mtumishi wa altare, Siriaki mwingine, Makari , Theosisti, rubani wa meli, Andrea, Sarapambo, Thekla na Kaldote.
Wanotajwa pamoja na Askofu Donasiani: Prese, Mansueti, Germano, Fuskulo na Laeto
[34] *Acta Sanctorum*. Rejea maisha yake tarehe 7 Septemba.
[35] Dictionary of Saints
[36] *Eastern Orthodox Liturgical Calendar*. Rejea maisha yake on Septemba 12.
[37] *Ethiopian Synaxarium, Pagumen 01*.

Zamani katika karne ya tano, uzushi wa Ario ulilivuruga sana Kanisa, hasa katika Afrika ya Kaskazini. Wakristo wengi, na hata mapadre, waliyakubali mawazo ya Ario ya kwamba Mungu Mwana si wa milele, kwa kuwa wakati ulikuwapo, ambapo Mwana hakuwapo; hivyo walimwona Yesu kuwa mwanadamu tu. Hali ya Kanisa ikawa mbaya zaidi, mfalme mwenyewe alipojiunga na kundi lao. Mwaka 484, mfalme huyo Hunnerik alitoa amri kali sana dhidi ya Wakristo waliokuwa waaminifu kwa Baba Mtakatifu: “makanisa yao yafungwe kabisa, na mali yote ya makanisa hayo pamoja na mali ya mapadre waaminifu imilikiwe na Waario.“

Maaskofu Donasiani, Prese, Mansueti, Germano na Fuskulo walipokataa kabisa mafundisho ya Ario na walipohubiri ukweli wa Kanisa Katoliki, walipigwa vibaya viboko na kufukuzwa mijini mwao hadi jangwani mbali na watu. Na huko walikufa kwa kiu na njaa. Pamoja nao kulikuwa askofu mmoja, jina lake Leto, mtu mshupavu na msomi, aliyechomwa moto akiwa mzima, baadaye ya kufungwa gerezani kwa muda mrefu.

Mt. Donasiani na wenzako, mtuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

## **Mtumishi wa Mungu Morisi Mikaeli Otunga, 2003**.



Morisi Mikaeli Otunga alikuwa Mkenya wa kwanza kuwa askofu mkuu na kardinali katika Kanisa Katoliki Kenya. Baba yake Morisi Mikaeli alikuwa chifu wa Wakhone, kwa jina Wasike Lusweti Sudi Namachanja na mama yake Rosa Namisi, mganga asilia. Alizaliwa tarehe 31 Januari, 1923 huko Chebukwa, Wilaya ya Bungoma, Jimbo la Kakamega, Kenya Magharibi. Inasemekana kwamba baba yake alikuwa ameoa wake wengi zaidi ya mia, ambao sabini tu walikuwa kweli wake zake.

Alipozaliwa alipewa jina la Simiyu linalomaanisha mmoja aliyezaliwa wakati wa kiangazi. Baba yake alimpa jina la Otunga, maana yake gongo lisaidialo mzee au mlemavu. Mama yake alipokuwa na kazi nyingi alikuwa anamlaza mtoto mchanga mahali pa salama. Bila mama yake kutambua, nyoka fulani alizoea kufika na kujivingirisha karibu na

mtoto bila kumdhuru na kuondoka mama yake alipokuwa anakuja. Siku moja mama yake alimwona nyoka. Akaogopa na kujaribu dawa zake zote kumzuia kuja, bure. Mwishoni alipoona kwamba nyoka hamdhuru mtoto, basi akatulia. Na siku moja mgeni akaja akamwita nyoka: “Njoo, tuondoke, umetimiza kazi yako.” Nyoka hakuonekana tena. Baada ya muda mama yake akamweka mtoto wake, aliyekuwa anatambaa, mahali pa salama. Mara akajisikia uwepo wa mtu. Akamwangalia mtoto na kamwona mtu mfupi aliyeshika mtoto, akamwinua juu na kumbariki kadiri ya mila zao: “Ukue, ukue na uwe mtu mshuhuri, lakini kama mimi utakaa peke yako, na utaishi maisha marefu.” Mama yake Namisi akamwuliza: “Wewe nani?” Mgeni akamjibu: “Je, hukuniona nilipokuwa nakuja kumlinda mtoto?” Namisi akamwuliza tena: “Unatoka wapi?” Mgeni akamwashiria Mlima Elgon. Akatoweka.

Otunga alikuwa mtoto mwenye akili sana. Baada ya kumaliza miaka miwili shuleni Sijei aliendelea kujifunza huko Kibabii na Kabaa, shule ambalo liliangaliwa na Mapadri wa Roho Mtakatifu (*Holy Ghost*). Akabatizwa alipokuwa Kibabii, mwaka 1935. Akachukua jina la Morisi. Akasema: “Nilijisikia mtu tofauti wakati nilipobatizwa”. Akapata kipa-imara huko Kabaa, mwaka 1938. Akachukua jina la Mikaeli kwa sababu siku ile ilikuwa sikukuu ya Mt. Mikaeli. Wakati ule Padri mmoja alimwuliza: “Kwa nini usiingie seminari na kuwa padri?” Otunga alishtuka. Alichojua kuhusu mapadri ni kwamba hawaoi. Akamjibu Padri: “Hapana, siwezi. Jambo hilo halipo katika mila zetu”. Lakini neno lilipandwa moyoni mwake na likastawi. Mwaka 1943 akarudi nyumbani wakati wa jando. Wakati wa ibada ya kutahiriwa, baba yake Sudi akamfunika na joho la ngozi ya swala, joho ambalo watu mashuhuri tu wanalovaa. Kwa tendo hilo baba yake alionyesha wazi kwamba Otunga alikuwa mwana wake mpendwa aliyechaguliwa kuchukua nafasi yake kama chifu. Ndipo moyoni mwake kulikuwa mashindano: Padri au Chifu. Mwishoni akaamua na uamuzi wake ulimpeleka mbali katika maisha yake. Akapanda ngazi za hierarkia hatua kwa hatua:

Akaingia seminari ya Kakamega baada ya kumaliza *Mangu High School*. Alimaliza Seminari kuu huko Roma na kupadirishwa kule kule tarehe 3 Oktoba 1950, akiwa na umri wa miaka 27. Baada ya upadirisho wake aliendelea masomo yake katika Chuo cha Kueneza Imani. Alirudi

Kenya na akaanza kufundisha teolojia katika Seminari Kuu ya Kisumu kwa muda wa miaka mitatu. Akafanya kazi pia pamoja na Mwakilishi wa kitume katika nchi ya Kenya.

Tarehe 7 Novemba, 1956 alichaguliwa kuwa askofu msaidizi wa Jimbo la Kisumu. Miaka mitatu baadaye, tarehe 21 Mei, 1960, Baba Mtakatifu Yohane XXIII akamchagua kuwa askofu wa Kisii. Akafanya kazi katika jimbo hilo hadi tarehe 15 Novemba, 1969, alipochaguliwa na Baba Mtakatifu Paulo VI kuwa askofu mwandamizi wa Askofu Mkuu wa Nairobi, John Joseph McCarthy CSSp. Baada ya miaka miwili, tarehe 24 Oktoba, 1971, akawa Askofu Mkuu wa Nairobi. Akaendelea kuhudumia Kanisa Katoliki la Kenya kama Rais ya Baraza la Maaskofu Kenya, pia Kanisa Katoliki la Afrika kama Mjumbe wa tume ya kudumu ya Baraza la Maaskofu wa SECAM, na Rais msaidizi wa Baraza la Maaskofu wa AMECEA. Tarehe 5 Machi, 1973, Baba Mtakatifu Paulo VI akampatia Ukardinali.

Mwaka 1994, katika Sinodi ya Maaskofu wa Afrika huko Vatikano, alitoa makala kuhusu: “Uenezaji wa Injili kwa Haki na Amani”. Alizungumza kwa niaba ya Maaskofu wote wa Kenya, akitetea haki ya raia wanaohamishwa huko na kule, kutafuta kazi, kuteseka kwa sababu ya ubaguzi, n.k.

Mwaka 1997, Otunga alipostaafu akaenda kukaa katika Nyumba ya Wazee, iliyoangaliwa na Masista wa Maskini, huko Nairobi. Katika uzee wake alichagua kuishi kama alivyoishi maisha yake yote, yaani maisha bila kutafuta mambo makuu, kuendesha gari ndogo, kuishi katika nyumba ndogo, n.k. Daima aliwaonya mapadri wake hatari ya unyakinifu ambao ni kizuizi cha kueneza Injili.

Morisi Mikaeli Kardinali Otunga alifariki tarehe 6 Septemba, 2003, akiwa umri wa miaka 80, baada ya kutumikia Kanisa kwa miaka 53, kama Padri, Askofu na Kardinali. Wakenya, wanamkumbuka kama mtumishi mwaminifu na mchungaji aliyeshika kazi kwa moyo. Pamoja na Askofu Mkuu Festo Olang’ wa Kanisa la Anglikana, Otunga anakumbukwa katika historia ya nchi ya Kenya kama Mtume Mkuu na Baba mmoja wa Ukristo katika Afrika.

Anakumbukwa hasa kwa mtindo wake wa uongozi wa ki-unyenyekevu. Alikuwa mnyenyekevu kiasi kwamba watu pengine walichukua unyenyekevu wake kuwa usongombwingo. Chini ya

uongozi wake Kanisa Katoliki likakua kwa kasi, hata kuwa, katika nchi ya Kenya, Kanisa lenye Waamini wengi zaidi. Idadi ya parokia za Jimbo la Nairobi ikaongezeka mara mbili. Kanisa likakua katika uwanja wa kueneza Injili, elimu, afya na haki ya jamii. Akakaza maendeleo ya mtu mzima: ki-mwili, ki-roho, ki-jamii na ki-uchumi. Kwa hiyo Kanisa likatafuta ubora wa shule, hospitali na vyuo katika miradi yake. Alitegemea maongozi ya Mungu: "Hatuna fedha lakini Mungu atatujalia". Pia alijitahidi kufanya ibada za Kanisa ziwe ki-Afrika zaidi, jambo ambalo liliwavuta mkutano mkubwa kukusanya kanisani.

Otunga alikuwa mwungama, mtu ambaye alijua kuwasikiliza watu. Alitatua matatizo kwa dialogia, akipenda zaidi kusahihisha kuliko kutoa adhabu. Alikuwa mtu wa ki-roho, akiishi kwa ajili ya Yesu Kristo. Daima alitabasamu kwa kila mtu. Kwa tabia yake na nguvu za Roho Mtakatifu, aliweza kuwaongoa ndugu zake na wake wengi za baba yake katika Kanisa Katoliki.[38]

Mtumishi wa Mungu Otunga, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

---

[38] Rejea *Cardinal Otunga*, Paulines Publications Africa, 2008.

**Septemba 7**

Huko Saluzzo, Italia, kumbukumbu ya Mt. **Chiafredo**, askari wa Jeshi la Theba, 289.[39]
Huko Kamenge, Bujumbura Kaskazini, Burundi, Wakatoliki wanawakumbuka **Lusia Pulici**, **Olga Raschietti** na **Bernadeta Boggian**, Masista wa Shirika la Wamisionari wa Ksaveri, waliouawa mwaka 2014.

Waorthodoksi wanamkumbuka Mt. **Onesifori** wa Kirene.[40]

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake! Amina.

## Mt. Onesifori wa Kirene, Karne la I

Mtakatifu huyu anaitwa wa Kirene, kwa hiyo tunafikiri kwamba alikuwa mzaliwa wa Kirene, Libya, kama Mt. Simoni Mkirene (Mk 15:21), Lukio Mkirene (Mdo 13:1). Onesifori anahesabiwa kuwa mmoja wa wafuasi 72 wa Yesu. Mt. Paulo anamtaja katika barua zake. Kadiri ya Pokeo aliwekwa kuwa askofu wa Colochon, Asia.
Kitabu cha Watakatifu wa Wagiriki kinatueleza kwamba Onesifori alikuwa ndugu na familia ya Malkia Trifene, akiishi katika mji wa Ikonio. Akamkaribisha Mtume Paulo nyumbani mwake na kwa neema ya Mungu akapokea imani na kubatizwa. Akawajali sana maskini na kumsaidia Paulo alipokuwa amefungwa, kama Paulo mwenyewe anavyosema katika barua yake kwa Timoteo: "*Bwana awape rehema wale walio wa mlango wake Onesifori, maana mara nyingi aliniburudisha, wala hakuuonea haya mnyororo wangu; bali, alipokuwapo hapa Rumi, alinitafuta kwa bidii akanipata. Bwana na ampe kuona rehema machoni pa Bwana siku ile. Na jinsi alivyonihudumu kwa mengi huko Efeso, wewe unajua sana.*" 2 Tim 1:15-18.

---

[39] *Acta Sanctorum*
[40] *Eastern Orthodox Liturgical Calend*

Inasimuliwa kwamba Onesifori, pamoja na mtumishi wake Porfiro, walikamatwa kwa sababu walikataa kuitolea miungu ya uongo sadaka na kuikana imani yao kwa Yesu Kristo. Wakalazwa juu ya vitanda vya chuma na chini wakawasha moto, wakapigwa, wakavunjwa mikono na miguu, lakini msaada wa Mungu na maono ya uzima wa milele viliwakinga na maumivu na kuwafariji katika mateso hayo. Jambo hili liliwakasirisha wapagani. Wakawafunga watakatifu hawa kwa farasi wasiofugwa na wakakokotwa juu ya mawe na miiba. Ndipo wakakata roho na kumsifu Mungu kwa vifo vyao. Wakristo wakachukua masalia ya miili yao na kuyazika kwa kumshukuru Mungu.
Wat. Onesifori na Porfiro, mtuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

## Mt. Chiafredo, Shahidi, 289

Jina la Mtakatifu wetu linaweza kuandikwa kwa namna nyingi: Chiafredo, Theofredo, Ciafrè, Chaffre, Jafredo, Eufredo, Jofredo, Sinfredo na Zafredo.
Inasimuliwa kwamba mnamo mwaka 522, mtu akaanguka kutoka jabali mpaka chini, karibu na Crissolo, lakini hakuumizwa. Wenyeji wanakaanza kusadiki kwamba hakuumizwa kwa sababu ya masalia yaliyochimbuliwa na mkulima. Ilisadikiwa kwamba kufichuliwa kwake maiti kulitokewa kwa sababu ya msaada wa Mungu. Maiti ikaitwa '*San Ciafre*' na kaburi likaheshimiwa sana kuwa mahali pa kuhiji kwa wenyeji wa Crissolo.
Mwaka 1516, wakati wa sinodi, Mheshimiwa Tornabuoni akatangaza Chiafredo kuwa somo wa Jimbo la Saluzzo, Italia. Masalia yake yalipelekwa Revello, mwaka 1593 na mwaka 1642 katika kanisa kuu la jimbo la Saluzzo. Chiafredo huheshimiwa nchi yote ya Piedmont, Italia.
Kadiri ya Pokeo, Chiafredo alikuwa askari mmoja wa Jeshi la Theba. Lakini kuliko kuchinjwa pamoja na askari wenzake huko Agaunum (kwa sasa Uswisi), akatoroka kwenda Piedmont, Italia, na huko akauawa. Mtaalam mmoja, Mwingereza, aliandika kwamba: "Chini ya kivuli cha Mlima Viso, Mt. Chiafredo, mtume wa Jeshi la Theba aliyetoroka, akachukua nafasi ya Eridamo, mungu wa uongo wa mto, aliyeheshimiwa zamani mahali pale."

Mt. Chiafredo, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

## Mauaji ya masista Kamenge, Burundi, 2014

Jumapili, tarehe 7 mwezi wa Septemba, mwaka 2014, masista watatu, Lusia Pulici, Olga Raschietti na Bernadeta Boggian, wa Shirika la Wamisionari wa Ksaveri waliuawa ki-katili huko Kamenge, Burundi. Polisi walimkamata Christian Claude Buto, 33 na kumtia mbaroni wakisema kwamba, huyu aliwaua masista hawa kwa sababu walijenga nyumba zao juu ya kiwanja chake!

Sista Delia Guadagnini, aliyekuwa Sista mkuu, alikanusha habari hiyo, akisema kwamba sababu hiyo ni kwa ajili ya kupotosha uchunguzi. "Hatufikiri kwamba uuaji huo ulitendwa na mtu mmoja. Mungu atahukumu. Sisi tunaendelea katika misioni yetu. Huko Bujumbura, tulipozika masista wetu, tulifarijika kwa kuona watu wengi waliohudhuria, watu wa kawaida kwa wakuu wa serikali. Nitashika nafasi iliyoachwa na masista waliouawa."

Masista 'mashahidi', mtuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

**Septemba 8**

Sisi Wakatoliki tunawakumbuka Wat. **Fausto**, **Dii** na **Amnoni** (*Amnonius*)**,** wote wafiadini Aleksandria, pamoja na Mt. **Petro** askofu.[41]
Huko Angola, kumbukumbu ya **Augustino Geve**, Padri, aliyeuawa, mwaka 2002.

Wakoptiki wanamkumbuka Mt. **Basilide** (Basilides, Wasilides), mfiadini, Misri.[42] Kumbukumbu ya Mt. **Panefisis**, bikira. Pia kumbukumbu ya Mt. **Kornelio** wa Kaizaria.
Huko Ethiopia, Wakristu wanamkumbuka Mt. **Serapio** wa Landun (*sindonite*). **Zara Ya'akob**, mfalme wa Ethiopia, 1468.[43]

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake! Amina.

## Mt. Kornelio wa Kaizaria,

Wakoptiki wa Misri wanamkumbuka leo Mt. Kornelio, aliyeishi wakati wa Mitume. Kama tunavyosoma katika Matendo ya Mitume, alikuwa "*akida wa kikosi kilichoitwa Kiitalia, mtu mtauwa, mchaji wa Mungu, yeye na nyumba yake yote, naye alikuwa akiwapa watu sadaka nyingi, na kumwomba Mungu daima*" Mdo 10:1-2. Malaika wa Mungu akamtokea na kumwomba kumwamuru Mtume Petro afike nyumbani mwake kumwambia yampasayo kutenda. Petro akaenda kwake na kuwaambia wale waliokusanyika nyumbani mwake maneno ya Bwana. Kornelio akaamini na kubatizwa, pamoja na watu wake wote.
Kanisa Katoliki, linalomkumbuka tarehe 2 Februari, linaamini kwamba, baada ya kubatizwa, Mtume Petro akamweka kuwa askofu wa mji Kaizaria. Baada ya kuongoza Kanisa la Kaizaria kwa muda, Kornelio

[41] *Martyrologium Romanum,* ed. 2005. Waliouawa pamoja nao: Theofilo, Neoterio, Serapio, Pio, Nemesio, Ario, Savino (au Sabino), Demetrio, Didimo, Mitisoro, Paneti, Achile, Isidori, Magita, Oroseo, Silvano, Arapio, Severo.
[42] *Coptic Synaxarium*: 11 Tute
[43] *The Ethiopian Rite Missal, Abba Emmanuel & Abba Brendan Cogavin, 2002, uk 332. Ethiopian Synaxarium, Pagumen 03.*

alilikabidhi Kanisa la Kaizaria kwa Theofilo, ambaye akawa askofu wake wa tatu. Yeye, Kornelio akaenda katika Asia ya Kati na kuihubiri Injili huko Scepsis. Akafanya mwujiza mkubwa kule, kwa kubomoa hekalu la miungu ya uongo, na kuwaongoa watu wengi. Akafariki kule kwa amani.

Wakoptiki wanaamini kwamba, Kornelio baada ya kubatizwa, Mtume Petro akamtuma aende mjini Aleksandria. Alipofika akakuta wakazi wengi wa mji ule wakiwaabudu miungu ya uongo. Akawabatiza wengi. Gavana Demetrio akaamini, yeye na watu wote wa nyumbani mwake. Kornelio akaishi maisha yake yote kama Mitume walivyoishi. Ndiye mpagani wa kwanza kumwamini Yesu Kristo.[44]

Mt. Kornelio, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

## Mt. Basilide, Mfiadini, mnamo 204

Tunasoma katika Kitabu cha Watakatifu wa Wakoptiki habari ifuatayo:

Basilide alikuwa waziri na mshauri wa Kaizari wa dola la Roma. Alikuwa na watumwa na watumishi wengi. Numeriani, Kaizari wa Roma alimwoa Patrisia, dada ya Basilide. Akamzalia mwana mmoja aliyeitwa Yusto. Patrisia alikuwa pia mama wa Theodori El-Mishreke. Naye Basilide alikuwa na wana wawili Eusebio (Awsabyos) na Makari.

Wapersi walipoanza vita na Warumi, Kaizari Numeriani alimtuma mwana wake Yusto, pamoja na Eusebio, mwana wa Basilide, kupigana nao. Yeye mwenyewe aliendа kupigana na adui mwingine. Akauawa vitani. Dola la Roma likabaki bila mtawala. Watu wakamchagua kati yao, mtu mmoja aitwaye Agripita. Alikuwa mchungaji na mtunzaji wa farasi wa Kaizari. Alikuwa mtu mwenye nguvu, hodari katika kazi, mjanja katika mapatano. Mmojawapo wa binti wa Kaizari akamtamani na akamchukua kuwa mume wake. Akamkalisha kuwa Kaizari na kumwita 'Dioklesiani'. Muda si muda alimwasi Bwana na kuiabudu miungu ya uongo.

Basilide aliposikia habari hizo alisikitika na hakutaka kurudi kumtumikia Kaizari. Na wakati ule Yusto, mwana wa Numeriani na Eusebio, mwana wa Basilide, wakarudi kama washindi juu ya maadui wa Dola. Walipoona kwamba Kaizari aliasi imani yake wakajaa na

---

[44] *Synaxarium Arabic-Jacobite*

uchungu. Wakataka kumwua Dioklesiani kwa upanga na kumtawaza Yusto, mrithi wa haki. Lakini Basilide akawazuia kutenda jambo hilo. Akakusanya jeshi lake na watumwa wake na kuwaambia kwamba yupo tayari kufariki kwa ajili ya Jina la Yesu Kristo. Wote wakamjibu: "Tutakufa pamoja nawe". Wakasimama mbele ya Dioklesiani aliyewaogopa sana. Ndipo baba wa Viktori alimshauri Dioklesiani kuwahamisha wote katika nchi ya Misri na kuwatesa. Dioklesiani akawatuma kila mmoja katika mkoa tofauti: Abadir (Apater), Erace (Herais) dada yake, Eusebio, Makari, Klaudio na Viktori. Yeye Theodori El-Mishreke alipigiliwa juu ya mti kwa misumari.
Alimtuma Basilide kwa Masro, Gavana wa Pentapolis. Masro alipomwona, akashangaa kwa nini aliacha ufalme na utukufu wake. Bwana Yesu Kristo aliwatuma malaika wake na kumwinua hadi mbinguni kwa Roho Mtakatifu na kumwonyesha makao huko. Roho yake ikafurahi, akatiwa nguvu. Baadhi ya watumwa wake, wengine waliachiliwa uhuru wengine waliteswa pamoja naye. Basilide alivumilia mateso mengi. Mara akalazwa juu ya kitanda cha chuma (*himbazeen*) na kubana kwa nguvu, mara mwili wake ukachanuliwa na chanuo la chuma. Wakati wengine aliinuliwa juu na kutupiliwa juu ya kitanda cha chuma kilicho na moto sana. Masro hakuacha njia moja ya kumtesa lakini Basilide akabaki imara katika imani yake. Basi Masro akaamuru akatwe kichwa.
Mtakatifu Basilide na wenzako, mtuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

**Septemba 9**

Sisi Wakatoliki tunamkumbuka Mt. **Petro Klaveri**, Padri.[45]
Huko Ethiopia, Wakatoliki wanamkumbuka **Poemen** wa Shete.[46]
Huko Misri, Wakatoliki wanamkumbuka Mt. **Dorotheo**, mkaa pweke, Theba, Misri.[47]
Katika Kisiwa cha Morisi, Wakatoliki wanamkumbuka Mwenyeheri **Yakobo Désiré Laval**, 1864.
Huko Yamboyo, Jamhuri ya ki-demokrasia ya Kongo, Wakatoliki wanawakumbuka **Yakobo Brits** (*Bruda Hugo*) wa Shirika la Mill Hill, **Jeni Delporte** (*Sista Marie-Loyola*), **Sesilia Barbaix** (*Sista Raphaël*) na **Maria Valerberghe** (*Sista Marie-Chantal*) wa Shirika la O.L. Vrouw-ten-Bunderen, waliouawa na waasi WaSimba, mwaka 1964.
Huko Gitega, Burundi, Wakatoliki wanawakumbuka **Yoakimu Ruhuna**, Askofu Mkuu, na **masista wawili**, waliouawa mwaka 1996.
Huko Uije, Angola, Wakatoliki wanamkumbuka **Abrao**, Mseminari wa Wakapuchini, aliyeuawa mwaka 1998.

Waorthodoksi wanamkumbuka Mt. **Poemen** wa Shete.[48]
Huko Ethiopia, Waorthodoksi Tewahedo wanamkumbuka Mt. Abba **Benyamini** (*Baymon*), wa mji wa Mesr, Kairo.[49]

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake! Amina.

## Mt. Dorotheo, mwisho wa karne la IV

Dorotheo alikuwa mtawa katika mkoa wa Theba, karne la IV. Hatuna habari sana kuhusu mtawa huyu. Palladio, askofu wa Helenopolis, alikuwa mfuasi wake kwa muda, wakati Dorotheo alipokuwa mzee. Anasemekana kwamba aliishi pangoni kwa miaka 60.

---

[45] *Martyrologium Romanum,* ed. 2001
[46] *The Ethiopian Rite Missal, Abba Emmanuel & Abba Brendan Cogavin, 2002, uk 332.*
[47] *Les petits Bollandistes*
[48] Rejea Orthodox Saints of the day.
[49] *Ethiopian Synaxarium, Pagumen 04.*

Palladio anatusimulia kwamba hakuweza kukaa kama mfuasi wake kwa sababu ya afya yake. “Ukikaa naye“, Palladio anatuambia, “unakaushwa na joto kali ya jua na mwili wako unakauka. Mchana kutwa, chini ya jua kali, Dorotheo anaokota mawe jangwani ili kuwajengea vijumba watawa wasioweza kufanya hivyo. Kila mwaka anamaliza kijumba kimoja. Mara moja nilimwambia: ‘Unamaanisha nini baba, kwa umri ulio nao, kujaribu kuua mwili wako maskini katika joto kali hiyo?‘ Akanijibu: ‘Mwili wangu unaniua, na mimi ninauua‘. Alizoea kula kila siku wakia sita za mkate na kicha cha mboga, na kunywa kadiri yake. Mungu ni shahidi wangu, sikumwona hata mara moja akinyosha miguu yake, wala kwenda kulala juu ya mkeka, au kitanda. Bali alikuwa anaketi usiku kucha na kusuka kamba ya makuti ili kujipatia chakula. Nilipofikiri kwamba alifanya hivyo kwa ajili yangu, niliwauliza wafuasi wake wengine walioishi peke yao na nilihakikisha kwamba lilikuwa zoezi lake tangu ujana wake. Kwa kusudi hakuenda kulala. Anapofanya kazi au anapokula, macho yake yanafungwa kwa kuwa anashindwa na usingizi. Mara nyingi akichukuliwa na usingizi alipokula, kipande cha chakula kilidondoka kutoka kinywa chake. Mara moja nilimsihi apumzike kidogo juu ya mkeka, akaudhiwa na kuniambia: ‘Ikiwa unaweza kuwalazimisha malaika kulala, utafaulu kumlazimisha pia mtu mwenye wivu kwa Mungu.‘

Siku moja, saa tisa, akanituma kuchota maji kisimani mwake kwa kuzingatia chakula saa tisa. Kweli, nikaenda. Nikaona kipili sehemu ya mwisho wa kisima. Niliacha kuchota maji, nikarudi na kumwambia: ‘Sisi tu watu wafu, baba, kwa sababu niliona kipili kisimani.‘ Yeye akatabasamu na aliponiangalia akaniambia: ‘Ikiwa Shetani aliamua kujibadilisha kuwa nyoka au kobe katika kile kisima na kuanguka katika akiba ya maji yetu, je, utaacha kunywa maji daima?‘ Akaondoka na kuchota maji yeye mwenyewe. Akawa wa kwanza kunywa maji haya na kusema: ‘Mahali popote msalaba unapopita uovu wa kiumbe hauna nguvu‘.

Mt. Dorotheo, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

## Mt. Petro Klaveri, Padri, 1654.

Ingawa Mtakatifu huyu hakukanyaga bara la Afrika hata mara moja, bali alifanya kazi Marekani wa Kusini, Baba Mtakatifu alimweka awe msimamizi wa kila kazi ya umisionari kati ya Waafrika.

Petro Klaveri alizaliwa mwaka 1582 katika nchi ya Hispania. Alipokua, aliingia shirika la Wayesuiti. Alijipanga urafiki na Bruda mmoja, jina lake Alfonsi Rodriges, aliyekuwa mngoja mlango wa monasteri. Huyu bruda mtakatifu alimwagulia Petro Klaveri kuwa atawaongoza watu wengi kwa Mungu. Wakuu wake Petro walimpa ruhusa kwenda katika misioni za Marekani ya Kusini. Alipanda merikebu akasafiri mpaka Marekani, mwaka 1610, na hakurudi tena nchi yake ya Hispania.

Huko Marekani akakaa katika mji wa Kartagena, nchi ya Kolombia. Zamani zile watu wa Kartagena walikuwa wakifanya biashara ya watumwa waliotoka Afrika. Hawa watumwa maskini walipakiwa merikebuni bila kitanda, wala mavazi; na chakula chao kilikuwa ni kidogo sana. Walifungwa wote pamoja kwa minyororo. Hawakuwa na nafasi ya kujilaza chini. Wengi waliugua, wakawa na majipu na madonda mwilini. Basi, padri Petro Klaveri, kila mara alipokuwa akisikia merikebu yenye watumwa imeingia bandarini, alikimbilia huko kwenda kuwagawia vyakula, mavazi na tumbako; aliwafunga vidonda vyao na kuwatunza kama vile anavyotunza watoto wake.

Kwa siku za Mungu na sikukuu nyingine alikwenda kuwatafuta kila mahali, shambani na mashimoni walimofanya kazi, na kuwaleta kanisani wapate kushiriki ibada ya Misa na kuyasikiliza mafundisho ya dini. Hakuchoka kuungamisha. Wakati wa mafungo alikuwa akiungamisha toka jogoo la kwanza mpaka adhuhuri. Saa nane alirudi kuwaungamisha wanawake mpaka usiku. Mara kwa mara padre huyu mtakatifu alichoka sana kiasi cha kutaka kuzimia. Aliporudi nyumbani kwake, alikula kidogo, kisha alianza kusali. Inasemekana ya kwamba padre Petro Klaveri amewabatiza Waafrika wapatao 30.000 na zaidi.

Inasikitisha kusoma kwamba kwa miaka minne ya mwisho wa maisha yake alikuwa mlemavu, akalazwa chumbani mwake, na mtumishi Mwafrika wa monasteri, aliyepewa jukumu la kumtunza Petro, mara kwa mara alisahau wajibu wake wa kumtunza vizuri. Lakini padri hakulalamika, alizoea kusema: “Ninastahili adhabu kubwa zaidi kuliko

hiyo kwa sababu ya dhambi zangu". Alifariki mwaka 1654. Toka siku ya kufa kwake hakusahauliwa tena. Walipofungua kaburi lake, mwaka 1657, waliukuta mwili wake mzima, haukuoza hata kidogo. Alitangazwa kuwa mtakatifu mwaka 1888 pamoja na rafiki yake bruda Alfonsi Rodriges.[50]
Mtakatifu Petro Klaveri, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

## **Mwenyeheri Yakobo Laval, 1864**.

Yakobo Laval alikuwa mmisionari wa Kanisa Katoliki katika kisiwa cha Morisi. Alizaliwa Ufaransa. Akafuata shule na kuhitimu kama daktari, mwaka 1830. Mwaka 1835, akapata ajali ya farasi, na jambo hilo lilimsaidia kuongoka. Akapadirishwa mwaka 1838. Akaanza kufundisha katika Seminari ya Mt. Sulpisi, Paris, na huko akakutana na Padri Fransisko Libermann, mwanzilishi wa Shirika la Moyo Mtakatifu wa Maria. Baada ya miaka mitatu ya kazi parokiani Ufaransa, akatumwa na Libernann huko kisiwa cha Morisi ili kuwahubiria Injili watumwa watokao bara la Afrika. Padri Yakobo alifaulu kuwasaidia Wakatoliki waliokuwa watumwa kuishi maisha yao ya ki-kristo. Kwanza, alitumia katekisimu katika lugha ya Kikrioli; Pili, aliwafundisha makatekista; Tatu, kuwatayarisha wanawake kuwa washauri. Pia, aliunda mfuko wa fedha kuwasaidia maskini uliosimamishwa na wenyeji wenyewe. Akaanzisha vigango vingi kuwahudumia waamini wao ki-roho kwa urahisi. Kwa sababu ya jitihada zake, dini Katoliki ilienea mahali pengi katika kisiwa cha Morisi. Akafariki tarehe 9 Septemba, 1864. Wakatoliki wengi wanahiji mahali alipozikwa.[51]
Baba Mtakatifu Yohane Paulo wa II alimtangaza kuwa Mwenyeheri, tarehe 24 April 1979, akiwa wa kwanza kati ya Wakristo 1340 waliotangazwa naye kuwa Wenyeheri au Watakatifu.
Mwenyeheri Yakobo, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

---

[50] Rejea maisha yake katika kitabu 'Maisha ya Watakatifu'.
[51] Rejea *Biographical Dictionary of Christian Missions* (DACB)

**Septemba 10**

Sisi Wakatoliki, tunawakumbuka Wat. **Nemesiani** (wa Thubune) **na wenzake.**[52] Kwa sababu ya dhiki kubwa wakati makaizari Valeriani na Gallieni walipotawala, walipigwa kwa mijeledi, waliwekwa juu ya gurudumu la chuma, na kutumwa kufanya kazi katika magodi. Walimaliza maisha yao kwa kumfia Yesu Kristo, mnamo mwaka 260.
Huko Afrika ya Kaskazini, kumbukumbu ya Wat. **Katulo** (*Doletatulus*), **Tusko, Valentino** na **Magaro**, wafiadini.[53] Pia, kumbukumbu ya Mt. **Paulino mdogo**, aliyeteswa wakati wa utawala wa Genserik, mfalme wa Waharabu, mwaka 437.[54] Kumbukumbu ya Mt. **Karmondika**, mwanamke, mkaapweke, Misri.[55]
Huko Peramiho, Tanzania Wakristu wanamkumbuka **Fransisko** (*Franziskus*) **Leuthner**, Padri, Osb, aliyeuawa na Majimaji, Ungoni, mwaka 1905

Huko Misri, Wakoptiki wanamkumbuka Mt. **Mathayo II**, Patriarka, askofu wa 92 wa Aleksandria.[56]
Huko Ethiopia, Wakristu wanawakumbuka Mt. Abba **Yakobo**, askofu wa mji wa Mesr, Kairo, Misri; Mt. Abba **Barsuma**, aliyeishi uchi.[57]
Waorthodoksi wanamkumbuka Mt. **Lukio** wa **Kirene**, karne la I.

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake! Amina.

## Mt. Nemesiani na wenzake, mnamo 260.

---

[52] *Martyrologium Romanum,* ed. 2005. Pamoja na Nemesiani tunakumbuka: **Feliksi** (wa Bagaie)**, Lusio** (Membrèse)**, Feliksi** (wa Utine), **Liteo** (wa Gemelles)**, Poliani** (wa Miliève)**, Viktori** (wa Assur)**, Yaderi** (wa Midile)**, Dativo** (wa Bade), maaskofu, **Ammoni**, na **Wenzao** mapadre na mashemasi.
[53] *Acta Sanctorum.* Majina ya Katulo, Tusko, Valentino na Magaro yameandikwa katika martirolojia ya Mt. Hieronimo.
[54] *Les petits Bollandistes*.
[55] Dictionary of Saint.
[56] *Coptic Synaxarium: 13 Tute*.
[57] *The Ethiopian Rite Missal, Abba Emmanuel & Abba Brendan Cogavin, 2002, uk 332. Ethiopian Synaxarium, Pagumen 05.*

Wakati wa dhiki ya Kaizari Valeriani na Gallieni, Mt. Sipriano, askofu wa Kartago alihamishwa Curubis, na wakati ule Liwali wa Numidia[58], alianza kuwatesa Wakristo, kwa kuwaua kikatili au kuwahamisha kufanya kazi katika magodi au katika machimbo ya marumaru. Maaskofu Nemesiani, Felisi wa Bagaie, Lusio, Felisi wa Utine, Liteo, Poliani, Viktori, Jaderi, Dativi, na Mapadri na Mashemasi wenzao, walipigwa viboko walipokaa juu ya vyuma na baadaye walitumwa kufanya kazi ngumu katika magodi. Kati yao wengine waliitwa tena na tena na kupigwa na kuchinjwa kama wanyama. Wengine walikufa kwa sababu ya njaa, kiu, baridi, kazi ngumu, michapo na matusi.

Mt. Sipriano aliwaandikia kutoka mahali alipohamishwa ili kuwatia moyo na kuwafariji walioteswa kwa ajili ya imani yao: "Kwa moyo na roho nipo pamoja nanyi, na barua yangu iwe kwa niaba ya midomo yangu, kuwapelekea furaha ya roho yangu kwa ajili ya utukufu wa fadhila zenu, na ushirika ninao, siyo ushirika wa mateso yenu, bali ushirika wa upendo. Siwezi kukaa kimya nikisikia mambo ya utukufu mnayotenda, ndugu zangu, kwa neema ya Mungu. Kati yenu wengine wamekwisha vishwa taji la ushahidi, wakati wengine waliofungwa kwa minyororo, au kukaa magodini, na kwa kusubiri kwao kuvishwa taji, wanawatia moyo ndugu waliobaki nyuma kutamani kupata taji la utukufu."

Mt. Sipriano aliendelea kuwatia moyo kwa barua yake. Aliwahakikisha kwamba taji zao zitazidishwa na zile za wale wote ambao, kwa ujasiri wao, watafuata fadhila zao. Alisema: "Idadi kubwa ya walei wamefuata mfano wenu, wamekiri Bwana wetu, na wanasimama wakisubiri pamoja nanyi taji la utukufu na kuunganika nanyi katika kifungo cha upendo. Hawakubali kutengwa na maaskofu wao waliopo magodini au gerezani. Pia kuna kundi la mabikira, wanaoelekea kupata taji la utukufu, kwa cheo la bikira na shahidi. Hata ujasiri wa watoto ulipita umri yao. Kwa hiyo kundi lenu la mashahidi limepambwa kwa watu wa kila umri na jinsia."

Mashahidi hao walimshukuru Mt. Sipriano kwa barua yake. Walisema kwamba barua ilisaidia kubeba mapigo na mateso yao na kutojali kelele za watu zilizojaa mahali pale. Wakamwambia kwamba kwa kumkiri

[58] Aljeria Mashariki ya siku hizi.

kwake Yesu mbele ya Liwali na kwenda kabla yao katika uhamisho, aliwapatia moyo wao askari wa Mungu, katika vita vyao. Walimaliza kuomba sala zake na kusema: “Tuombeane, ili Mungu na Kristo, pamoja na Malaika wote, watujalie msaada wao tutakaouhitaji.” Wakafariki huko, Aljeria, mnamo mwaka 260.
Mt. Nemesiani na wenzake, mtuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

**Septemba 11**

Sisi Wakatoliki, tunawakumbuka Wat. **Proto** na **Hiasinto**, matowashi, ndugu wa tumbo moja, wazaliwa wa Misri. Walimsindikiza Mt. Eugenia aliporudi Roma. Na huko walifia dini, Karne la III. Huko Uswisi, tunawakumbuka Wat. **Feliksi** na **Regula**, wa Jeshi la Theba[59] na **Eksuperansio**, mtumishi wao. Walifia dini huko Zürich, mnamo 286. Feliksi na Regula ni somo la mji Zürich. Pia tunamkumbuka Mt. **Pafnusi Mkuu**, askofu, Misri.[60]
Huko Aleksandria, kumbukumbu ya Mt. **Theodora**, ambaye, alipotenda dhambi kwa ujinga, akatubu na kwenda kujificha kama mtawa na kufanya matendo ya toba na majikanio kwa uvumilivu mkubwa, mpaka kufa kwake.[61]
Pia huko Aleksandria, Misri, kumbukumbu za Wat. **Siro** na **Serapio**, wafiadini.[62]
Huko Kenya, Washirika wa Mabruda wa Mt. Martin wa Porres wanamkumbuka mtu wa Mungu **Bruda Gabrieli**, 1966.[63]

Huko Misri, Wakoptiki wanamkumbuka Mt. **Agato** mkaa mnarani.[64].
Waorthodoksi wanamkumbuka Mt. **Eufrosino**, mpishi.
Huko Ethiopia, Wakristu wanasherehekea sikukuu ya Mwaka Mpya. Ni siku ya kwanza ambayo, huko Misri na Ethiopia, mchana na usiku ni sawa, mchana masaa 12 na usiku masaa 12. Kuanzia siku hiyo Jua linachelewa kutoka. Na wanakumbuka Mt. **Bartolomeo** mtume, na Malaika Mkuu **Ragueli**. Waamini wa Kanisa la Waorthodoksi Tewahedo wanawakumbuka Mt Abba **Melyos**, askofu wa tatu wa Aleksandria; Na Mt. Abba **Melki**.[65]

---

[59] *Martyrologium Romanum,* ed. 2005.
[60] *Martyrologium Romanum,* ed. 2001.
[61] *Roman Martyrology*, ed. 1956. Mt. Theodora anakumbukwa, huko Ethiopia, tarehe 21 Septemba.
[62] *Les Petits Bollandistes*. Wafiadini hawa Syr a Serapion wametajwa katika martirolojia ya Mt. Hieronimo
[63] Rejea kijitabu kilichoandikwa na Pd. John Marengoni MCCJ, *Brother Gabriel*, St. Paul Publications, 1987.
[64] *Coptic Synaxarium: 14 Tute*. Mtakatifu huyu hatajwi katika Martirolojia ya Roma.
[65] *The Ethiopian Rite Missal, Abba Emmanuel & Abba Brendan Cogavin, 2002, uk 163. Ethiopian Synaxarium: Meskerem 01.*

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake! Amina.

## Mt. Pafnusi Mkuu, aksofu, 356

Wakati wa utawala wa Kaizari Galerio Maksimini, Pafnusi aliteswa kwa kung'olewa jicho lake la kulia, kukatwa kiungo cha mguu wa kushoto na kuhukumiwa kufanya kazi katika machimbo ya marumaru. Baadaye, wakati wa utawala wa Kaizari Konstantino aliwapinga wafuasi wa Ario kwa kuitetea imani ya Kanisa Katoliki, hadi kifo chake, 356 B.K. Inasemekana kwamba alimsindikiza Mt. Atanasi kuhudhuria Mtaguso wa Tiro, mwaka 335. Alipomwona upande wa Waario, kati ya maaskofu waliokusanyika, Maksimo askofu wa Yerusalemu, aliyeteswa kwa ajili ya Yesu Kristo, alimchukua pembeni na kumweleza kinaganaga kuhusu njama za Waario ambazo hakuzifahamu. Tangu siku ile Askofu Maksimo alikaa katika imani Katoliki.
Mt. Panufsi, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

## Maisha ya Mt. Theodora, Mtubu, 477 au 491.

Zamani za Zeno, Rais wa Roma, Mt. Theodora na mume wake waliishi Aleksandria, mji mkuu wa Misri wakati ule. Upendo na amani vilitawala familia yao, na hiyo ndiyo ilisababisha chuki kubwa ya Adui wa wokovu. Kuongozwa na Shetani mtu tajiri, Shujaa, alihangaishwa na uzuri wa Theodora na akaanza, kwa kutumia mbinu zake zote, zawadi na barua, kumtongoza ili azini naye. Kwa muda mrefu hakufaulu. Mwishoni akamhonga mwanamke wa sifa mbaya, akamwahidia zawadi kubwa akifaulu kubadilisha nia yake. Basi mwanamke huyu akamwendea Theodora na kusihi kumhurumia mtu huyu tajiri na kukubali kutimiza haja yake. Theodora akamjibu kwamba Mungu anaona kila kitu na hayupo tayari kutenda dhambi kubwa kama hiyo. Basi mwanamke akamdanganya Theodora kwa kumwambia kwamba dhambi iliyotendeka sirini, ambayo Jua haliioni, (yaani jamii haliijui) ni

dhambi Mungu haijui.[66] Theodora akamwuliza, “Unaniambia kweli ?” “Ndiyo nakuambia ukweli”, mwanamke akamjibu. Basi Theodora alipodanganywa akakubali. Akamwambia mwanamke : “Mwanaume huyu afike usiku huu nitakubali kutimiza hamu yake.” Mwanamume akafurahi, akafika saa alipoambiwa na kutimiza haja yake. Theodora akamsaliti mume wake. Lakini mara akajitambua na alipoona ubaya wa kosa lake, akakasirika, akajipigapiga na kuchana nywele zake. “Ole wangu, nimepotea, nimeharibu uzuri wa jina langu.” Mume wake akaingia, akamwona mke wake akilialia. Akataka kujua sababu ya huzuni yake, lakini hakutaka kumwambia. Usiku kucha dhamira yake haikumpatia amani.

Asubuhi mapema akaenda kwa Mama Mkuu wa konventi, akamwuliza ikiwa Mungu anajua dhambi yoyote iliyotendeka usiku. Mama Mkuu akamjibu kwamba hakuna kitu kilichofichika kwa Mungu. Theodora akalia sana, akamwambia yote. Mama Mkuu alipoona kwamba Theodora anaonyesha toba kweli, akamweleza msamaha wa Mungu na kumkumbusha dhambi ya uzinzi ya mwanamke aliyeosha miguu ya Yesu kwa machozi yake na kupokea kutoka kwake msamaha wa dhambi zake.[67] Kwa kutamani huruma ya Mungu, Theodora akasema: “Namwamini Mungu wangu, na tangu saa hii, sitatenda dhambi ya namna hiyo, na nitajitahidi kumlipia kosa.”

Muda si muda, siku moja mume wake alipotoka, akakata nywele zake, na akivaa mavazi ya mume wake akaondoka kisirisiri, akaenda kwa monasteri[68], umbali wa kilomita 30 na nyumba yake, kwa sababu aliogopa kwamba mume wake atamtafuta katika konventi.

Abate, ili kumjaribu kandidati mpya, hakutaka hata kumbariki kwa kuingia uani. Basi usiku ule Theodora akalala kwenye mlango. Asubuhi mapema, akamwangukia magotini mwa Abate na kumwambia kwamba jina lake lilikuwa Theodoro kutoka Aleksandria. Akamsihi aingie monasteri ili atubu na kufanya kazi. Alipoona nia yake nzuri, Abate akakubali. Theodora akafurahi na mara akaanza kufuata sheria zote za

---

[66] Waislamu wanasadiki kwamba Allah hakiona kile ambacho Jamii hakioni. Kwa hiyo kuzini kunachotendeka sirini si dhambi.

[67] Rejea Lk 7:36-50

[68] Monasteri ni nyumba ya watawa wanaume kwa wanawake lakini konventi ni nyumba ya watawa wanawake tu.

monasteri kwa bidii sana. Hata watawa walioishi humo miaka mingi, wakashangaa kumwona Theodoro akikesha usiku mzima magotini, na kuona unyenyekevu wake, saburi yake na kujikana kwake. Mtawa Theodoro akafanya kazi kwa miaka minane. Mwili wake, ulionajisiwa siku moja kwa dhambi ya uzinzi, sasa ulianza kuwa chombo cha neema ya Mungu, na hekalu la Roho Mtakatifu.
Theodoro alizidi kukua katika utakatifu. Akafanya miujiza mingi. Kwa sala zake akamwokoa mwanamume mmoja aliyeraruliwa na mnyama wa pori. Akamlaani mnyama, na mara moja mnyama yule akaanguka na akafa. Shetani hakuweza kuvumilia utakatifu wake. Akamtokea na kumwambia : "Wewe Malaya kuliko wote, mzinzi, umemwacha mume wako na kufika hapa kunidharau. Kwa nguvu na uwezo wangu nitakupiga vita na kukufanya kwamba utamkana Yesu Kristo msulibiwa." Theodoro akafanya ishara ya msalaba, na mara Shetani akatoweka.
Siku moja alipotumwa kutafuta chakula mjini, baada ya kumbariki kwa ajili ya safari yake, Abate akamwambia, "Kama unachelewa, basi ulale katika monasteri huko Enata, ambayo iko njiani." Kumbe mtoto wa Abate wa monasteri ile alikuwa pia katika nyumba ya wageni ya monasteri. Alifika kumtembelea baba yake. Alipovutwa na uzuri wa mtawa huyu, akajaribu kumtongoza Theodoro kwa dhambi ya uasherati, asijue kwamba ni mwanamke anayekaa mbele yake. Alipokataliwa basi akaenda kuzini na mgeni mmoja aliyekuwa pia katika nyumba hiyo ya wageni. Akapata mimba. Wakati ule Mtawa Theodoro akarudi nyumbani na kuleta vyakula.
Baada ya muda, baba yake msichana huyu akatambua kwamba ana mimba, akaanza kumhoji ili kujua baba ya mtoto ni nani. Msichana huyu akamwambia baba yake kwamba ndiye Mtawa Theodoro. Mara moja, Abate wa monasteri ya Enata akampasha habari Abate wa monasteri ambayo Theodoro alikuwa anajitahidi kwa kufanya toba. Abate akamwita na kumweleza Theodoro. Mtakatifu akamjibu: "Mungu awe shahidi wangu, sikufanya tendo hilo." Abate akijua usafi wa moyo na utakatifu wa Theodoro hakuamini mashtaka haya. Muda ukapita, msichana akajifungua, mtoto wa kiume. Punde si punde Watawa wa Enata wakamleta mtoto kwenye monasteri Theodoro alipokaa. Wakaanza kumkaripia mtawa Theodoro kwa sababu ya uzinifu wake.

Wakatumia maneno mengi kwa nguvu nyingi, hata Abate wa Theodoro akaanza kuamini maneno ya watawa wa Enata na kumkasirikia. Wakamkabidhi Theodoro mtoto na kumtupa nje ya monasteri, kwa aibu. Akakaa karibu na monasteri akijilisha na majani na kumlisha mtoto na maziwa wachungaji waliyomletea.

Baada ya miaka saba, kwa ruhusa ya Abate, akarudi kuishi katika nyumba ya watawa, pamoja na mtoto. Siku moja, Abate akaangaziwa na Mungu kwamba dhambi ya mtawa Theodoro imesamehewa. "Neema ya Mungu i juu ya mtawa Theodoro, na karibuni hivi, watawa wote watashuhudia kazi zinazotendwa kwa njia ya sala ya Mtakatifu huyu." Kweli Theodoro akafanya miujiza mingi katika monasteri.


Kabla ya kifo chake, Mtakatifu Theodoro akajifungia ndani ya chumba chake, pamoja na mtoto. Abate alipopata habari akamtumia mtawa kusikiliza anachosema. Mtawa akaingia na akamsikia Theodoro akimfundisha mtoto kumpenda Mungu kuliko mambo yote. Akamwambia pia kumtii Abate na watawa, ili kukaa katika amani, kuwa mpole na bila hila, kuepuka upujufu na upuuzi, kutotamani, na kutokosa sala za pamoja. Baada ya hayo, akasali na kwa mara ya mwisho akamwomba Mungu amsamehe dhambi zake. Mtoto akasali pia pamoja naye. Mara maneno ya sala yake yakafifia midomoni mwake, na kwa amani akaaga dunia kuelekea makao bora. Ilikuwa mwaka 460.

Usiku ule Bwana Mungu akamfunulia Abate katika maono, mambo yote mtakatifu Theodora aliyoyafanya, na pia siri yake. Abate, ili kuondoa aibu juu ya Theodora, mbele ya Abate wa monasteri ya Enata na watawa wake wote, akawaambia maono yake. Alipomaliza maneno yake, akavua nguo iliyofunika maiti ya Theodora, na wote wakathibitisha kwa macho kwamba yeye alikuwa mwanamke.

Abate wa monasteri ya Enata na watawa wote wakahangaika wakikumbuka makosa yao. Wakamwangukia maiti ya mtakatifu kwa machozi na kumwomba msamaha. Habari za kifo cha Theodora zikamfikia mume wake wa zamani. Akafika kuhudhuria mazishi yake na pale pale akajiunga na watawa, na kuishi katika chumba kidogo kile kile mke wake alipoishi. Mtoto huyu pia akawa mtawa na baada ya miaka akawa Abate wa manasteri ile.

Mt. Theodora utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

## Mt. Eufrosino, mpishi wa Aleksandria, Karne la IX



Kwetu Mtakatifu huyu hajulikani, lakini katika Kanisa la Orthodoksi anajulikana kama mpishi wa mji wa Aleksandria, Misri. Karibu katika kila jiko ikon yake imebandikwa. Alikuwa mtu wa kawaida. Alipoingia utawani alidhaniwa kwamba hawezi kufanya kazi yoyote isipokuwa kazi ya jikoni. Basi akafanya kazi hiyo bila kulalamika. Akaangaliwa kwa dharau na watawa wengine.

Siku moja Abate aliota ndoto kwamba alijikuta kuwa paradisini. Huko akamkuta Eufrosino, ambaye akampatia tawi lililobeba matunda matatu yenye harufu nzuri. Alipoamka abate akakuta matunda haya matatu juu ya mto wake. Akaharakisha kwenda jikoni na kumwuliza Eufrosino: “Ulikuwa wapi usiku, ndugu?” Eufroniso akamjibu: “Ulikuwa wapi wewe Baba?” Abate akawakusanya watawa wote na kuwasimulia yaliyotokea. Wakatambua utakatifu wa mpishi wao. Lakini Eufroniso, akichukia sifa za watu, akatoroka na kukimbia jangwani.

Mt. Eufrosino, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

**Septemba 12**

Sisi Wakatoliki tunawakumbuka leo Wat. Mashahidi **Hieronide** (*Cronidis*)**, Leonsio** na **Serapio** waliofariki huko Aleksandria.[69] Walikuwa wenyeji wa Misri. Waliteswa kwa sababu ya ukristo wao, pamoja na **Stratiniko**, **Valeriani** na **Seleuko**, wakati wa utawala wa Kaizari Maksimiani, karne la tatu. Baada ya mateso mengi makali, watakatifu hawa waliuawa kikatili. Waliwafungia miguu na mikono yao na kutupa baharini. Miili yao ililetwa pwani kwa mawimbi. Wakristo wakawaokota na kuwazika ki-kristo.
Huko Aleksandria, Misri, kumbukumbu ya Mt. **Theodori**, askofu, mfiadini. Kwa sababu alihubiri hadharani imani kwa Yesu Kristo wapagani wakamtesa vibaya sana kwa njia nyingi. Mwishoni wakamtupa baharini, lakini Malaika akamrudisha pwani. Ndipo wapagani wakamkata kichwa, mnamo Karne ya III.[70] Pia kumbukumbu ya Mt. **Bona**, bikira na mtawa, Misri. Alipofika umri wa miaka 12, akaingia konventi. Akaishi maisha ya majikanio makali sana na kuzitii sheria zote za watawa. Inasemekana kwamba mwili wake ulitoa harufu nzuri sana wakati wote alimpozikwa, mwaka 260.[71]
Huko Owando, Kongo Brazzavile, Wakatoliki wanamkumbuka **Anjelo Redaelli**, Padri wa Shirika la Wafransisko, aliyeuawa na kundi la watu wenye fujo, mwaka 2005.

Huko Misri, Wakristo wanawakumbuka Mt. **Petro**, mkaa pweke; Mt. **Daudi** wa Hermopolis, Misri.[72]
Huko Ethiopia, Waorthodoksi Tewahedo, wanamkumbuka Mt. **Dasia**, askari wa mji Tayda, Misri, mfiadini.[73]

---

[69] *Martyrologium Romanum,* ed. 2005. Pamoja nao: Selesio, Valeriani na Straton (Rejea *Roman Martyrology*, ed. 1956).
[70] *Acta Sanctorum*
[71] *Les petits Bollandistes*
[72] Waorthodoksi wanamkumbuka tarehe 19 Septemba.
[73] *Ethiopian Synaxarium: Meskerem 02.*

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake! Amina.

## Mt. Daudi, Mkaa pweke, Misri

Daudi kabla ya kuingia katika utawa alikuwa mkuu wa kundi la majambazi huko Misri, katika jangwa la Hermopolis. Alitenda mauaji mengi na mambo mengine mabaya. Alipokaribisha uzee aliangalia maisha yake na akaanza kuogopa kwa sababu ya madhambi yake. Aliacha kundi lake la majambazi na akaenda monasteri kwa nia ya kutubu.

Alimsihi mkuu wa monasteri kumpokea, lakini yeye akakataa. Akamweleza Daudi kwamba maisha ya utawa ni maisha magumu sana na yatapita nguvu zake. Daudi akaendelea kumwomba na mwishoni akamfunulia mkuu wa monasteri kwamba yeye alikuwa kiongozi wa kundi la majambazi. Akamwambia kwamba kama hampokei basi atarudi katika maisha yake ya zamani, na baadaye atafika kuivamia monasteri na kuwaua watawa wote.

Mkuu wa monasteri akampokea na kwa ushangao wa watawa wote akawa mtawa mwenye mwenendo mzuri. Kwa majikanio yake Daudi akawapita watawa wote. Baada ya muda Bwana akamtuma Malaika Mkuu Gabrieli kumhakikisha kwamba amemsamehe madhambi yake yote. Daudi, katika unyenyekevu wake mkubwa, hakuamini kwamba Bwana amemsamehe mwenyedhambi mkubwa kama yeye, kwa muda mfupi namna hiyo. Malaika Mkuu akamwambia, "kwa sababu ya mashaka yako utakuwa bubu." Daudi akamwomba ruhusa kusema sala zake, sheria za ki-monasteri na kushiriki katika ibada za Kanisa. Akapewa ruhusa, lakini wakati mwingine akakaa bubu.

Mwishoni mwa maisha yake Daudi akapokea kutoka kwa Bwana uwezo wa kutenda miujiza. Akawaponya wagonjwa wengi na kuwafukuza pepo. Baada ya kuishi miaka mingi namna hiyo akalala katika Bwana.

Mt. Daudi, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

**Septemba 13**

Sisi Wakatoliki tunawakumbuka Wat. **Marselino**, **Augustino**, akida na **Hieronimo**, wafiadini huko Kartago, Tunisia kwa kuuawa na Wadonatisti.[74]
Mahali pengine, kumbukumbu ya Mt. **Heraklia**, bikira.[75] Pia kumbukumbu ya Mt. **Filipo**, baba ya Mt. Eugenia, bikira. Baada ya kustaafu kuwa Gavana wa Misri, alibatizwa. Kwa amri ya Gavana Terensio, aliyeshika nafasi yake, aliuawa aliposali, huko Aleksandria, kwa kukatwa koo lake kwa upanga. Pia huko Aleksandria, Mt. **Eulogi**, askofu na Patriarka wa Aleksandria, aliyesifiwa kwa elimu na utakatifu wake,[76] mnamo mwaka 608. Katika mji ule kumbukumbu ya Mt. **Theodolo**, askofu, mfiadini, Misri.[77]

Wakoptiki wanawakumbuka Mt. **Agathokles**, mfiadini.
Huko Ethiopia, Wakristu wanakumbuka siku hiyo Mtaguso wa Aleksandria uliofanyika mwaka wa pili wa utawala wa Askofu Dionisi, Patriarka wa Aleksandria. Wanakumbuka pia Abba '**Anbas** (Baba Simba) wa Ethiopia; Abba **Musa** wa Shete Misri. Waorthodoksi Tewahedo, wanamkumbuka Mt. **Dioskoro**, mfiadini; Pia wanakumbuka kwamba siku ile tetemeko kubwa lilitokea nchi ya Misri na makanisa mengine yalianguka.[78]
Waorthodoksi wanamkumbuka Wat. **Hieronide** (*Cronides*) wa Aleksandria.[79]

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake! Amina.

---

[74] *Martyrologium Romanum,* ed. 2005.
[75] *Dictionary of Saints*
[76] *Roman Martyrology*, ed. 1956. Kuhusu maisha ya Mt. Filipo rejea maisha ya Mt. Eugenia tarehe 25 Desemba. Kwa kuwa hayajulikani mengine kuhusu historia yao, hawaorodheshwai teni na Maryrologium Romanum.
[77] *Les petits Bollandistes*
[78] *The Ethiopian Rite Missal, Abba Emmanuel & Abba Brendan Cogavin, 2002, uk 164. Ethiopian Synaxarium: Meskerem 03.*
[79] OCA *Lives of the Saints, Africa*

## Mt. Eulogi, Askofu, 608.

Kwa kuzaliwa kwake Eulogi alikuwa Msiria. Akaingia utawani katika nchi ile. Wakati ule uzushi wa Waeutikiani [80] ulifarakanisha makanisa ya Siria na Misri. Watawa walikuwa wamelegea katika nidhamu zao na kupotea katika imani yao. Eulogi akajifunza, kwa mang'amuzi ya wengine, kusimama imara katika imani na kutunza maisha yake ya ki-roho. Akajipatia ujuzi katika fasihi, biblia na historia ya Kanisa. Akawa msomi na mwanga katika karne yake, pamoja na Mt. Gregori Mkuu na Mt. Eutikio. Akaheshimiwa kwa unyenyekevu wake na maisha yake ya sala. Akiondoshwa na mahali pake pa utulivu, kama mtawa, akapadirishwa na Askofu Anastasi na kuwa Padri wa Antiokia. Kama Padri alihusiana na Mt. Eutikio, Patriarka wa Konstantinopoli. Pamoja walianza kupinga maadui wa Kanisa. Wakati ule Kanisa la (Waorthodoksi Wagiriki la) Aleksandria, lililoshambuliwa na uzushi wa Waeutikiani, liliomba kuwa na Askofu mwenye wivu kwa Kanisa, msomi aliyeweza kuwaongoza Wakristo katika maisha yao ya imani. Eulogi, kwa mapendekezo ya Kaizari, akachaguliwa kuwa Patriarka wa Aleksandria, mwaka 583, kushika nafasi ya Patriarka Yohane.

Baada ya miaka miwili kuwa Askofu, Eulogi akalazimishwa kwenda Konstantinopoli kushughulikia mambo ya Kanisa lake. Huko akamkuta Mt. Gregori Mkuu. Akaanza urafiki mtakatifu. Tangu siku ile walionekana kuwa moyo mmoja na roho moja. Eulogi akaandika barua na vitabu vingi kwa kuwapinga wazushi. Lakini karibu yote yalipotea. Tunabaki na sehemu sehemu katika barua ya Mt. Gregori Mkuu na maandiko ya Phosio. Mt. Gregori Mkuu alimwandikia siku moja kuhusu maandiko yake: "Sitambui kosa lolote bali mambo tu ya kusifiwa". Akafariki mnamo 608, muda mfupi baada ya kifo cha Mt. Gregori Mkuu.[81]

Mt. Eulogi, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele.

---

[80] Waeutikiani (*Eutychians*) ni dhehebu kati ya madhehebu wanaofundisha monophysitism, yaani kutambua hali tu ya umungu katika Yesu Kristo.

[81] *From Nicephorus's Chronicle, the Paschal Chronicle*, *Photius*, Bibl. Cod. 181, 208, 226, 230, &c.

**Septemba 14**

Sisi Wakatoliki tunamkumbuka Mt. **Sipriano**, askofu wa Kartago, Tunisia, aliyesifiwa sana kwa elimu na utakatifu wake. Wakati wa utawala wa Makaizari Valeriani na Galieni, karibu na bahari, maili kama 6 kutoka mji, alikatwa kichwa, baada ya kuteswa sana uhamishoni. Sikukuu yake inaadhimishwa pamoja na Mt. Korneli, siku ya Septemba 16.[82] Pia Wakatoliki wanawakumbuka Wat. **Kresensiani, Viktori, Rosula**, na **Jenerali**, wafiadini, Tunisia.[83]

Huko Misri Wakoptiki wanawakumbuka Mt. **Hori**, askofu na **Serapio**, padre, wote wafiadini, Aleksandria.
Huko Ethiopia, Wakristu wanawakumbuka Abba **Makari II**, Patriarka, askofu wa 69 wa Aleksandria na Mt. **Theodori**, Askofu wa Debra 'Eldanu, Mwanateolojia.[84]
Huko Somalia, kumbukumbu ya Mtu wa Mungu **Nuru Ahmadey Osman** wa Kanisa moja la ki-Pentekoste, aliyeuawa mwaka 2008.

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake! Amina.

## Mtu wa Mungu Nuru Ahamadey Osman, 2008.

Tarehe 14 Septemba 2008, huko mji Afgoye, umbali na Mogadishu kama kms 35, Waislamu wenye imani kali wakampiga risasi na kumwua Mkristo aliyeongoka karibuni hivi kutoka dini la ki-islamu.
Nuru alialikwa kuhudhuria harusi ya ki-islamu iliyosherehekewa karibu na nyumba yake. Ibada ya harusi hiyo iliendeshwa kwa lugha ya Kiarabu, lugha ambalo hakuna kati ya wageni waliofahamu, isipokuwa Shehe aliyeongoza. Mwisho wa ibada yake, Nuru alimwomba Shehe kumjulisha ujumbe wake katika lugha ya Ki-somalia, lugha ya kuzaliwa kwa wale waliohudhuria harusi. Karibu wageni wote waliitikia ombi

[82] *Martyrologium Romanum,* ed. 2001.
[83] *Roman Martyrology*, ed. 1956.
[84] *The Ethiopian Rite Missal, Abba Emmanuel & Abba Brendan Cogavin, 2002, uk 164. Ethiopian Synaxarium: Meskerem 04.*

lake. Lakini Shehe aliyekuwa mmojawapo wa wale waliojiunga karibuni na Al Shabab, alichukizwa na ombi hilo. Alimwomba mmoja wa askari kumnyamazisha mwasi huyu. Kama Mkristo aliyetanasari, Nuru alitazamiwa na Shehe kama mwasi, kwa sababu lugha takatifu ndilo Kiarabu, lugha izungumzwayo peponi!

Rafiki zake Nuru walimshauri kukimbia saa hii, wakiogopa kwamba atapoteza maisha yake. Lakini askari, aliyekuwa na shotgun, akapiga risasi na kumwua Nuru alipotoka kwenda nyumbani. Kadiri ya bwana harusi aliyemwalika, Nuru akakumbuka kwa huruma aliyoonyesha kwa wazee mahali alipoishi. Mchungaji wa Nuru alisema kwamba Nuru atakumbuka kama Mkristo Msomalia wa kwanza katika wilaya wa Afgoye kukariri kitabu kizima cha Matendo ya Mitume, kitabu ambacho alikipenda kuliko vitabu vyote vingine vya biblia.

Kuanzisha mwezi wa Januari hadi Septemba 2002, Wakristo sita, tukihesabu Nuru, waliuawa kwa ajili ya imani yao. Watano wengine walikuwa Sayid Ali Sheik Luqman Hussein, David Abdulwahab Mohamed Ali, Da’ud ali, Mohamed Yusuf na Hassan Mo’alim.

Shahidi Nuru na wenzako, mwombe Mungu Waislamu wamtambue Yesu kuwa Kristo Bwana na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

**Septemba 15**

Huko Misri Wakatoliki wanamkumbuka Mt. **Yohane Kolobos**, mtawa Misri.[85]
Huko Afrika wa Kaskazini, Wakatoliki wanamkumbuka **Valeriani**, askofu wa Abbenza, aliyefariki shahidi, mwaka 457.
Huko Ethiopia, kumbukumbu ya Mt. **Anoreo**, Mwungama dini. Pia kumbukumbu ya **Yakobo**, Masketi.
Huko Moroko na Shirika la Wafransisko, kumbukumbu ya Watakatifu **Fransisko**, **Yakobo**, **Sancho**, **Idefonsi**, **Yohane** na **Denisio**, waliosulubiwa na Waislamu huko Moroko kwa ajili ya imani yao, 1437.
Huko Uganda, Wakatoliki wanamkumbuka **Odo Gaspero**, mwanasiasa na mlei, aliyeuawa na watu wasiojulikana, mwaka 1979.[86]

Huko Misri, Wakoptiki wanawakumbuka Wat. **Proforio** na **Niseta**, mashahidi na Mt. **Stefano**, Padri.[87] Pia kumbukumbu ya Mt. **Aleksandra**, mkaa pweke. Kwa miaka 10 aliishi katika kaburi moja, akipelekwa chakula na mwanamke. Kwa sababu ya toba hakutaka kumwona mtu yeyote. Melania mzee akamtembelea, lakini hakumwona. Alitumia muda wake kutafakari maisha na mafundisho ya mitume, mashahidi, maaskofu na manabii.
Huko Ethiopia, Wakristu, wanamkumbuka **Ewostatewos**, mtawa aliyefundisha kushika sabato. Pia kumbukumbu ya **Lebna Dengel**, or **Dawit II** (*David*) **Wanag Sagad**, Mfalme wa Ethiopia, toka 15 Agosti 1508 hadi 2 Septemba 1540.[88]

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake! Amina.

---

[85] *Les petits Bollandistes*
[86] Rejea Fr. Neno Contra,, Louis Kalonji, *African Lay Martyrs*, New People Media Centre, 2009, uk. 88-89.
[87] *Coptic Synaxarium: 18 Tute*.
[88] *The Ethiopian Rite Missal, Abba Emmanuel & Abba Brendan Cogavin, 2002, uk 164. Ethiopian Synaxarium: 05 Meskerem*.

## Mt. Yohane Kolobos, Mwanakoriti, 405.

Yohane alizaliwa katika mji wa Basta, Misri, na wazazi Wakristo lakini maskini. Aliitwa Kolobos kwa sababu alikuwa mfupi wa kimo. Alipokuwa na umri wa miaka 18, akaenda kuishi jangwani huko Shete, chini ya baba yake ya ki-roho Mt. Pambo. Tunasoma katika Kitabu cha Watakatifu Wakoptiki kwamba Pambo, kwa jina lingine Abba Bamonya, akamwambia: “Mwanangu, huwezi kukaa nami katika jangwa hii. Wale wanaokaa jangwani wanakula chakula kutokana na kazi ya mikono yao. Tena wanafunga sana, wanasali na kukesha muda mrefu, wanalala sakafuni na mambo mengine mengi magumu. Rudi ulimwenguni na kuishi katika hofu ya Mungu.“ Lakini Yohane akamjibu: “Usinirudishe ulimwenguni kwa sababu nilikuja kukaa chini yako na kujifunza kutoka kwako. Ukinipokea, naamini kwamba Mungu atakuhakikishia moyoni mwako kwamba ninastahili kuwa mfuasi wako.“

Pambo, akiwa amezoea kutochukua uamuzi haraka, akamwomba Kristo amfunulie wito wa Yohane. Malaika akamtokea na kumwambia: “Umpokee, kwa sababu atakuwa chombo kiteule“. Pambo akampokea na akamnyoa nywele zake. Akaichukua nguo ya kitawa na kwa muda wa siku tatu, usiku na mchana, akaiombea. Alipomvisha Yohane akamwona Malaika akifanya ishara ya msalaba juu yake.

Tangu siku ile Yohane akajitahidi kwa nguvu zake zote na moyo wake wote kutawala tamaa zake na kuvisha roho ya Kristo.

Pambo akaamua kumjaribu. Basi siku moja akamfukuza nje ya kijumba chake, akimwambia: “Siwezi kuishi nawe“. Yohanne akakaa nje mlangoni wa kijumba chake kwa wiki moja. Kila siku Pambo akaja na kumpiga kwa kuti moja na kila wakati Yohane aliinama na kusema: “Nimekosa“. Siku ya saba, Pambo akaenda kanisani na akawaona malaika saba wakishika mataji saba na kuyaweka juu ya kichwa cha Yohane. Tangu siku ile Pambo akamheshimu sana Yohane.

Yohane anakumbukwa kwa sababu ya utii wake. Siku moja Pambo akaokota fimbo iliyokauka sana. Akampatia Yohane na kumwambia: “Chukua fimbo hii, uipande na kumwagia maji“. Yohane akatii na kufanya kama Pambo alivyomwambia. Mara mbili kwa siku aliimwagia maji ingawa maji yalipatikana kwa mbali sana kutoka vijumba vyao. Baada ya miaka mitatu, fimbo ikaanza kuchipuka na kuwa mti wa

matunda. Abba Pambo akachuma baadhi ya matunda yake na akayaonyesha kwa watawa wengine akisema: “Twaeni na mle matunda ya utii“. Inasemekana kwamba mti huu bado upo katika monasteri ya Yohane Kolobos katika jangwa la Nitria.

Abba Pambo akaugua kwa miaka 12. Yohane akamtumikia kwa upendo mkubwa. Alipokaribia kufariki akawakusanya watawa wazee na akishika mkono wa Yohane akawapa akisema: “Mchukueni na kumlinda, kwa sababu yeye ni malaika na siyo mwanadamu.“ Akaamuru Yohane akae mahali alipopanda mti. Baada ya kifo cha Abba Pambo, Yohane akapadirishwa na Askofu Theofilo, Patriarka wa Aleksandria. Akawa Abate wa monasteri aliyoanzishwa karibu ya mti wa utii. Inasemekana kwamba alipokuwa anasoma misa, aliweza kutambua wale waliostahili kupokea Mwili na Damu ya Yesu na wale ambao hawakustahili.

Alikuwa mwangalifu sana kuepuka kila nafasi ya kupoteza amani moyoni mwake. Siku moja alipokuwa anasali na kusuka mikeka, njiani pa kwenda Shete, akakutana na msimamizi wa ngamia aliyeanza kumtukana kwa matusi makubwa. Mtakatifu huyu, ili asipoteze amani moyoni na kuanza kukasirika, akaacha kazi yake na kukimbia. Siku nyingine alipovuna ngano alikimbia kwa sababu alisikia mvunaji mmoja akilumbana na mwenzake. Tena siku nyingine alipokuwa anaenda kanisani alisikia watu wawili wakigombana. Akakimbilia kijumba chake na kuizunguka mara nyingi kabla ya kuingia ndani ili kujitakasa na maneno ya kashifa aliyesikia, na kutayarisha roho yake kuongeana na Mungu. Kwa hiyo, kwa sababu ya jitihada zake kujikinga na maneno na mawazo mabaya, alikua katika fadhila za upole, unyenyekevu na uvumilivu, kiasi kwamba hakuna kitu chochote kilichoweza kuvuruga moyo wake.

Ilikuwa desturi yake kutozungumza mambo ya kawaida. Siku moja watu walimjaribu na kusema: “Inatubidii kumshukuru Mungu kwa mvua ya mwaka huu. Mitende iliota vema na ndugu zetu wataweza kukata makuti kwa ajili ya kazi yao ya kusuka.“ Yohane akawajibu: “Vivyo hivyo, Roho wa Mungu anaposhuka mioyoni mwa watumishi wake, nyoyo zao zinaanza kuwa bishi tena, ningeweza kusema, na zinaanza kuhuishwa upya, na kuzaa matawi mabishi katika hofu ya Mungu.“ Kwa jibu hilo hawakuthubutu kumsumbua na mambo ya ki-dunia.

Wakati Wabarbari wakavamia nchi ya Shete, mwaka 395, akahamia mlima Kolzin, karibu na mji uitwao sasa Suez. Siyo kwamba aliogopa kufa, bali kama alivyoeleza mwenyewe hakutaka yule ambaye angemwua aende motoni. Wakati Mungu alitaka kumpokea katika heri ya milele, alituma watumishi wake Abba Makari na Abba Antoni kumfariji na kumpasha habari kwamba saa yake imekwisha fika. Usiku kuamkia Jumapili, Yohane akaugua na akamtuma mtumishi wake kununua kitu katika kijiji. Mtumishi wake alipoondoka, Malaika na Watakatifu wakafika na kumpokea roho yake mbinguni. Mtumishi aliporudi akaona roho ya Yohane ikizunguka na umati wa Watakatifu na Malaika wakiimbia sifa ya Mungu. Mbele yao kulikuwa mmoja aking’aa kama jua. Mtumishi akashangaa. Ndipo malaika mmoja akaja na kumtaja majina ya kila mmoja. Mtumishi akamwuliza na yule aliyetangulia ni nani? Malaika akamjibu: “Ndiye Antoni, baba ya watawa wote“.

Mt. Yohane Kolobos, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.


**Septemba 16**

Sisi Wakatoliki tunaadhimisha sikukuu ya Wat. Mashahidi **Kornelio**, Baba Mtakatifu na **Sipriano**, askofu wa Kartago, kama ilivyotajwa tarehe 14 mwezi wa Septemba.[89]
Siku ya leo Washirika la Ki-fransisko wanawakumbuka mashahidi wa Moroko, **Léon, Dominique, Hugues, Jean** na **Eloi** watawa, na walei wengi, mwaka 1232.[90]
Huko, Italia, Wakatoliki wanamkumbuka **Gislemeri**, Askari wa Jeshi la Theba, aliyeuawa, Italia, karne la III.[91]

Waorthodoksi wanamkumbuka Mt. **Dorotheo** wa Misri, Karne la IV.
Huko Ethiopia, Waorthodoksi Tewahedo, wanawakumbuka mwanamke **Baslantya**; mashahidi **Yakobo** mtawa, **'Atimos** askofu, **Baslis**, **'Arontos**, **Rawrewo**, **Sawlwas**, na **Sawa**, wafiadini.[92]

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake! Amina.

## Maisha ya Mt. Sipriano, Askofu na Mfiadini, 258.




Taschio Sipriano alizaliwa mnamo mwaka 200, huko Kartago, mji mkubwa katika Afrika ya Kaskazini, Tunisia ya siku hizi. Baba yake alikuwa mmojawapo wa wazee katika baraza la mji, mkufunzi wa usemaji, na aliheshimiwa sana na watu. Basi, alimtaka mwanae asomee maarifa yote yaliyofundishwa kwenye vyuo vya siku zile. Lakini Sipriano hakumfuata babae. Ingawa alikuwa bado mpagani, aliona kuwa makuu ya dunia ni kama upuuzi mtupu. Alipokuwa mtu wa makamo, mwenye umri

---

[89] *Roman Martyrolgoy*, ed. 2001
[90] *Le palmier seraphique*, IX, 261
[91] *Acta Sanctorum*
[92] *Ethiopian Synaxarium: 06 Meskerem.*

wa miaka arobaini, alianza kupata mafundisho ya dini kutokana na bidii za padre mmoja mzee, akaomba abatizwe. Kabla ya kubatizwa akagawa mali yake kwa maskini. Jambo la ajabu ni kwamba mwaka mmoja tu baada ya kubatizwa, alichaguliwa kuwa askofu wa Kartago. Ilikuwa mwaka 249.

Sifa yake ilieneza kila mahali, lakini makafiri walimchukia sana. Hao walimtafuta wakisema: "Mtupeni Sipriano kwa simba, wamtafune!" Sipriano akjificha, pengine akahamishwa Korba na toka huko alikoenda, aliandika barua nyingi kuwashauri na kuwahimiza wakristo wake. Baada ya muda, udhalimu ulipopungua, aliweza kurudi tena Kartago. Ilimbidi kulinda kwa hekima sana umoja wa Kanisa uliokuwa katika hatari ya kuvunjika kwa sababu ya mapadri Felisimo, Novisiani na Novato. Mwaka 252, wakati wa tauni, askofu Sipriano alijikalifu bila kikomo katika kuwatuliza wateseka, lakini hata hivyo, bidii zake hizo hazikuwazuia wapagani kuwasingizia wakristo sababu ya ugonjwa huo mbaya mno, kwa kuwa, eti, walikosa heshima kwa Mungu, na hususa kwa kiongozi wao mkuu. Lakini wakristo walimpenda sana kwa ajili ya wema wake, na pia kwa siasa yake ya kutokuamua na kukata shauri kabla ya kusikilizana na mapadre wa jimbo lake.

Wakristo walipoanza kudhulumiwa tena mnamo mwaka 258, askofu Sipriano alikamatwa upesi sana, akapelekwa mbele ya liwali. Kwanza alihamisha huko Corubisum. Shemasi Ponsio[93] alimfuata kwa hiari katika uhamisho wake. Baada ya mwaka , askofu Sipriano alipokataa kabisa kuitolea sadaka miungu ya uongo, akahukumiwa kufa. Saa ilipowadia aliwapatia chakari wake sarafu 25 za dhahabu, akajifungia mwenyewe kitambaa machoni pake, akakilaza kichwa chake mahali alipoonyeshwa na akakatwa kichwa.

Japo askofu Sipriano aliuawa tarehe 14 Septemba, sikukuu yake huadhimishwa tarehe 16, ili yeye na rafiki yake Mt. Korneli wakumbukwe pamoja siku ile ile.[94] Karne tano baadaye Kaizari Karolo Mkuu aliyahamisha masalia ya Mt. Sipriano huko Ufaransa.

Mt. Sipriano, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

---

[93] Rejea kumbukumbu yake tarehe 8 Machi

[94] Rejea *Maisha ya Watakatifu*, T.M.P. Book Department, Tabora, chapa 1996, uk 322-323.

## Mashahidi wa Moroko, 1232

Mfalme Miramolin alipokata vichwa vya mashahidi watano watawa wa Shirika la Ki-fransisko, tauni ikalipuka katika ufalme wa Moroko kwa miaka mitano, yaani mwaka mmoja kwa shahidi mmoja. Wapagani wakatambua kwamba Mungu huwalinda Wakristo na kwamba mlipuko wa tauni ulikuwa adhabu kutoka kwa Mungu kwa dhambi ya kuwaua watawa. Basi Mfalme Miramolin, kwa ajili ya kuzuia ugonjwa huo, akawaruhusu Wakristo kueneza imani yao katika dola yote.

Wakristo, ambao idadi yao ilikuwa kubwa, walikuwa na hitaji kubwa la wachungaji na madaktari. Hawakuwa bado watumwa kama itakavyotokea baadaye huko Moroko, Aljeria, Tunisia na Tripoli. Walikuwa katika nchi yao na kushiriki kila hali ya maisha. Wengi walihamishwa na Waislamu kutoka Hispania ili kuvunja uwezo wao.

Watawa wakaanzisha monasteri ndogo Moroko. Kanisa lao lilibarikiwa na kuwekwa chini ya ulinzi wa Bikira Maria. Likawa Kanisa Kuu la jimbo la Moroko. Mfalme Miramolin aliwatangazia raia wake wote kwamba ni marufuku kumdhulumu Mkristo. Wapo huru kufuata dini yao. Mwenyeheri Padri Agnello akawa askofu wa kwanza. Tarehe 20 Machi 1227 akaja, akisindikizwa na watawa wengine wa Ki-fransisko, na kukaribishwa vizuri na Mfalme.

Imani ikaenea kwa nguvu katika nchi hizo za Afrika Kaskazini na wengi wakatanasariwa. Waislamu wakaanza kulalamika. Wakala njama, wakavamia wakristo kwa hila na kuwaua wengi, mwaka 1232. Miongoni mwao watawa wengi, ambao majina yao yalisahauliwa, waliouawa. Mauaji makubwa yalitokea Moroko, kwa sababu imani ilienea sana huko. Kanisa likavamiwa na waamini waliokuwa ndani yake walichinjwa. Miongoni mwao watawa watano: Leo, Dominiko, Hugolino, Yohane na Eloi. Baada ya dhiki hiyo, hakuna mtu aliyethubutu kutangaza hadharani kwamba ni Mkristo. Lakini Mungu hawezi kuwasahau watumishi wake. Akawatisha Waislamu kwa mwanga utokao mbinguni usiku na kukaa juu ya Kanisa ambalo maiti wa mashahidi walikuwepo. Kengele zikalia peke yao na sauti za malaika zikasikika wakimwimbia Mungu.

Amani ikarudi, mitume wakaanza tena kuhubiri Injili na Kanisa likastawi kwa mara nyingine. Kama alivyoandika Baba Mtakatifu

Gregori IX, mwaka 1233: “Kristo akazaliwa upya ndani ya Shirika la Ki-fransisko, akawaongoa wengi kwa njia ya mifano ya maisha yao, mahubiri yao na miujiza yao”. Maaskofu wanne wa kwanza wa Moroko walikuwa watawa wa Shirika la Ki-fransisko.[95]

Mashahidi wa Moroko mtuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

[95] *Le Palmier Seraphique*, IX, 259-261

**Septemba 17**

Huko Misri, Wakatoliki wanamkumbuka Mt. **Medilama**, bikira mfiadini, Misri.[96]
Huko Somalia, kumbukumbu ya Mwenyeheri Mungu **Rosa Maria Sgorbati** (*Leonella*) sista wa Shirika la Consolata aliyeuawa mwaka 2006.
Huko Bomoanga, Niger, Wakatoliki wanamkumbuka **Luigi Macalli**, Padri wa Shirika la Misioni kwa Afrika, aliyetekwa nyara, mwaka 2018.

Wakoptiki wanawakumbuka Patriarka **Atanasi II**, askofu wa 28 wa Aleksandria; Mt. **Malatini**, bikira, na **Theopista**, mtawa.[97]
Huko Ethiopia, Wakristu wanamkumbuka Abba **Severiano** (Sawiros), askofu wa Gabla au Gabala (Byblos). Waorthodoksi Tewahedo, wanawakumbuka Abba **Dioskoro**, Patriarka, askofu wa 25 wa Aleksandria; Wat. **Agato**, **Petro**, **Yohane**, **Amoni**, **Amona** na mama yao **Rapika** (*Rebecca*), wafiadini, Misri. Pia **Fasiladas** na wenzake elfu mbili walikufa mashahidi.[98]
Waorthodoksi wanawakumbuka **Mashahidi elfu moja** huko Misri.

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake! Amina.

## Mwenyeheri Rosa Maria Sgorbati (Leonella), 2006

Rosa Maria alizaliwa Italia, tarehe 9 Desemba 1940. Tangu ujana wake alitamani kuwa sista mmisionari, lakini mama yake alimkatalia na kumwambia mpaka awe na umri wa miaka 20. Alipokuwa na miaka 20 akamwambia mama yake kwamba hakubadilisha nia yake. Akajiunga na Masista wa Consolata na kuweka nadhiri za maisha mwezi wa

[96] *Les petits Bollandistes.* Jina lake limefutwa katika Martyrologium Romanum kwa sababu ya kukosa uthibitisho wa historia;
[97] *Coptic Synaxarium : 20 Tute*
[98] *The Ethiopian Rite Missal, Abba Emmanuel & Abba Brendan Cogavin, 2002, uk 165. Ethiopian Synaxarium: Meskerem 07.*

Novemba, 1972. Wakati ule alifuata kozi ya nesi huko Uingereza, na mwezi wa Septemba 1970 akatumwa Kenya. Kwa miaka kumi na mitatu alihudumu katika Hospitali ya Wakonsolata Mathari, Nyeri, na baadaye huko Kiambu. Mwaka 1983 Leonella akaendelea masomo yake ya nesi na mwaka 1985 akateuliwa kuwa mkufunzi mkuu katika shule ya nesi huko Hospitali ya Nkubu, Meru, Kenya. Mwezi Novemba 1993 akachaguliwa kuwa Mama Mkuu wa Masista wa Consolata, katika nchi cha Kenya. Akatimiza kazi hiyo miaka 6.



Baada ya mwaka mmoja wa likizo wa kunoa ubongo (*sabbatical year*) akaenda Mogadishu, Somalia, akitafuta uwezekano wa kuanzisha shule ya nesi katika hosptiali ya Kijiji cha Watoto Yatima (*SOS Children's Village*). Mwaka 2002 Shule iitwayo Herman Gmeiner ilifunguliwa, na Sista Leonella akiwa mkurugenzi. Manesi Thelathini na wanne walihitimu miaka iliyofuata na walipokea Cheti na Diploma kutoka W.H.O. (*World Health Organization*) kwa sababu serikali haikuwepo Somalia tangu 1991.

Sista Leonella alitafuta kwa makini kuwasomesha wakufunzi kwa ajili ya Shule ya nesi. Akarudi Kenya pamoja na manesi watatu ili waweze kujifunza zaidi. Akakutana na matatizo kupata visa kurudi Mogadishu kwa sababu ya Waislamu waliotawala katika mji huo na ujirani wake wakati ule. Akafaulu kurudi tarehe 13 Septemba 2006. Siku 4 baadaye aliuawa kwa risasi nje ya hospitali ya Watoto Yatima. Mpambe wake, Mohamed Osman Mahamud, aliuawa pia. Tarehe 17 Septemba, 2006, watu wawili wenye bunduki wakatokea nyuma ya taxi na vibanda vya biashara na kumpiga Sista mgongoni. Sista akapelekwa kwa haraka hospitalini lakini muda si muda akafariki. Maneno yake ya mwisho aliyoweza kusema: "*Perdono, perdono*", maana yake: "Nawasamehe, nawasamehe".

Mwenyeheri Leonella, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

## Mtakatifu Theopista[99]

Theopista aliolewa na kumzalia mume wake mtoto wa kiume. Mume wake alifariki Theopista akiwa bado kijana. Akaamua kuwa mtawa, kwa hiyo akaanza kufuata nidhamu ya maisha ya ki-roho, kufunga, kusali bila kukoma na kuabudu usiku na mchana. Akamwendea Abate Makari, Askofu wa Nekios, kumwomba amwombee na kumvisha na nguo ya kitawa. Askofu akamshauri kujaribu kwanza kwa mwaka mmoja na kumwahidia kwamba atamvisha nguo ya kitawa baada ya mwaka mmoja. Basi akarudi nyumbani mwake, akajifungia katika chumba kidogo na kuacha tundu dogo. Mtoto wake, aliyekuwa na miaka 12 wakati ule, akamuhudumia. Akazidi kufunga na kusali.

Mwaka ulipita na askofu alisahau ahadi yake. Katika ndoto akamwona Theopista uso wake uking'aa. Theopista akamwambia: "Baba yangu, namna gani unanisahau na usiku wa leo nitakata roho". Askofu yeye aliona kama alikuwa yu macho, akamwombea na kumvisha nguo ya kitawa. Aliposhindwa kupata *Kalansowa* (nguo ya kufunika kichwa) alitumia yake na kumweka juu ya kichwa chake. Baadaye akamvisha na nguo ya kitawa. Akamwomba mfuasi wake *kalansowa* nyingine na kujifunika. Theopista alikuwa na msalaba wa fedha katika mkono wake, akampatia askofu na kumwambia: "Pokea hiyo zawadi kutoka mfuasi wako". Aliposema maneno hayo, askofu aliamka na kuona msalaba mkononi mwake. Akauangalia kwa makini kwa sababu msalaba ulichongwa vizuri sana. Akashangaa na kumsifu Mungu.

Asubuhi mapema alienda, pamoja na mfuasi wake, nyumbani mwa mwanamke huyu. Mtoto wake akampokea kwa machozi. Askofu alipomwuliza kwa nini alilia, alimjibu: "Mama yangu aliniita katikati ya usiku na kuniaga. Aliniambia kwamba yoyote askofu atakayokuambia uyafanye. Naondoka usiku huu kwenda kwa Bwana Yesu Kristo. Aliniombea na kunishauri: 'Shika yote niliyokuamuru, umtii askofu. Na sasa nipo mikononi mwako".

Askofu alifika mahali mtakatifu alipolala. Alibisha hodi mlangoni, lakini hakupata jibu. Akasema: "Kweli mtakatifu huyu alifariki". Akamwamuru mfuasi wake kufungua mlango. Askofu alipoingia

[99] Theopista huyu si Mt. Theopista, mke wa Mt. Eustakio, mshahidi huko Roma, tunayemkumbuka tarehe 20 Septemba katika *Roman Martyrology*

akamkuta mwanamke amekata roho. Alikuwa amevaa nguo ya kitawa aliyomvisha katika ndoto, na pia *kalansowa* yake. Macho yake yalijaa machozi. Akamsifu Mungu anayejibu maombi ya watakatifu wake. Akawaita mapadri. Wakampeleka kanisani na kumwombea kwa heshima kubwa.

Kulikuwa katika mji huo mtu aliyepooza na kupagawa na pepo. Aliposikia nyimbo zilizoimbwa na mapadri, akawaomba watu wambebe hadi kanisani na kumweka mahali ambapo mwili wa mtakatifu ulipolazwa. Alipofika kanisani akatambaa hadi karibu na mwili wa mtakatifu kwa imani na akaugusa na kupona mara. Pepo akatoka kwake. Watu wote wakamwamini Bwana Yesu Kristo na askofu akawabatiza. Na yeyote aliyekuwa na udhaifu wa mwili au ugonjwa alikuja kanisani kugusa mwili wa mtakatifu na akapona mara. Liwali aliposikia habari hizo, yeye na nusu ya mji wakamwamini Bwana Yesu Kristo. Akafika kanisani, akambeba mwili wa mtakatifu na kumzika kwa heshima.

Mt. Theopista, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

**Septemba 18**

Huko Misri, kumbukumbu ya Mt. **Eumenio**, askofu wa Gortyne, Ugiriki, alifariki huko Theba.[100]
Huko Misri, Wakatoliki wanawakumbuka Mt. **Tiberio**, mwungama dini, Mt. **Trofimo**, mfiadini, Misri.
Na huko Nubia, Mt. **Mathayo**, mwasketi.
Huko Aljeria, Wakatoliki wanamkumbuka Mhashamu **Hieronimo** (Geronimo), mfiadini, Aljeria. [101]
Huko Juba, Sudan ya Kusini, Wakatoliki wanamkumbuka Katekista **Ludoviko-Paulo Loku**, aliyefariki baada ya kuteswa na askari, mwaka 1990.[102]
Huko Niger, **Father Pierluigi Maccalli**, (SMA), aliyetekwa nyara usiku ya kuamkia tarehe 18, Septemba, mwaka 2018, katika misioni ya Bamoanga Hadi leo hatuna habari zaidi.

Wakoptiki wanawakumbuka Wat. **Sipriano** na **Yustina**, wafiadini.[103] Pia kumbukumbu ya Wat. **Dorotheo**, mwanakoriti, **Basilide**, baba ya wafalme; Mashahidi **Kasioni** wa Aleksandria, **Irene** na **Sofia**.
Huko Ethiopia, Wakristu wanamkumbuka **Musa**, nabii. Waorthodoksi Tewahedo, wanawakumbuka **Dimasio**, mfiadini;[104] **Lusiano**, mfiadini, **Yeremia** (*'Ermeyas*), **Andea**, **Elianos** na **Amon**, mkaa pweke.

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake! Amina.

## Mhashamu Hieronimo (Geronimo), Shahidi, 1569.

Hieronimo amezaliwa katika kabila la Waarabu waliokaa upande wa mji Oran, Aljeria, mnamo mwaka 1539. Wahispania waliteka mji ule mwaka

---

[100] *Acta Sanctorum*
[101] *Les petits Bollandistes*
[102] Rejea Fr. Neno Contra,, Louis Kalonji, *African Lay Martyrs*, New People Media Centre, 2009, uk. 181.
[103] *Coptic Synaxarium : 21 Tute.* Wakatoliki wanaadhimisha sikukuu yao tarehe 26 Septemba.
[104] *Ethiopian Synaxarium: Meskerem 08.*

1509. Kwa kulisha jeshi la askari waliokinga mji, Wahispania walikuwa wanashambulia mara kwa mara vijiji vya jirani. Basi siku moja ya mwaka 1543 wakifanya vile wakamkamata mtoto mdogo wa Waarabu. Mtoto yule akaonekana safi na mwenye adabu na akili sana. Wakampeleka mjini Oran pamoja na mali na vyakula walivyoteka. Desturi yao Waarabu wote waliokamatwa vitani wakawekwa utumwani. Wale watumwa wakatumikia kazi ya nyumbani. Basi yule mtoto Mwarabu akawekwa nyumbani mwa Padri fulani, jina lake Yohane Karo.

Padri huyu akamfundisha vizuri mtoto, kwani alikuwa mwenye akili nyepesi. Kisha siku si nyingi akajua katekisimu na mafundisho ya dini barabara. Akabatizwa na kuitwa kwa jina la Hieronimo. Hatuna habari nyingine juu ya maisha yake wakati ule. Tunajua tu kwamba alikaa mjini Oran mpaka mwaka 1547. Mwaka ule ugonjwa wa tauni ukazuka mjini. Kwa kuepuka maambukizo, wakaazi wengi wakalazimishwa kuondoka na kukaa nje katika mahema au mabanda ya majani. Siku zile watumwa wengi wakatoroka, kwa maana hawakuweza kuchunguliwa na kulindwa vema. Baadhi ya watoro waliokimbia wakamkamata mtoto Hieronimo, wakamchukua, wakampeleka nje ya mji wa Oran na wakamrudisha mjini kwake kwa ndugu zake. Basi wazee wake na wote wa kabila lake wakiwa Waislamu, wakamrudisha katika desturi za ki-islamu. Akaishi vile muda wa miaka mingi katika dini ya Uislamu akisahau dini ya kweli.

Kwa neema ya Mungu, alipofika umri wa miaka 25, akakumbuka ubatizo wake na mafundisho ya Padri Yohane Karo. Akafikirifikiri, akatambua ukweli wa dini ya kikristo. Akakusudia kufuata njia iendayo uzimani. Basi akarudi mji Oran, akamwendea Padri Yohane Karo, akamhadithia yote yaliyotukia tangu miaka 12. Akasema: “nimepelekwa katika mji wa kabila langu ningali mtoto. Nikafuata dini ya Uislamu, lakini sasa nataka kurudi katika dini ya kweli. Sitaki kuwa Mwislamu tena. Nimerudi nipate kuwa Mkristo wa kweli na mwema siku zote.” Akisikia habari zile, Padri akafurahi moyoni. Lakini akataka kwanza kumjaribu Hieronimo. Baada ya muda alipoona kuongoka na kutubu kwake si jambo la uongo, wala la unafiki na udanganyifu, akamfundisha na kumpokea tena katika Kanisa. Padri Yohane Karo alipouona wema

wake akamsaidia apate kuoa mwanamwali Mkristo aliyetoka naye katika kabila la Afrika. Wakaoana, wakakaa vizuri katika ndoa yao.

Hieronimo alikuwa mtu mwenye akili, hodari na mwenye nguvu ya mwili. Uhodari wake ulionekana mara kwa mara katika vita. Siku moja akakamatwa na Waturuki akiwa amepigwa mkononi kwa mshale. Akapelekwa mjini mwa Aljeria na kuuzwa kama mtumwa. Kufuatana desturi zao, watumwa wawili kati ya watumwa kumi walikuwa mali ya Pasha. Hieronimo akachaguliwa kuwa mtumwa wa Pasha Aluj Ali.[105] Waarabu walinzi wa gereza walipotambua kwamba Hieronimo alikuwa wa kabila lao na akaongoka kuwa Mkristo, wakakasirika. Wakamfunga kwa mnyororo mzito sana, hata kilo 50, wakamkaza asiondoke kamwe.

Vita vingine vikaanza, vita vya rohoni kulinda salama imani yake ya kweli. Walimu wa dini ya Uislamu wakaitwa kuzungumza na Hieronimo na kumshauri aache dini ya Kikristo na kurudi katika dini ya Uislamu. Walifikiri kwamba itakuwa kazi nyepesi. Kumbe sivyo. Hieronimo alikuwa na akili sana, aliwajibu kwa uhodari. Kwa neema ya Mungu, akabaki imara, na kuwaambia: “Mimi sitaacha kuwa Mkristo. Siogopi makamilio yenu.” Wakazidi kumshawishi, lakini yeye akawajibu: “Ondokeni, nendeni zenu, kwa ulinzi wa Mungu!” Alipokuwa pamoja na Wakristo aliwaambia: “Angalieni wanafikiri nini? Wanadhani kwamba wataweza kugeuza nia yangu na niwe Mwislamu. Hapana. Sitakuwa Mwilamu hata ikinibidii kuuawa.” Waarabu walipoona kwamba wanashindwa wakamwendea Aluj Ali kumhadithia maneno ya Hieronimo. Wakamwambia: “Bwana, tazama maneno ya mtumwa yule, ni maneno ya matusi. Usiogope kumwadhibu vibaya.” Aluj Ali mwenye akakusudia kumlazimisha Hieronimo amkane Yesu Kristo, na kuwa tena Mwislamu. Akikataa basi atamtesa na kumwua. Alifikiri kwamba, kwa njia ile, atawatisha watumwa wengine na kuwalazimisha kuacha dini yao.

Wakati ule Aluj Ali alikuwa anajenga ngome Bab-el-Wedi ili kulinda mji wa Aljeria. Basi siku ileile aliposikia habari juu ya Hieronimo,

---

[105] Aluj Ali zamani alikuwa Mkristo. Amezaliwa Kalabria, Italia. Alikuwa mvuvi wa samaki. Yeye pia alikamatwa na Waturuki wa Aljeria akawa mtumwa. Akakana dini ya Katoliki na kufuata dini ya Uislamu. Kwa sababu ya uhodari wake akawa Pasha wa Tripoli na mwishowe Sultani wa mji Aljeria. Alifariki Istambul, tarehe 27 Juni 1587, akiwa jemadari mkuu wa Waturuki.

akaenda vilevile alivyozoea kuchungulia kazi ya waashi. Kabla ya kurudi nyumbani mwake alimwita mwashi mkuu, ambaye alikuwa Mkristo, jina lake Mikaeli, aliyewasimamia wafanyakazi wote. Akamwambia: “Mikaeli, usijaze mbao ile sasa hivi; kwa sababu mimi nitaweka humo mbwa yule wa Oran, anayekataa kurudi katika dini ya Uislamu. Nitamzika humo mzima.” Kisha kusema maneno hayo akaenda zake.

Mikaeli akaacha mbao zile alivyoamriwa, lakini akahuzinika sana. Palepale walipomaliza kazi siku ile, akamwendea Hieronimo akamwambia wazi maneno yale aliyoambiwa. Tena akampa shauri, akamsihi: “Uwe imara katika imani yako. Uvumilie mateso, ujitayarishe kufa, kwani wewe u Mkristo mwema. Hakuna shaka, Pasha atafuata kusudi lake. Najua kwamba natayarisha kaburi lako.” Aliposikia habari hiyo, Shahidi hakulegea wala hakukata tamaa. Akasema kwa ujasiri: “Mungu ubarikiwe! Angalia wanadhani kwamba watanitisha. Kweli sitaacha kuwa Mkristo, hata kufa. Bwana wetu Yesu Kristo uwe radhi, unikumbuke, unihurumie, uniondolea dhambi zangu zote.” Wakristo wengine waliposikia habari hizo, wakamwendea na kumtia moyo: “Uwe mwaminifu, uvumilie yote kwa mapendo ya Mungu”. Akawajibu: “Namwamini Bwana, atanipa neema na nguvu kufa kwa ajili ya jina lake. Mniombee kwa Mungu.” Palikuwa na Padri nyumbani mwa watumwa. Akamwendea na kuungama vizuri katika kanisa ndogo ya gereza. Akabaki kanisani muda wa saa nzima. Baadaye Hieronimo akarudi chumbani kwake, akaongeza kusali usiku kucha, akimwomba Mwokozi wetu msaada wa neema ya Mungu. Kesho yake asubuhi akakomunika.

Siku ya 18, mwezi wa Septemba, 1569, saa tatu asubuhi, askari wanne wa Sultani wakaingia gerezani kwa kumtwaa Hieronimo. Huyu alikuwa bado kanisani. Walipomwona wakaanza kumtukana: “We, mbwa! mwenye pembe! Myahudi! Sababu gani unakataa kuwa Mwislamu?” Mtumishi wa Mungu hakuwajibu hata neno moja. Wakamkamata Hieronimo aliyefungwa kwa mnyororo mzito, wakamsukuma, wakampeleka kwa ngome ya Bab-el-Wedi, waliokuwepo Aluj Ali na Waturuki wengi na wakana dini. Alipomwona Hieronimo, Aluj Ali akalia kwa sauti kubwa: “Ewe mbwa, sababu gani unakataa kuwa Mwislamu ?” Shahidi akamjibu: “Sitakuwa Mwislamu kabisa, hata

ungenipa dunia yote, kwani mimi ni Mkristo, nitabaki Mkristo daima". Pasha akamwambia: "Basi, ukikataa kuwa Mwislamu, tazama – akionyesha mbao zilizokuwa tayari kwa kuaka – nitakuzika humo mzima." Hieronimo akamwitikia kwa uhodari wa ajabu: "Fanya tu unavyotaka. Nipo tayari kwa yote. Sitaacha imani ya Bwana wangu Yesu Kristo." Hapo Pasha akatoa amri ya kuondosha minyororo katika mguu wake na kumfuga mikono na miguu kwa kamba na kumweka kifudifudi katika mbao. Askari wakamshika, wakamwondoshea minyororo wa mguu wake, wakamfunga mikono na miguu, wakamlaza katika mbao watakapoaka. Alipowekwa pale, mkanadini Mhispania wa nyumba ya Haj Murad, jina lake Jafer, aliyeitwa zamani Tamango, akakamata mtwango, akaruka juu ya mgongo wake Hieronimo akawaambia waashi walete udongo, akaanza kutwanga udongo juu ya mwili wake shahidi. Wakana dini wengine, wakitaka kumpendeza Aluj Ali, wakamfuata mfano wake, wakakanyaga mwili wa Hieronimo wakautwanga, wakashindilia kwa nguvu udongo juu yake. Yeye hakulia, akawa kama mwanakondoo. Wakajaza vile mbao zile nusunusu kwa udongo, hata shahidi akakata roho kwa kukosa pumzi na kuharibika mwili. Halafu waashi wakaongeza kazi yao wakajaza kabisa mbao. Aluj Ali akasimama pale mpaka wamemaliza. Halafu wakirudi kwao akawaambia wasindikizi wake, njiani: "Kumbe, sikudhani kwamba Mkristo yule angekufa kwa uhodari jinsi tulivyoona".

Ewe, Maria, Mkingiwa dhambi, Malkia wa Afrika, uombe ili Hieronimo apate kutukuzwa, Waisalmu na Wapagani wa Afrika waongoke na waokoke.

Mhashamu Hieronimo, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

**Septemba 19**

Huko Misri, Wakatoliki wanawakumbuka Wat. **Peleo, Nilo** na **Eliya**, maaskofu wa Misri, na **wakleri wengine**, wote wafiadini. Wakahukumiwa kufanya kazi katika migodi huko Palestina. Mwisho wakatupwa motoni kwa ajili ya Yesu Kristo na hivi wakafa mashahidi, mnamo mwaka 310.[106]
Pia kumbukumbu ya Mt. **Kotola**, Misri.[107]
Huko Warri, Nigeria, Wakatoliki wanamkumbuka **Aloisi Odudu**, Padri wa Jimbo, aliyefariki hospitalini siku 4 baada ya kutoroka kutoka waliomteka nyara, mwaka 2018.

Wakoptiki wanamkumbuka Mt. **Julio El-Akfehas**, mwandishi wa maisha ya mashahidi. Yeye mwenyewe alikufa shahidi.[108]
Huko Ethiopia, Wakristu, wanawakumbuka Mt. Abba **Pisora (***Bishora*), askofu wa mji Masil (Meledj kwa Wakoptiki na Metelis kwa Wagiriki); Mfalme **Jusya (***Yasay*), karne la XVIII, alimaliza maisha yake akikaa mtini. Waorthodoksi Tewahedo, wanawakumbuka pia **Basilede** (*Fasiledes*) na **wanaume 14,730** na **wanawake 7** waliouawa pamoja naye.[109]
Waorthodoksi wa Magharibi wanamkumbuka Mt. **Daudi wa Misri**, Mtawa.[110]

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake! Amina.

## Mt. Peleo, Nilo na Eliya, mashahidi, 310.

Mashahidi hawa walihukumiwa kufanya kazi katika magodi huko Palestina, wakati wa dhiki ya mwisho. Waliweza kujenga vikanisa

---

[106] *Roman Martyrology, ed.* 2005.
[107] Dcitionary of Saints
[108] *Coptic Synaxarium: 22 Tute.* Waethiopian wanamkumbuka tarehe 2 Oktoba.
[109] *The Ethiopian Rite Missal, Abba Emmanuel & Abba Brendan Cogavin, 2002, uk 166. Ethiopian Synaxarium: Meskerem 09.*
[110] Rejea Orthodox Saints of the day.

vidogodogo, walipokutana na kuadhimisha misa. Kwa njia hiyo walipokea nguvu ya kuvumilia mateso yote. Gavana wa Palestina, Firmiliani, alipopata habari akamfahamisha Kaizari Galerio jambo hilo. Dikteta huyu akaamuru watu hawa watumwe kufanya kazi katika magodi ya Kipri, wengine katika Mlima Libanus, na wengine mahali pengine. Firmiliani, alipokatwa kichwa wakati ule kwa sababu ya mauji yake, afisa mtendaji akawahamisha Wakristo hawa katika mahali palipotajwa. Lakini kwanza aliamua wanne kati yao wachomwa moto wakiwa hai. Ndiyo Peleo na Nilo, mapadri wawili wamisri, Eliya pia alikuwa padri na Pathermutio, mmisri msomi mmoja mwenye sifa kubwa, wakatupwa motoni na wakafa mashahidi.
Mt. Peleo na wenzako, mtuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

## Mt. Julio Al-Akfehas, mfiadini.



Ni mmojawapo wa Watakatifu wa Kanisa la Koptiki, Misri, ambaye anaheshimiwa sana na kujulikana kama mwandishi wa maisha mengi ya Mashahidi. Julio Al-Akfehas aliishi wakati wa utawala wa Kaizari Dioklesiani mpagani na Kaizari Konstantino mwenye haki.
Tunasoma katika Kitabu cha Watakatifu wa Kanisa la Koptiki kwamba, Bwana Yesu Kristo alimteua kutunza miili ya mashahidi, kuifunika kwa sanda na kuipeleka katika miji yao. Bwana akawatia upofu magavana na hakuna mtu aliyemzuia. Tena hawakumlazimisha kuiabudu miungu ya uongo. Bwana akamlinda kwa ajili ya kuwatunza mashahidi. Aliwatumia vijana 300 kwa kusudi hilo. Wakaandika maisha ya mashahidi na kuyatuma kwa makanisa yao. Alizoea kuwahudumia na kuwafungia vidonda. Mashahidi walimwambia siku moja: “Lazima umwage damu kwa ajili ya Jina la Yesu Kristo, ili uhesabiwe kati ya mashahidi“.

Utawala wa Kaizari Dioklesiani mpagani ulipokwisha, Kaizari Konstantino alitawala. Bwana Yesu Kristo alitimiza waliyosema mashahadi. Bwana alimwamuru aende kwa Arkanio, Gavana wa Samanoud, na kukiri mbele yake Yesu kuwa Bwana. Julio akaenda na Gavana akamtesa vibaya kwa mateso mengi, lakini Bwana Yesu alikuwa anampatia nguvu. Gavana akaamuru aiabudu miungu ya uongo. Mtakatifu Julio akaomba na ardhi ikapasuka na kuwameza miungu ya uongo 70 na makuhani 140 waliowahudumia. Arkanio alipoona kwamba miungu yake na makuhani wao waliangamizwa, akamwamini Bwana Yesu. Julio akaenda, pamoja na Arkanio, kwa Gavana Athribis. Yeye akamtesa vibaya sana, lakini Yesu Kristo akampatia nguvu.
Palikuwa sikukuu kwa ajili ya miungu ya uongo. Wenyeji wakapamba hekalu yao kwa taa, sanamu na matawi ya mitende. Wakafunga malango hadi kesho yake, siku ya kuanza kusherehekea. Mtakatifu Julio akamwomba Bwana aiaibishe miungu yao ya uongo. Bwana akamtuma Malaika wake. Malaika huyu akakata vichwa vya miungu, akapaka rangi nyeusi uso wao kwa majivu, akachoma makuti na miungu yote hekaluni. Kesho yake, wenyeji walipofika kwa sikukuu, wakivaa mavazi mazuri, wakaona yaliyotukia na kutambua udhaifu wao. Basi Gavana Athribis na mkutano mkubwa wakaamini Bwana Yesu Kristo.
Mt. Julio akaenda, pamoja na magavana Arkanio na Athribis, mji Towa. Wakamkuta Iskandros gavana wake. Kwanza alijizuia kuwatesa, lakini baada ya muda, akaamuru askari wake kuwakata vichwa. Julio, na wana wake wawili, Tadros na Yunias; watumwa wake; na magavana Arkanio na Athribis, na watu wengi wakafia dini, kwa jumla watu 1500. Miili ya Julio na wana wake ikapelekwa Aleksandria, mji wao.
Mt. Julio na wenzako, mtuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

**Septemba 20**

Huko Tunisia, Wakatoliki wanamkumbuka, Mt. **Kandida**, bikira na mfiadini, Kartago, wakati wa utawala wa Kaizari Maksimiani. Baada ya kuparuliwa na mijeledi alirithi taji la ushahidi.[111]
Huko Palestina, Mt. **Yohane Mmisri**, mfiadini.[112]
Huko Aljeria na Hispania, Wakatoliki wanamkumbuka Mtumishi wa Mungu **Yohane de Palacios**, Padri wa Shirika la Utatu Mtakatifu, mfiadini Aljeria, mwaka 1616.

Huko Misri, Wakoptiki wanawakumbuka Wat. **Rufino** (*Eunobius*, au *Eunapios*, au *Onanius*) na **Andrea**, wafiadini, wakati wa utawala wa Kaizari Juliani.
Huko Ethiopia, Wakristu wanakumbuka **Kuzaliwa kwake Bikira Maria**. Pia wanamkumbuka Mt. **Matronya**, mfiadini.[113]

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake! Amina.

## **Mt. Yohane Mmisri, mfiadini**,

Hatuna habari nyingi kuhusu mfiadini huyu. Mwanahistoria Eusebio wa Kaizaria anamsifu kwa maneno haya: "Yohane alikatwa viungo kwa sababu ya imani yake kwa Yesu Kristo, na tangu zamani alikuwa amepofushwa, lakini Mungu akamzawadia kwa kumpatia macho ya akili. Mngalimsikia kusoma na kueleza sehemu kubwa za Maandiko Mtakatifu, mngalishangaa. Alikuwa na, siyo roho tu ya Maandiko, bali alikuwa anakariri hata maneno yote. Mimi, Eusebio, nilikuwa shahidi wa jambo hilo, tena siyo mara moja. Nilikuwa nafikiri kwamba mtu wa kweli, mtu muhimu, ni mtu wa ndani, mtu wa ki-roho, kwa sababu mtu wa ki-mwili ukifa, mwingine anaendelea kutenda."
Mt. Yohane, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

---

[111] *Roman Martyrology, ed. 1956*
[112] *Les petits Bollandistes*
[113] *The Ethiopian Rite Missal, Abba Emmanuel & Abba Brendan Cogavin, 2002, uk 167. Ethiopian Synaxarium: Meskerem 10.*

## Mtumishi wa Mungu Yohane de Palacios, 1616

Yohane de Palacios alizaliwa mnamo mwaka 1560 Hispania. Alikuwa mwana wa Bartolome de Palacios na Maria Santisteban. Akavishwa nguo za Shirika la Utatu Mtakatifu katika monasteri wa Burgos, alipoweka nadhiri mwaka 1578. Katika mji ule alijifunza falsafa na teolojia. Akapadirishwa baada ya kumaliza masomo yake. Akaanza kuwahudumia wakristo akihubiri na kuungamisha. Alikuwa mtu wa sala. Mwaka 1590 akachaguliwa kuwa Mwanasheria mkuu wa Ukombozi, yaani alisimamia matoleo yote na mali zote ili kushughulika kuwakomboa wakristo waliotekwa na Waislamu.

Mwaka 1591 akaenda Aljeria na kuwakomboa mateka 119 na 228 na kuwaleta Valencia, Hispania, kwa njia ya meli *Santa Maria de la Serena*, tarehe 20 Januari 1592. Kwa mara ya pili, akaenda tena Aljeria, kati ya Oktoba na Desemba 1594. Pamoja naye walisafiri watawa wenzake Yohane Sanze na Yohane del Aguila kwa kusudi kukaa Aljeria na kuwahudumia Wakristo mateka. Safari hiyo waliwakomboa mateka 189 na 225.

Mwaka 1609 ukombozi mwingine ulipangwa. Yohane del Aguila na Yohane de Palacios wangebaki Aljeria, baada ya mateka kuweka huru, ili kuwasaidia wale ambao wangebaki, na wakati ule Bernado de Monroy angerudi na mateka. Kuvuka bahari kulikuwa kugumu. Dhoruba iliwalazimisha kutia nanga katika bandari ya Ibiza. Wakashambuliwa na maharamia, na mwishowe walifaulu kufika Aljeria, tarehe 1 Aprili 1609. Tarehe 13 Mei, 1609, wakawakomboa Wakristo mateka 130, ambao 69 wakiachiliwa huru mara.

Lakini, kinyume cha mapatano, watawa hawa watatu wakaambiwa na Halmashauri wa mji Aljeria kwamba ni wafungwa. Sababu ni kwamba msichana wa umri wa miaka 10, kwa jina la Fatima, binti wa Mamet Aksa, mkuu mmoja kati ya Waturuki, alitekwa nyara na wabaharia wa Genoa. Tena huko Calvi, Korsica, alilazimishwa kubatizwa. Tena watekwa 130, ambao fidia ililipwa, walinyimwa uhuru. Halmashauri walimlazimisha Bernardo de Monroy kuwashughulikia kumrudisha huru binti huyu Fatima. Tarehe 16 Mei walifungwa katika chumba cha kuogea cha Pasha, mahali ambapo walitendewa vibaya na kula kwa

shida. Baadaye walifungwa katika minara ya mji. Kazi zote za ki-diplomasia za nchi za Ulaya zilikuwa bure. Watawa wakabaki wafungwa.
Miaka walipofungwa waliwahudumia Wakristo mateka, kuwaimarisha katika imani. Waliwapatia sakramenti na kuyaponya magonjwa yao. Hata mwaka 1612, kwa ruhusa ya Pasha, walianzisha hospitali katika mnara ya gereza. Kulikuwa pia chumba kidogo kama ki-kanisa kwa jina la Utatu Mtakatifu. Mbele ya hospitali kulikuwa daktari na nesi mmoja, kwa jina Petro de Torres Miranda, ambaye baadaye aliuawa kwa kuchomwa moto kwa sababu alikataa kukana imani yake.
Watawa hawa watatu walifariki kwa sababu ya mateso yao makali walioyavumilia. Juan del Aguila, kijana kuliko wote, alifariki wa kwanza, tarehe 5 June 1613. Bernardo de Monroy alifariki mwisho tarehe 31 Julai 1622. Yohane de Palacios yeye alifariki tarehe 20 Septemba 1616. Katika miaka ya kufungwa ilisemekana kwamba aliweza kusali masaa matatu kila siku. Mtu mmoja alishuhudia kwamba Yohane de Palacios alifungwa kwa minyororo, kutemewa mate, kupigwa, kubimbirishwa na kubingirishwa, lakini hakulalamika hata mara moja, bali aliwasamehe wote kila wakati.
Mtumishi wa Mungu Yohane de Palacios na wenzako, mtuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

**Septemba 21**

Sisi Wakatoliki tunaadhimisha sikukuu ya Mt. **Mathayo**, Mtume na Mwinjili, aliyefia dini huko Ethiopia. Injili yake iliyoandikwa kwa lugha ya Kiebrania ilipatikana kwa ufunuo wake, wakati wa utawala wa Kaizari Zeno, pamoja na masalia ya Mt. Barnaba, mtume.[114]

Pia, tunamkumbuka Mt. **Ifigenia**, bikira, aliyebatizwa huko Ethiopia na kuwekwa wakfu kwa Mungu na Mtume Matayo na kuishi kwa amani hadi kifo chake.[115]

Huko Mzitawombi, Zimbabwe, Wakatoliki wanamkumbuka **Jorji Bherebhende**, Katekista aliyeuawa, mwaka 1978.[116]

Huko Misri, Wakoptiki wanamkumbuka Mt. **Gregori**, mtawa, Misri.[117]

Huko Ethiopia, Wakristu, wanawakumbuka Mt. **Basilide** (*Fasiladas*), mfiadini, Misri; **Sures**, **Ankitios** na **Mashadra**, wafiadini, mji wa ‘Asni, Misri; **Kausto** (*Kawestos*), mkuu wa mashadhidi wa mji wa Aleksandria, na wenzake; Mt. **Theodora** aliyeishi kama mtawa wa kiume; Akida **Kornelio** wakiamini kwamba alitumwa na Mt. Petro kwenda kuhudumia Kanisa la Aleksandria.[118]

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake! Amina.

## **Mt. Mathayo, Mwinjili na mfiadini**,

Kabla ya kuongoka kwake Mathayo aliitwa Levi. Kwanza alikuwa mtoza ushuru, yaani mtoza kodi, katika pwani ya ziwa la Galilaya. Siku moja, alipokuwa akifanya kazi zake mezani, Bwana Yesu alipita, akamtazama kwa muda, na akamwambia amfuate. Mathayo, mtoza kodi,

---

[114] *Martyrologium Romanum*, ed. 2001.


[115] *Roman Martyrology,* ed. 1956.

[116] Rejea Fr. Neno Contra,, Louis Kalonji, *African Lay Martyrs*, New People Media Centre, 2009, uk.191-192.

[117] *Coptic Synaxarium: 24 Tute.*

[118] *The Ethiopian Rite Missal, Abba Emmanuel & Abba Brendan Cogavin, 2002, uk 167. Ethiopian Synaxarium: Meskerem 11.* Mt. Theodora anakumbukwa katika Kanisa Katoliki tarehe 11 Septemba.

aliacha mara moja ile kazi yake yenye faida nyingi. Kabla hajawaaga jamaa, Mathayo alimwalika Bwana Yesu na wafuasi wake kwenye karamu iliyoandaliwa nyumbani kwake. Wafarisayo, waliokuwa adui za Yesu, hawakupendezwa na jambo hilo. Wakawauliza mitume: “*Mbona mwalimu wenu anakula pamoja na watoza ushuru na wenye dhambi?*” Yesu aliposikia manung’uniko hayo, aliwaambia: “*Wenye afya hawahitaji tabibu, bali walio hawawezi. Lakini nendeni, mkajifunze maana yake maneno haya: ‘Nataka rehema, wala si sadaka’ (Hos 6:6). Kwa maana sikuja kuwaita wenye haki, bali wenye dhambi.*” Mt. 9: 11-13.




Wanahistoria Eusebio na Mt. Epifanio wanatuambia kwamba, baada ya Bwana wetu Yesu Kristo kupaa mbinguni, Mt. Mathayo akahubiri miaka kadhaa huko Uyahudi na nchi za jirani hadi Mitume walipotawanyika. Muda mfupi kabla aliandika kitabu chenye maneno, mafundisho na matendo ya Bwana wetu Yesu Kristo. Alikiita kitabu hicho ‘Injili’, maana yake Habari Njema, kwa kujibu ombi la Wayahudi, na pengine la Mitume wenzake. Alikiandika kitabu chake kwa Ki-aramu, ndiyo lugha ya Wayahudi wakati huo. Lakini nakala ya Kiaramu ya Injili yake imepotea. Nakala ya Injili ya Mathayo tunayo sasa hivi imeandikwa katika lugha ya Kiyunani. Kitabu hicho hakikukawia kutafsiriwa katika lugha nyingine, na baadaye Mt. Hieronimo akakitafsiri katika Kilatini pamoja na vyuo vingine vya Biblia. Inawezekana kwamba Mt. Bartolomeo amechukua nakala moja pamoja naye akienda kuhubiri huko India na kuiacha kule.

Kadiri ya pokeo moja,[119] Mathayo alienda kuhubiri Habari Njema ya Yesu Kristo huko Afrika, yaani Misri, Ethiopia na Aksum (*Axum Abyssinia*), kwa miaka 23. Katika Afrika aliitwa kwa jina la Mtume wa Waethiopia, ‘walio na uso uliounguliwa’. Huko Naddaver, mji mkuu wa

[119] Rejea Abdyas Histoire du combat apostolique, in Brunet Apocryphes, uk. 300 ss.

Ethiopia alipokelewa na Towashi aliyebatizwa na Filipo.[120] Aliposhindana na Waganga asilia wawili, Zaroës na Arfaksat, kwa neema ya Mungu aliwafunulia wenyeji udanganifu wao. Ndipo waganga asilia wakakimbilia Persia na watu wengi wakaongoka na kubatizwa. Alipomfufua Eufranor, mwana wa Mfalme Aeglippo, kutoka wafu, mfalme, malkia na watu wa nyumbani wao na wakuu wengi wa ufalme wakabatizwa.

Ifigenia, binti wa Mfalme wa Ethiopia, pamoja na wasichana wengine, wakaweka nadhiri ya usafi wa moyo na kuenda kuishi katika nyumba moja ambayo ikawa monasteri ya kwanza katika ufalme wa Ethiopia.

Mfalme Aeglippo alipofariki, ndugu yake Hirtace akashika utawala. Ili kuimarisha utawala wake alitaka kumwoa Ifigenia. Hirtace akamwendea Mathayo na kumwomba amshauri Ifigenia kukubali. Mtume akamjibu: "Mtukufu Mfalme afike kwa hotuba nitakayotoa kwa mabikira wakristo waliokusanyika pamoja na Ifigenia, ndipo ataona jinsi ninavyotimiza amri zake." Mathayo akasifu sana ubikira, akiwaalika mabikira wawe tayari kufa kuliko kuukana. Hirtace akakasirika na akaamua Mathayo afe. Inasemekana kwamba alifariki akipigwa mawe na kusulubishwa kichwa chini, huko Hierapolis, na mwishowe kukatwa kichwa.

Kadiri ya pokeo lingine, Mathayo, baada ya kuhubiri Injili katika nchi ya Siria, Persia, Parthia akafika Ethiopia na akaimaliza kazi yake ya utume kwa kumfia Kristo. Nchi ya Ethiopia ilikuwa nchi ya ki-pagani. Mtume akawaongoa baadhi ya wenyeji kwa imani katika Kristo. Akaanzisha Kanisa na kumtawaza Platoni, mfuasi wake, kuwa askofu.

Mathayo alipokuwa anasali kwa bidii kwa ajili ya wokovu wa wenyeji Bwana Yesu akamtokea kwa umbo la kijana. Akampatia gongo na kumwamuru aipande kwenye milango ya kanisa. Bwana akamwambia kwamba: "Gongo itakuwa mti na kuzaa matunda, na chemchemi ya maji itatoka kwenye mizizi yake. Waethiopia watakapojiosha katika maji na kula matunda yake, watapoteza tabia zao mbaya na kugeuzwa kuwa wapole na wema."

Mtume aliposhika gongo na kuelekea kanisani alikutana na mke na mwana wa Mtawala wa nchi, Fulviani, waliopagawa. Kwa jina la Kristo

---

[120] Mdo 8:26-40.

Mtume akawaponya. Mwujiza huu ukafanya kwamba wengi wakabatizwa. Lakini Mtawala hakutaka raia zake wawe Wakristo na kuiacha miungu ya uongo. Kwa hiyo alimshtaki Mathayo kuwa mchawi. Akaamuru kumwua. Wakamweka Mathayo juu ya kuni na kuwasha moto, lakini miali ya moto haikumgusa Mathayo. Fulviani aliaamuru kuzidisha kuni ili kuongeza moto na kuweka sanamu kumi na mbili za miungu ya uongo zikizunguka moto. Miali ikayeyusha sanamu na kuelekea Falviani. Ndipo akamgeukia Mathayo na kumwomba huruma. Kwa maombezi ya Mtume miali ikazimika. Mwili wa Mtume ukawa mzima, lakini akafariki na kumwelekea Bwana.

Mtawala akatubu lakini alikuwa bado na mashaka. Kwa amri yake wakaweka mwili ya Mathayo katika jeneza la chuma na kulitupa baharini. Alifikiri kwamba ikiwa Mungu aliyelinda mwili wake kutoka moto, atamlinda kutoka maji, basi itakuwa haki kumwabudu Mungu wa kweli. Usiku ule Mathayo akamtokea askofu Platoni katika ndoto na kumwamuru kwenda pwani, pamoja na makleri, watapata mwili wake. Fulviani, na serikali yake, wakaenda pamoja na askofu. Jeneza likabebwa na mawimbi, likapelekwa kanisani. Ndipo Fulviani alimwomba Mathayo msamaha. Askofu Platoni akambatiza na kumwita Mathayo kwa amri ya Mungu. Muda si muda Fulviani/Mathayo akajizuru na kupadirishwa. Askofu Platoni alipofariki, Fulviani akachaguliwa kuwa askofu mahali pake.

Inasemekana kwamba mwili wa Mtume Mathayo ukaheshimiwa sana huko Ethiopia hadi mwaka 956. Baadaye ulipelekwa Salerno, katika ufalme wa Napoli, Italia. Kwa sababu ya vita iliyotokea mara nyingi, mwili wake ukafichwa. Miaka mia moja na ishirini baadaye, mwili wake ukagunduliwa na kupelekwa katika monasteri wa Chartres, Ufaransa.

Wat. Mathayo na Ifigenia, mtuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

**Septemba 22**

Sisi Wakatoliki tunawakumbuka siku ya leo mashahidi wa Jeshi la Theba, **Morisi**, **Eksuperansio**, **Kandido**, **Viktori**, **Inosenti** na **Vitalis**, pamoja na **wenzio**, wafiadini. Kadiri ya Mt. Eucherio wa Lyon, Ufaransa, waliouawa kwa amri ya Kaizari Maksimiani, huko mji wa Mt. Morisi Uswisi,[121] mwaka 286.
Huko Misri, Wakatoliki wanawakumbuka Watakatifu **Iraida**, bikira wa mji wa Aleksandria, na **wenzi wake**, wafiadini Antinopolis.[122]
Kumbukumbu ya **Januari**, askari, mke wake **Stefana** (au *Corona*) na **Viktori**, wafiadini, karne la II. Stefana alifungwa kati ya miti miwili iliyobana kwa pamoja. Miti ilipoachiwa mwili wake ukararuliwa katikati. Januari akakatwa kichwa.
Huko Uganda, Wakatoliki wanawakumbuka **Benedikto Kiwanuka** na **Martini Rubanga Anyolitho**, wanasiasa walei, waliouawa na watu wa Idi Amin, 1972.[123].

Huko Ethiopia, Waorthodoksi Tewahedo, wanawakumbuka **Aflahos** na **wenzake**, wote wafiadini. Pia wanaadhimisha uhamisho wa masalia yao kwa mji wa Aleksandria, Misri.[124]
Waorthodoksi wanamkumbuka Mt. **Petro mtumwa**, karne la VI.

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake! Amina.

---

[121] *Martyrologium Romanum*, ed. 2005. Watakatifu wanaohusiana na Jeshi la Thebe: Maurice; Alexander wa Bergamo, Italia; Bessus; Candidus; Cassius and Florentius; Chiaffredo (Theofredus); Constantius; Defendens; Exuperius (Exupernis); Felix and Regula, Watakatifu walezi wa mji Zürich, Switzerland; Fidelis wa Como, Italia; Fortunatus wa Casei, Italia; Gangulphus; Gereon; Magnus wa Cuneo, Italia; Secundus wa Asti, Italia; Solutor, Octavius, na Adventor, Torino, Italia; Tegulus; Ursus wa Solothurn, Switzerland; Victor wa Xanten, Ujermani; Verena wa Switzerland.
[122] *Roman Martyrolgoy*, ed. 1956. Mt. Iraida au Irais anakumbukwa katika Kanisa Katoliki tarehe 22 au 23 Septemba. Wakoptiki wanamkumbuka Irais mwingine tarehe 25 mwezi wa Septemba.
[123] Rejea Fr. Neno Contra,, Louis Kalonji, *African Lay Martyrs*, New People Media Centre, 2009, uk 80-83, 92-93.
[124] *Ethiopian Synaxarum, Meskerem 12.*

## **Mt. Morisi na mashahidi 6600 wa Jeshi la Theba, 287**.



Simulizi la kushangaza mno katika Kanisa la karne la III ni simulizi la vifo vya Mt. Morisi na Jeshi la Theba, Misri. Hadi leo makanisa na miji mingi katika Ulaya inashuhudia tukio hilo na jinsi walivyoteseka kwa ajili ya imani yao kwa Yesu Kristo. Kutoka Genova, Uswisi, na kuelekea Italia, njiani msafiri anapita katika mji mdogo, uitwao Mt. Morisi wa Valais. Zamani mji huo ulifahamika kwa jina la "*Aguanum*", na baadaye uliitwa Mt. Morisi kwa sababu palepale Morisi alikufa shahidi, yeye na askari wenzi, alipokataa kuwaua Wakristo wa mahali pale waliokataa kuwatolea miungu ya Roma sadaka.

Mt. Eucherio,[125] aliandika historia ya mashahidi hawa. Alipendekeza kwamba *Aguanum* uheshimiwe sana, tena sana, "mahali ambapo maelfu wa mashahidi walikatwa vichwa kwa ajili ya Yesu Kristo". Maksimiani, (285-305 B.K.) aliyekuwa Kaizari msaidizi wa Dioklesiani, alituma jeshi kutuliza maasi ya Wagoli katika Ulaya wa kati. Lejioni moja ilikuwa kutoka Theba, Misri, na askari wote (2.000?) walikuwa Wakristo. Kuishukuru miungu ya Roma kwa ajili ya ushindi wao, wote walitazamiwa kuitolea sadaka miungu ya uongo. Askari wote wa Theba walikataa kufanya hivyo na wakaenda kukaa *Aguanum* kuliko kutia amri hiyo. Maksimiani aliposhindwa kuwawezesha kutii, aliamuru kwamba askari moja kwa kumi auawe. Wakafanya hivyo lakini bado askari wote walikataa kuitolea miungu ya Roma sadaka. Kaizari akatolea tena amri kama ya kwanza, lakini tena wote walikataa kutii amri ya kuitoa sadaka. Mt. Eucherio anaeleza kwamba wote waliichukia miungu ya uongo. "Walilelewa kama Wakristo na walifundishwa kwamba Mungu ni mmoja, mwenyezi. Walikuwa tayari kuteswa kuliko kutenda kitu kinyume cha imani yao."

---

125 Eucherio alikuwa askofu wa Lyon, Ufaransa, akafariki mwaka 494 B.K.,

Kiongozi wao na mwenye kuwatia moyo alikuwa Morisi. Chini ya uongozi wake walikuwa makapteni: Kandido, Innosenti, Eksuperansio, Viktori na Konstantino.

Walipokataa kutii amri yake, baada ya kuwauawa askari kwa mara ya pili, Kaizari Maksimiani aliwatisha, kama wataendelea kutotoa sadaka, kuwauawa wote. Mt. Eucherio aliandika jibu lao: "Kaizari, sisi tu askari lakini pia tu askari wa Mungu wa kweli. Tuwiwa kufanya kazi kama askari na kutii, lakini hatuwezi kumkana Yeye ambaye ni Mwumbaji na Bwana wetu, hata Bwana wako, ingawa unamkataa. Katika mambo yote, ambayo si kinyume cha sheria zake, tunakutii kwa nguvu zetu zote, kama tulivyofanya mpaka sasa. Tunawapinga adui wako awaye yeyote, lakini hatuwezi kuchafua mikono yetu na damu ya watu wasio na kosa (Wakristo). Tuliweka kiapo kwa Mungu kabla ya kuweka kiapo kwako. Huwezi kutegemea kiapo chetu cha pili kama tunakiuka cha kwanza. Ulituamuru kuwaua Wakristo, na sisi tu Wakristo. Tunamkiri Mungu Baba, Mwumbaji wa vitu vyote na Mwanawe Yesu Kristo, pia Mungu. Tunawaona ndugu zetu wakikatwa vichwa kwa upanga, na hatuwaombolezi bali tunafurahi kwa heshima yao. Siyo jambo hilo wala uchokozi uliotushawishi kuasi. Tazama, tunazo silaha mikononi mwetu, hatupingi, kwa sababu afadhali kufa tusio na kosa kuliko kuishi katika dhambi."

Katika hasira yake, Maksimiani akaamuru askari wote wa Lejioni wauawe. Wengine hawakuwepo *Aguanum* wakati wa uuaji, bali walikuwepo katika ngome zilizojengwa njiani kati ya Ujerumani, Uswisi na Italia. Wao pia waliuawa mahali walipoonekana. Ndivyo damu ya mashahidi wa Afrika ilitakasa mahali pengi huko Ulaya kwa ajili ya Yesu Kristo: *Aguanum*, Zurich, Soluthurn na Zurzach katika nchi ya Uswisi; Bergamo, Turino, Piacenza, mlima Alpu, Pinerolo, Milano na Ventimilia katika nchi ya Italia ; Terier, Bonn, Köln na Ksanten (Xanten) katika nchi ya Ujerumani.

Miujiza mengi ilitukiwa wakati wa kifo chao cha ushahidi, iliyoandamana na umati wa watu kuongoka. Mt. Eucherio anasema kwamba miujiza mingi ilitendeka mahali walipouawa, kama kufunguliwa na nguvu za Giza na kuponywa. "Nguvu za Bwana inafanya kazi kila siku kwa maombezi ya Watakatifu wake." Zaidi ya miji 70 katika Ulaya inaitwa kwa jina la Morisi. Katika monasteri ya

Mt. Morisi, Uswisi, mkesha wa masaa 24 unaendelea tangu miaka 500. Makanisa, sanamu, miji na mambo mengine yanashuhudia mashahidi hawa.
Mt. Morisi na wenzako, mtuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

**Septemba 23**

Sisi Wakatoliki tunawakumbuka Wat. **Andrea, Yohane, Petro** na **Antonino** wa Syracuse, wafiadini, Afrika ya Kaskazini,[126] mnamo mwaka 900.

Huko Misri kumbukumbu ya **Mathayo I** wa Aleksandira, Patriarki wa 90 wa Kanisa la Koptiki, 1465.
Huko Ethiopia, Wakristu wanamkumbuka Abba **Isaka**, mwanakoriti, mfiadini.[127]
Waorthodoksi wanamkumbuka pia Mt. **Irais**, bikira na shahidi, Aleksandria, 303.[128]

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake! Amina.

## Wat. Andrea na wenzake, 900

Mashahidi Andrea na Yohane, pamoja na watoto wa Yohane Petro na Antonino, waliteswa vibaya sana katika karne la tisa, chini ya utawala wa Ibrahimu. Baada ya kuteka mji Syracuse  Italia, na kuubomoa, Ibrahimu aliwakamata na kuwapeleka Afrika Andrea, Yohane na watoto wake wawili Petro na Antonino. Akawalazimisha kujifunza lugha ya kiarabu na sayansi.
Vijana walipokua, Mtawala Ibrahimu aliwapenda sana kwa sababu ya hekima na fadhila zao. Akamwita Antonino ndugu na akamteua Petro kuwa mkuu wa watumishi wake. Aliposikia kwamba vijana hawa walikuwa wanamwabudu Kristo kisirisiri, Ibrahimu alikasirika sana, aliamuru kuwafunga kwa minyororo ya chuma na kuwapiga kwa mijeledi. Baada ya kupigwa sana, wakamweka Antonino juu ya punda, wakamfunga kwa kamba na kumtembeza katika mitaa ya mji,

[126] *Martyrologium Romanum*, ed. 2005.
[127] *The Ethiopian Rite Missal, Abba Emmanuel & Abba Brendan Cogavin, 2002, uk 168. Ethiopian Synaxarium: Meskerem 13*.
[128] Irais ni Iraide sisi Wakatoliki tunayeheshimu tarehe 22 Septemba.

wakimpiga na kumdhihaki. Shahidi akavumilia yote na kumshukuru Mungu. Petro akatupwa gerezani baada ya kupigwa vikali sana.
Amri ikatangazwa kumkamata Yohane, baba wa vijana hao wawili. Ibrahimu akamshika shingoni kwa mkono wake wa kushoto na kwa mkono wake wa kulia akamchinja kwa kisu. Wakamtupa mwili wake pamoja na miili ya watoto wake. Wakawasha moto na kuitupa miili ndani yake.
Mt. Andrea akamteswa kwanza kwa njaa na baada akachomwa mkuki kifuani mwake. Shahidi alipoanza kumshukuru Mungu, Ibrahimu akamchoma kwa mara ya pili. Mwili wake ulipokaa katika damu yake, wakamkata kichwa kwa upanga.
Wat. Andrea na wenzako, mtuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

## Mt. Irais, bikira na mfiadini, 303

Inasemekana kwamba Irais alikuwa binti wa Padri mmoja wa mji Aleksandria, Misri. Alipokuwa na umri wa miaka 12 alitumwa kuishi katika monasteri moja ya akina mama. Siku moja, wakati wa dhiki iliyosababishwa na Kaizari Dioklesiani, mwaka 303 B.K. alipoenda, pamoja na masista wengine, kuchota maji katika chemchemi, aliona merikebu iliyojaa na mapadri, masista na wakristo waliofungwa na minyororo, chini ya uongozi wa Loukianos, tayari kuuawa kwa ajili ya imani yao. Irais aliacha mtungi wake na akajiunga nao. Akawakaripia walinzi na kudai kuuawa ikiwa watawaua wakristo hawa. Wakamkamata na kumfunga. Akapelekwa mpaka mji Antinopolis pamoja nao. Loukianos alipolia: “Namtemea mate Mungu wa Wakristo“, Irais akainuka na kumtemea mate Loukianos usoni mwake. Loukianos akakasirika na kuamua msichana huyu ateswe vibaya na kukatwa kichwa. Irais alikuwa wa kwanza kuuawa. Baadaye mapadri, mashemasi, mabikira na wengi waliuawa kwa ajili ya Yesu Kristo.
Mt. Irais na wenzako, mtuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

**Septemba 24**

Huko Misri, Wakatoliki wanawakumbuka Mt. **Pafnusi**, mkaa pweke na **wenzake** (kwa jumla 546), wote wafiadini, Misri. Alipoishi peke yake jangwani, alisikia kwamba Wakristo wengi walifungwa. Kwa kuongozwa na Roho Mtakatifu na kwa hiari alimwendea Gavana na kukiri mbele yake kwamba yeye ndiye Mkristo. Mara akafungwa na minyororo ya chuma na kwa muda mrefu akateswa kwa kulazwa juu ya kitanda cha kutesea. Hatimaye alitumwa, pamoja na wengine wengi, kwa Kaizari Dioklesiani. Kwa amri yake Pafnusi akatundikwa kwa mtende, wengine wakafa kwa upanga,[129] mnamo mwaka 303. Kati yao Mt. **Stefania**, shahidi, aliyeuawa huko Denderah, Misri. Alikuwa na umri wa miaka 18.
Huko Afrika ya Kaskazini, kumbukumbu ya Mt. **Leto**, askofu wa Neptis, mfiadini, 479.[130]
Katika Tanzania, Wakatoliki wanamkumbuka Mtu wa Mungu Padri **Stanislas Tessier**, aliyefariki Tanga, mwaka 1946.
Huko Benguela, Angola, Wakatoliki wanawakumbuka **Lusia Katihe**, Sista wa Wafransisko wa Yesu Sakramenti na **Fransisko H. Satchilombo**, Mseminari wa Shirika la Watumishi wa Maongozi ya Mungu, waliouawa mwaka 1998.

Huko Ethiopia, Wakristu, wanamkumbuka Abba **Agato**, mkaa mnarani. Waorthodoksi Tewahedo wanawakumbuka **Makari**, mfiadini, **Bartholomeo**, **Andrea** (*Awedra*), **Nasen** (*Naso*) na **Degana**, padre.[131]
Waorthodoksi wanamkumbuka **Eufrosina,** binti wa Mt. Pafnusi wa Misri.

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake! Amina.

[129] *Roman Martyrology, ed. 1956.*
[130] *Les petits Bollandistes*
[131] *Ethiopian Synaxarium: 14 Meskerem.*

## Mtu wa Mungu Stanislas Tessier, C.S.Sp., Padri 1946

Padri Tessier alizaliwa Ufaransa, mwaka 1887. Alipadirishwa tarehe 28 mwezi wa Oktoba 1912 na kufika Zanzibar mwaka unaofuata. Lakini aliitwa tena Ufaransa wakati wa Vita vya Kwanza vya Dunia kujiunga na jeshi. Alipoachiliwa akarudi Afrika ya Mashariki. Akaanza kazi katika Vikariati ya kitume ya Kilimanjaro na kubaki huko hadi kifo chake.

Kwa muda mfupi akakaa Kilomeni na Kimani, na baadaye akaenda Kilema. Akamsaidia Fr. Augusti Gommenginger hadi mwaka 1929. Akajenga kanisa nzuri linalobaki kuwa ushuhuda wa hamasa na wivu wake. Kazi yake ya kiroho Mungu tu anajua, lakini idadi ya Wakristo iliongezeka sana.

Mwaka 1929 akahamishiwa Kondoa-Irangi. Pamoja na Pd. Krieger, mwanzilishi wa Parokia, akajenga majengo madogo yanayounganishwa na Kondo, akajenga Haubi na shule nyingi. Lengo lake lilikuwa kueneza Elimu na Injili. Watu wakampenda. Mwaka 1934 akarudishwa tena Kilema kuwa msaidizi wa Vika wa kitume. Na wakati ule alikuwa Paroko wa Kilema. Bila kujibakiza alifanya kazi usiku na mchana. Wakati huu alinunua eneo la Maua, mahali ambapo Shirika la Mabruda wa Moyo Mtakatifu wa Maria watakapokaa, na eneo la Marangu, ili kuanzisha Misioni mpya. Mwaka 1937 aliadhimisha sikukuu yake ya miaka 25 ya upadri. Wakristo wengi na mapadri walikuja kumsherehekea. Akapewa zawadi nyingi kwa sababu ya kazi yake nzuri na kiasi cha T.Shs. 2000 ili kujenga shule ya Komela.

Kuanzia Aprili 1938 hadi Novemba 1939 alitawala Vikariati ya kitume wakati Vika alikuwa Ulaya. Wakati wa Vita vya Pili vya Dunia, Vika wa kitume wa Kilimanjaro alikabidhiwa kutawala Prefektura ya Dodoma. Kwa hiyo, Pd. Tessier akatumwa Dodoma kuwa mwakilishi wa Vika. Akafanya kazi kwa nguvu zake zote, siyo kulinda yote yaliyokuwepo bali hata kuwasaidia Wapasionisti kuendeleza kazi zao. Kanisa la Kurio likamalizika. Konventi nzuri ikajengwa huko Kondoa na shule huko Ikasi. Akawatia moyo kuanzisha Shirika la Masista Wazalendo na kujenga seminari.

Padri Tessier aliondoka Dodoma Machi mwaka 1943 na kwenda Misioni ya Gare, katika milima ya Usambara. Kama kawaida yake

alifanya kazi kwa nguvu zake zote. Akamaliza kujenga hospitali na konventi kwa masista wa Kilimanjaro. Alikuwa na ndoto ya kujenga shule kubwa wakati Mungu alimwita kwake. Jumanne, tarehe 24 mwezi wa Septemba, mwaka 1946, sikukuu ya Bikira Maria wa Huruma, Padri Tessier alifariki kati ya saa 3.45 na saa 4.00 kwa ajali. Mti ulimwangukia. Akapokea sakramenti kabla ya kufariki.

Baada ya misa na kifungua kinywa na kusoma ofisio, mnamo saa 3.00 asubuhi Padri alichukua jembe, na kama desturi yake, akaenda kuwaangalia wafanya kazi wakijenga hospitali. Watano walikuwa wanakata mti, siyo mkubwa sana, urefu kama wa mita 25. Wafanya kazi walikuwa wamekwisha funga kamba. Padri Tessier aliwasaidia kuvuta ili kuuangusha mti upande mmoja. Mti ulipoanza kukatika kutoka shina lake Padri Tessier alipaza sauti kubwa na kuwaambia wote kukimbia. Padri Tessier akakimbia kutoka chini kutafuta ulinzi wa mti mkubwa, lakini mti ukachenguka upande mwingine na kumwangukia Padri Tessier. Tawi likamwangukia na kupasua kichwa chake. Baada ya dakika chache akafariki. Kesho yake akazikwa katika shamba la wafu huko Gare.

Kazi zote za Padri Tessier zililenga kitu kimoja tu: wokovu wa watu. Siku moja alipoalikwa kupanda mlima wa Kilimanjaro, akawaambia: “Kwa kusudi gani? Kule hakuna roho ya kuokoa!“ Alikuwa mtume na mtume tu! Wakristo wanakumbuka jinsi alivyowatembelea vigangoni na mashuleni. Zaidi ya mara moja alitembea kms 60, pengine hadi 80 kwa siku moja, akibeba mfukoni mwake mlo wa siku moja, yaani, chupa moja ya maji, ndizi mbili na kipande cha mkate. Alipokuwa misioni alijishughulisha sana kupanga vizuri hifadhi za nyaraka na vitabu vya Parokia, hasa kitabu cha *Status Animarum*.

Alikuwa na upendo wa kitoto kwa Mungu Baba na kumwamini kwa kila jambo, kama Yesu alivyosema: “*kutojisumbua ya kesho, kwa kuwa kesho itajisumbukia yenyewe*“[132]. Alikuwa anafanya kazi kwa Mungu Baba na kwa hiyo alitegemea kupata msaada wake aliohitaji. Alipenda ufukara na aliishi kama mtu maskini, akijitoa kwa ajili ya roho za watu. Alipenda kuhubiri, kufundisha na kutoa sakramenti. Hamu yake kubwa ilikuwa kuokoa roho za watu na kuwapatia neema zote ili waishi

[132] Mt 6:34

ki-takatifu. Alionyesha fadhila za wivu kwa Mungu, upendo na kujinyima. Maneno yake ya mwisho yalikuwa maneno ya upendo kwa kuwatia moyo wengine. Kazi yake ya mwisho ilikuwa kwa ajili ya wagonjwa na wasiojiweza. Alitaka kuokoa hospitali kwa hatari ya kuangukiwa na mti na mti huu ukawa msalaba wake. Kila mwaka Wakristo kutoka parokia mbalimbali wanahiji huko Gare na kuomba kwenye kaburi lake.
Padri Stanilas Tessier, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

**Septemba 25**

Huko Ethiopia, kumbukumbu ya Mt. **Enkua-Marjam**, Mwumgama-dini.[133]

Huko Misri, Wakoptiki wanawakumbuka Wat. **Abadir** (*Apater*) na **Irais** (*Eraee*, au *Herais*, au *Iraja*), dada yake, na **wenzao 3685** wote wafiadini huko Antinoe, Misri.[134] Abadir na Irais walikuwa watoto wa dada ya Basilide, aliyeitwa Baba ya Wafalme.
Huko Ethiopia, Wakristu wanamkumbuka, Abba **Petro** wa mji wa Taraw, Mkoa wa Misri Kaskazini.[135]
Waorthodoksi wanawakumbuka Mt. **Pafnusi** na **wenzake 546** waliokufa mashahidi, chini ya utawala wa Kaizari Dioklesiani (284-305).
Waorthodoksi wa Magharibi wanamkumbuka **Eufrasina wa Aleksandria**.[136]

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake! Amina.

## Watakatifu Abadir na Irais, Mashahidi

Tunasoma katika Kitabu cha Watakatifu wa Wakoptiki habari zao. Walikuwa watoto wa dada ya Basilide, Baba ya Wafalme. Kwa sababu ya cheo ya baba yake, Abadir aliwekwa kuwa *El-Esfeh-selar*, cheo kikubwa katika serikali, huko Antiokia. Alikuwa na desturi ya kusali katika chumba chake. Siku moja Bwana Yesu Kristo akamtokea usiku wa manane na kumwambia: “Amka na umchukue dada yako Irais, muende Misri kupokea taji ya ushahidi. Nitamwagiza mtu mmoja, kwa

---

[133] Dictionary of Saints
[134] *Coptic Synaxarium: 28 Tute.* Baadhi yao: mapadre Cluthus, aliyekuwa pia daktari, Apa Paphnutius wa Tentyra, Apa Isaac wa Tiphre, Apa Shamul wa Taraphia, Apa Simeon wa Tapcho, Sissinius wa Tantatho, Theodore wa Chotep, Moses wa Psammanius, Philotheus wa Pendje, Macarius wa Fayum, Maximus wa Vuchim, Macroni wa Thoni, Senuthius wa Buasti, Simeon wa Thou, Ptolemaeus, mwana wa Eparch, na Thomas wa Tanphot.
[135] *The Ethiopian Rite Missal, Abba Emmanuel & Abba Brendan Cogavin, 2002, uk 169.*
[136] Rejea Orthodox Saints of the day

jina la Samueli, kutunza miili yenu na kuizika kwa heshima.“ Akamtakia amani na kupaa mbinguni. Dada yake pia aliona maono. Akaambiwa: “Nenda kwa Abadir na usivunje amri yake“. Alipoamka, akatetemeka. Akamwendea kaka yake na kumsimulia maono yake, akimwambia kwamba atamtii. Wakaahidi kwenda na kumwaga damu yao kwa ajili ya Yesu Kristo.

Mama yao aliposikia habari hiyo, yeye na watumishi wake wakachana nguo zao na kumfikia Abadir. Mama yake akamsihi asitafute kuwa shahidi. Akamwahidi kwamba hatakwenda kwa Kaizari Dioklesiani kutafuta kuwa shahidi. Moyo wa mama yake, asiyetambua nia yake kwenda mahali pengine kutafuta kuwa shahidi, ukalegea. Na kila siku, Abadir alizoea kubadilisha nguo zake, kwenda kuwaletea waliofungwa maji na kuwahudumia usiku kucha. Alimwomba mlinzi asimwambie mtu yeyote.



Baada ya muda akakumbushwa katika maono amri ya kusafiri. Akamchukua dada yake na wakaenda Aleksandria na Kairo. Wakamkuta Mt. Abekragon akiwatambua na kuwabariki. Kutoka Kairo wakasafiri kwenda Tomwah. Wakingia kanisani na kuomba. Wakaendelea mbele na kufika El-Ashmunin walipomkuta Shemasi Samueli. Siku iliyofuata, pamoja na Samueli walisafiri hadi Ansena (Antinoe). Huko, mbele ya Gavana, wakamkiri kuwa Yesu ni Bwana. Gavana Ariani akawatesa vibaya. Lakini Abadir, alikuwa anasali na kumwomba Mungu awaimarishe katika imani ya kweli. Bwana Yesu akachukua roho zao na kuzipeleka katika mji wa Yerusalemu wa mbinguni. Wakaona makao ya Watakatifu yalivyong’aa mwanga. Baada ya muda Bwana akazirudisha roho zao katika miili yao.

Gavana Ariani akaandika amri ya kuwaua. Akamwapisha Abadir kumwambia jina lake na alikuwa nani. Mtakatifu akamjibu: “Kwanza, apa kwamba hutabadilisha amri yako“. Ariani alipoapa, Abadir akamwambia: “Mimi ni Abadir, *El-Esfeh-selar*“. Gavana, aliposikia jina lake na cheo chake, akalia kwa sauti kuu: “Ole wangu, bwana wangu. Kwa nini hukuniambia kwamba wewe ndiye bwana wangu na

kuniruhusu kukutesa kwa mateso haya makali?“ Mtakatifu akamjibu: “Usiogope, karibu utapokea taji la ushahidi. Kaizari atanitafuta na kutonipata. Atasikia kwamba umeniua. Atakuita na kukutesa. Ndipo utakufa shahidi kwa jina la Yesu Kristo Bwana wetu. Sasa maliza kazi yako.“ Mara Gavana akaamuru wakatwe vichwa.

Waamini wakafunika miili yao katika sanda na Shemasi Samueli akaileta nyumbani mwake. Siku za dhiki zilizopita akailaza katika kanisa kubwa lililojengwa kwa heshima yao. Kule Osjut, Misri, kanisa moja limetabarukiwa kwa jina lao.

Watakatifu Abadir, Irais na wenzenu, mtuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

## Abba Petro wa Taraw

Mtu huyu alibarikiwa na Mungu tangu tumboni mwa mama yake. Alipokuwa mtu mzima alikuwa mtu mkamilifu moyoni mwake. Alijitahidi sana katika majikanio, akimtumikia Mungu kwa njia ya kufunga na kusali daima mchana na usiku. Hakula chakula cha kawaida kinacholiwa na binadamu, lakini aliishi kwa kula kidogo majani aliyopata jangwani. Kwa sababu ya kukosa chakula katika mashindano yake alifanana na malaika. Tena chakula chake kilikuwa kurudiarudia Jina la Bwana wetu Yesu Kristo, usiku na mchana, bila kukoma.

Ilikuwa vyema kwake kutembea juu ya maji ya mto Alon bila kulowesha miguu yake, kwa sababu mwili wake ulikuwa umekauka kabisa, kwa njia ya mateso aliyojipatia. Mateso hayo yalisababishwa na chuma kizito ambacho alibeba mwilini mwake siku zote za maisha yake. Alifanana na mnyama na siyo binadamu. Lakini Mungu alipendezwa kwa namna yake ya kuishi, na akamponya.[137]

Mt. Petro wa Taraw, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

---

[137] *Ethiopian Synaxarium: 15 Meskerem.*

**Septemba 26**

Huko Misri, Wakatoliki wanawakumbuka Wat. **Sipriano** na **Yustina**, bikira, wafiadini.[138] Pia kumbukumbu ya Mt. **Baba Mtakatifu Paul VI**, aliyefanya ziara ya kichungaji huko Uganda, akiwa Baba Mtakatifu wa kwanza kuzuru bara la Afrika kusini ya Sahara. Alifariki mwaka 1978.
Huko Bujumbura, Burundi, Wakatoliki wanawakumbuka **Wakatoliki 30** waliouawa na askari wakati waliohudhuria ibada ya misa, mwaka 1999.

Huko Ethiopia, Wakristo wanamkumbuka Abba **Agato** aliyeweka jiwe kinywani mwake.[139] Waorthodoksi Tewahedo, wanawakumbuka **Warkela**, **Simeoni**, **Marsiano** (*Markenos*), **Lusiano**, **Azremanos**, **Petro**, **Ana**.

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake! Amina.

## **Wat. Sipriano na Yustina, wafiadini, 257**.

Mnamo mwaka 249 Kaizari Desio aliwahamisha Wakristo wengi, waliokataa kuacha imani yao, kufanya kazi katika migodi au kufungwa gerezani. Wengi walikufa, wengine kwa njaa, wengine kwa kuuawa.
Kati yao, kadiri ya **pokeo moja**, Kanisa mahalia la Kartago linawakumbuka kwa namna ya ki-pekee Watakatifu Sipriano na Yustina waliouawa mwaka 257 B.K. Sikukuu yao inaadhimishwa tarehe 2 Oktoba, katika jimbo la Kartago.
Ingawa wote wawili walifariki kama mashahidi wa Kristo, mwanzoni maisha ya Mt Sipriano hayakuwa mazuri. Aliishi Kartago, mji mkuu wa zamani, katika nchi ya Tunisia, Afrika ya Kaskazini. Alikuwa mganga

[138] *Roman Martyrology, ed*. 1956. Majina yao yaliondolewa katika Roman Martyrology ya mwaka 2001, kwa sababu ya kukosa uhakika wa historia. Kadiri ya *Coptic Synaxarium*, sikukuu yao ni 21 Tute, au Septemba 18.
[139] *The Ethiopian Rite Missal, Abba Emmanuel & Abba Brendan Cogavin, 2002, uk 170. Ethiopian Synaxarium: 16 Meskerem.*

mkuu asilia. Na watu wengi walikuwa wanamwendea kutafuta dawa na mbinu zake ili kutega roho za watu na kuwatendea mabaya.

Kufuata **pokeo hilo** tunaambiwa kwamba Sipriano akaenda mji Antiokia kutumia ujuzi wake wa uganga. Siku moja, mvulana mmoja, kwa jina Aglaidas, akamwendea. Nia yake ilikuwa kumtongoza Yustina, msichana mmoja Mkristo. Yustina, katika imani yake ya ki-kristo, kwa kujikinga, alikuwa anafanya tu ishara ya msalaba. Mara mbili pepo walikimbia wakiona ishara hiyo ya msalaba. Mara ya tatu akamtuma Shetani mwenyewe. Yeye pia akakimbia alipoona ishara ya msalaba. Basi mganga alipigwa katika kiburi chake, akiona kwamba uwezo wake unashindwa. Baada ya majaribio mengi alitambua uweza wake Kristo na Injili yake. Akamgeukia Yesu. Akaacha njia zake za uganga na kuanza ukatekumeni. Akabatizwa. Muda si muda akawa Shemasi, tena akapadirishwa huko Antiokia, na mwisho akateuliwa kuwa Askofu wa Kartago. Kadiri ya martirologia ya Roma Sipriano akawa Askofu wa Antiokia.



Hatimaye, kadiri ya pokeo hilo, wakati wa dhiki wa Kaizari Desio, mnamo mwaka 257, B.K. wote wawili, Sipriano na Yustina, wakafa mashahidi wa Kristo. Inatukumbusha maneno ya Mtume Paulo kwamba "*Mungu aliyachagua mambo mapumbavu ya dunia awaaibishe wenye hekima; tena Mungu alivichagua vitu dhaifu vya dunia ili aviaibishe vyenye nguvu.*"1 Kor 1:27.

Wat. Sipriano na Yustina, mtuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

**Septemba 27**

Huko Misri, Wakatoliki wanamkumbuka Mt. **Baula**, mfiadini, Misri. Na huko Uhabeshi, kumbukumbu ya **Salusio**, abate.[140]
Huko Ufaransa na Tunisia, Wakatolii wanamkumbuka Mt. **Vinsenti wa Paulo**, aliyekaa Tunisia miaka miwili 1605-1606.

Wakoptiki wanakumbuka siku ya leo **Mwujiza Mungu aliofanya kwa ajili ya Mt. Atanasi**, Patriarka, na askofu wa 20 wa Aleksandria.[141]
Huko Ethiopia, Wakristu wanamkumbuka Abba **Dionisi**, Patriarka, askofu wa 14 wa Aleksandria.
Waorthodoksi Tewahedo, wanawakumbuka **Labiba** (*Liba*), **Siriano** (*Akirianos*), **Yustini**, na **Tekaseltes**.[142]
Waorthodoksi wanamkubuka **Absadi**, 1381, mfuasi wa Mt. Eustasio. Alianzisha monasteri ya Debra Mariam mnamo mwaka 1374, sasa katika nchi ya Eritrea. Pia wanawakumbuka Mt. **Kalistrasto** wa Kartago na **wenzake 49**, 304.

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake! Amina.

## Mwujiza kwa ajili ya Mt. Atanasi, Karne la IV

Mwujiza huu unasimuliwa katika kitabu cha Watakatifu wa Wakoptiki Misri. Kaizari Konstansio, mwana wa Kaizari Konstantino, alipoasi imani ya ki-katoliki na kujiunga na Wafuasi wa Ario, alimtuma Gawargios huko Aleksandria, pamoja na askari 500 na barua ya kutawazwa Gawargios askofu wa Aleksandria badala ya Askofu Atanasi. Akaamuru Gawargios kukiri imani ya Ario na kuwaua wote wasiokubali imani hiyo.
Alipofika Aleksandria alianza kuhubiri na kufundisha imani ya Ario, lakini watu wachache walimfuata. Kwa hiyo aliwaua watu wengi na

[140] *Les petits Bollandistes*
[141] *Coptic Synaxarium: 30 Tute.*
[142] *The Ethiopian Rite Missal, Abba Emmanuel & Abba Brendan Cogavin, 2002, uk 171. Ethiopian Synaxarium: 17 Meskerem.*

Askofu Atanasi akajificha kwa muda wa miaka 6. Baadaye akaenda Konstantinopoli kwa Kaizari na kumwambia kumrudisha katika kiti chake cha uaskofu au kumchinja, ili apate taji la ushahidi. Kaizari akawaamuru watu wake kumweka katika boti ndogo na kumwachia meli aende baharini bila chakula wala kinywaji, au kiongozi. Kaizari alifikiri kwamba Atanasi atakufa kwa njaa, au kiu au atazama baharini. Kwa njia hiyo alidhani kwamba atamwondoa mtakatifu huyo, pamoja na mafundisho yake yanayopinga uzushi wake. Wakafanya kama alivyoamuru.

Boti ikaenda kwa utaratibu na amani kadiri ya mapenzi ya Bwana na utunzaji wake. Atanasi alisindikizwa na malaika waliomhudumia hadi alipofika Aleksandria, siku tatu baadaye. Waamini waliposikia kwamba Mchungaji wao amefika, wakafurahi mno na wakaenda kumpokea kwa mishumaa na nyimbo za shangwe. Wakampeleka kanisani na kumfukuza Gawargios na wafuasi wake. Mtakatifu Atanasi akakumbuka siku hiyo kwa sikukuu kubwa kumshukuru Bwana.

Mt. Atanasi, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

## Mt. Vinsenti wa Paulo, 605-606

Katika maisha ya Mt. Visenti tunasoma mambo yafuatayo: Vinsenti alienda mji Marseilles kuchukua haki yake moja. Katika safari ya kurudi alipanda meli kuelekea Narbonne. Meli na watu wote wakaangukwa katika mikono ya maharamia. Wote wakauzwa kama watumwa huko Tunis. Vinsenti akabadilishwa mara nyingi na mabwana. Mungu alitaka aonje mambo yote watumwa wakristo wanaoteswa ili afanye kazi kwa nguvu kuwaweka huru.

Mwishoni muratadi (aliyeasi dini yake ya kikristo) mmoja wa mji Nice, Ufaransa, akamnunua na kumpeleka katika temat yake (yaani shamba lake). Kulikuwa nchi ya joto na jangwani. Mungu akatumia mke mmoja wa bwana wake kumwondoa mume wake katika ukanaji wa dini ya kikristo na kumweka huru Vinsenti. Aliandika katika barua moja: “mwanamke huyu, mdadisi kujua jinsi tunavyoishi, alikuwa anakuja kila siku mahali nilipoishi. Siku moja akaniamuru kuimba sifa ya Mungu wangu. Nikikumbuka *Quomodo cantabimus in tierra aliena* (tuimbieje katika nchi ya ugeni?) ya wana wa Israeli, watumwa wa

Babylonis, kwa machozi machoni, nakaanza kuimba *Super flumina Babylonis*, "*Kando ya mito ya Babeli*,"[143], na baadaye *Salve Regina*, na mambo mengine mengi. Ajabu! Jinsi alikuwa anafurahi sana kunisikiliza. Jioni hakukosa kumwambia mume wake kwamba alikosa kuacha dini yake, ambayo yeye aliona kwamba ni dini mzuri sana kwa sababu ya masimulizi na sifa chache nilizomwimbia. Alisema kwamba alijisikia raha kubwa nilipokuwa naimba sifa za Mungu."

Vinsenti alitambua kwamba kulikuwa maajabu yanayotendeka, mwanamke huyu akafanya juu chini ili neema ya Mungu imwangukie mume wake. Muda si muda mume wake akapanga kutoroka Ufaransa pamoja na Mtakatifu Vinsenti. Wakatimiza mipango yao baada ya miezi kumi. Muratadi huyu akapokelewa mji Avignon na Mkuu Montorio, ambaye alitaka kuwapeleka wote wawili Roma. Vinsenti akafarijika sana kujikuta mjini Roma, mji mkuu wa ukristo, makao wa Baba Mtakatifu, mahali ambapo miwili ya Mitume Petro na Paulo imezikwa, pamoja na watakatifru wengi na mashahidi wengi waliomwaga damu kwa ajili ya Yesu Kristo. Akalia machozi ya furaha.

Mt. Vinsenti utuombee na Mungu awajalie Waislamu wengi wamtambue Yesu Kristo kama Mwakozi na Bwana wao.

---

[143] Zab 137

**Septemba 28**

Huko Aljeria, Wakatoliki wanawakumbuka Wat. **Marsiali** na **Laurenti** na **wengine ishirini**, wote wafiadini.[144]
Huko Kenya, Wakatoliki wanamkumbuka Mtumishi wa Mungu, **Mariana Cavallo** (Eugenia), sista wa Shirika la Masista wa Consolata, aliyeuawa na waasi MauMau, mwaka 1953.
Huko Deim Zubeir, Sudan ya Kusini, Wakatoliki wanamkumbuka **Mariano Juma Sabun**, aliyefariki baada ya kuteswa na Waislamu, mwaka 1994.

Huko Ethiopia, Wakristu wanawakumbuka Abuna **Eustasio (Ewostatewos)**; **Mar Yakobo**, mpiganaji, padri, mfiadini huko Siria; Abba **Nob**, mwanakoriti. Waorthodoksi Tewahedo, wanawakumbuka Mt. Abba **Honorio** (*Onorewos*), mwalimu wa monasteri wa Segadj, Mt **Stephen**, padre, **Filotheo**, mtenda miujiza, **Aboli** na **wenzake wanaume arobaini na wanawake ishirini**, wote wafiadini. Pia wanawakumbuka **Eufemia** (*Efomya*), mfiadini, na Abba **Finomis**, **Selhan**, **Akalaeles** na **Isaka**.[145] Kumbukumbu ya Mt. **Absadi**, mmonaki, mfuasi wa Ewostatewos, Shahidi1381.

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake! Amina.

## Abuna Eustasio, Mmisionari

Eustasio anaitwa na Wakristo wa Ethiopia 'Mwalimu wa imani na Mhubiri wa Injili'. Baba yake aliitwa Christos Mo'A, na mama yake Sena Haywat. Wote wawili walikuwa wenye haki mbele ya Mungu. Baba yake, baada ya kupata habari njema kutoka kwa malaika, akampata mtoto na kumwita Ma'Akara ,'Egzi'E. Alimfundisha Zaburi za Daudi na mafundisho ya Kanisa. Baadaye akamchukua na kumpeleka

---

[144] *Roman Martyrology, ed. 1956.* Pamoja nao: Gagilio au Gargilio, Marko, Faustino, Viktori, Kandido, Valeria, Longese, Selerina, Donatula, Fortelea, Lusiosa, Emilie, Gagilo, Plasido, Viktoria, Prisko, Juliano, Kristofa, Nobili, Sekundilo
[145] *Ethiopian Synaxarium: 18 Meskerem.*

monasteri ya Abba Zakaria, mjomba wake. Abba Zakaria alipomwona alitambua kwamba neema ya Mungu ilikuwa juu yake. Akamfundisha sheria za utawa na kumvisha nguo za kitawa. Kijana huyu akafunga na kusali kwa utauwa wote hata watawa wazee wakamshangaa kwa ukakamavu wake. Akajaliwa na Mungu vipaji vya hekima na ujuzi. Baada ya muda akapewa daraja la ushemasi na akahudumia katika Kanisa la Mt. Stefano.

Bwana wetu akamtokea, pamoja na Mikaeli na Gabrieli, akamkumbatia na kumvuvia usoni mwake Roho Mtakatifu. Akamwambia: "Mpendwa Eustasio, nimekuchagua tangu tumboni mwa mama yako na kukutuma kuwa Mwalimu wa mataifa kutoka Ethiopia hadi Armenia. Utahubiri Injili bila kuogopa wala kutetemeka. Anayekusikiliza ananisikiliza; Anayekukataa ananikataa mimi mwenyewe." Bwana Yesu Kristo alipomwambia hayo akapaa mbinguni. Eutasio akamwendea askofu na akapadirishwa. Akaanza kuhuburi Injili. Watu wengi wakakusanyika na wakawa wafuasi wake. Mfuasi bora miongoni mwao alikuwa Abba 'Absadi. Wengi wakaongoka na kuacha matendo yao maovu. Mafundisho yake yakaenea ulimwenguni. Zamani zake sheria ya kushika Jumapili na sikukuu zikatangazwa. Hakutoka nje ya mafundisho ya Mitume, kwa upande wa kulia wala kwa upande wa kushoto.

Mara mbili akaenda kuhiji Yerusalemu. Mungu akafanya miujiza na maajabu mengi kwa mikono yake. Akafungua macho ya vipofu, akaponya wenye kupooza na kufukuza pepo. Kwa mapenzi ya Mungu alipoamua kwenda Yerusalemu, akawakusanya wafuasi wake na kuwaambia kushika sheria zote za utawa na kujilinda na wapagani. Akamteua 'Absadi kuwa mkuu wao. Akaenda Yerusalemu akifundisha na kushika Jumapili. Akamfikia Askofu Mkuu 'Abba Benyamini na kubarikiwa naye. Wakapatana kuhusu imani yao. Akazunguka mahali patakatifu, na baadaye akatelemka kwenye mto wa Yordani na huko akabatiza.

Akaelekea kwenda katika nchi ya Armenia. Alipofika pwani ya bahari aliwaomba mabaharia ruhusa ya kupanda katika meli. Wakakataa. Basi akatupa kilemba chake katika bahari, akakibariki kwa jina la Utatu Mtakatifu na kufanya ishara ya msalaba juu yake. Ndipo akapanda juu ya kilemba kama kupanda katika meli. Malaika wawili walimtendea kama mabaharia na Bwana mwenyewe alikuwa rubani wake.

Wakawachukua wafuasi wake ambao hawakuwa na hofu ya bahari. Eustasio akawaambia wafuasi wake: “Angalieni msilipe kisasi na msifuge moyoni mwenu uovu na kijicho. Lakini ni kama mmoja wenu yu karibu ya kufariki“. Kabla hajamaliza maneno yake mfuasi wake mmoja akaanguka baharini na kuzama majini, kwa sababu moyoni mwake alikuwa anafuga kisasi na kijicho. Kwa neema ya Mungu wakavuka bahari na kufika katika nchi ya Armenia. Akakutana na Askofu mkuu na kumtolea heshima. Askofu alipomwona akafurahi na kumpokea kwa furaha kubwa mno. Abba Eustasio akaendelea kuwafundisha watu kushika mafundisho ya Mitume kadiri ya maagizo ya Kanisa.

Wakati wa kuacha ulimwengu huu ulipotimia, Bwana Yesu Kristo akamtokea na kufanya agano naye kwa ajili ya wale watakaoomba kwa jina lake, wale watakaomkumbuka katika ibada na wale watakaoandika maisha yake. Alipofariki, askofu na mapadri wakamzika kwa heshima kubwa katika kanisa la Mar Mehnam, yaani Behnam Shahidi. Ishara na miujiza mingi ikatokea kwenye kaburi lake.

Mt. Eustasio, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

## Mariano Juma Sabun, 1994

Tarehe 18 Agosti, 1994, Wakristu wa Deim Zubeir walialikwa na Waislamu kushiriki katika sikukuu ya kuzaliwa kwake Muhammadi. Wakristo wachache waliweza kuhudhuria maandamano, baada ya kulazimishwa na waandalizi wake. Walipoandamana Maulana Faisal Miskin alianzisha wimbo: “*La Allah ila Allah*“, baadhi ya walioandamana walibadilisha maneno. Zaidi ya hayo, kuliko maneno: “*Muhammadi Rasuul Allah*“ (Muhammadi ni nabii wake) waliingiza kwa Kibelanda maneno yatokanayo na wimbo mmoja wa kutahiriwa: “*La hilah illa Allah vrumbete wa di so la‘ ku Nzobo la ku nazo ya*“ (mtu ambaye hajatahiriwa hasikii neno, ni mkaidi). Aliposikia mabadiliko ya maneno Antoni Petro alimtuma Fransisko kuwaambia watu kuacha kuimba. Maneno hayo hayakuwa matusi kwa Waislamu, lakini Waislamu walichukua nafasi hiyo kuwatesa Wakristo.

Jioni mwa tarehe 28 Agosti askari walianza kuwasumbua Wakristo. Kati ya 28 Agosti na 4 Septemba, watu 17 (wanaume 13 na wanawake 4)

walikamatwa, wakapelekwa katika kambi la jeshi na kupigwa. Walilazimishwa kukiri kwamba mabadiliko ya maneno katika wimbo wa kiislamu yamepangwa kabla na Mkatekista Mkuu Filipo Simon Rihan, au kwa msaidizi wake Petro Antoni Musa. Ilionekana wazi baadaye kwamba uvumi huo ulisambazwa na maulana Faisal Miskin ambaye alisilimu karibuni.

Mariano Juma Sabun, 23, alikuwa miongoni mwa wale waliokamatwa jioni mwa tarehe 28 Agosti. Walimlazimisha kumshtaki Filipo. Akakataa. Aliachiliwa tarehe 2 Septemba 1994, lakini, siku nne tu baadaye akakamatwa tena. Aliachiliwa siku nanne baadaye, kwa dhamana iliyolipwa na Mwalimu Dominiki Edwin Misa. Tarehe 23 Septemba akaitwa tena na Polisi, pamoja na watu 8. Wakalazimishwa kutembea kwa miguu kms 100, hadi Raga, mahali ambapo kesi yao itasikilizwa. Wakafika Raga jioni ya tarehe 26 Septemba. Usiku ule Mariano alipelekwa hospitalini akiumwa kifuani, matokeo ya mapigo aliyopokea kutoka kwa askari. Akafariki tarehe 28 Septemba 1994. Akazikwa kesho yake katika shamba la wafu la Khor Abuna.[146]

Mariano, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

[146] Rejea Fr. Neno Contra,, Louis Kalonji, *African Lay Martyrs*, New People Media Centre, 2009, uk. 178-179.

**Septemba 29**

Sisi Wakatoliki tunasherekea sikukuu ya Mt. **Mikaeli** Malaika Mkuu[147], na pamoja naye Malaika **Gabrieli** na **Rafaeli**.
Huko Ethiopia, Wakatoliki wanamkumbuka **Romana-Warq**, binti wa Na'od, Mfalme wa Ethiopia.[148]

Huko Misri, Wakoptiki wanakumbuka kwamba Patriarka **Severo**, askofu wa Antiokia, alizuru Misri.[149]
Huko Ethiopia, Wakristu wanamkumbuka **Siriaki** (*Kirkos*), mkaa pweke jangwani.[150]

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake! Amina.

## Sikukuu ya Wat. Malaika Wakuu Mikaeli, Gabrieli, Rafaeli.




Jina la 'Malaika' ni jina linalomaanisha ofisi na siyo hali. Malaika ni roho tupu, nao hukaa katika raha ya milele mbinguni, wakimtukuza Mungu daima. Wanaitwa Malaika wakati tu wanapotumwa na Mungu hapa duniani. Wanajulikana kwa majina pia ili kuonyesha nguvu waliyo nayo na kazi wazitendazo. Wale wanaotuletea habari ndogo kutoka kwa Mungu wanaitwa Malaika, lakini wale wanaotuletea habari kuu wanaitwa Malaika Wakuu. Kwa hiyo malaika aliyetumwa kwa Bikira Maria

---

147 *Roman Martyrology*, ed. 1956.
148 *The Ethiopian Rite Missal, Abba Emmanuel & Abba Brendan Cogavin, 2002, uk 171. Ethiopian Synaxarium: 19 Meskerem.*
149 *Coptic Synaxarium: 2 Babah.*
150 *The Ethiopian Rite Missal, Abba Emmanuel & Abba Brendan Cogavin, 2002, uk 171. Ethiopian Synaxarium: 19 Meskerem.*

alikuwa Gabrieli, mmojawapo wa Malaika wa tabaka la juu, kwa sababu alimletea Maria habari kuu kuliko zote zihusuzo wokovu wa wanadamu. Majina ambayo kwayo malaika wanajulikana wanapotuletea ujumbe wa Mungu yanaambatana na kazi zao. Ndiyo kusema yana maana maalum.
Mikaeli maana yake ni 'Nani aliye sawa na Mungu?'
Gabrieli maana yake ni 'Nguvu ya Mungu'.
Rafaeli maana yake ni 'Uponyaji wa Mungu'.
Kwanza Mungu aliwaumba malaika katika hali ya utakatifu. Kabla ya kuwaweka mbinguni kwenye raha ya siku zote, Mungu aliwajaribu kuona kama ni watii kweli. Malaika Lusifa alimwasi Mungu. Kwa kiburi chake alitaka kuwa kama Mungu aliposema: "*Nitapanda mpaka mbinguni, nitakiinua kiti changu juu kuliko nyota za Mungu; nami nitaketi juu ya mlima, nitafanana na yeye Aliye juu.*"[151]. Aliwaasisha pia malaika wengi pamoja naye. Malaika Mikaeli, pamoja na malaika wema, alipigana nao akisema: "Nani aliye sawa na Mungu?". Malaika waasi mara walifukuzwa mbinguni, lakini Malaika wema wakajaliwa kumwona Mungu na kufurahi bila kikomo. Mtakatifu Mikaeli ndiye mkubwa wa malaika wote wema.
Husemwa kuwa Malaika **Gabrieli** alimwongoza nabii Danieli kuandika juu ya kutawala kwake Masiya.[152]Alitumwa kwa Danieli, aliyekuwa akisali na kumwomba Mungu Waisraeli warudi kutoka uhamishoni, ili kumpasha habari kwamba watawekwa huru kutoka Shetani. Malaika huyu mkuu akamtokea Danieli na kumwambia kuwekwa huru wana wa Israeli kutokana na kufungwa kwao huko Babiloni; kujengwa upya Hekalu huko Yerusalemu na kutangaza ujio wa Bwana wetu Yesu Kristo. Akahesabu idadi ya miaka kwa ujio wa Yesu Kristo na kumfahamisha Danieli kwamba Yesu Kristo atauawa na baadaye, mji wa Yerusalemu utabomolewa; na kwamba hakuna Kristo atakayekuja baada ya yeye isipokuwa Makristo wa uongo.
Ndiye aliyepasha habari Zakaria ya kuwa Elizabeti katika uzee wake atamzaa mtoto atakayeitwa Yohane Mbatizaji,[153]. Ndiye, aliyempasha habari Bikira Maria ya kuwa atakuwa mama wa Mungu kwa tendo la

---

[151]Isa 14:13-14
[152]Dan 9:20-27.
[153] Lk 1:11-20

Roho Mtakatifu,[154] Inaonekana kwamba ndiye anayehusika kuhusu habari zote za ujio wa Masiya. Aliwapasha habari wachungaji ya kuwa Mkombozi amezaliwa Bethlehemu,[155] na alimwambia Mtakatifu Yosefu amkimbize mtoto pamoja na mama yake kwenda Misri,[156]. Na ndiye, aliyewashauri kurudi Nazareti.[157]

Mababu zetu wa Kanisa wanatusihi kusherehekea sikukuu kwa heshima yake kila mwaka. Tumwombe atuombee ili Bwana wetu Yesu Kristo, Mwokozi wetu, atuweke huru na maadui wetu, kwa sababu ni mkuu na anasimama mbele ya Kiti chake. Kwa maombezi yake tupate neema ya Mungu wetu, anayestahili kuupokea utukufu, heshima, uweza, sifa na shukrani zetu, siku baada ya siku.

Tunapata habari ya Malaika **Rafaeli** katika kitabu cha Tobiti. Siku moja baada ya kuzika maiti ya ndugu yake, Tobiti alichoka, akalala nje. Kinyesi cha shomoro kilimwangukia machoni, akawa kipofu. Tobiti alikuwa na mtoto aliyeitwa Tobia. Akamtuma kwenda mbio huko Rage, mji wa Umedi, kutaka fedha alizomkopesha mtu mmoja rafiki yake. Tobia hakujua njia, kwa hiyo akamtafuta kijana wa kwenda naye. Siku ya kwanza alipofika kwenye mto Tigri, Tobia alishuka mtoni kunawa. Alipoingia majini samaki mkubwa akajitokeza kutaka kumwuma. Tobia akapiga kelele kwa woga, lakini kijana alimwambia: "Mkamate samaki, umvute ng'ambo na kisha umpasue, uweke pembeni moyo, maini na nyongo, kwani ndiyo dawa ya kufaa".

Kisha kurudi kutoka safari yao, kabla ya kufika kwao, kijana akamwambia Tobia njiani: "Ukifika nyumbani, twaa nyongo ya samaki, mpake baba yako machoni, na kisha atapona". Tobiti na mkewe Anna walitoa machozi ya furaha walipomwona mtoto wao amerudi. Walimshukuru Mungu kwanza, halafu Tobia akatwaa ile nyongo, akaipaka kwenye macho ya baba yake. Yakatoka maganda meupe, kisha muda wa saa fulani baba yake aliona vizuri. Walimwita kijana kiongozi kumshukuru kwa kumpatia nusu ya mali yao, lakini yule kiongozi akawajibu: "*Mimi ndimi Rafaeli, mmojawapo wa malaika watakatifu*

[154] Lk 1:26-38.

[155] Lk 2:9-14,

[156] Mt 2:13

[157] Mt 2:19-20. Rejea tarehe 20 Juni Waethiopian wanamsherekea Malaika Mkuu Gabrieli

*saba, wapelekao sala za watakatifu, na kuingia mbele za utukufu wake Aliye Mtakatifu*.“ Tob 12:15.
Waorthodoksi wa Ethiopia wanataja majina ya Malaika Wakuu wanne wasiotajwa katika Biblia: Urieli, Surieli, Ragueli na Sakue’eli. Na kila Malaika Mkuu saba ana sikukuu yake tarehe fulani.[158]




Lakini Malaika **Mikaeli** ana nafasi ya pekee kwa Wakoptiki na Waorthodoksi, kwa sababu licha ya sikukuu yake, anakumbukwa tarehe 12 ya kila mwezi. Ndiye, yeye aliyewaua askari 185000 wa jeshi la Senakeribu, mfalme wa Ashuru aliyezingira mji Yerusalemu.[159] Ndiye yeye akamwokoa Danieli na makanwa ya simba.[160] Ndiye, yeye aliyetumwa na Mungu kwa nabii Habakuki, katika mji wa Yerusalemu, alipobeba mlo wa dengu kwa wavunaji mashambani. Mt. Mikaeli akamchukua Habakuki kwa nywele zake, alipobeba chakula, na alimpeleka mjini Babeli. Danieli akala chakula na Mikaeli akamrudisha nabii Habakuki huko Uyahudi.[161] Mara akasimama karibu na wavunaji. Kwa sababu hiyo Waalimu wa Kanisa waliamuru kumsherehekea Mikaeli, Malaika Mkuu, tarehe 12 ya mwezi wa Ginbot.
Simulizi ifuatayo inaeleza heshima kubwa Wakoptiki na Waorthodoksi wanayo kwa Malaika mkuu Mikaeli. Eufemia alikuwa mke wa mwanamume Mcha-Mungu na mwenye huruma kwa maskini. Mwanamume huyu aliadhimisha kila mwezi sikukuu kubwa tatu. Siku ya 12 ya mwezi[162] alimsherehekea Mt. Mikaeli, Malaika Mkuu; siku ya 21 ya mwezi alisherehekea sikukuu ya Bikira Maria, Mama wa Mungu na siku ya 29 alisherehekea sikukuu ya Kuzaliwa kwake Bwana Wetu

---

[158] Mikaeli tarehe 12 ya kila mwezi; Gabrieli tarehe 13 Senne; Rafaeli 13 Tahsas; Urieli tarehe 21 Hamle; Surieli tarehe 27 Tir; Ragueli tarehe 1 Meskerem; Sukue’eli tarehe 5 Hamle.
[159] 2 Fal 19:35.
[160] Dan 6:22
[161] Dan 14:33-39.
[162] Wapagani wa Aleksandria walimwabudu Zuhal, mungu wa uongo, aliyekuwa na sanamu na hekalu lililojengwa na Malkia Kleopatra, siku ya 12 ya mwezi wa Baounah.

Yesu Kristo. Siku ya kuaga dunia ilipofika alimwambia mke wake kushika desturi hizo, kuendelea kuwapa maskini na kutenda matendo ya huruma, hasa wakati wa sikukuu hizo tatu. Alichora picha ya Mt. Mikaeli na kumpatia mke wake.

Baada ya kifo cha mume wake, Eufemia aliendelea kuyatimiza mapenzi ya mume wake. Shetani, akimwonea wivu, akamtokea kwa umbo la mtawa. Akampatia pole kufiwa na mume wake na kumshauri kuolewa tena, kuzaa watoto na kuacha kutenda matendo ya huruma kwa sababu atafilisika baada ya muda mfupi. Akamwambia pia kwamba mume wake aliingia katika ufalme wa Mungu na kwa hiyo hahitaji tena matendo ya huruma. Eufemia akamjibu mtawa: "Niliahidi kutofunga ndoa tena baada ya kifo cha mume wangu." Na akaendelea kumwambia: "Ikiwa ndege, kama njiwa na kunguru, hawachukui mwenzio mwingine baada ya kufiwa, namna gani wanadamu, walioumbwa kwa sura na mfano wa Mungu, wanaweza kufanya hivyo?" Shetani akamwacha na kuondoka kwa hasira.

Sikukuu ya Mt. Mikaeli ilipofika na alipotayarisha kila kitu kadiri ya desturi, Shetani akamtokea kwa umbo la malaika na akamwambia: "Amani iwe kwako. Malaika Mikaeli amenituma kwako, na kukuambia kwamba uache kutoa sadaka kwa maskini, uolewe tena na mtu mwaamini." Tena akasema: "Mwanamke bila mwanamume ni kama meli bila nahodha."  Na akaanza kuthibitisha maneno yake kwa kuchukua kutoka biblia mifano ya watu watakatifu, Abrahamu, Isaka, Yakoko, Daudi na wengine wengi kama hao, waliochukua wake na kumpendeza Mungu. Huyu Eufemia akamjibu: "Ikiwa wewe ni malaika wa Mungu, msalaba, ishara ya kazi yake, uko wapi ? Kwa sababu askari wa Mfalme haendi mahali popote bila silaha hiyo." Shetani aliposikia maneno hayo alijigeuza na kuonekana kama Shetani kweli na akamrukia ili kumkaba na kumwua. Akalia na kumwita Mikaeli, ambaye ilikuwa sikukuu yake. Akamwokoa mara moja. Na baadaye akamwambia: "Nenda utayarishe mambo yako kwa sababu utaaga dunia leo hii. Na tazama Bwana amekutayarishia jambo ambalo jicho halijaliona na sikio halijalisikia, na halijaonekana moyoni mwa mtu." Baadaye akamsalimu kwa salama ya amani na kupaa mbinguni.

Baada ya kuadhimisha sikukuu ya Mikaeli, Malaika Mkuu, Eufemia akawaita baba Askofu na mapadri. Akawagawia fedha zake zote ili

awape maskini na wahitaji. Akaichukua picha ya Mikaeli na akasali mbele yake. Akaiweka usoni na kifuani mwake na akaaga dunia kwa amani.[163]

Malaika Wakuu wa Mungu, mtusaidie kumhimidi Bwana pamoja na malaika wote na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

[163] *Coptic Synaxarium: 12 Baounah. Na Ethiopian Synaxarium, Senne 12 au Juni 19.*

**Septemba 30**

Huko Uswiswi na Italia, Wakatoliki wanawakumbuka, Wat. **Viktori**, **Urso** na **Antonino**, askari wa Jeshi la Theba, waliofiadini,[164] wakati wa utawala wa Kaizari Maksiminiani. Waliteswa vibaya sana, lakini mwanga kutoka mbinguni ukang'aa juu yao na kuwaangusha chini watesaji wao. Wakatupwa motoni bila kupata majeraha. Mwishoni wakakatwa vichwa. Wakazikwa nje ya mjini.
Huko Burundi, Wakatoliki wanawakumbuka **Aldo Marchiol**, **Otorino Maule**, mapadri wa Shirika la Wamisionari wa Ksaveri, na **Katina Gubert**, Mmisionari Mlei, waliouawa mwaka 1995.

Huko Misri, Wakoptiki wanamkumbuka Mt. **Simeoni II**, Patriarka, askofu wa 51 wa Aleksandria. Pia Mt. **Yohane**, askari na mfiadini.[165]
Huko Ethiopia, Wakristu wanawakumbuka Mt. Abba **Atanasi II**, Patriarka, askofu wa 28 wa Aleksandria na Mt. **Melitina** (*Malidama*), bikira na mfiadini.
Waorthodoksi Tewahedo wanawakumbuka Mt. **Athena**, bikira, **Marena**, **Pila**, **Abrahamu**, mtawa, **Rade'e**, **Sades**,**Thaddei**, **Epifanio** na **Armenio**.[166]
Waorthodoksi wanamkumbuka Mt. **Daudi wa Hermopolis**, Misri, karne la VI

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake! Amina.

## Padri Aldo Marchiol na wenzake, 1995

Padri Aldo na mwenzake walikuwa wanafanya kazi katika nchi ya Burundi kwa miaka mingi. Walikuwa wanajaribu kuwapatanisha makundi mbalimbali waliokuwa wanapigana wenyewe kwa wenyewe. Kwa muda mrefu walipokea vitisho kutoka serikali kwa sababu

[164] *Roman Martyrology, ed*. 1956.
[165] *Coptic Synaxarium: 3 Babah.*
[166] *The Ethiopian Rite Missal, Abba Emmanuel & Abba Brendan Cogavin, 2002, uk 171. Ethiopian Synaxarium: 20 Meskerem.*

walikuwa wanazungumza na wenyeji hadharani bila kuogopa. Ikagunduliwa kwamba Serikali ilijaribu kuwaondoa, na kama ikishindikana basi iliamua kuwaua. Tarehe 30 Septemba 1995 Wamisionari watatu waliuawa nyumbani mwao: Padri Aldo Marchiol (65), padri Otorino Maule (53) na mwanamke mlei Bi. Katina Gubert (73).

Bi Katina Gubert alikuwa anatazamia kwenda Italia mwezi wa Julai, lakini aliahirisha safari yake kwa kusema: “Nilifikiri kwenda Italia baada ya Padri Otorino kurudi. Lakini namna gani naweza kuondoka sasa hivi? Kuna kazi nyingi, hasa wakati huu hali ya siasa inapokuwa baya siku baada ya siku. Najisikia siwezi kuwasaliti namna hii. Bwana ananijalia nguvu kukabili nyakati hizo ngumu. Kwa hiyo nabaki. Labda mwezi mmoja au miwili? Tutaona.“

Wamisionari walitambua hatari waliyokabili wakibaki. Siku moja Padri Otorino Maule aliulizwa na mtoto: “Je, ni kweli kwamba mtaondoka?“ Padri Maule alimjibu: “Tuliamua kubaki pamoja nanyi“.

Wakati wa mazishi Mama mzazi wa Padri Maule aliisema: “Mmwambia Padri kiongozi mkuu awatume wamisionari wapya kushika nafasi ya mwanangu“.

Padri Aldo na wenzake, mtuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

**Oktoba 1**

Sisi Wakatoliki tunamkumbuka Mt. **Terezia wa Mtoto Yesu**, 1897. Ingawa hakukanyaga hata mara moja bara la Afrika, alitangazwa kuwa Msimamizi wa misioni zote. Miaka ya mwisho wa maisha hapa duniani alitoa mateso yake yote, madogo kwa makubwa, kwa ajili Mmisionari mmoja huko Zambia, ili aweze kupata nguvu na neema ya Mungu kueneza Injili.[167]
Huko Yassa, Wouri, Kameroun, Wakatoliki wanamkumbuka Mtumishi wa Mungu **Roberti Naoussi**, mlei.
Huko Kitgum, Uganda, Wakatoliki wanamkumbuka **Rafaeli di Bari,** Padri, aliyeuawa na Waasi wa Kony, mwaka 2000. Alikuwa na umri wa miaka 71.

Huko Misri, Wakoptiki wanawakumbuka **Mama** na **Papa**, wafiadini, Misri; Mt. **Baula** (Paul, Amba Baula) wa Tama.
Huko Ethiopia, Wakristo wanawakumbuka **Sipriano** na **Yustina** bikira, wafiadini.[168]

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake! Amina.

## Mtumishi wa Mungu Roberti Naoussi, 1970

Hatujui habari nyingi kuhusu maisha yake ya utotoni. Roberti alizaliwa mwaka 1953, katika kijiji kimoja, mbali na mji, nchi ya Kameroun, mtoto wa kumi na mmoja, wa familia ya kipagani. Kwa lugha ya kibamiléké Naoussi inamaanisha ‘Ndege aliyeanguka‘.
Roberti alipokuwa na umri wa miaka saba alisikia habari ya mtu aliyejua kuandika na kusoma. Roberto akajiandikisha kwake na kwa kulipa ada alifanya kazi. Haraka akajifunza kuandika, kusoma na kuhesabu. Mwaka ule alijiandikisha kufuata ukatekumeni katika

[167] *Martyrologium Romanum*, ed. 2005
[168] *The Ethiopian Rite Missal, Abba Emmanuel & Abba Brendan Cogavin, 2002, uk 172. Ethiopian Synaxarium: 21 Meskerem.*

misioni ya Bangouo, umbali wa kilometa 4 kutoka nyumbani mwake. Kwa ruhusa ya baba yake mpagani, alibatizwa alipokuwa na umri wa miaka 10. Akawa Mkristo peke yake katika familia yake. Ilikuwa siku ya furaha kutambua kwamba Mungu ni baba yake, na Maria mama yake, hata ikiwa siku ile hakupokea chakula wala zawadi! Shuleni alikuwa daima na furaha, na kazini alikuwa anawasaidia wengine. Alipenda sana kucheza mpira. Alitengeneza mpira wake mwenyewe kwa majani ya mti fulani.




Mwenye akili Roberti akafaulu mtihani wa darasa la 7 huko Bafussam mwaka 1965. Alitaka kuingia seminari, lakini kaka yake mkubwa akamzuia. Akatumwa kwenda katika Shule ya Sekondari ya Manancouba huko Nkongsamba. Mambo mengi yalimfurahisha hisia zake. Kwa malazi alikaa kwa mkufunzi wake na wakati wa likizo alifanya kazi kutafuta ada za shule. Mara nyingi aliona njaa, lakini hata hivyo alifaulu kununua vitabu, daftari na kalamu. Alijua maana ya kuwa maskini. Chakula kilipokosekana nyumbani mwa mkufunzi na akimwona mwana wake akilia, alikuwa anajishughulisha ili apate, walau kidogo, na kumpatia. Na yeye Roberti alikuwa anaenda shuleni akiwa na njaa. Ingawa mkufunzi wake hakuenda misa Jumapili, Roberti yeye alikuwa anaenda na kutumikia kama mtumishi wa misa. Huko Nkongsamba aliwakusanya watoto ili kuwafundisha kusali. Kila wakati hakukosa kuwasaidia wenzake. Pia aliwafurahisha wengine kwa kipaji chake cha mchekeshaji.

Mwaka 1968 hakuweza kuendelea kucheza mpira. Pole pole alipoteza uzito. Vidonda vidogo vilienea mwili wote, vilitoweka na kurudia. Ukoma ulimshika Roberto, aina ya ukoma ambao hauna dawa. Afya yake ikaporomoka. Hakupata usingizi. Ilimbidi kuacha shule, michezo, na kuhamisha mbali na kijiji chake. Tarehe 16 Mei 1969, akahamishwa Dibamba, katika kambi la wakoma, kms 30 Kaskazini mwa Douala. Mateso makali yakaanza na kuzidishiwa siku kwa siku, hadi siku ya kufariki kwake tarehe 1 Oktoba 1970.

Kwa njia ya mateso alianza safari ya utakatifu. Alipofika Dibamba kwa siku tatu akawa chumbani kimya bila kula, kunywa wala kulala. Alitafuta jibu ya maswali mengi. Kwa nini nipo hapa? Siku ya tatu, Padri alipofika kumwona akasema: "Najua kwa nini nilifika hapa. Baba yangu ni mpagani mwenye wake wengi. Nina kaka na dada 10 na mimi nilibatizwa peke yangu. Ni kwa ajili ya familia yangu, wamjue Yesu na kubatizwa. Kwa hiyo nataka kumtolea Mungu maisha yangu jinsi nilivyo.“ Sadaka kweli! Vidonda vinaenea popote mwilini mwake: miguuni, mikononi. Mara mbili kwa wiki wanabadilisha bendeji ya vidonda. Vidonda vinashika bendeji, lazima kuzitoa kwa mateso. Ni mateso matupu, analia kwa nguvu. Hawezi tena kutembea, yupo kitandani tu. Hawezi kujigeuza mwenyewe! Hawezi kulala, anasali rozari. "Nateswa, lakini namwomba Mungu kunizidishia mateso ili nifanane zaidi na Yesu msalabani.“ Uso wake ulivimba, anafanana na uso wa Yesu msalabani.

Sadaka yake kwa ajili ya familia yake kuongoka haitoshi. Ni ulimwengu wote anataka uokolewe na Yesu. Siku nyingine alipotambua kwamba msalabani Yesu hakulia, aliahidi kutolia tena. "Yesu hakulia msalabani. Inawapasa wale wanaoteswa kupasua njia kwa ajili ya wengine!“ Kila jioni alipewa vidonge ili alale. Havikuchukua mara moja, bali anasubiri masaa kadhaa kabla ya kuvichukua akisema: "Kuna daima sehemu ya kumtolea Mungu“.

Asubuhi ya tarehe 15 Agosti, alimwambia Bikira Maria: "Mama, leo ni sikukuu yako na sina ya kukuzawadia. Ukinipatia kitu, ningeweza kukukitolea. Najua mateso, nimekaliwa na mateso, mwili wangu wote ni ukoma, miguu, mikononi, lakini macho yangu yamebaki. Ukiyapenda ninakutolea.“ Jioni ile ile akawa kipofu.

Ugonjwa ukazidi. Roberti alijua kwamba mwisho ni karibu: "Njia yangu ya msalaba inakaribia kumalizika. Imebaki kituo cha mwisho kabla ya kwenda kumwona Baba yetu. Nina shauku kubwa kuishi pamoja naye.“ Kabla ya kufa kwake alisema: "Nataka kuwavutia wengi mbinguni kwa njia ya mateso yangu na kuwafungulia milango ... Watakapofika kutoka pande nne za ulimwengu, wale ambao wapo mbali na Mungu watajiuliza kwa nini milango ni wazi. Na wale ambao walifunga mioyo yao kwa Upendo, Mungu atawakaribisha na

kuwaweka moyoni mwake na Bwana atasema: ‘Ni Roberti mdogo aliyefanya kazi hiyo.‘“
Mtumishi wa Mungu Roberti Naoussi, utuombee tuweze kumtolea Mungu mateso yetu yote kwa wokovu wa ulimwengu.

## Mtu wa Mungu Rafaeli di Bari, kuuawa 2000

Padri Rafaeli di Bari, wa Shirika la Comboni, alipoendesha gari lake kwenda kigango cha Aciolibur kuadhimisha misa siku ya Jumapili, akauawa na waasi wa LRA (*Lord Resistance Army of Kony*), katika uvamuzi. Ilikuwa mnamo saa 4.30 risasi zilipolia, bazzoka ilipopigwa, guruneti ilipolipuka. Guruneti ilipiga gari karibu na dreva, ilipasuka mlango, kumwua Padri, kupasua kioo cha mbele na kusababisha injini kuzima. Padri Rafaeli alipiga kelele “Ahi! Ahi! Ahi!“ mara tatu na kufariki pale pale. Sista mmoja na wengine waliosafiri pamoja naye walitoroka. Mwanamke aliyepita karibuni akapigwa na risasi na kuuawa. Waasi walizunguka gari na kuwachukua vijana mateka walioshindwa kutoroka. Walitafuta kuiba kila kitu, wakapata tu saa ya Padri Rafaeli. Baada ya kutafutatafuta kiongozi aliamuru kuchoma moto gari. Wakawachukua vijana na kuwaachilia baadaye, isipokuwa mmojawapo, mwana wa mpishi wa misioni. Hakuonekana tena.
Habari zilipofika Parokia, Padri Antonio Simeoni alienda pamoja na watu wengine mahali gari lilipoungua. Hawakuweza kuzima moto. Mwili wa Padri Rafaeli ukateketezwa kabisa na moto. Padri Antonio akachukua alba yake na kuweka masalia ya mwili wake. Mazishi yaliendeshwa na Naibu wa Askofu, Padri Sebastiani, akisindikizwa na mapadri wengi. Askofu mwanglikana wa *Church of Uganda*, ambaye mke wake aliuawa na guruneti, alikuwepo.
Padri Rafaeli alikuwa mmisionari wa 22 wa Shirika la Comboni kutoa maisha yake kwa ajili ya haki, upendo na uaminifu katika wito wao. Alitaka kushiriki maisha ya watu wa Karamoja, hata katika hatari ya kuawa, kuliko kukaa Parokiani tu au kurudi kupumzika Italia katika uzee wake.
Rafaeli alizaliwa tarehe 12 Januari 1929 huko Bari. Aliingia novisiati tarehe 14 Septemba 1946. Ulikuwa wakati wa kupima wito wake na kurekebisha tabia yake. Mkuu wake wa novisiati alimwelewa vizuri

sana. Aliandika: “Alikuwa na makusudi mema, lakini ilimbidi kutawala ulimi wake. Alitamka, bila kuogopa, mawazo yake na kuyahakiki mambo ambayo hayakuenda kadiri ya mapenzi yake. Lakini alikuwa tayari daima kukosolewa.“ Padri Rafaeli alipadirishwa tarehe 26 Mei 1956 na Askofu Montini aliyechaguliwa baadaye kuwa Baba Mtakatifu Paulo VI.

Akabaki Italia kwa muda wa miaka mitatu kabla ya kwenda Uganda, katika jimbo la Gulu. Kwanza, huko Moroleum, akajifunza lugha chini ya uongozi wa Padri Alfredo Malandra, na wakati ule kuwahudumia wakristo wa Parokia  na kuwatunza wenye ukoma. Kwa maisha yake yote aliwaonyesha walioteswa upendo wa pekee. Mwaka 1962 akatumwa Kalongo kukaa pamoja na Mwenyeheri Giuseppe Ambrosoli[169] daktari na mwanzilishi wa hospitali kubwa. Padri Rafaeli alimsaidia, kwa kuenda Kampala kupeleka daktari na dawa zilizohitajika hospitalini.

Kutoka mwaka 1968 hadi 1975 Padri Rafaeli alikuwa Paroko wa Awac. Akafanya kazi pamoja na Padri Giovanni Scalabrini kutekeleza miradi mbambali kwa ajili ya wenyeji. Licha ya kuweka mashine ya kukoboa na kusaga kuwasaidia akina mama, wakajenga mashule na makanisa na kuweka makatekista kuwahudumia wakristo. Walitafuta fedha kwa kuwasaidia vijana kujifunza katika Vyuo vikuu nje. Wakati wa mlipuko wa kipindupindu alijaribu kusaidia kwa nguvu zake zote kutafuta msaada kwa ajili ya walioathirika. Jambo hilo lilisababisha kupata kidonda chenye kutoa damu. Akalazimishwa kurudi Ulaya kutibiwa. Kwa neema ya Mungu madaktari walifaulu kumtibu kwa dawa bila kumpasua. Alipokabiliwa na njaa iliyoletwa na vita, aliwakusanya vijana na kuwahimiza kupanda mpunga na alizeti. “Nchi ina rutuba, pandeni na itatoa chakula kwa wote“. Ujumbe ulisikika na vijana wengine walimfuata. Aliwagawia mamia ya majembe. Kwa baraka ya Mungu mvua ilinyesha na watu waliweza kuvuna mahindi, kalanga, viazi vitamu, n.k.

Mwaka 1986, Rais Museveni alijaribu kuleta amani nchini kwa kuwasamehe wote waliorudisha silaha zao. Wamisionari waliwashauri watu kuifanya hivyo na kurudi kulima mashamba yao. Padri Rafaeli

[169] Rejea tarehe 27 Machi

alikuwa msitari wa kwanza kuwaonyesha kwamba msamaha huo haukuwa ujanja wa wenye siasa bali njia ya kweli kuleta amani. Lakini Waacholi hawakukubali, walibaki na silaha zao. Na mwaka ule ule 1986 walianzisha vita upya. Mwaka 1989 Padri Rafaeli alitumwa kukaa katika Parokia ya Pajule kushika kwa muda nafasi ya Padri mmoja aliyekwenda Ulaya kwa mapumziko. Wakati ule kikundi cha waasi wakazunguka misioni na kuanza kuivamia. Mapadri walipata nafasi kukimbia na kujificha. Nyumba ilipovamiwa, waasi wakaondoka.

Kwa sababu ya vita wamisionari walilazimishwa mara kwa mara kuacha misioni kadhaa. Amani ilipotawala wamisionari walirudi katika misioni zilizolindwa na Wakristo, Padri Rafaeli alienda Kalongo ili kuifungua tena, baadaye alienda kukaa Namokora kwa miaka miwili, na mwishoni parokia ya Opit. Alipokuwa Opit, waasi walivamia misioni. Tarehe 1 Novemba 1997, risasi zilizosambazwa huko na huko, zikapiga picha ya Mtakatifu Pio, lakini mapadri na masista hawakujeruhiwa. Wote walimshukuru Padri Pio kwa maombezi yake. Padri Rafaeli aliporudi Italia alipeleka picha ya Padri Pio iliyotobolewa kwa risasi huko San Giovanni Rotondo, kama ishara ya shukrani kwa ulinzi wake. Tarehe 29 Septemba 2000, huko Pajule, waasi walivamia pia misioni, lakini Padri Rafaeli hakujeruhiwa. Miaka ya nyuma siku moja alisukumwa na waasi kukaa mbele ya ukuta ili kupigwa risasi. Lakini akaepa kifo kwa kuzungumza na mmojawapo. Ingawa alionywa kukaa katika usalama, Padri Rafaeli hakutaka kuwaacha wakristo wake. Akaendelea kuwahudumia hadi siku ile alipouawa. Alikuwa na umri wa miaka 71.

Kwa nini Padri Rafaeli aliuawa jinsi hiyo? Yeye mwenyewe anatuambia sababu. Siku chache kabla ya kufariki alimwambia mwenzake kwa simu: "Kwa miaka mingi katika Afrika, kazi niliyopokea kutoka kwa Bwana, ni kuwa sauti ya wasio na sauti, wale wanaoteswa na waasi, kuambia ulimwengu wote ukatili wanaotenda karibu kila siku, hasa kwa watoto na wanawake ambao wanatekwa, kuharibiwa, kufanywa kuwa askari, kuwa wauaji, pia kwa ajili ya biashara ya viungo vya binadamu na kutafuta kuwatumia watoto kwa mapenzi. Siwezi kukaa kimya mbele ya maovu haya."

Padri Rafaeli, utuombee ili tuwe hodari kutangaza ukweli na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

**Oktoba 2**

Sisi Wakatoliki tunamkumbuka Mwenyeheri **Yohane Beyzym**, padri Mmisionari huko Malagasi.[170]
Huko Mwanza, Tanzania, Wakatoliki wanamkumbu **Renati Butibubage**, Askofu, aliyefariki mwaka 1988.
Huko Afrika ya Kusini, Wakatoliki wanamkumbuka **Gerardo Fitsimons**, Mmisionari, aliyeuawa mwaka 2004.

Huko Ethiopia, Wakristu wanamkumbuka Mt. **Julio wa 'Akfehas**, mfiadini. Waorthodoksi Tewahedo wanawakumbuka Wat. **Theodori**, **Ionias** na **wenzao elfu moja na mia tano** (1500), wote wafiadini. Wanamkumbuka pia **Balan**.[171]

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake! Amina.

## Mwenyeheri Yohane Beyzym, Padri, 1912

Yohane amezaliwa tarehe 15 mei 1850 huko mkoa wa Volhynie, zamani eneo la nchi Poland na siku hizi nchi ya Ukraine. Baada ya masomo ya Sekondari akajiunga na shirika la Majesuiti. Akaanza novisiati huko Stara Wiez, akaendelea masomo ya Falsafa na Teolojia huko Krakov na kule tarehe 26  Julai, 1881 akapadirishwa. Kwa miaka kumi na moja alifanya kazi katika shule ya Tamopol na seminari huko Chirow. Lakini tangu novisiati alikuwa na hamu ya kuwahudumia wenye ukoma. Ombi lake lililotumwa kwa nyumba ndogo ya wenye ukoma, Mangalore, India, halikupokelewa. Kwa hiyo aliomba kwenda Malagasi. Alipokuwa bado Poland alianza kukusanya vifaa kwa ajili ya wakoma, na mwaka 1898 alipanda merikebu *Oxus* huko Marseilles, Ufaransa.

---

[170] *Martyrologium Romanum 2001*

[171] *The Ethiopian Rite Missal, Abba Emmanuel & Abba Brendan Cogavin, 2002, uk 172. Ethiopian Synaxarium: 22 Meskerem*. Wakoptiki wanamkumbuka tarehe 19 Septemba.

Alipokuwa na umri wa miaka 48, alianza kuwatunza wakoma, huko Ambahivoraka, Malagasi. Hospitali ilikuwa na nyumba kubwa nne ambamo wakoma 150 waliishi katika umaskini. Hakuwa na daktari wala nesi, wala dawa. Kwa chakula kila wiki mkoma mmoja alipokea kilo moja ya mchele. Padri Beyzym akaanza kazi mara moja, akijitahidi kuwaokoa wagonjwa hawa na kifo kwa sababu ya kutolishwa vya kutosha na hasa kuwaponya maumivu yao ya ki-roho. Alikuwa anasema: “Wote wanaishi kwa pamoja, wakatoliki na wapagani, wanaume, wanawake, watoto, wote wakiishi pamoja kama wanyama.“

Kwa sababu ya mazingira hayo, Padri Beyzym aliandika mradi wa kujenga hospitali mpya. Alihitaji kiasi cha 30.000 Francs. Gharama zilikuwa kubwa na misioni ilikuwa maskini. Basi akaanza kutuma barua kwa wafadhili huko Poland, na mwisho wa mwaka 1900 alifaulu kukusanya kiasi cha 25,000 Francs.

Kwa sababu hospitali kubwa yenye vitanda 700 ilikuwepo karibu na Antananarivo, ilimbidi Padri Beyzym kutafuta mahali pengine kujenga hospitali yake. Akapata eneo huko Marana. Kazi ikaanza mwaka 1903 na ikamalizika mwaka 1911. Wakoma 140 waliweza kupokelewa na kuishi kwa raha zaidi wakiwa na maji, bafu, udobi, huduma ya kutengeneza nguo, pamoja na watumishi waliowahudumia, manesi, wapishi, n.k. Masista wa shirika wa Mt. Yosefu wa Cluny wakafika Marana kumsaidia Padri Beyzym. Kila mgonjwa alifanya kazi kadiri ya uwezo wake. Jinsi walivyoishi ilifanana zaidi ya maisha ya konventi kuliko hospitali, na Padri Beyzym alitunza roho za wagonjwa kama alivyotunza miili yao. Maisha hayakuwa rahisi. Mara kwa mara Padri Beyzym alijisikia kinyaa akihudumia wakoma na mara kadhaa alizimia na kuanguka. Aliandika kwa mkubwa wa Majesuiti huko Ufaransa: “Ni muhimu kila wakati kuwa na uhusiano wa karibu na Mungu. Inatubidii kuzoea harufu mbaya. Hatupumui harufu ya maua bali harufu ya mwili unaooza.“

Licha ya kazi yake hospitalini aliandika kamusi ya Kipolish na Kimalagasi na makala kwa magazeti ‘*Catholic Missions*‘ huko Poland.

Padri Beyzym akaambukizwa na ugonjwa kutoka mkoma mmoja. Akafariki tarehe 2 Oktoba 1912. Habari za kifo chake kimeenea kwa kazi, kwa sababu magazeti mengi huko Ufaransa, Ireland, Ujermani yakaeleza kazi na sifa yake. Katika gazeti la ‘*Gaulois*‘ mwandishi

aliandika: “Padri alipofika Ambahivoraka kila wiki watu watano walikufa, lakini kwa sababu ya jitihada zake sasa watu watano tu wanakufa kwa mwaka.“ Alitangazwa Mwenyeheri tarehe 22 mwezi wa Agosti, mwaka 2002 na Baba Mtakatifu Yohane Paulo II.

Mwenyeheri Padri Beyzym, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

**Oktoba 3**

Sisi Wakatoliki tunawakumbuka Wat. **Fausto, na wenzake**, wafiadini, huko Aleksandria, Misri, wakati wa utawala wa makaizari Desio na Valeriani[172], pamoja na **Dionisi**, askofu wa Aleksandria. Wengine wakiwahudumia mashahidi hao pia wakapata thawabu ya ushahidi.
Pia tunamkumbuka Mt. **Maksimiano**, askofu wa Bagaia, Aljeria. Tena na tena aliteswa sana na wafuasi wa Donati, hatimaye alitupwa chini, kichwa kwanza, toka mnara mrefu na kufikiriwa kuwa amekufa. Watembeaji walimkuta yupo bado mzima. Wakajitahidi kumhudumia hadi akapona. Akaendelea kuitetea dini ya Katoliki hadi kifo chake.
Huko Afrika wa Kaskazini, kumbukumbu ya Wat. **Viktori**, **Urbano**, **Sapargo**. Pia Wat. **Feliksi, Amponi** na **Kasto,** wafiadini.[173]

Waorthodoksi wanawakumbuka Mt. **Dionisi**, askofu wa Aleksandria na **wafuasi wake**, mwaka 258.
Huko Ethiopia, Wakristu wanamkumbuka Abba **Salama**, taa ya ulimwengu. Waorthodoksi Tewahedo, wanawakumbuka **Ensina**, **Belina**,[174]
Waorthodoksi wa Magharibi wanamkumbuka Mt. **Yohane Chozibite**.[175]

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake! Amina.

## Mt. Dionisi, Askofu wa Aleksandria, 265.

Dionisi aliitwa na Askofu Basil 'Dionisi Mkuu' na Askofu Atanasi anamwita Mwalimu wa Kanisa Katoliki. Dionisi alizaliwa na wazazi wapagani mwishoni mwa karne la II. Wazazi wake walikuwa tajiri na wa ukoo bora. Kwa kuzaliwa kwake alikuwa Sabaite, familia kutokea

---

[172] *Martyrologium Romanum*, ed. 2005. Wanatajwa pamoja na Fausto: Kayusi, Petro, Paulo, Eusebio, Cheremoni (Shenuf), Lusio na wenzao. Kadiri ya *Acta Sanctorum* zamani sikukuu ya Mt. Dionisi ilikumbukwa tarehe 17 Novemba


[173] *Acta Sanctorum*

[174] *The Ethiopian Rite Missal, Abba Emmanuel & Abba Brendan Cogavin, 2002, uk 173. Ethiopian Synaxarium: 23 Meskerem*.

[175] Rejea *Orthodox Saints of the day*. Maisha yake yameandikwa tarehe 28 Oktoba.

Arabia. Dionisi, mpagani bado alijifunza katika chuo kikuu cha Aleksandria na akafaulu sana katika ufasaha wa kusema. Alitumia muda wake mrefu kusoma vitabu, hasa kujifunza mapokeo ya wazushi. Aliposoma barua za Mtume Paulo, moyo wake ukafunguka kwa neema ya Mungu. Akaongoka kwa sababu ya maono na sauti aliyosikia. Akakanyaga kwa miguu yake fahari zote za ulimwengu na kumgeukia Mungu kikamilifu kwa moyo wake wote. Aliambiwa kujifunza kwa undani zaidi mapokeo ya wazushi ili baadaye aweze kuyapinga.

Akabatizwa akiwa mtu mzima, akajiunga na Shule ya Katekisimu huko Aleksandria, walimu wake wakiwa Origeni na Heraklasi. Akapadirishwa mwaka 221. Yeye mwenyewe baadaye akashika Uongozi wa Shule hiyo wakati Heraklasi alipochaguliwa kuwa Askofu Mkuu wa Aleksandria, mwaka 231. Na mwaka 248, akachaguliwa kuwa Askofu wa 14 wa Aleksandria. Akawa askofu wa kwanza wa Aleksandria kuitwa Askofu Mkuu.




Dionisi alikuwa mtawala kuliko mwanateolojia. Mwaka 249 dhiki ikatokea mjini Aleksandria, iliyosababishwa na ghasia ya watu. Wakristo wengi waliteswa na kuuawa, lakini yeye alifaulu kuendelea kuishi wakati wa dhiki na vita vya wenyewe kwa wenyewe iliyofuata.

Mwaka 250 Desio alipomwua Filipi na kutawala mahali pake, akaanzisha dhiki kubwa dhidi ya Wakristo. Wengi, wa kila rika na umri waliteseka vibaya sana. Wengine walikimbilia milimani na misituni, wengine walikufa kwa njaa, baridi, wanyama wakali au wajambazi. Wengine walitekwa nyara na kuwa watumwa. Maaskofu waliumizwa moyoni wakiona jinsi Wakristo wengine walivyokana Kristo chini ya mateso yao, lakini wakitiwa moyo wakiona wengine walivyomshuhudia Kristo. Ilikuwa ajabu kuona adui wakiongoka wakishuhudia jinsi Wakristo walivyomwamini Yesu Kristo. Wakajitangaza kuwa Wakristo na pale pale walikufa mashahidi.

Dionisi katika barua zake anawasimulia maaskofu wenzake kwamba Wakristo wengi waliasi kwa hofu. Wengine wakasimama imara katika

imani yao na wakauawa baada ya mateso mengi, na wengine walikimbia jangwani na kufa kwa njaa, kiu, mfichuo au kushambuliwa na wanyama wakali au wajambazi. Mt. Dionisi alikuwa amewatayarisha askari wa Kristo kuikabili dhiki hiyo. Ingawa Gavana Sabino aliwatuma askari kumkamata, wakashindwa. Dionisi akajificha nyumbani mwake kwa siku nne, na baadaye kwa kufuata msukumo wa Roho Mtakatifu, kama anavyosema mwenyewe, akaenda kujificha mahali pengine. Lakini njiani akakamatwa pamoja na Wakristo wengine. Wakapelekwa huko Taposiris, mji mdogo mkoani mwa Mareotis. Habari hiyo ilipoenea jeshi kubwa la Wakulima likashika silaha na kwenda kumwokoa Askofu wao. Askari wakakimbia wakiwaacha wafungwa nyuma yao. Wakristo wakamchukua askofu na kumpeleka jangwani, katika mkoa wa Marmarica, Libya, akihudumiwa na Petro. Akabaki pale mpaka mwisho wa dhiki, katikati ya mwaka 251.
Askofu Dionisi akaunga mkono na Baba Mtakatifu Kornelio akimpinga mafundisho ya Novatiani aliyekataa kuwapokea katika Kanisa Wakristo walioasi katika dhiki. Kinyume cha mafundisho yake, Dionisi aliwahimiza mapadri wake kutokataa kuwapa komunio wale walioomba, saa ya kufa kwao, hata wale walioasi dini wakati wa dhiki.
Mwaka 252 mlipuko wa tauni ukavamia mji wa Aleksandria. Askofu Dionisi pamoja na mapadri na mashemasi wake wakajitoa wakihudumia wagonjwa na wale waliokufa. Kwa sababu ya upendo wao wengi kati yao walifariki. Dionisi aliandika katika barua yake ya ki-uchungaji: “Ndugu zetu wapendwa waliacha maisha kwa njia hiyo, mapadri, mashemasi, walei; na kifo cha namna hiyo, kilichosababishwa na imani imara na upendo mkubwa, ni kifo kama kifo cha ushahidi.“
Mwaka 257, chini ya utawala wa Kaizari Valeriani, dhiki ilianzwa upya. Emiliani, Gavana wa Misri akawakamata askofu Dionisi, padre Maksimo na mashemasi Fausto, Eusebio na Cheremoni, na mlei Marseli, Mrumi. Wakapelekwa mbele yake na kulazimishwa kuwatolea miungu ya uongo sadaka, walinzi wa dola la Warumi. Dionisi akamjibu Gavana: “Watu hawaabudu miungu sawa. Sisi tunamwabudu Mungu mmoja, mwumba wa viumbe vyote, yeye aliyewakabidhi makaizari Valeriani na Galieni dola la Warumi. Tunamtolea dua bila kukoma kwa ajili ya amani na ustawi wa utawala wao.“ Gavana akawahamisha huko Kephro, Libya, na akawakataza Wakristo

kukusanyika pamoja na kuzitembelea kaburi za mashahidi. Huko Libya Dionisi akawaongoa wenyeji wa nchi ile, kwa hiyo Gavana akawahamisha Mareotis, panapoitwa sasa Ziwa la Aleksandria. Kwa sababu ya ukaribu wa mji Aleksandria Dionisi aliweza kupokea na kumtumia barua na kuongoza jimbo lake. Uhamisho wake ulidumu miaka miwili. Mwaka 260 Kaizari Valeriani alipotekwa nyara na Wawajemi, Galieni akawaruhusu Wakristo kuabudu. Askofu Dionisi akarudi Aleksandria.

Mt. Dionisi aliandika vitabu na barua nyingi, lakini maandiko yake yote yamepotea. Mwaka 264 alialikwa kuhudhuria sinodi huko Antiokia kuzungumza msimamo wa askofu Paulo wa Samosata aliyekana umungu wa Yesu Kristo. Kwa sababu ya umri wake na udhaifu wake hakuweza kwenda, lakini aliandika barua nyingi kwa Kanisa la Antiokia ili kukanusha uzushi wake. Karibu mwisho wa mwaka 265 akafariki. Kumbukumbu zake, asema Mt. Epifanio, zinaendelea huko Aleksandria, kwa sababu kanisa moja lilijengwa kwa heshima yake, lakini zaidi kwa sababu ya fadhila zake na maandiko yake bora.[176]

Mt. Dionisi, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

[176] Rejea *Butler's lives of the Saints*.

**Oktoba 4**

Katika Kanisa Katoliki tunamkumbuka Mt. **Fransisko wa Asizi**, aliyemhubiria Sultani wa Misri kwamba wokovu unapatikana tu katika imani kwa Yesu Kristo.[177]

Huko Afrika ya Kaskazini, Wakatoliki wa Afrika wanawakumbuka Wat. **Marko** na **Marsiano**, ndugu wa tumbo moja na wafiadini. Pamoja nao idadi kubwa ya **wanaume kwa wanawake**, waliofia dini, baada ya kuteswa vibaya kwa ajili ya Jina la Yesu Kristo. Wengine walitupwa motoni, wengine kutupwa baharini, wengine kukatwa vichwa, wengine kunyimwa chakula hadi kifo, wengine kunyongwa na wengine kuning'inizwa kwa mguu juu na kichwa chini.[178]

Huko Misri, Wakatoliki wanamkumbuka Mt. **Amoni Mkuu** (*Ammon*), mtawa.

Huko Genoa, Italia, kumbukumbu ya Mt. **Amphelio**, mhunzi mjini Aleksandria, na mkaa pweke Genoa, karne la V.

Huko Tunisia, kumbukumbu ya Wat. **Marusio**, **Restito**, **Julio**, (na **Maksimus**), wafiadini, Tunisia.

Huko Treves, Ujerumani, Wakatoliki wanamkumbuka Mt. **Thirsio, Bonifasio**, na **wenzao**, Askari wa Jeshi la Theba, waliouawa Treves.[179]

Katika Aljeria, Wakatoliki wanamkumbuka **Yohane Mbatizaji Barbier**, Padri wa Shirika la Wamisionari wa Afrika (*White Fathers*) aliyetoweka huko Djemmaa-Saharidj, Aljeria, wakati wa kazi ya ki-tume na hakuonekana tena, 1956.

Huko Bamenda, Kameroun, wakatoliki wanamkumbuka **Gerardo Anjiangwe**, Mseminari, aliyeuawa na askari mbele ya kanisa la Parokia ya Mt. Teresa wa Bamessing, mwaka 2018.

Wakoptiki wanawakumbuka Mt. **Paulo El-Tamouhi**.[180]; Amba **Baula** wa Tuwa, mwungama dini, Mt. **Barakial**, mfuasi wake, na **Psoi**, rafiki

[177] *Martyrologium Romanum*, ed. 2001

[178] *Roman Martyrology*, ed. 1956.


[179] *Actas Sanctorum*. Majina Marusio, Restito, Julio yanatajwa katika martirolojia ya Mt. Hieronimo.

[180] *Coptic Synaxarium: 7 Babah*.

wake; Wat. **Eusebio**, **Kayusi**, **Fausto**, **Cheremoni** wa Aleksandria, wote wafiadini; Mt. **Pafnusi** na **wenzake 546** wafiadini.
Waorthodoksi wanamkumbuka Mt. **Amon wa Misri**, Karne la IV.
Huko Ethiopia, Wakristu wanamkumbuka Abba **Gregori**, mtawa. Waorthodoksi Tewahedo, wanawakumbuka pia **Betrewa** na **Latayn**, wafiadini; Kuaga kwake **Gabrieli**, askofu mkuu, **Theodori**, **Netrolomes**, na vita ya Mt. **Eusanio**, (*Ausanius*), **Nestio**, **Ziano**, **Yusto**, ndugu yake, **Elsarey**, **Frato**.[181]

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake! Amina

## Mt. Amoni mkuu, Mtawa, Misri, 357.




Amoni alizaliwa Misri katika familia tajiri na ukoo bora. Alipofika umri wa miaka 22 alilazimishwa kuoa. Lakini siku ile ya harusi yake, alimsomea mke wake maneno ya Mtume Paulo kuhusu ubora wa ubikira. Akamshauri kuishi pamoja naye kama kaka na dada katika usafi kamili wa moyo. Wakaishi miaka 18 katika nyumba moja wakitumia muda wao kusali na kuwatendea watu mema.
Amoni alijitahidi kufuata majikanio ya kila aina. Mchana akisali na kufanya kazi kwa mikono yake. Kazi yake ilikuwa kulima bustani yake alipopanda miti Balsamum, miti yenye harufu nzuri. Chakula chake kilikuwa majani na matunda. Usiku alitumia muda mrefu kusali.
Baada ya kifo cha wazazi wake na rafiki zake ambao walimzuia kuishi maisha ya pweke, alienda kukaa katika mlima wa Nitria. Mke, aliyekubali kutengana naye, alikusanya katika nyumba yake mabikira wengi waliojitoa kwa Mungu na kuishi chini ya uongozi wake kama wanakoriti wa jangwani.

181 *The Ethiopian Rite Missal, Abba Emmanuel & Abba Brendan Cogavin, 2002, uk 173. Ethiopian Synaxarium: 24 Meskerem.*

Amoni aliishi katika mlima Nitria miaka ishirini na miwili. Watawa wengi walimfuata na kuishi, kila mmoja katika kijumba chake. Mt. Antoni alipomtembelea alimshauri kuanzisha monasteri na kuwakusanya wafuasi wake chini ya uongozi wake. Akaonyesha mahali pa kujenga monasteri kwa kuchomeka msalaba mmoja. Kasiani anatuambia kwamba monasteri hiyo ilikuwa mbali wa maili tano na mji Nitria. Mwisho wa karne la IV watawa elfu tano waliishi katika monasteri hamsini.

Mtakatifu Amoni alifanya majikanio ya ajabu bila kuacha kusali daima. Mwanzoni mwa kukaa Nitria alikula mara moja kwa siku, wakati wa jioni. Lakini kufunga kwake kilizidi mwaka kwa mwaka. Mara kwa mara alifunga siku nne bila chakula. Alitenda miujiza mingi. Katika maisha ya Mt. Antoni, Askofu Atanasi anatusimulia yafuatayo: "Mara moja alipotaka kuvuka mto ulioitwa Lycus (kipindi cha mafuriko), alimwomba mwenzie Theodori kuwa mbali naye, ili wasionane wakiwa uchi wakati wanavuka huo mto kwa kuogelea. Halafu wakati Theodori akiwa amekwisha kuondoka Amoni bado aliona aibu kujiona uchi. Wakati alipokuwa bado anafikiria fikiria akiwa amejaa soni, ghafla alikuwa amevushwa upande wa pili. Theodori, yeye mwenyewe akiwa mtu mwema, alimkaribia Amoni, na alipoona kwamba amevuka bila hata tone la maji kudondoka kutoka mwili wake alimwuliza akitaka kujua jinsi alivyovuka. Na alipoona kwamba Amoni hakuwa tayari kumwambia, alimshika miguu na akamwambia kwamba hatamwacha aende hadi atamwambia jinsi alivyopata kuvuka mkavu bila kulowa maji. Kwa hiyo Amoni alipoona uking'ang'anizi wa Theodori, na hasa kutokana na yale aliyoyatamka, na baada ya kumwonya asimwambie mtu yeyote kabla ya kufa kwake, alimwambia kwamba alikuwa amebebwa na kuvushwa upande wa pili. Na kwamba hakuwa amegusa maji, na hilo halikuwezekana kwa mwanadamu mwenyewe, bali kwa Bwana peke yake na wale ambao anawaruhusu, kama alivyofanya kwa mtume Petro.[182] Theodori kwa hiyo alisema haya baada ya kifo cha Amoni."

Mt. Antoni na Mt. Amoni walizoea kutembeleana ili kujijenga ki-roho. Amoni alitangulia kufariki mwaka 357. Siku moja Mt. Antoni alikuwa

---

[182] Mt 14 :29.

ameketi huko mlimani kwake, na akiangalia juu alimwona mtu akipaa juu, na kulikuwa na furaha sana miongoni mwa wale waliompokea. Hivyo akishangaa na kuchukulia kuwa kundi hilo lilikuwa la watakatifu, alisali kuomba tafsiri ya maono hayo. Mara moja sauti ilimjia: "Hii ni roho ya Amoni, mtawa wa Nitria." Wakati huo Amoni alikuwa amestahimili mateso ya nidhamu ya maisha ya ki-roho hadi kufikia umri wake wa uzeeni; na umbali kutoka Nitria hadi mlimani alikoishi Antoni ulikuwa safari ya siku kumi na tatu.

Mt. Amoni, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

## Mt. Fransisko wa Assisi

Hatuhitaji kuandika maisha ya Fransisko kwa sababu watu wote wanamfahamu na kumpenda. Kwa kifupi: "Fransisko alizaliwa Asizi, Italia, mwaka 1182. Mama yake alimfundisha mapema kumpenda Mungu na kuchukia dhambi. Baba yake alikuwa mchuuzi tajiri katika Italia na nchi nyingine. Fransisko alipozaliwa, baba yake alikuwa katika nchi ya Ufaransa akifanya biashara, na hivi mtoto wake alipangwa jina la Fransisko, maana yake 'Mfaransa mdogo'. Katika ujana wake, Fransisko alipenda kuvaa kimalidadi na kufanya karamu pamoja na wenzake. Lakini aliwasaidia pia maskini wote waliomjia kuomba sadaka. Baba yake alidhani kuwa Fransisko atapoteza mali zake zote kwa kuwagawia maskini, hivyo alimpeleka kwa askofu wa Asizi na kumshurutisha aubatilishe urithi wake. Hapo Fransisko akayavua mavazi yake, akamwachia baba yake vitu vyote alivyokuwa navyo akisema: 'mpaka saa nimekuita baba, tangu sasa nitaweza kusema kwa dhati: Baba yetu uliye mbinguni'. Akaenda kukaa karibu na kanisa iliyoitwa Porsiunkula ...

Vijana wanaume wengi walifuatana naye, na mwaka 1209 akawapa kanuni za kuwaongoza katika utakatifu. Baba Mtakatifu alikubali kanuni hizo, na shirila ndugu Wafransisko lilienea nchi zote. Lengo lilikuwa kuhubiri kitubio na kuhubiri Injili kwa watu wote."[183]

Kwa muda Fransisko alikuwa na hamu ya kuwenda Moroko kumwongoa Mfalme Moramolin, aliyeitwa Mohammadi, mtu rangi jani. Akaanza safari kwa njia ya Hispania. Hakufaulu. Mara ya pili

---

[183] Rejea *Maisha ya Watakatifu*, T.M.P. 1996, uk.345-346

aliamua kwenda Afrika, lakini Roho wa Mungu, kama alivyomzuia Paulo kwenda kuhubiri Injili Bithinia, akamzuia pia kwenda Moroko. Akaugua huko Hispania. Na alipokuwa mgonjwa akapokea kutoka Mbinguni amri ya kurudi Italia.

Kwa mara nyingine aliamua kwenda Siria, akijua kwamba, kama hapati nafasi ya kumwongoa Sultani wa Misri, walau alitumaini kupata taji la ushahidi. Akachagua watawa kumi na mmoja kwenda pamoja naye. Akavuka bahari kwa usalama na kufika bandari ya Akra, nchi ya Palestina, na kutoka kule kufika bandari ya Damiette, Misri, ambayo ilizunguka na jeshi la Wakristo. Hao, kwa sababu hawakusikia shauri za ki-nabii zilizotolewa, wakashindwa vibaya. Kutoka kule akaenda katika kambi la Waislamu. Njiani akapigwa na kudhulumiwa na Waislamu, lakini akafaulu kukaa mbele ya Sultani. Fransisko akaongea naye kwa uhuru na nguvu ya ajabu, hata akamchallenge kupita katika moto ili kuuthibitisha ukweli wa imani katoliki. Sultani, kwa hofu ya ki-binadamu, hakukubali kutanasari. Hamkutendea Fransisko vibaya, bali kinyume, akamheshimu sana. Akamruhusu kuhubiri katika nchi yake na kuwabatiza wale watakaotanasari. Fransisko na watawa wake wakafanya hivyo kwa mafanikio makubwa hata kuwapokea waliokuwa Waislamu katika Shirika lao.

Shetani hakuweza kukaa kimya. Akamshauri mwanamke Mwislamu kumtega Fransisko kwa njia ya uasherati. Fransisko akakubali, sharti atengeneze yeye mwenyewe kochi ya uzinifu. Akatayarisha moto wa makaa na kujilaza juu yake. Akamwambia mwanamke: “Ndiyo dawa ya tamaa“. Mwili wa Fransisko hakuugua. Mwanamke alipoona hayo Mungu akamfungua macho yake. Akatambua kosa lake na madhambi yake ya zamani. Akaongoka na kukiri kwamba ataishi katika usafi wa moyo. Kwa njia yake Mungu akawaongoa Waislamu wengi kutanasari.[184]

Mt. Fransisko wa Asizi, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

## Padri Barbier Jean-Baptiste, aliyeuawa, 1956

---

[184] *Le Palmier Seraphique*, X, uk 58-59, 72-73.

Padri J.B. Barbier alipadirishwa tarehe 29 Juni 1924. Akatumwa huko St. Laurent d'Olt, iliyoitwa baadaye Shule ya ki-tume ya Altkirch. Mwaka 1927 akachaguliwa kwenda Aljeria katika mkoa wa Kabylie. Akakaa katika misioni mbalimbali, Bou-Noh na Djemaa-Saharidj, misioni yake ya mwisho.

Mmisionari huyu ni mtu wa pekee, alikuwa daima kutembea barabarani, akibeba dawa katika mfuko wake na chakula katika juba lake. Hakuchoka kutembea. Alitembea kwa miguu, masaa sita hadi saba kila siku, akitafuta vijiji vipya na roho wapya. Hata ikiwa hakuweza kuingia katika nyumba moja, aliona kwamba hakupoteza muda wake kwa sababu: "Watu wameniona, lazima wajiulize mimi ni nani? Nafanya kazi gani?" Asubuhi, ikuwa mvua ilinyesha, alisubiri dalili moja kwamba mvua itakwisha, ili aanze kutembea. Pengine aliondoka wakati theluji iliponyesha. Pengine alirudi akilowa na kuchafuka kwa matope. Kesho yake alisafisha viatu vya na kuondoka tena.

Ni katika kazi hiyo Mungu alimwita kukaa naye milele. Kwa sababu ya hali ya siasa katika nchi ya Aljeria, Padri alijua kwamba hatari zilikuwepo. Siku moja alimwambia mmisionari mwenzake kwamba aliogopa. Lakini kwa sababu alijisikia uchovu wa uzee alizidisha maneno: "Ikiwa sitembei siku hizi, sitaweza kuanza kutembea upya baadaye". Kwa hiyo Mkuu wake alimruhusu kuendelea, akimwambia kuwa mwangalifu katika maneno yake na kutokaa katika kijiji kimoja kama atatambua uhasama wowote.

Tarehe 4 mwezi wa Oktoba, 1956, Padri Barbier akamwomba ruhusa kwa Mkuu wake kwenda katika kijiji cha 'Mekla mzee'. Mkuu akamruhusu akimwomba arudi saa 12.30 jioni misioni. Padri Barbier akamwahidi kwamba atafanya hivyo. Lakini hakurudi na hakuonekana tena. Siku baada ya siku, uhakika kwamba Padri Barbier aliuawa ukapokelewa mioyoni mwa watu. Mwili wake haukupatikana hadi leo.

Mtu wa Mungu Padri Barbier, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

**Oktoba 5**

Huko St-Cyprien les Attafs, Aljeria, Wakatoliki wanawakumbuka **Paulo Py** na **Bernardo Chassine,** mapadri wa Shirika la Wamisionari wa Afrika (*White Fathers*), waliotekwa nyara na kuuawa na waasi, 1962.
Huko Kikwit, Jamhuri ya ki-demokrasia ya Kongo, Wakatoliki wanamkumbuka **Dositheo Ntunga Kisila**, Bruda wa Shirika la Moyo Usio na Doa wa Bikira Maria, aliyeuawa mwaka 1999.
Huko Borama, Somalia, Wakatoliki wanamkumbuka Mtu wa Mungu **Analena Tonelli**, aliyeuawa mwaka 2003.

Huko Misri, Wakoptiki wanawakumbuka Mt. **Matra**, mzee, mfiadini; Wat. **Abahor**, **Tosia** na **watoto wake Hori na Agatho,** wafiadini; na Abba **Agato** mwanakoriti.[185] Pia kumbukumbu ya **Cheremoni** wa Aleksandria, Misri; **Susana** (Dhusina) wa Thmuis, Misri; **Dionisi** askofu wa Aleksandria, mfiadini, 265, B.K.
Huko Ethiopia, Wakristu wanawakumbuka **Barbara** na **Juliana**; Waorthodoksi Tewahedo, wanawakumbuka **Roka** (Foka), **Yohane**, **Andrea**, **Petro**, na **Antoni**.[186]
Kumbukumbu ya **Belaphio,** Misri**.**

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake! Amina.

## **Mtu wa Mungu, Analena Tonelli, aliyeuawa, 2003**.

Analena Tonelli alizaliwa tarehe 2 Aprili, mwaka 1943. Alisoma sheria na kuhitimu. Akawa wakili. Baada ya miaka sita kuwahudumia maskini, yatima na malemavu ya ki-akili na ki-mwili, katika mji wake Italia, akaenda Afrika, mwaka 1969, akitumwa na *Committee Against World Hunger* (Kamati ya kudhibiti Njaa Ulimwenguni). Akaenda Kenya akifanya kazi kama Mmisionari mlei. Akaishi mjini Wajir na kuwahudumia walio fukara na wagonjwa, kwa miaka kumi. Mwala

[185] *Coptic Synaxarium: 8 Babah.*
[186] *The Ethiopian Rite Missal, Abba Emmanuel & Abba Brendan Cogavin, 2002, uk 174. Ethiopian Synaxarium: 25 Meskerem.*

1976 akateuliwa na *World Health Organization* (WHO) kuongoza mradi wa kutibu ugonjwa wa Kifua Kikuu kati ya wahamahamaji. Tonelli alianzisha pia shule kwa waziwi. Wanafunzi wengi walitoka Somalia na kurudi katika nchi yao ili kuanzisha shule za namna hiyo. Huko Wajir shule kwa waziwi *Somali Signe Language*, yaani lugha ya Kisomalia kwa ishara, imezaliwa.



Mwaka 1984, mapigano ya ki-siasa kati ya makabila yakatokea. Jeshi la Kenya likanzisha kuwakomesha Wasomalia, Kabila la Degodia, walioishi katika maeneo ya Wajir. Wadegodia walifikiriwa kuwa wagaidi. Jeshi la Kenya likawachukua wanaume 5000 na kuwapeleka katika kiwanja cha ndege kiitwacho Wagalia. Wakawalazimisha kujilaza tumboni mwao uchi kwa siku 5. Pengine elfu moja wakauawa kwa risasi, kwa kuteswa au kwa mfichuo (*exposure*). Analena akaleta malori mawili na Toyota yake pale kiwanjani mwa ndege ili kuwaokota maiti na kuwahudumia waliojeruhiwa. Akakataliwa. Baadaye akafuata malori ya Jeshi walipoenda kutupa maiti nje ya kiwanja cha ndege cha Wagalia. Wengine waliishi bado na akawaokoa. Akamwita Mwanahabari kushuhudia na kupiga picha. Habari zikafika Jumuiya ya ki-mataifa. Uuaji ukasimamishwa. Tukio hilo linajulikana kwa jina la Mauaji ya Wagalia. Analena akashtakiwa mbele ya mahakama ya ki-jeshi.

Alipokataliwa na serikali kukaa zaidi Kenya, kwa sababu alipinga kwa nguvu jinsi askari walivyowatendea wakazi wa Wajir mwaka 1980, akaenda Merca, bandari ya Somalia. Na baadaye akahamia Borama, Kaskazini Magharibi ya Somalia. Akaishi katika mji wa Borama, kwa miaka 30, akijenga hospitali na kuwahudumia watu hasa wale walioteswa na kifua kikuu. Na kule Borama akauawa, tarehe 5 mwezi wa Oktoba, mwaka 2003, na watu wasiojulikana. Inasemekana kwamba watu wa Borama walipinga kazi yake ya kuwakaribisha katika hospitali yake wagonjwa wa HIV. Walimshtaki kwamba analeta katika mji wa Borama ugonjwa wa Ukimwi. Wengine wanasema kwamba aliuawa na wanajeshi wa *Al-Itihaad al-Islamiya*.

Mwezi wa Juni 2003 Analena alizawadiwa Tunzo la Nansen Mkimbizi (*Nansen Refugee Award*) na Umoja wa Mataifa kwa ajili ya kazi yake kati ya wakimbizi.
Mtu wa Mungu Analena Tonelli, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

**Oktoba 6**

Huko Afrika ya Kaskazini, Wakatoliki wanawakumbuka Wat. **Rogato, Saturnino, Faustino, Marsiali**, wote wafiadini.[187]
Huko Kigali, Ruanda, Wakatoliki wanamkumbuka **Giuliano Berizzi**, Mlei kutoka Italia, aliyeuawa nyumbani mwake, mwaka 2001.

Huko Misri, Wakoptiki wanamkumbuka Mt. **Eumenio**, Patriarka, askofu wa 7 wa Aleksandria, 146. Pia kukumkumbu ya kupatwa jua, mwaka 958 B.K., toka saa 2.30 hadi 3.30, asubuhi.[188]
Huko Ethiopia, Waorthodoksi Tewahedo, wanawakumbuka **Mashahidi kumi elfu** na **Agati** wa Misri na **Jorji**, mfiadini, baba ya Waorthodoksi Tewahedo.[189]
Huko Afrika ya Kusini, Waanglikana (*Church of South Afrika*) wanamkumbuka **Henrieta Stockdale**, Sista wa Shirika la Mt. Mikaeli na Malaika wote, 1911.

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake! Amina.

## Mt. Eumenio, Patriarka wa Aleksandria, 146

Eumenio akapata daraja la ushemasi na Patriarka Abremio, Askofu wa tano wa Aleksandria. Akahudumia kwa miaka kumi katika cheo hicho.

---

[187] *Acta Sanctorum*
[188] *Coptic Synaxarium: 9 Babah*. Wakatoliki wanamkumbuka Mt. Eumenio tarehe 7 Oktoba. Tunasoma katika kitabu cha Watakatifu wa Wakoptiki, Misri, habari za kupatwa jua na jinsi watu walivyoogopa kwa sababu hawakuelewa yaliyotokea. Wakati wa utawala wa Mfalme El-Saleh Ayound na utawala wa Patriarka Abba Sirili III, Askofu wa 75 wa Aleksandria, kitu cha ajabu kikatokea kilichoshangaza wote waliokiona na kukisikia. Pole pole Jua likaanza kupoteza mwanga hadi giza likaenea mahali popote na nyota zikaonekana. Watu wakawasha taa na wakaanza kuogopa sana. Wakamlilia Mungu Mwenyezi kwa moyo wote, awahurumie. Mungu akawahurumia. Akawaondoa hofu yao na giza pole pole likaondoka. Jua likaonekana tena kuangaza ulimwengu. Taa zikazimishwa. Kitu hiki kilitokea toka saa 2.30 hadi saa 3.30 asubuhi.Watu wakamtukuza Mungu mwenye huruma kwa sababu hakuwatendea kadiri ya madhambi yao, bali kadiri ya huruma na uvumilivu wake. Ee Mungu mwenye huruma, uendelee kuwatendea waamini wake kwa upendo wako. Amina.
[189] *Ethiopian Synaxarium: 26 Meskerem*.

Mt. Yusto alipoteuliwa kuwa Askofu wa sita wa Aleksandria alitambua ujuzi na imani ya Eumenio. Ndipo akampadirisha na kumkabidhi kazi ya kuwafundisha waamini wa Aleksandria, kuwachunga na kuwaimarisha katika misingi ya imani yao.

Askofu Yusto alipofariki, Eumenio alichaguliwa kuwa Patriarka. Akamkabidhi Padri Marsiani kazi ya kuwafundisha waamini wa Aleksandria, kuwarudisha wale waliopotea na kuwaeleza wapagani umungu wa Yesu Kristo. Akakaa katika kiti cha Mt. Marko kwa miaka 13.

Mt. Eumenio, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

## Sista Henrieta Stockdale, 1911.

Henrieta alizaliwa tarehe 9 Julai 1847 Uingereza. Alikuwa mtoto wa kwanza wa Padri Henry Stockdale, curate wa Parokia ya Misterton na baadaye Bole. Akapata Kipa-imara tarehe 22 Mach 1863. Katika ujana wake alipokutana na Mhashamu Eduardi Twells, Askofu wa Bloemfontein, Afrika wa Kusini, hamu ya kwenda misioni ikawaka moyoni mwake. Tangu siku ile, yeye na binamu yake, wakawa washiriki wa Bloemfontein Mission. Akatoa sala zake, mawazo yake, muda wake na mwishoni yeye mwenyewe kwa ajili ya Bloemfontein Mission.

Mwaka 1870 Askofu wa Bloemfontein, Allan Becher Webb akaenda Parokia ya Bole kumtembelea Henrieta na kumwomba aje Afrika ya Kusini kufanya kazi kama nesi. Henrieta akafuata shule ya nesi katika hospitali ya Clever na ya Great Ormond Street. Akapanda meli kuelekea Afrika ya Kusini pamoja na wenzake, tarehe 6 Machi 1874. Huko Bloemfontein Askofu Alan Webb akaanzisha Jumuiya ya Mt. Mikaeli na Malaika wote (CSM na AA),  shirika moja ya masista kuwafundisha wasichana. Henrieta akaweka nadhiri mwaka 1875 na kuitwa Sista Henrieta.[190]

Mwanzoni Sista Henrieta alifanya kazi kama Afisa ya afya, wilayani mwa Kimberley, katika kambi za kuchimba madini. Alipopata ugonjwa wa homa ya tumbo (*typhoid*), ilimbidii kurudi Uingereza kutibiwa.

[190] Jumuiya hiyo haipo tena. Sista Yohana Marsh, sista wa mwisho wa Shirika hilo, amefariki mwezi Mei 2016.

Wakati wa kupata ahueni akafuata kozi fupi huko Chuo Kikuu cha London. Aliporudi Kimberley akaanziha chuo cha mafunzo kwa manesi katika hospitali mpya ya Carnarvon, Kimberley. Sista Henrieta akajiunga na Chama cha Manesi wa Uingereza. Na katika Afrika ya Kusini akafanya juu chini ili Serikali iwasajili rasmi manesi na wakunga. Jambo hilo lilifanyikwa mwaka 1891, na nchi ya Afrika Kusini ikawa nchi ya kwanza ulimwenguni kutambua rasmi mafunzo ya manesi. Mwaka 1895 Jumuiya ya Mt. Mikaeli na Malaika wote wakajitenga na Hospitali ya Kimberley na kuanzisha nyumba mpya na zahanati. Sista Henrieta akafariki tarehe 6 Oktoba 1911, akiwa na umri wa miaka 64 na kuzikwa Kimberley, Afrika ya Kusini, katika shamba la wafu Dutoitspan.

Sista Henrieta alijitoa kabisa kwa Yesu, bila kujibakiza. Nia yake ilikuwa kueneza Injili kwa maneno na hasa kwa matendo ya huruma. Akatumia muda wake mwingi kuwafundisha wengine aliyoyapokea kwanza, kama Paulo anavyomwambia Timotheo: "*Na mambo yale uliyoyasikia kwangu mbele ya mashahidi, hayo uwakabidhi watu waaminifu watakaofaa kuwafundisha na wengine*"[191].

Anakumbukwa na kuheshimiwa sana katika Kanisa la Anglikana la Afrika ya Kusini. Miaka michache baada ya kifo chake, picha yake ikachorwa juu ya kioo cha rangi katika Kanisa Kuu la Mt. Sipriani Bloemfentein. Mwaka 1970 sanamu yake ikaweka uani mwa Kanisa Kuu Mt. Sipriani na mwaka 1984 masalia yake yakazikwa upya karibu na sanamu yake. Jina lake limeandikwa katika Kalenda ya watakatifu wa Kanisa la Anglikana ya Afrika Kusini. Anakumbukwa tarehe 6 Oktoba, siku ya kufa kwake, kwa sala ya pekee. Katika hospitali ya Kimberley kanisa ndogo limetabarukiwa tarehe 29 Septemba na madirisha yamechorwa picha za Malaika wakuu Mikaeli, Gabrieli, Urieli na wengine. Kanisa likaitwa kanisa la Sista Henrieta Stockdale.

Sista Henrieta, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

---

[191] 2 Tim 2:2

**Oktoba 7**

Huko Morogoro, Tanzania, Wakatoliki wanamkumbuka **Adriano Mkoba**, Askofu, aliyefariki mwaka 1995.
Huko Solwezi, Zambia, Wakatoliki wanamkumbuka **Floriana Torilli**, Sista wa Shirika la Yohane Mbatizaji, aliyeuawa mwaka 2000.

Huko Ethiopia, Wakristu wanamkumbuka Abba **Yohane wa Debra-Sege**.[192] Pia kumbukumbu ya **Antilario**, anayeitwa Petro Mtumwa kwa Wakatoliki na Waorhtodoksi.[193]

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake! Amina.

## Antilario au Mt. Petro, Mtunza fedha na mtumwa, karne la VI

Mt. Yohane mtoa sadaka, Patriarka wa Aleksandria, alipenda kuwasimulia waamini wake habari hiyo ili wasiwe wachoyo bali wasaidie maskini kwa kutoa kwa moyo wote. Zamani za Kaizari Justiniani, palikuwa na mtu, kwa jina Petro, mtunza fedha au mtoza ushuru, ambaye, wakati fulani, inasemekana kwamba alikuwa gavana wa Afrika nzima. Basi mwanaume huyu hakuwa na huruma kwa maskini, hata aliitwa ‘Bahili‘. Siku moja, maskini wa mji Aleksandria, Misri, walipokusanyika wakazungumza kati yao, wakiwasifu wale waliowasaidia na kumsemea vibaya Petro, ambaye hata mara moja, hakuwapa kitu. Mmoja wao, mjanja zaidi kuliko wenzake, akawahakikishia kwamba atapata kitu kutoka kwake. Kutimiza maneno yake, akaenda kukaa mlangoni mwa nyumba yake, akimsubiri mtu huyu arudi. Kwa neema ya Mungu Petro akarudi nyumbani wakati mwokaji mkate alipompelekea mikate. Akakutana naye mlangoni pake na akaanza kumsumbua kwa nguvu zake zote, hadi Petro, ili

---

[192] *The Ethiopian Rite Missal, Abba Emmanuel & Abba Brendan Cogavin, 2002, uk 175. Ethiopian Synaxarium: 27 Meskerem.*
[193] *The Ethiopian Synaxarium, Meskerem 27.* Rejea tarehe 22 Septemba/20 Januari

kumwondoa mbele yake, akatafuta kumtupia jiwe. Alipokosa jiwe akamtupia mkate mmoja kwa hasira. Maskini akampokea kwa furaha kubwa na akaenda kuuonyesha kwa wenzake.
Baada ya siku mbili, Petro akaugua mahututi. Katika maono akajiona mbele ya Mungu akihukumiwa. Kwa upande mmoja aliona jeshi la pepo waliokusanya katika sahani ya kushoto ya mizani dhambi zake zote alizozifanya maishani mwake, zile alizokumbuka na zile za ujana wake ambazo alizisahau. Kwa upande mwingine aliwaona watu, waliovaa nguo nyeupe na wenye mtazamo mkali, wakitafuta kitu chochote kukiweka katika sahani ya kulia. Walikuwa na uchungu sana: "Je hatutapata kitu chochote chema alichofanya mtu huyu." Mwishoni mmojawapo alisema: "Sioni kitu, isipokuwa mkate mmoja alimpatia Yesu Kristo, lakini kinyume cha upendo wake." Walipoweka mkate huu katika sahani ya kulia, mizani ikazama tena upande wa kushoto, lakini si kwa nguvu zote kama mwanzoni. Waliovaa nguo nyeupe wakamwambia Mtoza ushuru, tia katika sahani ya kulia, au utatiwa mikononi mwa jeshi la pepo.
Petro akaamka asubuhi akihangaika sana kwa sababu alitambua kwamba maono hayo yalimsemea yeye, akitambua madhambi yake yote ya ujana wake yaliyowekwa katika sahani ya kushoto, akaanza kulia. Akawaza: "Ikiwa mkate mmoja niliomtupia maskini kwa hasira ukanifaidika jinsi hii, je, kutoka maovu ngapi ataokolewa yule anayegawa kwa moyo mali yake kwa maskini?" Tangu siku ile aliamua kuwagawia maskini mali yake yote.
Siku moja akatoka nje kwenda kama desturi yake ofisini mwake. Akakutana na baharia aliyekuwa uchi, baada ya kujiokoa kutoka dhoruba. Papo hapo Petro akavua koti lake, akampatia na kumwambia kulitumia hadi litakalochakaa. Baharia, akiona haya kwa sababu koti lilo lilikuwa nzuri sana, akalipokea na kwenda kuliuza. Petro aliporudi nyumbani akaliona koti lake limetundikwa dukani. Akahuzunika sana na tendo hilo. Alikataa kula na kusema: "Mimi sistahili maskini huyu anikumbuke". Katika uchungu wake, akasinzia na kulala. Lakini Bwana Yesu akamfariji alipomtokea usiku, katika ndoto, akamwambia: "Petro kwa nini unalia?" Akamjibu, kama anazungumza na Mungu: "Nalia, Bwana, kwa sababu, nikiwatolea maskini mali uliyonijalia kwa furaha, wanaona haya ya kuyapokea". Mara Bwana akaonekana akivaa koti

lake. “Je, unalitambua? Tangu uliponipatia nilivaa. Nilikuwa na baridi sana, ukanivisha.“ Mtoza ushuru akaamka kwa furaha akishangaa kuhusu heri ya maskini. Akasema: “Bwana asifiwe! Kama Yesu Kristo anaishi tena ndani ya maskini, sitakufa kabla ya kuwa mmojawapo.“
Ndipo Petro akaamua, siyo tu kugawa mali yake, bali hata nafsi yake kwa ajili ya kuwatumikia maskini. Akamlazimisha mtumwa wake mmoja kumwongoza hadi Yerusalemu na kule kumwuza kwa Mkristo na kuwagawia maskini fedha ya bei yake. Akauzwa kwa vipande thelathini ya fedha kwa sonara mmoja, Zoile, akimtumikia mara kama mpishi, mara kama dobi. Zoile na familia yake wakabarikiwa sana na Mungu. Basi Zoile alipoona unyenyekevu wa ajabu na upendo mkubwa wa Petro, akamwambia kwamba anataka kumpatia uhuru na kuishi naye kama ndugu yake. Petro akakataa kupokea neema hiyo kutoka kwa bwana wake. Petro akaendelea kufunga na kusali. Akateswa sana na watumwa wengine, kuitwa mpumbavu hata kupigwa nao, na pengine kulala akiteswa na maumivu. Yesu, aliyemtokea huko Afrika, akamtokea tena, akiwa na vipande thelathini vya fedha: “Ndugu, nilipokea fedha ya bei uliyouzwa. Usihuzunike. Vumilia hadi utakapotambulika kama ulivyo.“ Siku moja sonara kutoka Aleksandria akaja kwa bwana wake. Walipokuwa wakila, Petro, alipotambuliwa na sonara huyu, aliacha chakula alichobeba na kutoroka kwa hofu kusifiwa. Mlangoni mwa nyumba alikutana na bawabu bubu kiziwi tangu kuzaliwa kwake. Akasema: “Kwa jina la Yesu Kristo nakuamuru usimame na kunifungulia mlango.“ Mara bubu kiziwi akasikia, akasimama na kumfungulia mlango. Papo hapo bawabu akalia: “Bwana, Bwana!“ Wote wa nyumbani wakamsikia. Huyu akatangaza maajabu ya Mungu Petro aliyomfanyia: “Nikaona mwali wa moto kutoka kinywani mwake, ukanigusa ulimi wangu na masikio yangu. Tangu wakati huu nilianza kusikia na kusema“. Wote wakatoka kumfuata Petro, lakini hawakumwona tena.[194] Hatuna habari kuhusu maisha yake ya baadaye na lini alipofariki, lakini anaheshimiwa kuwa mtakatifu kwa Wakristo wa Mashariki.
Mt. Petro mtumwa, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

---

[194] Rejea *Maisha ya Mt. Yohane mtoa sadaka*, yaliyoandikwa na Askofu Leontius, Sura XIII.

**Oktoba 8**

Huko Misri, Wakatoliki wanamkumbuka Mt. **Thais**, mwanamke mkaa pweke mtubu.[195]
Huko Lemera, Jamhuri ya ki-demokrasia ya Kongo, Wakatoliki wanawakumbuka **Bonifasio Kahegezo Koko** na **Yohane-Maria Ndogole Kasati Kashekezi**, mapadri wa Jimbo la Uvira, waliouawa mwaka 1996.

Waorthodoksi wa Magharibi wanamkumbuka pia Mt. **Thais**, Karne la IV.[196]
Huko Ethiopia, Wakristu wanawakumbuka Mt. **Apater** (Abadir**)** na dada yake **Irene** (Ira**)**, wafiadini, Misri. Waorthodoksi Tewahedo wanawakumbuka **Erani** (Irene), mfiadini na **Ankuo Maryam**, **Stefano** mwanae, **Ana** (Hannah), **Porfirina** na **Luka**, mtawa.[197]

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake! Amina.

## **Mt. Thais, mtubu, 350**.



Tais alizaliwa katika mji mdogo fulani wa nchi ya Misri. Wazazi wake walikuwa Wakristo wema. Kwa mapenzi ya Mungu wakafariki Tais angali bado mtoto mdogo.
Tais alipokua akaonekana kuwa msichana mwenye uzuri wa ajabu wa umbo na sura yake. Lakini Tais alikitumia kipaji hiki cha Mungu vibaya. Alipenda kustaajabiwa na watu kwa ajili ya haiba yake na kusifiwa kwa sababu ya uzuri wake. Akafanya umaridadi mwingi ili azidi kuwapendeza watu. Kwa hivi

[195] *Acta Sanctorum*
[196] Rejea *Orthodox Saints of the day*.
[197] *The Ethiopian Rite Missal, Abba Emmanuel & Abba Brendan Cogavin, 2002, uk 176. Ethiopian Synaxarium: Meskerem 28.*

hakukawia kupoteza uzuri wa roho yake aliopewa katika ubatizo. Alipokwisha haribika hakupenda kukaa tena kwa jamaa yake, akatoroka. Akaenda pwani akakaa katika mji wa Aleksandria ulio mji mkubwa sana kando ya bahari ya katikati.

Sifa yake mbaya ikaenea upesi sana katika mji ule walipokutana watu wabaya wengi sana. Hao wakamfikia kwa tamaa ya kutenda dhambi na mwanamke mzuri huyu. Thais akapewa mali nyingi sana, mshahara wa dhambi. Akavaa mavazi bora ya hariri, akajipamba kwa marembo ya lulu na ya dhahabu. Kwa njia hii alizidi kuwatamanisha vijana wengi sana. Mara nyingi ikatukia kuwa watu waliomfikia Thais nyumbani kwake walipigana hata waliuana, kwa sababu ya kuoneana wivu.

Basi habari hizi za kahaba huyu Thais zikasikika hata jangwani. Kule alikuwako mtu, jina lake Pafnusi, naye alikuwa mkaa pweke tangu miaka mingi.[198] Pafnusi huyu akasikia habari za ubaya wa Thais. Akasikitika sana kwa sababu kiumbe huyu anamkasirisha Baba yake wa mbinguni kwa kuvitumia vibaya vipaji vile vile alivyopewa naye. Akaogopa kuwa mwisho Thais, asipoacha kutenda dhambi, atapotea milele. Akamwombea kwa sala zake. Akajisumbua vibaya, kwa njaa na kiu na kwa mambo magumu mengine, ili amwombee huruma kwa Mungu Baba. Lakini Pafnusi hakupata raha moyoni mwake akiwaza kwamba Thais atatengwa milele na Muumba wake. Basi akakusudia kumwokoa katika dhambi zake. Siku moja Pafnusi akavua mavazi yake ya kitawa akavaa mavazi ya kidunia. Akachukua kipande cha dhahabu na akatoka jangwani kumwendea Thais nyumbani kwake huko Aleksandria. Akamkuta kwenye baraza ya nyumba yake. Pafnusi akajisingizia kama anamtamani sana, akampa kipande kile cha dhahabu kuwa mshahara wa dhambi. Thais akakipokea akamwambia Pafnusi akasema: “Basi, twende nyumbani!”

Pafnusi akamfuata Thais mpaka nyumbani. Wakaingia chumbani kwenye mapambo mazuri na kitanda. Pafnusi akawa anatazama huko na huko akionyesha kama anahangaikia mlango na madirisha. Akamwuliza Thais: “Je, kuna chumba kingine pembeni zaidi na pasipo madirisha? Tafadhali kama kiko twende huko huko!” Thais akamjibu akasema: “Kiko, lakini usiogope, hata katika chumba hiki watu hawawezi

---

[198] Rejea maisha yake tarehe 3 Machi.

kutuona wala hakuna mtu atakayeingia humu. Lakini ukimwogopa Mungu, ujue kuwa hatuwezi kujificha machoni pake!"

Basi Pafnusi akamwuliza Thais akasema: "Je, wewe unajua kuwa Mungu yuko?" Thais akajibu akasema: "Ndiyo najua kwamba Mungu yuko. Pia najua kuwa watu wema watapata maisha ya milele, bali wakosefu watapata mateso ya milele."

Pafnusi akamwitikia akasema: "Ndivyo itakavyokuwa! Je, kwa sababu gani wewe umeziharibu roho za vijana wengi hivi? Wewe utahukumiwa na utalaaniwa milele kwa sababu ya dhambi zako, pia kwa sababu ya dhambi za wale uliowaharibu kwa ubaya wako!"

Thais aliposikia maneno haya alimwangukia Pafnusi akashika miguu yake hali anatokwa na machozi mengi. Akamsihi mkaa pweke aliyetoka jangwani kwa ajili yake akasema: "Baba, unipe adhabu ya kufanya toba kweli. Uniombee mimi mkosefu mbaya, ili nipate matumaini ya kusamehewa dhambi zangu; Ninakuomba unipe muda wa saa tatu. Baadaye nitakuwa tayari kufika mahali utakaponiagiza na kufanya utakayoniamuru!"

Pafnusi akamwagiza mahali watakapokutana, akatoka. Thais akachukua mali zake zote, yaani mavazi na urembo na mapambo yaliyofanywa kwa fedha na dhahabu. Akavipeleka vitu hivi vyote sokoni bila kuangalia mshangao na dhihaka za watu aliowakuta njiani. Akavitupa vyote katika moto uliowaka sokoni. Akatangaza kwa nguvu yote ya sauti yake akasema: "Ninyi nyote mliotenda dhambi pamoja nami, njoni na mtazameni: ninateketeza vyote mlivyonipa!"

Vilipokwisha ungua vyote Thais alikwenda mahali alipoagizwa na Pafnusi. Huyu akamtangulia wakaenda katika konventi. Akamwingiza Thais katika kijumba kidogo akafunga mlango akavuta kifungio na kukitia muhuri. Akaacha dirisha dogo katika mlango ili watawa wapate kumpa chakula. Akamwagiza Mkuu wa watawa kwamba Thais apewe kipande kidogo cha mkate na birika la maji kila siku.

Pafnusi alipotaka kurudi Thais akamwuliza akasema: "Je, Baba, nisali nini kijumbani humu?" Pafnusi akasema: "Wewe hustahili kumtaja Mungu, na midomo yako isitamke hata jina lake takatifu, wala usiinue mikono yako mbinguni! Midomo yako na mikono yako imechafuka. Ujiinamishe upande wa maawio ya jua na kusema kila mara: 'Ewe uliyeniumba, unihurumie!'"

Ikapita miaka mitatu. Pafnusi akamkumbuka Thais akamwonea huruma. Kwa hivi akamwendea Antoni mtakatifu amwulize kama Mungu amesamehe dhambi za Thais. Antoni akawakusanya pamoja wanafunzi wake wote. Akawaagiza wote wakeshe usiku kucha na wasali, ili Mungu amfumbulie mmoja wao neno alilouliza Pafnusi.

Basi kila mwanafunzi akaenda katika kijumba chake na kukesha na kusali. Katika kundi la wanafunzi hawa alikuwa mtawa aliyeitwa Pauli mjinga. Huyu alikuwa mtawa mwema sana na mwanafunzi hodari kweli wa Antoni mtakatifu. Pauli huyu alipokuwa akisali usiku ule aliona maono. Aliona kiti kilichopambwa kwa ajabu sana. Kiti hiki kimelindwa na mabikira watatu wenye kung'aa sana. Pauli mjinga akistaajabia kiti pamoja na mabikira wale, akawaza moyoni mwake: "Hakika kiti hiki kitakuwa kiti cha baba yangu Antoni katika utukufu wa mbinguni!" Kumbe pale pale sauti kutoka mbinguni ikasema: "La, kiti hiki hakitakaliwa na baba yako Antoni. Kiti hiki ni cha Thais mwenye kutubu dhambi zake."

Asubuhi, walipokutana watawa wote, Pauli mjinga akawasimulia njozi yake. Basi Pafnusi akapokea neno la Mungu lililomhusu Thais, akiwa ana uhakika kwamba Mungu amemsamehe. Akaenda Aleksandria katika konventi alimofungwa Thais. Akafungua mlango wa kijumba chake. Thais akaomba akasema: "Tafadhali msifungue mlango! Mniache nikae humu!" Pafnusi lakini akafungua mlango na kwa furaha kubwa alimwambia Thais akasema: "Utoke sasa, maana Mungu amekusamehe dhambi zako!"

Thais akamwangukia Pafnusi miguuni pake akasema: "Ninashuhudia mbele ya Mungu: Tangu nimeingia humu sikuacha kukumbuka dhambi zangu. Zikawa kama mlima machoni pangu. Nikaona uchungu katika moyo wangu wala sikuacha kulia machozi siku zote." Pafnusi akamwambia kwa upole : "Mungu amekusamehe dhambi zako zote, kwa sababu ulizikumbuka kwa uchungu wa moyo wako!" Wakamtoa Thais. Naye akampokea Mkombozi wake katika sakramenti takatifu.

Pafnusi akatoka akarudi jangwani. Baada ya majuma mawili Thais akafariki katika amani ya Bwana.[199]

Mt. Thais, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

---

[199] Kutoka kitabu: *Kutoka Uzinifu hadi kufikia Utakatifu*. Manuskripto.

**Oktoba 9**

Sisi Wakatoliki tunamkumbuka Mt. **Abrahamu**, patriarka na baba ya waamini wote, aliyeacha nchi yake Ur na kuelekea nchi ya Kanaani, kwa kutii mwito wa Mungu.[200] Pamoja naye kumbukumbu ya mke wake **Sarah**.
Huko Misri, Wakatoliki wanawakumbuka Wat. **Androniko** na mke wake **Atanasia**, wenye ndoa na watawa. Pia wanamkumbuka Mt. **Demetrio**.[201]
Huko Sudan, Wakatoliki wanamkumbuka Mhashamu **Jerzy Ciesielski**, 1970, Khartoum.

Huko Misri, Wakoptiki wanamkumbuka Mt. **Demetrio**, Patrirarka, askofu wa 12 wa Aleksandria. Pia siku hiyo wanaadhimisha **Ushahidi wa Mt. Matayo**, Mtume na Mwinjili.[202]

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake! Amina.

## Wat. Androniko na mke wake Atanasia, karne la IV.

Wakati wa utawala wa Kaizari Theodosio Mkuu (379-395) mwanamume kijana, kwa jina Androniko, mwenye benki, akamwoa, katika mji wa Aleksandria Misri, msichana aliyeitwa Atanasia, ambaye baba yake alikuwa pia mkurugenzi wa benki. Walikuwa tajiri, lakini walitumia mali yao kwa busara. Walipendwa na wote kwa sababu ya uchaji kwa Mungu wao. Baada ya kupata kwa neema ya Mungu, mwana na binti waliowaita Yohane na Maria, waliamua kuishi katika usafi kamili wa moyo, yaani kujikatalia tamaa. Wakadumu katika hali hiyo maishani mwao mwote. Miaka kumi na miwili ikapita na kwa maongozi ya Mungu, watoto hawa, ambao walikuwa hazina yao, wakafariki. Androniko akajitupia chini na kuwatolea kwa Mungu akisema: "Kama

[200] *Martyrologium Romanum*, ed. 2001.
[201] *Acta Sanctorum*
[202] *Coptic Synaxarium: 12 Babah*. Wakatoliki wanamkumbuka Mt. Demetrio, tarehe 14 Agosti.

nilivyotoka uchi tumboni mwa mama yangu, nitatoka uchi ulimwenguni humu. Mungu amenijalia watoto hawa, Mungu amewachukua, mapenzi yake yatimizwe na jina lake litukuzwe daima!“ Naye Atanasia hakuweza kufajirika, na hawakuweza kumzuia kukesha, usiku wa kwanza, kaburini mwao, katika kanisa la Mt. Yuliani. Alipokuwa anaungua kwa majonzi, Mt. Yuliani akamtokea, akivaa nguo za kitawa na kumwambia kwamba watoto wao wanafurahi mbinguni. Akamkemea kwa sababu alilia kifo chao kuliko kulilia madhambi yake. Maneno yake yakamfariji na akakubali upuuzi wa tanafusi zake. Aliporudi nyumbani akamwomba mume wake ruhusa kwenda katika konventi ili atubu dhambi zake, hamu aliyokuwa moyoni mwake tangu zamani, lakini hakuweza kuiweka wazi mbele ya mume wake, wakati watoto wake walipoishi.




Wakaamua kuhiji kwanza Palestina. Wakawaweka huru watumwa wao na kumkabidhi baba ya Atanasia mali yao, waliondoka usiku kwenda Yerusalemu. Baada ya kuzuru mahali patakatifu, wakarudi Aleksandria, na kumpa Mt. Menas heshima yao. Atanasia akaamuru kubaki huko, wakati Androniko, peke yake, alitembelea monasteri huko Shete, jangwani, kwa sababu wanawake hawapewa ruhusa kuingia. Aliposikia utakatifu wa Abate Danieli akamwendea ili kutaka shauri kuhusu mpango wao, yeye na mke wake, kuishi katika monasteri moja. Abate Danieli akamshauri kumpeleka mke wake Atanasia katika monasteri moja ya Theba na akamkabidhia barua ili aingie katika monasteri ya Watebenesi. Androniko akamsindikiza mke wake. Kwa sababu ya barua za Abate Danieli, Atanasia akapokelewa, akificha jinsia yake kwa kuvaa nguo za mwanamume na kuitwa Atanasi. Androniko akarudi kwa Abate Danieli, akavishwa nguo ya kitawa, na kukaa pamoja naye. Wenye ndoa wakaishi namna hiyo kwa miaka kumi na miwili, mmoja mbali na mwenzake, wakishika sheria zote za utawa kwa uamanifu.

Miaka ikapita. Siku moja, na kila mmoja bila kushirikiana, walipewa kutoka wakuu wao, ruhusa kwenda kuhiji Yerusalemu. Wakakutana njiani. Atanasi akamtambua kwa urahisi mume wake, lakini yeye hakumtambua. Akamfikiria kuwa mtawa kutoka Misri, uso wake umebadilika kwa sababu ya majikanio makali. Wakakubaliana kuenda pamoja, kwa sharti kukaa kimya. Waliporudi Aleksandria kutoka Yerusalemu, Atanasi alimpendekeza mwenzake kujenga kijumba kimoja na wote wawili waishi humo kwa maisha ya toba zaidi. Androniko alitaka kwanza kumwomba shauri Abate Danieli. Akakubali. Basi watawa hawa wakabaki pamoja kwa ukimya kamili wakiyaelekeza mawazo yao kwa mambo ya Mungu tu. Abate Danieli hakukosa kuwatembelea kila wakati alipofika katika kuzuru Kanisa la Mt. Menas.

Siku moja alipowatembelea akamkuta Atanasi mahututi, akilia sana. Danieli akamwambia: "Unalia sasa kuliko kufurahi kwamba Bwana anakuita kukaa naye?" Atanasi akamjibu: "Silii juu yangu, bali juu ya mwenzangu Androniko ambaye nitamwacha katika mateso mengi. Nakusihi, baada ya kifo changu, uchukue barua utakapoona chini ya kitanda changu. Uisome na baadaye umpatie." Akaomba kukominika. Akafariki kwa amani. Waliposoma barua walitambua kwamba Atanasi alikuwa Atanasia mke wa Androniko. Watawa wote walipopata habari hiyo wakamsifu Mungu kumpatia Atanasia uvumilivu mkubwa, na kwa njia hiyo kushinda tamaa za mwili, anasa za ulimwengu na fahari za Adui. Watawa wengi, kutoka monasteri za Aleksandria na Shete, wakamzika Atanasia, wakiimba kwa furaha na shangwe. Wakamzika katika monasteri ya kumi ya Aleksandria. Abate Danieli alitaka kurudi na Androniko, lakini Mungu akaamua tofauti. Muda si muda Androniko akafariki na kuzikwa pamoja na mke wake.[203]

Wat. Androniko na Atanasia, mtuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

[203] Rejea *Les petits Bollandistes*.

**Oktoba 10**

Sisi Wakatoliki tunawakumbuka Wat. **Danieli**, **Samueli**, **Angelo**, **Leo**, **Nikola**, **Ugolino**, mapadri, na **Domino**, bruda, wa Shirika la Fransiskano, wote wafiadini, huko Ceuta Moroko.[204] Kwa sababu walihubiri Injili na kuyapinga mafundisho ya Muhammadi, wakadharauliwa, kufungwa mapingu, kupigwa mijeledi na Waislamu wa mahali pale. Mwishoni walikatwa vichwa na kufa mashahidi.
Katika jimbo la Mayence, Ujerumani, tunamkumbuka **Viktori**, askari wa Jeshi la Theba na mfiadini. Katika jimbo la Kölhn, kumbukumbu ya Mt. **Gereoni** na **wenzake**, askari wa Jeshi la Theba, wafiadini.[205]
Pia siku iyo hiyo, huko Khartoum Sudan, tunamkumbuka Mt. **Danieli Comboni**, askofu.[206]
Huko Italia, kumbukumbu ya Mt. **Serbonio**, aliyekuwa mmisionari wa Afrika katika nchi ya Italia, 573.
Huko Afrika ya Kaskazini, Wakatoliki wanawakumbuka wanaume Wat. **Eusebio, Eraklio, Dionisi na Septimo**, na wanawake Wat. **Septimia**, **Sekunda** na **Salsa**, wote wafiadini, karne la I.
Huko Tunisia, Wakatoliki wanawakumbuka Wat. **Kaisio** na **wenzake 13,** wafiadini, Kartago, Tunisia.
Katika Jimbo la Nevers, Ufaransa, kumbukumbu ya Mt. **Malo**, askari wa Jeshi la Theba, mfiadini.[207]

Wakoptiki wanamkumbuka Mt. **Zekaria**, mtawa, Shete, Misri.[208]
Huko Ethiopia, Wakristo wanakumbuka jambo la ajabu Bwana Yesu Kristo alimtendea Mt. Abba **Atanasi** (Atnatewos), Patriarka, askofu mkuu wa Aleksandria. Waamini wa Kanisa la Orthodoksi Tewahedo, wanawakumbuka Wat. Abba **Bula** (Pawle), **Maryu**, **Petro** (Peter), na **Asotares**, wote wafiadini.[209]

---

[204] Rejea maisha yao, tarehe 13 Oktoba.
[205] *Martyrologium Romanum*, ed. 2005.
[206] *Martyrologium Romanum*, ed. 2001
[207] *Acta Sanctorum*. Pamoja na Kaisio wanatajwa: Kwintasio, Septimino, Venusti, Beati, Sekundo, Donati, Sereno, Kresensi, Niseti, Vitalis (au Natalis), Firmini, Heraklio, Eusebio,
[208] *Coptic Synaxarium: 13 Babah*.
[209] *The Ethiopian Rite Missal, Abba Emmanuel & Abba Brendan Cogavin, 2002, uk 176. Ethiopian Synaxarium: Meskerem 30*

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake! Amina.

## Mt. Serbonio, 573

Kadiri ya pokeo moja Serbonio alikuwa mzaliwa wa Afrika ya Kaskazini. Wazazi wake walikuwa wakristo. Akapadirishwa na Mt. Regulo. Kwa sababu ya dhiki zilizosababishwa na Waharabu (*Vandals*) ambao walikuwa wafuasi wa Ario, Wakristo walisambaratika. Pamoja na Regulo, Feliksi na mapadri kadhaa, Serbonio aliweza kutoroka na kufika Italia. Baada ya dhoruba baharini walitua huko Tuscani. Wakaishi kama wakaa pweke. Wakati wa vita kati ya jeshi la Warumi na Wagotiki, Regulo akakamatwa, akishtakiwa kuwa upande wa Warumi, akatiwa gerezani na kukatwa kichwa.

Baada ya kifo cha Florentio, askofu wa Populonia, waraia na wakleri wa mji ule, wakamwomba Serbonio kuwa askofu wao. Lakini wakachoshwa naye kwa sababu, Serbonio kila jumapili aliamka mapema sana, alfajiri, kusoma misa, kuliko saa za kawaida. Wakamwendea Baba Mtakatifu Vijilio. Aliposikia mambo Serbonio aliyoyafanya akakasirika, akamtumia ujumbe ili askofu Serbonio aletwe Roma. Wakamkuta Serbonio akila chakula chake cha asubuhi. Wakamshtaki kuwa mzushi, wakifikiri kwamba alikuwa anakula kabla ya kusoma misa.[210]. Kwa kweli wakati ule amekwisha soma misa. Wakampeleka Roma. Njiani aliwaponya wanaume watatu walioteswa na homa kali. Pia aligeuza hali ya batamwitu kuwa bata wa kufugwa, kwa kuwafanyia ishara ya msalaba. Bata hawa wakamsindikiza hadi akafika kwenye Kanisa la Mt. Petro na wakaruka tena Serbonio alipowafanyia tena ishara ya msalaba.

Huko Roma, asubuhi ya kesho yake, Serbonio akaingia chumbani mwa Baba Mtakatifu na kumwamsha kutoka kitandani. Ndipo akamwuliza Baba Mtakatifu ikiwa hakusikia Malaika walioimba. Vijilio akamjibu kwamba alisikia jambo kama hilo. Serbonio akaenda kusoma misa na

[210] Zamani Wakristo walilazimishwa kufunga kuanzia saa 6 usiku, ili waweze kupokea komunio.

Vijilio akamruhusu kusoma misa kwa saa yoyote anayopenda. Akamrudisha Piombino.


Kwa sababu aliwaficha askari Warumi, Totila, Mfalme wa Waostrogoti, akaamua auawe na dubu mkali. Lakini dubu hakuweza kufanya kitu chochote mbele yake. Akasimama kwa miguu yake miwili ya nyuma na kufungua mataya yake, lakini akaanguka chini juu ya miguu yake minne na kuanza kulamba miguu ya Mtakatifu. Basi Totila akamhamisha Serbonio katika kisiwa cha Elba.

Mnamo mwaka 575, akiwa mzee na mgonjwa, Serbonio akaomba kuzikwa huko Populonia. Lakini aliomba kwamba wale watakaomzika warudi mara huko Elba. Rafiki zake wakamtii. Meli, iliyobeba mwili wake, ikagongana na dhoruba, lakini ikafika salama Populonia. Wakamzika Serbonio na wafuasi wake wakarudi haraka Elba. Muda si muda, Walombardi wakavamia Populonia. Serbonio alikuwa ameona hayo na alitaka kuwaokoa rafiki zake.

Mt. Serbonio, utombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

## **Mt. Daniel Comboni, askofu, 1881**.

Daniel Comboni alizaliwa Italia, tarehe 15, Machi, 1831. Wazazi wake Luigi na Domenika walikuwa wakulima. Watoto wanane walizaliwa lakini Danieli tu, mtoto wa nne, aliishi, wa sita walikufa wakiwa wachanga. Wakaishi katika umaskini wa mambo ya dunia, lakini katika utajiri wa mambo ya ki-roho. Danieli alienda shule huko Verona, kwa shirika lililoanzishwa na Padri Nicola Mazza. Wakati wa vita, huko Verona, Danieli alitambua mwito wake wa kuwa padre. Akamaliza masomo yake ya falsafa na teolojia. Alivutwa kwenda katika Afrika ya Kati aliposikiliza habari zilizoletwa na wamisionari wa Shirika la Mazza wakirudi kutoka Afrika. Akapadirishwa mwaka 1854, na baada ya miaka mitatu alienda Afrika, pamoja na wamisionari watano wa Shirika la Mazza. Mama



yake Domenika akambariki kwa kusema: “Nenda, Danieli, Mungu akubariki”.

Baada ya safari ya miezi minne Comboni alifika Khartoum, mji mkuu wa Sudan. Mara akayatambua matatizo mengi atakayoyakabili nayo. Lakini yote, kazi ngumu, hali ya hewa, magonjwa, vifo vya wamisionari wenzake, umaskini wa watu, yote yalimsukuma kwenda mbele, bila kukata tamaa. Akawaandikia wazazi wake: “Tutahitaji kufanya kazi kwa nguvu, kutoa jasho, hata kufa. Lakini wazo ya kutoa jasho na kufa kwa ajili ya upendo wa Yesu Kristo na wokovu wa watu wanaoishi hapa, ni tamu zaidi kuliko kuacha jambo kubwa kama hilo.” Baada ya kushuhudia kifo cha mmisionari mwenzake, Comboni akajisikia moyoni hamu kubwa ya kuendelea kazi ya misioni: ‘*O Nigrizia o morte!*’, yaani Afrika au Kifo, alikuwa anasema.

Aliporudi Italia, akapanga mikakati mipya kuendesha misioni. Mwaka 1864, alipokuwa anasali kwenye kaburi ya Mt. Petro, huko Roma, wazo likamjia kwa nguvu rohoni mwake. Akaanza kuandika mpango mpya kwa ajili ya kuzaliwa upya Africa: ‘Afrika utaokolewa na Waafrika!’ Ingawa aliyakabili matatizo mengi, Comboni alitembea Ulaya mzima kuliuza wazo hilo kwa Jamii, Wakuu wa dunia na Kanisa, akitafuta msaada wa ki-roho na hali kwa ajili ya Misioni ya Afrika ya Kati. Kwa kufaulu katika kazi hiyo alianzisha kuchapisha Gazeti moja la ki-misionari. Pia, mwaka 1867 na 1872, akaanzisha mashirika mawili, Wamisionari mapadri wa Comboni na Wamisionari masista wa Comboni. Akahudhuria Mtaguso wa Vatikano wa I, kama Mwanateolojia wa Askofu wa Verona na huko akapata sahihi za maaskofu sabini kwa ajili ya kuinjilisha Afrika ya Kati.

Mwaka 1877, tarehe 2 Julai, aliteuliwa kuwa Vika wa kitume wa Afrika ya Kati na baada ya mwezi mmoja kupata daraja ya uaskofu. Mwaka 1877 na 1878 njaa ilitokea katika Afrika ya Kati na watu wengi walifariki. Idadi ya watu ilipungua kwa nusu. Wamisionari walibaki bila kitu. Mwaka 1880, Comboni alisafiri huko Afrika kwa mara ya nane na mara ya mwisho, ili kusimama pamoja na wamisionari wake, akipinga kwa nguvu biashara ya watumwa na kuimarisha kazi ya umisionari iliyoendeshwa na Waafrika wenyewe. Mwaka mmoja baadaye, akilemewa na mizigo ya kupelekea Injili Afrika, Comboni akaugua. Tarehe 10, mwezi wa Oktoba, mwaka 1881, alifariki Khartoum, kati ya

watu wake, akiwa na miaka 50 tu. Akafariki lakini alijua kwamba kazi yake itaendelea: 'Nakufa lakini kazi yangu haitakufa'. Na kweli kazi yake inaendelezwa na wamisionari wake, huko Sudan, Uganda na Kenya, hadi leo. Tarehe 17, Machi 1996 akatangazwa kuwa Mwenyeheri na tarehe 5, Oktoba, 2003 kuwa Mtakatifu na Baba Mt. Yohane Paulo II.
Mt. Danieli Comboni, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

**Oktoba 11**

Sisi Wakatoliki tunamkumbuka Mt. **Sarmata**, mfuasi wa Mt. Antoni, aliyeuawa na Waarabu, huko Theba, Misri, 357.[211]
Huko Ethiopia, kumbukumbu ya Mt. **Mikaeli Aragawi**, mmoja wa Watakatifu tisa, karne la IV.[212]
Huko Senegal, Wakatoliki wanamkumbuka Mtumishi wa Mungu **Aloisi Kobes**, Vika wa kitume, Mtawa wa Shirika la Roho Mtakatifu, 1872.
Huko Bunia, Jamhuri ya ki-demokrasia ya Kongo, Wakatoliki wanamkumbuka **Veronika Dz'da**, mlei, aliyeuawa na Walendu, mwaka 2002. Ni mmojawapo miongoni wa Wahema 1200 waliuawa.

Huko Ethiopia, Wakristu wanamkumbuka Mt. **Cheriton** (*Haritan*), **Susana** bikira.[213]

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake! Amina.

## Mt. Sarmata, Mtawa, Shahidi, 357 au 362

Hatufahamu mengi kuhusu Mtakatifu huyu. Kwa uhakika, alikuwa mfuasi ya Mt. Antoni, aliyeuawa na kundi la Wasaraseni jangwani la Theba. Kuhusu yeye tunayo hadithi ifuatayo: Siku moja Sarmata alienda jangwani peke yake kwa muda wa siku 40, kufuata shauri la Abba Poemen. Aliporudi Abba Poemen akamwuliza alichojifunza. Mt. Sarmata akamjibu: "Mambo ya kawaida tu, abba". Lakini Abba Poemen akaendelea kumwuliza. Sarmata akamjibu kwa mara ya pili: "Nilitambua kitu kimoja tu. Ikiwa nauambia usingizi wangu, 'ondoka', basi unaondoka. Ikiwa nauambia: 'Njoo', unakuja". Sarmata akasema tena: "Nampenda zaidi mtu aliyetenda dhambi, na anajua namna ya kukiri dhambi zake na kutubu, kuliko mtu huyu, ingawa anatenda matendo ya haki, bado anajiridhisha nafsi na haki yake."

[211] *Martyrologium Romanum*, ed. 2005.
[212] *Acta Sanctorum.* Rejea maisha yake tarehe 24 Oktoba.
[213] *The Ethiopian Rite Missal, Abba Emmanuel & Abba Brendan Cogavin, 2002, uk 178. Ethiopian Synaxarium: Tekemt 01.*

Siku moja Abba mmoja akamwendea Sarmata na akakiri kwamba ni mzembe, anawaza mawazo mabaya, na akili yake daima inavurugika. Sarmata alimwambia kwenda chumbani mwake kwa ajili ya Jina la Mungu, kufanya yote anayoweza na hasijisumbue. Pia akamshauri kukesha muda mrefu, na kulala akijisikia amechoka; akajisikia ana njaa, ale; akijisikia ana kiu, anywe; na wakati mawazo yake yanamsumbua ayaambie: "Niliyasikiliza kabla, lakini naamua nisiyasikilize sasa." Mt. Sarmata alisema pia: "Ikiwa mtu hakimbii mambo yote anapoweza, basi anakaribisha dhambi."
Mt. Sarmata, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

## Mtumishi wa Mungu Aloisi Kobes, 1872

Aloisi alizaliwa Ufaransa, tarehe 27 Aprili 1820, mwana wa Yohane Kobès na Magdalena Braun. Akajifunza huko Strasbourg na kupadirishwa katika jimbo mwaka 1844. Miaka miwili baadaye akajiunga na Shirika la Roho Mtakatifu, lililoanzishwa na Mt. Fransisko Liberman. Akatumwa Gambia, Afrika ya Magharibi. Mwaka 1848 akateuliwa kuwa msaidizi wa Askofu Yohane (Jean) Remi Bessieux. Kwa maisha yote yote aliangalia sehemu ya Kaskazini ya Jimbo lake, wakati Askofu Bessieux akiangalia sehemu ya Kusini. Mwaka 1863 akateuliwa kuwa Vika wa kitume wa Senegambia, siku hizi nchi ya Senegal. Akakaa huko Dakar.
Aloisi alipewa na Mungu kipaji cha lugha. Alikuwa anazumgunza kwa ufasaha lugha tatu za wenyeji wa Senegal, Kiserere, Kisoninke na Kiwolof. Mwaka 1865 akachapisha kitabu: *Principles de la langue Wofol,* yaani 'Kanuni za lugha ya Kiwolof'.
Jitihada zake zote zilifanyika hasa kwenye mazingira ya Waislamu. Akakabiliwa na magumu mengi, hasa vifo vya mapema vya wamisionari wake. Apanga Ukristo katika jimbo lake akizidisha na kufadhili misioni nyingi mpya. Pia akatumiwa nguvu zake kwa kuwatayarisha mapadri wazalendo. Mapema, mwaka 1864, akapadirisha Guillaume Jouga, padri wa kwanza mwaafrika kutoka Senegal. Wengine wakafuata. Alishughulika pia kuanzisha shirika la masista wazalendo. Akaanzisha mashirika mawili ya wazalendo, Shirika la masista wa Moyo Mtakatifu wa Maria, na Shirika la mabruda

wa Mt. Yosefu. Mashirika hayo mawili ya wazalendo yalikuwa wa kwanza katika Afrika nzima. Wakati alipofariki huko Dakar, tarehe 11 Oktoba 1872, kulikuwa masista 28 walioweka nadhiri.
Mtumishi wa Mungu Aloisi Kobes, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

## Veronika Dz'da 2002

Veronika alizaliwa huko Iga-Barrière, Jamhuri ya ki-demokrasia ya Kongo, tarehe 13 Aprili 1948, katika familia ya watoto saba, wasichana sita na mvulana mmoja. Wazazi wake walikuwa Pierre Ngbape na Tereza Goy. Baba yake alipofariki akiwa na umri wa miaka sita, alijifunza mapema kuwatunza wadogo wake. Akabatizwa na kupokea kipa-imara katika parokia ya Lita, Jimbo la Bunia. Akaolewa kufuatana desturi ya mila na ki-jamii tarehe 3 Juni 1965 huko Djugu. Na tarehe 8 Aprili 1969 ndoa yake ikabarikiwa huko Parokia ya Kanzenze, Jimbo la Kolwezi, Katanga.
Watoto kumi na mmoja walizaliwa kwa ndoa hiyo: wavulana wanane na wasichana watatu. Kwa sababu mshahara ya mume wake, aliyekuwa Polisi, haukutosha Veronika akafanya kazi ya kulima kwa bidii. Akawafundisha watoto wake umuhimu wa kulima, na kwa mapato yake aliwawezesha watoto wake, wasichana kwa wavulana, kufuata shule. Akajitahidi kuwalea katika ukristo na kuwakabidhi imani yake. Tena alimwombea mume wake ili awe Mkatoliki.
Veronika aliuawa katika mauaji wa Hema huko Nizi. Akatekwa nyara tarehe 11 Oktoba 2002 na kupelekwa kutoka Nizi hadi Bambu, kwa amri ya Tekpate na Mambo, Jemadari wa FNI/KOBU (Lendu). Akapigwa risasi siyo mbali na Parokia ya Mt. Terezia huko Bambu-Mines. Mwili wake ulichomwa.
Tarehe 4 Januari 2003, Dikanza Stella, aliyetekwa nyara pamoja na Veronika aliyejiokoa nafsi yake, akaleta habari za kifo chake. Akapigwa na risasi tatu. Kabla ya kuuawa alilazimishwa kubeba mzigo mzito kichwani. Alipotembea, akasikiwa kusema mara nyingi neno Msamaha: "Mungu awasamehe askari wa Lendu kwa mauaji waliyotenda hadi leo. Mnaniua, sina kinyongo dhidi yenu, nawasamehe ninyi nyote mambo mnayonitendea. Naomba msamaha wa Mungu kwa yote niliyowatendea

vibaya kwa njia moja au nyingine." Aliposema maneno hayo, akakata roho.[214]
Veronika Dz'da na wenzako Wahema, mtuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

[214] Rejea Fr. Neno Contra,, Louis Kalonji, *African Lay Martyrs*, New People Media Centre, 2009, uk 148-150.

**Oktoba 12**

Sisi Wakatoliki tunawakumbuka **Feliksi** na **Sipriano** na wenzao **elfu nne na mia tisa na sitini na nne**, **Mashahidi** Afrika Kaskazini, mnamo 485. Kati yao wengine walikuwa maaskofu, **Feliksi** na **Sipriano**, wengine mapadri na mashemasi, walihamishwa jangwani kwa sababu ya kuitetea imani ya ki-katoliki. Wengi waliteswa vibaya na viongozi wao. Kwa mikuki yenye ncha kali na kwa mawe waliyotupwa walilazimishwa kuharakikisha mwenendo wao. Wengine, miguu ilifungwa, waliburutwa kama maiti hadi viungo vyote vya mwili wao viliraruliwa. Mwishoni, wakiteswa kwa namna mbalimbali, wote walifia dini.[215]
Huko Sudan, Wakatoliki wanamkumbuka Mtu wa Mungu **Fortunata Kwasche** (*Quasche*), Sista wa Shirika la Masista wamisionari wa Comboni, aliyefariki mwaka 1899.

Huko Ethiopia, Wakristu wanamkumbuka kuzuru kwake nchi ya Misri, Mt. Abba **Severo**, askofu wa Antiokia; Mt. **Taklat Sama'et**. Waorthodoksi Tewahedo, wanamkumbuka **Siriaki** (Heriacus).[216]

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake! Amina.

## Mtu wa Mungu Sista Fortunata Kwasche, 1899

Msichana aliyeitwa baadaye Sista Fortunata Kwasche, alizaliwa Mlima wa Nuba, Sudan, mnamo mwaka 1841. Akiwa na umri wa miaka 8 au 9, akakamatwa pamoja na wasichana na wavulana, na kuuzwa kama mtumwa sokoni mwa mji Kairo, mwaka 1853. Hatuelewi jinsi alivyosafiri kutoka Tongolo hadi Kairo. Akaokolewa na Geremia da Livorno, Mwitaliano, Padri wa Shirika la Wafransisko, aliyejitahidi kuwaokoa vijana waliokuwa wanauzwa sokoni. Hatujui kwa jina gani

[215] *Martyrologium Romanum*, ed. 2005.
[216] *The Ethiopian Rite Missal, Abba Emmanuel & Abba Brendan Cogavin, 2002, uk 178. Ethiopian Synaxarium: Tekemt 02.*

aliyeitwa, wala majina ya ndugu zake. Aliitwa bhakita na wachuuzi wa watumwa, jina la kawaida kwa wanawake watumwa.
Baada ya kuwekwa huru akatumwa Verona, Italia, mahali ambapo Padri Nikola Mazza alipoanzisha seminari na shule kwa ajili ya wasichana na wavulana wasiokuwa na uwezo. Nia ya Padri Nikola Mazza ilikuwa kuwatayarisha wamisionari kutoka Afrika yenyewe. Mtakatifu Danieli Comboni akawa mfuasi na mwandamizi wake. Tarehe 6 Januari, 1854, akabatizwa na kuitwa Fortunata, akapokea sakramenti ya Kipa-imara. Kwa miaka 11 alibaki shuleni, akijifunza Kiarabu na Kiitaliano, jeographia na historia, famasia na udaktari, na kazi ya akina mama, kama kushona, n.k.
Mwaka 1867, Fortunata na wenzake 9 wakachaguliwa kwenda Afrika kama Wamisionari Walei. Katika safari yao, mwezi wa Mei wakapita Roma na kukutana na Baba Mtakatifu Pio IX. Walipofika Kairo, katika barua yake moja, Daniel Comboni alieleza sababu yake kuwakutanisha na Baba Mtakatifu: "Kazi ya wongofu wa ki-roho ya Afrika inahitajika kuzinduliwa juu ya Kaburi ya Mkuu wa Mitume".
Daniel Comboni akawachukua wanawake 16 kuanzisha huko Kairo 'Chuo cha Weusi' kwa ajili ya kuwalea wasichana wa Afrika. Walimu walikuwa Waafrika tu waliotayarishwa huko Ulaya. Fortunata alikuwa mmojawapo. Fortunata akakaa Kairo kwa muda wa miaka 6. Tarehe 26 Janauari 1873, Daniel Comboni akaongoza kikundi cha Wamisionari kwenda Sudan Kusini. Fortunata alikuwa mmojawapo pia. Huko Khartoum Fortunata akakaa miezi michache, na baadaye akaelekea kwenda El Obeid, pamoja na mwenzake Donatilla Bakhita. Akakaa huko miaka 6 akifundisha katika Shule ya Kordofan, iliyoanzishwa na Wamisionari.
Mwaka 1878 Masista wa Shirika la '*Pious mothers of Africa*', shirika lililoanzishwa na Daniel Comboni, wakafika Sudan. Fortunata akaomba kujiunga nao. Akaanza novisiati huko El Obeid na mwaka 1882, tarehe 9 Aprili, akaweka nadhiri zake za kwanza. Mwaka ule Muhammadi Ahmad, aliyejiita El Mahdi, na wafuasi wake wakaingia El Obeid na Dilling, misioni mbili zilizoanzishwa na wa Comboni. Sista Fortunata akatekwa nyara, pamoja na mapadri na masista wengine, na kufungwa kambini. Kulikuwa wakati wa mateso yake, hasa kudharauliwa kwa njia nyingi ili akubali kusilimishwa. Akakataakataa. Baada ya miaka mitatu

kufungwa, Sista Fortunata na Sista Maria Caprini walifaulu kutoroka, tarehe 7 Oktoba 1885 na kufika Kairo tarehe 9 Novemba ya mwaka ule. Fortunata akarudi kufundisha katika Chuo cha Weusi. Baada ya muda Wamisionari wakanunua eneo katika kisiwa cha Zamalek. Huko waliweza kujenga nyumba za mapadri, masista, kupokea watumwa wakristo na wakatekumeni, na kulima. Mahali paliitwa Ghesira, wamisionari wakapaita '*Colonia Antischiavista Leo XIII*'. Fortunata akakaa huko kwa muda mfupi, akahamishwa Aswan awe mmojawapo wa walimu. Lakini kwa sababu wanafunzi wengi walikuwa Waarabu wa Misri, yaani weupe, wazazi wao walipinga utaratibu uliokuwepo shuleni, yaani, watoto wao wafundishwe na Mwalimu Mweusi. Ilikuwa gumu kwa Sr. Fortunata kupokea jambo hilo, kudharauliwa na Waarabu kwa sababu kuwa mweusi, kwa hiyo, akarudi kukaa Ghesika, huko Zamalek. Na huko akafariki tarehe 12 Oktoba, mwaka 1899, siku ambayo tunakumbuka Mt. Fortunata.

Hatuna maandishi kutoka Sr. Fortunata, isipokuwa barua chache. Ni vigumu kutambua hali yake ya ki-roho, jinsi alivyoshinda vishawishi, na kuvumilia mateso. Mara moja Sr. Giuseppa Scandola[217] akamwandikia Sr. Costanza Caldara, mjumbe rasmi wa Mama Mkuu, aliyewatembelea wenzake Kairo, kuhusu Sr. Fortunata. Akamaliza kwa maneno: "Sista mwenye wivu kwa Mungu, na kujitoa kabisa kutenda mema".

Mtu wa Mungu Sista Fortunata Kwasche, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

---

[217] Rejea maisha yake tarehe 1 Septemba

**Oktoba 13**

Shirika la Ki-fransisko wanawakumbuka mashahidi **Danieli, Samueli, Anjelo, Leo, Domino, Nikola na Hugolino**, waliouawa Moroko, 1221.

Huko Misri, Wakoptiki wanamkumbuka Mt. **Agato**, Patriarka, askofu wa 39 wa Aleksandria. Pia kumbukumbu ya Wat. **Karbu**, **Apolo** na **Petro**.[218]
Huko Ethiopia, Wakethiopia wanamkumbuka Abba **Simeoni II**, Patriarka, askofu wa 51 wa Aleksandria, Misri. Waorthodoksi Tewahedo, wanawakumbuka pia Wat. **Makari**, **Theofilo**, **Eumara**.[219]

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake! Amina.

## Watakatifu Danieli, Samueli, Anjelo, Leo, Domino, Nikola na Hugolino, 1221.

Ndugu Danieli, mtawa mwenye busara na mtaratibu, aliyewahi kuwa Provinsiali wa Kalabria, pamoja na ndugu wengine sita wenye uchaji na bidii, walitamani kwa moyo wao wote kujitoa kwa ajili ya wokovu wa Waislamu. Hawakuogopa kuhatarisha maisha yao, ili mradi wampatie Mungu matunda bora, yaani uongofu wa Waislamu. Mwaka 1221, baada ya kupata ruhusa kutoka Mkuu wao, Ndugu Eliya, wakapanda meli bandarini mwa Toscane, Italia, wakavuka hadi Tarragone, Hispania, na kutoka kule wakafika Ceuta.
Danieli na wenzake watatu walifika kwanza, kwa sababu rubani wa meli alikataa kuwachukua watu zaidi. Wakakaa kwa muda kanda ya kiunga cha mji Ceuta, mahali ambapo wafanyabiashara Wakristo kutoka miji ya Pise, Genoa na Marseilles, walipoishi. Kulikuwa marufuku kwa Wakristo kuingia mjini. Wakaanza kuwahubiria wafanyabiashara Neno la Mungu wakati walipongojea ndugu wenzao waliofika tarehe 29 Septemba.

[218] *Coptic Synaxarium: 16 Babah.*
[219] *The Ethiopian Rite Missal, Abba Emmanuel & Abba Brendan Cogavin, 2002, uk 178. Ethiopian Synaxarium: Tekemt 03*

Ijumaa ya tarehe 1 Oktoba, walitafakari faraghani juu ya wokovu wa roho zao wenyewe na wokovu wa wengine. Siku iliyofuata yaani Jumamosi, walikwenda kuungama kwa ndugu Danieli na kupokea sakramenti ya Ekaristi, na bila hofu, walijiweka moja kwa moja mikononi mwa Mungu. Jioni ya siku ile walitawadhana miguu ili kumwiga Mwana wa Mungu aliyewatawadha miguu ya Mitume wake kabla ya Mateso yake.

Kisha kujiandaa hivyo, Jumapili asubuhi na mapema askari hawa wa Kristo waliingia katika mapambano. Walikuwa wamevinyunyizia vichwa vyao majivu na kwa siri waliingia mjini na kusonga mbele bila woga. Wakiwa wameimarishwa kwa nguvu ya Roho Mtakatifu, walilitangaza jina la Bwana katika mitaa wakisema pande zote kwamba hakuna wokovu wa kweli kwa jina jingine lo lote.

Neno la Mungu lilikuwa likiwaka kama moto katika moyo wa kila mmoja. Walionekana kama watu walioshindwa kujitawala katika kuustahimili utamu huo wa upendo wa kimungu. Waislamu hata hivyo, waliwapiga kichwani na kuwalundikia madharau pamoja na mapigo mengi. Hatimaye, walikamatwa na kufikishwa mbele ya mfalme. Kwa kupitia kwa mkalimani, walisikilizwa mbele ya mfalme, huku wakilitangaza jina la Bwana kama watu waliolevywa na Roho Mtakatifu. Mfalme na washauri wake, wakiona jinsi walivyovaa na vichwa vyao kunyolewa vikibakizwa taji ya nywele, waliwapuuza kama wenda wazimu, wakaamuru watupwe gerezani; Wakakaa humo siku nane, wakifungwa kwa minyororo ya chuma na kudharauliwa. Kwa neema ya Mungu wakapata nafasi kuwaandikia barua Padri Hugo aliyewahudumia Wakristo wa Genoa, na watawa wawili waliofika karibuni kutoka Mauretania:

"Asifiwe Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, Baba wa huruma na Mungu wa faraja zote. Anatufariji katika shida zetu zote. Alimpa babu yetu Abrahamu kafara kwa ajili ya kutoa sadaka, ambaye kwa amri ya Bwana aliiacha nchi yake bila kujua alikokuwa akienda. Kwa tendo hilo alihesabiwa kama mtu mwenye haki na kuitwa rafiki wa Mungu. Kwa hiyo, yeyote aliye na busara na ajifanye mjinga kusudi awe na hekima, kwani hekima ya ulimwengu huu ni upuuzi machoni pa Mungu. Hivyo, jueni kwamba Bwana Yesu Kristo aliyeteseka kwa ajili yetu na aliyesema, *'nendeni, mkahubiri Injili kwa kila kiumbe'* na *'tena mtumishi si mkuu zaidi kuliko Bwana wake'* na

*'ikiwa walinitesa mimi, watawatesa na ninyi vile vile'*, aliziongoza njia zetu kwa njia zake kwa utukufu wake na kwa wokovu wa waumini, kwa heshima ya Wakristo, kifo na hukumu ya wasioamini.

Kama mtume anavyosema, '*sisi ni harufu nzuri ya Kristo*,' kwa baadhi, harufu nzuri ya uhai kwa maisha, na kwa wengine harufu ya kifo cha mauti. Kwani Kristo anasema, 'Kama nisingalifika na kusema nao, wasingalikuwa na dhambi, lakini sasa hawana kisingizio.' Kwa hiyo tumelihubiri jina la Kristo kwa wakazi wa mji wa Ceuta, na hata mbele ya mfalme. Tumetoa ushuhuda kuwa hakuna wokovu wa kweli kwa mwingine ye yote, na kwa njia ya mkalimani tulionyesha ushuhuda hai mbele ya wasomi wake. Mfalme, akifikiri tu wenda wazimu, akatutia gerezani. Tuliona vema kuwapasha habari. Ingawa tunapata mateso mengi, tunafarijiwa na upendo wa Yesu Kristo, ambaye tumemtolea maisha yetu yawe sadaka ya kumpendeza. Kwa hiyo, kwa mfalme wa karne zote, asiyekufa na asiyeonekana, kwa Mungu peke yake iwe heshima na utukufu milele na milele. Amina."

Hakimu Arbaldo aliyetaka kuwavisia wafungwa, kwa njia ya mwanya ukutani, akaamuru minyororo iondolewe. Akawaona wanamsifu Mungu kwa furaha, uso wao uking'aa mwanga wa ajabu. Akampasha habari Mfalme. Siku ya Jumapili asubuhi, tarehe 10 Oktoba, hao ndugu waliongozwa kutoka gerezani kwenda kwa mfalme. Walipoulizwa kama walijuta kwa kusema maneno ya namna ile kinyume cha sheria ya mtume Muhammadi, walijibu kuwa hawakujuta tena walithibitisha yote waliyosema kwamba hakuna wokovu kwa ajili yao katika sheria waliyokuwa wakiifuata, na pia wasingeweza kuokolewa isipokuwa kwa njia ya ubatizo na imani katika Yesu Kristo Bwana wetu, ambaye kwa ajili yake walikuwa tayari kufa.

Ndipo hawa askari shupavu wa Kristo walivuliwa nguo zao na watumishi hawa wa shetani na mikono yao ilifungwa nyuma. Waliongozwa kutoka jumba la kifalme kuelekea nje ya mji wakichukua shutumu za Kristo. Waliongozwa kama kondoo kwenda kuchinjwa. Hata hivyo, waliharakisha kwa furaha kwenda kuchinjwa, tena kwa shangwe kama kwamba walikuwa wamealikwa kwenye karamu. Walipofika mahali pa kuuawa, uhai wao uliondolewa kwa kukatwa vichwa wakiwa mikononi mwa watu waovu. Walizitoa roho zao takatifu kwa Bwana zikiwa zimepakwa damu yao wenyewe.

Waislamu walivunjavunja vichwa vyao na kukatakata miili yao. Masalia yao yaliokotwa na Wakristo na kuwekwa katika ghala ya

wafanyabiashara wa mji Marseilles. Baadaye walizika miili yao katika kiunga cha Ceuta. Miaka ikapita miili yao ikapelekwa katika kanisa la Mt. Maria. Miujiza mingi ikatendeka, hasa mwanga mkubwa ukaonekana, ambao Waislamu waliweza kuuona kila siku juu ya Kanisa la Mt. Maria. Na baadaye Mreno mmoja, kwa ruhusa ya Mfalme wa Moroko, akayachukua na kuyapeleka katika Uhispania. Miujiza mingi ikatendeka tena, lakini haijulikani sasa masalia yapo wapi. Baba Mtakatifu Leo X aliwatangaza kuwa mashahidi na kuweka sikukuu yao tarehe 13 Oktoba.[220]

Watakatifu Danieli na wenzake, mtuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

[220] Kutoka: *Le palmier serafique*, tome X, na *Sala ya Kanisa ya Ki-fransisko*, Ndanda-Peramiho, uk. 378-381.

**Oktoba 14**

Katika Tanzania, Wakatoliki wanamkumbuka Mtumishi wa Mungu **Julius K. Nyerere**, 1999.

Huko Misri, Wakoptiki wanamkumbuka Mt. **Dioskoro II**, Patriarka, askofu wa 31 wa Aleksandria.[221]
Huko Ethiopia, Wakristo wanawakumbuka wafalme wakristo wa kwanza, **Abraha** (‘Abreha) na **Atsbeha** (‘Asbeha), waliotawala juu ya ‘Aksum, Ethiopia. Waorthodoksi Tewahedo, wanawakumbuka Wat. **Romano**, **Gabra Krestos** na **Yohane**, towashi. Pia wanakumbuka **kutabarukiwa Kanisa la Senhar**.[222]

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake! Amina.

## Wat. Abraha wa Aksum na Atsbeha ndugu yake,

Abraha (Aizan) alikuwa mtawala wa ufalme wa Aksum (320 – 360), kwa sasa Ethiopia Kusini, nchi za Eritrea na Yemen. Akajiita ‘Mfalme wa Saba na Salhen, Himyar na Dhu-Raydan’. Pokeo inatueleza kwamba Abraha alirihti ufalme kutoka kwa baba yake Ella Amida (Ousanas) alipokuwa bado mtoto mdogo. Mama yake Sofia akawa mtawala wa muda. Abraha alikuwa mfalme wa kwanza kubatizwa. Akamteua Frumensio, mwalimu wake binafsi wakati wa utoto wake, kuwa mkuu wa Kanisa la Ethiopia. Kaizari Konstansio II, mfuasi wa Ario, alipomwandikia barua kumwomba Frumensio aje Aleksandria ili kupima imani yake - Kaizari alitaka kumweka askofu mmoja, mfuasi wa Ario, kuwa mkuu wa Kanisa la Ethiopia - Abraha na Atsbeha walikataa kwa kutomjibu
Abraha akafanya vita mbali mbali na shindi zake ziliandikwa katika mnara wa ukumbusho. Akaenda kwa ushindi mpaka Meroe, katika ufalme wa Kushi. Alisimamisha wima minara mbalimbali mirefu yenye

[221] *Coptic Synaxarium : 17 Babah.*
[222] *The Ethiopian Rite Missal, Abba Emmanuel & Abba Brendan Cogavin, 2002, uk 179. Ethiopian Synaxarium : Tekemt 04*

pande mraba zilizochongoka juu. Akamtuma pacha wake Atsbeha (Sazan) na ndugu yake Adefa kuzima maasi Wabeja. Ndugu hawa walipata ushindi mkubwa. Wakawahamisha katika mkoa wa Maltlia, kwa sasa unaoitwa Begemder.

Sarafu nyingi zilizochimbuka zimechapwa na jina la Aizan (Abraha) pamoja na mchoro wa msalaba. Inaonekana kwamba wakati wa utawala wake Waaksum walienda hadi India kufanya biashara na nchi hiyo. Kauli mbiu yake ilikuwa: "Jambo hilo lipendeze taifa".

Majina ya Aizan na Sazan hayapo katika orodha ya Wafalme wa Aksum, bali majina Abreha na Atzbeha, ambayo ni majina ya ubatizo wao.

Wat. Abraha na Atsbeha, mtuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

## Mtumishi wa Mungu Julius Kambarage Nyerere, 1999.



Julius Kambarage Nyerere, aliyejulikana kama 'Mwalimu' na 'Baba wa Taifa', alizaliwa tarehe 13 Aprili, mwaka 1922, huko Butiama, Musoma, mkoa wa Mara Tanganyika. Baba yake alikuwa Burito Nyerere, chifu wa Wazanaki. Mama yake alikuwa Kristina Mgaya Nyang'ombe. Kambarage alikuwa mmoja wa watoto 26 wa baba yake, aliyefariki mwaka 1942, wakati Kambarage alipokuwa bado kijana na mama yake alifariki mwaka 1997, akifika umri wa miaka 100. Kwa Ki-zanaki jina la Kambarage linamaanisha 'roho iletayo mvua', kwa sababu alipozaliwa mvua kubwa ilinyesha.

Kambarage alikuwa mwanafunzi mwenye akili sana. Alianza shule na miaka 12, Mwisenge, mjini Musoma, umbali wa kms 42 kutoka nyumbani mwake. Alisoma huko miaka minne. Akapata alama za juu kabisa na alikuwa daima wa kwanza katika mitihani. Akaenda *St. Mary's School Tabora*, mwaka 1937 na kuhitimu mwaka 1942. Katika mtihani wa Kidato cha IV wa ki-taifa akapata marks kubwa kuliko watu wote.

Baada ya kumaliza shule ya Sekondari, akaenda *Makerere University*, Uganda, mwaka 1945. Akapata Diploma yake mwaka 1947 na kurudi Tanzania. Akaanza kufanya kazi katika Shule ya *St Mary's School Tabora*, akifundisha biolojia na Kiingereza, kwa muda wa miaka mitatu. Nyerere akajaliwa msaada wa kusoma Chuo kikuu cha Edinburgh, Scotland. Huko akajifunza Historia, Siasa na Uchumi. Tena kila wakati alipopata nafasi alijifunza Kigiriki na Kilatini. Mwaka 1952 alikuwa Mtanzania wa kwanza kupata *Master Degree* katika Historia na Uchumi. Aliporudi Tanzania alianza kufundisha katika Shule ya *St Francis*, Pugu, Dar es Salaam.
Mungu akaweka moyoni mwake hamu ya kugombea uhuru wa Tanganyika kwa njia za amani. Huko *Makerere University* alipenda kuzungumza na wanafunzi wenzake siasa ya kupatia uhuru. Akaanzisha *Tanganyika Welfare Association*. Chama hicho baadaye kiliungana na *Tanganyika African Association* (TAA). Mwaka 1954 akabadilisha TAA kuwa *Tanganyika African National Union* (TANU). Ndipo viongozi wa Shule Katoliki ya *St Francis* walimwomba achague kati ya kuwa Mwalimu katika shule yao au kufanya kazi ya siasa. Akachagua kazi ya siasa. Februari 1955 alikwenda UNO (*United Nations Organization*) kwa mara ya kwanza kuiombea Tanganyika uhuru. Aliambiwa kwamba itachukua miaka 25 kwa Tanganyika kujitawala. Lakini Oktoba 1956 aliporudi kuwajulisha UNO ratiba ya mpango wa uhuru, walitarajia kupata Serikali ya Madaraka mwaka 1960 baada ya uchaguzi. Tarehe ya uhuru akaitaja, 9 Desemba 1961.
Mwaka 1961 akachaguliwa kuwa Waziri Mkuu, na mwaka ufuatao 1962 akateuliwa kuwa Rais wa kwanza wa Tanganyika. Mwaka 1964 Tanganyika na Zanzibar vikaungana kuwa Tanzania. Mwaka 1965 akachaguliwa kwa mara ya pili kuwa Rais wa Tanzania na akendelea kushika nafasi hiyo hadi mwaka 1985, alipostaafu, ingawa akabaki Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi hadi kifo chake.
Alipokuwa na umri wa miaka 20 akaanza ukatekumeni katika Kanisa Katoliki. Na mwaka 1943, Desemba 23 akabatizwa na Padri Mathias Koenen na kuitwa kwa jina la Julius.
Akafunga ndoa na Maria Gabriel Magige, mwalimu wa shule ya msingi, tarehe 24 Januari, 1953. Padri William Collins akaadhimisha ibada.

Julius Kambarage Nyerere aliishi maisha yake ya ki-kristo kweli na kwa wazi. Kila siku, asubuhi, akiwa nyumbani, alihudhuria misa katika Kanisa la Mt. Petro, Dar es Salaam. Alikuwa mtu wa sala. Kabla ya kutoa hotuba muhimu, alifunga. Hakuna jambo la maana ambalo Mwalimu alilichukulia hatua bila kusali kwanza. Hapo awali viongozi wengi wa Jeshi la Wananchi walimfuata kumshauri atangaze vita dhidi ya uchokozi wa Idi Amin. Wakati wote jibu lake lilikuwa: 'Siwezi, siwezi kutangaza vita. Watu wengi watakufa'. Lakini baada ya Idi Amin kuvamia Kagera, Mwalimu alikesha usiku mzima kwenye kanisa la Mt. Petro, akisali na kumwomba Mungu amsaidie kutoa uamuzi mwema; Aibariki vita nzima na kuisimamia, ili nduli Amin ang'olewe bila kumwaga damu nchini Tanzania na bila kuangamiza maisha mengi ya watu wasio na hatia katika nchi ya Uganda. Asubuhi, baada ya Misa, akatangaza vita.

Ki-tabia hakunywa pombe na hakupendeza sana na michezo ya ki-zungu, akipendelea zaidi ngoma za Afrika. Alijitahidi kuishi Injili na kuongozwa nayo katika maisha yake yote. Kufuatana na Neno la Kristo: "*Mtu atakaye kuwa wa kwanza atakuwa mtumishi wa wote* [223] hakutumia cheo chake kijitajirisha bali kuwatumikia Watanzania wote. Aliingiza katika siasa yake mawazo ya Ujamaa na kujitegemea, ili watu waishi kwa pamoja, na kwa pamoja kukua katika heshima na uhuru na kupokea faida kutokana na kazi zao. Kama Mkristo, alichota mawazo hayo katika kitabu cha Matendo ya Mitume: "*Na jamii ya watu walioamini walikuwa na moyo mmoja na roho moja; wala hapana mmoja aliyesema ya kuwa kitu chochote alicho nacho ni mali yake mwenyewe; bali walikuwa na vitu vyote shirika*." [224]. Lakini maono yake yakakutana na upingamizi mwingi na damu ikamwagika wakati wa utekelezaji wa kuwakusanya watu katika vijiji vya Ujamaa, mwaka 1970. Uchumi uliporomoka na Tanzania ilikabili njaa kubwa. Rushwa ikaanza kuenea nchini.

Alipendelea kuitwa Mwalimu, kuliko kutumia vyeo vingine. Katika Katiba ya Serikali ya Tanzania alikazania uhuru wa dini. Mara nyingi alijitahidi kuhusiana na viongozi wa dini mbalimbali zilizokuwepo

---

[223] Mk. 9:35
[224] Mdo 4:32

katika Tanzania. Alichukua kila nafasi kuongea na Viongozi wa makanisa ya ki-kristo na kuwahimiza kutimiza wito na wajibu wao kuhusu jamii, hasa kazi ya kuziba utengano kati ya maskini na matajiri. Alinukuu maneno ya Yohane: "*Mtu akiwa na riziki ya dunia, kisha akamwona ndugu yake ni mhitaji, akamzuilia huruma zake, je, upendo wa Mungu wakaaje ndani yake huyo?*"[225]. Wote tunaitwa kukuza maendeleo ya ki-binadamu na ki-roho ya watu wote, yaani manufaa ya jamii, ili amani itawale. Amani ni kitu kinachojengwa siku baada ya siku, kwa kutafuta utaratibu uliowekwa na Mungu, katika haki ya kweli kati ya wanadamu. Alijua kwamba sababu za mapigano kati ya watu ni umaskini, tamaa ya madaraka na ukabila.
Mwalimu aliitwa ki-fimbo kwa sababu ya ile tabia yake ya kuchukua fimbo ndogo fupi mkononi mwake. Watu wengine walifikiri kwamba si fimbo ya kawaida bali ya ushirikina. Inasemekana kwamba alipewa fimbo hiyo na Baba Mtakatifu Pio XII, mwaka 1948. Baba Mtakatifu alimwuliza:"Ndiwe unayetafuta uhuru wa Watanganyika?" Akajibu: "Ndiyo, Baba." Baba Mtakatifu akamwambia: "Chukua fimbo hii ukatawale watu wangu kwa mkono wa amani." Aliporudi Tanganyika aliwaomba wachongaji wachonge fimbo nyingine na kutia hiyo fimbo ndogo fupi ndani yake.
Nyerere aliandika vitabu vingi na hotuba zake zimekusanyika katika vitabu. Vitabu vingine vinatumika katika Vyuo Vikuu kama vitabu vya kiada. Alitafsiri pia baadhi ya vitabu vya biblia katika lugha ya Kizanaki. Na mwaka 1996 aliandika mashairi na tenzi za ki-roho kufuatana Injili za Mathayo, Marko, Luka, Yohane na Matendo ya Mitume.
Siku chache kabla ya kufa kwake alisema: "Najua sitapona toka ugonjwa huu. Nasikitika kuwaacha Warundi wangu. Lakini mimi nitawaombea mbele ya Mungu". Wakati huo alikuwa anawapatanisha Warundi na Wanyarwanda. Alifariki tarehe 14, Oktoba, 1999, saa 10.30, katika hospitali ya Mt. Thomas, London, Uingereza, kwa ugonjwa wa Leukemia. Mwili wake ulipelekwa Dar es Salaam, tarehe 18 Oktoba, na kuwekwa katika Uwanja wa Taifa, ili watu wote waweze kumuaga 'Baba ya Taifa'. Akazikwa Butiama, tarehe 21 Oktoba, 1999. Tarehe

[225] 1 Yoh 3:17

13, mwezi wa 5, mwaka 2005 Jimbo Katoliki la Musoma limeanza mikakati ya kumtangaza Julius Kambarage Nyerere kuwa Mtakatifu. Mwezi wa Julai, mwaka 2013 mchakato wa kumtangaza Mwenyeheri ulianza.

Mtumishi wa Mungu Julius K. Nyerere, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

**Oktoba 15**

Huko Tunisia, Wakatoliki wanamkumbuka Mt. **Agileo**, mfiadini, Kartago, Tunisia, 300. Masalia ya Mt. Agileo yalihamishwa Roma. Mt. Augustino alihubiri wakati wa sikukuu yake.[226]
Huko Ethiopia, Wakatoliki wanamkumbuka Abuna **Gabra Manfas-Qedus**.[227]
Huko Gihiza, Burundi, Wakatoliki wanamkumbuka **Gina Simionato**, Sista wa Shirika la Mt. Dorotea, aliyeuawa mwaka 2000.

Huko Misri, Wakoptiki wanamkumbuka Mt. **Theofilo**, Patriarka, askofu wa 23 wa Aleksandria, Misri.[228]
Huko Ethiopia Waorthodoksi Tewahedo wanawakumbuka Wat. **Adrawos**, **Awaras**, **Aldrakwos**, wote wafiadini na **Endronos** (*'Adronos?*).[229]

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake! Amina.

## Mt. Theofilo, Askofu, 412

Theofilo, askofu wa 23 wa Aleksandria, Patriarka, anaheshimiwa na Wakoptiki wa Misri kama Mtakatifu. Tunasoma katika kitabu chao cha Watakatifu kwamba alikuwa mwanafunzi wa Mt. Atanasi. Alilelewa na kufundishwa mambo yote yahusuyo maisha ya ki-roho na mambo ya Kanisa.
Patriarka Timoteo I alipofariki, Theofilo aliteuliwa kushika nafasi yake, mwaka 385. Alikuwa msomi na kuelewa vizuri sana mafundisho yote ya Kanisa. Akaandika hotuba nyingi, akiwasihi Wakristo kutenda matendo ya huruma, kuwaonya kupokea komunio baada ya kujihoji na kutafakari ufufuko na hukumu ya mwisho.

---

[226] *Les Petits Bollandistes. Anakumbuka katika Afrika tarehe 25 Januari.*
[227] *The Ethiopian Rite Missal, Abba Emmanuel & Abba Brendan Cogavin, 2002, uk 179.* Rejea maisha yake tarehe 8 Aprili.
[228] *Coptic Synaxarium: 18 Babah.*
[229] *Ethiopian Synaxarium: Tekemt 05.*

Mt. Sirili alikuwa mpwa wake. Akamhakikishia kwamba atajifunza kwa usahihi kabisa, kwa hiyo alimtuma kwa Abba Serapio, katika jangwa la Shete. Huko Sirili alijifunza mambo yote kuhusu Kanisa, akibaki kule kwa muda wa miaka mitano.

Siku moja Theofilo alipokuwa pamoja na Mt. Atanasi na kutazama vilima karibu na kijumba chake, alimsikia akisema: "Nikipata nafasi, nitaondoa vilima hivyo na kujenga kanisa moja kwa heshima ya Wat. Yohane Mbatizaji na Eliya Nabii." Basi alipoteuliwa kuwa Patriarka alikumbuka maneno hayo na kuyazungumza mara nyingi. Huko Roma, mume wa mwanamke tajiri akafariki. Mke wake akaachwa na wana wawili. Akawachukua, pamoja na fedha nyingi, picha ya Malaika Mkuu Rafaeli na kufika Aleksandria. Aliposikia habari ya Askofu Theofilo na hamu ya kuondoa vilima hivyo, akampatia fedha ya kufanya kazi hiyo. Kazi ilipomalizika, hazina ikagundiliwa chini ya vilima hivyo na kufunika na jiwe lililoandikwa kwa herufi tatu za Theta kwa lugha ya kikoptiki. Abba Theofilo alipoziona, alijua siri zake, akiongozwa na Roho Mtakatifu. Akasema: "Wakati umefika wa hazina hiyo kugunduliwa kwa sababu herufi tatu hizi za theta zilikusanya pamoja kwa wakati mmoja. Thoes ni kwa ajili ya Mungu; Na Theodosio, yule Kaizari, mwana wa Arkadio, mwanawe wa Theodosio Mkuu; na Theofilo, Patriarka, yaani mimi mwenyewe." Hazina hiyo ilifukia wakati wa Aleksanda, mwana wa Filipi, Mtawala wa Makedonia, yaani miaka 700 iliyopita.

Patriarka Theofilo akamtaarifu Kaizari kuhusu hazina hiyo na akamwomba aje mwenyewe. Kaizari akaja, akaona hazina hiyo na kumpa Theofilo fedha nyingi. Kwa fedha hizo alijenga makanisa mengi. Kwanza akajenga Kanisa kwa heshima ya Wat. Yohane Mbatizaji na Eliya nabii, na kupeleka masalia yao katika Kanisa hilo. Baadaye akajenga Kanisa kwa heshima ya Bikira Maria, Kanisa kwa heshima ya Malaika Mkuu Rafaeli, huko El-Gizira na makanisa mengine saba.

Kuhusu wana wawili wa mwanamke aliyekuja kutoka Roma, akawapa daraja ya uaskofu. Kaizari alipotambua hamu ya Patriarka Theofilo kujenga makanisa, akampa hekalu zote za miungu wa uongo zisizotumika. Theofilo akazibadilisha kuwa makanisa, nyumba kwa

wageni na kuongeza eneo.[230] Mara moja Wapagani wakachochesha ghasia, wakawaua Wakristo wengi barabarani, wakawashika wengine na wakajifungia katika hekalu lao kubwa la Serapis. Ndani ya hekalu wakawalazimisha Wakristo kumtolea Serapis sadaka. Walipokataa wakauawa kwa mateso mengi, au kwa kuwasulubisha, au kwa kuvunja miguu yao na kuwatupa katika sinki na vyoo vya hekalu, pamoja na damu ya kafara zao. Kaizari akamwandikia Patriarka Theofilo kuwasamehe wauaji, lakini alimruhusu kubomoa hekalu lao.[231]

Mt. Theofilo, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

---

[230] *Coptic Synaxarium*: 18 Babah

[231] Kuhusu mashahidi wa Serapis, tazama habari zao tarehe 17 Machi.

**Oktoba 16**

Sisi Wakatoliki tunawakumbuka Wat. **Martiniano** na **Saturiano**, pamoja na **ndugu zao wawili**, na **Maksima**, wote wafiadini, Moroko.[232]
Huko Afrika ya Kaskazini, kumbukumbu ya **Mashahidi mia mbili na sabini**, waliofia dini kwa pamoja, kati yao Mt. **Serea**. Pia kumbukumbu ya **Mashahidi 365** pamoja na **Saturnino** na **Nereo**,[233] na Wat. **Mireo** na **Auside**, wafiadini.[234]
Huko Kenya, Wakatoliki wanawakumbuka Watumishi wa Mungu **Diomede Njoka**, kijana wa miaka 15 wa jimbo la Murang'a; **Praksede Wangeci** (Cecilia) na **Benedikta Njeri** (Roseta), masista wa Shirika la Moyo Mtakatifu wa Maria wa Nyeri, waliouawa na waasi MauMau, mwaka 1953.
Huko Rulenge, Tanzania, Wakatoliki wanamkumbuka **Kristofa Mwoleka**, Askofu, aliyefariki mwaka 2002.

Huko Misri, Wakoptiki wanawakumbuka Mt. **Theofilo** na **mke wake**, (**Patrisia** na mtoto wao **Damalio**) wafiadini, Fayoum, Misri.[235] Walitupwa katika shimo kubwa na kufukiwa na mchanga na mawe.
Huko Ethiopia, Wakristo wanawakumbuka Mt. Abba **Pantaleoni** (wa kijumba) na Padre **Bestalota Mika'el**, ambaye damu yake ilionekana bado uwowenu kama maji wakati walipohamisha mwili wake katika kaburi nyingine. Waorthodoksi Tewahedo, wanawakumbuka mashahidi Wat. **Rewaki** na **Antonio** ('Entona), askofu wa Bana; **Hermolao**, padre na kaka yake **Herakleto**.[236]

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake! Amina.

---

[232] *Martyrologium Romanum*, ed. 2005.
[233] *Roman Martyrology,* ed. 1956.
[234] *Les petits Bollandistes*
[235] *Coptic Synaxarium: 19 Babah*.
[236] *The Ethiopian Rite Missal, Abba Emmanuel & Abba Brendan Cogavin, 2002, uk 180. Ethiopian Synaxarium: Tekemt 06.*

## Wat. Martiniano, Saturiano na Maksima, wafiadini

Wakati wa dhiki iliyosababishwa na Waharabu (*Vandals*), Mfalme Genserik, mfuasi wa Ario, alipotawala, palikuwa watumwa wawili wa mtu mmoja wa kabila yao. Waliongoka kwa dini ya kikristo kwa juhudi ya mwanamke Maksima, mtumwa kama wao. Wakashika imani yao kwa bidii hata wakapigwa na marungu na kuraruliwa katika mwili wao mzima, hadi mifupa ikaonekana. Ingawa jambo hilo liliendelea kwa muda mrefu, majeraha yao yaliponywa kila mara usiku. Mwishoni walihamishwa katika nchi mbali na huko wakawaongoa wapagani wengi, hadi wakamwomba Baba Mt. awatume padre, na wahudumu wengine, kuwabatiza wote. Hatimaye walihukumiwa kufa, miguu yao ikifungwa nyuma ya vibandawazi na kuburutwa kati ya miiba. Maksima, baada ya kuteswa vibaya, akapona ki-mwujiza, akawekwa huru na kuchaguliwa kuwa abatisa wa monasteri kubwa ya mabikira. Kule akafariki katika amani ya Bwana.

Wat. Martiniano na wenzako, mtuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

## Abba Pantaleoni

Pantaleoni ni mmojawapo wa Watakatifu tisa wa Ethiopia.[237] Aliitwa 'Pantaleoni wa kijumba'. Alikuwa mwana wa mtu wa ukoo bora, rafiki wa Kaizari. Mama yake alipomwachisha ziwa akampeleka kwa monasteri moja. Kule akakua katika hekima na hofu ya Mungu, akifunga na kusali.

Baadaye akasafiri kwenda Ethiopia pamoja na Watakatifu tisa, wakati wa Mfalme 'Al'meda, mwana wa Sal'Adab mfalme. Wakaishi huko Bet Ktin. Baadaye wakatengana. Abba Pantaleoni akapanda kilima, akajenga kijumba cha dhiraa tano urefu kwa dhiraa mbili upana na dhiraa tatu kwenda juu. Paa yake ilikuwa jiwe moja tu. Mlango haukuwepo, bali tundu moja ndogo. Akasimama wima kwa muda wa miaka arobaini na mitano, bila kukaa wala kujilaza ili kulala. Akula na kunywa kidogo kiasi kwamba ngozi yake ikaganda na mifupa yake. Kope zake zilichakaa kwa sababu ya machozi yake. Mungu kwa mikono yake alitenda miujiza mingi, kuwaponya wagonjwa na

[237] Rejea tarehe 24 Oktoba maisha ya Watakatifu tisa wa Ethiopia.

kuwafungua vipofu macho yao. Siku moja alipanda mti wakati wa kupambazuka. Jioni mti huyu ukawa mkubwa sana. Ukakauka siku ile ile hata mfuasi wake akatengeneza mkaa kwa ajili ya chetezo yake.
Mfalme Kaleb alipoenda kupiga vita dhidi ya mfalme mwingine, akamwendea na kumwambia shida zake. Abba Pantaleoni akamwambia: ”Nenda kwa amani, kwa sababu Mungu anaweza kutenda yote. Atakupatia ushindi juu ya adui zako, na kurudi kwa usalama katika nchi yako.” Basi Mfalme Kaleb alipofika katika nchi ya Saba, akapigana vita na watu wa nchi ile na kuwateka, na hakuna aliyebaki kwa sababu wengine wote wakasambaratika kama majani ya mti. Miongoni wa wale walienda vitani walimwona Abba Pantaleoni kati yao na wakashuhudia wakisema: ”Tulimwona Abba Pantaleoni akisimama pamoja nasi katika mashindano na akawashinda adui zetu”. Mfalme Kaleb aliporudi baada ya kuwashinda adui zake, aling'akuta cheo chake cha Mfalme na kwenda kuishi pamoja na Abba Pantaleoni.
Wakati wake wa kuaga ulimwengu huu ulipotimia Bwana Yesu Kristo akamtokea Abba Pantaleoni na kufanya agano naye kwa ajili ya wale watakaomwomba kwa jina lake, wale watakaomkumbuka katika ibada na wale watakaoyaandika maisha yake. Bwana Yesu akamwambia: “Inatosha, nenda sasa kupumzika”. Na mara mifupa yake ikavunjika na akafariki kwa amani na kuzikwa katika kijumba chake.
Mt. Pantaleoni, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

**Oktoba 17**

Huko Vole, Afrika ya Kaskazini, sisi Wakatoliki tunawakumbuka **Mashahidi watakatifu Volitani; Mt Nino na wenzake**, mnamo mwaka 304.[238] Mt. Augustino aliwasifu katika hotuba yake.
Zamani huko Misri, Wakatoliki walimkumbuka Mt. **Yohane Kolobos**.[239]
Huko Kabylie, Aljeria, Wakatoliki wanamkumbuka Mtu wa Mungu **Maria-Petro Fourier** (*Marie Julien*), Sista wa Shirika la Masista Wamisionari wa Bikira Maria wa Afrika (MSOLA), aliyeuawa mwaka 1956.
Huko Uganda, Wakatoliki wanamkumbuka Mtumishi wa Mungu **Terezia Keaney**, Mama Kevin, aliyeanzisha Shirika la *Franciscan Missionary Sisters for Africa*, 1957.
Huko Rwanda, Wakatoliki wanamkumbuka **Klaudio Simard**, Padri wa Shirika la Msalaba Mtakatifu, aliyeuawa mwaka 1994.

Na huko Misri, Wakoptiki waamkumbuka, Mt. **Yohane Kolobos**, (yaani mfupi), mkaa pweke.[240]
Huko Ethiopia, Wakristu wanamkumbuka Mt. Abba **Paulo** wa Thmuis (Pawli wa mji wa Tamaw), Misri.[241]

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake! Amina.

## Abba Paulo wa Thmuis

---

[238] *Martyrologium Romanum*, ed. 2005. Kati ya Mashahidi wa Volitani pamoja na Mt. Nino: Wat. Viktori, Nobilitano (Jubilitano), Mariani, Lusio, Sitino, Kresensio, Rufiniano, Donati, Defensor, Rustisiani, Servilianus, Sokrates, Venerio, Januari, Mustoli (au Neustoli), Kwintasio, Memio, Isitano (Yzitiano), Magnilio, na wanawake Prima, Donata, Severa, Viktoria, Basilia, wote wafiadinini, Moroko. Mt. Augustino alitoa hotuba wakati wa sikukuu yao, *Sermo* 156. Pia 43 de *Verbis apostoli*.
[239] *Acta Sanctorum*. Katika Kanisa Katoliki kumbukumbu yake inaadhimisha sasa hivi tarehe 15 Septemba.
[240] *Coptic Synaxarium: 20 Babah*.
[241] *The Ethiopian Rite Missal, Abba Emmanuel & Abba Brendan Cogavin, 2002, uk 180.*

Tunasoma katika kitabu cha Watakatifu wa Ethiopia habari za ajabu kuhusu Mtakatifu huyu. Alipokuwa kijana tu aliingia utawani katika monasteri ya Debra ‘Ensena, karibu na Asna, katika mkoa wa Misri Kusini. Mfuasi wake Ezekieli akashuhudia maisha bora ya Mwalimu wake na majikanio yake.

Abba Paulo alipiga vita ya ki-roho kwa sababu alimpenda Kristo. Akajiua mara saba. Mara ya kwanza akajifunga juu ya mti, kichwa chini na miguu juu. Akabaki katika hali hiyo muda wa siku arobaini, usiku na mchana, hadi damu ikatoka puani mwake na akafariki. Mungu akamwinua kutoka wafu. Mara ya pili akajitupa katika mawimbi ya bahari, akifikiri kwamba samaki kubwa na papa atammeza. Hakuna papa aliyemgusa na akabaki majini miaka mingi hadi akafa. Bwana Yesu akamwinua kutoka wafu kwa mara ya pili. Mara ya tatu akajitupa mchangani na akafa, lakini Bwana akamwinua kutoka wafu. Mara ya nne akajitupa kutoka juu ya mlima mrefu na kujivingirisha chini. Mawe yenye ncha kali, yaliyokuwa mengi upande wa mlima, yalitoboa viungo vyote vya mwili wake. Mara akafariki. Na Ezekieli, mfuasi wake, akamlilia. Bwana Yesu Kristo akamtulia na kumfariji kwa kumwinua kutoka wafu. Mara ya tano akajitupa kutoka juu ya mti mrefu na kuanguka juu ya jiwe lenye ncha kali kama upanga. Mwili wake ukapasuka na akafa. Lakini Bwana akamwinua kutoka wafu. Mara ya sita akajiunganisha kichwa chake na miguu yake na akabaki katika hali hiyo kwa muda wa siku arobaini, usiku na mchana. Akafa. Bwana akamtuma malaika wake kumwinua na kumfariji. Kwa njia hiyo Mtakatifu huyu akajitesa mara sita na kufa mara sita na kila mara Bwana akamwinua tena kutoka wafu. Mara ya saba akanyosha miguu yake juu ya kisima na kubaki hivyo muda wa siku arobaini, usiku na mchana na akafa.

Bwana Yesu Kristo akamtokea, akamwinua kutoka wafu, akamtia nguvu na kumwambia: “Paulo, mpendwa wangu, je, hukujitaabisha ya kutosha na kujiua ya kutosha?“ Na Paulo akamjibu: “Uniache, Bwana wangu, nijitese kwa ajili ya jina lako takatifu, kama wewe ulivyojitesa kwa ajili ya wanadamu. Wewe ni Mungu, na Mwana wa Mungu, na ulikufa kwa ajili ya madhambi yetu. Sisi hatustahili kwamba wewe hujitesa kwa ajili yetu.“ Bwana akamtia nguvu na kumfariji na akapaa mbinguni.

Wakati Abba Besoi alipoenda monasteri ya Debra ‘Ensena, alikutana na Abba Paulo. Na Bwana Yesu akamtokea Paulo na kumwambia: “Mwili wako utalazwa pamoja na mwili wa Abba Besoi“. Abba Paulo alipofariki, wakalaza mwili wake karibu na mwili wa Abba Besoi, kama Bwana Yesu Kristo alivyosema. Walipotaka kuhamisha mwili wa Mt. Abba Besoi kwa monasteri ya Debra Shete, wakauchukua mwili wake na kuuweka katika meli na wakauacha mwili wa Abba Paulo. Meli ilibaki tuli na haikiweza kusogea mbele. Lakini walipouchukua mwili wa Abba Paulo na kuulaza pamoja na mwili wa Abba Besoi katika meli, mara meli ikaenda na kuwapeleka kwa Debra Shete. Hadi leo miili yote miwili imezikwa katika Kanisa la Abba Besoi.[242]
Mt. Abba Paulo, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

## Mtu wa Mungu Sista Maria Petro Fourier, msola, 1956

Maria Julien alizaliwa tarehe 7 Aprili 1907 huko Ufaransa. Baba yake aliitwa Paulo Julien na mama yake Albertina Kopf. Baada ya shule alifuata kozi ya Katibu na Uhasibu. Alipokuwa na umri wa miaka 19 alijiunga na Shirika la Masista Wamisionari wa Bikira Maria wa Afrika. Akavishwa nguo za utawa tarehe 1 Mei 1927 na kuitwa Sista Petro Fourier.[243] Akaweka nadhiri zake za kwanza, tarehe 30 Oktoba 1928, na nadhiri za daima tarehe 25 Oktoba 1931 huko Aljeria. Baada ya kuweka nadhiri zake za kwanza alifuata kozi ya nesi na kutumwa kufanya kazi katika misioni ya Bou-Nouh na katika hospitali ya Mengallet.
Sista Fourier akaishi miaka 14 katika Kabylie. Akajifunza lugha, mila, tabia za wenyeji ili awafahamu zaidi wenyeji aliowapenda sana na kujitoa kwao. Akawavutia masista wenzake kufanya hivyo. Akawa Mkuu wa kwanza wa “Nyumba ya masomo” huko Tizi-ouzou. Ilikuwa vigumu kwake kuwaacha Wakabylie na kwenda ‘Saint Charles’, mwaka 1949, kuanzisha Chuo cha maarifa ya nyumbani. Hata hivyo hakusahau Wakabylie. Mwanzoni wanafunzi wake walikuwa hasa watoto wa

---

[242] *Ethiopian Synaxarium: Tekemt 07*
[243] Pierre Fourier ni Mwenyeheri, alikuwa Paroko de Mattaincourt, Ufaransa, karne la XVI. Anakumbukwa tarehe 7 Julai. Kufuata desturi za zamani Masista walipewa jina la Mtakatifu fulani, hata jina la Mtakatifu mwanamume.

wazungu. Sista akajaribu kuwavutia kuwafahamu Waislamu, kujenga mawasiliano nao na kuwapenda. Pole pole Chuo kilianza kupokea zaidi na zaidi wenyeji.

Baadaye akahamishwa Tizi-Hibel, mkoa wa Kabylie. Akafurahi kurudi katika nchi aliyopenda na kuanza kuwahudumia maskini na walioteswa. Akaendelea kujifunza lugha na wakati huo kufundisha katika shule ya maarifa ya nyumbani.

Akaenda Ufaransa kwa likizo na akirudi akatumwa kukaa huko Ighil-Ali. Hali ya kisiasa ilianza kuchafuka. Huko Tizi-Hibel alikutana matatizo, lakini huko Ighil-Ali alijua hali ilikuwa mbaya. Tangu miezi na miezi watu hawakuenda katika shule na zahanati. Swali lake lilikuwa: “Je, tuwezeje kuwahudumia watu hawa? Nifanyeje huko milimani?” lakini alikuwa anamaliza kusema: “Kazi moja tu, nijifanye Mkabylie kati ya Wakabylie. Nilipokea neema nyingi kutoka kwa Mungu mwaka huu, najiuliza anataka nini kutoka kwangu ... Haidhuru nipo tayari.” Kweli alikuwa tayari, amekwisha kujitoa kabisa kutimiza mapenzi yake. Alipofika Ighil-Ali, tarehe 31 Agosti 1956, Sista Fourier akashangaa. Wenyeji walianza kuwatafuta masista kwa ajili ya wagonjwa, tena mara nyingi, hata wakashindwa kujibu kila ombi.

Asubuhi ya tarehe 13 Septemba masista waliitwa kwa kumhudumia mtoto mgonjwa katika kijiji cha Tazaiert. Siku ile Sista Fourier hakujisikia vizuri, lakini, kadiri ya desturi yake, akaenda pamoja na Sista Fransisko Solano. Wakaondoka saa 11 jioni. Walipofika Tazaiert mwanamume mmoja akawaomba wamfuate hadi mwisho wa kijiji ili wamhudumia mgonjwa. Wakakubali … Mara wakatekwa nyara. Wakafungwa kambini siku 34. Wakatunzwa vizuri, lakini wakateswa kutojua kesho itakuwaje. Mwenzake akionyesha hofu fulani, Sista Fourier alimwambia “Tusifikiri juu ya kesho, tuishi wakati huu. Mungu anayetujalia neema saa hadi saa, atatujalia tunachohitaji. ”

Sista Fourier akatumia muda wake kusali sana. Wakati wa kufungwa kwake kulikuwa kama wakati wa kufanya mafungo. Akashika kila nafasi kuonyesha upendo kwa wale waliokuwepo. Akashiriki mateso yao, huzuni yao na masumbufu yao. Mang’amuzi yake yalimfundisha : “Ikiwa masista wetu hawawezi kuwa wema, wapole, wanyenyekevu, wakiwahudumia Wakabylie, afadhali wabaki kwao. Ah! Ningalipenda

kumwona Mama wetu Mkuu ili kumwambia na kumwomba akazane jambo hilo”.

Kati ya mwezi wa Oktoba wakasindikizwa kurudi Ighil-Ali. Kesho yake, tarehe 16 Oktoba, msafara ukakutana na mashambulizi. Kutoka kila upande risasi zikalia. Pia ilikuwa inanyesha sana… Kwa mwenzake aliyesikitika kufariki namna hii kuliko kufa shahidi, Sista Fourier alimwambia: “Kwa macho ya Mungu, kila kitu kina bei. Maisha yetu yametolewa kwa ajili ya Wakabylie. Atafurahi kuona tukifariki hivi hivi tu.” Usiku ulipokaribia, Sista Fourier, nguvu zake zilipokwisha, akamsihi Mungu: “Bwana unijalie kufariki hapa, siwezi tena .” Ndiyo maneno ya mwisho mwenzake aliyosikia kutoka mahali alipojikinga chini ya mwamba. Sista Fourier akapigwa risasi na kufariki pale pale. Kesho yake, waasi wa F.L.N. waliposambaratika askari wakakuta maiti ya Sista Fourier kati ya waasi waliofariki. Akazikwa tarehe 19 Oktoba. Kuhusu kifo chake kaimu wa Askofu aliandika katika gazeti la jimbo: “Ndiyo njia ya kushiriki katika fumbo la msalaba, ambao kwa mara ya kwanza ulibomoa ukuta wa uadui. Ndiyo njia ya mtume: upuuzi kwa wengi, aibu na uasi kwa wengine; Mikono ilinyoka kujenga umoja na inakuta tu watu wanaokataa”.

Sista Fourier, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

**Oktoba 18**

Sisi Wakatoliki tunawakumbuka Wenyeheri **Daudi Okelo** na **Jildo Irwa**, wafiadini, Uganda.
Huko Afrika ya Kaskazini, kumbukumbu ya Wat. **Lusio** na **wenzake 8,** wafiadini, karne la III au IV[244].
Huko kisiwa cha Madeira kumbukumbu ya Mhashamu **Jane Mary Wilson**, 1916.
Huko Afrika na Ulaya, Wakatoliki wanamkumbuka Mtu wa Mungu Mama **Maria Salome**, Sista wa Shirika la Masista Wamisionari wa Bikira Maria wa Afrika (MSOLA), mwaka 1930.

Huko Misri, Wakoptiki wanamkumbuka Mt. **Freig**, kwa jina lingine Abba Roweiss, 1405.[245] Waorthodoksi wanawakumbuka Wat. **Gabrieli** na **Sirmidol** wa Misri, wafiadini, 1522.
Huko Ethiopia, Wakristo wanawakumbuka Wat. **Metra**, mzee, na **wenzake**, wote wafiadini; Wat. **Bako** (*Bacchus*), **Pelagia**, Abba **Hor**, Abba **Bula**, **Susana**, na **watoto wake**, wafiadini katika mji wa Semwah. Waorthodoksi Tewahedo, wanamkumbuka Mt. **Agato**, mwanakoriti.[246]

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake! Amina.

## Wenye heri Daudi Okelo na Jildo Irwa, 1918

Wamisionari wa Comboni waliingia Uganda mwaka 1910. Miaka sita baadaye waliwabatiza wakatekumeni wa kwanza, kati yao Daudi, mwenye miaka 16 na Jildo mwenye miaka 13. Baada ya kubatizwa wote wawili waliomba kuhudhuria shule ya Makatekista.
Walipomaliza shule Paroko wa Kitgum, Padri Gambaretto, wakawatuma huko Paimol, (paliitwa baadaye Wi-polo), mbali na Parokia ya Kitgum

[244] *Acta Sanctorum.* Pamoja na Lusio: Viktori, Dasio, Leusio, Viktoriko, Bereso, askofu, Viktrisio, Faustino, Marsiali.
[245] *Coptic Synaxarium: 21 Babah.*
[246] *The Ethiopian Rite Missal, Abba Emmanuel & Abba Brendan Cogavin, 2002, uk 181. Ethiopian Synaxarium: Tekemt 08.*

kwa kms 70. Paroko akawapa katekisimu, vijitabu vichache na rozari na akawabariki. Wanakijiji wakawapokea vizuri, wakawalisha. Na wao wakaanza kazi zao kuwatumikia watu. Wakawafundisha Neno la Mungu, chini ya mti, wote waliotaka kujifunza. Wakawatembelea wazee na wagonjwa.

Lakini amani haikudumu kwa muda mrefu. Lakidi, chifu mdogo wa Paimol, alilazimishwa kuacha uchifu wake kwa Amet, akapelekwa huko Kitgum na kuweka chini ya ulinzi. Muda si muda akaachiliwa huru. Lakidi akaenda Karamoja na huko akakutana na wafanya biashara waislamu, kutoka Somalia na Ethiopia, wenye silaha. Wakakubali kumsaidia Lakidi dhidi ya Amet.



Wakati huo maneno yakasambazwa kwamba ndio Wamisionari walioleta njaa na magonjwa, hawana budi kufukuzwa, jambo ambalo wazee wa dini ya jadi walikubali. Jumamosi, tarehe 17 mwezi wa Aprili 1918, Katekista mkuu akashambuliwa na kundi la watu waliolia: “Mnatusumbua bure ya kutosha!” Akashangaa kwa sababu hajasikia mtu yeyote aliyelalamika. Wakazidisha: “Subiri na utaona yatatokea kesho!”

Tarehe 18 mwezi wa Oktoba 1918, karibu na saa sita, magaidi wakashambulia eneo la chifu mdogo Amet. Baada ya kuchoma nyumba yake na kuwaua watu waliolala humo, wakaenda kwenye nyumba ya Makatekista. Wakamkamata kwanza Daudi na kuvuta nje. Jildo alilia kwa sauti kubwa: “Msaada!” na kumwambia Daudi usihangaike, hawakutenda kitu kibaya.

Lakini magaidi wakaanza kuvua nguo zao, ingawa watu waliokuja wakasema: “Kwa nini mnataka kuwaua Waalimu hawa? Hawakutenda kitu kibaya. Wanawafundisha watoto wetu”. Magaidi waliwachukua Makatekista nje ya eneo. Kwanza wakamtesa Daudi kwa kumchoma mkuki. Baadaye Opio alitupa mkuki katika kifua cha Jildo. Akaanguka chini, akaamka tena, mkuki ukiwa kifuani mwake. Akaanguka mara ya pili, akafa. Watu wa karibu walimsikia akanena: “Nakufa bila kumwona mama yangu”. Mwuaji wa Jildo akamkata kichwa na baada ya kuchukua

kutoka Kanisani kitabu kimoja, akakiweka usoni mwa Jildo na kulia: "Sasa soma habari unazotaka kutusomea!" Kwa sababu Makatekista walikuwa wageni sehemu hizi maiti yao hayakuzikwa. Baada ya siku chache yalivutwa kwa kamba karibu na kichuguu, lakini ajabu ya Mungu, wanyama wakali wa pori wala ndege hawakugusa maiti yao.

Baada ya mashambulizi haya magaidi wakatoweka. Lakidi akajificha katika milima ya karibu. Magaidi wakawachukua wanawake kadhaa kama watumwa na baada ya kuahidi kurudi tena wakaondoka kwenda Karamoja. Kutoka Gulu, kapteni Wagstuff, mkuu wa wilaya, akafika na watu wake. Pamoja na polisi wa sehemu hizo wakazingira milima Lakidi na watu wake walipokaa. Mashambulizi yakadumu siku themanini. Mwishowe Lakidi na watu wake wakasalimu amri. Chifu wanne walihukumiwa kunyongwa, magaidi wengine walifungwa na baada ya muda kuachiliwa.

Kabla ya kufa Lakidi akaomba kubatizwa. Akamwambia Padri: "Sina neno dhidi ya Wakristo, bali dhidi ya serikali". Mwaka 1926 Monsignore Antoni Vignato, Prefekti wa kitume wa Gulu, akaenda kuchukua masalia ya Makatekista wawili na kuyazika katika Kanisa la Kitgum.[247] Wakatangazwa kuwa wenye heri tarehe 20 Oktoba 2002.

Wenye heri Daudi na Jildo, mtuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

## Mtu wa Mungu Mama Maria Salome, 1930

Maria-Renata Roudaut alizaliwa Ufaranza, tarehe 3 Machi 1847. Alikuwa mtoto wa sita wa Renato Roudaut, baba yake na Yohana Lessec, mama yake. Watoto wawili walizaliwa baadaye. Akalelewa katika familia ya ki-kristo, wazazi wakiwafundisha watoto wao, busara, ujasiri na imani. Alipokuwa na umri wa miaka kumi, huko shule kwa Mabinti wa Roho Mtakatifu, Maria-Renata akajitayarisha kupokea komunio kwa mara ya kwanza. Kesho yake akamwambia Katekista wake kwamba alipopokea sakramenti alimwomba Mungu neema ya: "Kuwa mtakatifu kwa kutenda mambo yote Mungu ataniomba".

---

[247] Rejea kitabu cha Mapadri Neno Contran na Louis Kalonji, *African Lay Martyrs, that their lives be told*, ed. New People Media Centre, Makuyu, Oct. 2009, uk.116-119

Baba yake alipofariki, akaacha shule na kuanza kumsaidia mama yake katika kazi ya shamba. Akajisikia kwamba Mungu anamwita kuwa sista. Kwa hiyo akarudi shuleni kwa Mabinti wa Roho Mtakatifu kutambua mwito wake. Akachaguliwa kuingia katika novisiati ya Shirika lao. Lakini akakataa. Baadaye akakubali tarehe fulani kujiunga nao. Alipojitayarisha kwa safari yake, akaanguka kutoka mkokoteni na kujiumiza. Akachukua tukio hilo kama ishara kwamba Mungu alimtaka mahali pengine.

Mwaka 1869, mlipuko wa kipindupindu na njaa vilienea kati ya wakazi wa mji Aljeria. Mhashamu Karolo Lavigerie, askofu wa Aljeria, akamtuma Padri Le Mauff kuwatafuta akina mama kuwasaidia watoto yatima. Akaanza kufikiri kuanzisha Shirika la Masista watakaosaidia kueneza Injili, sambamba na Shirika la Wamisionari wa Afrika (*White Fathers*) aliyeanzisha mwaka mmoja kabla. Akafikiri Shirika la Masista watakaolima na kuwatunza wagonjwa chini ya Somo wa Mhashamu Hieronimo (au Geronimo)[248]. Tarehe 9 Septemba 1869 Padri Le Mauff akarudi pamoja na wasichana wanane. Wanne wakaendelea na kuwa nguzo za Shirika mpya. Mmojawapo alikuwa binamu wa Maria Renata, lakini alirudi kwa sababu ya afya yake. Maria-Renata alipokutana na kuongeana naye aliamuru kushika nafasi yake. Akaingia katika nyumba ya majiundo Ufaransa, na miezi kadhaa baadaye alitumwa mji Aljeria kuendelea malezi yake. Masista vijana waliwatunza watoto yatima 300 na kulima ekari 400, wakipanda mizabibu.

Katika novisiati Maria-Renata akaitwa Sista Maria-Salome. Malezi yalikuwa na changamoto zake, hata wakati fulani Sista Maria-Salome alitaka kuacha. Lakini akabaki na kusema baadaye: “Bila malezi tuliyopokea, hatungeweza kukabili mambo ya mbele”. Akaweka nadhiri zake za kwanza tarehe 6 Julai 1873 na pia kuweka nadhiri ya binafsi: “Naahidi kufanya kazi kwa mikono yangu, kadiri ya nguvu zangu, ili kuendeleza kazi ya upendo ya masista na kwa ajili ya manufaa ya ki-roho ya Waafrika”. Kwa miaka kadhaa akawahudumia watu katika misioni mbalimbali. Mwaka 1880 Mhashamu Karolo Lavigerie akamchagua kuwa mama mkubwa wa jumuiya ya masista huko Les Attafs, misioni yenye hospitali kubwa na vijiji viwili vya familia za

---

[248] Rejea maisha yake tarehe 18 Septemba

yatima, kijiji cha Mt. Sipriano na kijiji cha Mt. Ana. Akaitwa Mama Maria Salome.
Mhashamu Lavigerie alipotambua ujasiri na tabia nzuri yake, akamkabidhi uongozi wa Shirika. Kwanza akawa mkuu wa manovisi. Ili kuwaunganisha katika roho moja manovisi kutoka nchi mbalimbali, aliwaambia mara nyingi: "Pendaneni". Tena akadai utii kamili. Hata Karolo Kardinali Lavigerie aliwaambia manovisi: "Mwaminini mama yenu, yeye ni mtu asijifanya, ni mtakatifu."
Wakati wa mkutano mkuu wa kwanza, mwaka 1882, Mama Maria Salome akachaguliwa kwa kura zote kuwa mama mkuu wa Shirika. Alikuwa na umri wa miaka 35 tu. Alipopata habari alitetemeka. Baadaye aliandika: "Nilijitupa miguuni mwa mama mwema Bikira Maria, katika kanisa lake (Kanisa la Bikira Maria wa Afrika). Nilimwambia kwamba yeye ndiye mkuu wa shirika hili ndogo, mimi sina karama ya pekee kuwaongoza masista hawa, lazima afanye kila kitu, kama sivyo shirika litasambaratika." Kwa kweli Mwadhama Karolo Kardinali Lavigerie, mara nyingi, alikuwa tayari kulifuta shirika. Mwaka 1885 alikuwa ametayarisha amri ya utume kuvunja shirika, baada ya mwaka mmoja. Mama Maria Salome, baada ya kujadiliana na masista wa bunge lake na chapleni akathubutu kuipinga amri hiyo, alipokutana na Kardinali tarehe 16 Aprili 1885. Kardinali hakubadilisha nia yake, bali alimkataza kupokea komunio kwa mwezi mzima. Masista wakamwendea Bikira Maria katika kanisa lake na kuahidi kuweka sanamu ya Bikira Maria mbele ya Makao Makuu ya Shirika kama ataliokoa shirika lake. Wakati ule Mama Maria Salome na bunge lake wakamwandikia Kardinali ripoti kuhusu karama ya pekee ya shirika: kuwa wamisionari, karibu na watu na kujifunza lugha ili waweze kuwapenda zaidi Waafrika. Wakashinda. Kardinali akafuta amri yake.
Ingawa kulikuwa matumaini mapya kwa Shirika Mama Maria Salome aliwaza kustaafu na kuishi kama mkaa pweke kutubu kwa ajili ya dhambi zake na kuliombea Shirika. Kardinali akamwambia: "Wewe umenilazimisha kuendelea na shirika hili na sasa unataka kuniambia unaondoka. Nakukataza kuwaza daima jambo kama hilo kwa sababu linapinga wajibu na heshima yako". Kabla ya kufa kwake, tarehe 26 Novemba, 1892, Kardinali akambariki Mama Maria Salome kwa niaba

ya shirika akisema: “Shirika listawi, lipokee miito mingi, likue katika utakatifu”.

Mama Maria Salome alichaguliwa mara nyingi kuwa tena Mama Mkuu wa Shirika hadi mwaka 1925, ingawa aliona daima kazi yake kama mzigo mkubwa. Mara moja alimwandikia Taassisi Roma kutokubali uchaguzi huo. Walikataa, wakijibu kwamba hawana nia kuweka mipaka katika uhuru wa masista wanaojua nani kumchagua. Shirika likastawi. Kwa miaka 50 likaotesha mizizi katika Aljeria na Tunisia, na baadaye vikundi vya masista wakaenda Tanzania, Kongo, Uganda, Zambia, Burundi, Kenya, Rwanda na Malawi. Pia masista wakaanzisha nyumba huko Afrika Magharibi: Mali, Burkina Faso na Ghana. Mwaka 1893 Sheria za Shirika zikakubaliwa na Roma. Maneno ya mwisho wa Kardinali kwa Mama Maria Salome yalikuwa: ”Usiogope kwa Shirika lako, litastawi:”

Mama Maria Salome alikuwa umri wa miaka 78 alipoondolewa kazi ya kuwa Mama Mkuu wa Shirika. Alizoea kuwaambia masista wenzake: “Umwombee sista mzee ambao moyo peke yake tu hauzeeki”. Aliwaambia tena kwamba huko mbinguni atawaombea ili wawe masista wamisionari watakatifu, na kulinda roho ya Baba na Mwanzilishi wetu mpendwa. Hadi kifo chake akamheshimu sana Kardinali Karolo Lavigerie, ambaye kwa mikono yake, alijitoa kwa Mungu kutimiza mapenzi yake. Akafariki tarehe 18 Oktoba 1930, akiwa na umri wa miaka 83.

Siri ya maisha yake ilikuwa kutafuta daima kutimiza mapenzi ya Mungu. Tangu siku ile ya Komunio yake ya kwanza. Baadaye alipokuwa sista aliandika: “Mama yangu Maria unisaidie kufuata mfano wako kwa kujibu: “Mimi ndimi mtumishi wa Mungu”. Alitaka kuwa mtakatifu kwa kutenda yote Kardinali alivyotaka na kuwaka na roho yake. Alikuwa na uhakika kwamba mapenzi ya Mungu yalikuwa mapenzi ya Mwanzilishi wa shirika la *White Sisters*.

Mtu wa Mungu Mama Maria Salome, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

**Oktoba 19**

Huko Misri, Wakatoliki wanawakumbuka Mt. **Vari**, askari na mfiadini,[249] na **wenzake sita** na Mt. **Kleopatra**, 307.
Huko Afrika, Wakristo wanamkumbuka Mt. **Eumenio**, Askofu wa Saba wa Aleksandria, mwaka 143[250].
Huko Bururi, Burundi, Wakatoliki wanamkumbuka **Gerardo Nzeyimana**, Padri wa jimbo, aliyeuawa mwkaa 2004.

Huko Ethiopia, Wakristu wanamkumbuka **Daudi**, Mfalme wa Ethiopia. Waorhtodoksi wanakumbuka kupatwa jua mwaka 1269, kuanzia saa 8.30 hadi saa 9.30.[251]

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake! Amina.

## Mt. Vari, 307.



Wakati wa utawala wa Kaizari Maksimiani, Vari, kutoka mji Setnuf, Misri, alikuwa askari wa Jeshi la Warumi huko Misri. Alimtumikia Mungu Baba wa Yesu Kristo kwa siri, kwa sababu ya hofu, lakini baadaye alijidhihirisha wazi kuwa Mkristo. Maksimiani akaanza kuwadhuru Wakristo na kuamua kwamba, katika kila mkoa wa Dola ya Warumi, kila Mkristo asiyeitolea sadaka miungu wa uongo, auawe. Damu ya Wakristo ikamwagika bila huruma, wengi wakateswa vibaya na kufungwa gerezani. Vari, alikuwa anawatembelea usiku, akiingia gerezani kwa kuwapa fedha nyingi walinzi. Akawahudumia watakatifu kwa kufunga vidonda

[249] *Roman Martyrology,* ed. 2005
[250] *Acta Sanctorum.* Wakoptiki wanamkumbuka tarehe 6 Septemba.
[251] *The Ethiopian Rite Missal, Abba Emmanuel & Abba Brendan Cogavin, 2002, uk 181. Ethiopian Synaxariulm: Tekemt 09.*

vyao, kuosha damu yao, kuwaletea chakula na kuwasihi wamwombee ili Kristo amhurumie.

Ikatokea kwamba kulikuwa Wakristo saba, wakaa jangwani, walioletwa mbele ya Gavana wa Misri. Alipowauliza akatambua kwamba ni Wakristo, basi akaamua wapigwe mijeledi na kuwatupa gerezani. Vari aliposikia hayo akaharakisha usiku kuwahudumia. Akawaletea chakula na kuwasihi kula, kwa sababu kwa siku saba hawakula chakula. Akaanguka miguuni mwao, kuwabusu na kuwasifu akisema: "Heri ninyi watumishi waaminifu wa Bwana! Mtaingia katika furaha ya Bwana kwa sababu mlishinda hata kumwaga damu. Heri ninyi, askari hodari, kwa sababu mkono wa Mungu Mkuu ametayarisha taji yenu huko mbinguni! '*Mlipiga mbio kwa saburi katika yale mashindano yaliyowekwa mbele yenu!*'[252]. Najua kwa hakika kwamba mateso yenu yatafika mwisho. Heri ninyi mliobarikiwa na Mungu, ufalme wa Mungu ni wenu kwa sababu mliteswa pamoja na Kristo. Kama Mtume anavyosema: '*Tukiteswa pamoja naye tutatukuzwa pamoja naye*'[253]. Nawasihi uniombee, Kristo anihurumie, kwa sababu nataka kuteswa kwa ajili yake lakini sina nguvu kufanya hivyo. Naogopa mateso makali ninayoona mmeteswa."

Watakatifu walimjibu: "Mpendwa, hakuna mtu mwenye hofu anayeweza kufika katika ukamilifu, wala asiyepanda hawezi kuvuna. Vivyo hivyo mtu asiyetaka kuteswa kwa Kristo hawezi kupokea taji. Kumbuka maneno ya Injili: '*Mtu yeyote atakayenikana mbele ya watu, nami nitamkana mbele za Baba yangu aliye mbinguni*'[254]. Ukiogopa mateso, hutaepa mateso ya milele. Ukiogopa kumkiri Kristo hapa duniani, hutamwona katika utukufu wake. Kwa hiyo ndugu mpenda, kanyaga njia ya ushahidi, njia inayokuongoza kwa Bwana anayetutunza katika mateso yetu. Tesa pamoja nasi, kwa sababu hutapata nafasi nyingine."

Vari aliposikia maneno hayo, moyo wake ukawaka moto kwa upendo wa Mungu na akatamani kuteswa kwa ajili ya Yesu Kristo. Akakesha pamoja na watakatifu usiku kucha, akisali pamoja nao na kusikia kwa furaha mafundisho yao.

---

[252] Ebr 12:1
[253] Rum 8:17
[254] Mt 10:33

Asubuhi, Gavana akawaita wafungwa kufika mbele ya Baraza. Watumishi wake walipoingia wakamkuta Vari akikaa pamoja nao. Wakashangaa na kumwuliza: “Unafanya nini hapa, Vari? Je, umepotea akili kwa kusadiki hadithi za watu wabaya hao? Je, humwogopi kwamba mtu mmoja atapeleka habari hiyo kwa Gavana? Utapotea cheo chake katika jeshi pamoja na maisha yako.

Vari akawajibu: “Atakayemwambia Gavana, atakuwa mfadhili wangu. Mjue kwamba nipo tayari kufa kwa ajili ya Kristo pamoja na hawa waliomo humo.” Wakanyamaza. Wakachukua mashahidi sita na kumwacha wa saba kwa sababu alidhoofika sana na kufariki. Watakatifu wakafika mbele ya Gavana, wakapigwa vibaya sana ili wakubali kuitolea miungu wa uongo sadaka. Mateso hayo yakazidisha mateso ya zamani, lakini wakateswa kwa saburi na kusema: “Tu Wakristo”.

Gavana akauliza: “Je, hawakuwa saba? Hapa wapo sita. Wa saba yupo wapi?” Mara Vari akaingia na kusema: “Mimi ni wa saba. Yule unayemtaja amemaliza mwendo wake na sasa yupo pamoja na Kristo. Akaniacha kutimiza mateso uliyotayarisha kwa ajili yake.” Gavana aliposikia hayo aliwauliza watumishi wake: “Huyu ni nani ?” Wakamjibu: “Huyu ndiye Vari, akida wa jeshi la Tyanis.” Gavana akamwambia Vari: “Pepo gani amekushauri kuacha cheo chako katika jeshi na sifa zote zilizokungoja?” Vari akamjibu: “Sitafuti cheo wala sifa, lakini kuteswa kwa ajili ya Kristo ndiyo sifa kuliko zote.”

Gavana akakasirika. Akaamuru Vari afungwe juu ya mti kichwa chini ili aweze kumtesa. Walipoanza kumtesa Vari, akawaambia mashahidi sita: “Mnibariki, mimi mtumishi wenu, ili niweze kushiriki bahati yenu. Msihi Bwana Kristo kwa ajili yangu ili anijalie uvumilivu, kwa sababu anajua kwamba mimi ni mdhaifu. ‘*Roho i radhi, lakini mwili ni dhaifu’*[255]. Watakatifu wakapaza sauti na kumwambia: “Jipe moyo, Vari, roho yake iimarishwe kwa sababu Kristo anasimama mbele yako na kukuimarisha!” Vari akawajibu: “Kweli najisikia msaada wa Kristo wangu, kwa sababu mateso haya yanaonekana kama si kitu kwangu”.

Wakachana ubavu wake kwa kucha za chuma. Wakachuna ngozi ya mgongo wake, wakakata nyama yake kwa wembe, na kumcharaza kwa

[255] Mt. 26:41

michapo hadi matumbo yakatoka nje na kuanguka chini. Watakatifu walipoona matumbo yake chini wakaanza kulia. Gavana akawaona wakilia akawaambia: “Lo, mmeshindwa! Mnalia kwa sababu mnaogopa mateso! Kwa nini kuendelea kumkiri Kristo asiyeweza kuwaokoa kutoka katika mikono yangu. Mwacheni na anzeni kuiabudu miungu yetu”. Wakamjibu: “Wewe ni mnyama na siyo mtu! Sisi hatujashindwa bali tunakiri uwezo wa Yesu, anayetuimarisha. Hatulii kwa sababu ya hofu, bali kwa sababu tunampenda ndugu yetu, unayetaka kumwua ki-nyama. Kiroho tunafurahi kwa ajili yake, kwa sababu taji imetayarishwa mbinguni.” Gavana akaamuru watakatifu warudishwe gerezani.

Vari akavumilia mateso muda wa masaa matano. Ndipo akamkabidhi roho yake mikononi mwa Yesu Kristo. Wakatupa mwili wake nje ya mji mahali ambapo mbwa wanakuja kujishibisha na nyama za wanyama.

Katika mji ule aliishi mjane Mkristo, Kleopatra, mzaliwa wa Palestina. Usiku ule alienda, pamoja na watumishi wake kuchukua mwili wa Mtakatifu, akautunza nyumbani mwake. Baada ya muda Kleopatra alichukua mwili wa Vari, kutoka Misri na kumpeleka Palestina. Akajenga kanisa nzuri kwa heshima ya shahidi huyu na kumzika mle. Akaweka kaburi lake katika kanisa lile na akazikwa pamoja na mwana wake Yohane.[256]

Mt. Vari, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina

[256] Rejea *the Slavonic Menologion of St. Demetrius of Rostov*

**Oktoba 20**

Huko Antiokia na Misri, Wakatoliki wanamkumbuka Mt. **Artemio**, jemadari wa jeshi, mfiadini, Misri.[257]
Huko Ethiopia, Wakatoliki wanamkumbuka **Eumenio**, Askofu wa 7 wa Aleksandria.[258]

Wakoptiki wanamkumbuka Mt. **Yosefu I** (*Yousab I*), Patriarka, askofu wa 52 wa Aleksandria, 841.[259]

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake! Amina.

## Mt. Artemio, mfiadini, 362




Kaizari hakutaka kumkabidhi utawala wa nchi ya Misri, nchi ya chakula tele kwa ajili ya Roma, kwa Seneta mmoja, kama mikoa mingine wa dola la Roma, akaamua kuikabidhi kwa Shujaa mmoja (*knight*), kwa cheo cha *Augusta*, yaani Gavana. Utawala wa Misri ulikabidhiwa kwa Jemadari aliyechukua cheo cha Jemadari wa Misri. Artemio alikuwa Jemadari wa Misri wakati wa Kaizari Konstansio.
Akishika nafasi hiyo Artemio alimsaidia Mt. Atanasi mara nyingi kuepuka kukamatwa. Ingawa alimtii Kaizari, hata wakati Kaizari alikana ukristo, na wakati wa wafuasi wa Ario walikuwa na nguvu, Artemio alibaki kuwa Mkristo hodari. Neema za Mungu zilimlinda asianguke katika mitego ya Adui. Wapagani walimshtaki kwamba alibomoa hekalu zao na kuvunja sanamu zao, kwa hiyo Kaizari Juliani Mpagani akaamuru afike mbele yake huko Antiokia, mwaka 360. Akashtakiwa rasmi na Kaizari Juliani

[257] *Acta Sanctorum*
[258] *The Ethiopian Rite Missal, Abba Emmanuel & Abba Brendan Cogavin, 2002, uk 182.*
[259] *Coptic Synaxarium: 23 Babah.*

akaamuru akatwe kichwa katika mji wa Antiokia, mwezi wa Juni, mwaka 362.[260]
Mt. Artemio, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

## Mt. Yosefu I, Askofu wa 52 wa Aleksandria, 849.

Yousab na familia yake walikuwa wenyeji wa mji Manouf. Familia yake ilikuwa tajari sana. Wazazi wake walipofariki, yatima Yousab akalelewa na mtu mtauwa. Alipokuwa kijana, akaenda kuchukua mali yake. Akawagawia wahitaji sehemu kubwa na akaenda jangwani kuishi kama mtawa chini ya uongozi wa mzee. Abba Marko alipoteuliwa kuwa Patriarka wa Aleksandria, mwaka 799, akasikia habari zake, jinsi alivyoishi ki-takatifu. Akamwita akae karibu naye. Yousab akafika kwake, akakaa kwa muda katika kijumba chake na akamwomba Patriarka kurudi jangwani. Patriarka akampadirisha na kumtuma akae jangwani. Akakaa kule miaka mingi hadi kifo cha Patriarka Abba Simeoni. Kiti cha Mt. Marko kikabaki tupu kwa miaka.
Maaskofu wakamwomba Mungu kwa bidii. Mungu akawakumbusha mtawa huyu aliyekuwa amekaa na Patriarka Marko kwa muda. Wakakumbuka jinsi alivyoishi ki-takatifu na jinsi alivyoongoza shughuli za Kanisa. Wakatuma maaskofu kadhaa kumtafuta na kumleta Aleksandria. Kabla ya kwenda wakamwomba Mungu awaonyeshe kwa hakika ikiwa huyu ndiye aliyemchagua kuwa Patriarka. Kwa dalili waliomba wakute mlango wazi wa kijumba chake watakapofika kwake. Walipofika wakakuta mlango wazi. Alikuwa amewaaga watawa wengine na alijitayarisha kufunga mlango na kuondoka. Alipowaona akawakaribisha kwa furaha na kuwaingiza katika kijumba chake. Walipokuwa ndani wakamshika na kumfunga kwa kamba, wakisema: “Anastahili!“ Alipiga kelele, akalia kwa sauti kuu na kuanza kuwaambia makosa yake na madhaifu yake, lakini bure, hawakumsikiliza. Wakamshika na kumpeleka hadi Aleksandria. Wakamwekea mikono na kumtawaza awe Patriarka wa Aleksandria.
Yosefu akayasimamia makanisa kwa busara sana. Kutokana na faida ya monasteri zake, alikuwa ananunua mashamba na kuyaweka mahali fulani ili kuzalisha mali kwa ajili ya makanisa. Aliwafundisha mara

[260] Rejea *Theodoret, Hist. Eccles*. 1. 3, c. 18

nyingi waamini bila kusahau mtu. Shetani akamchukia na kumhuzunisha sana. Hakuogopa kuwakemea wachungaji wawili, akiwaomba kuwachunga kwa upole kondoo zao. Hawakumsikia, basi akawaacha. Waamini walimwendea kumwomba msaada, walisema: “Kama unawaweka kuwa maaskofu juu yetu, basi tutabadilisha dini.“ Akatumia nguvu zake nyingi ili wakae katika amani, bila kufaulu. Akawakusanya maaskofu wote wa nchi na kuwaambia kwamba wahukumiwe. Maaskofu wote wakawatenga na Kanisa. Mara walipotengwa wakamwendea Pasha wa Kairo na kumshtaki Patriarka kwa uongo na hila. Pasha akatuma ndugu yake pamoja na askari ili wampige na kumletea. Ndugu wa Pasha alipofika, akaamuru aletwe. Akashika sime yake na kutaka kumwua. Alipompiga Mungu akauzuia mkono wake, akapiga nguzo na sime yake ikapasuka. Akakasirika. Akachukua kisu chake na kwa nguvu zake zote akampiga Patriarka ubavuni. Nguo zake zikakatwa, hata mkanda wake, lakini kisu hakigusa mwili wake. Ndipo Ndugu wa Pasha akatambua kwamba neema ya Mungu ilikuwa pamoja na Patriarka. Akaacha kutafuta kumwua, akaanza kumheshimu. Akamleta kwa Pasha na kumweleza yote yaliyotokea. Pasha akamheshimu na kumwogopa. Akamweleza mashtaki yaliyofikia. Patriarka akamtaarifu kwamba maaskofu hawa wawili walitengwa na Kanisa na yote aliyoambiwa ni uongo. Pasha akaandika amri kwamba mtu yeyote asimpinge Patriarka katika uamuzi wake na kazi yake, wala katika matendo yake.

Mnamo mwaka 829, Wakoptiki wa delta ya mto Nile wakauasi utawala wa Waislamu kwa sababu ya kodi kubwa na kudhulumiwa. Uasi ukaenea hadi Misri Kusini. Mwaka 831 Khalifa Al-Ma’mun akamwomba Patriarka kuwatuliza waasi na kuwatii utawala wa Waislamu. Wote walimsikia Patriarka isipokuwa kabila la Bashmuriani walioishi upande wa kaskazini mwa delta. Wakakataa shauri lake. Mwishoni Al-Ma’mun akaleta jeshi kubwa na tembo kutoka Uturuki ili kuwatiisha Wabashumuriani. Bila msaada wa Wakoptiki wa Misri Kusini uasi ukashindwa. Wengi wakauawa na nchi ikaachwa tupu. Walionusurika kifo wakahamishwa kwa nguvu katika nchi ya Siria.

Patriarka alikuwa mwenye raghba kuwakemea wenyedhambi na wazushi. Aliwaimarisha waamini wake katika imani ya kweli. Aliwaeleza sehemu ngumu za Maandiko Matakatifu na kuwalinda kwa

sala zake. Mungu alifanya miujiza mingi kwa mikono yake. Akafariki kwa amani, akiwa umri wa miaka 82, baada ya kutawala Kanisa la Aleksandria kwa miaka 19, na kukaa miaka 39 kama mtawa jangwani. Mt. Yosefu, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

**Oktoba 21**

Huko Misri, Wakatoliki na Wakoptiki kwa pamoja wanamkumbuka Mt. **Hilarion**, mwanakoriti.[261]
Huko Afrika ya Kaskazini, Wakatoliki wanawakumbuka Wat. **Modesto, Eutikio, Mauro** (au **Materio), Diseo**, wafiadini. Pia kumbukumbu ya Wat. **Naseo**, **Rogato**, **Malenti** na **Maksimo**, wafiadini huko Renault, Aljeria, 329.[262]
Huko Sudan, Wakatoliki wanamkumbuka Mtumishi wa Mungu Mama **Teresa Grigolini Cocorempas**, Sista wa Shirika la Masista wa Comboni, aliyefariki mwaka 1931.[263] Pia huko Wau, Sudan ya Kusini, wanawakumbuka **Selina Utu** na **Kristina**, waliouawa wakivuna kalanga shambani mwao, mwaka 2002.[264]
Huko Msumbiji, Wakatoliki wanamkumbuka **Mutuali Raoul dos Santos**, mlei, aliyeuawa mwaka 1991.

Huko Misri, Wakoptiki wanawakumbuka pia Wat. **Paulo**, **Longino** na **Zaina**, wafiadini.[265]
Waorthodoksi wa Magharibi wanamkumbu Mt. **Hilarion**, 371.
Huko Ethiopia, Waorthodoksi Tewahedo, wanawakumbuka Wat. **Arkelao**, mfiadini, **Elisa**, abate, **Pakomi** na **Minasio**, mfiadini na mama yake **Urania**.[266]

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake! Amina.

# St. Hilarion, mwanakoriti, 371

---

[261] *Roman Martyrology, ed. 1956 na Coptic Synaxarium: 24 Babah.*
[262] *Les petits Bollandistes*. Majina yao yameandikwa katika martirolojia ya Mt. Hieronimo.
[263] Rejea *Servans of the Gospel, witnesses in the footsteps of Saint Daniele Comboni in Sudan and South Sudan*, Paulines Publications Africa, 2014, uk.40-45.
[264] Rejea Fr. Neno Contra,, Louis Kalonji, *African Lay Martyrs*, New People Media Centre, 2009, uk. 48;183-185.
[265] Majina yao yameandikwa katika Ethiopian Synaxarium kwa tarehe 3 Novemba.
[266] *Ethiopian Synaxarium: Tekemt 11.*



Hilarion siyo mzaliwa wa Afrika, lakini aliishi Misri na Libya miaka kadhaa. Tunayo habari kuhusu Mtakatifu huyu kwa sababu Mt. Sofronio aliyeishi Palestina ameandika maisha yake, kama Mt. Hieronimo anavyotuambia.[267] Hilarion alizaliwa katika mji mdogo Tabatha, maili tano kusini ya Gaza, Palestina. Wazazi wake walikuwa wapagani. Akiwa bado mdogo akatumwa nao huko Aleksandria kujifunza sarufi. Alionyesha kwamba ana akili na tabia nzuri. Kwa hiyo alipendwa na wote waliomfahamu. Huko Aleksandria akafuata mafundisho ya ki-kristo na kubatizwa na Patriarka Aleksanda (*Alexandros*). Akazaliwa upya, ndiyo mara akaacha fahari za ulimwengu, michezo ya sarakasi na tamthilia, na kufurahia ibada kanisani.

Kwa muda akakaa pamoja na Patriarka Aleksanda, baadaye aliposikia habari za Mt. Antoni, sifa zake zilizoenea nchi kote, akaenda kwake. Akaguswa na fadhila zake. Akakaa naye muda wa miezi miwili, akichunguza njia zake za kuishi, bidii yake ya kusali, unyenyekevu wa kuwapokea ndugu, ukali wake wa kuwashutumu, moyo wa kuwasihi na saburi yake katika kushikilia maadili. Lakini aliposhindwa kuvumilia umati wa watu waliomfikia Mt. Antoni, ili kuponywa au kufunguliwa na nguvu za Giza, na akitamani kumtumikia Mungu kama Mt. Antoni katika upweke kamili, akarudi Palestina, pamoja na watawa wengine.

Alipofika katika nchi yake, mwaka 307 alikuta baba na mama yake wamefariki. Basi akawagawia ndugu zake na maskini mali yake yote. Hakubakizwa cho chote. Alikuwa na umri wa miaka kumi na mitano tu. Akaenda jangwani, maili saba kutoka Majuma, kuelekea Misri, kati ya pwani upande mmoja na mbuga yenye kinamasi upande mwingine. Rafiki zake walimwonya kwa kumwambia kwamba mahali pale ni mahali pa hatari, mahali pa wizi na uuaji. Lakini yeye akawajibu kwamba haogopi kitu isipokuwa kifo cha milele. Kila mtu alishangaa

[267] Mt. Hieronimo, Illustre men and women, sura 135

kuhusu bidii yake na namna zake za kuishi. Mwanzoni mwa kukaa kule, wezi walimfikia na kumwambia: “Utafanya nini ikiwa wezi na wauaji wanakufikia?” Akawajibu: “Maskini na wale wenye uchi hawaogopi wezi”. Lakini walizidi kusema: “Wanaweza kukuua”. Akawajibu: “Ndiyo ni kweli. Na hata hiyo siwaogopi, kwa sababu ninajitayarisha kufa wakati wowote.”

Bidii na ujasiri wa kijana huyu vikashangaza wote waliomfahamu. Afya yake haikuwa nzuri, joto na baridi vilimsumbua sana. Hata hivyo nguo zake zilikuwa kipande cha gunia, koti zawadi wa Mt. Antoni na joho fupi. Alipoishi katika upweke wake alikuwa na uhuru kujikania kweli kweli. Akakata nywele zake mara moja kwa mwaka. Hakubadilisha nguo mpaka imechakaa kabisa. Hakufua kipande cha gunia hata mara moja akisema: “Ni kazi bure kutafuta usafi katika shati ya singa”.

Kwa miaka ya kwanza chakula chake kilikuwa matini makavu kumi na tano aliyokula baada ya machweo wa jua. Baadaye, kwa miaka sita, aliishi kwa mkate kavu, chumvi na maji. Alipokuwa na umri wa miaka ishirini na saba hadi miaka thelathini na moja alijilisha na majani na mizizi. Kuanzia umri wa miaka thelathini na moja na kuendelea alichukua wakia chache za mkate wa shairi na majani kidogo. Hata katika uzee wake aliendelea kuzidisha kufunga. Kweli alitimiza usemi: “Ili kula kwa muda mrefu, kula kidogo kila siku”.

Aliposhawishiwa na tamaa za mwili alikuwa anajiambia: “Nakuamuru, wewe punda mdogo, usipige teke. Nitakulisha na majani kuliko mahindi; na nitakuvisha mizigo mizito na kukuchosha, ili ufikiri kula kidogo kuliko kutafuta raha.” Baada ya kusema hiyo, alitenga sehemu ya mlo wake na kufunga siku tatu hadi nne mfululizo. Akififia, alikula matini chache na juisi kutoka majani. Na wakati ule alikuwa anasali na kuimba, akilima nchi kwa nguvu ili azidishe maumivu ya kufunga kwake. Kazi yake ilikuwa kulima, na hasa kusuka vikapu kama watawa wa nchi ya Misri.

Alijua sehemu kubwa ya Maandiko Matakatifu kwa kichwa, na daima kukariri sehemu sehemu baada ya kumaliza kusali zabari na sala zake. Alisali kwa uchaji kama Bwana Yesu mwenyewe alikuwepo wakati ule. Aliishi chini ya kibanda kidogo, futi nne kwa futi nne. Kwa hiyo siyo kushangaza kwamba Adui wa wokovu wetu alimpiga vita sana. Mara kwa mara roho yake ilifunika na giza, moyo ulikauka na kushikwa na

uchungu. Zaidi mbingu zilifungwa, zaidi alidumu katika kusali na kufunga. Mara nyingine akili yake ilijaa na mawazo ya uchafu, fahari za ulimwengu, n.k. Adui alizidisha kelele, kutisha kwa kuchukua umbo za ajabu, hadi kujionyesha kwa umbo la mwanamke ili kubembeleza na kufurahisha tamaa zake. Lakini Hilarion akipata nguvu kutoka kwa Mungu alishinda yote, kwa kupiga magoti na kufanya ishara ya msalaba katika paji la uso. Kwa kushinda kwake alijifunza kuwa mnyenyekevu na mwangalifu zaidi.

Baada ya kuishi miaka ishirini jangwani Mungu alianza kutenda miujiza na maajabu kwa mikono yake. Wagonjwa wakaponywa na wenye pepo wakafunguliwa. Hapa inatosha kusimulia mwujiza mmoja kati ya maelfu. Kulikuwa katika mji wa Majuma, bikira aliyejiweka wakfu kwa Mungu na pia mvulana aliyempenda sana. Kijana huyu alitumia maneno matamu, vichekesho na mbinu zote kumtongoza, bila kufaulu. Basi akaenda Memphis, Misri, kwa waganga asilia, makuhani wa mungu Eskulapio. Wakampatia hirizi na sanamu zilizochorwa juu ya sahani ya shaba. Akazifukia chini ya kizingiti cha mlango wa nyumba alimoishi msichana. Mara moja msichana akapagawa na pepo na akaanza kuwaka na upendo mkubwa kwa mvulana. Akatupa kitambaa cha kichwa chake, akashagharabagara nywele zake, akasaga meno na daima kutaja jina la mvulana. Basi wazazi wake wakamleta kwa Mt. Hilarion. Mara pepo akaanza kulia kwa nguvu na kusema:

“Nililazimishwa kuingia ndani yake. Nililetwa kutoka Memphis, kinyume cha mapenzi yangu. Huko nilifaulu sana kuwadanganya watu kwa njia ya ndoto zao. Lakini hapa ninateswa sana. Unanilazimisha kuondoka, lakini nimefungwa kwa njia ya nyuzi na sahani zilizowekwa chini ya kizingiti cha mlango wa nyumba yake. Siwezi kuondoka mpaka mvulana anayenishika hapa ataniruhusu kuondoka.”

“Kweli wewe una nguvu”, akamjibu Mtakatifu “ikiwa umeshikwa na nyuzi na sahani. Lakini uniambie, namna gani ulithubutu kuwingilia msichana aliyewekwa wakfu kwa Mungu?”

“Ilikuwa kulinda ubikira wake”.

“Nini? Kulinda ubikira wake, wewe adui wa usafi wa moyo. Kwa nini hukumwingilia yeye aliyekutuma?”

“Oh, hakuwepo nafasi kumwingilia, kwa sababu amekwisha pagawa na pepo wa uasherati”

Mtakatifu hakutaka kusikia zaidi, wala kumwita mvulana. Kuonyesha kwamba hakujali maneno na matendo ya pepo, akamfukuza pepo na kumrudisha msichana nyumbani akiwa mzima, baada ya kumkaripia kuchukua uhuru kuongea ovyo na mvulana na kwa hiyo kumpatia Adui uwezo wa kumwingilia.

Alipokuwa na umri wa miaka sitini na tano alifunuliwa kwa maono kifo cha Mt. Antoni. Akaenda kuhiji mahali Mt. Antoni alipoishi ili kuadhimisha, kwa kukesha usiku kucha, siku ya kufa kwake Antoni. Akarudi katika nchi yake na wafuasi wake wawili tu na kukaa Afroditon, jangwani. Lakini hakuweza kukaa huko kwa sababu ya umati wa watu waliomwangalia kama mrithi wa Mt. Antoni. Akaamua kwenda nchi ya Misri kuelekea jangwa la Oasis. Njiani pembezoni mwa Aleksandria, akakaa na watawa huko Brutium. Kesho yake aliondoka. Watawa walimsihi kubaki, lakini yeye akawaambia kwamba, kwa ajili ya usalama wao ni afadhali aondoke. Kumbe punde si punde usiku ufuatao askari waliotumwa kumkamata wakaja. Walipewa amri kutoka Kaizari Valeriani kumwua kwa sababu alimwaibisha mungu wa uongo Mamas na kuwaongoa watu wengi huko Gaza.

Mt. Hilarion akakaa mwaka mmoja jangwani mwa Oasis, lakini alipoona tena kwamba anajulikana mno huko na hawezi kukaa katika upweke, akaamua kwenda kukaa katika kisiwa cha mbali. Akapanda meli na kuelekea Sisilia. Akafika pwani mahali panapoitwa Capo di Passaro. Akaenda maili chache ndani ya nchi. Lakini tena huko watu wakafika kutoka kila sehemu kuombewa. Akaondoka tena na kwenda nchi ya Dalmatia, kati ya magofu ya mji Ragusa. Hapa akapigana na joka mkubwa aliyewamaliza watu kwa wanyama. Mwaka 365 tetemeko kubwa likatokea na tsunami likajitayarisha kufurika nchi. Wakazi wakamfikia Hilarion wakiogopa sana. Yeye akachora ishara ya msalaba mara tatu katika mchanga na akanyosha mikono kuelekea bahari. Wimbi la tsunami likasimama kama mlima na kurudi nyuma.

Usiku ule Mt. Hilarion akaamka na kutoroka kwenda Kisiwa cha Kipro. Akakaa karibu na mji Paphos. Alipokaa huko wiki tatu tu wote waliopagawa na pepo kisiwani walianza kutangaza kwamba Mt. Hilarion alifika kwao. Akawafukuza pepo wote. Akaenda kukaa mbali kidogo mlimani na mfuasi wake Hesykio. Na baada ya miaka mitano akiwa na umri wa miaka 80 akafariki akijiambia: ”Nenda sasa, kwa nini

kuogopa? Nenda sasa roho yangu, kwa nini kusita? Tazama sasa ni karibu miaka sabini ninamtumikia Kristo. Je, unaogopa kifo?" Aliposema maneno hayo akakata roho. Akazikwa mara kama alivyoamuru.

Mfuasi wake Hesykio hakuwepo alipofariki. Baada ya miezi kumi akapata nafasi kisirisiri kuchukua mwili wake ambao ulikuwa mzima na kumzika katika monasteri, karibu na Majuma, huko Palestina.[268]

Mt. Hilarion, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

## Mtumishi wa Mungu Terezia Grigolini, sista na mama, 1931

Terezia alizaliwa tarehe 18 Januari 1853, huko Italia.[269] Alikuwa binti wa Lorenzo and Stella Vaona, watu wamilikio ardhi na wamcha Mungu. Terezia alikuwa mtoto wa pili kati ya watoto kumi na mmoja. Tarehe 23 Januari 1874 alijiunga na Shirika la *Pious Mothers of Africa*, siku hizi linaitwa Masista Wamisionari wa Comboni, lililoanzishwa miaka miwili kabla na Danieli Comboni ili kupeleka Injili katika Afrika ya kati. Tarehe 15 Oktoba 1876 aliweka nadhiri, pamoja na sista Maria Bollezzoli, mwalimu na mama mkuu wa Shirika. Danieli Comboni aliongoza ibada. Ilikuwa kwake kama kuweka tofali la kwanza katika kazi yake.

Tarehe 12 Desemba, 1877, Sista Terezia aliondoka pamoja na msafara wa kwanza wa masista na mapadri kwenda Sudan. Danieli Comboni, wakati huu alikuwa Askofu, akawasindikiza. Sista Terezia aliteuliwa kuwa Mkuu wa Jumuiya ya masista huko Afrika. Mt. Danieli Comboni alimheshimu sana Sista huyu, akimwona kuwa: "mfano wa kweli kwa Masista Wamisionari wa Afrika ya Kati."

Wakachagua El Obeid, Sudan, kuwa makao yao. Amani haikudumu muda mrefu. Askofu Danieli Comboni akafa tarehe 10 Oktoba 1881. Mwaka ule, miezi michache kabla, Muhammadi Ahmed akadai kuwa Mahdi, yaani Mkombozi wa Uislamu, mtu aliyechaguliwa na Mungu kusudi kuwakomboa Wakazi wa Sudan na wakoloni. Mwaka 1882 uasi, ulioitwa Mahdiyah, ulibadilishwa kuwa jeshi la waasi. Wakavamia

---

[268] Rejea maisha yake yaliyoandikwa na Mt. Sofronio, kabla ya mwaka 392.

[269] Mambrotta, kijiji cha San Martino Buon albergo, mkoa wa Verona

misioni za Dalang na Al-ubayyid na wamisionari wote, wanaume kwa wanawake walifungwa gerezani. Wakavumilia mateso mengi kwa sababu hawakutaka kuasi imani yao.

Tarehe 8 Mei, 1884, Mahdi aliamuru kwamba masista wote wafunge ndoa, kama ilivyodaiwa katika Qur'ani. Kuepa tatizo hilo masista walioandikishwa ndoa ya bandia. Mapadri watatu wa Kanisa la kigiriki la Orthodoksi walikubali kuandika jina lao katika vyeti vya ndoa. Mwezi wa Agosti 1890 jambo hilo halikuweza kutumika, tena lilikuwa hatari kwa masista. Kwa hiyo Padri Josef Ohrwalder, mkuu wa Wamisionari wa Comboni, akaamua, kwa ajili ya usalama wa wote, kwamba Sista Terezia afunge ndoa na padri mmoja wa Kanisa la Orthodoksi, Padri Demetrio Cocorempas. Kwa uchungu mkubwa Sista Terezia alikubali sadaka hiyo ya namna yake.

Sista Terezia alikaa gerezani miaka 16. Mwaka 1885 masista wawili waliweza kutoroka. Miaka sita baadaye Padri Josef Ohrwalder na masista wawili tena walifaulu kutoroka. Baada ya kifo cha sista Conchetta Corsi, tarehe 3 Oktoba 1891, Sista Terezia alibaki peke yake, mbali na yeyote, bila na tumaini kuacha mahali pale. Kwa watoto sita waliozaliwa wakati wa kufungwa, mmoja tu aliishi: Giuseppe. Mtoto mwingine Giorgio alizaliwa baada ya kupata huru.

Mwaka 1898, uasi wa Mahdiyah ulipokwisha, Terezia alikaa Ugiriki mwaka mmoja, pamoja na mume wake na watoto wake. Mwaka uliofuata, mume wake Demetrio akaamua kurudi Sudan. Kama mke mtiifu alirudi pamoja naye huko Ondurman na baadaye El Obeid. Mwaka 1915, Demetrio alifariki kama Mkatoliki wa kweli. Terezia akarudi Ulaya mnamo mwaka 1918. Akakaa karibu na kaka yake Padri Luigi, Paroko wa Mambrotta, Verona. Akafariki tarehe 21 Oktoba, 1931, mikononi mwa masista wa Comboni waliofika kumsaidia katika ugonjwa wake. Alipenda shirika lake na daima alitaka kurudi kujiunga na masista wenzake, lakini kwa sababu ya familia yake alishindwa.

Mtumishi wa Mungu Terezia Grigolini, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele.

**Oktoba 22**

Wakatoliki tunamkumbuka leo Mt. **Yohane Paulo II**, Baba Mtakatifu aliyezuru bara la Afrika.
Huko Misri, Wakatoliki na Wakoptiki wanawakumbuka Wat. **Julio**, mfiadini, **Abibo** (Abib) na **Apolo** (*Apolonio*), watawa na wafiadini, Misri.[270]
Huko Ethiopia, Wakatoliki wanamkumbuka Mt. **Mathayo** Mtume.[271]
Shirika la Wamisionari wa Afrika (*White Fathers*) wanamkumbuka **Huberti Bruchez**, Padri aliyeuawa aliporudi parokiani mwake, huko Ighil-Mahani, Aljeria, baada ya kuwahudumia Wakristo, 1956.

Wakoptiki wanawakumbuka pia Wat. **Aleksanda**, askofu, **na wenzake**, wafiadini Adrianopolis, Misri, karne la III;[272] Mt. **Theodosioni**, mfiadini huko Kleopatria, Misri, na Mt. **Lot**, mwalimu wa Petro na Agato. Siku ile wanaadhimisha **Kutabarukiwa Kanisa la Mt. Julio El-Akfehas.**[273]
Waorthodoksi wanamkumbuka Mhashamu **Lot** wa Misri, Karne la V.
Huko Ethiopia, Wakristu wanamkumbuka Mt. Abba **Demetrio**, Patriarka, aksofu wa 12 wa Aleksandria. Waorthodoksi Tewahedo, wanawakumbuka wenye haki **Petro**, **Dionimo** (or Diyonas), na vita ya Wat. **Ya'ekob**, **Abu Tefa** na **Theodori**.[274]

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake! Amina.

## Wat. Apolo na Abibo, watawa, Karne la IV.

Abba Apolo alizaliwa katika mji wa Akhmin. Baba yake aliitwa Amani (Hamai) na mama yake Isa (Eyse). Walikuwa wenye haki mbele ya Mungu, wakishika amri zake na kuwatendea vema Wakristo na Wageni.

---

[270] *Acta Sanctorum*
[271] *The Ethiopian Rite Missal, Abba Emmanuel & Abba Brendan Cogavin, 2002, uk 183.*
[272] Baadhi yao: Heraklio, Anna, Elizabeth, Theodota, Glyceria, Donatiani, Praesidio, Germano, Rutino, Marko, Valerio.
[273] *Coptic Synaxarium: 25 Babah.*
[274] *Ethiopian Synaxarium: Tekemt 12.*

Hawakupata mtoto. Siku moja, wakati wa usiku, Isa akaona katika ndoto mtu aliyeng'aa sana mwenye mche wa mti mikononi mwake. Akaupanda katika nyumba yake, ukaota na kuzaa matunda. Akamwambia: ”Yeyote atakayekula tunda kutoka mti huu ataishi milele.” Akala tunda. Akatambua kwamba tunda lile ni tamu. Akasema: ”Sijui kama nitakuwa na tunda? ” Alipoamka kutoka usingizini akamwambia mume wake ndoto yake. Akamwambia kwamba aliota ndoto ile ile. Basi wakamsifu Mungu kwa furaha. Wakafunga siku mbili wakila tu mkate na chumvi. Baada ya muda Isa akapata mimba. Akasali kwa bidii mpaka akajifungua mtoto mwanaume. Wakamwita Apolo. Wakajitahidi kuishi kitakatifu.

Mtoto akakua, akaanza kujifunza teolojia, lakini moyoni mwake ulitamani sana kuishi kama mtawa. Hamu hiyo ikakua zaidi alipokutana na rafiki Abibo. Abibo alionyesha tangu utoto wake hamu ya kupenda upweke. Alikula kidogo, kunywa tu maji na kujitenga farakani ili kusali. Baba yake, ambaye hakutaka awe mkaapweke akmwonyesha kazi mbalimbali. Akishindwa kumbadilisha nia yake, baba yake alikuwa anakasirika na kumwonyesha kazi bora ya ndugu zake. Abibo hakuwa na kumjibu baba yake na alivumulia hasira ya baba yake. Kwa sababu alipendwa na kila mtu, baba yake alipokuwa mgonjwa karibu kufa, wazazi wake na rafiki zake wakamsihi hasiendelee kumchukia mtoto wake na kumwima urithi wake. Ndipo baba yake akamwita Abibo, na kwa ushangao wa kila mtu, akampigia magoti na kumwomba msamaha, “wewe ulimtafuta Yesu Kristo tu, mimi nilitawaliwa na anasa za dunia.” Akiwaita waana wake wengine akawaambia akimwonyesha Abibo: tazameni baba yenu na bwana wenu. Ni yeye atakayegawa mali yangu. Mtiini katika kila jambo. Baba yake alipofariki Abibo akagawa mali yake katika sehemu sawasawa, na akawapatia maskini sehemu yake. Akaenda kuishi katika kijumba kimoja hadi alipokutana na Apolo. Pamoja wakaenda kwa monasteri moja. Wakaanza kuishi maisha ya utawa na kujifunza kujikana ili kutawala mwili wao. Kweli waliishi maisha matakatifu wakimpendeza Mungu kwa kila jambo.

Abibo akafariki tarehe 22 Oktoba. Ndipo Apolo akaenda kukaa kwenye mlima Ablug na watu wengi wakakusanyika karibu naye. Akawa mwalimu wao. Kila mwaka tarehe 22 Oktoba wakakumbuka Abba Abibo ili kutimiza Neno la Mungu: ”*Mwenye haki atakumbukwa milele*” [275].

Abba Apolo akaishi miaka mingi, akajenga monasteri mbalimbali na watawa wengi wakamfuata. Aliishi wakati Mt. Makari wa Misri alipokaa jangwani. Siku moja Makari akamwandikia barua ili kumfariji yeye na watawa wenzake na kuwaimarisha katika njia za Bwana. Apolo alijua katika roho kwamba Makari alimwandikia barua. Akawaambia wale waliosikiliza: ”Makari mkuu anatuandikia barua yenye mafundisho mazuri ya ki-roho.” Alipofika na barua ndugu wakampokea kwa furaha, wakasoma barua na kufarajika sana.

Apolo alikuwa mmojawapo aliyeenda kwa Mt. Amonio kumwona mwanamke aliyesimama kati ya moto bila kuungua. Akaenda kwa Bwana katika amani.

Wat. Apolo na Abibo, mtuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

## **Mtu wa Mungu Padri Bruchez Hubert, aliyeuawa, 1956**.

Padri huyu alizaliwa tarehe 24 Januari 1916, huko Uswiswi.[276] Akasoma shule za sekondari za Altkirch na Tournus. Baada ya kujifunza falsafa huko Kerlois, Ufaransa, akaingia novisiati huko Maison Carrée, Aljeria, tarehe 2 Oktoba 1938. Akapadirishwa tarehe 11 Aprili 1943. Kwa sababu Vita vya pili vya Dunia vilikuwepo Ulaya, hakuweza kurudi Uswiswi, akabaki Afrika ya Kaskazini, huko Maison Carrée na Ouarzen.

Baada ya vita, mwaka 1946, akawa mwalimu na mweka hazina huko St. Maurice, Uswiswi. Akabaki miaka miwili tu na mwaka 1950 akarudi Aljeria. Akafanya kazi Tagmount-Azouz, Ighil-Ali, Fort National, Kjemaa-Saharidj. Mwaka 1955 akateuliwa kuwa Paroko wa Azazga na kuangalia eneo kubwa la Port Gueydon. Mwaka 1956, kwa ajili ya kupumzika kidogo, Mkuu wake akampendekeza akashike kwa muda

---

[275] Zab 112:6

[276] Bagnes, jimbo la Sion

mfupi nafasi ya Paroko wa El Affroun, katika bonde la Mitidja. Akarudi Azazga mwezi wa Septemba, baada ya mafungo yake ya mwaka.

Jumamosi, mnamo saa 14.30, Padri akaondoka kwa gari lake, pamoja na watu watatu wa Port Gueydon. Safari ya kwenda Port Gueydon ilikuwa bila shida, walisema waliosafiri pamoja naye. Wakati wa kurudi, Jumatatu asubuhi, Padri alitekwa. Alipochelewa kuondoka Port Gueydon, kinyume cha mazoea yake, kwa sababu ya kazi yake ya kitume, akaondoka mnamo saa 4.00 asubuhi. Akiwa na kilomita moja na nusu na Ighil, akauawa kwa risasi 15 alipokuwa bado katika gari lake. Lakini mwili wake uligunduliwa ukiwa pembeni mwa barabara, mikono yake ikinyoshwa kama msalabani. Juu ya kifua chake karatasi ilibandikwa. Maneno yalisomwa: ”Jeshi la Wafaransa waliwaua mashehe na waraia. Tunalazimishwa kulipa kisasi cha kifo cha Shehe wa Tmeline na mwenzake aliuawa bila huruma na askari wa Wafaransa”. Aliyetia sahihi: Amiri wa eneo la Kaskazini, Jeshi la ukombozi wa Aljeria. Alitoa uhai wake, bila kujua, kwa ajili ya wengine.

Mtu wa Mungu, Padri Bruchez, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

**Oktoba 23**

Huko Ethopia, kumbukumbu ya **Huras**, Shahidi, Ethopia.[277]
Huko Katako-Kombo, Jamhuri ya ki-demokrasia ya Kongo, Wakatoliki wanawakumbuka **Hendrik-Theodori Janssen** na **Firmini Halkett** (Padri *Raimundi*), mapadri wa Shirika la Passionisti waliouawa mwaka 1964.
Huko Aljeria Wakatoliki wanawakumbuka Wenyeheri **Esta Paniagua Alonso** na **Karitas (Caritas) Alvarez Martin**, masista wa Shirika la Masista Wamisionari wa Augustino, waliouawa mwaka 1994.

Huko Misri, Wakoptiki wanawakumbuka **Mashahidi Saba** waliouawa juu ya mlima wa Mt. Antoni na Wabarbari;[278] Mt. **Petronio**, mfuasi wa Pakomi.
Huko Ethiopia, Wakristu wanawakumbuka **Paulo** wa Thumuis; Mt. Abba **Zakaria** wa Shete, mtawa. Waorthodoksi Tewahedo, Ethiopia, wanawakumbuka pia **Eulana**, **Eulasio** (Eulochius), **Theodori**, **Ablas** na **ndugu zake**, na **Nitolao**, na **Abela**.[279]

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake! Amina.

## Wenyeheri Esta na Caritas, Wafiadini, 1994.

Esta Paniagua Alonso alizaliwa Izagre, mkoa wa Leon, Hispania, tarehe 7 Juni 1949. Alikuwa binti wa Dolores Alonso na Nicasio Paniagua. Baada ya kuhangaika na kutafutatafuta alitambua wito wake, kuwa sista. Akaingia katika shirika la Masista wa Augustino. Mwaka 1970 akaweka nadhiri za maisha.
Akajifunza unesi na akatumwa kufanya kazi katika nchi ya Aljeria. Kuishi kati ya Waislamu kulimshawishi kujifunza utamaduni wao na kuelewa kwa undani zaidi dini yao. Akajitoa kwao bila kujibakiza.

[277] Dictionary of Saints
[278] *Coptic Synaxarium: 26 Babah.*
[279] *The Ethiopian Rite Missal, Abba Emmanuel & Abba Brendan Cogavin, 2002, uk 183. Ethiopian Synaxarium: Tekemt 13.*

Akafanya kazi katika hospitali mbalimbali kuwahudumia wagonjwa hasa watoto walemavu. Kwa ajili yao hakuna utaratibu. Walizoea kumwita: “Malaika wao“. Mtu mmoja akamwuliza: “Je, humwogopi hali ya machafuko katika nchi“. Akamjibu: “Hakuna mtu awezaye kutoa maisha yetu kwa sababu tumekwisha toa kwa Mungu. Hakuna kitu kitakachotutokea kwa sababu tu mikononi mwa Mungu ... Na ikiwa itatokea, bado tupo mikononi mwake.“ Katika mkutano wao wa kuamua kurudi nyumbani au kukaa katika nchi ya Aljeria akawaambia masista wenzake: “Kwa wakati huu, kwangu mfano kamili ndiye Yesu. Aliteswa. Ilimbidii kuyashinda matatizo na mwisho akafa juu ya msalaba uliotufungulia chemchemi ya maji ya uzima.“ Alipenda sana kusoma biblia ambayo iliangazia maisha yake. Alisoma pia Qur’ani ili kuelewa zaidi dini ya ki-islamu, na vitabu vya maisha ya Wasufi.

Caritas alizaliwa huko Hispania,[280] tarehe 9 Mei 1933. Baba yake alikuwa Constantino Alvarez na mama yake Sotera Martin. Mwaka 1955 akaingia katika shirika la Masista wa Augustino. Akatumwa kufanya kazi katika nchi ya Aljeria. Akajitoa kabisa kwa kazi yake. Akaweka nadhiri yake ya maisha tarehe 3 Mei 1960. Kwa sababu ya afya yake dhaifu ilimbidi arudi Hispania. Mara alipopona tena akarudi Aljeria na akabaki huko zaidi ya miaka 30. Aliwahudumia wazee na maskini.

Akapita katika machafuko ya nchi, yaliyoanza mwaka 1990, bila kufikiri hata mara moja kurudi nyumbani na kuwaacha watu aliyewahudumia na waliompenda sana. “Nipo tayari kupokea yote Mungu na wakubwa wangu wanaotaka kutoka kwangu. Bikira Maria akabaki tayari kwa mapenzi ya Mungu, ambayo bila shaka yalikuwa magumu kwake. Mimi nataka kubaki kama yeye katika hali hiyo ya nchi.“ Kila siku alisali rozari na upendo wake kwa Maria ulimkumbusha kuwa mtu aliyejiweka wakfu kwa Mungu. Tarehe 23 Oktaba 1994, Caritas na Esta waliuawa njiani wakienda kuhudhuria misa Jumapili. Tarehe 8 mwezi wa 12, 2018, walitangazwa kuwa Wenyeheri pamoja na wengine 17.

Wenyeheri Esta na Caritas, mtuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

---

[280] Santa Cruz de la Salceda, mkoa wa Burgos

**Oktoba 24**

Huko Aljeria na Sisilia (Italia), Wakatoliki wanawakumbuka Wat. **Feliksi**, askofu, **Audakto** na **Januari**, mapadre, **Fortunati** na **Septimo**, wasomaji, wote wafiadini.[281] Kwa sababu Feliksi alikataa kumpatia Hakimu Magniliani Vitabu Vitakatifu, wote waliuawa kwa upanga, mwaka 303.

Huko Ethiopia, Wakatoliki wanawakumbuka **Towashi**, mtumishi wa Kandake, Malkia wa Kushi, na **Musa**, 'Mtu wa Mungu'.[282] Pia kumbukumbu ya Mt. **Elesbaan**, Mfalme.[283]

Huko Ethiopia, Wakristo wanamkumuka Mt. **Aretha**, mzaliwa wa Ethiopia.

Huko Kiziwa cha Kanari, Wakatoliki wanamkumbuka **Antoni Maria Klaret**, Askofu, aliyezaliwa kwao mwaka 1807.

Huko Njombe, Tanzania, Wakatoliki wanamkumbuka **Raimundi Mwanyika**, Askofu, aliyefariki mwaka 2013.

Wakoptiki wanamkumbuka Mt. **Makari**, askofu wa Edkov.[284]

Huko Ethiopia, Wakristu wanamkumbuka Abba **Aragawi**, aliyejulikana kwa jina la **Za-Mikaeli**.

Huko Ethiopia, Waorthodoksi Tewahedo, pia wanawakumbuka **Tarakwa**, mfiadini na wenzake, **Damasio**, **Emraya**, mfiadini na **wenzake mia nne na thelathini na mmoja**.[285]

Waorthodoksi wanamkumbuka **Elesbaan**, Mfalme wa Ethiopia, mnamo 540.

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake! Amina.

## Mt. Feliksi, askofu na mfiadini, 303

---

[281] *Roman Martyrology, ed*. 1956.

[282] *The Ethiopian Rite Missal, Abba Emmanuel & Abba Brendan Cogavin, 2002, uk 184.*

[283] Dictionary of Saints, inamkumbuka tarehe 27 Oktoba.

[284] *Coptic Synaxarium: 27 Babah.*

[285] *Ethiopian Synaxarium: Tekemt 14.*

Mwanzoni mwa dhiki iliyosababiswa na Kaizari Dioklesiani Wakristo wengi walioogopa mateso makali walivikabidhi Vitabu vitakatifu mikononi mwa watesaji ili vichomwe moto. Wengi tena walitafuta kujisafisha na kosa lile kubwa wakisema kwamba ilikuwa halali. Feliksi, askofu wa Thiabura, katika mkoa wa *Proconsularis* (Tunisia siku hizi), Afrika, alikwazwa na mwenendo wa Wakristo wenzake.

Magniliani, hakimu wa mji ule, akatafuta kumkamata na kumwamuru kumkabidhi vitabu vyote vya Kanisa ili vichomwe. Akamjibu: "Ni afadhali mimi nichomwe". Magniliani akamtuma kwa balozi wa Kartago, na yeye akamtuma kwa Liwali, aliyekuwa Mkuu wa Afrika wakati huu. Afisa mkuu huyu, aliyeudhiwa kwa maneno yake ya ujasiri, akaamuru afungwe na minyororo na vyuma vingine na kutiwa gerezani. Akabaki humo siku 9, baadaye wakampandisha merikebu wakisema kwamba ahukumiwe mbele ya Kaizari. Askofu akalazwa kati ya miguu ya farasi kwa siku nne bila kula wala kunywa.

Merikebu akafika Agrigentum, Sisilia, Italia. Askofu akahudumia kwa heshima kubwa na Wakristo wa kisiwa kile katika kila mji alipopita. Walipofika Venosa katika Apulia, Liwali aliamuru kwamba minyororo iondolewe. Akamwuliza tena ikiwa alikuwa na vitabu. Askofu Feliksi akakataa kuvikabidhi. Hakukana kwamba alikuwa navyo bali alikataa kuvikabidhi. Ndipo Liwali akaamuru akatwe kichwa bila kumwuliza zaidi. Mahali pa mateso Feliksi akamshukuru Mungu kwa neema zake zote. Akainamisha kichwa chake na kutolea Mungu maisha yake kuwa sadaka ipendezayo. Akafariki mwaka 303, alipokuwa na umri wa miaka 56. Siku ya kifo chake alitangaza kwamba alitunza ubikira wake bila doa na kumhubiri Kristo na kweli zake kwa bidii maishani mwote.

Mt. Feliksi, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

## Abba Aragawi na wenzake, karne la V-VI

Abuna Aragawi, anayeitwa pia Za-Mikael'Aragawi, ni mmojawapo wa Watakatifu tisa waliofika Ethiopia, katika karne la VI. Wamefika Ethiopia kutoka sehemu mbalimbali za Dola la Roma, kukwepa dhiki



baada ya Mtaguso wa Kalsedoni (451). Walikuwa watawa wenye elimu. Inasemekana kwamba walitafsiri Agano Jipya kwa lugha ya Kigé'ez. Walipofika Ethiopia walikuta imani ya Wakristo ilififia. Lakini kwa juhudi zao walifufua Ukristo. Inafikiriwa kwamba kila mmoja wao alijenga kanisa au monasteri inayoitwa kwa jina la mmoja wao. Kwa kweli makanisa na monasteri nyingi zimejengwa na Watawa hawa. Wote tisa wanaangaliwa na Kanisa la Orthodoksi kuwa Watakatifu.

Abba **Aragawi** alitoka Konstantinopoli. Alikuwa mwana wa Yeshaq na 'Edna, familia ya ki-falme huko Konstantinopoli. Akawa mtawa katika monasteri ya Pakomi alipokuwa umri wa miaka 14. Pakomi akamwita Za-Mika'el. Sifa yake ikawavuta watakatifu wanane wengine, waliokaa pamoja naye na Pakomi. Hata mama yake 'Edna akajiunga na kuwa mtawa katika konventi ya wanawake. Miaka saba baada ya kifo cha Pakomi, Za-Mika'el akarudi Konstantinopoki na baadaye akaenda Aksum. Akawaita Watakatifu wanane na wazazi wake wafike Aksum. Wakakaribishwa na Mfalme 'Ella-'Ameda II katika mwaka wa tano wa utawala wake.

Baada ya kukaa miaka 12 katika ikulu ya Mfalme Ella Ameda wa Aksum, yeye na Wenzake wakaondoka kila mmoja kwenda mahali pake. Aragawi alijenga monasteri ya Debre Damo, kati ya Aduma na Addi Grate. Kadiri ya pokeo fulani Mungu alimjalia Abuna Aragawi nyoka mkubwa sana kumsaidia kupanda mlima alipojenga Debre Damo. "Wakati Abba Aragawi, alipofika kwenye mlima, nyoka mkubwa akamtokea. Malaika Mkuu Mikaeli alisimama karibu na kumwelekeza dira. Nyoka akamviringisha Aragawi na kumkokota hadi kilele cha mlima." Inasemekana kwamba kabla ya kuenda kupigana na Mfalme wa ki-yahudi Dhu Nuwas, huko Arabia, mnamo mwaka 525 B.K., Mfalme Kaleb alienda kutafuta shauri lake.

Abba **Pantaleoni**,[286] kadiri ya Matendo yake yaliyoandikwa katika karne la XV, alizaliwa katika familia ya ukoo bora huko Konstantinopoli. Aliingia monasteri akiwa mtoto mdogo bado. Akafika Ethiopia wakati wa utawala wa Mfalme 'Ella-'Améda II, bin Rais Sal'adoba. Baada ya kutengana na wenzake, yeye alipanda Bet Qatin, kilima karibu na Aksum. Akajenga kijumba. Akakaa miaka arobaini na mitano,

---

[286] Rejea pia tarehe 16 Oktoba

akisimama wima na kusali. Ndiyo maana anaitwa ‘Pantaleoni wa kijumba’. Alitenda miujiza mingi hasa kuwaponya wagonjwa. Mfalme Kaleb kabla ya kwenda kupigana na Mfalme Dhu Nuwas, alimtembelea. Kaleb alipong’atuka katika cheo chake cha Mfalme, alijiunga naye na kuwa mtawa.

Abba **Guba**, kutoka Silisia, akakaa pamoja na Abba Pantaleoni kwa muda. Baadaye aliendа katika jangwa la Baraka na kutoweka. Inasemekana kwamba monasteri ya Endebaguba, karibu na Adua ilijengwa naye.

Abba **Garima** au abba **Yeshaq**, alitoka Konstinopoli. Kadiri ya matendo yake, yaliyoandikwa pia katika karne la XV, alizaliwa kwa maombezi ya Bikira Maria, mama yake akiwa tasa kwa miaka 15. Baba yake alikuwa mfalme wa sehemu fulani. Alipokuwa na umri wa miaka 12 alitumwa kujifunza teolojia. Lakini baada ya kifo cha baba yake akafanywa kuwa Mfalme. Alipotawala kwa muda wa miaka saba akaitwa na Abba Pantaleoni. Kwa msaada wa Malaika Gabrieli aliweza kufika Aksum, Ethiopia, kwa masaa matatu tu. Akakaa pamoja na Abba Pantaleoni kwa muda wa miaka mitano. Akajitenga naye na kwenda Madara na kuanzisha monasteri huko. Akakaa kule kwa muda wa miaka 17 au 23, akitenda miujiza mingi, kuwinga pepo na kuwaponya wagonjwa. Inasemekana kwamba Mfalme Gabra Masqual akamjengea kanisa. Akafariki tarehe 17 Sane (Juni 24).

Abba **‘Afse**, kutoka na Edessa. Kadiri ya Matendo yake, kutoka Edessa Abba ‘Afse alienda Roma na kule alikutana na Abba Yeshaq (Garima). Kutoka Roma alikwenda Ethiopia. Yeye alikwenda karibu ya mto Geba na nchi ya Bäläsat. Kutoka huko akaenda Mujja na Dabra Gännät, akivumilia mateso njiani mwote kutokana na wenyeji. Baada ya miaka 12 akakaa monasteri ya Garima. Akajenga kanisa ndogo na kuanza jumuiya ya waamini, akipokea zaka kutoka na wenyeji na Mfalme Kaleb. Akafariki akiwa na miaka mingi.

Abba **Libanos**, au Abba **Mata’a**, alifanya kazi katika nchi ya mito Marab-Belesa, kaskazini ya Ethiopia, siku hizi Eritrea. Inasemekana kwamba alikuwa mtawa pamoja na Pakomi, ndiye yeye aliyemtuma kwenda Ethiopia. Akakaa Beqela kwa muda wa miaka saba, akitafsiri Injili ya Mathayo kwa lugha ya Kige’ez. Akaitwa kwenda Aksum na Abuna Eliya (*‘Eleyas*). Alipomkosoa kwa kumwonyesha tabia yake

mbaya ilimbidi kukimbilia Darraqa akifukuzwa na Mfalme ‘Za-Gabazza Aksum. Akakaa katika kijumba kimoja hadi Abuna na Mfalme, wakilazimishwa na Mungu, kutambua makosa yao. Akaenda Guna Guna. Mfalme Gabra-Masqual akamjengea kanisa la Bfeta Masqual. Mwisho mwa maisha yake akawaendea wapagani waliokaa Tarqa. Akafariki kule.

Abba **Likanos** kutoka Konstantinopoli akakaa Dabra Qwanasel, monasteri moja karibu na Adwa.

Abba **Yamata** alijenga monasteri Gär'alta huko Endärta, mkoani mwa Tigre.

Abba **Tsehma**, kutoka Antioka, alijenga monasteri Sedenya, karibu na Adwa.

Watakatifu Tisa, mtuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

**Oktoba 25**

Huko Roma, Wakatoliki wanawakumbuka **Krisantho**, kutoka Aleksandria na mke wake **Daria,** kutoka Ugiriki, wafiadini, Roma.[287]
Huko Afrika ya Kaskazini, Wakatoliki wanawakumbuka Wat. **Saturnino, Klaudiano, Primo, Flaviano, Zotiko, Asterio, Karo, Saturo**, wafiadini.[288]
Huko Kalenda, Jamhuri ya ki-demokrasia ya Kongo, Wakatoliki wanamkumbuka **Tomaso Beya**, Padri wa jimbo, aliyeuawa mwaka 1960 na Wanyoka.
Huko Zambia, Wakatoiki wanamkumbuka Sista **Matilda Mulengachonzi,** aliyefariki baada ya kujeruhiwa tarehe 24 Agosti, mwaka 2020.

Huko Ethiopia, Wakristu wanawakumbuka Mt. **Pantaleoni**, mfiadini na **wenzake 560**, wote wafiadini. Waorthodoksi Tewahedo, wanawakumbuka pia **Salasioni**, **Atrakio**, Abba **Yarpes** (*Iphrasius*), **Androniko**, **Armolio** (*Hermolius*), **Hermesi**, **Harmoktis**, na wanawake **Admania** na **Samata**, na Padri **Isaya**.[289]

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake! Amina.

## Wat. Krisantho na Daria, wafiadini, 284.

Polemeo, baba yake Krisantho, alikuwa mzaliwa wa Misri, mwenyeji wa mji Aleksandria, mtu kutoka ukoo bora. Krisantho alikuwa mwana wake wa peke. Wakati wa Kaizari Numeriani familia yake wakahamia Roma. Huko Krisantho alilelewa na walimu mashuhuri. Alipoona jinsi Warumi walivyoishi katika anasa, akamgeukia Mungu, akaanza kusoma kitabu cha Matendo ya Mitume. Ndipo akabatizwa na kulelewa kikristo na Padri mmoja, kwa jina Karpoforo. Baba yake hakufurahi uongofu wa mwanaye. Akamfungia Krisantho katika jumba lake na kujaribu

[287] *Roman Martyrology*, 1956.
[288] *Acta Sanctorum*
[289] *Ethiopian Synaxarium: Tekemt 15.*

kumshawishi kwa kumletea malaya. Lakini Krisantho akabaki imara katika imani yake na katika ubikira wake. Basi baba yake akamletea Daria, Vestali mmoja,[290] mashahuri kwa kuwashawishi wanaume kuiabudu miungu. Daria, aliyekuwa amemtumikia mungu wa uongo Vesta, akajaribu kumbadilisha, kuacha imani yake na kuiabudu miungu, bila mafanikio. Bali yeye mwenyewe akabadilishwa, akapokea neema ya Mungu na kumfuata Krisantho katika imani yake. Wakiungana katika imani, matumaini na upendo, wakafunga ndoa. Kwa njia hiyo baba yake akamfungulia Krisantho na kumweka huru. Krisantho akamshauri Daria kuishi katika hali ya ubikira kuliko kutumia ndoa, ili waweze, katika usafi wa moyo, kukana malimwengu na kutimiza ahadi zao za ubatizo.




Jinsi walivyoishi na kushuhudia imani yao ya kikristo iliwatofautisha na watu wengine. Wakawaongoa Warumi wengi. Akida Klaudio, na mke wake Hilaria, na wana wake wawili, Mauro na Jasoni wakaongoka, wakawa Wakristo, pamoja na askari wake sabini. Basi Krisantho na Daria wakasthakiwa kwa liwali Selerino. Akamfunga Krisantho katika gereza la Mamertine, na Daria, mke wake akatumwa kuishi katika danguro. Lakini Mungu hawaachi wale wanaomwamini, akawalinda. Simba jike akamkingia Daria ubikira wake. Kaizari alipokasirika akawahukumu wapigwa mawe na kuzikwa hai katika mchanga. Inawezekana kwamba mateso hayo yalichaguliwa kwa sababu ndiyo mateso na kifo cha *Vestale* anayeasi kazi yake. Na mahali palipozikwa ni karibu ya Via Salaria, mahali pa mateso ya *Vestale*.

[290] Vestali walikuwa jumuiya ya mabikira sita waliomhudumia Vesta, mungu wa kike wa nyumba. Walichaguliwa walipokuwa kati ya umri wa miaka 6 hadi 10. Waliweka nadhiri ya useja na usafi wa moyo kwa miaka thelathini. Kazi yao hasa ilikuwa kutunza moto wa hekalu la Vesta ili usizimike.Wwalikuwa na mamlaka na waliheshimiwa sana. Walijifunza na kuhakikisha jinsi ibada za taifa zilivyoadhimishwa. Jumuiya ya Vestali imefutwa mwaka 394 na Kaizari Theodosio.

Walifariki mnamo mwaka 237, wakati wa utawala wa Kaizari Numeriani.
Kaizari akaamuru pia walioongoka wauawe. Klaudio akazamishwa katika maji, wana wake wawili walikatwa vichwa, mke wake Hilaria akanyongwa. Wakazikwa karibu na kaburi la Krisantho na Daria. Mt. Gregori wa Tours anatusimulia kwamba, muda mfupi baada ya kifo chao, Wakristo waliozoea kukusanyika kusali penye kaburi lao. Kwa amri ya Liwali wa Roma, walifungwa katika pango na kuzikwa wazima.
Miili ya Krisantho na Daria ilivumbuliwa wakati wa utawala wa Konstantino Mkuu. Sehemu hiyo ya makatakombi ilijulikana kwa muda mrefu kama Shamba la wafu la Krisantho na Daria. Kaburi lao limepambwa na Baba Mtakatifu Damasi alitunga maneno ya kuwasifu marehemu.
Wat. Krisantho na Daria, mtuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

**Oktoba 26**

Sisi Wakatoliki tunawakumbuka Wat. **Rogasiano**, padre, mfiadini na **Felisisimo**. Mt. Sipriano aliwataja katika barua yake kwa 'Walioungama imani'.[291]
Huko Tunisia, Wakatoliki wanamkumbuka Mt. **Kwod-Vult-Deo**, askofu wa Kartago, Tunisia.[292] Pia kumbukumbu ya Mt. **Aurelio**, askofu wa Kartago, Tunisia.[293]
Huko Misri, Wakatoliki wanamkumbuka Mtumishi wa Mungu **Helena** (Hélène) **Beghian** (*Marie de Béthanie*), 1945.
Huko Kameroun, Wakatoliki wanamkumbuka **Yosefu** (*Joseph*) **Mbassi**, Padri wa Jimbo, aliyeuawa mwaka 1988.

Huko Ethiopia, Wakristu wanawakumbuka Patriarka **Agato**, askofu wa 39 wa Aleksandria na Mt. Abba **Macrobio**. Waorthodoksi Tewahedo, wanawakumbuka Mt. Abba **Eblo** (or Apollo); Mt. Abba **Petro**, mfuasi wa Abba Isaiah, mwanakoriti; **Paraku, wenyehaki arobaini na watano wa El-Derke**, na **Aroni**, **Karbu**, **Analyu**, Abba **Paulo** (Pawli**)**, **Marko**, na **Gadeli**,[294].

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake! Amina.

## Quodvultdeo, askofu, 450.

Maana ya Jina lake ni 'Mungu apendavyo'. Hatujui tarehe alipozaliwa na alipofariki. Tunajua kwamba alizaliwa Afrika. Mnamo mwaka 407/408 alipokuwa kijana alikaa katika mji wa Kartago, na mwaka 421 akawa Shemasi katika mji ule. Kwa barua kwa askofu Augustino akamwomba aandike kitabu kuhusu uzushi. Augustino akaandika kitabu cha *De Haeresibus* kwa heshima ya Quodvultdeo.

---

[291] *Martyrologium Romanum,* ed. 2001.
[292] *Roman Martyrology, ed*. 1942.
[293] *Acta Sanctorum*
[294] *Ethiopian Synaxarium: Tekemt 16.*

Mnamo mwaka 437 akawa askofu wa Kartago. Mfalme Genserik alipoteka mji wa Kartago, mali yote ya kanisa ikachukuliwa na Genserik, Quodvultdeo akahamishwa, pamoja na makleri wote. Wakawekwa katika mashua madogo. Upepo ukavuma na kuwapeleka huko Napoli. Huko, akawahudumia Wakristo. Kati ya mwaka 445 na 451 akaandika kitabu chake, "*Kitabu cha ahadi na maelezo ya Mungu*". Inawezekana kwamba aliviandika vitabu vingine vingi ambavyo viliwekwa chini ya majina ya Mt. Augustino na Mt. Prosper.

Hatujui tarehe alipofariki. Wengi wanafikiria kwamba alifariki mwaka 450. Mwili wake ulizikwa katika Shamba la wafu la Santo Gennaro, Capodimonte, Italia.

Mt. Quodvultdeo, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

## Mtumishi wa Mungu Helena (Nelly) Beghian, 1945

Hatuna habari nyingi kuhusu Mtumishi huyu wa Mungu. Baba yake alikuwa Mkatoliki na mama yake Mworthodoksi. Waliishi Aleksandria, Misri. Nelly au kwa jina lingine Helena, alichagua kuwa Mkatoliki kama baba yake. Akaingia katika Shirika la Mama wa Mungu, na kuitwa Sista Maria wa Bethania. Aliishi Aleksandria na kazi yake ilikuwa kufundisha. Lakini anakumbukwa hasa kwa sababu ya sala zake na kujitoa kwake kwa ajili ya utakatifu wa mapadri. Akafariki mwaka 1945.

Mtumishi wa Mungu Nelly, utuombee ili Mungu atukuzwe ndani ya mapadri wake. Amina.

**Oktoba 27**

Sisi Wakatoliki tunamkumbuka Mt. **Frumensio** (Abba Salama), askofu, Ethiopia. Alipokuwa mtekwa huko alitawazwa kuwa askofu na Patriarka Atanasi, na akaeneza Injili katika nchi hiyo.[295]
Huko Italia,tunamkumbuka Mt. **Gaudioso**, askofu kutoka Afrika, aliyekuja Campania, Italia, kwa sababu ya dhiki ya Waharabu (*Vandals*) na alikufa ki-takatifu katika monasteri moja ya mji ule.[296]
Huko Misri, Wakatoliki wanamkumbuka Mt. **Abrahamu wa Menouf**, mwanafunzi wa Pakomi, (aliyejulikana pia kwa jina la Abrahamu maskini au Abraham mtoto) mkaa pweke, Misri. Alifariki mwaka 367. Mt. **Tekla Haimanot**, mtawa, Ethiopia, 1313. Pia kumbukumbu za Watakatifu tisa wa Ethiopia: **Aragawi**, **Pantaleoni**, **Garima**, **Alef**, **Tzehma**, **Alftze**, **Liqanos**, **Imeata**, **Guba** (au Otz).[297]

Wakoptiki wanawakumbuka pia Mt. **Theodori**; Mt. **Yared**, abate huko Aleksandria, Misri; Mt. **Lalibela (Ghebre Mesqel)**, Kaizari wa Ethiopia, 1255. Pia wanakumbuka siku ya leo **Kutabarukiwa kwa Kanisa la Mt. Marko**.[298]
Huko Ethiopia, Wakristu[299] wanamkumbuka Mt. **Dioskoro**, Patriarka, askofu wa 31 wa Aleksandria. Pia kumbukumbu ya **Watakatifu wa tisa**, waanzilishi wa Kanisa la Ethiopia, 380.

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake! Amina.

## Mt. Abrahamu wa Menouf, 372

Tunasoma habari zake katika kitabu cha Watakatifu wa Wakoptiki wa Misri. Abrahamu alizaliwa Menouf, mahali karibu ya delta ya mto Nile.

---

[295] *Martyrologium Romanum,* ed. 2005.
[296] *Martyrologium Romanum,* ed. 2001.
[297] *Acta Sanctorum.* Rejea maisha ya Takla Haimanot tarehe 17 Agosti na ya Watakatifu tisa wa Ethiopia tarehe 24 Oktoba.
[298] *Coptic Synaxarium: 30 Babah.*
[299] *Ethiopian Synaxarium: Tekemt 17.*

Baba yake alikuwa Mkristo Tajiri. Tangu ujana wake alitamani sana kuwa mtawa. Akaenda kwanza Akhemeen na kutoka huko aliingia utawa katika manasteri ya Mt. Pakomi. Akabaki pamoja naye miaka 23, akijikania, kwa kufunga na kusali. Ndipo alimwomba Pakomi ruhusa kuishi kama mkaa pweke.

Katika pango mojawapo, alikaa miaka 17 mpaka kifo chake. Alitengeneza nyavu za kukamata samaki. Mlei mmoja alizoea kumtembelea, kupokea kazi yake na kuiuza, kununua maharage kwa ajili yake. Fedha zilizobaki aliwagawia maskini. Kwa miaka 13 alikuwa anakula maharage yaliyoloweka katika maji yenye chumvi. Nguo zake zilipochanika, akajifunika na kipande cha gunia. Akaitwa na watu ‘Abrahamu maskini‘ au ‘Abrahamu mtoto‘ kwa sababu ya maisha yake sahili na imani yake kama imani ya mtoto kwa wazazi wake.

Alienda monasteri ya Mt. Pakomi, kila baada ya miaka 2 au miaka 3 kupokea komunio.


Shetani akapigana naye vita tangu alipohamia pangoni. Wakamsumbua kwa kupiga kelele za ajabu na kumtisha kwa picha za kuogofya. Kwa neema ya Mungu alizoea kuwashinda na kuwafukuza. Wakati wa kuacha ulimwengu huu na kwenda kwa Mungu, akamtuma mlei aende monasteri kumleta Abate Theodori (*Tadros*), mfuasi wa Mt. Pakomi. Abate Theodori alipomfikia, alijiinamisha mbele yake na kumwomba sala zake. Wote wawili wakaamka na kuanza kuomba. Ndipo Abrahamu akajilaza kwa kuelekea Mashariki na kukata roho. Abate Theodori akawataarifia watawa wa monasteri. Wakaja na kubeba mwili wake. Wakamwomba kuwabariki na wakamzika pamoja na miili ya watakatifu.

Mt. Abrahamu, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

## **Mt. Frumensio, mwungama dini, askofu na mtume wa Ethiopia, 383**.

Mt. Frumensio ni askofu wa kwanza wa Aksum (*Axum*), Ethiopia. Wengi wanasema kwamba alikuwa wa kwanza kuleta Ukristo katika nchi ya Ethiopia, ingawa, kadiri ya pokeo, Mt. Matayo alikuwa Mtume

wa kwanza kuhubiri katika nchi hiyo. Towashi,[300] aliyebatizwa na Mt. Filipo, aliporudi katika Ikulu ya Malkia Kandake, akawa Mkristo wa kwanza katika nchi hiyo.[301]



Mwanahistoria Rufino anatuambia kwamba Frumensio alizaliwa katika mji wa Tiro, siku hizi Sur, Lebanon. Mwaka 316, Frumensio pamoja na kaka yake Edesio walisindikiza Meropio, mjomba wao, katika safari kwenda Ethiopia. Meli yao ilipokaa katika bandari moja ya Bahari ya Sham, wenyeji wa nchi hiyo waliwaua mabaharia na watu wote, isipokuwa vijana wawili waliopelekwa, kama watekwa, katika Ikulu ya mfalme wa Aksum. Zamani ufalme huo ulitawaliwa na Malkia wa Kandake.

Vijana hawa walimpendeza mfalme. Akawaweka katika kazi za uaminifu, Edesio akawa Mnyweshaji mkuu na Fremensio Mtunza hazina na Waziri Mkuu. Kabla ya kufa kwake mfalme akawaachilia uhuru. Lakini Malkia aliwaomba wabaki Ikuluni na kumfundisha mtoto wake Ezana atakayekuwa mfalme baadaye. Akamwomba Frumensio amsaidie katika mambo ya utawala. Wakabaki na Frumensio akashika nafasi ya kueneza Ukristo. Kwanza wakawashauri wenyebiashara waliokuwepo katika nchi hiyo kuishi kadiri ya imani yao waziwazi. Baadaye waliwaongoa baadhi ya wenyeji.

Wakati Ezana aliposhika utawala wa ufalme, basi Edesio alirudi katika Tiro, mji wake. Akapadirishwa kule. Frumensio akiwa na hamu ya kueneza Injili katika nchi ya Ethiopia, akamsindikiza Edesio mpaka Aleksandria. Akamwomba Mt. Atanasi, Patriarka wa Aleksandria, kumtuma askofu na mapadri huko Ethiopia. Atanasi alikusanya sinodi na kwa shauri yao akampadirisha Frumensio awe askofu, mwaka 328. Frumensio akarudi Ethiopia. Akaanzisha kiti cha uaskofu katika mji wa Aksum. Akambatiza Ezana (‘Abreha) na ndugu yake Saizana (‘Asbeha)

[300] Towashi naitwa katika Kanisa la Mashariki *Chrysanthius Eunuchus*, maana yake Towashi Krisantho.
[301] Mdo 8:27-39.

aliyemshirikisha utawala wake, akajenga makanisa mengi na kueneza Ukristo katika nchi yote ya Ethiopia kwa mahubiri yake na miujiza yake. Wengi wakaongoka, wakisaidiwa na wafalme wao kushika imani. Wenyeji wakamwita Frumensio, *Kesate Birhan*, yaani 'Aliyeleta Mwanga' na pia kwa jina la Abba Salamu, yaani Baba wa amani. Akawa Abune, cheo anachopewa Mkuu wa Kanisa la Ethiopia.

Kaizari Konstansio II akawaandikia Mfalme Ezana na ndugu yake Saizana barua akimwomba askofu Theofilo, mfuasi wa Ario, ashike nafasi ya Frumensio. Mfalme hakukubali ombi lake.

Kadiri ya pokeo moja ya Wakoptiki, Frumensio alikuwa wa kwanza kuandika Agano Jipya kwa lugha ya Kige'ez.[302]

Mt. Frumensio, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele.

[302] Sikukuu yake inaadhimishwa na Wakoptiki wa Misri tarehe 18, mwezi wa Desemba, Waorthodoksi wa Mashariki tarehe 30, mwezi wa Novemba, Waamini wa Kanisa la Orthodoksi Tewahedo, Ethiopia, tarehe 1, mwezi wa Agosti.

**Oktoba 28**

Sisi Wakatoliki tunawakumbuka Wat. **Simoni** na **Tadei**, aliyeitwa Yuda, mitume. Simoni alihubiri kwanza Injili huko Misri, na Tadei huko Mesopotamia. Baadaye wote wawili kwa pamoja waliingia Persia. Wakawaongoa wenyeji wengi kumwamini Kristo, kabla ya kufa mashahdi.[303]
Huko Tunisia, kumbukumbu ya Wat. **Sofroniano**, **Amaranto**, **Kwinto** na **Lusio**, wafiadini.
Huko Kaisaria, mji wa Palestina, kumbukumbu ya Mt. **Yohane Chozeba**, abate na askofu, mzaliwa wa Theba, Misri.[304]
Huko Ethiopia, Wakatoliki wanamkumbuka pia **Yemrehana-Krestos**, mfalme wa Ethiopia.[305]

Huko Misri, Wakoptiki wanawakumbuka Wat. **Maksimo**, **Nomesio**, **Boktori** na **Filopo**.[306]
Huko Ethiopia, Wakristu wanamkumbuka Mt. **Theofilo**, Patriarka, askofu wa 23 wa Aleksandria.[307]

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake! Amina.

## Wat. Simoni na Yuda Taddei, Mitume, Karne ya I.

Simoni aliitwa Mkananayo na Wainjili Mathayo na Marko, au Zelote na Mwinjili Luka, ili kumtofautisha na Mtume Petro aliyeitwa pia Simoni, na Mt. Simeoni, ndugu ya Mtume Yakobo. Pengine aliitwa Mkananayo kwa sababu alitoka mji wa Kana. Ndiye aliyemwalika Yesu kuhudhuria harusi yake huko Kana. Lakini kwa lugha ya Kisyrokaldaiki au lugha ya Kiebrania ya siku hizi, neno Kana linamaanisha mtu mwenye wivu,

[303] *Martyrologium Romanum,* ed. 2001.
[304] *Les petits Bollandistes*
[305] *The Ethiopian Rite Missal, Abba Emmanuel & Abba Brendan Cogavin, 2002, uk 186.*

[306] *Coptic Synaxarium: 1 Hatour.*
[307] *Ethiopian Synaxarium: Tekemt 18.*

sawa sawa kama neno Zelote kwa lugha ya Kigiriki. Inawezekana kwamba alipewa jina hilo wakati wa utume wake, kwa sababu alikuwa na wivu na upendo kwa Bwana wake.

Yuda aliitwa Tadei [308] maana yake hodari, kumtofautisha na Yuda Iskariote. Mt. Hieronimo anatafsiri 'mtu mwenye moyo na akili'. Alikuwa ndugu wa Mtume Yakobo mdogo tunavyosoma katika Injili na anavyosema mwenyewe katika barua yake ijulikanayo kama 'Barua ya Yuda'. Yuda alikuwa ameoa na kulima shamba lake ili kulisha familia yake, kabla Bwana Yesu alipomwita.

Baada ya Pentekoste, kadiri ya Dorotheo, askofu wa Tiro, Simoni alitumwa kuhubiri nchi ya Misri, Libya na Mauritania. Mt. Yuda pia akaenda Afrika, akihubiri Injili katika nchi ya Libya, Mauritania na sehemu ya Afrika Magharibi. Mt. Augustino anatuambia kwamba bara la Afrika lilipokea imani kutoka kinywa cha Mitume wenyewe. Ingawa walifanya kazi katika nchi zile zile inawezekana kwamba hawakufanya kazi kwa pamoja. Walihubiri mahali tofauti wakisaidia na wafuasi kadhaa miongoni wa Wafuasi 72.

Kadiri ya pokeo moja baada ya kuhubiri Injili katika Afrika Simoni alisafiri kwa merikebu kwenda Uingereza. Akawahubiria wapagani na akasulubishwa na wasioamini. Lakini inaonekana kwamba, kuliko kwenda Uingereza, alikwenda pamoja na Mtume Yuda Tadei kuhubiri Injili huko Asia. Mababu wengi wa imani wanatuambia kwamba walifariki huko mjini Suanir katika nchi ya Sarmatia, wakiuawa na makuhani wa wapagani.

Wat. Simoni na Yuda Tadei, mtuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

## Mt. Yohane wa Chozeba, 532.

Yohane kwa kuzaliwa kwake alikuwa Mmisri, mwenyeji wa Theba. Akalelewa katika imani ya umonofiziti na kuishi miongoni wa wamonofiziti. Tangu ujana wake alikuwa mtawa. Siku moja akaenda kuhiji Yerusalemu. Alipojaribu kuingia katika Kanisa la Mkombozi ili kuuheshimu Msalaba Mtakatifu, uwezo usioonekana ulimzuia kuingia. Usiku akasikia katika ndoto sauti ikimwambia: "Wale wasiokiri imani

[308] Rejea Mt 10:3

ya Kiorthodosi hawastahili kuuabudu msalaba mtakatifu wa Mwokozi wetu.' Yohane akaamka na kwenda haraka katika kanisa. Akalia na kukiri imani ya kiorthodoksi.

Hakurudi Misri, bali akakaa Palestina, akiishi katika pango mkoani mwa Chozeba. Huko akaishi katika upweke hadi siku moja wazazi wakamletea mwana wao aliyepagawa. Walitumwa kwa Yohane na Ananias, mwasketi mwenye sifa katika Palestina. Kwa unyenyekevu wake Yohane alijiona hastahili kumwombea ili kumfukuza pepo. Kwa hiyo aliomba kwa jina la Ananias, na kijana akapona. Ndipo uwezo wa Yohane wa kutenda miujiza ukajulikana na wengi walimwendea kwa ajili ya uponyaji wa kiroho na kimwili.

Ikatokea kwamba, kinyume cha mapenzi yake, alitawazwa kuwa Askofu wa Kaizaria. Lakini hakuweza kuvumilia kazi ya uaskofu akatoroka kukaa jangwani. Wengi walimwendea na ishara na maajabu yalitendea kwa njia ya maombi yake. Akafariki kwa amani mwaka 532, akiwa mzee sana.

Mt. Yohane wa Chozeba, utuombee na Mungu atukuzwe katika maisha yetu. Amina.

**Oktoba 29**

Sisi Wakatoliki tunamkumbuka, huko Kartago, Tunisia, Mt. **Felisiani**, mfiadini.[309]

Huko Pavie, mji wa Italia, kumbukumbu ya Mt. **Apiano**, aliyekuwa askofu huko Afrika. Inasemekana kwamba masalia yake yaliletwa kutoka Afrika hadi Sardinia, Italia, na Mt. Fulgensio, askofu wa Ruspe, alipokimbia dhiki ya Waharabu (*Vandals*). Kutoka Sardinia masalia yake yaliweka katika basilika ya Mt. Petro, Pavie.[310]

Huko Bukavu, Jamhuri ya ki-demokrasia ya Kongo, Wakatoliki wanamkumbuka Mtumishi wa Mungu **Kristofa Munzihirwa Mwene Ngabo**, Mtawa wa Shirika la Majesuiti, Askofu Mkuu wa Bukavu, aliyeuawa mwaka 1996.

Huko Misri, Wakoptiki wanawakumbuka Mt. **Petro III**, Patriarka, askofu wa 27 wa Aleksandria,[311] na **Sanisio II (***Shenudi II*), Patriarka, askofu wa 63 wa Aleksandria, Misri.

Huko Ethiopia, Wakristu wanawakumbuka Mt. **Bartholomeo** na **mke wake**, wafiadini. Waorthodoksi Tewahedo wanawakumbuka **Wenyehaki wa Al-Matra**, waliouawa na watu waovu, pengine waliuawa na Mfalme Yemraha.[312]

Waanglikana (*church of England*) wanamkumbuka Mtu wa Mungu **Yakobo Hannington**, askofu wa Afrika ya Kati na Mashariki, 1885.

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake! Amina.

## Mtumishi wa Mungu Kristofa Munzihirwa Mwene Ngabo, 1996

---

309 *Martyrologium Romanum,* ed. 2005.

310 *Acta Sanctorum* na *Les petits Bollandistes*

311 *Coptic Synaxarium: 2 Hatour.*

312 *The Ethiopian Rite Missal, Abba Emmanuel & Abba Brendan Cogavin, 2002, uk 186. Ethiopian Synaxarium: Tekemt 19.*



Mzee Kristofa alizaliwa Lukumbo, Jamhuri ya ki-demokrasia ya Kongo, mwaka 1926. Akafuata shule ya msingi iliyopo parokiani na chuo cha walimu, kabla ya kuingia seminari ndogo ya Mugeri. Akaendelea masomo yake katika seminari kubwa ya Nyakibanda, Rwanda na ya Moba, (zamani iliitwa Baudoinville). Akapadirishwa tarehe 17 Agosti 1958 huko Walungu, Jimbo la Bukavu. Akawahudumia waamini wa jimbo kwa miaka mitano. Baadaye akaomba kujiunga na Shirika la Majesuiti. Akaanza novisiati huko Djuma wakati uasi ulishambulia maeneo hayo. Wiki za mwisho ya maisha yake, kabla ya kufariki alieleza jinsi wenyeji wakiwa nyuma ya wachifu wao walipigana kwa nguvu kulinda mashamba na vijiji vyao. Akaweka nadhiri tarehe 8 Septemba 1965. Akaendelea katika masomo yake ya ki-teolojia huko Kinshasa na Ubelgiji. Akasoma mambo ya ki-jamii na uchumi.

Akaanza kazi yake ya kufundisha huko Bukavu katika Chuo cha ‘Bikira Maria wa Ushindi‘, na baadaye akapelekwa Zaire kuwalea wanafunzi Majesuiti huko Kimwenza. Wakati huo alikuwa paroko msaidizi wa parokia ya Chuo Kikuu. Wakati wanafunzi wote walilazimishwa kujiunga na jeshi, yeye, kwa hiari, akawafuata. Akakaa kambi la jeshi Mikondo na baadaye katika kambi la jeshi Tshatshi, huko Ngaliema. Mwaka 1973, Padri Munzihirwa akapelekwa Kinshasa kufanya kazi kwa CEPAS (*Centre d’Etudes pour l’Action sociale*) na kwa CADICEC (*Centre Chrétien pour les Dirigeants et Cadres des Entreprises*) na wakati huo kuwaongoza ki-roho mapadri vijana majesuiti. Kazi yake haikuzuia kuendelea kujifunza katika Chuo cha Lubumbashi na hata Ubelgeji. Na mwaka 1978 akateuwa na Padri mkuu wa majesuiti kuwa Gombera wa taasisi ya falsafa ya Mt. Petro Kanisio huko Kimwenza. Hakubaki muda mrefu, miaka miwili tu, kwa sababu, mwaka 1980, akachaguliwa kuwa Mkuu wa Majesuiti waliokaa Kongo, Burundi na Rwanda. Alipotimiza kazi yake kama Provincial, akateuliwa kuwa Askofu Msaidizi wa Askofu Pingisha, jimbo la Kasongo, na mwaka 1990 akawa Askofu wa Kasongo. Na mwaka 1994 akateuliwa kuwa Askofu Mkuu wa Bukavu.

Mwaka huu, 1994, wakimbizi wengi walikimbia Rwanda wakaingia Burundi kuokoa maisha yao. Kwa muda wa miaka miwili Askofu Kristofa akapendekeza njia ya amani katika nchi za Visiwa Vikubwa. Akionyesha tena na tena hatari ya nchi ya Burundi kupokea wakimbizi wengi zaidi kuliko nchi inavyoweza kupokea. Akatangaza, bila hofu, haki ya wote kupata mahali pa kuishi kwa amani. Akaendelea hivyo, hadi askari wa Jeshi la Rwanda (APR) wakamwua tarehe 29 Oktoba 1996, wakati aliporudi nyumbani baada ya kuwaokoa maisha ya wengi, kuwafariji waliokuwa wamekata tamaa, bila msaada wowote kutoka na watumishi wa Serikali. Yeye peke yake alikuwa amebaki kuwa sauti inajulishayo ulimwengu hali ilivyokuwa. Alipendekeza amani kati ya makabila, kama wewe ni Mkristo unayempenda Mungu lazima umpende jirani.[313] Aliwaalika wakazi wa Bukavu kutoondoka mjini, yoyote inayotukia, na watu walimsikia. Daima aliwakumbusha watu wa kila upande wajibu wao kuacha kupigana na kuwafukuza watu kutoka nchi yao, kubagua, n.k. Alijiweka upande wa maskini, watu wasio na sauti, wasio na uwezo wa kujitetea.
Alipenda kuitwa ‘Mzee‘, pengine ‘Mhudumu‘. Watu wengi wanasema kwamba yeye alikuwa shahidi. Damu ya Mzee Munzihirwa iliyomwagika ni mbegu ya amani kwa ajili ya Kongo na Visiwa Vikubwa. Alifariki akipiga vita, mwenye silaha ya Injili, sala na elimu yake. Aliuawa kwa sababu aliwashutumu wale waliokanyaga miguuni mwao haki za wanadamu.
Bila shaka Mzee Munzihirwa yupo mbinguni kwa sababu hapa duniani aliishi kama mtakatifu. Siku moja aliandika: “Tumaini ambalo Yesu Mfufuka anatuletea ni tumaini la kuwekwa huru, binafsi na kwa pamoja, uhuru wa mtu mzima, mwili, nafsi na roho. Lakini linadai watu wawe tayari kulipa bei: ‘*Mtu atakaye kuiokoa nafsi yake, ataipoteza; na mtu atakayepoteza nafsi yake kwa ajili yangu ataiona.*‘“[314] Amelipa bei. Kardinali Yosefu Tomko alisema: “Askofu Munzihirwa alifariki kama shahidi! Alikuwa nabii. Afrika, Jamhuri ya ki-demokrasia ya Kongo, Nchi zizungukazo Ziwa la Viktoria, hasa Jimbo Kuu la Bukavu

---

[313] Rejea Mt. 22:34-40.
[314] Mt 16:25

vilipotea lulu lenye thamani sana. Ole wale wanaofikiri kuweka kiti chao kaburini.“
Mtumishi wa Mungu Kristofa Munzihirwa, utuombee na Mungu atujalie amani katika bara la Afrika. Amina.

## Yakobo Hannington, askofu, shahidi, 1885

Yakobo Hannington alikuwa Mwingereza, mmisionari na askofu wa kwanza wa Kanisa la Anglikana katika Afrika ya Mashariki. Alizaliwa tarehe 3 Septemba 1847 katika mkoa wa Sussex, Uingereza. Baba yake, Charles Smith Hannington, alimiliki bohari. Mama yake alikuwa kwa maneno ya kijana Yakobo "mpole na mwema kuliko mama wengine wote walioishi". Hannington hakupenda sana shule. Alipokuwa umri wa miaka 15 aliacha shule na kuanza kushugulika kazi ya baba yake. Baada ya miaka akaingia katika jeshi na kupata cheo cha Meja. Kama afisa ya Jeshi alionyesha tabia yake nzuri ya uongozi.
Alipokuwa umri wa miaka 21 aliamua kuwa mtumishi wa Kanisa. Akajiunga na Chuo cha *St. Mary Hall, Oxford*. Alionekana kama alijiunga na Chuo kwa ajili ya kujifurahisha kuliko kujifunza, lakini mwaka 1872 mama yake alipofariki ndipo akaanza kubadilisha maisha yake. Tarehe 1 Machi 1874 akapata daraja la ushemasi na kuhudumia kanisa ndogo la Mt. Petro huko Trentishoe Devon. Mwaka 1875 akawa paroko wa parokia ya Mt. Jorji, Hurstpierpoint. Alibaki katika kazi hiyo hadi aliamua kwenda Afrika.
Mnamo mwaka 1882, Hannington alisikia mauaji ya wamisionari wawili katika eneo la Ziwa Viktoria. Jambo hilo lilimsukuma kuingia katika Shirika la CMS (*Church Missionary Society*). Akaondoka Uingereza tarehe 17 Mei na kufika Zanzibar tarehe 29 Juni 1882, akiwa mkuu wa msafara wa wamisionari saba. Lakini homa ikamshika na kumlazimisha kurudi Uingereza mwaka 1883. Mwaka 1884, alipopona, akapewa daraja la uaskofu wa Afrika ya Mashariki na mwezi wa Januari 1885, akiwa na umri wa miaka 37 akarudi Afrika. Jimbo lake lilienea kutoka pwani hadi Buganda. Akafika Freetown, karibu na bandari ya Mombasa, Kenya, akitafuta njia mpya kufika Buganda. Wapagazi wake walikuwa Wakristo ili kuepa njia ya watumwa wa ki-arabu. Alipoingia Busoga, wakati ule Wajerumani waliingia Afrika

ya Mashariki na Kabaka Mwanga, Mfalme wa Buganda, alikuwa na mashaka kuhusu nia ya Hannington. Akamzuia kupita Busoga, bali akamtumia mtumbwi kumchukua via Sukumaland. Hannington akakataa. Akafaulu kufika Ziwa Viktoria tarehe 21 Oktoba, lakini kwa amri ya Mfalme Mwanga II wamisionari wakafungwa na Wachifu wa Basoga.

Baada ya siku nane kufungwa, wapagazi wake, kwa amri ya Mfalme, waliuawa, na tarehe 29 Oktoba, Hannington mwenyewe alichomwa mkuki kwa pande mbili. Alipofariki, maneno yake ya mwisho kwa askari waliomwua yalikuwa: “Nenda, kamwambie Mwanga nilinunua njia kwenda Uganda kwa damu yangu“. Dhiki kubwa dhidi ya Wakristo iliendelea. Wengi waliuawa na wengine waliuzwa kama watumwa kwa Waarabu.

Mtu wa Mungu Hannington, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

**Oktoba 30**

Sisi Wakatoliki tunamkumbuka, Mt. **Eutropia**, mfiadini, Aleksandria, Misri. Alizoea kuwatembelea Wakristo waliofungwa gerezani kwa ajili ya imani yao. Aliwafariji na kuwatia moyo ili wavumilie mateso makali kwa ajili ya Yesu Kristo. Siku moja alikamatwa akiwatembelea mashahidi. Aliposimama mbele ya Hakimu alikiri kwa ujasiri imani yake kwa Yesu Kristo. Alipoteswa kwa kuchomwa kwa mishumaa, mtu akasimama karibu naye akituliza mateso yake kwa kumnyunyizia maji ili asisikie moto wa miali. Alifariki baada ya mateso makali, mnamo mwaka 250.

Huko Tangiers, Moroko, Mt. **Marseli**, ofisa ya jeshi, baba ya Wat. Klaudio, Luperko na Viktorio (mashahidi huko Leon, Hispania). Alimaliza ushahidi wake kwa kukatwa kichwa, Agrikulano alipokuwa liwali.[315]

Huko Afrika ya Kaskazini, kumbukumbu ya **Askari mia mbili na ishirini**, **Mashahidi** , manmo mwaka 482. Huko Misri, Wakatoliki wanawakumbuka, **Mashahidi kumi na watatu** walioteswa, mjini Aleksandria, wakati wa utawala wa Kaizari Desio, pamoja na Wat. **Juliano**, **Euno**, (Aleksanda, Cronion**)** na **Makari**.[316]

Huko Misri (pengine Ethiopia), kumbukumbu ya Wat. **Irene** na **Atanasi**, wafiadini.[317]

Huko Luanda, Angola, Wakatoliki wanamkumbuka **Umberto Nigrini**, Padri wa Shirika la *Divine Providence*, aliyeuawa mwaka 1999.

Wakoptiki wanawakumbuka Wat. **Atanasi** na dada yake **Irene**, wafiadini Ethiopia.[318]

Huko Ethiopia, Wakristu wanamkumbuka Mt. **Yohane Kolobos**.[319]

---

[315] *Martyrologium Romanum,* ed. 2005.

[316] *Roman Martyrology,* ed. 1956. Pengine baadhi yao : Dionisi, askofu, Feliksi, Petro, Kwinto, Urbano, Viktori na Vitalis.

[317] *Acta Sanctorum*

[318] *Coptic Synaxarium: 3 Hatour*

[319] *The Ethiopian Rite Missal, Abba Emmanuel & Abba Brendan Cogavin, 2002, uk 187. Ethiopian Synaxarium: Tekemt 20.* Wakatoliki wanamkumbuka tarehe 15 Septemba na Wakoptiki tarehe 9 Novemba.

Huko, Bamenda, Kameroun, kumbukumbu ya **Karolo Wesco**, Missionari wa Kanisa la Baptisti aliyeuawa mwaka 2018.

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake! Amina.

## Mt. Marseli, Mfiadini, 298

Tarehe kwa kuzaliwa kwake Marseli haijulikani, lakini aliishi katika karne la tatu. Alikuwa askari katika jeshi la Waroma, Akida wa Lejio ya Trajan, huko Hispania. Alipoongoka na kubatizwa alijua kwa hakika kwamba hataweza kuendelea kuwa askari Mroma.
Wakati wa sherehe ya Kaizari Dioklesiano iliyofanyika mjini Tangiers, Moroko, Marseli aliutupa chini mkanda wake wa kijeshi. Akatupa pia silaha zake na tawi la mzabibu, alama yake ya kuwa Akida. Kwa sauti kubwa akasema: "Mimi namtumikia Yesu Kristo, mfalme wa milele. Sitawatumikia tena makaizari wenu. Nadharau kuiabudu miungu ya ubao na ya mawe, kwani ni vipofu na bubu." Askari wenzake wakashtuka kusikia maneno hayo, na kiongozi wa sherehe akatoa amri ya kumtupa Marseli gerezani. Baada ya sherehe akaletwa mbele ya baraza, akaulizwa maana ya kuutupa chini ule mkanda wake wa kijeshi.
Akajibu hivi: "Mnamo tarehe 21 Julai, mbele ya bendera ya jeshi, nilitaja wazi kuwa mimi ni Mkristo, na kwamba nitaweza kumtumikia Bwana mmoja tu, naye ni Yesu Kristo, Mwana wa Baba Mwenyezi". Fortunati, mkuu wa baraza akamwambia: "Siwezi kuusamehe ujinga wako. Kwa hiyo nitamwarifu Kaizari."
Basi, Marseli alipelekwa mbele ya maafisa wa daraja la juu zaidi ili ahojiwe. Katibu wa baraza akasema: "Liwali Fortunati alitupelekea Marseli na kutuandikia barua. Ukitaka barua hiyo itasomwa. Barua ikasomwa:
" Mheshimiwa Aurelio Agrikulano, siku yenye heri kwa ulimwengu, sikukuu ya Makaizari, wakati tuliposherehekea, akida Marseli, akisukumwa na aina gani ya ujinga, kwa hiari yake, akang'oa mkanda, panga na alama ya madaraka yake na kuvitupa mbele ya Jeshi. Niliona vema kuupeleka kesi hiyo mbele yako."

Baada ya kusoma barua Agrikulano akamwuliza Marseli: “Je, ulisema maneno yaliyoandikwa katika barua hiyo?“
Marseli akamjibu: “Niliyasema“.
Agrikulano: “Je, uliyasema kweli kweli?“
Marseli: “Ndiyo, maneno yote“.
Agrikulano: “Ulitumikia kama akida?“
Marseli: “Ndiyo“
Agrikulano: “Ujinga gani ulikusukuma kutupa alama ya madaraka yako na kutamka maneno kama hayo?“
Marseli: “Hakuna ujinga kwa wale wanaomcha Mungu“.
Agrikulano: “Ulitupa silaha?“
Marseli: “Nilizitupa kwa sababu haiwezekani kwa Mkristo kutumikia katika jeshi la dunia, wakati alijiweka tayari kumtumikia Bwana Kristo“.
Agrikulano: “Lazima aadhibiwe kadiri ya sheria ya jeshi“. Na baadaye alisema: “Mwenendo wa Marseli unastahili adhabu kali, kwa kuwa alijishusha hadharani akitumia lugha ya kijinga. Basi, tumeamua auawe kwa kukatwa kichwa.“
Marseli: “Tumshukuru Mungu!“
Marseli alipopelekwa nje auawe, akamwambia: “Agrikulano, Mungu akubariki".[320]
Kasiani, katibu wa baraza, alikataa kuandika hukumu iliyotolewa. Akatupa kalamu yake nchini. Agrikulano, akikasirika, akainuka kutoka kiti chake na kumwuliza: “Kwa nini ulitenda hivyo?“ Kasiani akamjibu: “Hukumu uliyotolea siyo hukumu ya haki“. Mara Kasiani akafungwa gerezani. Baada ya mwezi mmoja akakatwa kichwa. Anakumbukwa tarehe 3 Desemba.
Mt. Marseli, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

[320] Kutoka maandishi ya hukumu yake. Rejea pia *Maisha ya Watakatifu*, chapa 1996, TMP Book Department, Tabora, uk. 383-384

**Oktoba 31**

Sisi Wakatoliki tunamkumbuka Mt. **Epimaki Pelusium**, mfiadini, Misri, wakati wa utawala wa Kaizari Desio (*Decius*).[321]
Huko Kenya kumbukumbu ya Mwenyeheri **Stefania Aurelia Mercede** (*Irene*), Sista wa shirika la Masista Wamisionari wa Consolata, 1930.
Huko Ethiopia, Wakatoliki wanawakumbuka Wat. **Aziriano, Epimaki, Felisisimi, Mimo**, wafiadini na **wenzao 6**; **Abaidusi** (*Abaidas au Abadias*), mlei, mwungama dini;[322] Wat. **Rogasiano**, **Vinsenti**, **Rustisiani**, wafiadini ; Mt. **Zakaria**, aliyejulikana kama Baba Mkuu.
Katika Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo, huko Kambi ya Nyamurangwe, Wakatoliki wanawakumbuka **Servando Mayor Garcia**, **Miguel Angel Isia Lucio**, **Fernando de La Fuente**, **Jorge Julio Rodriguez**, mabruda wa Shirika la wa Maristi, waliouawa mwaka 1996.
Huko Brazaville, Kongo, Wakatoliki wanamkumbuka Mtumishi wa Mungu Padri **Yohane Czuba**, mfiadini, mwaka 1998.

Huko Ethiopia, Wakristu wanamkumbuka Mt. **Yohane** wa **Yerusalemu** aliyefariki Ethiopia.[323] Mtu wa Mungu mama **Irene** (Irini) abasia wa Mt. Philopateer Mercurius, Kairo, 2006.

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake! Amina.

## Mtakatifu Epimaki, 250

Epimaki alikuwa mzaliwa wa Misri. Kwa miaka mingi aliishi maisha ya upweke huko mlima wa Pelusium. Wakati wa dhiki ya Wakristo huko Aleksandria, mnamo mwaka 250, Epimaki kwa wivu wake alifika mjini Aleksandria, akizibomoa sanamu za miungu wa uongo na kumkiri kwa ujasiri mkubwa kwamba Kristo ndiye Mungu. Kwa hiyo Mtakatifu huyu akakamtwa na kuteswa vibaya. Miongoni mwa watu walioangalia

---

[321] *Martyrologium Romanum,* ed. 2005.
[322] *Les petits Bollandistes*
[323] *The Ethiopian Rite Missal, Abba Emmanuel & Abba Brendan Cogavin, 2002, uk 187. Ethiopian Synaxarium: Tekemt 21.*

mateso ya shahidi huyu palikuwa mwanamke kipofu kwa jicho moja. Tone la damu ya shahidi lilimponya jicho lake. Baada ya mateso makali Mtakatifu alikatwa kichwa.
Mt. Epimaki, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

## Mwenyeheri Sista Irene Stefani, 1930.



Sista alizaliwa Italia, tarehe 22 Agosti 1891. Irene alikuwa mtoto wa tano wa familia ya watoto 11. Alibaki katika familia yake hadi akifika umri wa miaka 20, akisaidia kuwalea wadogo wake baada ya kifo cha mama yake. Alikuwa anasaidia pia kuwafundisha vijana katika parokia yake.
Mungu akamwita. Mwaka 1911 akawa mmojawapo wa kwanza kujiunga na Shirika la Masista Wamisionari wa Consolata, lililoanzishwa na Yosefu Allamano mwaka uliotangulia. Tarehe 29 Januari, 1914 akaweka nadhiri zake. Wakati huu aliandika maneno machache yanayojumlisha mpango wake wa maisha: ”Yesu tu, Pamoja na Yesu tu, Kuishi kwa Yesu tu, Kwa Yesu tu. Fanya hivi na utaishi”.
Mwaka uliofuata alitumwa kuenda Kenya, akafika Kenya mwaka 1915. Huko akaishi maisha ya umaskini, ya kazi ngumu na upweke. Moyo wake haukuja mipaka ya kujitoa kabisa kwa wengine akiwatangazia Habari Njema ya Yesu, Mwana wa Mungu, na Mwokozi wao.
Miezi michache baada ya kufika Kenya Vita vya Kwanza vya Dunia vikaenea katika koloni za Waingereza na Wajerumani katika Afrika ya Mashariki. Akajiunga na masista na mapadri wengine waliokuwa wanahudumia waliojeuriwa na wagonjwa hospitalini na kambini katika nchi za Kenya na Tanzania, wakati wa Vita.
Baada ya Vita, kwa miaka 10, alifanya kazi kama mmisionari katika misioni ya Gikondi, akijitoa kabisa kwa Wakikuyu. Aliwafundisha, aliwahudumia, aliwatembelea familia zao, akiwa tayari daima

kuwapokea, kuwasaidia, kuwashauri vijana ili waweze kuishi kikamilifu imani yao. Kwa hiyo waliomwita *Nyaatha,* kifupi kwa *Nyina wa tha,* maana yake 'Mama mwenye huruma na upendo'.
Mwaka 1930 ulikuwa mwaka mgumu kwa misioni. Sista Irene akajitoa mhanga, kwa ruhusa ya wakuu wake, kwa ajili ya misioni. Hakujua kwamba Mungu atamjibu mapema. Wiki mbili tu baadaye, tarehe 31 Oktoba 1930 akafariki baada ya kuambukizwa na ugonjwa wa tauni alipowahudumia wagonjwa walioteswa na ugonjwa huo. Masalia yake yanakaa sasa katika Kanisa la Masista wa Consolata, Nyeri. Kanisa la Nyeri na Kanisa la Torino, Italia, walianza mchakato wa kutangaza Sista Irene kuwa mtakatifu. Tarehe 23 Mei 2015, alitangazwa Mwenyeheri, wakati wa ibada kubwa huko Nyeri, Kenya, iliyoadhimishwa na Mwadhama Polycarp Kardinali Pengo.
Sista mwenzake, Gian Paola Mina aliandika maisha yake.[324] Huko Torino, Italia masista wa Shirika lake wakaanzisha Kituo, kinachochapisha vitabu kuhusu maisha yake. Huko Iringa, Tanzania, kuna pia Kituo kinachoitwa kwa jina lake.
Mwenyeheri Irene Stefani, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

[324] Gian Paola Mina, *Gli scarponi della Gloria* (Viatu vya utukufu).

**Novemba 1**

Sisi Wakatoliki tunaadhiisha leo sikukuu ya **Watakatifu wote**, ambayo Baba Mt. Bonifasio IV, baada ya kutabaruku Pantheon,[325] aliamua kwamba sikukuu hiyo ikumbukwe kila mwaka tarehe 13 Mei, katika mji wa Roma, kwa heshima ya Bikira Maria, Mama wa Mungu, na mashahidi wote. Baadaye Baba Mt. Gregory IV aliamua kwamba sikukuu hiyo iadhimishwe katika Kanisa nzima, siku ya 1 Novemba, kwa heshima ya Watakatifu wote.[326]

Waamini wa Kanisa la Anglikana, Lutheri na Moravian wanaadhimisha Sikukuu ya Watakatifu wote tarehe 1 Novemba au Jumapili ya kwanza ya Novemba.[327]

Huko Misri kumbukumbu ya pekee ya Wat. **Acha** mwungama dini na **Yohane** ndugu yake; Wat. **Kristato** na **Saturnino**, wafiadini huko Melitene, Misri; Mt. **Timotheo** (*Dometius*), mfiadini huko Benhor, Misri; **Primo**, Patriarka wa Aleksandria. Pia kumbukumbu ya Mt. **Chaesarii**, Shemani, shahidi Italia.[328]

Huko Ethiopia, Wakatoliki wanamkumbuka **Gabra-Maryam**.[329]

Huko Sudan, Wakatoliki wanamkumbuka **Anjelo Arpe,** Padri wa Shirika la Wamisionari wa *Comboni Fathers*, aliyeuawa mwaka 1946.[330]

Huko Ikela, Jamhuri ya ki-demokrasia ya Kongo, Wakatoliki wanamkumbuka **Karoli Weber**, Padri wa Shirika la M.S.C. aliyeuawa mwaka 1964.

Huko Fort Portal, Uganda, Wakatoliki wanamkumbuka Mtumishi wa Mungu **Vinsenti Mc Cauley**, Askofu, wa Shirika la Msalaba Mtakatifu aliyefariki Marekani, mwaka 1982.

---

[325] Pantheon lilikuwa hekalu kwa miungu wote ya uongo lililojengwa Roma, mwaka 27 K.K.

[326] *Roman Martyrology,* ed. 1956.

[327] Rejea maana yake katika utangulizi.

[328] Dict(ionary of Saints

[329] *The Ethiopian Rite Missal, Abba Emmanuel & Abba Brendan Cogavin, 2002, uk 188.*

[330] Rejea *Servans of the Gospel, witnesses in the footsteps of Saint Daniele Comboni in Sudan and South Sudan*, Paulines Publications Africa, 2014, uk.89-92.

Waorthodoksi wanawakumbuka Mt. **Kaizari Shemasi wa Afrika**, pamoja na **Padri mmoja wa Terracina**, Italia, Wafiadini, mnamo 284-305.

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake! Amina.

## Watakatifu wote

Siku ya leo tunakumbuka watakatifu wote wa Afrika, wanaojulikana na wasiojulikana. Tuwakumbuke Wakristo wote waliouawa kwa nyakati mbalimbali, wakati wa vita na wakati wa machafuko ya siasa, kwa sababu ya chuki ya Imani ya kikristo.

Tuwakumbuke wamisionari wengi waliofariki muda mfupi baada ya kukanyaga bara la Afrika kwa sababu ya homa, magonjwa na maisha magumu.

Tuwakumbuke wote walioishi maisha ya kujitoa kwa wenzao kwa kuwahudumia, hata kujisahau wenyewe, ili kuwapatia raha, amani na kuonja upendo wa Mungu. Akina mama wengi waliishi maisha kama hayo, maisha matakatifu.

Inafaa hapa kusimulia kwa kifupi habari za mwanamke Ivona kwa niaba ya wanawake wote wa Afrika au walioishi katika Afrika, na utakatifu wao haujulikani. Kwa njia ya wanawake kama hawa ukristo ulienea katika Afrika. Mbegu ya Neno la Mungu lilipandwa mioyoni mwa watoto wao tangu kuzaliwa kwao, likakua na kuzaa matunda.

Mama huyu alizaliwa Ufaransa mwaka 1906. Alikuwa mzaliwa wa kwanza kati ya watoto 12. Aliolewa na Aloisi, mzaliwa wa kwanza miongoni wa watoto 14. Walipofunga ndoa, yeye na mume wake walihamia Moroko. Wakaanza maisha yao wakilima sehemu ya ardhi iliyogawiwa na serikali ya Ufaransa. Watoto kumi wamezaliwa, wengine katika Afrika, wengine katika Ulaya. Vita vya Pili vya Dunia viliwakuta Moroko. Walilazimishwa kuacha kazi ya kilimo na Baba Aloisi akaajiriwa na serikali kama mtumishi mdogo.

Wakati wa vita maisha yao yalikuwa magumu. Chakula hakikupatikana kwa wingi. Kwa hiyo ilikuwa marufuku kuacha chakula chochote

katika sahani. Kama mtoto akiacha chakula katika sahani yake, mara moja aliambiwa kwenda kulala chumbani. Na baadaye chakula kilichobaki kiliwekwa tena mezani mbele yake hadi amalize chote. Lakini chakula kilichobaki katika sufulia kilisagwa na kuwekwa mezani jioni kama supu.

Kabla ya kuolewa Mama Ivona alihitimu kuwa Nesi Mkuu. Kwa sababu hiyo aliwatunza watoto wake wote katika afya nzuri. Siku moja miongoni mwa watoto, wawili waliugua, pamoja na wanafunzi wote wa darasa lao. Madaktari walishindwa kuwatibu kwa sababu hawakutambua waliumwa ugonjwa gani. Mama huyu akatambua ugonjwa, akawahudumia wanafunzi na wote wakapona.

Ivona alikuwa na akili na elimu kubwa kuliko mume wake. Aloisi hakuona wivu bali alimkabidhi kazi ya kuangalia nyumba na kuwalea watoto. Alipopata mshahara wa mwezi aliweka yote mezani. Ndipo Ivona alikuwa anagawa kadiri ya mahitaji ya familia: sehemu hiyo kwa chakula, hii kwa nguo, hii kwa ada za shule, hii kwa maburudisho ya Aloisi, n.k. Kwa njia hiyo na kujinyima anasa, ingawa mshahara ulikuwa mdogo, walifaulu kuwasomesha watoto wote hadi form IV.

Kila siku mume wake Aloisi alipokuwa anarudi nyumbani baada ya kumaliza kazi, yeye na mke wake walipashana habari za siku ile. Aloisi alieleza yote yaliyotendeka kazini, na Ivona yeye alieleza yote yaliyotokea nyumbani, habari za watoto, habari za jirani wagonjwa aliowatembelea, n.k. Baada ya muda Aloisi alienda kufanya kazi bustanini. Hawakubishana hata mara moja.

Mama huyu alikuwa mtu wa sala kinyume cha mume wake Aloisi. Kila siku jioni wote walipomaliza kula chakula, kabla ya kufanya kitu kingine chochote, walipiga magoti na akaongoza sala ya jioni. Kila Ijumaa ya kwanza ya mwezi Mama huyu aliongoza sala ya Moyo Mtakatifu wa Yesu, Mtawala wa familia: ”Moyo Mtakatifu wa Yesu, wewe uliyejumlisha Mt. Margareti Alakok, hamu ya kuzitawala familia za kikristo, tunakuja kwako leo hii kutangaza utawala kamili wako juu ya familia yetu … ” Kwa kweli Yesu alitawala familia hiyo na kuibariki. Watoto wanane walifunga ndoa kanisani, mtoto mmoja wa kiume akawa Padri na mmoja wa kike akawa Sista.

Wakati nchi ya Moroko ilipopata uhuru, mnamo mwaka 1956, iliwabidi kurudi Ufaransa. Huko Ufaransa, maisha yalikuwa magumu. Ingawa

Aloisi aliahidiwa na serikali kupata kazi, hakupata kazi na mshahara kwa miaka miwili. Ilimbidi Ivona aanze tena kufanya kazi ya unesi ili kulisha familia yake. Wakati ule Ivona akawa Katekista katika kijiji chake, kwa sababu ya uhaba wa mapadri. Aliwahudumia Wakristo wa kijiji chake hadi alipofika umri wa miaka 80 kwa kuongoza ibada ya Jumapili bila Padri na kuhubiri kila Jumapili. Miaka ya mwisho ya maisha yake aliugua na saratani ya mapafu. Aliteseka sana lakini hakulalamika. Akafariki kwa amani, mwaka 1990.
Ninyi Watakatifu nyote mnaoshiriki furaha ya mbinguni, mtuombee na Mungu atukuzwe hapa duniani daima na milele. Amina.

## Mtumishi wa Mungu, Vinsenti Mc Cauley, Askofu, 1982

Vinsenti, mtoto wa kwanza kati ya watoto sita, alizaliwa Marekani, mwaka 1906. Baba yake alikuwa mhandisi katika kampuni ya Simu, mama yake alikuwa mama wa nyumbani. Familia ilisali rozari kila siku. Baba yake alikuwa mmojawapo wa *Knights of Columbus*, mama yake alishiriki katika vyama mbalimbali vya sala.
Vinsenti alihudhuria shule Creighton, akahitimu na kuingia chuo kikuu cha Creighton kujifunza 'Sanaa na Barua'. Mwezi Novemba 1924 akajiunga na Shirika la Msalaba Mtakatifu. Tarehe 24 Juni, mwaka 1934 akapadirishwa.
Baada ya miaka miwili ya upadirisho alitumwa Bengali, bara la Asia, akisindikizwa na Padri mmoja na Mabruda wawili wa Shirika lake. Akafanya kazi kule hadi mwaka 1944. Lakini afya yake ilikuwa dhaifu. Mwaka 1944, wakati wa Vita vya Pili vya dunia, aliugua kwa ugonjwa wa Uvimbe wa mshipa. Akabaki hospitalini miezi miwili, kabla ya kurudishwa katika nchi yake Marekani. Akafanya kazi huko hadi aliweza kutumwa kwenda Uganda, mwaka 1958. Akafika Uwanja wa ndege wa ki-mataifa Entebbe, tarehe 4 Novemba, pamoja na mapadri watatu waliopadirishwa karibuni. Wakaanza misioni yao karibu na Fort Portal. Baada ya miaka mitatu Jimbo la Fort Portal likaundwa na Padri Vinsenti Mc Cauley akachaguliwa kuwa Askofu wake wa kwanza.
Alifanya kazi kubwa kama askofu katika jimbo lake. Alijitahidi kutamadunisha Imani na kupata mapadri wazalendo. Akawatetea wakimbizi kutoka Rwanda, Kongo na Sudan. Akajenga uhusiano kati

ya mapadri wa kila umri, kabila, lugha na shirika. Akawa mpatanishi kati ya makabila ya Jimbo lake. Alisaidia kuanzisha shirika la akina mama wazalendo na kuwaongoza katika utume wao. Hakusahau kuwasaidia walei kushika nafasi yao katika Kanisa mahalia. Tena alikuwa katika msitari wa mbele kutafuta umoja wa Wakristo.

Wakati wa Mtaguso wa Vatikano II, alichaguliwa kuwa Mwenyekiti wa *AMECEA* (*Association of Member Episcopal Conferences in Eastern Africa)*. Akawaongoza maaskofu wa Afrika ya Mashariki kuwa na sauti katika Mtaguso. Lakini hasa kwa miaka kadhaa, pamoja na Katibu wa Amecea, Padri Kilian Flynn, Ofm, alipanga chama cha Amecea, idara zake n.k. na kuweka misingi ya mapato na matumizi yake. Ni yeye aliyeanzisha *Gaba Pastoral Institute* kwa ajili ya Makatekista. Mwaka 1973, muda wake wa kuwa mwenyekiti ulipokwisha, akachukua nafasi ya Padri Kilian Flynn, kama Katibu wa Amecea. Akahamia Nairobi.

Hali ya afya yake ilikuwa mbaya. Kwa miaka mingi Askofu Mc Cauley aliteswa na saratani ya ngozi, usoni mwake. Kwa jumla, alipata upasuaji zaidi ya mara hamsini. Mwaka 1976, akapasuliwa na kuwekwa mkole wa plastiki moyoni mwake. Mwanzoni wa Julai 1982 akateswa na hemoraji katika mapafu yake. Mwaka uleule alirudi Marekani na wakati wa upasuaji alifariki tarehe 1 Novemba 1982.

Mwezi Agosti 2006, jimbo la Fort Portal, lilianza mchakato wa kumtangaza Mwenyeheri.

Mtumishi wa Mungu Vinsenti Mc Cauley, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

**Novemba 2**

Huko Moroko, Wakatoliki wanawakumbuka Wat. **Publio, Viktori, Hermesi**, na **Papiasi**, wote wafiadini, Moroko.[331]
Huko Bukoba, Tanzania, Wakatoliki wanamkumbuka Mtu wa Mungu **Abrahamu Kazigu**, Katekista aliyefariki mwaka 1953. Alizaliwa Muhutwe mwaka 1889 na anakumbukwa kwa sababu ya imani yake.
Huko Tanzania na Kenya,Wakatoliki wanamkumbuka Mtu wa Mungu **Florensia wa Yesu**, Sista wa Shirika la Masista wa Ivrea, aliyefariki mwaka 2004.

Huko Misri, Wakoptiki wanakumbuka **kutabarukiwa Kanisa la Bikira Maria** katika monasteri ya Mouharaque, mlimani mwa Kuesquam.[332]Pia wanawakumbuka **Wakristo 7** waliouawa na askari wa I.S. (*Islamic State*) walipoenda kuhiji katika Monasteri ya Mt. Samueli, mkoa wa Minya, Misri, mwaka 2018.
Huko Ethiopia, Wakristu wanamkumbuka Mt. **Yosefu**, Patriarka, wa 52 wa Aleksandria.[333] Waorthodoksi wa Ethiopia wanamkumbuka Mt. **Yäm'ata**, mmojawapo wa Watakatifu tisa.
Waanglikana wa Afrika ya Kusini (*Church of South Africa*) wanawakumbuka **Mashahidi wa Mbokotwana**, 1880.

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake! Amina.

## Mtu wa Mungu, Sista Florensia wa Yesu, 2004

Mpendwa sana Sr. Florensia Anna Ogutu alizaliwa kunako tarehe 27 Novemba 1979, mkoani Nyanza, Wilaya ya Homa Bay, nchini Kenya. Wazazi wake ni Mzee Silas Ogutu na Mama Teresia Aoko. Alibatizwa kunako tarehe 13/01/1980. Komunyo ya kwanza alipewa mwaka 1988. Aliimarishwa kwa sakramenti ya Kipa-imara kunako tarehe 13/11/1992.

---

[331] *Roman Martyrology,* ed. 1956.
[332] *Coptic Synaxarium: 6 Hatour.*
[333] *The Ethiopian Rite Missal, Abba Emmanuel & Abba Brendan Cogavin, 2002, uk 188..Ethiopian Synaxarium: Tekemt 23.*

Alihitimu shule ya msingi kunako mwaka 1994 na shule ya sekondari mwaka 1997.



Baada ya kuhitimu masomo ya sekondari, Sr. Florensia alijisikia wito wa kuwa mtawa katika Shirkia la Upendo la Bikira Maria Mkingiwa Dhambi ya Asili la Ivrea. Alionyesha nia hiyo waziwazi kwa viongozi wa Kanisa na baadaye alikubaliwa kujiunga na Masista hawa katika mwaka wa matazamio.
Alipelekwa kunolewa katika katekesi kwenye Chuo cha Makatekista Komuyge, kilichoko Jimbo Katoliki la Musoma, Tanzania, kwa kipindi cha mwaka mmoja. Kunako mwaka 1999 alipiga hatua na kujiunga na Upostulanti. Kunako mwaka 2000 aligundulika kuwa na uvimbe sehemu ya shingo, hali ambayo iliwafanya walezi wake kutia shaka na hivyo kuamua kumfanyia uchunguzi wa kina katika Taasisi ya Magonjwa ya Saratani, *Ocean Road*, Jijini Dar-es-Salaam. Lakini ugonjwa haukuweza kugundulika mara moja.
Ilipotimia tarehe 10/12/2001 alipelekwa katika hatua ya Unovisi, huko Miyuji, Jimbo la Dodoma, Tanzania. Wakati wa maadhimisho ya Sikukuu ya Paska, mwaka 2002, Sr. Florensia alihisi maumivu makali ya kichwa yaliyopelekea kutoka na damu puani. Hali hii ilizua wasiwasi miongoni mwa wanajumuiya na hivyo viongozi wa Shirika wakaamua kumpeleka Nairobi kwa uchunguzi na tiba zaidi. Alipofika huko aligundulika kuwa na saratani mbaya iliyokuwa imeanza kuenea kwa kasi mwili mzima. Alifanyiwa upasuaji na kuendelea na matibabu katika ngazi mbalimbali za tiba ya ugonjwa wa saratani.
Alikuwa kwenye mwezi wa sita wa mwaka wa kwanza wa Novisiati. Kwa ruhusa ya pekee ya Mama Generali aliweza kuendelea na malezi huko Nairobi na huko Veyula, pale alipoendelea kupata tiba yake. Kwa sababu hiyo alifunga nadhiri za kwanza tarehe 8/12/2003 katika Kanisa hili la Kristo Mfalme, Parokia ya Veyula.
Tiba hii ilimalizika hapo tarehe 10/09/2004. Na kwa muda wa miezi miwili alipewa mapumziko mafupi ili baadaye arudi Nairobi kwa

uchunguzi zaidi. Askofu Matthias Isuja Joseph wa Jimbo Katoliki la Dodoma, kwa ukaribu wake, alifika kumsalimu, kumpokea Uwanja wa Ndege wakati akirudi kutoka katika tiba. Kwa hakika alionyesha upendo wa kibaba.

Hali ya Sr. Florensia ilibadilika ghafla, kunako tarehe 20/10/2004. Alihisi uchovu mkubwa, shinikizo la damu pamoja na maumivu makali ya mwili. Tarehe Mosi, Novemba 2004 , akalazwa kwenye Hospitali ya Mkoa wa Dodoma. Jitihada kubwa zilifanyika na madaktari pamoja wauguzi, kuyaokoa maisha ya Sr. Florensia, lakini mauti ilikuwa inabisha hodi.

Jumuiya yake iliyompenda upeo, ilimwandaa kwa Sakramenti ya Mpako Mtakatifu, ili iweze kumfariji katika mapambano yake ya mwisho kiimani. Na tarehe 2 Novemba 2004, saa 10:15 aliaga dunia katika hali ya tabasamu, baada ya kupambana kwa imani thabiti na ugonjwa sartani kwa miaka mitatu.

Mpendwa wetu Sr. Florensia Ogutu anakumbukwa sana kwa uvumilivu katika hali yake ya ugonjwa. Aliupokea ugonjwa wake na kuuona kuwa ni sehemu ya mapenzi ya Mungu katika maisha yake. Kamwe hakulalamika. Alikuwa jasiri na mtu mwenye imani thabiti, daima tabasamu lilisheheni katika midomo yake. Alikuwa mtu wa sala na tafakari ya kina kwani, ilikuwa ni hamu ya moyo wake kuuona uso wa Mungu, ili aweze kupumzika makaoni mwake milele alipokuwa anakazana kujisafisha kwa njia ya Fumbo la Msalaba katika maisha yake.

Alipambana vikali, pale ubinadamu ulipomzidi na kutaka kuukimbia Msalaba, lakini kwa njia ya sala alishinda, na machozi yakanyauka katika uso wake. Alijiachia mikono mwa Mungu na daima aliomba mapenzi yake yafanyike katika maisha yake, sala ambayo mwanzoni ilikuwa ni ngumu kuipokea. Hata siku moja Sr. Florensia hakulalamika kwa maumivu ingawa yalikuwa makali na badala yake aliwaonea huruma wale waliokuwa wanamwuguza kwa moyo wa upendo wa dhati na wale waliofika kufanya hija katika madhabahu ya mahangaiko ya mwanadamu.

Mpendwa wetu Sr. Florensia alifanya sherehe ya Mtakatifu somo wake tarehe 27/10/2004. Aliwashukuru Masista wenzake kwa ukaribu wao na moyo wa sala uliomtia nguvu kusonga mbele pasipo kushindwa, katika

jitihada za kuyatimiza mapenzi ya Mungu. Hii ndiyo sala yake hadi mauti inamfikia.[334]

Mtu wa Mungu Sr. Florensia, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

[334] Kutoka *Wasifu wa Sr. Florence A. Ogutu, SCIC*, na Sr. Palma Porro, katika Ibada ya mazishi, tarehe 4/11/2004, Kanisani Veyula, Dodoma. Rejea kijitabu: "*God! You are so sweet*", Autobiography, Part I, written by Novice Florence A. Ogutu, SCIC. Na "*Cruel Sweetest Love*", written by Sr. Florence of Jesus after her Profession, 8/12/2003. Published by the Sisters of Ivrea, Veyula, Dodoma, Tanzania, 27th November 2005.

**Novemba 3**

Huko katika Jamhuri ya ki-demokrasia ya Kongo, Wakatoliki wanamkubumka Mtumishi wa Mungu **Akwilino Longo (***Bernardo***)**, Padri, mfiadini, 1964.

Huko Misri, Wakoptiki wanawakumbuka Mt. **Jorji**, mwenyeji wa Aleksandria, mfiadini; Mt. **Nehroua**, mfiadini; Mt. **Mina**, askofu wa Tamai (Thmoui).[335]
Huko Ethiopia, Wakristu wanawakumbuka Abba **Hilario** wa Gaza (Ablarius), mtawa na mwanakoriti; **Dabala-Maryam** (Sabla Mariyam).[336]

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake! Amina.

## Mt. Jorji wa Aleksandria, Shahidi

Baba yake alikuwa mgeni aliyeishi Aleksandria. Hakuwa na mwana. Wakati wa sikukuu ya kutabarukiwa Kanisa la Mt. Jorji, Shahidi, katika mji wa Lydda, tarehe 7 mwezi wa Khedar, akamsihi Mungu kumpatia mwana kwa njia ya maombezi ya Mt. Jorji. Mungu akasikiliza sala yake. Akapata mwana na akamwita Jorji. Mama yake alikuwa dada ya Armenio, gavana wa mji wa Aleksandria. Alipokuwa na umri wa miaka 15 wazazi wake walifariki. Akaenda kuishi na mjomba wake, na Jorji alipenda Kanisa. Armenio alikuwa na binti mmoja tu. Siku moja binti huyu aliendа pamoja na rafiki zake kujiburudisha. Akaona monasteri moja, nje ya mji wa Aleksandria, na kusikia watawa wakiimba nyimbo za kumsifu Mungu. Sauti ya nyimbo na sifa zao ziliingia moyoni mwake. Akamwuliza Jorji, mwana wa shangazi yake, kumwambia maana ya maneno ya nyimbo watawa walikuwa wanaimba. Na akaanza kumwelezea maana ya nyimbo na kuzifahamisha. Akamweleza pia

[335] *Coptic Synaxarium: 7 Hatour*.
[336] *The Ethiopian Rite Missal, Abba Emmanuel & Abba Brendan Cogavin, 2002, uk 188..Ethiopian Synaxarium: Tekemt 24.* Rejea *Coptic Synaxarium* tarehe 21 Oktoba.

adhabu itakayokuja juu ya wenyedhambi na amani na furaha vitakayowajalia wenye haki.

Aliporudi nyumbani mwa baba yake Armenio, mbele yake akamkiri Bwana Yesu Kristo. Armenio akaanza kumsihi na kumwambia: "Binti yangu, usifanye mambo hayo"; lakini hakumsikiliza wala kumtii. Kwa hiyo baba yake akawaamuru askari kumkata kichwa chake. Akapokea taji la ushahidi.

Watu fulani wakamwambia gavana: "Ndiye Jorji, mwana wa dada yako, aliyemdanganya binti yako. Gavana akamshika Jorji na baada ya kumtesa vibaya sana akamtuma katika mji wa 'Ensena, mahali ambapo wakamtesa vikali tena na baadaye wakamkata kichwa. Akapokea taji la utukufu katika ufalme wa mbinguni.

Sasa kulikuwa Shemasi mmoja, kwa jina la Samueli, akachukua mwili wake na kuupeleka kwa mji wa Manuf. Mke wa Armenio, kaka ya mama wa Mt. Jorji, alijua kwamba Jorji alikufa shahidi, akatuma ujumbe kuuchukua mwili wake na akuweka pamoja na mwili wa binti yake katika mji wa Aleksandria.

Mt. Jorji, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina

## Mtumishi wa Mungu, Akwilino Longo, Padri na mfiadini, 1964.



Alizaliwa tarehe 25 Agosti, 1907, Italia. Akaingia katika shirika la Moyo Mtakatifu wa Yesu (*Dahnians*). Akapadirishwa mwaka 1936. Miaka miwili baadaye alielekea Argentina, lakini kwa sababu ya matayarisho ya Vita vya Pili vya Dunia, aliamua kwenda Afrika, katika Jamhuri ya demokrasia ya Kongo, zamani iliyoitwa Zaire. Mwaka 1939 akaanzisha misioni katika kijiji cha Nduye, ndani ya msitu wa Ituri. Akaishi kule miaka 26 hadi kifo chake. Pole pole akajenga nyumba kwa mapadri, masista, shule kwa ajili ya wavulana na wasichana, zahanati na karakana kufundisha makanika.

Baada ya kupata uhuru nchi ikazama katika machafuko. Vikundi vya wanamapinduzi vikaenea popote. Miaka ifuatayo watu wengi waliuawa hasa na kikundi cha wanamapinduzi Simba. Siku moja, jioni, Padri

Longo alichukuliwa na WaSimba kutengeneza gari lao – alikuwa fundi kweli kweli – akarudi usiku wa manane. Akijua itakayotokea Padri Longo akamkabidhi Parokia kwa mlei mmoja Albert Dark pamoja na misioni na hostia ndogo katika tabernakulo.

Tarehe 29 Oktoba, WaSimba wakaja wakamchukua Padri na masista. Wakawaamuru kutembea kwenda Mambasa. Waliwaambia kwamba baada ya siku tatu masista wataachiliwa na baada ya siku sita Padri mwenyewe ataachiliwa. Ahadi zao kuhusu padri ilikuwa ahadi ya upepo. Askari mmoja akamjeruhi Padri kwa bunduki yake na kupasua mdomo wa juu. Bila dawa siku kwa siku uso wake ukaanza kuvimba.

Huko Mambasa wakafungwa gerezani, pamoja na wazungu wachache, watawa 4 wa Shirika la Ndugu Wadogo wa Mt. Karolo wa Foucauld. Gerezani wakateswa vibaya sana. Wakati ule misioni ikavamiwa na wakachukua Radio Call iliyokuwepo. Gerezani Padri Longo akapata nafasi kuungama kwa Padri mmoja wa Ndugu Wadogo wa Mt. Karolo wa Foucauld.

Tarehe 3 Novemba masista wakaachiliwa, na Padri Longo akasimama barazani mbele ya WaSimba. Akashtakiwa kuwa na Radio Call iliyopatikana katika misioni na kwa hiyo alistahiliwa afe. Komanda wa WaSimba alitangaza hukumu ya kifo chake mbele ya watu wa Mambasa, lakini wakapiga kelele kuonyesha kutokubali kwao kwa sababu Padri alipendwa sana. Hata hivyo mwishoni sauti ya Komanda ikawashinda. Askari wachache, wakibeba mikuki, wakamsindikiza Padri Longo hadi njiapanda. Mmoja akatupa mkuki wake na kumchoma Padri Longo kifuani. Akaanguka magotini mwake na kumbariki askari akisema: “Siyo kifo bali usingizi“. Akapigwa risasi, akafariki.

Padri Longo, utuombee na Mungu akatukuzwe daima na milele. Amina.

**Novemba 4**

Sisi Wakatoliki tunamkumbuka Mt. **Pierio**, padre wa Aleksandria, (Karne la IV), mwungama dini. Baada ya dhiki, aliishi huko Roma, alipofariki kwa amani.[337]

Huko Afrika ya Kaskazini, kumbukumbu za Wat. **Primo, Kaizari** (Caesarius Anda), **Perpetua, Porfirio, Publio, Kwarto, Saturo, Viktori, Viktorina,** wote wafiadini.

Huko Ethiopia, Wakristu wanamkumbuka Abba **Apolo** (‘Ebloy). Waorthodoksi Tewahedo, pia wanakumbuka **Kutabarukiwa Kanisa Mt. Julius wa ‘Akpahos** (Acfaha), mfiadini.[338]

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake! Amina.

## Mt. Pierio, Mwungama dini, 309

Pierio aliishi wakati wa makaizari Karo na Dioklesiani walipotawala, wakati wa Patriarka Theonas, askofu wa Aleksandria, Misri. Akapadirishwa katika karne ya III na Mt. Theonas. Akahudumu katika Kanisa lake kama mkuu wa Shule ya Katekesi ya Aleksandria. alikuwa mhubiri maarufu. Alikuwa msomi wa Maandiko Matakatifu, mwenye moyo safi, na hodari katika falsafa ya kikristo. Ndiyo maana alipewa jina la “Origene mdogo“.

Aliishi maisha masahili akishikilia shauri ya ufukara. Aliandika vitabu viwili, kimoja kihusucho mambo ya Paska na kingine kihusucho nabii Hosea. Lakini hadi leo vitabu viwili hivyo vimepotea. Vipande vipande tu vimetufikia.

Mababu zetu wengine walisema kwamba alikufa shahidi, lakini Mt. Hieronimo anatuhakikishia kwamba aliendelea kuishi baada ya dhiki ya

---

[337] *Martyrologium Romanum,* ed. 2001.

[338] *The Ethiopian Rite Missal, Abba Emmanuel & Abba Brendan Cogavin, 2002, uk 189..Ethiopian Synaxarium: Tekemt 25.*

Dioklesiani na akaenda kuishi Roma hadi kifo chake, mwaka 309. Ingawa hakuuawa aliteseka sana kwa ajili ya Yesu Kristo.[339]

Mt. Pierio, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

[339] Rejea Mt. Hieronimo, *De viris illustribus*, Sura 76

**Novemba 5**

Huko Emese, Fenisia, Wakristo wanamkumbuka Wat. **Galasioni** na **Episteme**, mke wake, mashahidi, Emese (au Aleksandria), mnamo mwaka 253.[340]
Huko Gulu, Uganda, Wakatoliki wanawakumbuka **Pierina Asienzo** na **Dorotea Akweyo**, Masista wa Shirika la Wadogo wa Maria Immakulata, waliouawa mwaka 2000.

Waorthodoksi wanawakumbuka Wat. **Galasioni** na mke wake **Episteme**, watawa na mashahidi. Pia wanamkumbuka Mt. **Gregori**, Mwungama-dini, Patriarka wa Aleksandria, Karne la IX.
Huko Misri, Wakoptiki wanamkumbuka Patriarka Abba **Isaka**, askofu wa 41 wa Aleksandria.[341].

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake! Amina.

## Watakatifu Galasioni na Episteme, Mnamo 253

Wakristo hawa wanaheshimiwa katika Kanisa la Orthodoksi kama Watakatifu walioishi Sinai. Katika kitabu cha *Les Petits Bollandistes*, wanaheshimiwa kama mashahidi, huko Emese, Fenisia (*Phénicie*).
Galasioni alikuwa mwana wa wazazi wapagani Keitofoni na Leucippa. Ingawa waliwatolea sadaka nyingi miungu ya uongo, walibaki bila kupata mtoto. Kwa neema ya Mungu, walishauriwa na Padri mmoja kumwomba mtoto kwa Mungu wa Wakristo. Galasioni akazaliwa na kulelewa kikristo. Wazazi wake wakabatizwa.
Galasioni akamwoa Episteme, pia aliyezaliwa na wazazi wapagani, na kumbatiza. Walipomtolea Mungu ubikira wao, wakatumia muda wao kumwabudu Mungu na baadaye wakaanza kuishi kama watawa. Wakakaa huko Sinai, pamoja na wafuasi wao, ili wamtumikie Mungu katika maisha yao na kuepuka dhiki iliyosababishwa na Kaizari Desio,

[340] Les Petits Bollandistes
[341] *Coptic Synaxarium: 9 Hatour.*

dhidi ya Wakristo. Lakini walikamatwa na Warumi. Wakapelekwa mbele ya Gavana Urso na kuulizwa kuhusu imani yao. Wakateswa vikali, kwa kupigwa, kuingizwa mianzi iliyochongwa, chini ya kucha za mikono yao, kujeruhiwa viungo vya ulimi, mikono na miguu. Mwishoni wakauawa katika uwanja wa michezo wa mji Aleksandria. Galasioni alikuwa na umri wa miaka thelathini na Episteme miaka kumi na sita.

Watakatifu Galasioni na Episteme, mtuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

**Novemba 6**

Sisi Wakatoliki tunamkumbuka Mt. **Feliksi wa Toniza**, mfiadini, Tunisia. Baada ya kumkiri Yesu Kristo, akafungwa gerezani. Hukumu yake ikaahirishwa, lakini kesho yake walimkuta amefariki gerezani, kama Mt. Augustino anavyotueleza alipowafafanuilia Wakristo maana ya Zaburi moja.[342]
Huko Buhimba, Goma, Jamhuri ya ki-demokrasia ya Kongo, Wakatoliki wanawakumbuka **Konstantino Gatuku Kanyamihigo**, **Andrea Munyankuyo**, mapadri wa Jimbo la Goma, **Laurensia Sebarija Nyirangumliza**, sista wa Shirika la Mt. Vinsenti wa Roeselare, waliouawa mwaka 1966.
Huko Shinyanga, Tanzania, Wakatoliki wanamkumbu **Aloisi** (Aloisius) **Balina**, Askofu, aliyefariki mwaka 2013.

Wakoptiki wanamkumbuka Anba **Markia**, mtawa.[343]
Huko Ethiopia, Wakristu wanawakumbuka Abba **Makari**, askofu wa mji wa Thaw; **Makari** wa kijumba (au na Paul wa kijumba na **Juliano** mwenzake), wafiadini.[344]

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake! Amina.

## Abba Makari, askofu wa Thaw

Wakristo wa Ethiopia wanamkumbuka Abba Makari, Askofu wa mji wa Kaw (au Thaw). Kitabu cha Watakatifu wa Ethiopia wanatupasha habari hiyo kwa macho ya Wakristo ambao hawakupokea maagizo ya Mtaguso wa Kalsedoni.
Katika yeye maneno ya Nabii Daudi yametimizwa: "*Heri mtu yule asiyekwenda katika shauri la wasio haki; wala hakusimama katika njia ya wakosaji; wala hakuketi barazani pa wenye mizaha. Bali sheria ya*

[342] *Martyrologium Romanum,* ed. 2005.
[343] *Synaxarium Arabic-Jacobite*
[344]*The Ethiopian Rite Missal, Abba Emmanuel & Abba Brendan Cogavin, 2002, uk 190. Ethiopian*

*Bwana ndiyo impendezayo, na sheria yake huitafakari mchana na usiku.*“ Zab 1:1-2. Mtakatifu huyu alishika amri za Mungu. Akatumia talanta zake na kuzalisha faida. Ishara na maajabu mengi Mungu aliyatenda kwa mikono yake! Kuhusu yeye inasemekana kwamba wakati alipokuwa katika mji wa Kaw, kila mara alipoketi kuwafundisha watu alilia daima. Mfuasi wake mmojawapo, aliyempenda sana, akamsihi kwa kusema: “Kwa nini unalia daima, baba yangu?“ Kwa sababu ya maneno ya mfuasi wake mpendwa alijibu: “Nalia ninapoona madhambi ya watu na uovu wa matendo yao; kama mafuta inavyoonekana juu ya kioo.“

Wakati mwingine alimwona Bwana Yesu Kristo akiketi juu ya altare na malaika wakimletea matendo ya kila mtu. Na akasikia sauti ikisema: “Askofu, kwa nini unajificha kwa watu? Kwa nini usiwakemee na kuwafundisha?“ Na askofu akasema: “Bwana wangu, hawapokei maneno yangu.“ Na Bwana akamwambia: “Ni haki kwa askofu kuwakemea na kukaripia watu na kuwafundisha; na kama hawapokei maneno yake, damu yao iwe juu ya vichwa vyao.“ Ndiyo maana Mtakatifu huyu alikuwa analia daima.

Akaitwa kwenda pamoja na Abba Dioskoro kwa Mtaguso wa Kalsedoni ulioitishwa na Kaizari Marsiani. Alipofika katika ikulu, askari walimzuia kuingia, kwa sababu ya mavazi ya kimaskini. Abba Dioskoro akawaambia: “Mleteni ndani, kwa sababu yeye ni askofu“. Alipoingia na aliposikia maneno yaliyosemwa kuhusu Bwana, kwamba alikuwa na hali mbili, mtakatifu huyu akakasirika, akamlaani Kaizari Marsiani katika mtaguso. Akazungumza na Kaizari bila hofu kwa sababu aliacha imani ya kweli. Kaizari akawahamisha yeye na Askofu Dioskoro kwa kisiwa cha Gagra. Kutoka Gagra, Dioskoro akamtuma pamoja na mwamini fulani kwa mji wa Aleksandria na kumwambia maneno ya unabii: “Utapokea taji la ushahidi“. Askofu Makari alipofika Aleksandria, barua kutoka Kaizari Marsiani ikamfikia pamoja na hati ya Nasadiki ya Mtaguso wa Kalsedoni, kwamba ndani ya Kristo kuna hali mbili. Kaizari aliamuru wajumbe wake kwamba: “Kwanza atoe sahihi katika hati ya Nasadiki na baadaye umtawaze kama Askofu wa Aleksandria.“

Katika mji wa Aleksandria kulikuwepo padri mmoja, mwasi, kwa jina ‘Abrotari. Akachukua hati hiyo na akatamani kuandika jina lake. Abba

Makari akamwambia: "'Abrotari, kumbuka neno Abba Dioskoro alikuambia alipokimbia mji wa Aleksandria: "Utatawala Kanisa baada yangu". 'Abrotari alikumbuka maneno ya Abba Dioskoro na hakutaka kutoa sahihi katika hati hiyo. Kaizari Marsiani akapata habari kwamba Askofu Makari hakuamini imani iliyotangazwa huko Kalsedoni na hakutaka kutoa sahihi juu ya hati. Aliposikia jambo hilo Kaizari akakasirika na akaamuru Askofu Makari kupigwa ki-sirisiri na mara Askofu Makari alifariki na kupokea taji la ushahidi.
Waamini wakamchukua mwili wake na kumweka pamoja na miili ya Mt. Yohane Mbatizaji na Elisha, nabii. Sasa Abba Makari aliona katika maono kwamba watakatifu hawa walimwambia: "Mwili wako utalazwa pamoja na miili yetu". Na mwili wa Mtakatifu Abba Makari akawa pamoja na mwili wa Abba Makari Mkuu na Makari wa Aleksandria katika monasteri ya Shete. Mke wa gavana alipoweka mkono wake juu ya uso wa mwili wa mtakatifu huyu mara akatakaswa na ukoma wake na akawa mzima.[345]
Mtakatifu Makari, utuombee na Mungu atujalie umoja wa imani katika Kanisa. Amina.

## Mt. Anba Markia

Wakoptiki wanamheshimu Anba Markia kama nyota moja ya mji Aleksandria. Markia akaenda kuishi jangwani. Akabaki huko muda mrefu na kuishi kama masketi, akijikania kwa kufunga na kukesha. Adui wa wokovu wa wanadamu akampiga vita, akitumia silaha yake ya kinenani, kwa kumletea mawazo machafu, usiku na mchana, kwa muda wa miaka 15. Akafikiri moyoni mwake: "Markia, sasa ni miaka 15 unapigana na Adui. Amka, nenda katika mji wa Aleksandria, ujifanye kuwa kichaa kwa ajili ya upendo wa Mungu." Basi akaenda Aleksandria, akaishi kama mwenye kichaa, akitembeatembea katika mitaa yote, akidharauliwa na wote. Fedha aliyopokea aliwagawia maskini. Alisali na kufunga daima. Yeyote aliyemwona alimfikiria kuwa kichaa. Wengi wapumbavu walimfuata nyuma yake.
Ikatokea kwamba Anba Danieli, kama desturi yake, akafika Aleksandria kuadhimisha pamoja na Patriarka sikukuu ya Paska.

[345] *Synaxarium: Tekemt 27.*

Akamwona mtakatifu huyu akitembea uchi na kufuatana na watu wengi. Alikuwa anatembeatembea mitaani mchana na kulala usiku katika hamamu. Alipomwona akamwambia mfuasi wake: “Nenda, mwanangu na upate habari mpumbavu huyu anakaa wapi.“ Mfuasi akaenda na kuelezwa kwamba kichaa huyu alikuwa anaishi katika hamamu.

Anba Danieli akamwendea Patriarka na kuzungumza naye kuhusu mambo ya Mungu. Alipomaliza akatoka na akakutana na kichaa. Mzee Danieli akamshika mara na kusema kwa sauti kubwa: “Karibuni, ninyi wakazi wa mji, mtazameni mtumishi wa Mungu.“ Mara watu wakamkusanyika na kumzunguka mzee Danieli wakimwambia: “Baba, umwache, au atakuumiza kwa sababu ni kichaa.“ Anba Danieli akawajibu: “Ninyi ni vichaa. Hakuna mashambani au mjini, mtakatifu kama huyu.“ Mara akamshika na kumpeleka kwa Patriarka na kumwambia: “Baba, hakuna katika karne hii mtu kulingana naye“. Mara Patriarka akatambua kwamba Danieli alifichua siri yake. Basi wakajinyenyekea mbele yake na kumwomba awaambie sababu ya kuishi kama kichaa. Alitaka kuepa kuwajibu, lakini hakuweza. Akawaambia: “Mimi ni mtawa, na vishawishi vya zinaa vilinishika. Niliondoka na kwenda katika mji huu. Niliishi kama kichaa kwa ajili ya upendo wa Mungu. Tangu miaka minane nipo mjini, nikisali na kufuata sheria ya utawa. Nafunga na usiku nakesha.“ Waliposikia maneno hayo wakalia. Siku ile Danieli akakaa kwa Patriarka.

Kesho yake Danieli akamwambia mfuasi wake: “Mwanangu nenda kumtafuta Markia atuombee ili tuende jangwani.“ Mfuasi alifika penye hamamu Mtakatifu alipoishi, akamkuta amelala katika Bwana. Akarudi na kumtaarifu Baba yake. Danieli akamtaarifu Patriarka. Huyu akawapasha habari katika monasteri, na watawa wengi, kutoka Shete na mahali pengine wakafika wakishika mikononi mwao matawi ya mizeituni. Wakamheshimu sana, wakimpulizia manukato mazuri sana, hata wakashindwa kumzika kwa muda wa siku tano. Siku hiyo ya mazishi, wenyeji wa mji wakamsindikiza wakishika mikononi mwao mishumaa na manukato. Wakamzika mtumishi wa Mungu kwa furaha na machozi.

Miujiza mingi ikafanyika kwa njia ya mwili wake: wagonjwa wakapona, pepo wakakimbia, wenye kuteswa wakapata raha.

Wakamzika kwa heshima kubwa, wakimsifu Mungu anayewatukuza wale wanaompenda na kutimiza mapenzi yake daima. Duniani Mungu anawatukuza na mbinguni anawakaribisha katika utukufu wake. Mungu atuhurumie hadi siku ya mwisho.

Mt. Anba Markia, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

**Novemba 7**

Huko Misri, Wakatoliki wanamkumbuka Mt. **Achillas**, askofu wa Aleksandria, aliyesifiwa sana kwa sababu ya elimu, imani na utakatifu wa maisha yake,[346] 313 B.K. Akawa Patriarka wa Aleksandria kwa muda wa miezi michache tu.
Huko Kamerun (Cameroon), kumbukumbu wa Mtumishi wa Mungu **Henriko** (Heinrich) **Vieter**, askofu, 1914.
Huko Sudan, wanamkumbuka **Amalia Andeis**, sista wa Shirika la Masista Wamisionari wa Comboni, alifariki gerezani, akifungwa na jeshi la Mahdiya, 1882.
Huko Ziguinchor, Senegal, Wakatoliki wanamkumbuka **Simeoni Coly**, 40, Padri wa Jimbo la Ziguinchor, aliyeuawa na wagaidi, mwaka 2001.

Wakoptiki wanakumbuka kwamba siku ya leo Mtaguso ulikusanyika Roma ili kuamua kwa pamoja tarehe ya kufunga wakati wa Kwaresima.[347]
Huko Ethiopia, Wakristu wanamkumbuka Mt. Abba **Yam'ata**, mmoja wa Watakatifu Tisa.[348]

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake! Amina.

## Mt Achillas, askofu, 313.

Achillas alikuwa mtawa huko Shete, mmojawapo wa watawa mashuhuri wa wakati ule. Abate Theodori wa Pherme alimnenea: "Alikuwa kama simba huko Shete, kutisha kwa namna yake". Tunayo maneno machache aliyotamka na yaliyokusanywa katika misemo ya mababu wa imani walioishi jangwani. Kwa mfano, "Mzee mmoja akamwendea Abate Achillas na akamkuta akitema damu. Akamwuliza: 'Ni nini baba?' Achillas akamjibu: 'Ni neno aliloniambia ndugu mmoja

---

[346] *Roman Martyrology,* ed. 1956.
[347] *Coptic Synaxarium: 10 Hatour.*
[348] *The Ethiopian Rite Missal, Abba Emmanuel & Abba Brendan Cogavin, 2002, uk 190. Ethiopian Synaxarium: Tekemt 28*

na limeniumiza. Nilishindana ili nisimwambie, na nilimwomba Mungu aniondoe neno hilo moyoni. Neno likawa kama damu kinywani mwangu na nililitema. Na Sasa najisikia amani.'" Alisema pia: "Uwe kama mnyama, ili katika yote unayofanya usijulikane."
Kadiri ya maneno yake alionekana kama mtu amejaa hekima na upendo. Sifa yake imeenea mahali pengi. Baada ya Askofu Petro wa Aleksandria kufariki shahidi, Achillas alichaguliwa kushika nafasi yake. Achillas alimpadirisha Ario, aliyeanzisha uzushi wa Arianism. Achillas alipotambua mahubiri potovu ya Ario, akaanza kumpinga ili kulinda ukweli wa Imani Katoliki. Mtaguso, uliokusanyika huko Aleksandria, ulimhukumu Ario. Ario akatoroka kwenda Palestina. Achillas hakuishi muda mrefu, akawa Askofu wa Aleksandria kwa miezi michache tu.
Mt. Achillas, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

## Mtumishi wa Mungu Henriko (Heinrich) Vieter, askofu, 1914.

Henriko alizaliwa tarehe 13 Februari 1853, huko Cappenberg, North Rhine-Westpahlia, Ujerumani. Baada ya kufanya kazi ya seremala, mwaka 1883 alijiunga na Shirika la Pallotine huko Masio. Akajifunza teolojia Roma kwa miaka mitatu, akapadirishwa tarehe 8 Mei 1887. Kwanza alitumwa kufundisha katika Seminari ya Masio. Baada ya miaka mitatu alitumwa Kamerun, koloni ya Wajerumani.
Henriko Vieter akateuliwa kuwa Vika wa kitume katika maeneo hayo. Akisindikizwa na wamisionari saba akafika Kamerun na kukaa Douala. Lakini kwa sababu ya ugomvi wa wamisionari wa Kanisa la Presbiteri akaondoka na kujenga kijiji cha Marienberg, karibu na Edea. Baada ya miaka 14 ya kujenga shule na misioni, akawa Vika wa kitume wa kwanza wa Kamerun, tarehe 24 Desemba 1904. Baba Mtakatifu Pio X akamchagua kuwa askofu *in partibus* wa *Paraetonium*. Akapata daraja la uaskofu tarehe 22 Januari 1905.
Wakati chifu Martin-Paul Samba, wa kabila la Boulou, alihukumiwa kunyongwa kwa sababu ya usaliti, alijaribu kuwazuia Watawala kutimiza amri hiyo. Akashindwa. Wakati wa miaka ya mwisho wa maisha yake aliteswa na magonjwa ya nchi hiyo na akafa mnamo

mwaka 1914, uaskofuni mwa Yaoundé. Mkutano mkubwa akahudhuria mazishi yake.

Askofu mkuu wa Yaoundé, wakati wa kusherehekea miaka mia ya kuunda Vikariati ya Kamerun alianzisha mchakato wa kumtangaza Mtakatifu, mwaka 2005.

Mtumishi wa Mungu Henriko Vieter, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

**Novemba 8**

Huko Msumbiji, Wakatoliki wanamkumbuka Mtu wa Mungu **Alberti Patia Joäo**, Mkatekista, aliyefariki mwaka 1979.[349]
Katika Jamhuri ya ki-demokrasia ya Kongo, huko Yamboyo Basanku, Wakatoliki wanamkumbuka **Bartolomeo Santbergen**, Padri wa Shirika la Mill Hill, aliyeuawa mwaka 1964. Huko Tshumbe, Wakatoliki wanamkumbuka **Roberti Lomomba Ndjeka**, padri wa Jimbo la Tshumbe, aliyeuawa mwaka 1997.
Huko Mapere, Kivu Kaskazini, wanamkumbuka **Kristiani Bakulene**, Padri, aliyeuawa kwa sababu yeye ni Padri, mwaka 2010.
Huko Musenyi, Burundi, Wakatoliki wanamkumbuka **Berthilda Ndayishimiye**, Sista wa Shirika la Bene-Tereziya, aliyeuawa mwaka 1999.

Waorthodoksi wa Ethiopia wanamkumbuka Mt. **Samueli wa Dabra Wagag**, karne la XIV.

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake! Amina.

## Mt. Samueli wa Dabra Wagag.

Mtakatifu huyu hajulikani nje ya nchi yake Ethiopia.[350] Samueli alizaliwa mnamo mwaka 1350. Kama Anna, katika kitabu cha Samueli, alivyotamani kupata mtoto, vivyo hivyo wazazi wa Samueli Andra na Arsonwa walitamani kupata mtoto, lakini walikwisha fika uzee, bila tumaini la kufanikiwa. Hata hivyo baada ya kutembelewa na Mtakatifu Haymanot, Arsonwa akapata mimba na kumzaa mwana. Mtoto,

[349] Rejea Fr. Neno Contra,, Louis Kalonji, *African Lay Martyrs*, New People Media Centre, 2009, uk. 54-55.
[350] Mtakatifu huyu hajulikani sana nje ya nchi yake Ethiopia. Namshukuru Mungu kwamba karibuni hivi maisha yake yalitafsiriwa kwa Kifaransa na Stanislas Kur, *Actes de Samuel de Dabra Wagag*..

inasemekana, alizaliwa ameshika Ekaristi katika mkono wake wa kulia. Mtakatifu Haymanot alimbatiza na kumwita Samueli.
Samueli alipokuwa na umri wa miaka saba, alitazamiwa kuwa mkubwa wa kutosha kujifunza. Akaacha nyumba yake na kwenda katika monasteri moja pamoja na Teklat Haymanot, mwalimu na baba yake wa kiroho. Akapata daraja la ushemasi na kupadirishwa. Baada ya kuwa mtawa akamwacha mwalimu wake na kuenda kuishi kwenye mkoa wa Yagmu, ulioitwa baadaye Wagag, maana yake ‘mapambazuko‘. Huko akajenga kanisa lake la kwanza lililoitwa Hagere Maskal, maana yake ‘Jumuiya ya Msalaba‘.
Zamani za baba yake, Mfalme Amda Seyon I wa Ethiopia akamfukuza Teklat Haymanot na wafuasi wake, kwa sababu walishutumu kufunga ndoa na hawara wa baba yake. Andrea alifukuzwa huko Krestos Fatar. Baada ya kuishi maisha kama mtawa akaitwa tena na Mfalme. Lakini safari hii aliteswa naye pamoja na wenzake na baadaye akahamishwa. Alifariki njiani na kuzikwa Enasedestey. Mfalme Dawit I alipotawala, Samueli aliweza kuzuru kaburi la baba yake na kujenga kanisa ndogo, kwenye mlima wa Tabot.
Mwokaji wa Mfalme Dawit I akamwendea Samueli kuomba msaada wake, kwa sababu aliunguza mikate ya Mfalme. Samueli akamfariji na kumwambia kuwa na imani. Mfalme alipotambua kwamba mikate yake imeungua, akakasirika na kuamuru mwokaji apigwe mijeledi. Mjeledi ulipokaribia kugusa mgongo wa mwokaji ukavunjika vipande viwili. Chakari akachukua kipande kimoja na kujaribu mara ya pili lakini mjeledi ukavunjika tena. Chakari alijaribu tena na tena, akashindwa. Mfalme aliposikia kwamba mwokaji alilindwa na maombi ya Samueli, akatulia na kumhurumia mwokaji.
Mfalme Dawit I akamteua Samueli awe Patriarka juu ya nchi ya Endagabton. Basi Samueli, njiani, alienda kumsalimia mama yake. Arsonwa alikuwa mwanamke mzee sana. Samueli akamweka katika monasteri ya Wagag, akawa mtawa na akabaki huko hadi alipomaliza maisha yake. Samueli akamwomboleza siku arobaini, mchana na usiku, na baadaye akajitakasa katika mto Setal. Alipoingia majini, akagundua hila ya pepo Qwetel, kwa umbo la kamba ya urefu wa mita arobaini. Akasali na kufukuza pepo. Akatoa kamba kutoka majini na kuitumia kutengeneza upya paa la kanisa lake.

Baada ya kujenga Hagere Maskal, Samueli alijenga makanisa mahali popote aliposafiri. Daima alifuata utaratibu huu: baada ya kuwafukuza pepo waliotawala mahali pale, akawabatiza wenyeji na kuwafundisha imani ya Orthodoksi. Ndipo akawaomba wenyeji kumpatia maeneo kujenga makanisa na monasteri. Matendo yake ya maisha yake yanasema kwamba alijenga makanisa na monasteri walau kumi, akawapadirisha mapadri wengi na kuweka viongozi kwa jumuiya mpya. Mara nyingi wenyeji waliiheshimu miti fulani na waliogopa kuikata kwa sababu ilipagawa na pepo Dask. Wakikata mti namna hiyo mti utawaangukia na kuwaua. Samueli, kwa kufukuza pepo na kukata miti, alipata mbao kwa ajili ya kutengeneza milango, madirisha na paa za makanisa yake. Kwa mfano, katika nchi ya Zem kulikuwa mti, kwa jina daero. Mti huo ulitokwa damu, kama mwanamke, kila baada ya mwezi mmoja na nyoka ulijibanza katika matawi yake. Abba Samueli akafika Zem kufukuza nyoka na kukata mti. Akafaulu kukata mti baada ya kupiga ishara ya msalaba na kuanza kutumia shoka lake kwa jina la Utatu Mtakatifu. Joka mwenye sumu kali akakimbia kutoka juu ya mti. Samueli alizimua sumu yake kwa maombezi yake na wenyeji wakampiga mapigo 81hadi akafa. Mwishoni Samueli aliwabatiza watu, akafundisha kushika imani ya Orthodoksi na kujenga kanisa la Zem kwa heshima ya Bikira Maria.

Samueli alifariki tarehe 8 Novemba (*29 Tequemt*) huko Yazarzar, alipozikwa. Mwaka alipofariki haukutajwa. Miezi saba baadaye mfuasi wake Samra Krestos akachukua masalia yake na kuyazika katika kanisa la Wagag.[351]

Mt. Samueli, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

## Mtu wa Mungu Mkatekista Alberti Patia Joäo , 1979

Alberti alizaliwa Memba, jimbo la Nacala, Msumbiji, mwaka 1931. Alikuwa mkulima, lakini aliweza kuandika na kusoma. Kwa hiyo, mwaka 1971 alichaguliwa kuwa Mkatekista huko misioni ya Ocua. Aliwasindikiza mapadri katika safari zao za ki-roho walipotembelea waamini katika vigango vyao. Alisifiwa kwa imani yake, na pia kwa wema na unyenyekevu wake. Alikuwa mpendwa wa wote.

---

[351] Rejea *Actes de Samuel de Dabra Wagag*.

Baada ya uhuru, serikali ya ki-komunisti ilizuia mara nyingi shughuli za Kanisa. Mapadri hawakuweza kutembea kama zamani, hata hivyo Alberti hakuogopa kuwasindikiza. Usiku mmoja waligonga mlangoni mwa nyumba yake na kusema: “Ikiwa padri anawatembelea waamini wa Nivussacove, tutamkamata.“ Ingawa ilikuwa usiku Alberti akaenda kumwona Padri na kumwambia: “Usiende Nivussacove. Nitaenda. Mimi ni raia wa Usumbiji. Wanatangaza kwamba kuna uhuru wa dini. Ikiwa watanitendea kitu itakuwa kwa ajili ya Yesu Kristo.“ Akaondoka kama kawaida wake, yaani akibebwa juu ya baiskeli na rafiki yake, kwa sababu aliteswa na kifua kikuu na hakuwa na nguvu ya kuendesha baiskeli. Jioni ile alirudi kuhakikisha kwamba kila kitu kiliendelea vizuri.
Wamisionari walipofukuzwa nje ya nchi, watu walitumwa na serikali ya wilaya kupora mali ya Alberti nyumbani mwake. Walichukua kila kitu: nguo za mke na watoto wake, chakula, baiskeli, hata dawa. Alikuwa anateswa pia na magonjwa ya kichocho na upungufu wa damu. Alikatazwa kwenda nje ya kijiji chake na kulazimishwa kutoa ripoti kwa hospitali ya Namoja. Kwa msaada wa nesi wa Ocua, mapadri walifaulu kumpeleka kwa hospitali ya Memba. Alikata roho alipofika. Benedikta, sista na nesi, alishuhudia kwamba aliomba padri aje ili aungame na kupokea Ekaristi. Padri alipofika alikwisha pumua pumzi ya mwisho. Alikuwa na umri wa miaka 48. Akaacha mke na watoto watatu, mabinti wawili na mwana mmoja.
Injili ilikuwa hai ndani yake. Alipofahamu kwamba mtu fulani alikuwa na neno kwake na familia yake, hakutamka neno lolote ya kulipa kisasi, bali alimwambia mke wake: “Ikiwa anakuja kwa mazishi yangu, usimfukuze, nimekwisha samehe kwa jina la Yesu.“
Mtu wa Mungu Alberti, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

**Novemba 9**

Huko Ethiopia, Wakatoliki wanamkumbuka Mt. **Yohane wa Bizane**, padri na mtawa.[352]
Huko Uganda, Wakatoliki wanamkumbuka **Leopoldo Anywar**, Padri, aliyeuawa mwaka 1968.

Huko Misri, Wakoptiki wanawakumbuka Mt. **Timotheo**, askofu wa Ansena; Abba **Zakaria**, Patriarka, askofu wa 64 wa Aleksandria, 1032.[353]
Waorthodoksi wanawakumbuka Mt. **Nektario**, askofu wa Pentapolis, 1920;[354] Mt. **Yohane mfupi**, mtawa, Karne la IV.
Huko Ethiopia, Wakristu wanamkumbuka **Abrahamu wa Manuf**, mwanakoriti.[355]

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake! Amina.

## Mt. Zakaria, Patriarka wa 64 wa Aleksandria, 1032.

Zakaria alikuwa mzaliwa wa Aleksandria na akapadirishwa kule. Akatunza usafi wa moyo na kukuza fadhila ya upole. Askofu Filotheo, Patriarka wa 63 wa Aleksandria alipofariki, maaskofu walikusanyika katika Kanisa la Mt. Marko kutafuta mwandamizi wake. Walipojadiliana, walipewa habari kwamba mtu tajiri wa Aleksandria, Ibrahimu Ben-Bishr, aliyekuwa karibu na Khalifa (Gavana), akampatia Gavana rushwa ili aandike barua kusudi achaguliwe kuwa Patriarka. Gavana akamtuma Aleksandria, akisindikiza na askari. Maaskofu walihuzunika sana na wakamwomba Mungu kwa sauti moja kulinda Kanisa, akimfukuza yule anayekuja kuwa mchungaji kwa kutumia rushwa. Wakamsihi Mungu amteue yule aliyestahili cheo hicho.

---

[352] *Acta Sanctorum*
[353] *Coptic Synaxarium: 13 Hatour.*
[354] Orthodox Saints of the Day
[355] *The Ethiopian Rite Missal, Abba Emmanuel & Abba Brendan Cogavin, 2002, uk 192. Ethiopian Synaxarium: Tekemt 30*


Walipokuwa katika maombi, Abba Zakaria akatelemka ngazi ya Kanisa la Mtakatifu Marko, akibeba chombo. Mguu wake ukatereza, akaanguka na kuporomoka ngazi za kanisa hadi sakafuni akishika chombo kizima mikononi mwake. Maaskofu na mapadri wakashangaa. Wakawauliza waamini wa Aleksandria maoni yao. Wote, pamoja na maaskofu na mapadri, wakakubali kwamba Zakaria apadirishwe kuwa Patriarka kwa sababu ya haki na ujuzi wake. Ibrahimu Ben-Bishr alipofika, akamkuta Zakaria amekwisha tawazwa kuwa Patriarka. Maaskofu waliposoma barua ya Gavana, wakamtuliza Ibrahimu kwa kumpadirisha awe Padri, tena hegumen. Wakamwahidia kwamba atapadirishwa kuwa askofu wakati nafasi itakapopatikana.

Zakaria akavumulia taabu nyingi. Kwa mfano, mtawa mmoja akamstaki mastaka mengi mbele ya El-Hakem (Be-Amr-Allah) aliyeteuliwa kuwa Gavana mwaka 989 B.K. El-Hakem akamkamata Patriarka na kumtupa kwa simba. Lakini simba hawakumgusa. Gavana akamkasirikia mlinzi wa simba akififikiri kwamba akachukua rushwa kutoka Patriarka. Gavana akaamua simba wasile kwa muda mrefu. Baadaye akachinja kondoo, akapaka damu ya kondoo nguo za Patriarka. Ndipo akamtupa kwa simba, lakini kwa mara ya pili, simba hawakumdhuru, kwa sababu Bwana alimlinda. Gavana akashangaa na akaamua aondolewe. Akamtupa gerezani. Kwa miezi mitatu akamtisha kumwua na kumtupa motoni ikiwa hakani imani yake kwa Kristo. Patriarka hakuogopa. Gavana akajaribu kumhonga akimwahidi kuwa Hakimu mkuu mwenye mamlaka juu ya mahakimu wote nchini. Patriarka hakujali heshima na cheo hicho, hakumsikiliza Gavana. Mwishoni, kwa njia ya mwanamfalme mmoja, Gavana akamachilia huru.

Zakaria akaenda jangwani mwa Shete na akakaa huko kwa miaka tisa wakati waamini waliendelea kukateswa sana. Makanisa mengi yakabomolewa. Lakini wakati ulipowadia Bwana Yesu Kristo akalihurumia Kanisa lake, akaondoa taabu hizo zote miongoni mwa waamini. Pia akabadilisha mawazo ya uovu ya Gavana na kuyaweka mawazo ya haki. Kwa hiyo Gavana akaamuru kwamba makanisa yaliyobomolewa yajengwe upya. Isitoshe akaamuru kwamba mambo yote yaliyochukuliwa kutoka na makanisa yarudishwe. Vyengele vikasikika tena kati ya watu.

Abba Zakaria aliishi miaka 12 baada ya kurudi kutoka Shete. Akajitoa kukarabati upya makanisa yaliyoharibika na kuyajenga mengine. Akatawala kama Patriarka kwa muda wa miaka 28. Akafariki katika amani.
Mt. Zakaria, utuombee na Mungu awahurumie Wakristo wanaoishi chini ya Utawala wa Waislamu. Amina.

## Mt. Nektario, askofu, 1920



Askofu huyu wa Kanisa la Orthodoksi wa Mashariki anaheshimiwa kama Mtakatifu. Nektario alizaliwa Selyvria wa Thrace, tarehe 11 Oktoba, 1846. Baada ya kufuata shule, aliamua kuwa mtawa huko Chios. Kwa sababu ya fadhila zake, alipata daraja la Ushemasi, na kuitwa Nektario. Chini ya uongozi wa Patriarka Sofronio wa Aleksandria, alikwenda mji Athena kujifunza kwa miaka mitatu. Akarudi Aleksandria na Askofu Sofronio akampadirisha, tarehe 23 Machi, mwaka 1886. Na mwaka ule ule, mwezi wa Agosti akafanywa kuwa Archimandrite. Akaanza kuonyesha wivu wake wa kuhubiri Neno la Mungu na kupamba makanisa. Akapamba kwa uzuri sana kanisa la Mt. Nikola huko Kairo. Miaka ilipopita alipokuwa Athena, Ugiriki, alimwona katika ndoto Mt. Nikola akimkumbatia na kumwambia kwamba atamwinua sana.
Tarehe 9 Januari, 1889, katika kanisa la Mt. Nikola, Nektario akateuliwa kuwa askofu wa Pentapolis, Libya. Akapata daraja la uaskofu kwa mikono ya Patriarka Sofronio. Jimbo la Pentapolis lilikuwa chini ya Patriarka wa Aleksandria. Ingawa alipanda hatua za Hierarkia kwa haraka sana, Nectario aliendelea kuwa na fadhila ya unyenyekevu. Lakini watu wengine walionea wivu na kuanza kusema kwamba moyoni mwake anawaza kuwa Patriarka wa Aleksandria. Kwa sababu watu walimpenda Nektario, Pariarka alihangahika kwa

masingizio hayo. Tarehe 3 Mei, 1890, Patriarka Sofronio alimwondoa katika kiti cha Pentapolis na mwezi wa Julai akamwamuru kuhamia Misri.

Bila kutafuta kulipa kisasi wala kujitetea, Askofu Nektario akaenda Athena. Kule tayari akasikia kwamba alishtakiwa kuishi kinyume cha maadili. Kwa sababu sifa ya jina lake liliharibika hakuweza kuheshimiwa kama askofu. Akaanza kufanya kazi ya Mhubiri mkoani wa Euboia. Na mwaka 1894 akachaguliwa kuwa Mkuu wa *Rizarios Ecclesiastical School* huko Athena. Kwa njia ya mahubiri, jitihada kuwatayarisha wanaume kuwa mapadri, sadaka zake kwa maskini, upole wake na upendo wa ki-baba, akaanza kuwa Mwanga na Kiongozi wa ki-roho kwa wengi. Kwa maombezi ya wanawake kadhaa, mwaka 1904 akajenga konventi ya Utatu Mtakatifu katika kisiwa cha Aegina, wakati bado ni Mkuu wa *Rizarios School*. Mwaka 1908 akahamia Aegina, mahali alipoishi hadi kifo chake, ili kuongoza konventi. Akaendelea kuzama katika sala, na mara kwa mara alionekana akiinuliwa juu wakati aliposali. Akawa mlinzi wa wenyeji wa kisiwa cha Aegina, akawaokoa kwa njia ya sala zake na balaa ya ukame, kuwaponya wagonjwa, na kufukuza pepo. Hapo pia alisingiziwa, lakini aliwavumilia na kuwasamehe wasingizaji bila kutafuta kujitetea wala kulipa kisasi. Ingawa alifanya maajabu mengi alipoishi, miujiza mingi zaidi ilitendeka baada ya kifo chake, mwaka 1920. Anakumbuka na kusifiwa sana ulimwenguni kote kwa ajili ya uponyaji wa kansa.

Mt. Nektario, utuombee ili tuvumilie masingizio na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

**Novemba 10**

Huko Ethiopia, Wakatoliki wanamkumbuka **Kaleb**, mfalme wa Ethiopia.[356]
Huko Basoko, Jamhuri ya ki-demokrasia ya Kongo, Wakatoliki wanamkumbuka **Vennix Walther**, (Bruda Clément), wa Shirika la Montfortain, aliyeuawa mwaka 1964.
Huko Aljeria, Wakatoliki wanamkumbuka Mwenyeheri **Odeta Prévost**, Sista wa Shirika la Masista wadogo wa Moyo Mt., aliyeuawa 1995.

Waorthodoksi wa Mashariki wanamkumbuka Mt. **Nonni**, askofu wa Heliopolis, aliyeongoa Pelagia.[357]

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake! Amina.

## Mt. Nonni, askofu, mnamo 468 au 471

Tunasoma habari zake katika maisha ya Mt. Pelagia, yaliyoandikwa na Yakobo, Shemasi wa Kanisa la Heliopolis, (Balbek, Lebanon ya siku hizi).
Shemasi Yakobo anatuambia kwamba Nonni alikuwa mtawa wa monasteri ya Tabena, Misri. Kwa sababu ya fadhila zake na mafundisho yake yenye mvuto na ukweli, aliteuliwa kuwa Askofu wa Heliopolis. Alikuwa amekwisha ongoa Waarabu elfu thelathini kabla ya kufika Heliopolis. Na huko katika jimbo lake aliwaletea Yesu Kristo watu wengi sana.
Siku moja Patriarka wa Antiokia aliwakusanya maaskofu masufraganei wake saba katika Kanisa la Mt. Juliani. Walipokuwa wanajadiliana, mkutano mkuu ukapita mbele zao. Mmojawapo mashuhuri wa kahaba wa mji, aliyeitwa Margareta, au lulu, jina alilopewa na watu kwa sababu daima alikuwa amevaa lulu na vito, akapita. Alikuwa amepanda punda akivaa nguo nzuri sana, lakini bila adabu, na kusindikizwa na

---

[356] *The Ethiopian Rite Missal, Abba Emmanuel & Abba Brendan Cogavin, 2002, uk 193.*
[357] *Eastern Orthodox Liturgical Calendar*.. Mt. Nonnus anaheshimiwa katika Kanisa Katoliki tarehe 2 Desemba.

mkutano mkubwa wa vijana wa kiume na kike. Akapita mbele ya maaskofu kama jemadari mshindi. Wote wakainama kichwa ili wasimwone, isipokuwa Askofu Nonni, ambaye alimfuata kwa macho mpaka alipotoweka. Akawaambia maaskofu wenzake: “Je, hamkustaajabia uzuri wa mwanamke huyo?“ Wakakaa kimya. Akarudia tena: “Je, hamkustaajabia uzuri wa mwanamke huyo? Mimi nilimtazama sana, na ninaogopa kwamba mwenendo wake utatuhukumu mbele ya baraza la hukumu la Mungu. Angalieni, ametumia muda kiasi gani kujipamba? Amevumulia shida ngapi kujipodoa ili kuwapendeza tu wanadamu? Ni upendo wa wanadamu anautafuta, ambao leo wapo na kesho wametoweka. Na sisi tunaye mbinguni Baba Mwenyezi na Bwana aishiye milele, mchumba wetu, ambaye hazina zake hazihesabiki. Na tunatumaini kuuona uso wake milele na milele. Je, tunajitahidi namna gani kutakasa na kupamba roho zetu? Je, siyo tujihukumu sisi wenyewe kutochukua muda na jitihada kuzipamba roho zetu?“

Aliposema hayo akaenda chumbani mwake, pamoja na Shemasi wake Yakobo, akamsujudia Mungu na kulia machozi mengi akisema: “Mwokozi wangu, umsamehe mwenye-dhambi, ambaye katika maisha yake, alitumia muda mchache sana kupamba roho yake ili ikupendeze, kuliko kutumia muda wa siku moja kupamba mwili wake. Mwanamke huyo aliahidi kuwapendeza watu, akatimiza ahadi yake, na mimi nimekuahidi kukutumikia lakini sikutimiza ahadi yangu kwa sababu ya udhaifu wangu.“ Kwa maneno mengi alimlilia Mungu na kujinyenyekea mbele yake.

Kesho yake, ambayo ilikuwa Jumapili, akamweleza Shemasi wake Yakobo ndoto yake. “Nilikuwa penye altareni, nikaona njiwa mweusi na mchafu kabisa, ambaye alinuka sana, hata sikuweza kuvumilia harufu yake. Akarukaruka juu hadi mwisho wa ibada kwa Wakatekumeni. Shemasi alipowaambia Wakatekumeni kuondoka, njiwa akaenda pia. Misa ilipomalizika, njiwa huyo akarudi tena na kurukaruka juu. Shemasi akamkamata na kumtupa katika kisima cha ubatizo. Akatoka majini akiwa mweupe pe. Akaondoka na sikumwona tena.“ Hakuelewa maana ya ndoto hiyo.

Alipoenda kanisani, Patriarka akamwomba kuwahutubia waamini. Akafanya hivyo kwa nguvu za Mungu, hata waamini wakaanza kujuta

madhambi yao. Alionekana wazi kwamba Roho Mtakatifu alikuwa anasema kwa kinywa chake kwa sababu kila mwaamini alilialia. Kwa neema ya Mungu, kahaba mkuu huyo Margareta alifika kanisani na kusikiliza maneno yaliyosemwa na Askofu Nonni. Alipoyasikia akalialia. Akachomwa moyoni mwake na kumwandikia Askofu Nonni ujumbe: "Kwa mfuasi mtakatifu wa Yesu Kristo, mimi mwenyedhambi na mfuasi wa Shetani, Salaam. Nimesikia kwamba Mungu wenu alishuka mbinguni, siyo kwa ajili ya wenye haki bali wenye dhambi ... Naomba neema ya kuzungumza nawe ili niweze kuona uso wa Mwokozi."

Mtakatifu wetu alimjibu kufika kuongea naye mbele ya maaskofu wote. Lulu akaharakisha kukutana naye katika Kanisa la Mt. Juliani. Akajitupa miguuni mwa Askofu Nonni mbele ya maaskofu wote na kumwomba abatizwe. Maaskofu wote walipotambua toba ya mwanamke huyo walikubali abatizwe. Askofu Nonni akamwuliza jina lake. Akamjibu kwamba alipozaliwa wazazi wake walimwita Pelagia, lakini watu wa Antiokia walimwita Margareta. Akambatiza kwa jina la Pelagia.

Askofu Nonni akamwambia Shemasi wake kufurahi pamoja na Malaika wa Mungu. Wakaanza kula kwa furaha. Walipokuwa wakila, Shetani akasikika kwa sauti kubwa akisema: "Ole wangu! Jinsi gani ninateswa na mzee huyu mbovu! Umenipokonya Waarabu elfu thelathini, na wenyeji wa Heliopolis ambao walikuwa mali yangu. Na sasa unanipokonya yule ambaye nilimtegemea kwamba atafanya kazi yangu. Ilaaniwe siku ya kuzaliwa kwako!" Maneno hayo yalisikika na watu wote waliopo na hasa Pelagia. Shetani akamwambia kwamba alimpamba kwa mali na sifa, na sasa alimsaliti. Askofu Nonni akamwambia asiogope, bali afanye ishara ya msalaba. Akafanya hivyo na Shetani akatoroka.

Siku tatu baada ya ubatizo wake alimletea Askofu mali yake yote. Askofu akaipokea na kuikabidhi Kanisa, ili igawiwe miongoni mwa maskini. Hatujui tarehe Askofu Nonni alipofariki.

Mt. Nonni, utuombee ili Viongozi wote wa Kanisa wahubiri huruma ya Mungu na Mungu atukuzwe daima na milele.

## Mwenyeheri Odeta Prévost, mfiadini, 1995.



Odeta alizaliwa tarehe 17 Julai 1932 huko Ufaransa. Mwaka 1950 akahitimu kuwa Mwalimu na akafundisha miaka mitatu, lakini mwaka 1957 akajiunga na Shirika la Masista Wadogo wa Moyo Mtakatifu wa Karolo de Foucauld. Na mwaka 1959 akaweka nadhiri za maisha.

Mwaka 1958 alitumwa kwenda Kbab, Moroko, na muda si muda kufanya kazi Ufaransa kati ya Waislamu watokao Afrika ya Kaskazini. Akatumwa tena Afrika, Aljeria, mwaka 1968. Akajitahidi kuelewa maisha ya ki-roho ya Waislamu, kwa kusoma Qu'rani na kusali pamoja nao. Alijua namna ya kuishi karibu na majirani, watu maskini, katika upendo, urafiki na heshima, akiwahudumia kwa utumishi wa kila siku. Akamruhusu Yesu aonyeshe upendo wa Mungu ndani yake.

Alijua kupima hali ya nchi na hatari zake. "Ni faida kubwa kuishi kwa uaminifu kwa Yesu na Injili yake." Akafariki Aljeria akipigwa rizazi na gaidi alipokuwa anaenda kuhudhuria misa tarehe 10 Novemba 1995. Akatangazwa kuwa Mwenyeheri tarehe 8/12018 na Baba Mtakatifu Fransisko.

Mwenyeheri Odeta Prévost, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

**Novemba 11**

Sisi Wakatoliki tunamkumbuka Mt. **Mina** (Menas), mfiadini, Mareotis, Misri.[358] Pia kumbukumbu ya Mt. **Kandidiano**, Shahidi.[359]
Huko Uganda, kumbukumbu ya Mtumishi wa Mungu **Angelo Negri**, askofu, wa Shirika la Wamisionari wa Comboni, 1949.
Huko Uganda na Tanzania Wakatoliki wanamkumbuka Mtu wa Mungu **Augusto-Leoni** (Auguste-Léon) **Livinhac**, askofu, wa Shirika la Wamisionari wa Afrika, (*White Fathers*) aliyefariki mwaka 1922 (Rejea maisha yake tarehe 12 Novemba).
Huko Mwembe, Jamhuri ya ki-demokrasia ya Kongo, Wakatoliki wanamkumbuka **Karoli Rommens**, padri wa Shirika la *Oblat de Marie*, aliyeuawa mwaka 1972.
Huko Jimbo la Jos, Nigeria, Wakatoliki wanamkumbuka Mtumishi wa Mungu **Gabrieli Gonsum Ganaka**, Askofu Mkuu, 1999.
Huko Man, Ivory Coast, Wakatoliki wanamkumbuka **Regis Grange**, Padri wa Shirika la Mabruda wa Moyo Mtakatifu (*Sacred Heart Brothers*), aliyeuawa maka 2000.

Huko Misri, Waorthodoksi na Wakoptiki wanamkumbuka pia Mt. **Mina** (Menas), mfanya miujiza, mfiadini, 304.
Huko Ethiopia, Wakristu wanawakumbuka Mt. **Petro III**, Patriarka, askofu wa 27 wa Aleksandria na Abba **Shenoute II** (Sanitius), Patriarka, askofu wa 63 wa Aleksandria; Abba **Libano** (Libanos) na **Satenwa** (Setenna), nabii wa Aleksandria.[360]

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake! Amina.

## Mt. Mina, mfiadini, 309.

[358] *Martyrologium Romanum,* ed. 2005.
[359] Dicitonary of Saints
[360] *The Ethiopian Rite Missal, Abba Emmanuel & Abba Brendan Cogavin, 2002, uk 193. Ethiopian Synaxarium: Hedar 02.*



Anajulikana kama Mina wa Kotyauem, au Mina wa Misri, au wa Mareotis. Pengine jina lake linaandikwa Menas. Maana ya jina lake ni ’kuamini‘ au ‘mwaminifu‘. Ni mmojawapo wa Watakatifu wa zamani aliyesifiwa sana.

Kadiri ya Ethiopian *Synaxarium*, baba yake Eudoksio, mwenyeji wa mji Nakiyos, alikuwa mkuu wa mkoa wa Afrakya (au Phrygia), mtu mpole na mwenye huruma, aliyependwa na watu wengi. Lakini hakuwa na mtoto. Siku moja mke wake alienda kanisani akamwomba Bikira Maria mbele ya picha yake, amwombee ili Mungu amjalie mtoto mwanamume. Akasikia sauti kutoka picha ya Bikira Maria ikiitikia: “Amina“. Mara akakimbilia nyumbani mwake na kumwambia mumewe mambo yaliyotokea. Mume wake akamjibu: “Mapenzi ya Mungu yatimizwe!“. Mwanamke akapata mimba, akamzaa mtoto mwanamume, akamwita ’Mina‘, kufuatana na maneno aliyosikia kutoka picha ya Bikira Maria.

Mtoto alipokua baba yake alimfundisha Maandiko Matakatifu na maisha ya ki-roho. Alipokuwa na umri wa miaka 11 baba yake alifariki. Miaka mitatu baadaye mama yake alifariki. Mina akabaki peke yake, akafunga na kuomba. Kaizari Dioklesiani alipokana Kristo, akaamua watu wote waiabudu miungu wa uongo. Wakristo wengi wakateswa kwa ajili ya imani yao wakikataa kuiabudu miungu wa uongo.

Mina akaacha mahali alipoishi na kukumbilia jangwani. Akabaki kwa muda. Siku moja mbingu zikafunguka na akawaona mashahidi wakipokea taji yao nzuri. Akasikia sauti ikisema: “Yule anayefanya kazi kwa bidii kwa sababu ya Jina la Bwana wetu Yesu Kristo atapokea taji hiyo“. Mara akarudi mjini na kutangaza kwamba yeye ni Mkristo. Wengi, waliomjua baba yake kwamba alikuwa na ukoo bora, wakamjaribu kumzuia kujitangaza, hata liwali akamwahidi heshima na mali, lakini bure. Basi liwali akaamuru askari wake kumkamata na kumtesa vibaya sana. Walipochoka kumtesa walimkata kichwa. Mara

akapokea taji la shahidi. Liwali akawaamuru askari wake kuutupa mwili wake katika moto, lakini waamini fulani waliuchukua kutoka motoni. Mwili wake haukuungua wala kuharibika. Wakaufunika katika sanda nzuri na kuuweka mahali fulani hadi mwisho wa dhiki.

Wakati ule wenyeji wa wilaya ya Mareotis walijaribu kukusanya jeshi kutoka Pentapolis. Wakauchukua mwili wa Mina pamoja nao ili uwe msaada na kinga njiani. Walipokuwa katika marikebu wanyama kutoka bahari wenye kichwa cha nyoka na shingo ya ngamia, wakaonekana wakinyosha shingo yao ili kulamba mwili wa Mina. Wanamaji wakaogopa sana. Mara moto ukatoka mwilini mwa Mina na kuungua uso wa wanyama hawa. Walipofika mji Aleksandria watu walitaka kurudi kwao kwa kuuchukua mwili wa Mina. Walipomweka juu ya ngamia, ngamia hakuweza kuondoka. Walipomweka juu ya ngamia mwingine, vivyo hivyo. Basi walitambua mapenzi ya Mungu, wakamzika pale na kurundika udongo juu ya mwili wake.

Mungu aliyetaka kaburi lake lijulikane, siku moja kondoo mgonjwa mwenye vidonda vingi, akapita juu ya rondo la udongo, na kutereza katika kisima cha maji kilichokuwepo karibuni. Mara kondoo akapona. Mchungaji alipoona yaliyotokea akashangaa sana. Tangu siku ile kila mara kondoo wake mmoja alipokuwa mgonjwa alitumia udongo wa rundo la udongo, akauchanganya na maji ya kisima na kumpaka kondoo. Na mara akapona. Akazoea kufanya hivyo na akawapona, hata watu wote waliokuwa wagonjwa.

Kaizari Konstantino alisikia habari hizo. Alikuwa na binti mmoja, mgonjwa mwenye vidonda sugu, basi akamtuma kule. Binti huyu hakuweza kuvua nguo zake zote na kuonekana uchi mbele ya wanaume waliokuwepo. Akamwuliza mchungaji alifanya nini wakati kondoo walipokuwa wagonjwa na wakapona. Mchungaji akamweleza. Basi binti huyu akachukua udongo kutoka mwinuko wa ardhi, akauchanganya na maji na kujipaka mwili wake wote. Usiku ule alilala pale pale. Mt. Mina akamtokea usiku na kumwambia: “Utakapoamka asubuhi, chimba na utaona mwili wangu.“ Mara akapona. Alipoamka na kuona kwamba alipona, akawaamuru watumishi wake kuchimba mahali pale pale. Wakavumbua mwili wa Mt. Mina. Akatuma barua kwa baba yake Kaizari na kumweleza yote yaliyotokea. Basi Kaizari akajenga kanisa kubwa juu ya kaburi ya Mt. Mina. Makaizari Arkadio na

Honorio wakaamua mji ujengwe pia. Wakauchukua mwili wa Mt. Mina na kumweka katika Kanisa hilo. Miujiza mingi ikatokea katika kanisa hilo ambalo linajulikana kwa jina la "Utukufu wa Jangwa la Libya". [361]
Mt. Mina, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

## Mtumishi wa Mungu Gabrieli Gonsum Ganaka, Askofu, 1999



Gabrieli alizaliwa huko Pankshin, Nigeria, tarehe 24 Mei 1937. Baba yake alikuwa Chinkida na mama yake Gwanwa, wakaitwa Petro na Sesilia walipoongoka. Chinkida alikuwa mwenyeji wa Wuseli, kijiji kimoja cha kabila la Wangas, Kusini pa Pankshin. Akahamia Ampang Mashariki, mahali alipokutana na Sesilia na kumwoa. Akaafikiana na Wamisionari Waanglikana, Chama cha C.M.S., waliokuwa wamefanya kazi kati ya Wangas tangu mwaka 1910. Akaongoka na kufuata shule ya misioni. Baadaye Chinkida alijiunga na Polisi na kufanya kazi huko Pankshin, mahali ambapo Gwanwa alimzalia watoto wawili, Joshua Sati na Gabrieli Gonsum. Jina la Gonsum linalomaanisha 'mmoja aliyekuja kutoka Sum', liliwakumbusha kwamba ukoo wao ulikuwa Sum. Ganaka, jina la utani, rafiki Wahausa alilompatia baba yake, linamaanisha 'uwe pia yako'.
Gabrieli alibatizwa na Padri Benedikto Sands, mwaka 1947, akiwa na umri wa miaka kumi, katika Kanisa la Msalaba Mtakatifu, Pankshin. Alipopendezwa na Padri Benedikto, alitaka kuwa Padri. Akafuata shule ya msingi parokiani na shule ya sekondari huko Mt. Tereza. Wakati huo, baba yake na mama yake wakabatizwa katika Kanisa Katoliki na kufunga ndoa. Lakini Jashua Sati akabaki kuwa Mwanglikana.
Gabrieli akajiunga na Seminari kubwa, huko Bodija, Ibadan, kuanzia mwaka 1957 hadi 1965. Alipomaliza akarudi katika jimbo lake Jos, na mwaka ule akapadirishwa na Askofu John Redington katika Kanisa Kuu la jimbo. Akawa padri mkatoliki mwenyeji wa kwanza katika uwanja wa juu wa Jos. Akatumwa na Askofu wake kufanya kazi katika

---

[361] Kutoka *Ethiopian Synaxarium*, Hedar 15

Parokia ya Shendam. Gabrieli alikuwa mtu mrefu na mzuri. Inasemekana kwamba mwanamke mmoja alilia machozi akimwona mtu mzuri namna hii awe padri. Muda si muda akatumwa Roma kuendeleza masomo yake. Akapata Master mwaka 1967 na shahada ya udaktari katika teolojia. Aliporudi Nigeria alitumia Kanisa kwa vitengo mbalimbali ki-jimbo na ki-taifa, kama Katibu mkuu wa Baraza la Maaskofu. Mwaka 1973, Baba Mtakatifu Paulo VI akamteua kuwa Askofu msaidizi wa Jimbo la Jos. Na tarehe 2 Februari 1974 alitawazwa kuwa Askofu wa Jimbo la Jos, na mwaka 1994 akainuliwa kuwa Askofu Mkuu wa Jos.

Ingawa Jimbo Kuu la Jos linaenea mikoa sita, Gabrieli alishika nafasi mbalimbali ki-taifa katika Kanisa, kama Makamu wa Mwenyekiti wa Baraza la Maaskofu wa nchi yake, na baadaye Mwenyekiti wa baraza za Maaskofu katika Afrika na Malagasi. Moyoni aliamua kupigania haki na amani katika jamii. Siku moja wakati wa upadrisho akawahutubia mapadri wapya: “Ibada ya upadirisho siyo mazigaombwe yanayobadilisha mtu mwovu kuwa mtakatifu. Wito wenu hauwapatii ‘kinga ya ki-diplomasia‘ kuhusu mateso na hata kukoswa haki, kwa hiyo fikirini vema mnaposhughulika mambo yasiyo na haki.“

Gabrieli Gonsum akaongoza Karismatiki Katoliki hadi kifo chake. Alikuwa anasema kwamba Karismatiki Katoliki ni jambo moja jema, baadhi ya mambo mengine, Mungu analojalia Kanisa Katoliki, kwa sababu “inaunganisha imani (*faith*) na maisha, itikadi (*creed*) na matendo. Kanisa linahitaji ‘Wenye imani kali‘ (*fanatics*), kwa kuwa inawezekana kupunguza juhudi za ‘Mwenye imani kali‘, lakini haiwekani kuamsha maiti ya Mkatoliki mfu“. Mara nyingi alipatembelea mahali pa kutokewa Maria, kama Lourdes, Ufaransa, Medjurgorje, Slovakia au Aokpe, Nigeria. Alijitazama kuwa Mwingaji wa pepo. Alipenda kuimba mapambio, hasa pambio moja kwa lugha ya *Pigeon English*:

*The biggy-biggy things Jesus done for me (x2),*
*He bless my papa, he bless my mama,*
*He buttered my bread and sugared my tea,*
*He carried Satan up; he nack'am for ground,*
*The biggy-biggy things he has done for me.*

Gabrieli Gonsum alikuwa mtu wa kuchapa kazi. Alizungumza lugha mbalimbali: Kiingereza, Kifaransa, Kiitaliano, Kijermani, pamoja na Kiigbo, Kihausa na Kingas, lugha yake asili. Gabrieli alikuwa mnyenyekevu na rahisi kuzungumza naye, akiwakaribisha kila wakati mapadri, walei na hata wasio wakatoliki. Kauli mbiu yake ilikuwa "*Nisi Dominus frustra*", maana yake "Bila Bwana tunafanya kazi bure", kutokana na Zab 127:1.

Tarehe 11 Novemba, 1999, akafariki katika hospitali moja ya New York, alipotibiwa kwa ugonjwa wa moyo. Akazikwa katika Kanisa Kuu alipopadirishwa mwaka 1965.

Mtumishi wa Mungu Gabrieli, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

**Novemba 12**

Huko Misri, Wakatoliki wanamkumbuka Mt. **Nilo wa Sinai**, abate, aliyestaafu kama Gavana wa Konstanipoli na kwenda kuishi kama mkaa pweke katika jangwa la Sinai.[362]
Huko Hispania na Visiwa vya Kanisari kumbukumbu ya Mtakatifu **Diego wa Alkala**, OFM, Bruda, alifanya kazi ya umisionari katika visiwa vya Kanari, 1463.
Huko Ethiopia, Wakatoliki wanawakumbuka **Madhanina-Egzi**, Abba; **Amda-Mikaeli**, Jemadari wa Ethiopia, na **Na'akweto-la-Ab**, mfalme wa Ethiopia.[363] Pia kumbukumbu ya Mt. **Auluceto**, mwungama dini.[364]

Wakoptiki wanamkumbuka Mt. **Yusto**, askofu na mfiadini, pia **Kutabarukiwa Kanisa la Mt. Abu Nofr**, mkaa pweke.[365] Pia kumbukumbu ya **Gregori**, Askofu Mkuu wa Aleksandria, Mt. **Publio**, **Mauruto**, na askofu **Ksisto**, wote wafiadini.
Waorthodoksi wanamkumbuka Mt. **Yohane mtoa sadaka**, Patriarka wa Alelsandria, 619.

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake! Amina.

## Mt. Nilo wa Sinai, mwanakoriti, padre, Mwalimu wa Kanisa, 430

Nilo alikuwa mlei, aliyeoa na akawa baba wa watoto wawili. Aliishi maisha ya raha na furaha na kufanywa Gavana wa Konstantinopoli. Mt. Yohane Krisostomos, askofu mkuu wa Konstantinopoli alimfundisha Maandiko Matakatifu na maisha ya ki-roho. Moyoni alipenda kuishi kwa ajili ya Mungu tu. Kwa hiyo mnamo mwaka 390, (au labda 404), baada ya kukubaliana na mke wake, akaenda kukaa Mlimani Sinai pamoja na mwana wake mdogo Theodulo. Akamwacha mwana wake

---

362 *Roman Martyrology*, ed. 1956.
363 *The Ethiopian Rite Missal, Abba Emmanuel & Abba Brendan Cogavin, 2002, uk 194.*
364 Dicitonary of the Saints.
365 *Coptic Synaxarium: 16 Hatour.*

wa kwanza kwa mke wake ili alelewe kadiri ya wito wake. Yeye na Theodulo wakaishi maisha ya kimonaki.

Hatujui jinsi walivyoishi maisha yao. Nilo alidharau mambo ya ki-dunia kwa ajili ya upendo wa Yesu Kristo kiasi kwamba hakusema lolote kuhusu maisha yake huko Sinai. Tunaweza kukisia, kutokana na vitabu alivyoandika, kwamba alijitahidi kufikia ukamilifu wa maisha ya kiroho na kujipatia fadhila za ufukara, utii, maelewano na unyenyekevu. Kuhusu sala anatuhimiza kuomba Mungu kipaji cha sala. Roho Mtakatifu atufundishe kusali jinsi ipasavyo na kumwomba Mungu tu kwamba mapenzi yake yatimizwe ndani mwetu. Akatambua kwamba wakaa pweke wanapita katika majaribio makubwa na vishawishi vikali. Alishambuliwa na Adui hata kiasi cha kupoteza amani ya roho. Lakini alishinda yote kwa kuomba daima, kusoma Maandiko Matakatifu, kuimba tenzi za roho, kupiga magoti, kufanya ishara ya msalaba na hasa kuishi katika unyenyekevu.



Mwaka 410 Waarabu wakavamia jangwa la Sinai, wakawaua wamonaki wengi na kuwateka wengine kama wafungwa wa vita, miongoni mwao Theodulo. Walikusudia kumtolea sadaka kwa miungu wao, lakini baadaye wakabadilisha mawazo na kumwuza kama mtumwa. Ikatokea kwamba askofu wa Eleusa, Palestina, akamkomboa. Akamfanya kuwa mmojawapo wa wahudumu wa Kanisa. Akamweka mlinzi wa mlango wa kanisa lake. Wakati ule Nilo aliacha monasteri yake na kumtafuta mwanawe. Yeye mwenyewe alianguka mikononi mwa wavamizi, lakini mara akaweza kupata uhuru wake. Akamkuta mwanawe huko Eleusa. Basi askofu akafurahia kumrudisha Theodolo kwa baba yake na katika furaha yake akawapadirisha wote wawili. Nilo alikuwa na umri wa miaka hamsini. Labda ni wakati huu kwamba Nilo alipata habari kwamba mke wake na mtoto wake wa kwanza walifika Misri na kuishi maisha ya kitawa.

Askofu akawaruhusu warudi Sinai. Kama hatujui alivyoishi maisha yake ya kitawa ndivyo hatujui jinsi alivyofariki. Kifo chake kilitokea

wakati wa utawala wa Kaizari Marsiani. Baadaye masalia yake yalipelekwa Konstantinopoli, wakati wa Kaizari Yustini mdogo, na yalizikwa katika Kanisa la Mitume Kumi na wawili.
Mt. Nilo alikuwa daima tayari kuwashirikisha wenzake sayansi ya maisha ya kiroho. Katika ukimya wa jangwa alimfahamu Mungu jinsi tofauti alivyofahamika katika kelele za ulimwengu huu. Aliandika vitabu muhimu sana kuhusu maisha ya kiroho na barua nyingi, ambazo zaidi ya 350 zilichapishwa.
Mt. Nilo, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

## Mtu wa Mungu Augusto Leoni Livinhac, 1922

Augusto Leoni Livinhac alikuwa Mkuu wa Wamisionari wa Afrika (*White Fathers*) kwa miaka mingi na wakati muhimu kwa shirika lake. Alizaliwa Ufaransa. Aliacha seminari kubwa, jimbo la Rodez, kujiunga na Shirika la Wamsionari wa Afrika, lililokuwa limeanzishwa na Karolo Kardinali Lavigerie,[366] askofu mkuu wa Aljeria. Akapadirishwa mwaka 1873 na kujitoa kabisa kwa kazi ya umisionari katika Afrika.



Mwaka 1878 Karolo Kardinali Lavigerie akamchagua kuongoza msafara wa kwanza kwenda Afrika ya kati. Walikuwa wamisionari kumi, watano kuelekea Uganda na watano kuelekea Ujiji (Kigoma). Tarehe 22 Aprili 1878, pamoja na Wamisionari wengine 9, mapadri 8 na bruda mmoja, akapanda meli huko Marseilles. Msafara ukafika Zanzibar tarehe 18 Mei mwaka ule. Wakavuka bahari kufika Bagamoyo. Wakakaribishwa kwa upendo mkubwa na furaha na mapadri wa Holy Ghost, waliofika Bagamoyo miaka 10 kabla. Na kutoka huko wakaanza safari kwa miguu, au kwa punda, hadi Uganda, kwa njia ya Tabora. Mmoja wao Padri Yoakim Pascal[367] alifariki njiani, mahali panapoitwa siku hizi Mahaka, wilaya ya Bahi.

[366] Rejea tarehe 26 Novemba.
[367] Rejea maisha yake kwa ki-fupi tarehe 19 Agosti

Alikuwa kiongozi wa msafara kwenda Ujiji. Huko Tabora, wakagawanywa, wanne wakaenda Ujiji na watano wakaelekea Uganda, Leoni Livinhac, Ludoviki Girault, Leoni Barbot, Simeoni Lourdel na Amans Delmas, bruda. Wakafika Ziwa la Viktoria tarehe 30 Desemba 1878. Lourdel na Amans wakatangulia kutafuta makusudi mema ya Mfalme, wakati Livinhac na wenzake waliwasubiri upande wa Tanzania. Wakafika Entebbe tarehe 19 Februari 1879, wakiwa Wamisionari Wakatoliki wa kwanza kukanyaga nchi ya Uganda. Kwa wiki mbili waliweka mahabusuni wakati kumsubiri kumwona Mfalme. Mwishowe walimwona Mfalme Mutesa I. Mprotestanti Aleksander Mackay alikuwepo pia. Mutesa akawaweka Wamisionari Wakatoliki chini ya ulinzi, hadi Machi 1879, akiwaruhusu kukaa Kasubi, karibu na mji mkuu, kama kms tatu.

Padri Livinhac alipofika Uganda alianza kujifunza Luganda. Akatayarisha kitabu cha sarufi na kamusi. Katekisimu ya kwanza kwa lugha ya Luganda ikachapishwa Aljeria, mwaka 1881.

Wengi kati ya wahudumu wa Mfalme wakawaendea na kujifunza kutoka kwao dini ya Kikatoliki. Wakawakomboa watumwa na kuanza kuwafundisha kusoma na kuandika. Mwezi Novemba, 1879, wakatekumeni wa kwanza waliandikishwa.

Kama ilivyoandikwa katika maisha ya Padri Simeoni Lourdel,[368] Mutesa alikuwa mtu wa siasa. Kwa hiyo mintarifu ya dini alikuwa mtu mgeugeu. Mara anawapendekeza wamisionari Wakristo, mara aliwapendekeza Waislamu. “Mwezi Aprili 1880, Mutesa alipotoa sadaka ya watu 99, Mapadri waliona vema kuwabatiza wakatekumeni wanne waliokuwa tayari, na mwezi Mei wanne zaidi walibatizwa. Ugonjwa wa tauni ulipolipuka, wakatekumeni walio katika hatari ya kufa wakabatizwa. Muda si muda, vijana Wakristo walieneza dini yao katika mikoa ya Buddu na Singo. Mwaka 1882, uhasama na vurugu dhidi ya Wakristo vilipoonekana, mapadri waliamua kuacha misioni ya Buganda na kuelekea Bukumbi, Tanzania. Waliaacha nyuma yao Wakatoliki 20 waliobatizwa na Wakatekumeni 400. Yatima 34 waliwasindikiza. Walibaki karibu miaka mitatu Tanzania. Yatima

[368] Rejea maisha yake kwa ki-fupi tarehe 12 Mei

waligawanyika katika vikundi viwili, kimoja kilibaki Kamoga (Bukumbi) na kikundi kingine walienda Kipalapala, Tabora."

Mwezi Juni 1883, Mapera, jinsi Padri Lourdel alivyoitwa kutokana na maneno ya Kifaransa '*Mon Père*' Bruda Amans aliyomwita, alipowatembelea yatima wa Kipalapala aliombwa kuanzisha misioni huko Bukune, Tanzania. Wakati ule, mwaka 1884 padri Livinhac akateuliwa kuwa askofu na kuwekwa wakfu huko Ulaya. Mwishoni mwa mwaka 1884, Mutesa alipofariki, na mwana wake Mwanga alirithi utawala wake, misioni ya Bukune ikafungwa na mapadri wakajitayarisha kurudi Uganda. Mwezi Juni, mwaka 1885, Mwanga akatuma mitumbwi mingi na watu 300 kuwapokea tena mapadri katika nchi ya Buganda. Tarehe 12 Julai walipokelewa kwa furaha na kupewa Nalukolongo, karibu ya Ikulu ya Rubaga, kuwa makao yao. Wamisionari walishangaa kuwakuta wakristo wengi katika ikulu. Mmoja wapo alikuwa Nalumamsi, binti mpendwa wa Mfalme Mutesa. Amani haikudumu muda mrefu. Livinhac akarudi Uganda mwaka 1885, wakati wa dhiki kuu. Mashahidi wengi waliokuwa wamebatizwa naye wakauawa mwaka 1886.

Pamoja na kikundi cha Waganda, Askofu Livinhac akaenda Ulaya kuhudhuria mkutano mkuu kupinga utumwa, huko Paris, mwaka 1890. Mwaka ule ule akateuliwa kuwa Kaimu wa Mkuu wa Shirika la Wamisionari wa Afrika. Karolo Kardinali Lavigerie alipofariki, mwaka 1892, akachaguliwa kuwa Mkuu wa *White Fathers*. Afya yake na kuchaguliwa tena na tena kuwa Mkuu wa Shirika (1894-1912) vilimzuia kurudi Uganda. Alipostaafu kama Mkuu wa Shirika alianza, mwaka 1920, kutayarisha uandikaji wa hati kuhusu Mashahidi wa Uganda, ambao wakatangazwa kuwa Watakatifu na Baba Mtakatifu Paulo VI, mwaka 1964. Mwisho wa utawala wake wanashirika waliongozeka hadi kufika 930, kutoka Ufaransa, Ujerumani, Argentina, Ukanada, Ubelgiji, Uswiswi, Uingereza na Uholandsi. Livinhac akafariki tarehe 11 Novemba mwaka 1922, huko Maison Carrée, Aljeria. Alikuwa na miaka 76.

Mtu wa Mungu Askofu Leon Livinhac, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

**Novemba 13**

Sisi Wakatoliki tunawakumbuka Wat. **Arkadio**, **Paskasio**, **Probo** na **Eutikiani**, wafiadini, Afrika ya Kaskazini, 437. Wote walikuwa wenyeji wa Hispania, waliokataa kufuata Ario, wakati wa dhiki iliyosababishwa na Waharabu. Kwa hiyo walihukumiwa na Mfalme Genserik, kuhamishwa. Waliteseka sana na mwishoni waliuawa kwa namna mbalimbali. Pia wakati ule kulikuwa kijana mmoja **Paulilo**, ndugu wa Mt. Paskasio na Eutikiani. Kwa sababu hakuacha imani ya kikatoliki, alipigwa vibaya kwa viboko na kuhukumiwa kuwa mtumwa, mwaka 437.
Huko Ufaransa, Wakatoliki wanamkumbuka Mt. **Kwinksiani**, askofu. Alikuwa mwenyeji wa Afrika lakini alikimbilia Ufaransa kuepuka dhiki ya Waario. Alichaguliwa kuwa askofu wa Rodez, Ufaransa, na kufa mnamo mwaka 525, B.K.[369]
Huko Kenya, Wakatoliki wanamkumbuka Mwenyeheri, **Fiorina Cecchin** (Sista *Maria Karola*), 1925.
Huko Kamerun, Wakatoliki wanamkumbuka **Ngongo Ottou**, Wakili, aliyejeruhiwa tarehe 30 Oktoba na kufariki tarehe 13 Novemba huko Paris, mwaka 1988.

Huko Ethiopia, Waorthodoksi Tewahedo, Ethiopia, wanawakumbuka Abba **Abaidusi** (Abaydo), mtawa mkamilifu, **Abba Yohane**, mfuasi wake; na **Petro**, Patriarka, askofu wa Aleksandria, na wafiadini wengi.[370]

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake! Amina.

## Mt. Kwinksiani, askofu, Mmsionari katika Ufaransa, 527.

[369] *Martyrologium Romanum,* ed. 2001. Anatajwa pia tarhe 14 Juni, lakini wengi wanafikiri kwamba tarehe ya kufa kwake ndiyo tarehe 13 Novemba.
[370] *Ethiopian Synaxarium: Hedar 04.*

Kwinksiani alizaliwa Afrika. Alikuwa mpwa wa Askofu Fausto, askofu wa Kartagao, mwenye sifa sana kwa sababu kwa jina la Yesu alimfufua mama yake. Alipozaliwa, Afrika ya Kaskazini ilitawaliwa na Waharabu (*Vandals*). Viongozi wao, wafuasi wa Ario, walikuwa wanawadhulumu sana Wakatoliki. Dhiki ile ilisababisha kwamba wengi wakahamia Ulaya kwa kutafuta mahali pa usalama. Mmojawapo ndiye Kwinksiani, padri wa jimbo la Kartago, aliyeenda kukaa Rodez, Ufaransa. Fadhila zake zikamjulisha mbele ya Wakristo. Kwa miaka 27 Jimbo la Rodez halikupata askofu. Kwinksiani akateuliwa kushika kiti kile. Akiwa askofu fadhila zake zikaonekana tena zaidi, hasa usafi wa moyo na upendo usio na mipaka. Hakulegea hata mara moja kuwalinda kondoo zake, akiwa makini kutambua mahitaji wao na kuwasaidia. "*Akajifanya kuwa hali zote kwa watu wote*" 1 Kor 9:22.

Miujiza mingi ilipotendeka kaburini mwa Mt. Amans, aliyemtangulia katika kiti cha uaskofu Kwinksiani akajenga kanisa kubwa kwa heshima ya Mt. Amans na akalipamba vizuri sana. Kanisa lilipomalizika akatangaza sikukuu siku ile alipohamisha masalia ya Mt. Amans, akiwaalika waamini wote wa jimbo lake na majimbo ya jirani.

Mwaka 506 alihudhuria Mtaguso wa Agde. Mwaka mmoja baada ya kurudi katika jimbo lake, wakazi wa Rodez wakatafuta kumwua kwa sababu walishuku kwamba Kwinksiani alitaka kuweka mji Rodez chini ya utawala wa Mfalme Clovis, Mkatoliki. Wakati huo mji Rodez alitawaliwa na Wavisigot, wafuasi wa Ario. Kwinksiani, pamoja na watumishi wake wachache, wakatoroka usiku na kwenda mji wa Klermont. Akapokelewa kwa furaha na Eufraisio, askofu wake.

Eufraisio alipofariki, mwaka 515, Kwinksiani akateuliwa kushika nafasi yake. Ingawa aliheshimiwa na wengi kwa sababu ya fadhila zake, akapita njia ya mateso. Prokulo, ambaye Kwinksiani kutoka mfanyakazi akamwinua kuwa Padri, akamshutumu na kumtendea vibaya. Akamvulia mali yake yote aliyosimamia. Kwinksiani akavumilia yote kwa unyenyekevu na saburi. Mateso hayo hayakumwondoa upendo Kwinksiani aliokuwa kwa waamini Mungu aliyemkabidhi.

Kwinksiani alikuwa mtaalum wa Maandiko Matakatifu na mambo ya Kanisa. Alionekana kama mfalme akitoa sadaka kwa maskini; mwenye uwezo juu ya Shetani, akiwawinga pepo kwa wale waliopagawa na kuwarudisha afya; mfano wa mtu aliyejaa upole na upendo. Akafaulu

kumtuliza mfalme Thierry aliye na hasira kuhusu watu wa mkoa wa Klermont waliomwasi. Alikuwa rafiki wa raia wa jimbo lake. Baada ya kupiga magoti, kuomba na kujitesa, Mungu akamjalia mvua na kuwaokoa wenzake na njaa.

Tarehe 13 Novemba, akafariki. Mwili wake ukazikwa Klermont katika Kanisa la Mt. Stefano. Muda si muda masalia yake yakahamishwa katika Kanisa la Mt. Genez katika mji ule. Waamini wanamwomba Kwinksiani wanapoteswa na homa.

Mt. Kwinksiani, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

## **Mwenyeheri Sista Maria Karola, Mmisionari, 1925**.

Fiorina alizaliwa Italia tarehe 3 Aprili 1877. Akajiunga na Shirika la Masista wa Mtakatifu Yosefu Benedikto wa Cottolengo, Torino, mwaka 1896 na muda si muda akaanza novisiati, kwa jina la Sista Maria Karola. Katika ulimwengu alijulikana kwa jina la Fiorina, maana yake, ua mdogo, na kwa kweli alikuwa ua wa imani, usafi wa moyo, akimpenda Yesu kwa moyo wake wote. Kama Mtawa aliendeleza fadhila hizo, akiwapendeza wote aliokutana naye.

Wakati wa sikukuu ya Tokeo la Bwana, akaweka nadhiri. Akaanza kazi jikoni mwa seminari huko Giaveno, kwa muda wa miaka michache, na baadaye jikoni mwa, ‘*Little House*‘ huko Torino, pamoja na Sista Theobalda. Lakini akavutwa kwenda misioni ili kuongoa roho za watu kwa Mungu. Tarehe 28 Januari, 1905, akaondoka kwenda Afrika pamoja na msafara wa tatu, masista 6 wa Shirika lake. Alikuwa na umri wa miaka 28.

Huko Kenya akakaa Limuru, Tusu, Iciagaki, Mogoiri, Wambogo na mwishoni Tigania-Meru. Mama Skolastika anasema kwamba: “Alijionyesha kuwa mwanamke mwenye busara, mchapa kazi bila kupoteza muda bure, mwenye adabu, asiyeogopa kusema, lakini mwenye huruma na upole“.

‘*Na bona mort*‘ (yaani kifo chema), ndiyo kauli mbiu yake. Maana yake, katika kufaili, katika kutoelewana, hakutafuta kulipa kisasi. Hakuhuzunika wakati wa matukio mabaya ya maisha yake, kwa sababu

alijua kwamba thawabu ya kifo chema inafanya kwamba mtu anashinda uchungu wa moyo.

Huko Iciagaki, akaanzisha misioni mpya. “Nyumba ilikuwa banda moja, lakini pole pole alijenga nyumba nzuri ya mbao.“ Waliweza kuishi. Akalima bustani ya mboga, kupamba ua, kukusanya jumuiya ndogo. Yote alifanya kwa sababu ya upendo wake kwa Yesu. Na baada ya kazi ngumu, wakati walianza kuishi maisha ya kawaida, akaombwa kwenda Mogoiri. Akakubali kwa furaha kufuata kauli mbiu yake. Vivyo hivyo alipotumwa kwenda Wambogo. Ulikuwa wakati mgumu, wakati wa Vita vya Kwanza vya Dunia. Masista Maria na Rakeli waliondoka ili kwenda kuwahudumia wagonjwa huko hospitalini Daria. Wenyeji waliteseka sana kwa namna mbalimbali. Sista Karola aliishi wakati huu kwa nguvu ya upendo wa Kristo na mwanga wa Roho Mtakatifu. “*Caritas Christi impels us*“, yaani; “*Upendo wa Kristo watubidisha*“ 2 Kor 5:14. Alikuwa msaada wa watu wote, maskini kwa watajiri, akimwona Kristo katika wote.

Misioni yake ya mwisho ilikuwa Tigania, mkoa wa Meru. Akiacha nyumba nzuri kwa mara nyingine ilimbidii kuanzisha upya mambo mengi. Huko Tigania, akaanza kuteswa na ugonjwa wa *enterocolitis*, hadi kifo chake. Tarehe 14 Machi, 1919, masista wagonjwa waliitwa kurudi Italia kwa ajili ya afya yao. Sista Karola na Sista Kresentina wakawa wa mwisho kuondoka, mwezi wa Oktoka 1925. Walipokuwa katika meli, katika Bahari Nyekundu, kati ya Misri na Saudi Arabia, Sista Karola alifariki tarehe 13 Novemba 1925, akiwa na umri wa miaka 48. Hakuzikwa, bali kama desturi ya wanabaharia, mwili wake ulitupwa baharini.

Tarehe 5 Novemba 2022, katika Kinoru Stadium Kenya, jimbo la Meru, alitangazwa kuwa Mwenyeheri na Kardinali Kambanda wa Ruanda, aliyeadhimisha ibada kwa niaba ya Baba Mtakatifu Fransisko. Kardinali Kambanda aliwaalika waamini wamwona Mwenyeheri Cecchin kama mfano wa kuiga katika maisha yetu. Ni juu yetu sasa kupeleka habari njema ya Yesu Mwokozi katika maisha ya ulimwengu wa siku hizi.

Mwenyeheri Sista Karola, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

**Novemba 14**

Sisi Wakatoliki tunamkumbuka siku ya leo Mwenyeheri **Serapio**, mfiadini, huko Aljeria.[371]
Huko Ethiopia, kumbukumbu ya Mt. **Iona**, Mwanamke, Shahidi.[372]
Huko Visiwa vya Kanari, kumbukumbu ya Mt. **Didas**, mmisionari kwa visiwa vya Kanari;
Huko Nyeri, Kenya, Wakatoliki wanawakumbuka Watumishi wa Mungu **Luka Mboge**, Katekista, baba ya watoto 8, **Yosefu Wambugu**, **Simoni Ndegwa**, **Rukwaro**, **Kuru Micinyo**, wote walei wa Jimbo Kuu la Nyeri, waliouawa huko Mathari na waasi MauMau, mwaka 1953.
Huko Sudan ya Kusini, Wakatoliki wanamkumbuka **Viktori-Luka Odhiambo**, Padri wa shirika la Majesuiti, aliyeuawa usiku wa kuamkia tarehe 14 Novemba, mwaka 2018.

Wakoptiki wanamkumbuka Mt. **Filipo**, Mtume, aliyehubiri Injili huko Afrika.[373]
Huko Ethiopia, Wakristu wanawakumbuka **Timotheo**, mfiadini, na Abba **Yohane** wa Dabra-Damo. Pia wanakumbuka kuhamisha mwili wa Mt. Theodori, mfiadini, aliyekuwa akida wa askari mjini mwa Setb, mkoa wa Assiut, Misri. Kanisa limetabarukiwa kwa heshima ya jina lake, na miujiza mingi inatendeka kwa njia ya mwili wake.[374]

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake! Amina.

## **Mwenyeheri Serapio, Mfiadini, 1240**.

Alikuwa Mwingereza, lakini kwanza askari wa Mfalme wa Hispania. Siku moja alipowaona watawa wa Shirika la Bikira Maria wakileta

[371] *Martyrologium Romanum,* ed. 2005.
[372] Dictionary of Saints
[373] *Coptic Synaxarium: Hatour* 18.
[374] *The Ethiopian Rite Missal, Abba Emmanuel & Abba Brendan Cogavin, 2002, uk 195. Ethiopian Synaxarium: Hedar* 05.

watumwa waliokombolewa, Serapio akashtuka, akakusudia kufuata



mwendo ule bora. Akajiunga na Shirika la Bikira Maria mwenye huruma. Akapokelewa na Mt. Petro Nolasko, huko Barcelona. Mnamo mwaka 1240, yeye mwenyewe akafanya safari mbili kuwakomboa Wakristo. Safari ya kwanza alienda Murcia, nchi ya Hispania, kuwakomboa watumwa 98. Safari ya pili akaenda mji wa Aljeria na akawakomboa watumwa Wahispania 87. Akitaka kufunga safari kurudi Hispania, watumwa wengine waliobaki wakalia ya kwamba wangeweza kupoteza imani yao. Serapio akawahurumia, akabaki, wakati mwenzake akiondoka na wale watumwa 87. Mjini mwa Aljeria, Serapio akawatuliza watumwa, akafundisha Injili Waislamu. Baadhi yao wakaongoka. Sultani alipopashwa habari akaamuru kumtupa gerezani na kumpigapiga na mwisho kumpigilia msalabani. Watesi wake wakamkatakata mwili wake wote vipandevipande, mwisho akakatwa kichwa, akafa. Alikuwa wa kwanza kwa Shirika lake kufa shahidi. Baba Mtakatifu Benedikto XIII akamtangaza kuwa Shahidi, mwaka 1728.[375]
Mwenyeheri Serapio, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

[375] *Pope Benedict XIII. declared him a martyr, and approved his immemorial veneration in his Order, by a decree in 1728, as Benedict XIV. relates. I,. 2, de Canoniz. c. 24, p. 296.*

**Novemba 15**

Sisi Wakatoliki, huko Nakivuko, Uganda, tunamkumbuka Mt. **Yosefu Mkasa Balikuddembe**, mfiadini, wakati wa mfalme Mwanga.[376]
Huko Aljeria, Wakatoliki wanawakumbuka mashahidi **watakatifu ishirini**, Wat. **Fidensiano** (au **Fidensii** [377]), askofu, **Sekundo** and **Variko** na **wenzao** waliokufa mashahidi huko Hippo, wakati wa dhiki Kaizari Valeriani alipotawala. Mt. Augustino alisifu imani na ushindi wao.[378]
Huko Jomba, Jamhuri ya ki-demokrasia ya Kongo, Wakatoliki wanawakumbuka **Benedikto** (Benoit) **Nirere Cyitatire**, padri wa Jimbo la Goma, **Koleta Vunabandi Ngerageze**, **Yosefina Gakondo Nyirampgabakuze**, **Yudithi Katungu Mwendakwabo**, masista wa Mt. Vinsenti wa Roeselare, waliouawa mwaka 1996.
Huko Ilindao, Jamhuri ya Afrika ya Kati, Wakatoliki wanawakumbuka **Selestini Ngoumbago**, **Blesio Mada**, Mapadri wa Jimbo na **watu 60** (maiti waliopatikana), waliouawa karibu na Kanisa Kuu la Jimbo, mwaka 2018, na askari wa U.P.C. (Umoja kwa amani katika Afrika ya Kati). Kundi hilo limevamia kambi ya Ippy, kms 100 kutoka Bambari, tarehe 4 Desemba.

Huko Ethiopia, Wakristu wanawakumbuka wenzi wa Isidori, waliofia dini, Wat. **Afro**, **Adinio**, **Justo**, **Martro**, **Lusirio**, au Lucinius, **Sunino**, **Bandikoro**, au Labandicorus, **Eulasio**, **Kornelio** na **elfu nane** au kumi na saba elfu. Pia wanakumbuka **Ujio wa Yesu Kristo** na Mitume wake huko Dabra-Qwesquwam.[379]

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake! Amina.

---

376 *Martyrologium Romanum,* ed. 2005.
377 Dictionary of Saints
378 *Roman Martyrology*, ed. 1956. Inawezekana kwamba kati yao walikuwepo pia: Kalaegeri, Demetrio, Siddino, Saturnino, Servo, Galano, Primigeno, Theodoto, Parensi, Satura, Viktoria, Kalendioni na Firma.
379 *The Ethiopian Rite Missal, Abba Emmanuel & Abba Brendan Cogavin, 2002, uk 195. Ethiopian Synaxarium: Hedar 06.*

## **Mt. Yosefu Mukasa Balikuddembe, shahidi, 1885**.

Alizaliwa mwaka 1860. Wazazi wake walikuwa Njuba Eseta na mama yake Kalwayo. Alibatizwa tarehe 30 Aprili 1882. Alikuwa kijana mwenye sura nzuri na kuvutia. Tena alipenda michezo ya riadha. Kutokana na werevu wake na akili yake angavu, alichaguliwa kuwa msaidizi mahususi wa Kabaka Mutesa na bawabu wa Mwanga. Kwa sababu ya ushupavu wake kutetea maslahi ya wamisionari na wa wafuasi wengine wa dini, Yosefu Mukasa, ambaye pia alikuwa mtu mwenye madaraka makubwa katika mamlaka ya Ikulu ya Kabaka, alionekana mtu kichwa maji.

"Siku mmoja Mwanga akamkalia kitako Yosefu usiku kucha akimtukana na kumwonya juu ya tabia yake ya kutetea wamisionari na shughuli nyingine za madhehebu ya kikristu. Hata kulipokucha Mukasa hakujali kitu, asubuhi akaenda kanisani kusali Misa na kupokea Komunio. Aliporejea kutoka misioni, alimkuta Mwanga amepanga mikakati ya kila njama ya kutaka kumwua.

Mfalme aliita washauri wake wakuu wakiwemo Mtumishi Mkuu wa Ikulu na baadhi ya watemi aliowaamini sana akawaomba washirikiane naye katika kauli yake mbaya ya kutaka kumwua Yosefu. Baadhi ya hoja alizosema ni kumsingizia Mukasa kwamba yeye ndiye aliyemkaribisha Askofu Hannington kuja Uganda kupitia Busoga. Kabaka akawaunga mkono bila kupingwa.

Basi, hapo Kabaka Mwanga akapata moyo wa kuzua maovu zaidi juu ya mwenendo wa Mukasa akawaambia wenzie, 'Huyu mwananchi Yusufu ni mtu mbaya sana. Kwanza kabisa, kanitukana mimi, Mfalme, wakati nilipoamuru kumwua Askofu Mzungu, yeye alidai ya kwamba iwapo baba marehemu, Mutesa, angekuwa hai, hangefanya kitendo kama hiki. Pili, yeye akishirikiana na Padri Mapeera (Simeon Lourdel) alitaka kuniua kwa sumu. Mbali ya yote hayo, Mukasa sasa ni kichwa maji, kila ukimwonya hataki kusikia. Badala ya kutii amri zangu anazidi kuwafundisha dini hata watumishi wema katika mamlaka ya Ikulu. Hivi sasa, baadhi ya watumishi wangu hawanitii bali hudharau kila agizo langu!'

Akiungwa mkono, Kabaka Mwanga alifurahi kusikia ya kwamba baadhi ya Maafisa wake walipendekeza Yusufu auwe mara moja. ‘Kwa vile yeye alitaka kumwua Mfalme, basi haki yake afe yeye kwanza’.
Mukasa aliposikia kauli hii ya kutaka kuuawa, hakujali kitu. ‘Potelea mbali. Sijali kitu kufa kwa ajili ya dini yangu’, alimwambia mnyongaji wa Serikali. Mnyongaji aliamurisha ziletwe kuni ambazo angechomwa Yosefu. Pindi Padri Mapeera aliposikia kwamba Yosefu Mukasa alihukumiwa kifo, akajaribu kumwendea Kabaka ili amwachilie huru. Hakupewa nafasi ya kuonana na Mfalme, hadi aliposikia ya kwamba Mukasa alikuwa amefungwa akipelekwa kuuawa. Padri Mapeera akarudi kwa wenzie akiwa na majonzi mengi moyoni, asiweze kitu isipokuwa kusali na kuomba msaada wa Mungu.
Mnyongaji wa Serikali, Mukajanga, akamwongoza Yosefu Mukasa kuelekea katika bonde la Nakivubo ambako alipangiwa kuuawa. Njiani, Yosefu akamwambia mnyongaji, ‘Ukimwona Kabaka, mwambie kwamba ametenda dhambi kwa kunihukumu kufa. Atubu dhambi yake, la sivyo nitamshitaki kwa mwenyezi Mungu’.
Baada ya kufika Mukasa akalazwa juu ya kuni kavu akiwa amefungwa mwili wote pamoja na kuni. Upanga ukamwangukia shingoni. Hapo moto ukaanza kuwaka ukimwunguza mwili wake uwe majivu.
Punde akaja tarishi kutoka kwa Kabaka akileta ujumbe wa kwamba Yosefu asiuawe bali afungwe tu. Mambo yalikuwa tayari, amekufa. Mfalme akawa mtu mwenye dhamiri mbaya ya kuua mtu bure. Hapo akaamuru mtu mwingine achomwe moto mahali alipochomewa Mukasa. Mwanga alitoa amri hii akiamini ya kwamba eti majivu ya marehemu Mukasa yakichanganyikana na majivu ya mtu mwingine, hawezi kupatwa na balaa la mizimu. Kabaka akawa anajituliza moyo kwamba sasa ilikuwa vigumu mizimu kumwadhibu.
Siku hiyo ya kuuawa Yosefu Mukasa ilikuwa tarehe 14 Novemba. Alikuwa shahidi wa kwanza wa Kikatoliki kufa kwa jina la Yesu Kristu. Aliaga dunia akiwa na umri wa miaka 25, akamwacha mkewe Klara Batudde akiomboleza kifo chake ki-takatifu.”[380]
Huyu ndiye wa kwanza kati ya Wakatoliki wengi kumwaga damu kwa ajili ya Yesu Kristo katika nchi ya Uganda. Kabla yake vijana watatu

[380] Rejea Pd. J. Franse, *Mashahidi 22 wa Uganda*, T.M.P. Book Department, Tabora, uk.23-26.

Waanglikana, Yosefu Lagamala, Marko Kakumba na Noah Seruwanga, waliuawa na Kabaka Mwanga, Januari 1885.
Mt. Yosefu Mukasa, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

**Novemba 16**

Huko Afrika ya Kaskazini, Wakatoliki wanawakumbuka Wat. **Rufino, Marko, Valerio** na **wenzao**, wote wafiadini.[381]
Huko Bbali, Jamhuri ya ki-demokrasia ya Kongo, Wakatoliki wanamkumbuka **Bernadeta Avutia Namia**, sista wa Shirika la Masista wa Upendo wa ki-mama, aliyeuawa mwaka 2001.

Huko Misri, Wakoptiki wanamkumbuka Mt. **Aniano**, askofu wa pili wa Aleksandria. Pia wanakumbuka siku ile **Kutabarukiwa Makanisa ya Mwanamfalme Theodoro**, mwana wa **Yohane El-Sharbe** na Mwanamfalme **Theodoro El-Mishreke**.[382] Pia kumbukumbu ya Wat. **Dalasina**, **Sofronio** na **Shanazum** (au Shenetom), wafiadini Louksor; Wat. **Fidensiano** na **Potiani**, wafiadini, wakati wa Kaizari Valeriani; **Fulviano**, mwana wa mfalme, Ethiopia, kadiri ya pokeo moja alibatizwa na Mtume Mathayo, katika Karne ya I.
Huko Ethiopia, Wakristu, wanawakumbuka Mt. **Jorji Mkuu** wa mji wa Aleksandria, Misri, mfiadini; Mt. Abba **Nahrou** (Nahrew), mfiadini; Abba **Mina**, askofu wa mji Thmuis (Tamai); Wat. **Zenobio** na dada yake **Zenobia**, na **wenzao wengi** waliokufa wakati huo; Wat. **Merkurio** na kaka yake **Yohane**, watawa Wamisiri.[383]
Waorthodoksi wanawakumbuka Mt. **Mathayo**, Mwinjili na Mt. **Fulvanio**, Mwana Mfalme wa Ethiopia, aliyebatizwa na Mathayo.

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake! Amina.

## Wat. Dalasina na wenzake, Mashahidi

---

[381] *Roman Martyrology,* ed. 1956. Pamoja nao: Bariko, Viktori, Paulo, Honorati, Donati, Vitalis, Januari, and Justo

[382] *Coptic Synaxarium: 20 Hatour.* Wakoptiki wanawakumbuka Mwanamfalme Theodori El-Shotbe tarehe 20 Abib na Mwanamfalme Theodore El-Mishreke tarehe 12 Tubah.

[383] *The Ethiopian Rite Missal, Abba Emmanuel & Abba Brendan Cogavin, 2002, uk 196. Ethiopian Synaxarium: Hedar 07.*

Gavana, Ariani, alipofika Louksor, Misri, akaona moshi kutoka hekaluni. Akauliza kulikoni. Akaambiwa kwamba wenyeji wamekusanyika hekaluni kwa ajili ya kusherehekea sikukuu moja na kuitolea miungu ubani. Akafurahia na kujiambia: “Mji huu unafurahisha moyo wangu.“ Kulikuwa katika mji huu mtu mmoja, kwa jina Shanazum. Alikuwa askari na tangu ujana wake alikuwa anafunga na kusali. Akamwendea Gavana na kusema kwa sauti kubwa: “Mimi ni Mkristo“. Gavana akamwangalia na kumwambia: “Wenyeji wote wa mji huu ni watu wenye hekima, lakini wewe ni mjinga“. Mtakatifu akamjibu: “Mimi si mjinga bali mwenye hekima, nikikusikiliza nitakuwa mjinga.“ Gavana akamwambia: “Njoo na uifukuzie ubani miungu“. “Kumsujudia Shetani! Sitatenda jambo hilo. Ninamwabudu Yesu, Bwana wangu, Kristo, anayesimama karibu nami ili kuniimarisha niweze kukujibu kwa hekima.“ Gavana akaamuru kumtia mnyororo shingoni, kufunga miguu na mikono yake, na kumtia gerezani hadi kesho yake.

Kesho asubuhi mapema, akaketi juu ya kiti chake cha hukumu. Bikira mmoja, kwa jina Dalasina, akamwendea na kusema: “Mimi ni Mkristo“. Gavana akamwambia: “Uisujudie miungu.“ “Kuisujudia miungu, ni jambo moja ambalo sitalitenda kamwe“. Kwa maneno hayo Gavana akakasirika, akaamuru kumning’iniza, kichwa chini miguu juu, na kumpiga na makuti, hadi kifo chake. Dalasina akavumilia mateso hayo mpaka mwisho akimshukuru Mungu. Akasalimia roho yake pole pole na malaika wakaichukua mbinguni. Ilikuwa saa tatu asubuhi.

Baadaye Gawana akaamuru Shanazum kuletwa mbele yake. Akamwambia: “Toa sadaka kwa miungu.“ Akamjibu: “Siwezi kutimiza maneno yako.“ Alipokuwa anasema hayo, askari, kwa jina Sofronio, ambaye alikuwa amesimama mbele ya Gavana, akalia kwa sauti kubwa: “Mimi ni Mkristo!“ Akafungua mkanda wake na kuutupa usoni mwa Gavana akisema: “Tangu leo mimi si askari chini ya amri zako. Mfalme wangu wa kweli ndiye Yesu Kristo. Apewe utukufu.“ Mzee wa baraza akamwambia Gavana: “Bwana, uandike hukumu ya mchawi Shanazum, kwa sababu kama utamwacha, atawaloga mkutano na atatuingiza katika matata kwa sababu yake.“ Akamhukumu mara. Akaamuru kuwafunga Shanazum na Sofronio na kuwaning’iniza kichwa chini na miguu juu na baadaye kukata kamba ili waanguke juu ya kichwa chao na kufa mara.

Askari wakafanya kama Gavana alivyoamuru. Lakini malaika wa Bwana akawashika Sofronio na Shanazum na kuwatelemsha polepole. Minyonyoro ya chuma ikayeyuka kama nta mbele ya moto. Watakatifu wakasimama wazima mbele ya Gavana na kumwambia: "Fungua macho na ututazame, wewe mfuasi wa Ario". Gavana akaamuru kuwafunga juu ya gurudumu na kupigwa na askari. Askari wakawapiga mpaka kuchokachoka, wakati watakatifu hawakujali, kwa sababu malaika wa Bwana aliwasaidia. Gavana akaamuru askari walete mienge na kuwaunguza watakatifu hadi miili yao ipasuke, lakini wao hawakusikia mateso kwa sababu malaika wa Bwana alikuwa pamoja nao kwa kuwaimarisha. Gavana akawaambia: "Mfukuzieni ubani miungu, ama sivyo mtakufa vibaya". Wakamjibu: "Kuhusu maisha, yeyote anayekutii unamtuma motoni. Kifo kwa jina la Kristo ni maisha ya milele, ndiye yule anao uwezo kutuliza mateso yetu." Gavana akaamuru aletwe mafuta ya moto sana na kumwaga katika makoo yao. Wakanena: "Usifikiri kwamba mafuta haya mwenye moto sana yatatudhuru, bali mafuta haya yametutuliza, yamekuwa sababu ya furaha kwa ajili ya roho na mwili wetu. Bwana Yesu ametufundisha akisema, '*Msiwaogope wauuao mwili, wasiweze kuiua na roho; afadhali mwongopeni yule awezaye kuangamiza mwili na roho pia katika Jehanum*' Mt. 10:28". Tena: "*Apendaye baba au mama kuliko mimi, hanistahili; wala apendaye mwana au binti kuliko mimi, hanistahili*." Mt 10:37. Wakatumia maneno mengi ya Biblia.

Gavana akakasirika na maneno yao. Akaamuru kuwapeleka juu ya hekalu refu na kuwatupa, kichwa chini, ili wafe. Askari wakafanya kama walivyoamriwa. Walipowatupa chini, watakatifu hawakuumizwa, kama ilivyoandikwa: "*Kwa kuwa atakuagizia malaika zake wakulinde katika njia zako zote. Mikononi mwao watakuchukua, usije ukajikwaa mguu wako katika jiwe.*" Zab 91:11-12. Basi Gavana akaamuru wakatwe vichwa. Ndipo wakapewa taji la ushahidi.[384]

Mt. Dalasina na wenzake, mtuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

[384] *Arabi-Jacobite Synaxarium*

**Novemba 17**

Huko Kartago, Tunisia, Wakatoliki wanawakumbuka Wat. **Valentino** na **Dubatasio** waliofia dini Kartago.
Huko Visiwa vya Kanari (*Canary*), kumbukumbu ya Mwenyeheri **Lorenza Dias Bolanos**, Sista wa Shirika la Mabinti wa upendo wa Padri Vinsenti Paulo, 1936.
Huko Bunia, katika Jamhuri ya ki-demokrasia ya Kongo, Wakatoliki wanamkumbuka **Mimia Simons** (Sista Thérèse) wa Shirika la Elimu ya ki-kristo, aliyeuawa mwaka 1964. Huko katika Kambi ya Chimanga, Wakatoliki wanawakumbuka **Yohane Klaudio** (Jean-Claude) **Buhendwa**, padri wa Jimbo la Bukavu na wakimbizi Wahutu kama 500, waliouawa na waasi Banyamulenge, mwaka 1966.
Huko Msumbiji, Wakatoliki wanamkumbuka **Alfredi Dos Santos Tinancha**, mlei, aliyetekwa nyara, pamoja na **wengine 15** na kuuawa na waasi.
Huko Gulu, Uganda, Wakatoliki wanamkumbuka **Gresi Akullu**, mlei nesi, aliyeuawa mwaka 2000.

Wakoptiki wanamkuwabuka Patriarka **Kosma II**, askofu wa 54 wa Aleksandria; Wat. **Alfeo**, **Zakeo**, **Romano** na **Yohane**, na Wat. **Tomaso**, **Viktori** and **Isaka** wa mji wa Ashmunen;[385] Pia kumbukumbu za Wat. **Viktori**, mfiadini Hierapolis, **Watawa 100** wanakoriti wa jangwa la Watzif, Misri, wafiadini. Pia kumbukumbu ya Mt. **Yohane wa Assiut**, mwanakoriti.[386]
Waorthodoksi wanamkumbuka Mt. **Longino**, Karne la IV au V.
Huko Ethiopia, Wakristu wanamkumbuka Mt. **Kopronio** (Kefrenya). Waorthodoksi Tewahedo, wanawakumbuka **Mashahidi mia nne na themanini na wanne** waliokuwa wenzake Isidori.[387]

---

385 *Coptic Synaxarium: 21 Hatour.* Watakatifu hawa wanakumbukwa katika Ethiopian Synaxarium tarehe
386 *Arabi-Jacobite Synaxarium*
387 *The Ethiopian Rite Missal, Abba Emmanuel & Abba Brendan Cogavin, 2002, uk 196. Ethiopian Synaxarium: Hedar 08.*

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake! Amina.

## Mt. Longino, Karne la IV au V

Longino aliishi jangwani mwa Misri, katika Karne la IV au V. Anakumbuka kwa misemo yake: “Mtu aliyefariki hahukumu yeyote, vivyo hivyo kwa mtu mnyenyekevu“. Kwa mtu aliyetaka kuhama mbali alimwambia: “Usipolinda ulimi wako huwezi kuishi mahali popote uendapo.“ Na kwa mtu aliyetaka kuishi katika upweke, alimwambia: “Usipojipatia fadhila unapoishi miongoni mwa watu, hutaweza kufanya hivyo katika maisha ya upweke.“

Kwa maisha yake na maneno yake aliwafundisha watu kupenda unyenyekevu, fadhila bora kuliko kazi zote za kujikania: “Kufunga, kunanyenyekeza mwili, kukesha kunasafisha akili na kukaa kimya kunaongoza mtu kuhuzunika, na kwa kuhuzunika kunaubatiza utu upya na kuutakasa kwa kila dhambi“. Pia ni yeye aliyesema: “Mwaga damu yako na pokea Roho Mtakatifu“.

Mt. Longino, utuombee ili kwa fadhila ya unyenyekevu tumpendeze Mungu daima na milele. Amina.

## Mwenyeheri Sista Lorenza Dias Bolanos, Shahidi 1936

Sista Lorenza alizaliwa katika pango, kama pango wa Bethlehemu, katika mlima wa Azucena, mmoja wa milima ya Roque Nublo, Visiwa vya Kanari, tarehe 10 Agosti 1896. Alikuwa mtoto wa kwanza, kati ya watoto watano. Baba yake alikuwa Juan Diaz Guillen na mama yake Maria del Pino Bolanos Delgado, wote wakulima. Baada ya siku tano akabatizwa katika Parokia ya Guia. Familia yake iliishi mlimani, mbali ya mji, yenye mapato madogo. Kwa hiyo wakati wa utoto na ujana wake baba yake na kaka yake walihamia Cuba kutafuta kazi. Miaka michache kaka yake Manueli akarudi nyumbani, lakini baba yake alibaki Cuba hadi kifo chake, akiacha familia yake katika umaskini.

Lorenza akajifunza kwa mama yake kusoma na kuandika. Akaanza kuwafundisha watoto wa jirani wasioweza kuhudhuria shule kwa sababu ya umbali wa mji Guia na hali mbaya ya barabara. Wakati wa

mavuno alifanya kazi kusaidia familia yake. Akirudi nyumbani baada ya kazi ya siku ile, alioga na kuanza kuwafundisha watoto kusoma na kuandika na kujifunza katekisimu.

Kaka yake Manueli aliporudi, familia ikahamia karibu na mji Guia. Ndipo Lorenza akaanza kuwasiliana na Mabinti wa Upendo wa Mtakatifu Vinsenti wa Paulo. Jumapili alipohudhuria misa katika kanisa la Parokia, mbali na nyumba yao, alienda kuwatembelea wagonjwa hospitalini Mabinti wa Upendo walipofanya kazi. Mdogo wake Jose Ignacio alimsindikiza. Alishuhudia kwamba ni yeye Lorenza aliyemfundisha kusoma na kuandika, kujifunza kusali na kumfundisha katekisimu. Aliongoza rozari kila siku. Alisema: "Daima alikuwa mnyenyekevu. Hakusema neno baya na kuwatendea mabaya mama yetu, familia yetu na jirani zetu. Daima alitaka kutenda mema na kuwasaidia waliohitaji. Ndiyo yeye aliyeimarisha imani ya familia."

Alipojulisha hamu yake ya kujiunga na Shirika la Mabinti wa Upendo, alishauriwa kwanza kwenda shuleni na kujifunza zaidi. Akaingia shule ya Mt. Augustino, huko Las Palmas, mji mkuu wa visiwa wa Kanari. Mwaka 1920 akajiunga na Mabinti wa Upendo na kuanza upostulanti. Tarehe 12 Aprili, 1921, akahamia Madrid, mji mkuu wa Hispania, kuendelea masomo yake katika Shirika. Wakati wa majiundo alitafakari maneno ya Mt. Vinsenti wa Paulo kwa masista: "Maskini wanahitaji mana ya mbinguni; wanahitaji Roho wa Mungu; na wapi mtampata ili kuwashirikisha? Kwa Komunio Takatifu, masista. Wote masista, wakubwa kwa wadogo, wanamhitaji. Ndiyo maana, mjitayarishe vema kupokea uwingi wa Roho wa Mungu". Ekaristi ilikuwa chakula chake cha kila siku na fadhila ya upendo kiini cha maisha yake.

Alipomaliza majiundo yake akapelekwa kufanya kazi katika Chuo cha mabadilisho, Madrid. Akaenda Cadiz kujifunza uuguzi na kupata cheti chake katika somo la magonjwa ya akili. Tarehe 11 Mei 1926 akaweka nadhiri zake. Akakaa huko miaka tisa hadi kifo chake. Wakati ule hali ya siasa katika nchi ya Hispania ilianza kuwa baya dhidi ya dini ya kikristo. Tarehe 22 Novemba 1936 akafariki shahidi. Alikuwa na umri wa miaka arobaini.

Mwenyeheri Sista Lorenza, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

**Novemba 18**

Huko Tunisia, Wakatoliki wanawakumbuka Wat. **Orikulo** na **wenzake**, wafiadini, Tunisia. Waliouawa kwa ajili ya imani ya Kanisa Katoliki, wakati wa dhiki iliyosababishwa na Waharabu (*Vandals*).[388]
Huko visiwa vya Kanari, kumbukumbu ya Mtumishi wa Mungu **Bonaventura Godina Augerolas**, Askofu, 1857.
Huko Uganda, Wakatoliki wanamkumbuka **Fransisko Bakanibona**, mlei, aliyeuawa mwaka 1982.

Huko Ethiopia, Wakristu wanamkumbuka Abba **Isaka**, Patriarka, askofu wa 41 wa Aleksandria.[389]

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake! Amina.

## Mtumishi wa Mungu Bonaventura, 1857

Bonaventura alizaliwa tarehe 3 Juni 1785 huko Girona, Hispania. Alijifunza falsafa na teolojia. Mwaka 1809 akajiunga na Shirika la Mt. Vinsenti wa Paulo. Akapadirishwa. Kwa muda wa miaka ishirini alikuwa anawaongoza Masista wa Shirika la Mabinti wa Upendo wa Mt. Vinsenti wa Paulo, huko Hispania. Mwaka 1848 alipata daraja la uaskofu na akawa askofu wa visiwa wa Kanari. Katika safari yake ya kwanza alisindikizwa na Mtakatifu Klareti. Wakati wa mlipuko wa tauni aliwatunza wagonjwa bila kujibakiza. Akafariki mwaka 1857, akiacha kumbukumbu ya kuishi maisha matakatifu. Baada ya miaka walipofungua kaburi lake waliukuta mwili wake haujaoza. Mchakato wa kumtangaza Mtakatifu ulianza mwaka 1993.
Mtumishi wa Mungu Buanaventura, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

---

[388] *Roman Martyrology,* ed. 1956.
[389] *The Ethiopian Rite Missal, Abba Emmanuel & Abba Brendan Cogavin, 2002, uk 197. Ethiopian Synaxarium: Hedar 09.*

## Fransisko Bakanibona, 1982

Fransisko alizaliwa Bamugolodde, karibu na Kasaala, Uganda, tarehe 11 mwezi wa Februari, mwaka 1957. Wazazi wake walikuwa Laurenti Minani na Terezia Tawakiliye, wakristo. Alibatizwa tarehe 27 mwezi ule na mwaka ule. Akapata kipa-imara tarehe 14, mwezi wa Novemba, mwaka 1965. Baada ya muda katika Shirika la Mitume wa Yesu, alirudi Kasaala na kuanza kujitoa katika Jumuiya ya Wakristo, kama mwalimu, kiongozi wa kwaya na shughuli nyingine za parokia. Mwaka 1972 akafahamiana na mkondo wa neema uitwao ‘Ushirika na Uhuru‘ (*Communion and Liberation*).

Kwa sababu ya hali ya kukosa usalama katika mkoa wa Luweero, siku moja Padri akamwambia: “Bakanibona ni hatari, kuna vizuizi vingi, siyo salama kufika kila siku kwa misa“. Akamjibu: “Nakutii, lakini tarehe 4 Oktoba, sikukuu ya somo wangu nitakuja, hata ikiwa wanataka kuniua“. Alipoondoka kwenda Kanisani, mama yake alikuwa na wasiwasi mwingi. Fransisko akamwambia: “Naenda kusali, kupokea komunio na kukutana na rafiki zangu. Sikutenda mabaya yoyote, kwa nini kuniua?“

Tarehe 18 Novemba, mwaka 1982 alikamatwa na askari, akishtakiwa kuwafundisha waasi katika darasa lake: “Wewe ni mmojawapo anayewafundisha waasi!“ Askari mmoja akampiga kichwani kwa rungu. Fransisko akalia: “Maria, mama, wanataka kuniua! Sikutenda mabaya yoteyote. Sina uhusiano wowote na waasi.“ Na mara akaanguka chini, akafa. Baadaye, baba yake akauawa pia.

Siku chache kabla ya kufariki Fransisko alimwandikia mmisionari mmoja barua: “Ahsante sana, kwa barua yako ya tarehe 14 Oktoba, unaponitia moyo kwa kuwakumbusha watu kwamba ni kwa njia ya Ushirika tunapata amani, upendo na umoja. Tuliongea na walimu kuhusu jambo hilo na baadhi yao walianza kubadilisha mwenendo wao. Wengine zamani hawakuenda kanisani, sasa wanaenda. Katika mazungumzo yetu wengi walitambua kwamba ‘Ushirika na Upendo‘ vinaleta umoja na mwisho amani. Lakini kuna swali moja: ‘Namna gani tunaweza kuweka Kristo awe kiini cha Ushirika huo? Ndilo tunalojaribu kuwaeleza watu tunaokutana nao. Wanaelewa kwamba Ushirika unazaa amani, hasa wakati tunaoishi. Lakini namna gani

tunaweza kuunda umoja huo? ‘Farijianeni ninyi kwa ninyi wakati tunao mwanga wa mchana‘, ndiyo wito wetu. Lazima Kristo awe kiini cha maisha yetu. Tunakuomba utuombee Padri. Leo tunaenda kwa likizo, wote tunaenda nyumbani. Hakutakuwa na mkutano wowote, lakini yaliyopandwa moyoni mwetu, ndiyo tutakayowapa wengine ... Utusamehe, hatukuandikia mengi. Kwa sababu ya kukosa usalama hatubaki mahali pamoja muda mrefu. Tukipata nafasi tutakuambia mang’amuzi yetu tutakayopata wakati wa likizo. Yote kwa sifa ya Mungu. Wako, Fransisko Bakanibona“.[390]

Fransisko, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

[390] Rejea Fr. Neno Contra,, Louis Kalonji, *African Lay Martyrs*, New People Media Centre, 2009, uk 75-76.

**Novemba 19**

Huko Misri, Wakatoliki wanamkumbuka Mt. **Fausto**, shemasi, mfiadini Aleksandria. Alihamishwa pamoja na Mt. Dionisi, wakati wa dhiki iliyosababishwa na Kaizari Valeriani. Baadaye, wakati wa Kaizari Dioklesiani, akiwa mzee, aliuawa kwa upanga.[391]
Huko Gethrabi, karibu na Sinai, kumbukumbu ya **watawa 12** na **wenyeji 26** waliouawa na Wasarasins.[392]
Huko Isangi, Jamhuri ya ki-demokrasia ya Kongo, Wakatoliki wanawakumbuka **Anne Lucy Donniacuo** (Sista Marie-Antoinette), **Kristiana Guillaume** (Sista Anne-Françoise) wa Shirika la Mabinti wa Hekima (*Filles de la Sagesse*), na **Leo Ammerlaan,** Padri wa Shirika la Montfortain, waliouawa mwaka 1964. Na huko Boso Djanoa, Wakatoliki wanamkumbuka Mtu wa Mungu **Rafaeli Assimoa**, Katekista, aliyefariki mwaka 2001.
Huko Kenya, Wamisioanri wa Shirika la *Consolata* wanamkumbuka Padri **Mikaeli** (Michele) **Stallone**, aliyeuawa mwka 1995.
Huko Jamhuri ya Afrika ya Kati, Wakatoliki wanamkumbuka **Raimundi** (Raymond) **Daké**, mwandishi wa habari, mlei, aliyeuawa na waasi, mwaka 2002.

Huko Ethiopia, Waorthodoksi Tewahedo, Ethiopia, wanamkumbuka **Gabra Maryam**.[393]

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake! Amina.

## Daké Raimundi, 2002

Raimundi alizaliwa tarehe 16 Aprili, 1962, Baouar, Wilaya wa Nana Mambere, nchi ya Tchad. Alikuwa mwana wa Bouca Victor na Kondjo Antoinette. Familia yake ilikuwa maskini. Raimundi alikuwa na akili na

---

391 *Roman Martyrology,* ed. 1956.
392 *Les Petits Bollandistes*
393 *Ethiopian Synaxarium, Hedar* 10.

vipaji vingi, kwa hiyo alisaidiwa na wafadhili kumaliza shule ya msingi na ya sekondari. Baada ya kuhitimu katika *Martyrs College*, huko Bangui, akajiunga na Chuo Kikuu akichukua masomo ya Modern Art.

Mwanzoni alifundisha huko Birao na baadaye huko Bossangoa na Batangafo. Alifanya kazi kwa bidii kuwalelea ki-maadili wanafunzi wake. Akaenda Lyon, Ufaransa, kuchukua kozi ya uandishi wa habari. Aliporudi akafanya kazi katika Radio Ndoyé, katika jimbo katoliki la Bossangoa mwaka 1994.

Askari wa majeshi ya Fransisko Bozizé walifika Bossangoa tarehe 19 Novemba mwaka 2002. Wakaanza kupora mali. Watu wote wa maeneo ya mji walikimbia, isipokuwa wenyeji wa eneo la Waislamu na wa soko la Boro. Askari wakapora na kuharibu hospitali, duka la madawa, zahanati, kituo cha wenye ukoma wa Raoul Follereau,[394] kituo cha Ndjobombe, ofisi za serikali, makao ya maji na mawasiliano, nyumba za mapadri na masista, nyumba za VIP, gareji ya Askofu, n.k. Nyumba ya Askofu ilibomoka kabisa. Mungu anajua kwa nini! Baadhi ya wamisionari waliteswa. Wakati ule Padri Jean Claude Kilamong aliuawa na waasi Waislamu kutoka nchi ya Chad.[395] Jioni waasi waliingia katika ofisi za Radio Ndoyé, Raimundi alipokuwa anatangaza programu yake. Wakawauawa walinzi wawili na kumshtaki Raimundi kuwa msaliti, wakifikiri kwamba anawasemea vibaya. Wakachukua fedha aliyokuwa nayo na kumpeleka sokoni. Akateswa na mwisho wakamwua.[396]

Mtu wa Mungu Raimundi, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

[394] Rejea tarehe 6 Desemba
[395] Rejea tarehe 9 Desemba
[396] Rejea Fr. Neno Contra,, Louis Kalonji, *African Lay Martyrs*, New People Media Centre, 2009, uk. 120.

**Novemba 20**

Huko Torino, Italia, Wakatoliki wanawakumbuka, Wat. **Oktavio**, **Solutori** na **Adventori**, askari wa jeshi la Theba, waliopiga vita kwa ujasiri kwa ajili ya imani yao na kufa mashahidi, Kaizari Maksiminiani alipotawala.[397]

Huko Nampula, Msumbiji, Wakatoliki wanamkumbuka **Baptista Alirio**, Padri, aliyeuawa mwaka 1983.[398]

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake! Amina.

## Oktavio na wenzake, Karne la III-IV

Hatujui habari nyingi kuhusu Watakatifu hawa. Wote watatu walitajwa katika hotuba moja na Mt. Maksimo wa Turino, lakini hataji mahali walipouawa wala wakati gani.

Inasemekana kwamba walikuwa askari ya jeshi la Theba, mwishoni mwa Karne la III. Kiongozi wao, Mt. Morisi, alipouawa huko Agaumun, pamoja na askari wengi, Solutori, Adventori na Oktavio walitoroka. Lakini Adventori na Oktavio walikamatwa huko Dora Riparia na kuuawa palepale. Solutor aliuawa katika machimbo huko Dora Baltea, karibu na Caravino. Mama Mkristo mmoja alichukua miili yao na kuipeleka Turino.

Mwaka 490 Viktori wa Turino, askofu wa mji Turino, alipanua kanisa lililohifadhi masalia yao. Mwaka 1006 monasteri Mtakatifu Solutori ilijengwa pale pale. Monasteri ilipobomolewa masalia yao yalipelekwa Turino na mwaka 1619 waliwekwa katika Kanisa la Mashahidi Watakatifu (*Sancti Martiri*).

Kadiri ya Ngano moja, mnamo mwaka 1844 Bikira Maria alimtokea Mt. Don Bosco katika ndoto, na kumwonyesha mahali ambapo Adventori na Oktavio walipouawa. Basilika la Bikira Maria Msaidizi

---

[397] *Roman Martyrology,* ed. 1956.

[398] Rejea Fr. Neno Contra,, Louis Kalonji, *African Lay Martyrs*, New People Media Centre, 2009, uk. 52

(*Auxiliatrix*) limejengwa pale pale. Mt. Solutori anaheshimiwa hasa katika jimbo la Ivrea, Italia.
Wat. Solutori, Adventori na Oktavio, mtuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

**Novemba 21**

Sisi Wakatoliki tunamkumbuka, huko Roma, Mt. **Gelasio** Mwafrika, Baba Mtakatifu aliyetoka Afrika ya Kaskazini, akiheshimiwa sana kwa elimu na utakatifu wake.[399]

Huko Libya, kumbukumbu ya Mt. **Rufo** (*Rufus*), mmoja wa wafanyakazi wa Kanisa la awali.[400]

Huko Ethiopia, Wakatoliki wanakumbuka pia tokeo la Mt. Yohane Mbatizaji huko Dabra-Mahew.[401] Kumbukumbu pia ya Mt. **Diseo,** Mwungama-dini.[402]

Huko Kenya, Wakatoliki wanamkumbuka Mtumishi wa Mungu **Petro Kamako**, mlei wa jimbo la Murang'a, Kenya, aliyezaliwa Zanzibar, Tanzania, mwaka 1899 na kuuawa na waasi MauMau, Kirinyaga East, Kenya, mwaka 1953.

Huko Moshi, Tanzania, Wakatoliki wanamkumbuka **Yosefu** (*Joseph*) **Kilasala**, Askofu, aliyefariki mwaka 1978.

Huko Mongbwalu, Jamhuri ya ki-demokrasia ya Kongo, Wakatoliki wanamkumbuka **Bonifasio Bwanalongba wo Tsatsi**, padri wa Jimbo la Bunia, aliyeuawa wakati jeshi la UPC na MLC waliteka mji. Watu karibu 200 waliuawa, mwaka 2002.

Huko Kembong Manfz, Kameroun, Wakatoliki wanamkumbuka **Kosma Omboto Ondari**, Mkenya, Padri na Missionari wa Mill Hill, aliyeuawa mwaka 2019.

Huko Ethiopia, Wakristu wanamkumbuka Mt. **Filoteo**, Patrirarka, askofu wa 63 wa Aleksandria, Misri na kifo cha **Ba'eda Maryam I**, Mfalme wa Ethiopia.[403]

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake! Amina.

---

[399] *Martyrologium Romanum,* ed. 2001.

[400] *Les Petits Bollandiste.*

[401] *The Ethiopian Rite Missal, Abba Emmanuel & Abba Brendan Cogavin, 2002, uk 198.*

[402] Dictionary of Saints

[403] *Ethiopian Synaxarium: Hedar 11.*

## Mt. Rufo, karne la I

Alikuwa mwana wa Simoni wa Kirene, Libya, aliyebeba msalaba wa Yesu Kristo. Alitajwa katika Mk 15:21 na Paulo katika barua yake kwa Rum 16:13. Inaonekana kwamba alijulikana sana katika Kanisa la awali.

Kitabu cha zamani cha Watakatifu wa Kanisa Katoliki kilimtaja kama Wafuasi wa kwanza wa Yesu Kristo, waliokuwa waanzilishi wa Kanisa miongoni mwa Wayahudi na Wapagani. Kwa sababu baba yake alikuwa na mashamba huko Palestina, mababu wa imani yetu walifikiri kwamba walikuwa Wayahudi, lakini walizaliwa Kirene, Libya, Afrika. Baada ya kupaa Yesu Kristo Rufo aliendа kuhuburi Habari Njema ya Yesu huko Misri, nchi nyingine za Afrika, Ugiriki, Roma, Hispania na Asia. Inawezekana kwamba Rufo alikuwepo Roma wakati Mt. Paulo aliandika barua yake kwa Warumi na kusema: "*Nisalimieni Rufo, mteule katika Bwana, na mama yake, aliye mama yangu pia*." Rum 16:13. Maneno hayo yanaweza kumaanisha kwamba Bwana Yesu mwenyewe aliyemchagua Rufo kuwa mtumishi wake. Polikarpo katika barua yake kwa Wafilipi, kilichoandikwa mnamo mwaka 107, anampendekeza Rufo kama mfano wa uvumilivu na utakatifu.

Mapokeo yanatuambia kwamba Mt. Petro alimtawaza Rufo kuwa askofu wa Theba, Misri, wakati ule ule alimtawaza Marko kuwa askofu wa Aleksandria. Baadaye Rufo aliendа Hispania na kuwa askofu wa mji wa Tortosa. Akafariki katika mji ule, bila kumwaga damu yake kama watumishi wengine wa Yesu Kristo.

Mt. Rufo, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

## Mt. Gelasio, Baba Mtakatifu, 496.

Gelasio I alikuwa Mwafrika kwa wazazi wake, ingawa alizaliwa Roma, Italia. Akateuliwa kuwa Baba Mtakatifu mwaka 492. Kabla alikuwa Shemasi Mkuu kwa Baba Mtakatifu Feliksi III. Wakati wa utawala wake uhusiano na Askofu Eufemio wa Konstantinopoli haukuwa mzuri kwa sababu jina la askofu Akasio liliandikwa katika *diptychs* za Kanisa la Konstantinopoli na kusomwa wakati wa ibada ya misa. Wakati

alipokuwa askofu wa Konstantinopoli, Akasio alionyesha mwelekeo wa kujitenga.

Utawala wake unakumbuka kwa mambo muhimu aliyotenda. Mwaka 494 aliandika barua *Duo sunt* kwa Kaizari Anastasio kuhusu ushusiano kati ya Serikali na Kanisa. Akafundisha utengano wa mamlaka ya ki-roho na mamlaka ya ki-dunia. Mamlaka ya ki-roho yakiwa juu ya mamlaka ya ki-dunia. Pia akapigana sana kukomesha michezo ya ki-pagani *Lupercalia* huko Roma. Siku hiyo, iliyoadhimishwa mwezi wa Februari (kwa Kilatini *februare* inamaanisha kutakasa), iliangaliwa na wapagani kama siku ya kurutubishwa (*fertility*) na kutakaswa. Mahali pake aliweka sikukuu ya kutakaswa Bikira Maria, tarehe 2 Februari. Akasababisha vitabu vya uzushi wa Manikeo vichomwe. Akafariki tarehe 21 Novemba, mwaka 496 B.K.

Mt. Gelasio, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

**Novemba 22**

Huko Moroko na Roma, Wakatoliki wanamkumbuka, Mt. **Mauro**, shahidi, alipotoka Afrika kutembelea makaburi ya Mitume, akakamatwa kwa sababu alikuwa Mkristo na kuhukumiwa afe, wakati wa utawala wa Kaizari Numeriani, na Selerino alipokuwa Liwali wa Roma.[404]
Huko Aljeria, Wakatoliki wanawakumbuka **Yohana de Patmos** (*Andrée Heymann*), **Maria de Borgia** (*Francis Wilkinson*), **Maria Domitila** (*Emma Tetu*), **Maria Angelika** (*Madeleine Hertzog*), **Fransiska wa Geneva** (*Louise Marsat*), na **Maria Hermina** (*Victorine Biard*), masista wa Shirika la Masista Wamisionari wa Bikira Maria wa Afrika (MSOLA), waliouawa kwa shambulio la mizinga mwaka 1942 huko mji Aljeria.
Huko Kalonge, Jamhuri wa Ki-demokrasia ya Kongo, Wakatoliki wanamkumbuka **Jorji Kakuja**, Padri wa Jimbo, aliyeuawa mwaka 1999.

Huko Misri, Wakoptiki wanawakumbuka Wat. **Krisogono**, **Verosiono**, **Selariano** na dada yake **Tatusbaya**, wote wafiadini.
Huko Ethiopia, Wakristu wanawakumbuka Mt. **Zakaria**, Patriarka, askofu wa 64 wa Aleksandria, Misri; Abba **Timotheo**, askofu wa Ansena.[405]

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake! Amina.

## Masista waliouawa Aljeria, 1942

Wakati wa Vita vya Pili vya Dunia, nchi ya Aljeria ilikuwa nchi ya amani. Lakini mwezi wa Novemba, mwaka 1942, majeshi ya *Alliés* walitua Moroko na Aljeria. Wajerumani walianza kushambulia kwa

---

[404] *Roman Martyrology,* ed. 1956
[405] *The Ethiopian Rite Missal, Abba Emmanuel & Abba Brendan Cogavin, 2002, uk 199. Ethiopian Synaxarium, Hedar 13*.

makombora maeneo muhimu kuzuia adui yao kuingia ndani zaidi. Mji Aljeria lilikuwa moja. Walilenga majengo ya ki-jeshi, lakini makombora mengine yalianguka kati ya nyumba za raia wa kawaida.
Wakati wa mashambulizi Sista Yohana de Patmos na wenzake walikataa kuacha wagonjwa wao na kukimbia mahali pengine pa usalama. Jioni ya tarehe 22 Novemba, masista walipokusanyika kanisani, kombora moja ilianguka juu ya ki-kanisa. Watano walifariki siku hiyo. Sista Yohana de Patmos akaanguka mbele ya tabernakulo. Sista Maria Hermina akafariki siku chache baadaye, tarehe 27 Novemba, kutokana na majeraha yake.
Mungu kaamua na anajua la kufanya. Sista Maria Angelika alikuwa tayari kukutana na Bwana wake. Baada ya kifo chake, karatasi iliyoandikwa na mkono wake, asubuhi ya tarehe hiyo Novemba 22 ilipatikana. Aliandika kwamba anarudia kumtolea Mungu maisha yake yote na kuwa tayari kutenda tu mapenzi ya Mungu.
Sista Maria de Borgia alikuwa daktari kabla ya kujiunga na Shirika la Wamisionari wa Afrika. Siku moja mama mkubwa akamwuliza kwa nini hakuingia katika Shirika ambalo lina madaktari na kazi yake ni kuwatunza wagonjwa. Akamjibu ”Ningeingia katika shirika kama hilo ningekuwa daktari tu na ningetafuta bado wito wangu. Katika Shirika letu, nimeingia kama mmisionari ili kuwaletea mwanga wa Injili wale ambao hawamjui bado Kristo”.
Siku nyingine alisema ”Mimi ni daktari na ninapenda kazi yangu, lakini kama ningekuwa sista bora kwa kuwa dobi tu, basi mahali pangu ni katika udobi”.
Sista Yohana de Patmos kwa tabia yake nzuri, mpole lakini mwenye nguvu sana na upendo mkubwa kwa watu aliwavuta urafiki wa wote. Maisha yake ya kila siku yalikuwa ‘Ndiyo’ kwa mapenzi ya Mungu. ‘Ndiyo ‘ yake ikazawadiwa kwa sadaka ya maisha yake. Mungu alimwita awe karibu naye daima.
Masista hawa walitimiza katika maisha yao maneno ya Karolo Kardinali Lavigerie aliyowaandikia: “Masista wajifanye watumwa wa wote (1 Kor 9:19) ... wasirudi nyuma mbele ya mateso, hata mbele ya kifo, ili waeneze Ufalme wa Mungu“. Maneno hayo yaliandikwa tena na tena katika Katiba ya Shirika lao: ‘*Upendo wa Kristo watubidisha*‘ (2 Kor 5:14), unatupatia nguvu ya kuishi kweli upinzani wa misioni

yetu ... unatusukuma kujifanya watumwa wa wote, tusirudi nyuma mbele ya mateso, hata mbele ya kifo, ili tueneze Ufalme wa Mungu.“[406] Masista ‘watakatifu‘, mtuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

[406] *Constitutions*, 1981, N°9.

**Novemba 23**

Huko Misri, Wakatoliki wanawakumbu Wat **Augusta** na **Faustina**, wanawake wa Aleksandria walioishi vizuri ukristo wao hadi kufa.[407]
Wakatoliki pia wanawakumbuka Wat. **Takla Hawaryat** na **Gabra Yohane,** waungama-dini.[408]

Wakoptiki wanamkumbuka Mt. **Yakobo mwili uliokatwakatwa** (James the Mangled). Aliuawa huko Persia, lakini baada ya dhiki, mwili wake ukahamishwa Misri na kuzikwa katika monasteri ya mji Behnasa.[409] Pia kumbukumbu ya Mt. **Iskirioni**, askofu na mkaa pweke, huko Shete, Misri.
Huko Ethiopia, Wakristu wanamkumbuka Abba **Yohane** wa Dabra-Bizen. Waorthodoksi Tewahedo wanawakumbuka **Garses**, **Balaten**, **Lauresto**, **Andrea**, **Mabrano**, **Tratina**, **Justina** na **Kutabarukiwa Kanisa la Monasteri ya Kalmon**.[410] Kumbukumbu ya **Walata Petros**.

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake! Amina.

## Walata Petros Orthodox, Ethiopia, 1643



Walata Petros ndiye mmojawapo miongoni mwa wanawake wachache watakatifu wa Ethiopia. Alishika nafasi kubwa katika mabishano kati ya Waorthodoksi na Wakatoliki kuhusu nafsi ya Yesu Kristo, hulka mbili, msimamo wa Wakatoliki, au hulka

[407] Kwa kuwa hayajulikani mengine kuhusu historia yao, hawaorodheshwai teni na Maryrologium Romanum. Pengine Augusta ni yule aliyetajwa tarehe 23 Novemba na kheshimiwa na Wakoptiki.
[408] *Les petits Bollandistes*
[409] *Coptic Synaxarium: 27 Hatour.*
[410] *The Ethiopian Rite Missal, Abba Emmanuel & Abba Brendan Cogavin, 2002, uk 199. Ethiopian Synaxarium: Hedar 14.*

moja, msimamo wa Waorthodoksi, wakati wa utawala wa Kaizari Susneyos (1607-1632). Kaizari huyu aliwapokea wamisionari wakatoliki na kukubali imani yao. Mwandika wasifu, ambaye hajulikani, anatusimulia kwamba Walata amezaliwa mwaka 1594. Baba yake Baher Saggad alikuwa mtu wa ukoo bora wa mkoa Dawaro na Fatajar. Mama yake alikuwa Krestos Ebaya.

Walata Petros akaolewa na Malkea Krestos, mtu maarufu wa utawala wa Susneyos. Lakini hakujali upendo wa mume wake, wala mali aliyomjalia. Tangu ujana wake alitamani kuwa mtawa. Wamisionari Wajesuiti na Waorthodoksi walipoanza malumbano Walata akawa upande wa Waorthodoksi. Mume wake alimzuia jaribu lake la kwanza kuingia katika konventi. Baada ya maasi ya Yolyos, mkwe wa Mfalme Susneyos, mwezi wa Mei 1617, Yolyos mwenyewe na Abuna Semeon Askofu Mkuu wa Wakoptiki walipofariki, mabishano yalianza kuwa mabaya zaidi. Ndipo Walata Petros, akiwa na umri wa miaka 24 aliamua kuvunja ndoa yake. Akikusanya kikundi cha wanawake, miongoni mwao wafuasi wake waaminifu Walata Krestos na Eheta Krestos, akakaa huko Waldebba, karibu kilomita 150 kaskazini mwa Gondar, mahali marudufu kwa wakaa pweke na wanakoriti.

Kwa sababu ya kazi ya Walata Petros na wafuasi wake kupinga msimamo wa Kanisa Katoliki Mfalme Susneyos akawaita mbele ya Baraza. Muda mrefu wakadhurumiwa. Na wakati ule wakapinga jitihada zote za Askofu Mkatoliki, Alfonso Mendez, kuwaongoa ili washike imani Katoliki. Kwa amri ya Mfalme Susneyos wakahamishwa huko Jabal, Magharibi mwa Ethiopia. Huko wakavumilia aina mbalimbali ya mateso, kwa ujasiri na hadhi, kiasi kwamba walinzi walimruhusu kuwakusanya watu na kuwafundisha.

Huko Jabal alianzisha Jumuiya ya kwanza kati ya jumuiya saba atakazoanzisha, kufuata unabii aliosikia alipokuwa Waldebba. Mwishoni Waorthodoksi wakashinda huko Ikulu, na Walata Petros akaruhusiwa kwenda kwenye ziwa la Tana, mahali alipoanzisha jumuiya mbili, ya Chenqwa na Mesela.

Mwaka 1632 Mfalme Susneyos akaacha kuwalazimisha raia kufuata dini ya Katoliki huko Ethiopia. Muda si muda akafariki. Mwanaye Fasilidas (1632-1667) akatawala. Akarudisha dini ya Orthodoksi. Ndipo Walata Petros akaheshimiwa sana na kuangaliwa kuwa shujaa. Lakini

kuliko kurudi katika jumuiya moja, kwa miaka 12 ya mwisho ya maisha yake, akasafiri katika nchi yake, akifundisha kwa nguvu zaidi, na kuwakusanya wafuasi wapya. Akafariki tarehe 24 Novemba, 1643, baada ya kutaja mwandamizi wake Eheta Krestos. Alizikwa katika kisiwa cha Rema kati ya ziwa Tana.
Mt. Walata Petros, utuombee ili Wakristo wote wawe na imani moja na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

**Novemba 24**

Huko Abyssinia, Wakatoliki wanamkumbuka Mt. **Likani** (au Abeb Lican), karne la V.[411]
Huko Uganda, Wakatoliki wanamkumbuka **Petro Obore Oromo**, Padri aliyeuawa na Waasi wa Kony, (*Lord Resistance Army*), mwaka 2001.

Huko Misri, Wakoptiki wanamkumbuka Mt. **Sarapamon** (Serabamon), askofu na mfiadini, Nikin, Misri, wakati wa utawala wa Kaizari Dioklesiani, Ariani akiwa gawana wa Antinoe.[412] Huko Aleksandria, Misri, wakati wa ushahidi wa Mt. Katarina, kumbukumbu ya Wat. **Augusta**, malkia, **Porforio**, Jemadari, na **askari 200** (au 300), wote wafiadini.
Waorthodoksi wanamkumbuka Mt. **Petro**, Patriarka wa Aleksandria, Shahidi, 312. Waorthodoksi wa Russia wanawakumbuka leo Mt. **Katarina na wenzake**, na **Mastrida**, bikira, waliofia dini, 303-315.
Huko Ethiopia, Wakristu wanaukumbuka ushahidi wa Mt. **Mina** (Menas). Pia wanamkumbuka Abba **Mina** (Menas II), askofu, Patriarka wa 61 wa Aleksandria, Misri.[413]

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake! Amina.

## Mt. Sarapamon, askofu na mfiadini,

Habari zake zinapatikana katika Kitabu cha Watakatifu wa Kanisa la Wakoptiki. Sarapamon alizaliwa Yerusalemu. Baba yake aliitwa Abrahamu, mwana wa Levi, mwana wa Yosefu, kaka wa Simon na mjomba wa Stefano, Shemasi mkuu na Shahidi wa kwanza. Alikuwa Myahudi kwa kuzaliwa kwake na akaitwa Simoni kama babu yake.
Baba yake alipofariki, Simoni alitamani sana kuwa Mkristo. Malaika wa Bwana akamtokea na kumwambia kwenda kwa Abba Yohane,

[411] *Les petits Bollandistes*
[412] *Coptic Synaxarium: 28 Hatour.*
[413] *The Ethiopian Rite Missal, Abba Emmanuel & Abba Brendan Cogavin, 2002, uk 200. Ethiopian Synaxarium: Hedar 15.*

Askofu wa Yerusalemu, aliyemfundisha fumbo la kujimwilisha Bwana wetu Yesu Kristo. Lakini hakuthubutu kumbatiza mjini Yerusalemu, kwa hofu ya Wayahudi. Hakujua la kufanya.

Bikira Maria akamtokea Simoni na kumwambia kwenda Aleksandria, kwa Patriarka Theonas, askofu wa 16 wa Aleksandria. Basi akaondoka, na Malaika wa Bwana, kwa umbo la kibinadamu, alimsindikiza mpaka mji Aleksandria. Akamwendea Patriarka Theonas. Yeye akafurahi kumwona, akamfundisha na kumbatiza.

Baada ya muda akaingia katika monasteri, akawa mtawa katika monasteri wa Abba Severo, El-Zogag pembezoni mwa Aleksandria. Patriarka Theonas alipofariki, Abba Petro, muhuri wa mashahidi, akashika nafasi yake. Askofu Petro akamwita Simoni ili amsaidie katika kazi ya ofisi yake.

Askofu wa mji Niku (Nakiyos) alipokwenda kwa Bwana, Patriarka Petro akamteua Simoni awe askofu wa mji huo. Wakristo wa jimbo la Nakiyos walifurahi sana. Bwana, kwa mikono ya Simoni, akatenda miujiza mingi. Kulikuwepo hekalu la wapagani karibu na mji huo. Askofu Simoni akaombaomba hadi hekalu hilo lilibomoka na kufunikwa na maji. Na upagani ukaondolewa kabisa katika jimbo lake. Pia huko mkoa wa Misri Kusini, uzushi wa Sabilio, aliyefundisha kwamba Baba, Mwana na Roho Mtakatifu ni nafsi mmoja, ulifutwa.

Kaizari Dioklesiani alipomkana Kristo, akaambiwa kwamba Sarapamon, askofu, alizuia dini ya kuiabudu miungu wa uongo, kwa mafundisho yake. Kaizari akaamuru askofu aletwe mbele yake. Anba Sarapamon alipofika Aleksandria, akalala gerezani. Patriarka Petro akafika, akisindikizwa na mapadre kumtazama. Walipokumbatiana wakamwona uso wake uling’aa kama uso wa malaika.

Dioklesiani akamtesa Anba Sarapamon kwa mateso mengi, lakini kila mara Bwana Yesu Kristo akamwinua upya na yeye hakusikia maumivu. Dioklesiani alipoona kwamba watu wengi walimwamini Bwana kwa sababu yake, akamtuma kwa Ariani, Gavana wa Ansena. Akamtesa na kumwonya kwamba atamkata kichwa asipobadilisha mawazo yake. Ikatokea kwamba Ariani alikuwa Aleksandria, kwa hiyo alimchukua Mt. Sarapamon pamoja naye katika meli. Walipofika Niku, mji wake, meli ikasimama na hakuna mtu aliyeweza kuisogeza. Basi wakamtelemsha Mt. na kumpeleka kaskazini wa mji, mahali ambapo

walimkata kichwa. Wakristo walichukua mwili wake kwa heshima kubwa na kuupeleka kanisani.

Mt. Sarapamon, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

**Novemba 25**

Sisi Wakatoliki tunawakumbuka leo Mt. **Katarina**, bikira na shahidi, wakati wa utawala wa Kaizari Maximini; Mt. **Petro**, Patriarka 17 wa mji wa Aleksandria na mfiadini. Alipambwa na fadhila zote. Akakatwa kichwa kwa amri ya Kaizari Galerio Maksimiani; Pamoja naye maaskofu Esiki, Pakomi na Theodori, mapadri Fausto, Dio na Amoni na wengine wengi.

Na huko Moroko Mt. **Markuli**, askofu.[414]

Katika Jamhuri ya ki-demokrasia ya Kongo, Wakatoliki wanawakumbuka:

Huko Dakwa, **Oliva Bradley** (Sista Marguerite) wa Shirika la *Ursuline of Overpelt*, **Arnoldi Vervoord** na **Guilemo Van Wetten**, mapadri wa Shirika la *Le Croisier*, waliouawa mwaka 1964.

Huko Banalia, **Bishop Hermann** (Wenceslas) Padri wa Shirika la Moyo Mtakatifu, **Nera Planquette** (Sista Marie-Pia), **Hilda Tanghe** (Sista Marie-Augusta), **Julia Klara Vandendriessche** (Sista Marie-Juliana), masista wa Shirika la Mt. Vinsenti wa Paulo wa Gits, waliouawa mwaka 1964.

Huko Stanleyville, **Henriko Van der Vegt** (Père Boniface) padri wa Shirika la Moyo Mtakatifu na **wenzake 25**,[415] mapadri, mabruda na masista, waliouawa mwaka 1964.

Tena huko Paulis, **Remi Paramni**, padri wa Shirika la Comboni, **Karolo Van den Broeck** (Ignace), **Yosefu Robberechts** (Valentin), **Martini Albert** (Pie) na **Yohane Deltour** (Xavier), mapadri wa Shirika la Dominiko, waliouawa mwaka 1964.

---

[414] *Martyrologium Romanum,* ed. 2005. Pamoja na Mt. Petro, katika dhiki ile ile, wakateswa mashahidi Fausto padre, Didio na Amonio. Pia wakati ule waliuawa, kwa upanga, maaskofu wanne wa Misri, Fileas, Hesikio, Pakomi na Theodori, pamoja na Wakristo mia sita na sitini.

[415] Waliouawa siku ile: Verberne Henri, padri; Ten Bosch François, Padri; Brabers Martin, Bruda; Conrad Joseph, Padri; Aubert Amor, Padri; Paps Joseph, Bruda; Trausch Jean, Padri; Venerbeek Henri, Bruda; Nieuwkamp Gérard, Padri; Marion Madeleine, Sista; Bauer Julia, Sista; Huberty Elizabeth, sista; Bach Nelly, sista; Kaufmann Marie, sista; Berens Hilda, sista; Henry Hélène, sista; Henry Hélène, sista; Alvarez Maria Dolores, sista; Del Prado Angela, sista; Eslava Irène Pilar, sista; Gorostiaga Rosa, sista;Kraus Thérèse, sissta; Lommel Marie-Thérèse, sista; Roob Anna, sista; Dischiena Angela, sista; Prez Irène, sista.

Huko Leseke, Uganda, Wakatoliki wanamkumbuka **Yohane Mbatizaji Muhindo Januario**, Katekista, aliyeuawa mwaka 1996, pamoja na Mchungaji **Sabuni**, mwanglikana.

Huko Uganda, Waanglikana wanamkumbuka **Sabuni** Mchungaji aliyeuawa mwaka 1996.
Huko Misri, Wakoptiki wanamkumbuka pia Mt. **Petro**, Patriarka, askofu wa 17 wa Aleksandria, Misri, mfiadini.[416]
Huko Ethiopia, Wakristu wanawakumbuka Abba **Yohane wa Huruma**, Patriarka, askofu wa 48 wa Aleksandria, Misri; Mt. **Ksisto**, askofu na mfiadini. Pia wanaadhimisha kumbukumbu ya **Kutabarukiwa Kanisa la Mt.Onufrio (‘Abunafer)**, mkaa jangwani, lililojengwa nje ya mji wa Mesr (Kairo). Waorthodoksi Tewahedo, wanamkumbuka pia Mt. **Danieli**, mtawa.[417]
Waorthodoksi wanawakumbuka Mt. **Augusta**, binti mfalme, **Porfirio Stasteleastes**, jemadari na **askari 200** waliouawa pamoja na Mt. Katarina.

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake! Amina.

## Mt. Katarina, bikira na shahidi (282 – 307)

Katarina alizaliwa Aleksandria na kulelewa ki-pagani. Alikuwa binti wa Kosto (Costus), Gavana wa Aleksandria. Alipata nafasi kujifunza mambo mengi. Aliwaambia wazazi wake kwamba ataolewa tu na mtu ambaye anampita kwa uzuri wake, akili yake, mali yake na cheo chake. Jambo hilo lilikuwa kama unabii wa kumtambua Kristo na kumchukua kama Bwana wake. Akaongoka na kuwa mkristo katika ujana wake.
Kadiri ya masimulizi, yasiyo na uhakika, inasemekana kwamba alimtembelea Kaizari Maksimini na kujaribu kumridhisha kwamba anakosea kuwadhulumu wakristo. Alifaulu kuwaongoa mke wake na

[416] *Coptic Synaxarium: 29 Hatour.*
[417] *The Ethiopian Rite Missal, Abba Emmanuel & Abba Brendan Cogavin, 2002, uk 200. Ethiopian Synaxarium: Hedar 16.*

wanafalsafa wengi ambao Kaizari aliwatuma kushindana naye. Wote baadaye walifariki mashahidi. Lakini alishindwa kumridhisha Kaizari. Kaizari Maksimini akatoa amri kumtupa Katarina gerezani. Watu walipoenda kumtembelea gerezani wakaongoka. Basi Kaizari akaamua afe kwa kulazwa juu ya gurudmu la mateso, lakini gurudumu likavunjika alipoligusa. Basi akakatwa kichwa.



Ki-mapokeo malaika walipeleka mwili wake kwa Mlima Sinai, mahali ambapo, karne la VI, Kaizari Yustini alijenga nyumba ya watawa. Kanisa likajengwa katika ya mwaka 548 ha 565 na likapambwa na picha (*ikons*) nzuri na thamani sana. Wakristo kutoka nchi zote za ulimwengu wanakuja kuhiji.

Heshima ya Mt. Katarina ikaenea mahali pengi. Katika Kanisa Katoliki anasifiwa kama mmoja wa wale waombezi watakatifu kumi na wanne, pamoja na Wat. Barbara, Margarita bikira na Jorji. Inasemekana kwamba alipofariki alimsihi Mungu kujibu maombi ya wale watakaotaja jina lake. Mnamo mwaka 800 watawa waligundua mwili wake huko Mlima Sinai. Nywele zake zikiendelea kukua na mafuta ya uponyaji yakitokea kwenye mwili wake. Wanawake wengi wanamwangalia kama mfano wa ubikira na usafi wa moyo. Ndiye somo wa wasichana na wanafunzi wa kike, mlinzi wa mabikira. Wanawake wa ki-orthodoksi wanamsihi wakati wa kujifungua kwao. Wanafalsafa, wanateolojia, walumbaji wengi wanatafuta maombezi yake kabla ya kuanza kazi zao. Inasemekana kwamba Mt. Yohana wa Ark alisikia sauti yake na kuwa mshauri wake.[418]

Kwa sababu ya ukosefu wa uhakika wa maisha yake, mwaka 1969, baada ya Mtaguso wa Vatikano wa pili, Kanisa Katoliki limeondoa sikukuu yake katika Kalenda yake. Lakini mwaka 2002 sikukuu yake imerudishwa katika Kalenda yake, kama kumbukumbu ya hiari.

Mt. Katarina, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

---

[418] Maisha yake ya ajabu yamesimuliwa katika kitabu cha Askofu Mkuu wa Genoa, Jacobus de Voragine, 1275: *The Golden Legend*, tome VII. Kitabu hicho kilichapwa mara ya kwanza mwaka 1470.

## Mt. Petro I, Patriarka na mfiadini, 311.

Wakoptiki wanasadiki kwamba Petro alikabidhiwa na wazazi wake kwa Mwadhama Patriarka Theonas ili kulelewa hadi kuwa padri, sawa sawa kama Samueli katika Agano la Kale, alivyokabidhiwa kwa Kuhani Eli, huko Shilo. Akapanda daraja za upadrisho, kwanza kuwa msomaji, baadaye shemasi, na mwisho padri. Patriarka Theonas alipokaribia kufariki aliwashauri viongozi wa Kanisa kumchagua Petro awe mwandamizi wake. Wakafanya hivyo.

Alipokuwa askofu, aliliongoza Kanisa la Mungu katika amani miaka mitatu, akifundisha wakristo wake na kuonyesha fadhila zake nyingi. Akawapadirisha maaskofu hamsini na tano. Askofu wa mwisho alikuwa Meletio wa Likopolis, aliyetengwa baadaye na Kanisa. Lakini wakati wa Kaizari Dioklesiani, madhulumu mabaya dhidi ya wakristo yalianza mwaka 303 na kuendelea miaka kumi kwa mfululizo. Patriarka Petro alitupwa gerezani pamoja na Askofu Meletio of Likopolis. Wakaanza kubishana kuhusu namna ya kuwatendea wakristo waliotoa sadaka kwa miungu wa kipagani au kuyakabidhi Maandiko Matakatifu kwa viongozi wa Serikali ili kujisalimisha. Partriarka Petro alidai huruma wakati Askofu Melitio alisisitiza kwamba wale walioanguka ni waasi, walimkana Yesu, wanahitaji kubatizwa upya. Wakabishanabishana hadi Askofu Petro akaweka pazia kati ya yeye na Askofu mwenzake Melitio.

Kaisari Dioklesiani alipopata habari kwamba Patriarka Petro yupo gerezani alitoa amri kwamba akatwe kichwa. Tendo hilo lilizuiliwa na umati wa wakristo waliokusanyika mlangoni pa gereza, wakiwa tayari kufariki kwa ajili ya Patriarka wao. Maaskari walikawiza kutekeleza amri hiyo kwa sababu hawakuwa tayari kuwaua watu wengi namna hiyo, wala kusababisha ghasia. Patriarka Petro, akiogopa vifo vya wakristo wake, akawashauri askari kumtoa gerezani kwa kutoboa tundu katika ukuta wa gereza. Kwa namna hiyo ataweza kutoka na kupokea hukumu yake.

Alipotoka gerezani akapelekwa mahali pa kuawa. Njiani aliwaomba askari kumpeleka kwenye kaburi ya Mt. Marko. Akapiga magoti na kusali kwa muda mrefu akiomba kuimarishwa katika imani yake. Mwishoni akasema: “Yesu Kristo, Mwana wa pekee, Neno la Mungu

Baba, unisikilize ninapokusihi huruma yako. Nena amani kwa dhoruba inayotikisa Kanisa lako. Kwa kumwaga damu yangu, mimi mtumishi wako, usimamishe madhulumu ya taifa lako." Usiku ule alipokuwa anaomba, akasikia sauti kutoka mbinguni: "Petro alikuwa wa kwanza kati ya Mitume, Petro ni askofu wa mwisho wa Aleksandria atakayekufa shahidi." Alipomaliza sala zake akabusu kaburi la Mt. Marko na kuwaendea askari.

Alipokaribia kukatwa kichwa, Patriarka akavua omoforion yake [419], na, akiwa shingo tupu akawaambia askari: “Tendeni kama mlivyoamriwa". Lakini askari waliogopa kwamba watapata shida kwa sababu yake. Kwa hiyo wakatazamana na hakuna hata mmoja aliyethubutu kumkata kichwa, kwa sababu ya hofu iliyowaangukia. Basi wakashauriana na kusema: “Kwa yule atakayemkata kichwa kila mmoja atampatia denari tano". Walikuwa askari sita. Mmoja wao alikuwa na fedha. Basi akatoa denari ishirini na tano na kusema: “Yule atakayeenda kumkata kichwa atapokea fedha hizo kutoka kwangu na wenzangu wanne“. Mmoja wao akaenda mbele, na akijipa moyo akamkata kichwa cha Patriarka. Ilikuwa tarehe 25 (au 26), mwezi wa Novemba, mwaka 311.[420]

Mt. Petro, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

[419] *Omopharion* ni kitambaa chembamba kilichotaraziwa na chenye misalaba minne na nyota yenye ncha nane. Askofu anaivaa shingoni mwake, hasa wakati wa ibada.

[420] Maisha yake yameandikwa na Anastasio Bibliothecarius kwa lugha ya Kilatini.

**November 26**

Huko Aleksandria, Misri, Wakatoliki wanawakumbuka Wat. **Fausto**, padri, **Didio** na **Amonio**, pamoja na **Fileas**, **Hesikio**, **Pakomi** na **Theodori**, maaskofu, na wenzao **waamini mia sita sitini**, waliokufa mashahidi, wakati wa utawala wa Makaisari Galerio na Maksimiani.
Huko Afrika ya Kaskazini, kumbukumbu ya Mt. **Viktorina**, mfiadini.[421]
Huko Ethiopia, Wakatoliki wanamkumbuka **Shenouti**.
Huko Ufaransa, Aljeria na Tunisia, kumbukumbu ya Mtu wa Mungu Mwadhama **Karolo Kardinali Lavigerie**, mwanzilishi wa Shirika la Wamisionari wa Afrika (*White Fathers*) na Shirika la Wamisionari wa Masista wa Bikira Maria wa Afrika (*White Sisters*). Alifariki mwaka 1892.
Katika Jamhuri ya ki-demokrasia ya Kongo, Wakatoliki wanawakumbuka:

Huko Watsa, **Aleksi Duchesne** (*Reginald*), padri wa Shirika la Dominiko na **wenzake 14** mapadri, mabruda na masista waliouawa mwaka 1964.

Huko Wamba, **Yosefu Wittebols**, askofu, na **wenzake 7** mapadri na bruda wa Shirika la Moyo Mtakatifu.

Huko Mambasa, **Bernardo Sarnes**, **Henriko** (*Heinz*) **Eberlein**, **Andrea Gorse**, **Bernardo Mathias**, wote mabruda wa Shirika la Ndugu wadogo wa Yesu (*Petit Frère de Jésus*) waliouawa mwaka 1964. [422]

Huko Misri, Wakoptiki wanawakumbuka Wat. **Beirina**, **Monas**, **Viktoriana**, Wafiadini; Wat. **Hesikio** (Heyschius) na **Theodori**, maaskofu, Misri.

---

[421] *Les petits Bollandistes*

[422] Waliouawa huko Watsa: Dox Pierre, padri; Dox François, padri; Broche Maurice, bruda; Jacobs Charles, padri; Bayens Michel, bruda; Balfroid Luce, sista; Branle Juliette, sista; Burnotte Jeanne Marie, sista; Caprasse Elizabeth, sista; George Marie Louise, sista; Longly Simone, sista; Merry Jeanne, sista; Pepinster Germaine, sista; Royer Ida, sista.
Waliouawa huko Wamba: Bellinckx Charles, padre; Vandael Christian, padri; Vandemoere Jerôme, padre; Janssen Léon, padre; Burnotte Clément, padri; Moreau Jacques, padre; Laureys André, bruda.

Huko Ethiopia, Wakristu wanamkumbuka **Walata-Petros**, mwanamke wa Ethiopia.[423] Waorthodoksi Tewahedo wanawakumbuka Wat. **Abrahamu,** mke wake **Harika** na mtoto wao **Kedo 'Amlak**; na wenye haki, wafiadini katika jangwa la Wasif, na Abba **Sinoda**, abate.[424]

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake! Amina.

## Mtu wa Mungu, Karolo Kardinali Lavigerie, 1892.

Karolo Martial Allemand Lavigerie, Kardinali na Askofu Mkuu wa Aljeria na Kartago, Primate wa Afrika nzima, Mfanya Kampeni kupinga utumwa, Mmisionari na Mwanzilishi wa mashirika, alizaliwa Bayonne, Ufaransa, mwaka 1825. Baada ya kumaliza shule za sekondari alijifunza teolojia huko Paris. Akapadirishwa, na mwaka 1854, akawa Profesa wa Historia ya Kanisa, katika Chuo kikuu cha *La Sorbonne*, Paris. Mwaka 1860 akasafiri kwenda Lebanoni na Siria, kuwasaidia Wakristo waliodhulumiwa na Wadruse. Katika safari yake alikutana na Abd el Kader, kiongozi wa nchi ya Aljeria, aliyehamishwa na serikali ya Ufaransa. Akavutiwa na ubinadamu na Uislamu wake. Akapenda sana Makanisa ya Mashariki na liturujia zao, akitambua hatari kumezwa na Uislamu na liturujia ya ki-Latini ya Kanisa Katoliki. Aliporudi akachaguliwa kuwa mmojawapo wa mahakama ya kipapa. Kule Roma akakutana na Mt. Danieli Comboni aliyemweleza mipango yake kuhusu Afrika.

Mwaka 1983 akateuliwa kuwa Askofu wa Nancy, Ufaransa. Muda si muda jina lake lilipendekezwa kuwa Askofu Mkuu wa Lyons, Primate wa Wafaransa, lakini alikataa, kwa sababu alipenda zaidi kuwa askofu huko Afrika. Mwaka 1867 akachaguliwa kuwa Askofu Mkuu wa mji Aljeria. Wakati huo, tangu mwaka 1930, nchi ya Aljeria ilikuwa koloni la Wafaransa na chini ya utawala wa Napoleon III ikaitwa 'Ufalme wa ki-Arabu'. Ingawa Serikali ya Ufaransa iliweka vikwazo kuwaongoa

[423] Rejea maisha yake tarehe 23 Novemba

[424] *The Ethiopian Rite Missal, Abba Emmanuel & Abba Brendan Cogavin, 2002, uk 201. Ethiopian Synaxarium: Hedar 17.*

Waislamu, Lavigerie alitangaza wazi kwamba alikuja Aljeria kuwahudumia watu wote wa Aljeria, na nia yake ilikuwa kuinjilisha bara yote ya Afrika.

Kwa kutimiza lengo lake mwaka 1868 alianzisha Shirika la Wamisionari wa Afrika, waliojulikana kwa jina la *White Fathers*, na mwaka ufuatao alianzisha Shirika la Masista wa Mama wa Afrika, waliojulikana kwa jina la *White Sisters*. Mwanzo ulikuwa mgumu, lakini baadaye Mashirika hayo ya ki-mataifa yaliwavuta watu wengi kutoka Ufaransa, Ubelgiji, Uholanzi, Ujerumani na Canada. Lavigerie akajenga nyumba za yatima na mashule ya watoto walioteseka na njaa katika Aljeria.



Mwaka 1868 aliteuliwa na Baba Mtakatifu kuwa Mwakilishi wa kitume wa eneo la Sahara na Sudan na miaka kumi baadaye alikabidhiwa kazi ya kuinjilisha Afrika chini ya jangwa la Sahara. Mwaka 1878 alianzisha seminari huko Yerusalemu kwa ajili ya wanafunzi Wakatoliki wa Kanisa la ki-Melkiti. Lengo lake, kuwa Patriarka wa Yerusalemu ili kuzuia kuwalazimisha Wakristo wa Makanisa ya Mashariki kufuata liturujia ya Kilatini, halikutimizwa.

Kuanzia mwaka 1878 Wamisionari wake wakaingia katika Afrika ya kati maeneo ya maziwa matano makubwa na, baada ya kifo chake, wakaingia katika Afrika wa Magharibi. Aliwapa amri hiyo: "Mwe mitume na mitume tu". Mtume Paulo alikuwa mfano bora kwa Wamisionari wake. Alipenda kuwaambia maneno yake: "*Nimekuwa hali zote kwa watu wote, ili kwa njia zote nipate kuwaokoa watu.*" 1 Kor 9:22. Aliamini kwamba Waafrika, ndio wale watakaoinjilisha bara la Afrika.

Mwaka mzima wa 1878 aliendesha kampeni katika miji mikubwa ya Ulaya ili utumwa ufutwe kabisa ulimwenguni. Katika kampeni hiyo alisimulia jinsi wamisionari walivyoshuhudia mateso makali ya watumwa katika Afrika.

Mwaka 1882, alipofanywa Kardinali, akafufua kiti cha Kartago, Tunisia, akipewa cheo cha Askofu Mkuu (*Primate*) wa Afrika nzima. Na mwaka 1890, kujibu mwaliko wa Baba Mtakatifu Leo XIII, aliwahimiza Wakatoliki wa Ufaransa kuungana na Serikali yao ya ki-jamhuri. Kwa kufanya hivyo alipoteza misaada ya Wakatoliki wengi wa Ufaransa kwa ajili ya misioni zake.

Lavigerie alikuwa na nia thabiti katika kazi yake ya kuwatetea haki za watu. "Mimi ni mwanadamu na hakuna kitu cha ki-binadamu ambacho ni kigeni kwangu. Mimi ni mwanadamu na dhalimu (*injustices*) zinachukiza moyo wangu. Mimi ni mwanadamu na ukandamizaji unaudhi utu wangu." Alimpenda Yesu sana, kiasi kwamba aliweza kuwaambia wamisionari wake: "Watoto wangu, lazima mwe kichaa kuhusu Yesu, kama mimi nilivyo". Akafariki tarehe 26 Novemba 1892.[425]

Mtu wa Mungu Karolo Lavigerie, utuombee Waafrika wamjue Yesu Kristo na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

[425] Habari hizo fupi zimeandikwa kwa Kiingereza na Aylward Shorter, M.afr.

**Novemba 27**

Huko Aleksandira, Wakatoliki wanamkumbuka **Amoni,** Padri na Shahidi, wakati wa dhiki ya Kaizari Maksimini II, mwaka 311.
Huko Abyssinia, Wakatoliki wanamkumbuku Mt. **Mora wa Benhor**, mfiadini.[426]
Huko Aljeria, Wakatoliki wanamkumbuka Mt. **Papiniano**, Askofu, Shahidi Aljeria. Pia wanamkumbuka **Maria Hermina** (Victorine Biard), Sista wa Shirika la Wamisionari wa Bikira Maria wa Afrika, alifariki tarehe 27 baada ya majeraha yaliyosababishwa na mashambulio ya mazinga, tarehe 22 Novemba, mwaka 1942.
Katika Jamhuri ya ki-demokrasia ya Kongo, Wakatoliki wanawakumbuka:

Huko Aba, **Laur Coninx, Leo De Meyer, Paulo D'hoore, Paulo Leys, Karolo Pauwelijn, Alberti Verlinder**, mapadri wa Shirika la Wamisionari wa Afrika (*White Fathers*); **Maria Coopman** (Marie Irène), **Maria Dupont** (Marie-Louise), **Van Dorpe** (Marie-Thérèse), **Adriana Verhoye** (Marie Gerarda), masista wa Shirika la Marie d'Ingelmunster, walioteswa na baadaye kuuawa na waasi WaSimba, mwaka 1964.

Huko Isangi, **Yohane** (Yan) **Groenewege**, Padri na **Yakobo Vos Petrus** (Bruda Isidore), wa Shirika la Mill Hill, waliouawa mwaka 1964.

Huko Bafwasede, **Yohane** (Johannes) **De Vries** (Boniface), **Henriko** (Hans) **Hendrick** (Donat), **Petro Van den Biggelaar** (Joseph), **Arnoldi Schouenberg** (Wiro), **Yohane Slenter** (Louis), **William Vranken** (Pius), mapadri na **William Schouenberg** (Arnulf) bruda wa Shirika la Moyo Mtakatifu, waliouawa mwaka 1964.
Huko Ghana, Wakatoliki wanamkumbuka **Richardi Kardinali Kuuia Baawobr**, askofu wa Wa; aliyechaguliwa kuwa Kardinali mwezi wa Mei 2021 na Mwenyekiti wa Amecea mwezi wa 9 mwaka ule 2021. Alifariki Roma, mwaka 2022.

[426] *Les petits Bollandistes*

Huko Misri, Wakoptiki wanakumbuka **Kutabarukiwa Kanisa la Mt.** Abba **Shenouda**.[427]
Waorthodoksi wanawakumbuka Mt. **Nathanieli wa Nitria** na **Pinoufrio wa Misri**, 375.

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake! Amina.

## Mapadri na Masista waliouawa Aba, 1964

Mwezi wa Novemba mwaka 1964 ulikuwa mwezi wa sadaka ya mapadri, mabruda, masista na walei wengi, waliouawa na waasi WaSimba: huko Ikela, Mambasa, Basoko, Bunia, Isangi, Dakwa, Banalia, Stanleyville, Paulis, Watsa, Wamba, Aba, Bafwasende, Fizi, Paulis, kwa jumla watumishi 103 wa Kanisa, kutoka mashirika mbalimbali na majimbo. Kweli waasi walilenga zaidi kuwaua wamisionari kutoka Ubelgiji, wakifikiriwa kuwa wapelelezi na wasaidizi wa Jeshi la Kongo, lakini chuki yao iligeuka mara nyingi kuwa chuki kwa Kanisa. Ni vigumu kueleza mateso ya wamisionari hawa, ingetumia sehemu kubwa ya kitabu hiki. Vitabu vingi vimeandikwa.[428] Hapa inatosha kueleza kwa kifupi mauaji yalitokea Aba.
Tarehe 26 mwezi Novemba, asubuhi, kundi la waasi WaSimba, walifika misioni ya Aba na wakawashika wamisionari wote, mapadri na masista. Mapadri walipelekwa nyumbani mwa mabruda wazalendo na masista kwa konventi ya masista wazalendo. Mnamo saa 6.00 gari aina ya pick-up iliyojaa waasi ilifika mbele ya nyumba ya mabruda. Mapadri walilazimishwa kuvua soksi na viatu vyao. Padri Coninx mzee ambaye hakuweza kutii haraka alipigwa mateke miguuni mwake, hadi damu ikaanza kutiririka. Mapadri walilundikwa katika gari, mmoja juu ya mwingine, wakipigwa. Masista wakaletwa pia wakati ule katika gari

[427] *Coptic Synaxarium: 1 Kiahk.*
[428] Luc de l'Arbre, *Ils étaient tous fidèles*, Kivu Presses, 2005. Pia rejea Neno Contran na Gilbert Kadjemenje: *Cibles, 235 prêtres africains tués*, Editions Afrique Espoir, Kinshasa ,2002. Pia rejea Neno Contran, *Ils vous ont guettées, 221 religieuses tuées en Afrique*, Editions Espoir, Kinshasa and New People, Nairobi 2000.

iliyofungwa, wakivuliwa shela na viatu. Wote wakafika katika kambi ya jeshi, umbali wa kilometa moja tu. Mateka wakasukumwa nje ya gari na kuingizwa katika darasa. Ndipo ikaanza mateso, madharau, uchokozi, mapigo kwa fimbo. Wafanya biashara wa jirani wakafika na kuwajaribu kuwaokoa kwa kutoa fedha na pombe, lakini askari walinzi, ingawa hawakulipwa kwa wiki nyingi, wakakataa. Hatujui mambo yalivyotukia wakati ule, kwa sababu askari waliowatesa wamisionari waliuawa baadaye na Jeshi la Kongo.

Tarehe 27 Novemba, asubuhi, mnamo saa 1.00, wamisionari wote walikusanywa mahali pa kuwaua. Wakamvuta Padri Coninx nchini. Mapadri wakapigwa risasi. Masista wakateswa zaidi, wakachomwa kwa mikuki na kisu. Mashahidi wanasimulia kwamba waliwaona watu wakivuta maiti na kuwalundika kwa pamoja. Wakamwaga petroli na kuwachoma. Yaliyobaki yakakusanyika na kutupwa shimoni.

Mabruda na masista wazalendo walipopata habari ya mambo yaliyotokea wakakimbia porini, umbali wa kilometa 10 kutoka misioni. Kwa miezi minne wakaishi kule, wakijificha mchana na kutembea usiku. Kila siku walibadilisha mahali pao. Walisaidiwa na wenyeji. Mara chache Mkristo aliweza kuwakaribia na kuwaletea komunio. Kwa neema ya Mungu walikuwa na fedha kidogo na waliweza kununua chakula.

Inaonekana kwamba mauaji hayo yalikuwa shauri la watu wachache. Jumamosi, tarehe 28 Novemba, wakuu wa waasi walipopita Aba, walipopata habari, wakakasirika. Wakalinda kundi lingine la wamisionari, mapadri wa Mt. Augustino na wa Shirika la Verona, waliowaleta Aba. Hawa wakabaki misioni, na miezi mitatu baadaye, waliweza kwenda Sudan na kutoka nchi ile kuruka kwenda Ulaya, kwa msaada wa Wagiriki wafanyakazi, waliowakomboa kwa fedha.

Mapadri na Masista ‘mashahidi‘, mtuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

**Novemba 28**

Huko Afrika wa Kaskazini, Wakatoliki wanawakumbuka Wat. **Papiniano Vitensis** na **Mansueti**, maaskofu na wafiadini wakati ya utawala wa Mfalme Genserik mfuasi wa Ario. Kila kiungo cha mwili wao kilichomwa kwa vyuma vya moto. Pia wakati ule Wat. **Urbano** (wa Girbitano)**, Kresensiani** (Crescens)**, Habetdeo** (au Habedeum)**, Eustrasio, Kreskonio, Vicis, Feliksi**, **Hortulano**, **Florensiano** (au Fientanus), maaskofu, waliohamishwa ugenini kutoka Afrika ya Kaskazini kwa ajili ya dini yao.[429]
Huko Aljeria, Wakatoliki wanamkukumbuka Mt. **Honorati**, Shahidi.[430]
Huko Tunisia, kumbukumbu ya Mt. **Eustrasio** wa Sufres (Sbiba, Tunisia), alihamishwa na Mfalme Genseriki, 453.[431]
Katika Jamhuri ya ki-demokrasia ya Kongo:

Huko Baraka, Wakatoliki wanawakumbuka **Ludoviko Carrara**, padri na **Vittorio Faccin**, bruda, wa Shirika la Wamisionari wa Mt. Ksaveri.

Huko Fizi, Wakatoliki wanawakumbuka **Yohane Didone**, padri wa Shirika la Wamisionari wa Mt. Ksaveri, **Joubert**, padri wa jimbo, waliouawa wote mwaka 1964.
Huko Kibeho, Ruanda, kumbukumbu ya **Matokeo ya Bikira Maria, 1981**.
Huko Butamwa Kigali, Rwanda, Wakatoliki wanamkumbuka **Fransisko Cardinal**, Bruda wa Shirika la Mabruda wa *De La Mennais*, aliyeuawa mwaka 1992.

Huko Misri, Wakoptiki wanamkumbuka Mt. Abba **Hori** (aliyeitwa Hor mwenye nguvu), mwanakoriti. Alimfufua mtoto aliyekufa huko Aleksandria na akarudi kukaa jangwani.[432] Pamoja naye kumbukumbu ya Mt. **Hermini**, mwanakoriti, Misri. Pia kumbukumbu ya mashahidi watakatifu: **Timotheo** na **Theodori**, maaskofu; **Niseforo**, **Petro**,

[429] *Roman Martyrology,* ed. 2005. Pamoja nao: Quodvultdeus, Valerianus. Maisha ya Mansueti yameandikwa na Victor wa Vita.
[430] *Les Petits Bollandistes*
[431] Maisha yake yameandikwa na Askofu Victor wa Vita.
[432] *Coptic Synaxarium: 2 Kiahk.*

**Yohane Sergio** na **Theodori**, mapadre; **Basili** na **Tomaso**, mashemasi; **Danieli**, **Hieroteo**, **Chariton**, **Sokrates**, **Komasio**, **Eusebio**, watawa; na **Etimasio**, wote wafiadini Tiberiopolis, Misri, mwaka 361, 362 B.K.

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake! Amina.

## Wat. Abba Hori na Abba Hermini, wanakoriti

Wakoptiki wa Misri wanamkumbuka leo Abba Hori. Alizaliwa katika mji wa Abraht, wilaya ya Ashmunein. Alikuwa mtawa mteule aliyewapita watakatifu wengi katika kumwabudu Mungu. Alipenda maisha ya upweke, kwa hiyo aliishi jangwani peke yake. Shetani alimwonea wivu. Akamtokea Abba Hori na kumwambia: "Jangwani huwezi kunishinda kwa sababu upo peke yake. Lakini kama wewe ni jasiri, nenda Aleksandria na kule nitakushawishi." Abba Hori alipoyasikia maneno hayo alienda mara Aleksandria. Alibaki kule kwa muda akichota maji kwa wafungwa. Siku moja farasi walikimbia kati ya mji, na mmojawapo alimpiga mtoto na kumwua mara. Abba Hori alisimama mahali mtoto alipouawa. Shetani aliingia moyoni mwa watu waliosimama pale na kuwafanya wapiga kelele: "Aliyeua mtoto huyu ndiye mtawa huyu". Watu wengine walipita kwa njia hiyo na wakasikia. Wakazunguka Abba Hori na kuanza kumdhihaki. Mtakatifu hakuhangaika. Akamchukua mtoto mikononi mwake na alipomwomba Bwana Kristo moyoni, alimfanyia ishara ya msalaba. Roho ya mtoto ikamrudia, na Abba Hori akamkabidhi kwa wazazi wake. Watu wote wakashangaa na kumsifu Mungu. Nyoyo na akili zao zikamwangalia Abba Hori. Yeye akiogopa majivuno, akarudi jangwani na kukaa katika monasteri mmojawapo maishani mwake mwote.

Abba Hori anakumbuka hasa kwa sababu ya uhusiano na Mt. Hermini, Abba, aliyeishi jangwani mwa Misri, na kufariki siku hiyohiyo, mwaka mmoja kabla. Siku moja Mtume Yohane akamtokea. Abba Hori alipotembea jangwani, akamwona mtu aliyevaa nguo za makuti, akifanana na roho. Uso wake uling'aa kwa mwanga mkubwa. Akamkaribia na kuinama mbele yake. Akasema: "Msiogope, mimi

ndimi Yohane Mtume, mwanafunzi mpendwa wa Bwana Yesu Kristo. Hori harakisha kwenda jangwani, na huko utamwona mtu mwenye haki, kwa jina Hermini. Utamtambua kwa sababu anavaa kofia ya kitawa. Yeye ni wa mkoa wa El Bahnasa na anaishi jangwani tangu muda wa miaka sitini akipiga vita ya ki-roho.“ Ndipo Mwinjili Yohane akamsimulia Abba Hori maisha ya Abba Hermini.

“Alipokuwa umri wa miaka kumi akaanza kuwachunga mifugo ya baba yake. Akajifunza zaburi na namna ya kusali. Akafunga kila siku tangu asubuhi hadi jioni. Aliwapenda watu hata mgeni akipita karibu naye akamkaribisha: ‘Tafadhali unibariki kwa uwepo wako na kushiriki chakula pamoja nami‘. Akamtumikia kwa upendo na kumpa maji ya kunywa kutoka kisimani, akibeba mizigo yake na kutembea naye maili moja. Kisha kurudi kuwachunga kondoo wa baba yake. Aliishi fadhila kikamilifu.

Siku moja, Mimi Yohane na Mtume Petro, tukivaa nguo za kitawa tukamtembelea. Alipotuona alitukaribisha. Akatuomba kukaa kijijini mwake hadi kesho asubuhi, lakini tulikataa: ‘Ni afadhali tukae na ndugu zetu katika monasteri‘. Akatusihi: ‘Afadhali mnichukue kwenda pamoja nanyi, kwa sababu Neno la Mungu linasema: ‘*Hakuna mtu aliyeacha nyumba, au ndugu waume, au ndugu wake, au mama, au baba, au watoto, au mashamba, kwa ajili yangu na kwa ajili ya Injili, ila atapewa mara mia sasa wakati huu‘* Mk 10:29-30. Nikamwuliza ikiwa angependa kuwa monaki. Akanijibu: ‘Nipo tayari ikiwa ni mapenzi ya Bwana, na kwa njia ya sala zenu‘. Mara nikachukua mkasi na kunyoa nywele zake na kumvisha nguo ya kitawa. Tukaenda monasteri. Akapokea Komunio na tukamwombea Bwana Yesu Kristo ambariki na kumlinda na hila za Adui, ili Jina la Bwana litukuzwe kila mahali aendapo. Tukamkabidhi kwa Abba Yakobo ili amfundishe sheria za utawa hadi Bwana Yesu atakapomwongoza mahali atakapomchagulia.

Mimi Yohane nikarudi monasteri. Nikapiga hodi mlangoni mwa kijumba chake na nikaingia. Akanisujudia, tukasali. Baada ya kusali nikamwambia: ‘Tuende Kusini hadi mlima Kaw, unaoitwa mlima wa furaha na faraja‘. Abba Yakobo akambariki, tukaenda. Njiani akaniuliza: ‘Mwalimu sijajua jina lako‘. Nikamjibu: ‘Mimi ni Yohane, mwana wa Zebedayo. Tulipokuvisha nguo ya kitawa, Mitume Petro na Paulo, na Mfalme Daudi walikuwa pamoja nami.‘ Tukapita Mlima Assiut na baada ya siku mbili tulifika katika bonde moja. Pango lilikuwepo juu na chini yake chemchemi ya maji ilibubujika, na karibu na maji mitende iliyojaa matunda. Mimi Yohane nilimwambia: ‘Kaa hapa, ule matunda ya miti na kunywa maji ya chemchemi.‘ Nikambariki na nikaondoka.

Hermini akaanza vita vya ki-roho, akisali bila kukoma na kufunga. Malaika walikuwa wakija kumfariji na kumwimarisha, hasa Malaika mkuu Mikaeli, msaada wa watakatifu wanaoishi jangwani. Akaishi miaka mingi maisha ya majikanio, hadi mwili wake ukawa mdhaifu. Mara kwa mara Bwana akamwonyesha mahali palipotayarishwa kwa watakatifu, wale wanaopenda Mungu. Mara nyingi akainuliwa hadi mbingu ya tatu, kama Mtume Paulo.

Shetani akakasirika akimwonea wivu taji zilizotayarishwa kwa ajili ya Hermini. Basi siku moja akimtokea kama malaika mwema akamwambia: ‘Hermini, amka, nenda monasteri na kuishi pamoja na Abba Yakobo.‘ Lakini mtakatifu akijua kwamba tokeo hilo siyo la Mungu akamwambia: ‘Wewe ni nani?‘ Shetani akamjibu: ‘Mimi ni Mikaeli anayesimama mbele ya Mungu!‘ Mtakatifu akasema: ‘Kama ni hivyo tuombe kabla ya kuanza safari‘. Lakini Shetani akasema: ‘Sivyo, siwezi kusali bila jeshi langu la malaika.‘ Mtakatifu akasema: ‘kwa jina la Bwana Yesu Kristo, nakuambia sitaacha mahali hapa hadi utakaponifunulia wewe ni nani!‘ Baada ya kusema hayo, akaanza kusali. Mara wingu la moto likashuka kutoka mbinguni ili kuteketeza Shetani. Akiungua akamlia na kumsihi Hermini kumwokoa kutoka moto huu. Mtakatifu, akisukumwa na upendo mkubwa, akamwokoa. Shetani akamgeukia na kumwambia: ‘Sitapumzika hadi nitakushinda wewe na wale wanaoishi kama wewe‘. Shetani akaondoka, hakuweza kuvumilia nguvu za ki-roho ndani ya Hermini. Basi akakusanya jeshi la askari wake na kuwaambia: ‘Twende na kumshinda Hermini, kwa sababu hakutii sauti yangu na mapenzi yangu! Lazima tumshinde kwa nguvu zetu na kumwibia taji lake la utukufu!‘ Malaika wa Bwana wakamtokea Hermini na kumwambia: ‘Mbarikiwa Hermini uwe hodari na moyo wako usiwe na hofu, kwa sababu Bwana yu pamoja nawe.‘

Shetani akachukua umbo la uongo na kuonekana kama Mfalme katika utukufu wake, akisindikizwa na askari wake sabini. Wakakaribia pango la Mtakatifu na kupiga hodi. Hermini akatoka akisali Zaburi. Alipowaona, akafanya ishara ya msalaba akisema: ‘Bwana anitumie msaada kutoka mbinguni.‘ Ndipo Malaika Mikaeli na Gabrieli wakashuka kutoka mbinguni na kuanza kuwapiga viboko hadi walipolia kwa sauti: ‘Utuhurumie, kwa sababu tuliamriwa na Chifu wetu kuangamiza Hermini. Mtuache na hatutarudi tena mahali hapa.‘ Shetani alipoona mambo hayo, akawa kama upepo na kutoweka jangwani pamoja na askari wake. Mtakatifu akafurahi na kusema: ‘Nilishawishiwa karibu kuanguka, lakini Bwana akanitia nguvu, kwa sababu yeye ndiye utakatifu wangu na wokovu wangu. Ndiyo maana midomo yangu itaimba sifa yako, na Jina lako litahimidiwa milele!‘

Shetani akachungulia kwa mbali. Mwishoni akamtuma mmoja wa askari wake kama dhoruba ya mchanga ikifunika kabisa pango lake. Mtakatifu akainua macho mbinguni na kuomba: ‘Wewe Bwana mwenye huruma uliyejibu sala ya vijana watatu katikati ya moto na kuwaokoa; Uliyesikia ombi la baba yetu Abrahamu na kusikiliza Susana na kumwokoa; Uliyesikia sala ya Yosefu kutoka gerezani na kumwokoa. Nakuomba sasa kunisikia na kunitumia Malaika!‘ Mara Malaika Mikaeli akatokea, akamfunga pepo na kumwambia Hermini: ‘Bwana Yesu Kristo akamweka pepo huyu mikononi mwako ili umfanyie upendavyo‘. Baada ya kusema hayo alipanda mbinguni. Mtakatifu akamwambia pepo: ‘Wewe Adui, unayewapigana na Watakatifu, nakuambia kwa Mungu aliye Hai, sitakuacha hadi utakapoondoa mchanga wote unaofunika pango langu.‘ Mara pepo akawa kama simba na akaanza kuondoa mchanga. Tena Mtakatifu akamwambia: ‘Sitakuacha hadi nitakutesa kama unavyowatesa watakatifu!‘ Pepo akalia na kumwambia chifu wake: “Je, hatukuambia kumwacha Hermini, mtu wa Mungu, katika amani, asitutendee yote aliyotenda Bebnoda, aliyeamuru mwamba

mkubwa utuangamize huko mlima Tookh?‘ Pepo akamsihi na kumwomba Mtakatifu huruma, akaahidi kama akiachiliwa, hatarudi. Kwa hiyo Mtakatifu akamsifu Mungu akisema: ‘Mbingu na Dunia na yote yaliyokuwepo wakusifu, kwa sababu kwa pumzi yako yaliumbwa na kwa sababu ya upendo wako mkubwa, humruhusu Adui wetu kutukanyaga. Kwako utukufu na uweza milele. Amina!‘ Baada ya hayo Hermini akaishi kwa amani, akisali mchana na usiku. Bwana Mungu alimpatia nguvu mpya.“

Baadaye Mtume Yohane akamwambia Abba Hori: “Sasa nimekuambia maisha ya Mtu wa Mungu Hermini, inuka na nenda kumtafuta, ni mzee na mwili wake unaanza kuwa mdhaifu kwa sababu ya majikanio yake. Utamkuta katika pango huko Mlimani Kaw. Andika maisha yake kama nilivyokuambia. Atakuwa mfariji wa wale watakayasoma.“ Mara Abba Hori akainuka na, baada ya kubarikiwa na Mtume Yohane, akaenda kumtafuta. Akamwona akisimama karibu na kisima, katika sala, akinyosha mikono yake. Kutoka vidole vyake ikatoka mionzi ya nuru ikifikia mbinguni. Na harufu nzuri, kama harufu ya ubani, ikamzunguka. Abba Hori akamkaribia kwa upole na kupiga magoti mbele yake. Hermini akamwombea na kumwambia: “Heri wewe unayefika kunitazama kwa sababu Bwana alikutuma kwangu.“

Mara mbili Abba Hori akamtembelea Abba Hermini. Mtume Yohane akamtokea Abba Hori mara nyingine na kumwambia: “Nenda sasa kwa rafiki yako Hermini kwa sababu siku ya kuaga dunia ni karibu. Ni wakati wake kupumzika na magumu ya ulimwengu huu.“ Abba Hori akaenda mara. Akamkuta Abba Hermini katika hali ya kusali, akipiga magoti na kuinama chini. Alibaki hivyo kwa siku arobaini katika sala zake. Abba Hori alipoona jambo hilo alilia sana kwa sababu ya madhaifu yake na majikanio yake ambayo hayakulingana na yale ya watakatifu wake. Akainua macho na kumwona Bwana Yesu Kristo, akishuka kutoka mbinguni katika gari la makerubim, kati ya mkutano mkubwa wa malaika wakimsifu. Bwana Yesu akamwambia Hermini: “Heri wewe, mpendwa wangu, utajazi mara nyingi zaidi. Nitajulisha jina lako ulimwenguni kote. Nimekutayarishia taji tatu, moja kwa usafi wako wa moyo, moja kuishi kama mgeni ulimwenguni humu, na moja kwa sababu ya mateso uliyoteswa kwa jina langu.“ Bwana Yesu akambariki na kurudi mbinguni.

Siku ya kwanza ya mwezi wa Kiahk (Novemba) Abba Hori alimkuta Hermini, uso wake uking’aa kama jua, ndipo alianza kulia. Hermini

akamwambia: “Kwa nini unalia?“ Hori akamjibu: “Kwa sababu utaondoka na kuniacha!“ Akamwangalia Abba Hori na kumwambia: “Ndugu yangu mpendwa Hori, kama jina la Eliya lililojulikana mahali pote, vivyo hivyo jina lako litajulikana na utakuwa baraka kwa wengi, na Bwana atatenda miujiza kwa jina lako.“ Aliposema hiyo akamkumbatia Abba Hori na kurudi kijumbani mwake.

Tarehe 2 mwezi wa Kiahk, Abba Hermini akafariki. Kwa macho yake Hori akashuhudia malaika wakipokea roho ya mtakatifu katika nguo za nuru na kuipeleka mbinguni katika gari la mwanga. Malaika wakuu Mikaeli na Gabrieli walikuwepo wakimsifu Mungu, pamoja na malaika wote, wakiimba na kupiga matarumbeta, njiani mwote kwenda Yerusalemu ya juu.

Mwaka mmoja baadaye, siku ile ya tarehe 2 mwezi wa Kiahk, ilikuwa zamu ya Abba Hori kufariki. Siku ya kuaga duniani ilipokaribia akawaona kundi la watakatifu wakimwita. Akafurahi sana. Akawaita wafuasi wake na kuwaamuru kupiga vita vya ki-roho bila kuchoka na kwamba karibuni atawaaga kwenda kwa Bwana Yesu Kristo. Wakahuzunika na kufikiri kwamba watakuwa yatima bila yeye. Baada ya ugonjwa uliodumu muda mfupi akaisalimia roho yake mikononi mwa Bwana.[433]

Abba Hori na Abba Hermini, mtuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

## Matokeo ya Bikira Maria huko Kibeho, Ruanda, 1981

Matokeo huko Kibeho, Rwanda, yalitukia kuanzia mwaka 1981 hadi mwaka 1989. Bikira Maria aliwatokea wasichana sita na mvulana mmoja. Parokia ya Kibeho iliyoanzishwa mwaka 1935, ilikuwa kwanza parokia moja ya jimbo la Butare hadi mwaka 1990. Wakati jimbo la Gikongoro likasimikwa, Parokia ya Kibeho, ikahesabiwa kuwa parokia mojawapo ya Jimbo mpya. Waamini wengi wakawa mapadri na watawa. Timu ya mapadri wakahudumia Wakristo na Jumuiya ya masista wanafundisha katika shule ya msingi na shule ya sekondari kwa wasichana.

---

[433] Rejea kitabu cha *The Hermit Fathers*, kilichoandikwa na Samaan Pl Souriany.



Mwaka 1981, tarehe 28 Novemba, Bikira Maria alimtokea Msichana mmoja, kwa jina Alfonsina, huko Kibeho. Tokeo la kwanza kwa msichana Alfonsina Mumureke, 16, likatukia katika mesini ya shule kwa wasichana saa 12.35. Akasikia kwamba anaitwa kutoka ushoroba. Akaenda na kumwona Mama wa mbinguni. Akamwomba awe tayari kutenda yote atakayomwambia kutenda. Akaanguka katika jazba. Sista mmoja akamtikisatikisa na kumpeleka katika ofisi yake. Alfonsina akasimulia kila kitu alichoona.“Mama huyu alikuwa mzuri sana. Alivaa kanzu nyeupe. Hakuvaa viatu. Mikono yake ilifungwa pamoja vidole vyake vikielekea mbinguni.“ Lakini hakuna hata mmoja aliyemsadiki. Masista na wanafunzi wakafikiri kwamba alipagawa na kumwona pepo. Akawadharauliwa na wenzake na kuteswa sana. Siku zifuatazo, kila usiku, baada ya saa 3.00, Bikira Maria alimtokea mara kadhaa, na mwishoni akamwomba ‘amwage maji maua yaliyofifia‘. (Inawezekana kwamba inamaanisha ubaya wa dhambi na ufanisi wa maombezi yake).

Tarehe 12 Januari 1982, Bikira Maria akamtokea kwa msichana mwingine Anatalia Mukamazimpaka, 17. Na miezi miwili baadaye akamtokea kwa msichana wa tatu, Maria Klara Mukangango, 21, mmojawapo ambaye hakutaka kuamini. Tangu siku ile wasichana wengine wakaamini.

Habari za matokeo zikaenea kama moto. Watu wengi wakafika Kibeho, wadadisi kwa wamcha Mungu. Tangu mwanzo wa matokeo kulikuwa uponyaji, uongofu na maajabu nyingine ambayo ni vigumu kuyaelewa.

Uchunguzi uliofanywa na viongozi wa Kanisa ukaanza mapema. Mwezi wa Januari, 1982, Askofu akamwalika Alfonsina na kumsihi kumwomba Bikira Maria mambo manne: kumjulisha jina lake; kusema wazi kama ujumbe wake ni kwa ajili ya Kibeho, au Rwanda, au Afrika, au kwa ajili ya ulimwengu mzima; kueleza wazi ujumbe wake; na mwisho kutokea, siyo saa za usiku, bali mahali pakubwa ambapo watu wengi wanaweza kukusanyika.

Tokeo lililofuata, Maria akaonekana uwanjani mwa shule, saa 9.00 alasiri. Akatangaza jina lake: “*Nyina wa Jambo*“, yaani “Mama wa

Neno", mama yake kwa lugha yao "*Umubyeyl w'Imana*" yaani "Mama wa Mungu", au " aliyemzaa Mungu" kama alivyoeleza mwenyewe.
Bikira akaeleza kwamba kusudi la matokeo yake ni kuwapasha watu ujumbe wa uongofu. Akakazana sana ubaya wa dhambi. Akawaonyesha waonaji damu kwa wingi ikitiririka kama mkondo wa maji. Akasisitiza kuacha dhambi na kusali bila kukoma ili kuhusiana daima na Utatu Mtakatifu. Akawafundisha roho ya kujinyima katika kula, kulala, kutumia hella na pia kujifunza kutokana na matukio na mateso ya kila siku. Lakini kwa yote aliwaahidi msaada wake.
Matokeo yaliendelea hadi tarehe 15 Agosti 1983. Kila tokeo lilidumа saa 3 hadi 4. Mwonaji hakuteswa wakati ule ingawa mara alianguka chini, au akakaa muda mrefu juani akiangalia mbinguni. Waliohudhuria walikuwa wengi wakisikiliza kwa makini maneno yaliyosemwa. Wakati wa miaka 1982 na 1983 matokeo yalikuwa marefu kila wiki, bila kuhesabu matokeo mengi zaidi ya binafsi.
Mambo ya ajabu yalitokea kama, mvua ikinywesha wakati wa tokeo, watu walilowana, lakini mwonaji hakulowa, au hostia kubwa kuonekana, au jua kucheza. Jambo la jua kucheza limerudia mara tano. Waonaji walizoea kufunga siku 8, au 14 hadi 15, bila kula wala kunywa. Waliangaliwa kwa makini na madaktari na kulindwa na kundi la masista usiku na mchana. Hata hivyo viungo vyao vyote vilifanya kazi kama kawaida. Walirudia katika uzito wao baada ya siku mbili tu. Mara moja wakati wa tokeo, Alfonsina akamwambia Sista mmoja kwamba Bikira Maria atamchukua katika safari moja: "Nitaonekana kama mfu lakini usinizike." Shahidi mmoja baadaye alisimulia kwamba wakati wa safari hiyo ya ki-roho, ambayo ilidumu saa 6, mwili wake ulikuwa usiopindika, mzito na kama katika hali ya kuzimia. Wakaingiza pini chini ya kucha zake, kuhakikisha pumzi yake, kumwinua, yote bure. Yesu, kama Maria, waliwaomba kukaa katika unyenyekevu na shukrani
Mwisho wa mwezi Machi 1982, Msgr. Jean Baptiste Gahamanyi akaamua uchunguzi rasmi ufanyike. Mwezi wa April 1982, tume mbili zikaundwa, moja ya madaktari na moja ya wanateolojia. Tarehe 15 Agosti, mwaka1988, askofu wa jimbo, akaruhusu rasmi ibada zifanyike huko Kibeho. Jiwe la msingi la Kanisa la kuhiji likawekwa tarehe 28 Novemba 1992. Kanisa likapewa jina la 'Kanisa la Mama wa mateso".

Na tarehe 29 Juni 2001, Mhashamu Misago, askofu wa Gikongoro, siku ya sikukuu ya Wat. Petro na Paulo, wakati wa misa mkuu katika Kanisa kuu la Gikongoro, akatangaza rasmi kwamba Bikira Maria alitokea kweli huko Kibeho. Alionekana kwa uhakika na wasichana watatu.
Bikira Maria, utuombee sisi wakosefu na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

**Novemba 29**

Wafransiskano wanamkumbuka Bruda **Salvatori wa Napoli** aliyetekwa nyara na Waturuki na kubaki utumwani Afrika ya Kaskazini miaka 14. Akafariki mwaka 1641.

Katika Jamhuri ya ki-demokrasia ya Kongo, Wakatoliki wanawakumbuka:

Huko Paulis, Mwenyeheri **Nangapeta Anuarite Alfonsina** (Clémentine), sista wa Shirika la Familia Mtakatifu, aliyeuawa mwaka 1964. Sikukuu yake inaadhimishwa tarehe 1 Desemba.

Huko Kananga, **Yohane Mukoma Mudiandambu**, padri wa Jimbo la Luiza, aliyeuawa mwaka 1993.

Huko Uvira, **Juma Pili Rumanya**, aliyeuawa na askari wasiojulikana, mwaka 2001.[434]

Katika Kanisa Katoliki Tanzania, Jimbo la Songea, kumbukumbu ya Mtumishi wa Mungu Sr. **Bernadeta Mbawala**, Osb. 1950.

Huko Jamhuri ya Afrika ya Kati, kumbukumbu ya **Kolins Declean**, Padri aliyeuawa, 2002.

Huko Misri, Wakoptiki wanawakumbuka Mt. **Fanueli**, askofu, Misri; Mt. **Pitirimi** (au Pitirun, Pithyrion), mtawa na mwungama dini, Misri.

Waorthodoksi wanamkumbuka pia Mt. **Pitirimi**, Karne la IV.

Huko Ethiopia, Wakristu wanamkumbuka Mt. **Aniano**, Patriarka, askofu wa II wa Aleksandria, Misri.[435]

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake! Amina.

## Mt. Pitirimi, mtawa, Karne la IV

Pitirimi aliwaongoza kundi la wasketi mlimani wa Theba. Yeye mwenyewe alikuwa mfuasi na mwandamizi wa tatu wa Mt. Antoni,

[434] Rejea Fr. Neno Contran, Louis Kalonji, *African Lay Martyrs*, New People Media Centre, 2009, uk. 151-152.

[435] *The Ethiopian Rite Missal, Abba Emmanuel & Abba Brendan Cogavin, 2002, uk 202. Ethiopian Synaxarium: Hedar 20.*

kijumbani mwake. Alikula tu unga kidogo uliochanganywa na maji kidogo, mara mbili kwa wiki. Akaendelea katika majikanio na kujaliwa neema nyingi za Roho Mtakatifu. Alifundisha kwamba kwa kila tamaa kuna pepo anayejaribu kuamsha tamaa hiyo kwa njia ya vishawishi mbalimbali. Ili kufukuza pepo huyo na mawazo mabaya, Aba Pitirimi alisema kwamba inatubidii kwanza kutakasa moyo wetu na tamaa.
Mt. Pitirimi, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

## Mtu wa Mungu Bruda Salvatori, 1641

Slavadori akazaliwa huko Villa Magna katika ufalme wa Napoli, Italia. Katika ujana wake aliishi na mjomba wake, mkanoni wa Ortona, karibu na bahari. Siku moja Waturuki waharamia wakamkamata ghafla na kumchukua Afrika. Kwa miaka kumi na nne alivumulia madharau na mateso mengi chini ya mabwana mbalimbali. Mwishoni akawa mtumwa wa mtu mkuu wa Caramania.
Mungu akamhurumia. Ingawa alizungushwa na watu waovu wa dini nyingine, kushauriwa vibaya na kutishwa kupata mateso makali, akabaki Mkristo. Akaafikiana na watumwa wanne Wakristo waliomkumbusha sala alizojifunza ujanani mwake, na kumfundisha kweli za dini letu. Wakamwombea. Pamoja naye walimwomba Mungu awahurumie. Wakapata nguvu za ki-roho na wakaamua kutoroka na wakaanza kujitayarisha kwa siri.
Wakachagua usiku ufuatao mwisho wa Ramadani, usiku Waturuki wanafurahi, wanacheza na kula kwa ulafi. Wakifaulu kutoka kwa aina ya gereza waliomo, wakatembea masaa ishirini na nne wakilindwa na Mungu mwenyesi. Walipoingia katika pango moja, wakasikia sauti iliyowaamuru: “Msitoke mule, au mtafanywa watumwa tena, kwa sababu bwana wenu anawatafuta kila mahali.“ Wakatii na kubaki ndani ya pango.
Lakini akiba yao ya chakula ilipungua na waliogopa siku ambapo watalazimishwa kutoka nje ili kutafuta chakula, wasipotaka kufa kwa njaa. Mungu akawapatia chakula. Asubuhi moja walipoamka wakakuta mikate iliyookwa siku hiyo. Mwujiza huo ukaendelea fululizo kwa muda wa mwezi mmoja. Sauti waliyosikia siku ya kwanza ikasikika tena: “Ndugu zangu, sasa mnaweza kuenda, adui wenu amewasahau.“

Wakaruka nje ya pango na kukimbia kuliko kutembea, wakipita milima na misitu bila njia hadi walifika pwani mwa bahari ya kati. Wakakuta tumbwi ndogo iliyoachwa yenye silaha. Bila kusitasita wakapanda ili kuvuka bahari. Lakini mara walianza safari ngalawa nne wakawafuata. Hawakusita wakatumia bunduki na kuwapiga risasi. Wakaonyesha ushupavu wa ajabu hata waturuki sitini wakakimbia wakibeba wafu na wajeruhi wao. Kwa bahati baya Salvatori akajeruhiwa mkononi.
Walipookolewa na hatari hiyo sasa wakajikuta mbele ya bahari kubwa, ambao hawakuifahamu, yenye dhoruba kali, bila akiba ya chakula, na msaada wa mwanadamu yeyote. Wakamsihi Bikira Maria na wakichota katika ujasiri wa imani yao nguvu, wakatua katika pwani wa Italia. Huko wakimshukuru Mungu kwa msaada aliowapatia, wakatengana, kila mmoja akirudi kwao. Bruda Slavatori akaenda Villa Magna, nchi yake. Akatambuliwa na dada yake. Akapumzika kwa muda katika familia yake. Ndipo Mungu akamwita kumtumikia katika maisha ya kiutawa, shirika la Wafransiskano. Akaishi kitakatifu na kufariki tarehe monasteri ya Sulmoni, Italia, tarehe 29 Novemba 1641.
Br. Salvatori, utuombee kwa Mungu mwenyezi, mjali wetu, ili tukue katika imani yetu.

## Mtumishi wa Mungu Sr. Bernadeta Mbawala, bikira, 1950



Alizaliwa tarehe 27/10/1911 huko Peramiho. [436] Baba yake aliitwa Stefano na mama yake Agata. Tangu kuzaliwa afya yake ilikuwa dhaifu sana. Mkunga aliyemzalisha akamshika mtoto mikononi akimtazama kwa mashaka sana. Akakata tamaa akisema: "Mwasiwawaka! Afwiri!" Maana yake: "Tumesumbuka bure, amekufa!" Lakini mtoto alianza kujimudu, akalia mara moja, akaishi.

[436] Rejea kitabu: Pd. Heribert Meyer, *Sr. Bernadeta Mbawala*, Ndanda-Peramiho Publications. Kitabu hicho kinapatikana katika C. D. Watakatifu wa Afrika, Watu wa Mungu.

Tarehe 5/11/1911 mtoto akabatizwa, akapewa jina la Klara. Alipokuwa na miaka miwili na nusu, Klara alishikwa na ugonjwa mkali. Alikuwa amekonda sana. Basi wazazi wakamchukua na kumpeleka kwa Padri Hilari, katika misioni ya Peramiho, ili ambariki. Akawaambia wampeleke mtoto huyo kanisani kwenye altare ya Bikira Maria Imakulata na kumtolea kwake. Wakafanya hivyo na Klara alipona polepole, akawa mzima tena.

Alipokuwa msichana mwenye umri wa miaka 16 hivi, baba yake alimchumbisha kwa kijana mkristo, lakini Klara akaona kwamba Yesu anamtaka awe mchumba wake wa milele. Hakupata raha moyoni mwake, mpaka aliposhinda vipingamizi vyote vya baba yake. Januari 1928 alipata ruhusa kutoka kwa baba yake na kuingia utawa na masista wenyeji. Wakubwa walimpokea kwa nia ya kumjaribu tu, kwa kuwa hakutimiza umri uliotakiwa. Kwa hiyo baada ya mwaka mmoja akarudishwa nyumbani kwao mpaka atakapotimiza umri wa miaka 18. Alipoomba tena akakubaliwa kuwa mkandidati wa Shirika la Masista wa Mt. Agnes. Sikukuu ya watakatifu wote alifanywa mnovisi na kaitwa Sr. Maria Bernadeta. Daima alijisikia maumivu ya kichwa na ya tumbo. Kwa sababu hiyo, karibu na mwisho wa unovisi wake, wakubwa waliona mashaka sana juu ya afya yake na walitaka kumrudisha nyumbani kwake. Lakini wale waliojua zaidi, walimtetea, kwa sababu waliona jinsi alivyokuwa mfano mzuri kwa wanafunzi wote wa Shirika la Masista. Tarehe 11/11/1934 Sr. Bernadeta na wanovisi wenzake wanne waliweka nadhiri zao za kwanza kwa muda wa mwaka mmoja.

Alipokuwa sista, hakuweza kufanya kazi ngumu kwa sababu ya udhaifu na unyonge wake. Akafanya kazi ndogo ndogo, kama kushona vitu vidogo vidogo kwa mikono. Akawekwa kuwa msimamizi wa nyumba waliomolala wakandidati, kwa sababu ya uaminifu wake wa kushika taratibu za utawa, upole wake na kimya wake. Lakini pole pole mwili wake ulidhoofika.

Wakati wa Kwaresima ya mwaka 1949, alianza kukohoa kidogo kidogo alipokuwa amelala tena kitandani muda wa majuma kadhaa. Yalipochunguzwa makohozi yake kwa darubini, vijidudu vingi vya ugonjwa wa Kifua Kikuu vilionekana. Sr. Bernadeta amekuwa na ugonjwa wa Kifua Kikuu uliokwisha enea sana, hata pafu lake la

kushoto limekwisha oza, kiasi kwamba asiweze kupona wala kupata nafuu. Kadiri ya maoni ya mganga muda wake wa kuishi bado si zaidi ya miaka miwili. Sr. Bernadeta aliposikia habari hizo alizipokea kwa unyofu, akikubali kwa moyo wote mapenzi ya Baba wa milele. Akaoneyesha furaha kweli iliyong'aa usoni pake, kwa sababu alitamani kwa moyo wake wote kumwendea Baba wa mbinguni.

Ilimpasa kuyavumilia mateso makali hayo muda wa mwaka mmoja na nusu, mpaka mwaka 1950. Alifanya hivyo kwa imani kubwa. Padri Heribert aliandika: “Mtumishi wa Mungu Sr. Bernadeta alianza kushiriki kwa upendo mateso ya Mkombozi wetu, na hasa hofu kali aliyoiona katika bustani ya Getsemane alipotokwa na jasho la damu. Kila usiku wa kuamkia Ijumaa, hasa wakati wa Kwaresima na katika siku za Ijumaa za Moyo Mt. wa Yesu, alitumia muda wa saa mbili na zaidi, kumwaza hata kumtazama Yesu mwenye kusongwa moyoni mwake kwa ajili ya mateso makali yatakayompata kwa sababu ya dhambi za wanadamu wote, akajaribu kumtuliza. Ingawa alijibidisha kwa moyo wake wote kumfariji Yesu, Sr. Bernadeta aliona kwamba hafanikiwi kwa kuwa Mkombozi hakutulizwa moyo. Mara kadha wa kadha, Sr. Bernadeta alimwomba padre kwa uchungu na mahangaiko ya mtoto mwema, amwoneshe njia ya kumtuliza Yesu, hata alimwomba akisema: ‘Baba, tusaidiane kumtuliza Yesu!’”[437]

Tarehe 29/11/1950, sikukuu ya Mtume Andrea, mnamo saa 5 ya usiku alifariki katika bwana, akiweka roho yake safi mikononi mwa Baba wa milele. Masista wenzake wote walikuwa wamekusanyika kwenye kitanda chake. Alipozimia roho yake waliimba wimbo wa kuweka nadhiri, huku machozi yakitiriika mashavuni mwao wakisema: "*Unipokee, ee Bwana, ulivyosema, nami nitaishi, wala usikubali nidanganywe na matumaini yangu*", Zab 118.

Mtumishi wa Mungu Bernadeta, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

---

[437] Pd. Heribert Meyer, *Sr. Bernadeta Mbawala OSB*, Benedictine Publications Ndanda – Peramiho, Peramiho Printing Press, 3/2002, p.29-30.

**Novemba 30**

Huko Karema, Tanzania, Wakatoliki wanamkumbuka Mtu wa Mungu **Adolfo Lechaptois**, Askofu, wa Shirika la Wamisionari wa Afrika (*White Fathers*), aliyefariki mwaka 1917.
Huko Kaduna, Nigeria, Wakatoliki wanamkumbuka, **Yakobo Lyere**, Padri, aliyepigwa na baadaye kuchomwa moto na Waislamu wenye imani kali.
Huko Goma, Jamhuri ya ki-demokrasia ya Kongo, Wakatoliki wanamkumbuka **Fokasi Nikwigize**, askofu wa Ruhengeri, Uganda, aliyeuawa mwaka 1996.

Huko Misri, Wakoptiki wanamkumbu Mt. **Psoi** (Bishoi, Besoi), abate na mfuasi wa Pakomi.
Waorthodoksi wanamkumbuka Mt. **Frumensio**, askofu wa kwanza wa Ethiopia, Karne la IV.
Huko Ethiopia, Wakristu wanawakumbuka Mt. Abba **Kosma**, Patriarka, askofu wa 51 wa Aleksandria. Abba **Yohane** wa mji wa Assiut. Waorthodoksi Tehawedo pia wanawakumbuka Wat. **Alfeo**, **Zakeo**, **Romano**, **Yohane**, **Tomaso**, **Viktori**, **Isaka**, wote wa mji wa Eshmunen, wafiadini.[438]

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake! Amina.

## Abba Yohane wa Assiut

Mtakatifu huyu si Yohane Nabii tunayopata habari tarehe 27 Machi, ingawa inaonekana kwamba ana karama ya unabii kama Yohane Nabii na akamtabiria ushindi kwa Kaizari Theodosio. Yohane nabii aliishi huko Likopolis, na Yohane huyu aliishi Assiut.
Wazazi wake walifanya kazi ya kutengeneza vyoo. Akalelewa katika familia ya kikristo. Alipokuwa kijana akajifunza ufundi wa seremala. Wazazi wake walipofariki akawaendea Abba Isidori na Abba Baymani.

[438] *The Ethiopian Rite Missal, Abba Emmanuel & Abba Brendan Cogavin, 2002, uk 203.*

Akavishwa nguo ya utawa. Akaanza maisha ya nidhamu, kwa njia ya kufunga na kusali kwa bidii hata jina lake likaenea katika monasteri nyingine.
Siku moja Malaika wa Bwana akamtokea na kumwamuru aende katika nchi yake na kuwafundisha watu njia ya utakatifu. Wakati ule hakutoka nje ya kijumba, isipokuwa kuhudhuria ibada kanisani. Wazee wawili, Abba Abzeli na Abba Besoi wakafika kwake. Kabla hawajakaribia akalia kwa sauti kuu kutoka mbali: "Amani kwenu, baba zangu" na akawaita kwa majina yao, ingawa hakuwafahamu kabla. Pia Mt. Sinoda, 'Nguzo ya Misri' alizoea kumtembelea na kukumbatia.
Wagapani waliposhambulia nchi ya Misri, Kaizari Theodosio akamtuma Gavana wa Misri kupigana nao. Mtakatifu Yohane akachukua msalaba wake na kumwambia Gavana: "Usiogope. Utashinda". Ndiyo yaliyotokea kadiri ya maneno yake. Mara ya pili vita ikatokea, Kaizari Theodosio akamwuliza Yohane tena. Mtakatifu akamjibu: "Usihuzunike, utashinda." Na Kaizari Maksimiani akawashinda.
Siku moja Kaizari Theodosio akaamuru kuwatuma askari zake kwa mji wa Assiut ili kuwaua wanaume na kuvamia mji kwa sababu kazi ya upuuzi iliyotendeka kule. Sasa Malaika wa Bwana akamjulisha Yohane habari hiyo kabla ya Gavana kufika. Watu waliposikia amri ya Kaizari wakapanda mlima kwenda kwa Abba Yohane. Akawaambia: "Msihuzunike, kwa sababu mapenzi ya Mungu ni kuwaokoa". Gavana alipofika, alienda kwa kijumba cha Mtakatifu Yohane ili kubarikiwa naye. Abba Yohane akamwambia kila kitu Kaizari aliyoamuru. Gavana aliposikia hayo alishangaa, akamsujudia. Alikuwa na mwana wa umri wa miaka kumi na nane ambaye alikuwa amepagawa. Akamwomba Mtakatifu kumponya. Yohane akabariki mafuta na maji, na baada ya kumpaka akapona mara. Ndipo Yohane akamwomba Gavana kumwandikia Kaizari kuacha kuwaua wanaume wa mji wa Assiut. Gavana akafanya hivyo na kumpatia Yohane barua. Akachukua barua na kuingia katika kijumba chake. Akaanza kusali, mara wingu la mwanga likamchukua Abba Yohane na kumpeleka mbele ya Kaizari. Yohane akatupa barua mezani. Kaizari akapokea barua na kuisoma bila kumwona Yohane. Alipoinua macho yake akaona wingu la mwanga lilikuwepo juu ya Yohane. Akaogopa sana. Mara akaandika barua kwa

Gavana kwa mkono wake na kuifunga kwa muhuri wake, ili aache kuuvamia mji wa Assiut. Kaizari akatupa barua juu ya wingu, na wale waliokusanyika pale waliona mkono ukaipokea. Ukaiingiza ndani ya wingu. Usiku ule Mtakatifu akarudi kwa kijumba chake. Kesho yake akampatia Gavana barua hiyo. Gavana akashangaa sana, akamsifu Mungu aliyeokoa mji wa Assiut. Akarudi katika nchi yake.

Sifa za Yohane ikaenea katika nchi ya mbali. Mwanamke mmoja wa ukoo bora, ndugu wa Kaizari akamwenda ili amponye na ugonjwa wake. Kwa maombi yake akapona. Kaizari akafariki na Marsiani mbaya akatawala. Akamtesa Dioskoro. Abba Yohane akamtuma barua akimlaani kwa sababu alibadilisha imani. Baada ya siku chache Mungu akamua.

Yohane alipokuwa na miaka mia moja na ishirini na tano alijua kwamba muda wa kuaga dunia umetimia. Alipokuwa akisali akaanguka nchini na kusalimia roho yake kwa Muumbaji. Ishara na miujiza mingi ikatokea kwenye kaburi lake.[439]

Mt. Yohane utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

## Mtu wa Mungu Adolfo Lechaptois, Askofu, 1917

Kwa miaka ishirini na sita Adolfo Lechasptois alikuwa askofu wa vikariati ya Tanganyika, sasa majimbo ya Sumbawanga, Kigoma, Mpanda na Mbeya katika Tanzania. Alizaliwa tarehe 6 Juni, 1852 huko Ufaransa. Akafuata seminari pamoja na Gerboin, ambaye atachaguliwa kuwa Vika wa kitume wa Unyanyembe, yaani Tabora siku hizi. Akajiunga na Shirika la Wamisionari wa Afrika (*White Fathers*), mwaka 1872. Alipadirishwa na kardinali Lavigerie, mwaka 1878. Kwa miaka mitano alikuwa anafundisha katika Seminari ndogo, na pengine alimsaidia Mlezi wa manovisi huko Maison Carrée. Mwaka 1882 akawa Mlezi wa manovisi mwenyewe na mwaka 1886 Padri mkuu wa mkoa wa Kabylia huko Aljeria. Mwaka 1898 akateuliwa kwenda Afrika ya ndani.

Lechaptois alichaguliwa kuwa Pro-Vika wa Nyasa, kwa hiyo alisafiri kwa njia ya Msumbiji kufikie eneo lake. Akaanzisha misioni ya Mponda, Desemba 1890, kwa kufungua huduma ya kuwatunza

[439] *Ethiopian Synaxarium: Hedar 21.*

wagonjwa na kuwafundisha watu wa Kabila la Yao. Mafundisho yalitolewa kwa lugha ya ki-yao. Kwa muda mfupi akapata wafuasi waaminifu 116. Lakini mambo ya siasa yalimlazimisha kufunga Mponda mwaka 1891 na kwenda huko Mambwe, Rhodesia Kaskazini, siku hizi Zambia, ambayo ilikuwa chini ya madaraka ya *British Souuth Africa Company.*

Mwezi wa Julai 1891 Lechaptois alichaguliwa kuwa Vika wa kitume wa Tanganyika na Msarifu (*Administrator*) wa Nyasa (Mambwe). Alikuwa askofu wa tatu katika eneo linalozunguka ziwa la Tanganyika, sasa kati ya Jamhuri ya ki-demokrasia ya Kongo na Tanzania. Waliomtangulia waliishi muda mfupi. Mhashamu Charbonnier aliishi miezi saba na Mhashamu Bridoux mwaka mmoja tu. Lechaptois akachagua kukaa Karema, zamani ilikuwa Fort Leopold, yaani Ngome ya Leopold. Akaanza kuzuru misioni za Kongo: Mpala, Mrumbi na Kibanga. Eneo lote lilikuwa katika machafuko, kwa sababu ya kazi ya uharibifu uliosababishwa na wafanya biashara ya watumwa, Waarabu kwa Waafrika. Hakuweza kutenda mengi kuuzuia uovu huo isipokuwa kuimarisha misioni na kuendesha vituo vya yatima waliokombolewa kutoka utumwa. Mnamo mwaka 1892 Lechaptois akaikabidhi misioni za Kongo na Askofu Viktori Roelens, pia wa Shirika la Wamisionari wa Afrika, aliyesimamia vikaria hiyo kwa muda wa miaka thelathini na sita.

Mwaka 1895 Lachaptois akapata daraja la uaskofu na Mhashamu Dusserre huko Ufaransa. Akarudi Karema, pamoja na kundi la Masista wa Shirika la Masista wa Bikira Maria wa Afrika, masista wa kwanza kufanya kazi katika eneo hilo. Kati ya 1895 hadi 1901 alianzisha misioni mitano: Kala, Zimba, Utinta, Mkulwe na Galula. Mwanzoni wa Karne la XX kulikuwepo mkazo kujenga shule na vijiji vya Wakristo. Mnamo mwaka 1896 kulikuwepo shule 77 katika misioni na vigango vya vikaria, nyumba 4 za yatima kwa wavulana na moja kwa ajili ya wasichana. Daktari Adrian Atiman aliendesha shule huko Kala. Lechaptois akahamisha shule ya makatekista kutoka Mambwe kwa Utinta pwani mwa ziwa Tanganyika na mwaka 1899 akaihamisha huko Karema. Makatekista walijifunza sambasamba na waseminari. Lakini baadaye, kati ya mwaka 1912 na 1913, Shule ya makatekista ilihamishwa tena kwenda Zimba na Kituo cha Karema kikawa Seminari

ndogo. Miaka miwili waseminari wawili walikuwa tayari kuingia seminari kubwa kujifunza falsafa na teolojia. Lechaptois akaanzisha seminari kubwa huko Utinta chini ya kombera Joseph Birraux, ambaye atashika nafasi yake kama askofu wa Karema, na baadaye kuwa Mkuu wa Shirika la Wamisionari wa Afrika, kutoka mwaka 1936 hadi 1947. Mapadri wawili wa kwanza wa Tanganyika, kutoka Utinta, walipadirishwa mwaka 1923, mmojawapo alikuwa mwana wa Adrian Atiman.

Lechaptois alikuwa kiongozi mwema kwa wamisionari wake. Mtu mwenye bidii sana, wema wa ki-asili na urahisi. Alitembelea kila misioni walau mara moja kwa mwaka. Upendo kwa watu wake na wafanya kazi wenzake ulikuwa kweli. Alikuwa pia mtaalam, akipenda kusoma na kuandika vitabu. Mwaka 1912, huko Paris, kitabu chake kuhusu ethnografia, *Aux Rives du Tanganyika*, kilichapishwa na kupokea tuzo la *Geographical Society of Paris*, mwaka 1912. Kazi yake inaonyesha mtazamo mzuri kwa wenyeji wa eneo, tabia, mila, sanaa na mpangilio wao. Lechaptois, mmojawapo wa waanzishi wa Kanisa Katoliki Tanzania, alifariki kwa pigo la moyo, mwaka 1917.

Mtu wa Mungu Lechaptois, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

**Desemba 1**

Sisi Wakatoliki tunawakumbuka Mt. **Karolo de Foucauld** na Mwenyeheri **Maria Klementina Anwarite Negepeta**.[440]
Kumbukumbu ya Mt. **Simoni wa Kirene**.[441]
Huko Sisilia, Italia, Wakatoliki na Watawa wa Shirika la Ki-fransisko, wanamkumbuka Mhashamu **Inosentia Rizzo**, bikira, mtawa, aliyefariki mwaka 1624. Kwa sababu hakuweza kwenda Afrika kueneza Injili kati ya Waislamu, aliwaombea na kuwashughulikia watumwa Waislamu mahali pake. Akiwa na umri wa miaka kumi na mitano, akakubaliwa na wazazi wake kumpatia uhuru mtumwa Mwislamu. Akamfundisha na akabatizwa. Mtumwa alipokuwa mgonjwa sana, Innosensia akahamia kwenye kitanda chake ili kumtumikia na kumfariji hadi alipofariki.[442]
Huko Hispania na shirika la OdM, wanamkumbuka mtawa Mtakatifu **Yeronimo** (Jeromu) **wa Pratis**, aliyeenda Tunisia kuwakomboa watumwa. Aliuawa na Waislamu kwa mishale kwa ajili ya imani yake, mwaka 1431.
Katika Jamhuri ya ki-demokrasia ya Kongo, Wakatoliki wanawakumbuka:

Huko Bunia, **Petro** (Piet) **De Meyer, Eugenio Pauwelijn, Ludoviko Smissaert**, mapadri wa Shirika la Wamisionari wa Afrika (*White Fathers*) walioteswa na baadaye kuuawa na waasi, kundi la Simba, mwaka 1964.

Huko Rungu, Wakatoliki wanawakumbuka **Fransisko Van den Wyngaert** (Augustin), padri, **Marseli De Doncker** (Vincent), padri, **Norberti Cools** (Joseph), Bruda, wote watawa wa Shirika la Dominiko; **Lorensio Piazza**, **Evaristi Migotti**, **Antoni Zuccali**, mapadri, wa Shirika la Comboni, waliouawa mwaka 1964.

Huko Misri, Wakoptiki wanawakumbuka Mt. **Viktori** (*Boctor*) wa Assiut, mfiadini huko Chu, Misri, na Mt. **Isidori**, mfiadini.[443]

---

[440] *Roman Martyrology,* ed. 2005.
[441] *Roman Martyrology* ya zamani.
[442] *Le Palmier Seraphique*, XII, uk. 21-22.
[443] *Coptic Synaxarium: 5 Kiahk*.. Masalio ya Mt. Besuss yamo katika Kanisa Kuu la Irrea

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake! Amina.


## Mt. Simoni wa Kirene, karne ya I.

Injili za Matayo, Marko na Luka zinamtaja mtu aliyelazimishwa na Warumi kumsaidia Yesu kubeba msalaba wake kuwa Simoni wa Kirene. Kirene palikuwa mahali Wagiriki walipoishi pwani ya Afrika ya Kaskazini. Wayahudi kama 100.000 kutoka Yudea walihamia kule, wakati wa utawala wa Ptomeli Soter (323-285 K.K.). Inawezekana kwamba Simoni alikuwa Myahudi aliyeenda Yerusalemu kuadhimisha sikukuu ya Pasaka. Pengine alikuwa mwenyeji wa Yerusalemu, lakini alizaliwa huko Kirene. Luka anamtofautisha na Simoni mwingine ambaye anamwita Nigeri, yaani Mweusi, (Mdo 13:1). Marko anatuambia kwamba alikuwa baba wa Aleksanda na Rufo, Wakristo waliofahamika sana katika Kanisa la kwanza.
Kadiri ya Pokeo ya zamani, Simoni aliondoka Yerusalemu na kwenda Hispania kuwasaidia waana wake Rufo na Aleksanda waliokuwa wanahubiri Habari Njema ya Yesu huko. Akamshukuru Mungu alipoona jinsi walivyomshuhudia Kristo kati ya wapagani. Akafanya kazi pamoja nao. Inasemekana kwamba Mtume Petro akampatia daraja la uaskofu. Baada ya kumhubiri Yesu Kristo kwa muda katika nchi hiyo alirudi Yerusalemu na kufariki kule. Sikukuu yake inaadhimishwa tarehe 1 Desemba huko Yerusalemu.
Mt. Simoni wa Kirene, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

## Mtakatifu Karolo de Foucauld, padri na mfiadini, 1916

Karolo de Foucauld (Bruda Karolo wa Yesu) alizaliwa mjini Strasbourg, Ufaransa, tarehe 15 Septemba 1858. Alipokuwa na umri wa miaka 6 akawa yatima. Yeye na dada yake Maria wakalelewa na babu yao, afisa wa Jeshi la Ufaransa.
Katika ujana wake aliacha imani yake na hakuenda tena kanisani. Akaanza kuishi maisha ya anasa. Akaonyesha nia thabiti na uvumilivu mkubwa katika matatizo. Akaanza upelelezi nchini Moroko

(1883-1884). Kuona jinsi Waislamu walivyoonyesha imani yao kulimfanya ajiulize: ”Mungu wangu, kama unaishi, unijalie kukufahamu.”
Aliporudi katika Ufaransa alipokelewa vizuri na familia yake na hii ilimsadia kuendelea kumtafuta Mungu. Padri Huvelin alimsaidia kumtambua Mungu upya na mwezi wa Oktoba 1886 akaongoka. Alikuwa na umri wa miaka 28. Akasema: ”Mara nilipomwamini Mungu, nalijua kwamba sikuweza kufanya jambo lingine isipokuwa kuishi kwa ajili yake.”
Alipohiji katika Nchi Takatifu alitambua wito wake: kumfuata Yesu katika maisha yake ya Nazareti. Alikaa miaka 7 katika monasteri ya



ki-Trappist, kwanza katika Ufaransa na baadaye huko Akbès, Siria. Baadaye aliishi peke yake, karibu na konventi ya Wafukara wa Yesu wa Mt. Klara (*Poor Clares*) huko Nazareti, akitumia muda wake kusali na kuabudu.
Akapadirishwa alipokuwa na umri wa miaka 43, mwaka 1901 na alienda kuishi jangwani, kwanza Beni Abbès na baadaye Tamanrasset kati ya Watuaregs mlimani mwa Hoggar, Aljeria. Alitaka kuwa mmoja wa wale “waliokuwa mbali zaidi, na walioachwa”. Alijitahidi kujionyesha kuwa ndugu wa kila mmoja aliyemkaribia, yaani kuwa “ndugu wa wote”. Akiheshimu utamaduni na imani ya wale alioishi nao alijitahidi kutangaza Injili ya Yesu kwa maisha yake. “Nataka kuwa mwema ili watu waseme: ’Ikiwa mtumishi ni mwema kiasi hiki, je, Bwana wake atakuwa mwema kiasi gani?’”
Jioni ya tarehe 1 Desemba 1916, aliuawa na kundi la majambazi waliozingira nyumba yake. Alitangazwa kuwa mwenyeheri tarehe 13 Novemba 2005 na Baba Mtakatifu Yohane Paulo II na Mtkatifu tarhe 15 Mei 2022 na Baba Mtakatifu Fransisko.
Daima alitamani kushirikisha wito wake na wengine. Baada ya kuandika sheria za maisha ya kitawa, alijihakikisha kwamba ‘maisha ya Nazareti’ yanaweza kuishi na wote. Leo kuna shirika mbalimbali zinazofuata roho ya Bruda Karolo wa Yesu.

Mtakatifu Karolo wa Yesu, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

## Mwenyeheri Maria Klementina Anwarite Nengepeta, Mtawa na Mfiadini, 1964



Alfonsina Nengepeta alizaliwa mjini Wamba, Jamhuri ya ki-demokrasia ya Kongo, 29/12/1939, akiwa mtoto wa nne wa Amisi Badjulu na Juliana Isude. Alipofikia umri wa kutosha, alienda kusoma shuleni, na siku ya kwanza alipelekwa na mkubwa wake ambaye aliitwa jina lake Leontina Anwarite. Badala ya kuandika 'Alfonsina Nengepeta', Mwalimu Mkuu alikosea akaandika 'Alfonsina Anwarite'. Hivyo akaanza kuitwa kwa jina la Anwarite.

Alipokuwa bado mtoto, alipenda sana kusali, na kila mara dada zake walipojaribu kumzuia kusali kwa kumcheka na kumkejeli, alikasirika na kulia kwa sauti: "Sitaki kula bila kusali kwanza!" Akiwa na umri wa miaka kumi na miwili, alijiunga na chama cha Watoto wa Ekaristi Takatifu. Alikuwa mfano wa bidii na mwenye upendo kwa wanachama wenzake.

Mwaka 1955, alijiunga na shirika la Masista wa Familia Takatifu lililokuwa limeanzishwa katika mwaka 1936 huko Kongo, akaanza kuitwa Sista Maria Klementina. Siku moja baada ya kuweka nadhiri za kitawa, alishawishiwa sana na mama yake mzazi atoke utawani ili apate kumsaidia katika shughuli za nyumbani. Lakini Sista Anwarite akamjibu kwa ukali: "Wito ni kitu kikubwa. Hatuwezi kuuacha vivi hivi tu. Kwa hilo kosa lako, mama, utafanya malipizi kwa kusali rozari nzima leo hii!"

Mwaka 1960, alihitimu masomo ya ualimu akapewa shahada. Ingawa alikuwa akikasirika haraka, wanafunzi wake waliyaelewa mapendo yake. Alipokuwa katika hali ya kukasirika, alizoea kugugumia mithili ya bubu. Alipomkasirisha mwingine, yeye alinyamaa na kutulia kidogo ili afanye kila lililowezekana kumfurashisha yule aliyemkosea na kumwomba msamaha.

Mwaka 1964, nchi ya Kongo ilikuwa na balaa la mapinduzi. Watu walitishwa na habari za unyang'anyi na mauaji yaliyofanywa na askari waasi waliojaribu kuipindua serikali, nao walijiita Simba. Mnamo tarehe 29 Novemba 1964, kundi la Simba lilifika kwenye konventi ya masista huko Bafwabaka, nao wakaamriwa na Kanali Olombe Openge, wajiandae kwa safari kwenda Paulis. Usiku walipumzika kidogo kwenye misioni ya kijiji kimojawapo, na asubuhi safari ikaendelea tena. Mara kwa mara walilazimika kuzisikiliza kashifa za askari. Wakavuliwa rozari na medali, kuzitupa chini kwa kukufuru. Walipowasili kijiji Isiro, masista walipelekwa kwenye nyumba mojawapo. Wakapumzika na kula chakula kidogo.

Jioni Kanali Ngalo akaja. Akawaangalia masista wote na kusema akimwona Sr. Anwarite, Kanali Olombe akaniambia: "Nataka msichana huyu". Mara akakemewa sana na Mama Mkuu akisema: Jambo hilo halitawezekana kwa kuwa yeye ni bikira aliyebarikiwa kwa ajili ya Mungu". Kanali Ngalo akakasirika mno, akampiga Mama Mkuu kichwani na mikononi, naye akaanza kuvimba sehemu hizo; hata hivyo, hakuchoka kumtetea Sista Anwarite. Basi, wakamchukua na kumpeleka kwenye chumba kingine, na Sista Anwarite akabaki yeye na askari tu. Nao wakamvua shela ya kitawa na kumpiga makofi.

Sista Anwarite akasema wazi: "Mimi sitaki kwenda kwa kanali wenu na kutenda dhambi hii. Iwapo unataka kuniua, basi niue." Alipigwa kikatili na Kanali Petro Olombe, akimwambia: "Wewe unafikirije? Unafikiri kwamba wewe ni mzuri kuliko mke wangu Angelika, ambaye nimemwacha Wamba? Kwa vyovyote ni mzuri kuliko wewe." Sr. Anwarite akamjibu: "Ikiwa ulijua kwamba mke wako ni mzuri kuliko mimi, kwa nini hukumchukua pamoja nawe," Kanali Olombe akakasirika. Wakati huo Sr. Anwarite alikuwa ameangukia magoti, akapigwa tena kichwani na kanali huyo huyo kwa tako la bunduki, akapoteza fahamu. Olombe akaenda kumwambia kanali Ngalo. Akaamriwa kumleta kwa nguvu sista huyu na kuambiwa kwamba Sr. akikataa, basi unaweza kumtendea yote unayotaka. "Ikiwa hamtaki kutii, wewe mwenyewe utauawa kuliko yeye!" Basi Olombe akaamua kumwua kuliko yeye kuuawa.

Afisa mwingine alipoingia katika chumba na kuitambua hasira kubwa ya Kanali Olombe, aliiondoa bunduki yake ili asije akawaua watawa

wote. Lakini huyo aliposhindwa kuiona bunduki, akapiga mayowe na mara wakatokea vijana wawili wenye visu virefu. Wakaamriwa kuchoma Sista Anwarite: "Ingizeni visu vyenu moyoni" akasema mara tatu. Basi, wakamchoma kinyama, kila mmoja wao akifanya hivyo mara nne au tano hivi. Kwa kila pigo Sr. Anwarite alisema kwa sauti ndogo: "Ouh ! Ouh ! Ouh ! " Karibu kufa akasema: "Mniue, lakini msiwatese masista wenzangu. Nawasamehe kwa sababu hamjui mtendalo!" Kanali Olombe, alipoona kwamba Sr. anapumua bado kidogo, akachukua bastola yake, akampiga risasi juu ya mkono wake wa kushoto, akatoka akawaita watawa wengine wauondoe mwili wake. Sista alikuwa bado anapumua, na ilikuwa wazi kwamba alikuwa katika hatua ya mwisho ya kufa. Baada ya muda mfupi tu alikabidhi roho yake kwa Mungu.
Sr. Yohane Baptista, akiona mateso makali hayo, akazimia. Masista wengine waliobaki katika nyumba waliposikia kelele ya bastola wakaanza kuimba "*Magnificat*". Olombe akakasirika sana. Akaingia chumbani, akachukua nondo na kuwapiga masista waliokuwa magotini. Alipoondoka, masista wote wamejeruhiwa, wawili walikuwa na mikono iliyovunjika. Wakalala bila kutibiwa. Asubuhi mapema WaSimba walipoona kwamba wameshindwa wakasema: "Hatujaona wanawake wenye moyo mgumu kama ninyi. Ninyi ni wachawi. Hatutaki mubaki hapa Paulis, nendeni katika konventi yenu Bafwabaka." Afisa mmoja akawarudisha katika konventi yao.
Ilikuwa mnamo tarehe 29 Novemba 1964. Sr. Anwarite alikuwa na umri wa miaka ishirini na sita. Licha ya Sista huyu kutufundisha thamani ya fadhila ya usafi wa moyo, lakini pia maishani mwake twaona vilevile ile bidii ya kuitawala hasira yake, pamoja na upendo mkubwa kwa Yesu wa Ekaristi na kwa Mama Maria. Alipokuwa anashawishiwa na kupigwa na askari, alikuwa na sanamu ndogo ya Mama Maria mfukoni. Waliitambua miezi sita baadaye walipofukua maiti yake ili kuizika kwenye kaburi zuri na bora zaidi. Upendo wake kwa Bikira Maria ulimwimarisha kuulinda usafi wa moyo. Baba Mtakatifu, huko Kinshasa, alimtangaza Mwenye heri tarehe 15 Agosti mwaka 1985, wakati wa ziari yake ya ki-chungaji nchini Kongo. Sikukuu yake

inaadhimishwa tarehe 1 Desemba.[444] Pamoja na Maria Klementina, tukumbuke mamia ya masista wazalendo na wamisionari waliouawa wakati wa machafuko ya ki-siasa.

Mwenyeheri Maria Klementina, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

---

[444] Kadiri ya mashahidi mbalimbali. Pia rejea *Maisha ya Wataktifu*, T.M.P. Book Department, Tabora, chapa 1966, uk 426-428. Rejea kitabu: J. Franse, M.afr. na A.J. Malumwene, Sista Anwarite, Benedictine Publications Ndanda-Peramiho, Tanzania, 1986.

**Desemba 2**

Huko Aljeria, Wakatoliki wanawakumbuka Wat. **Severo** (*Verus*), **Sekundo** (*Securus*), **Januari**, **Viktorino**, wafiadini.[445]
Huko Misri, Wakatoliki wanawakumbuka Mt. **Heraklemoni**, mwanakoriti na wenzake (**Andrea**, **Yohane** na **Theofilo**). Huko Abyssinia, Wakatoliki, pamoja na Waorthodoksi, wanawakumbuka Mt. **Eliabu** na Mt. **Simeoni Afamarie**, waungama dini.[446]
Huko Ethiopia, Wakatoliki wanamkumbuka Mwenyeheri **Elisa Angela Meneguzzi** (*Liduina*), Sista, Dire Dawa, 1941.

Huko Misri, Wakoptiki wanamkumbuka Mt. **Abrahamu**, Patriarka, askofu wa 62 wa Aleksandria, Misri, 978. Inasadikiwa kwamba kwa maombi yake na maombi ya Mt. Simon (Mtengeneza ngozi) ya siku tatu, mlima Mokattam, Mashariki wa Kairo, ukatembea. Pia wanamkumbuka Mt. **Anatolio**, mfiadini.[447]
Huko Ethiopia, Wakristo wanamkumbuka **Kornelio**, akida, aliyetumwa na Mtume Petro kuhubiri Injili mjini Aleksandria. Waorthodoksi Tewahedo wanaadhimisha kumbukumbu ya **kutabarukiwa Kanisa la Marina**.[448]
Waorthodoksi wanawakumbuka pia vijana 4 walioishi jangwani na waliotembelewa na Mt. Pafnusi, **Yohane, Andrea, Heraklemoni** na **Theofilo.**

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake! Amina.

## Mt. Heraklemoni na wenzake, Karne la IV

---

[445] *Martyrologium Romanum,* ed. 1956. Pamoja na Heraklemoni, Yohane, Andrea na Theofilo.
[446] *Les Petits Bollandistes.* Eliabi na Simeoni, kwa kuwa hayajulikani mengine kuhusu historia yao, hawaorodheshwai teni na Maryrologium Romanum.
[447] *Coptic Synaxarium: 6 Kiahk.*
[448] *The Ethiopian Rite Missal, Abba Emmanuel & Abba Brendan Cogavin, 2002, uk 203. Ethiopian Synaxarium: Hedar 23.*

Tunasoma katika maisha ya Mt. Onufrio kwamba baada ya kumzika Onufrio, Mt. Pafnusi alifika katika oasisi ambayo ilimpendeza kwa uzuri wake na uwingi wa matunda yake. Vijana wanne walioishi mahali pale walitoka jangwani na kumkaribisha. Wakamwambia kwamba katika ujana wao waliishi katika mji wa Oxyrhynchus (Mkoa wa Theba) na walijifunza kwa pamoja. Waliwaka na hamu ya kujitoa kwa Mungu. Basi wakafanya shauri kwenda jangwani kwa pamoja. Wakatoka mjini Oxyrhynchus na kutembea kwa siku nyingi, kabla ya kufika mahali pale.


Mtu, aliyeng'aa sana na mwanga wa mbinguni, aliwakaribisha na kuwaongoza kwa Mtawa mzee. "Tumekwisha ishi miaka sita" wakamwambia Pafnusi. "Mzee wetu akaishi mwaka mmoja na kufariki. Sasa tunaishi peke yetu, tunakula matunda ya miti na kunywa maji ya chemchemi." Vijana wakamwambia majina yao: Yohane, Andrea, Heraklemoni na Theofilo.

Vijana walishinda kila mmoja peke yake siku tano ya wiki. Lakini siku ya Jumamosi na Jumapili wanakusanyika pamoja katika oasisi na kumwabudu Mungu. Siku zile malaika wa Mungu anawatokea na kuwakomunisha. Lakini wakati ule wa Mt. Pafnusi walikaa pamoja wiki nzima, hawakuenda jangwani. Jumamosi na Jumapili iliyofuata Mt. Pafnusi pamoja na vijana alijaliwa kupokea komunio kutoka mikono ya malaika na kusikia maneno haya: "Pokea chakula kisichoharibika, heri na uzima wa milele, Mwili na Damu ya Bwana Yesu Kristo, Mungu wetu."

Pafnusi akathubutu kumwomba Malaika ruhusa kukaa jangwani hadi mwisho wa maisha yake. Malaika akamjibu: "Mungu ana mipango mingine kwa ajili yako. Lazima urudi Misri na kuwasimulia Wakristo maisha ya wale wanaokaa jangwani." Alipowaaga vijana, Pafnusi akafika mpakani mwa jangwa baada ya siku tatu ya safari. Hapa alikutana na Watawa katika skete ndogo. Ndugu wakamkaribisha kwa upendo. Akawasimulia yote aliyojifunza kuhusu Mababu Watakatifu aliowakuta jangwani. Ndugu wakaandika yote Mt. Pafnusi aliwaeleza na kuyaweka kanisani, mahali ambapo kila mmoja aliweza kuyasoma akitaka. Pafnusi akamshukuru Mungu aliyemjalia kujifunza hayo na akarudi katika monasteri yake.

Mt. Heraklemoni na wenzako, mtuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

## Mt. Abraham, Pastriarka wa 62 wa Aleksandria




Mwaka 970 B.K. Anba Abrahamu, alikyekuwa Patriarka wa 62 wa Aleksandria, alifariki. Aliitwa Ebn-Zaraa, Msiria, kwa sababu baba yake kutoka Mashariki, mwanabiashara tajiri, alikuwa anatembelea Misri, na mwishoni akakaa huko.

Abrahamu alikuwa Mkristo mwenye fadhila nyingi, hasa kuwa mkarimu kwa maskini. Sifa zake za haki na elimu vilijulikana sana. Kiti cha Mt. Marko kilipokuwa bila mtu, maaskofu wote walimchagua kuwa Patriarka. Alipokaa juu ya kiti cha Mt. Marko kwanza aliwagawia mali yake maskini na wahitaji.

Kazi yake ya kwanza ilikuwa kuondoa mila mbaya zilizopinga Injili ya Yesu Kristo. Akaonya kumtenga na Kanisa, kila mmoja aliyechukua rushwa ili kupata cheo katika Kanisa. Pia alipinga vibaya desturi ya kubaki na masuria. Wote waliosikia na kutambua msimamno wake walirekebisha, kwa hofu ya Mungu, wasitengwe naye kwa Kanisa.

Mungu alikuwa pamoja naye kuimarisha imani ya waamini wa Kanisa lake. Katika mwujiza mmoja Mungu alionyesha utakatifu wake mbele ya watu wote. Wakati wa utawala wa Sultani El-Mu'izz, Myahudi mmoja Yakobo Ebn-Yousef, Waziri mkuu, aliyeacha imani yake na kusimilishwa, alikuwa na rafiki yake Myahudi, Ebn-Killis, akizoea kwenda pamoja naye kwa Sultani na kuongeana naye. Siku moja Myahudi huyu alimwomba Sultani kujadiliana na Patriarka mbele yake. Patriarka alikuja pamoja na Abba Severus Ebn-el-Mukafaa, askofu wa Ashumunein. El-Mu'izz akawaamua kukaa, kwa hiyo wakakaa kimya. Akauliza: "Kwa nini hajadiliani?" Askofu Severus akamjibu, "Namna gani tuweze kujadiliana mbele na Sultani, na mtu ambaye akili yake ni ndogo kuliko ng'ombe." Sultani akaomba maelezo. Askofu Severus akasema: "Mungu alinena kwa kinywa cha nabii, '*Ng'ombe amjua bwana wake, na punda ajua kibanda cha bwana wake, bali Israeli*

*hajui*.‘ Isa 1:3. Wakajadiliana na Myahudi huyu na kumwaibisha kwa hoja zinazohakikisha ukweli wa Imani ya Kikristo. Patriarka na Aksofu Severus wakaondoka mbele ya Sultani kwa heshima kubwa.
Waziri na rafiki wake hawakuweza kuvumilia matusi hayo. Kwa hiyo wakatafuta kuwalipia kisasi. Siku chache baadaye, Myahudi Yakobo Ebn-Yousef alimwendea Sultani na kwa ujanja akamwambia: “Mheshimiwa unajua kwamba imani ya kikirsto haina msingi imara. Biblia yao inasema: ‘*Mkiwa na imani kiasi cha punje cha haradali mtauambia mlima huu, ‘Ondoka hapa uende kule‘ nao utaondoka*‘ Mt 17:20. Mfalme wa waumini, utambue upuuzi wa usemi huu. Na kwa kuhakikisha jambo hilo tumwite Patriarka kuonyesha uthibitisho kwamba usemi huo wa Kristo ni kweli.“
Sultani akafikiria, “Ikiwa usemi wa Kristo ni kweli, jambo hilo litakuwa na faida kubwa kwa ajili yetu, kwa sababu Mlima Mukatam ni karibu mno kwetu. Ikiwa mlima unaweza kuhamishwa, usalama wa mji Kairo utakuwa kubwa kuliko kwa sasa hivi. Ikiwa usemi si kweli, jambo hilo litanipatia sababu ya kudhulumu Wakristo.“
Sultani akamwita Patriarka na kumweka mbele yake usemi huu. Akamwomba amwonyesha ukweli wa usemi huu. Patriarka akaomba muda wa siku tatu. Akakubaliwa. Patriarka alipomwacha Sultani, akawakusanya wamonaki na maaskofu wote. Wakakaa katika kanisa la El-Mualaqua, mji mkongwe Kairo, siku tatu fululizo wakifunga na kumwomba Mungu.
Siku ya tatu kulikopambazuka, Bikira Maria, Mama wa Mungu, akamtokea na kumwambia kuinuka na kwenda mtaa uendao sokoni. Huko atamwona mwanamume, chongo, akibeba chungu cha maji mabegani mwake. Akamwagiza Abba Abrahamu kumwambia kwamba ndiye yeye atakayetenda mwujiza huu. Mtakatifu huyu aliitwa Simoni mtengeneza ngozi. Patriarka akamchukua naye, pamoja na mapadri, wamonaki na wakristo kumwona Sultani El-Mu’izz, ambaye alitoka pamoja na viongozi wa serikali yake na watu wakubwa na mji, na kufika karibu na mlima Mukatam. Patriarka na



**Simoni Mtengeneza ngozi**

watu wake wakakaa upande mmoja wa mlima na Sultani na watu wake upande mwingine wa mlima.

Patriarka na waamini wakasali, kuinama vichwa vyao na kupiga magoti mara tatu. Kila mara wakipiga magoti walisema: "*Kyrie eleison, Bwana utuhurumie*." Wakati wowote Patriarka na waamini waliinua vichwa vyao baada ya kuinama, mlima uliinuka na wakati walipoinamisha kichwa chao chini mlima ulishuka chini. Na wakati wowote walitembea, mlima ulihama mbele yao. Katikati miali ya jua ilipita na kuwezesha wote kuona ajabu hilo. Wakati huo Simoni alitoweka, na Al Muizz alisema kwa nguvu "*Allahu Akbar*".

Hofu kubwa ulimvamia Sultani na wenzake na wengi walianguka chini. Sultani, juu ya farasi yake, akamwendea Patriarka na kumwambia: "Mwalimu mkubwa, sasa najua kwamba wewe ni mtakatifu, omba yoyote utakayo nitakupatia." Patriarka alikataa kuomba kitu chochote, lakini Sultani alipomsihi, akamwomba Liwali amruhusu kujenga makanisa, hasa kanisa la Mt. Merkurio, huko mji mkongwe Kairo. Akaandika amri kumruhusu kujenga na kuyakarabati makanisa na akampatia fedha nyingi kutoka hazina ya nchi. Patriarka akamshukuru na kumwombea, lakini alikataa kupokea fedha. Kwa hiyo Sultani akamheshimu sana kwa sababu ya imani na haki yake. Patriarka akayakarabati makanisa mengi.

Alipomaliza maisha yake, akafariki katika amani. Alikaa juu ya kiti cha Mt. Marko, miaka mitatu na siku sita tu.

Mt. Abraham utuombee na Mungu asifiwe milele na milele. Amina.

## Mwenyeheri Liduina, Sista, 1941.



Elisa Angela Meneguzzi (Sista Liduina) alizaliwa tarehe 12 Septemba 1901 huko Italia. Wazazi wake walikuwa wakulima lakini matajiri kwa fadhila za uaminifu na imani. Huyu mtoto akaonyesha mapema roho ya sala akihudhuria misa kila siku, hata ikiwa ilimbidi kutembea kwa kilomita 2. Akajifunza katekisimu na baadaye akawa mwenyewe Katekista. Alifurahi

kuzungumza kuhusu Mungu kwa ndugu zake. Kila jioni alisali pamoja na familia yake.
Alipokuwa na miaka 14 akaenda kufanya kazi katika hoteli, ili aweze kusaidia familia yake. Watu wote walimpenda na kufurahia tabasamu yake. Alikuwa na hamu kuishi kwa ajili ya Bwana, kwa hiyo tarehe 5 Machi 1926 alijiunga na Shirika la Mt. Fransisko wa Sales, ambalo makao yake yalikuwa Padova, Italia.
Huko aliweza kujitoa kabisa kwa Mungu na kuendelea kueneza hazina ya moyo wake. Katika shule ya bweni huko Santa Croce, alifanya kazi kama msimamizi wa vitambaa, muuguzi na mtunzaji wa vifaa vya kanisa. Wasichana wote walimpenda, wakimwangalia kama rafiki yao kwa sababu alikuwa anawasikiliza, kuwasaidia kutatua shida zao kwa kuwapa shauri nzuri.
Mwaka 1937 aliweza kutimiza ndoto yake kuenda katika nchi ya misioni kuwaletea watu wasiomjua bado Kristo upendo na imani yake. Wakubwa wake walimtuma huko Dire-Dawa, nchi ya Ethiopia. Huko Dire-Dawa kulikuwa watu wa dini na tamaduni mbalimbali. Akafanya kazi ya uuguzi katika hospitali ya serikali ya Parini. Wakati wa Vita vya Pili vya Dunia vikaanza, hospitali ikawa hospitali ya kijeshi. Liduina akawa kama malaika wa upendo kwa askari waliojeruhiwa. Akawahudumia kwa upole na bila kujibakiza. Alimwona Kristo ndani ya kila mmoja aliyeteswa. Muda si muda jina lake likajulikana mahali pengi na kila mtu alimtafuta ili awaombee. Wenyeji wakamwita ‘Sista Gudda‘, maana yake ‘Sista Mkuu‘. Mji uliposhambuliwa na makombora, wote walilia: “Sista Liduina, utusaidie!“ Na yeye, bila kujali hatari aliwabeba waliojeruhiwa mahali pa usalama. Kwa walio karibu kufariki, aliwasihi kwa upole kusema sala ya kutubu. Kwa watoto, daima alichukua naye chupa ya maji, na kuwabatiza katika hatari.
Aliwahudumia watu wote, wazungu kwa waafrika, wakristo kwa waislamu na wapagani. Alipenda sana kuzungumza kuhusu upendo wa Mungu Baba na mahali pa ajabu Mungu alitengeneza kwa sisi sote, waana wake. Wenyeji, ambao karibu wote walikuwa Waislamu, walijisikia kuvutwa naye, na kwa njia yake, kwa dini ya Katoliki. Akaitwa ‘Mwale wa ki-ekumene‘.

Ugonjwa sugu ukamwingia. Akaukubali kwa amani. Pole pole nguvu zake za mwili zikapunguka, lakini yeye aliendelea kuwahudumia waliojeruhiwa hadi kifo chake. Mwishowe alipasuliwa kwa mafanikio, lakini matatizo yakaonekana baadaye. Uganzi ukamshika tumbo lake na akafariki tarehe 2 Desemba 1941. Alikuwa na umri wa miaka 40. Daktari mmoja aliyemhudumia katika siku zake za mwisho alisema: “Sijaona mtu aliyefariki kwa furaha, na furaha tele kama yeye“. Askari walidai kwamba alikuwa mmojawapo, ndiyo maana akazikwa katika shamba lao la wafu huko Dire-Dawa. Miaka 20 baadaye, mwezi wa Julai 1961, mwili wake ulihamishwa katika kanisa la makao makuu ya shirika lake huko Padova. Akatangazwa kuwa Mwenyeheri tarehe 20 Oktoba 2002.

Sista Luduina anatuachia ujumbe wa tumanini na upendo. Aina ya tumaini inayowaokoa watu kutoka ubinafsi wao na kuwaweka huru na ukatili wao. Aina ya upendo inayowasukuma watu kushirikiana, kuhudumiana, kufuata mfano wa Yesu Kristo aliyekuja kutumikia na siyo kutumikiwa.

Mwenyeheri Luduina, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

**Desemba 3**

Sisi Wakatoliki tunawakumbuka Mt. **Kasiani**, mfiadini, Tangiers Moroko, 298; Mt. **Fransisko Ksaveri**, 1552, somo wa Idara ya kueneza Injili na mlinzi wa wamisionari popote duniani.[449]
Huko Afrika ya Kaskazini, Wakatoliki wanawakumbuka Wat. **Klaudio**, **Krispini**, **Magina**, **Yohane**, **Stefano**, wafiadini.[450]

Huko Misri, Wakoptiki wanamkumbuka Mt. **Mathayo**, maskini.[451]
Huko Ethiopia, Wakristo wanamkumbuka Mt. Abba **Yosefu** wa mji wa Heliopolis.[452] Pia kumbukumbu ya Abba **Banina** na Abba **Naou**.[453]
Waorthodoksi wanamkumbuka Mt. **Theodori**, Askofu wa Aleksandria.

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake! Amina.


## Mt. Kasiani, mfiadini, 298

Kasiani alikuwa katibu wa Hakimu Aurelio Agricola. Alikuwa anaandika maneno yote wakati Mt. Marseli alihukumiwa na Hakimu huyu. Tarehe 30 Oktoba Marseli, askari, akaletwa mbele ya Aurelio, ambaye kwa nguvu zake zote alijaribu kumshauri kukana dini yake. Lakini Marseli, akamjibu kwamba yeye ni askari wa Yesu na haiwezekani kwake kurudi kuhudumia kama askari katika ulimwengu. Kwa majibu yake na msimamo wake Marseli alionekana kama mtawala aliyehukumu Hakimu wake. Aurelio alikasirikakasirika bila kujua la kumjibu.
Kasiani, aliyeandika maneno yote, akashtuka kuona kwamba Aurelio alishindwa na ujasiri wa shahidi huyu. Aliposikia kwamba Hakimu akamhukumu Marseli afe, akaudhika sana kiasi kwamba akatupa mbali

449 *Martyrologium Romanum,* ed. 2005.
450 *Les petits Bollandistes*
451 *Coptic Synaxarium: 7 Kiahk.*
452 *The Ethiopian Rite Missal, Abba Emmanuel & Abba Brendan Cogavin, 2002, uk 204. Ethiopian Synaxarium: Hedar 24.*
453 *Arabic-jacobite synaxarium*

kalamu yake na mbao yake. Kufuatana na mawazo kutoka mbinguni alitambua kwamba kuwaua Wakristo ni jambo la kuchukiza, basi akastaafu na kujitangaza kuwa Mkristo. Watumishi wa Hakimu walishangaa na Marseli yeye alitabasamu. Aurelio akaruka kutoka kiti chake, akitetemeka kwa hasira na kumwuliza katibu wake maana yake tendo lake. Kasiani akamwambia: "Hukumhukumu mtu huyu kwa haki". Hakimu akaamua mara moja Kasiani atupwe gerezani.
Marseli alifurahi, kwa sababu Roho Mtakatifu alikuwa amemjulisha kwamba Kasiani atakuwa shahidi mwenzake. Siku ile Marseli akauawa kwa ajili ya dini yake. Tarehe 3 Desemba, Kasiani kwa zamu yake, mahali pale pale, akahukumiwa afe. Kwa neema ya Mungu alihesabiwa kuwa shahidi mwaminifu wa Yesu Kristo.
Mt. Kasiani, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

## Mt. Theodori, askofu na shahidi



Theodori alizaliwa Misri katika mji wa Aleksandria. Akachaguliwa kuwa askofu wa Aleksandria. Inasikitisha kwamba hatuna habari za tarehe na matendo makuu ya maisha yake. Lakini Kanisa la Waorthodoksi limehifadhi daima jina lake katika liturjia yake.
Inasemekana kwamba alikuwa mhubiri mkuu, mwenye maneno ya nguvu yanayochoma mioyo ya watu. Wakazi wa Aleksandria hawakupenda mahubiri yake. Siku moja alipohubiri wakamzunguka na kumshika Mtakatifu huyu. Wakampiga vibaya, wakamzomea, lakini yeye hakuwapinga. Akavikwa kichwani mwake taji la miiba na kutembezwa katika mitaa ya mji Aleksandria. Baadaye wakamleta pwani na kutoka jabali wakamtupa chini baharini. Lakini mawimbi yakamrudisha katika nchi kavu. Wapagani walishangaa, basi wakampeleka kwa Gavana wa mji. Akaamuru ateswe vikali. Hata neno moja halikusikika kutoka kinywani mwake, isipokuwa sala zake kwa

Bwana. Baadaye akapelekwa kwa askari na kufariki kwa kukatwa kichwa kwa upanga.[454]
Mt. Theodori, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

## Mt. Fransisko Ksaveri, 1552

Mt. Fransisko hakuzaliwa Afrika na hakuishi Afrika, lakini alikanyaga mahali pawili; Msumbiji na Malindi. Nakuru baadhi ya maneno ya barua zake. Fransisko aliondoka Lisboa, tarehe 13 Mei 1541, kwenda kutangaza Injili India na Uchina. Mwisho wa mwezi Agosti, meli tano na watu wote walisimama katika bandari moja ya kisiwa cha Msumbiji, majira wa baridi, kwa muda wa miezi sita. Katika kisiwa hicho kulikuwa miji miwili, moja ambao askari wa Wareno walipokaa, na wa pili uliojaa na Waislamu wenye ukarimu. Tulipokuwa tunakaa, wengi kati yetu waliugua, hata watu themanimi walifariki. Tulihama hospitalini ili tupate nafasi kuwatunza wagonjwa. Padri Paulo na Padri Mancias waliwahudumia ki-mwili wakati niliwahudumia ki-roho. Hata hivyo sikuweza kutenda kila kitu kilichohitajika. Siku ya Jumapili niliwahubiria umati wa watu. Gavana mwenyewe alikuwa anahudhuria. Na mara nyingi niliitwa kusikia maungamo mahali pengine. Kwa kweli, muda wote tulipokuwa Msumbiji tulikuwa na kazi nyingi. Govana na watu wake, na askari wote walituonyesha heshima kubwa, na kwa neema ya Mungu tulitumia muda wa miezi sita kwa faida ya wote ki-mwili na ki-roho.
Gavana alitaka kuendelea safari mara ikiwezekanapo. Lakini kulikuwa bado watu wengi wagonjwa kwa sababu ya hali ya hewa. Kwa hiyo aliomba kwamba, kati yetu, wengine wabaki kuwatunza wale ambao hawakuweza kuendelea safari zao. Alifikiri vema kwamba Padri Paulo na Padri Mancias wabaki, wakati mimi niliendele safari pamoja naye. Nilisindikiza Gavana, ambaye hakuwa na afya nzuri, ili ikiwa ugonjwa wake unazidi, niweze kumwungamisha.
Safari yetu kutoka Msumbiji hadi Goa ilidumu miezi miwili. Tarehe 13 Machi 1452 tulifika Malindi, Kenya. Tulikaa siku chache huko Malindi, bandari inayotawaliwa na Waislamu, ambao ni rafiki wa Wareno wafanya biashara, wanaoishi hapa. Ikiwa mmojawapo anafariki,

[454] OCA *Lives of the Saints of Africa*

anazikwa na juu ya kaburi lake udongo mwingi unalundika na msalaba unachomeka. Wareno waliinua, karibu ya mji, msalaba mzuri kwa mawe ambao unang'aa kama ungefunikwa na dhahabu.[455] Sijui namna ya kueleza furaha yangu nikiutazama. Inaonekana kwamba uwezo wa msalaba unaenea juu ya wenyeji wasioamini. Mtawala wa Malindi alipanda katika meli ili kumpongeza Gavana na kumkaribisha kwa ukarimu na urafiki. Nilipokuwa Malindi tulimzika mtu aliyefariki merikebuni. Tulifanya ibada kubwa, kwa ushangao wa Waislamu, waliopenda sana ibada yetu.

Mmoja wa Waislamu, mwenyeji wa Malindi, aliniuliza ikiwa makanisa yetu tunapoenda kusali, yalijaa watu wakimwabudu Kristo. Kwa sababu, uchaji wa Mungu, ulianza kuwa baridi miongoni wa watu wake. Alitaka kujua kama ilikuwa hivyo kati ya Wakristo. Kulikuwa misikiti kumi na saba lakini tatu tu iliudhuriwa na Waislamu wachache. Mtu huyu mwema alihangaika na hakujua la kufanya, asijue kwa nini watu wake walipoteza uchaji wa Mungu. Aliwaza bila shaka ni kwa sababu ya dhambi kubwa ya watu wake. Tulikuwa na mazungumzo marefu kuhusu jambo hilo. Nilimwambia kwamba Mungu, aliye Mwaminifu na Mkweli, anawaangalia wasioamini na sala zao kuwa machukizo na anataka kwamba ibada yao, anayochukia, iishiwe. Rafiki yangu, aliyekuwa na mawazo tofauti nami, hakufurahi. Kadhi akafika, mtu mwenye ujuzi mwingi, msomi, akasema kwamba, kama Muhammadi hataonekana tena duniani kuwatembelea chini ya miaka miwili, yeye mwenye ataasi dini hiyo. Tunaweza kuona jinsi wasioamini wanavyohangaika na kupotea tumaini. Kweli, hii ndiyo baraka iliyotumwa na Mungu, ili watambue hali yao na kuongoka.

Mt. Fransisko Ksaveri utuombee na Mungu atukuzwe mahali popote, daima na milele. Amina.

---

[455] Inaonakana kwamba Vasco de Gama, katika safari yake, mwaka 1497 hadi 1499, alipopita Rasi ya Tumaini Jema (*Cape of Good Hope*), na kufika India, aliiinua misalaba sita mahali tofauti. Mojayapo, ulikuwa huko Malindi, Kenya.

**Desemba 4**

Sisi Wakatoliki tunamkumbuka Mt. **Heraklas**, Patriarka, askofu wa Aleksandria, Misri,[456] ambaye sifa yake ilikuwa kubwa hata mwanahistoria Julio Afrikano alikiri kwamba alienda mpaka Aleksandria kumwona. Pia kumbukumbu ya Mt. **Klementi**, Padri, Alesandria, 215.[457]

Huko Heliopolis, Misri, au Nikodemia, kumbukumbu ya Mt. **Barbara**, bikira, shahidi, mwaka 306, chini ya utawala wa Kaizari Galerus. Kadiri ya pokeo moja, akateswa kwa kuunguzwa mwili wake kwa mienge, kukatwa matiti na mwisho kukatwa kichwa.

Huko Wau, Sudan ya Kusini, Wakatoliki wanamkumbuka Mtumishi wa Mungu **Yosefu dei Cas,** mtawa wa Shirika la Wamisionari wa Comboni.

Huko Misri, Wakoptiki wanawakumbuka Mt. **Heraklas**, Patriarka, askofu wa 13 wa Aleksandria, Misri; Wat. **Esi** na dada yake **Thekla**, wafiadini; Mt. **Samueli**, abate wa monasteri ya Kwalamon, Misri; Salaamu kwa **Yusto**, mtawa wa monasteri ya Mt. Antoni.[458] 1976.

Huko Ethiopia, Wakristo wanawakumbuka Mt. **Filopator** "*Mercurius*" na mwongofu wake **Yohane** kutoka dini ya ki-islamu; **Sabla Wangel**, Malkia wa Ethiopia.[459]

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake. Amina.

## Mt. Klementi, Padri, mnamo mwaka 216

Ingawa jina la Klementi halipo katika martirolojia ya Kanisa la Roma, tunalikuta katika orodha ya watakatifu mahali pengi. Anaheshimiwa

---

[456] *Martyrologium Romanum,* ed. 2001.

[457] *Les petits Bollandistes*

[458] *Coptic Synaxarium: 8 Khiahk..* Pamoja na Tekla,  Abba Isa, Appolonius, Paisi, dada ya Tekla. Katika Kanisa la Othodoksi la Tehawedo Mt. Samueli anaadhimisha tarehe 21 mwezi wa 12.

[459] *The Ethiopian Rite Missal, Abba Emmanuel & Abba Brendan Cogavin, 2002, uk 204. Ethiopian Synaxarium: Hedar 25.*

kuwa Mtakatifu katika makanisa ya Katoliki, Orthodoksi na Anglikana. Hadi mwaka 1568 jina lake lilikuwa katika martyrolojia ya ki-roma, lakini limefutwa kwa shauri ya Baronius.
Flavio Clemens alizaliwa Athene, Ugiriki. Alianza kujifunza Ugiriki, akaendelea kujifunza huko Italia, Asia, Assyria na Palestina na akamaliza Aleksandria, Misri. Alikuwa msomi kweli katika falsafa, akiwa na walimu watano maarufu. Mwalimu wake wa mwisho, aliyempenda zaidi ya wote, alikuwa Pantaeno wa Shule ya katekesi ya Aleksandria. Huko akatambua ukweli wa Yesu Kristo, akabatizwa. Tangu siku ile alilenga kuishi maisha matakatifu yaliyopambwa na fadhila zote. Pantaeno alipotumwa na askofu wake Demetrio kwenda India, mwaka 189, Klementi akachukua nafasi yake kama mwalimu, akifundisha pamoja na Origene na Aleksanda.
Klementi akapadirishwa wakati Kaizari Septimo Severo alipoanza kutawala, labda mnamo 195. Wakati wa dhiki ilimbidii akimbie mpaka Kapadokia. Baadaye akaenda Yerusalemu, akihubiri kwa mafanikio makubwa. Akapita Antiokia kabla ya kurudi Aleksandria.
Klementi alikuwa mwandishi maarufu. Akaandika vitabu vingi kuonyesha upuuzi wa kuabudu miungu ya uongo, udanganyifu wa uzushi wa ujuzi, ubora wa ukristo, upendo wa Mungu Baba na upendo kwa ndugu zetu, na maisha ya kikristo pamoja na fadhila zote, n.k. Ni mwalimu bora wa maisha ya ki-roho. Theodoret alisema: “Mtu huyu mtakatifu amewapita wote kwa ujuzi wake.“ Amefariki mwisho wa utawala wa Kaizari Karakalla kwa kuchinjwa mwaka 216.
Mt. Klementi, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

## Mt. Heraklas, Patriarka, 247

Heraklas alikuwa askofu wa Aleksandria, kuanzia mwaka 231 hadi 247. Alizaliwa mwaka 185. Origene alipoanza kufundisha falsafa, akiwa na umri wa miaka 18, baada ya kifodini cha baba yake Leonidas, Heraklas na ndugu yake Plutarko, walikuwa miongoni mwa wanafunzi wake. Origene akawaongoa wote wawili kwa imani ya Kristo. Na baada ya muda mfupi Plutarko akafa shahidi, akawa mwanafunzi wa kwanza wa Origene kuwa shahidi.

Heraklas alijua falsafa na lugha ya Kigiriki kwa ufarisi, ndiyo maana alitembelewa na Julio Afrikani alipofika Aleksandria. Origene alipochukua nafasi ya Klementi kama mkuu wa shule ya Katekesi, akamchagua Heraklas awe msaidizi wake. Heraklas akapadirishwa na Patriarka Demetrio. Na mwaka 231, wakati Origene alipokaa Kaizaria, Demetrio alipomtenga na Kanisa, Heraklas akashika nafasi yake kuwa mkuu wa shule ya Katekesi. Muda si muda akachaguliwa kuwa mwandamizi wa Demetrio. Kama Askofu wa Aleksandria akawa wa kwanza kujipatia cheo cha *Pope* wa Aleksandria.

Kadiri ya Theofilo wa Aleksandria, wakati Origene aliporudi Aleksandria, Heraklas akamvua upadri wake na kumfukuza atoke Aleksandria. Tunasoma katika maandiko ya Phosio yafuatayo: "Wakati wa Heraklas, Origene, kwa jina lingine Adamansio, alikuwa anaeleza wazi uzushi wake, siku za Jumatano na Ijumaa. Basi Heraklas, mtakatifu, akamtenga na Kanisa na kumfukuza nje ya Aleksandria, kama mtu ambaye anavuruga mafundisho ya Kanisa na kuharibu imani ya ki-orthodoksi. Origene njiani kwenda Siria, akasimama Thmuis. Askofu Ammonio, akamwalika kufundisha kanisani. Heraklas aliposikia, akaenda Thmuis, akamwondoa Ammonio kama askofu na kumuweka kwenye nafasi yake Filipo. Lakini, kwa maombi ya wakristo wa Thmuis, Heraklas akamrudisha Ammonio kuwa askofu na kuwapa Ammonio na Filipo kiti cha uaskofu. Lakini Heraklas aliporudi Aleksandria, Filipo hakukaa katika kiti cha uaskofu kwa unyenyekevu wakati wa ibada. Ammonio alipofariki, ndipo akakaa katika kiti cha uaskofu wa Thmuis na akawa askofu mwenye fadhila nyingi."

Heraklas akafariki mwaka 247 na Dionisi akawa Askofu wa Aleksandria. Akamsifu Heraklas kwa desturi ya kuwapokea wazushi katika Kanisa bila kuwabatiza tena, lakini baada ya kuwachunguza hadharani.

Mt. Heraklas, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

## Mtumishi wa Mungu Yosefu de Cas, mwenye ukoma, 1932

Yosefu De Cas alizaliwa Italia, tarehe 27 Septemba, 1880. Alipokuwa na umri wa miaka 25 alisikia wito wa kuwa Misionari kama Bruda.

Mwaka uliofuata alienda Verona kwa ajili ya Novisiati. Wakubwa wake walisitasita kumpokea. Ingawa alikuwa na akili na fadhila, alikuwa mlemavu mgongoni mwake. Hakuweza kuvaa vizuri nguo ya ki-tawa. Walitaka kumrudisha nyumbani, lakini mwishoni walikubali kumpokea kama msaidizi, akiahidi kuitumikia misioni na kuwatii wakuu wake. Yeye mwenyewe alifikiri: “Haidhuru, umuhimu ni kuweza kwenda Afrika kama mmisionari”. Akaenda Sudan ya Kusini, tarehe 15 Agosti, 1907, hata bila kuaga familia yake.

Akakaa kwanza Tonga, kati ya Washilluki, mkoa wa Nile Kusini. Aliwaandikia wa ndugu zake: “Ni mahali pazuri sana. Hakuna mahali pazuri zaidi”. Lakini hakutaja mbuga, mbu na ugonjwa wa malaria! Alifanya kazi kubwa kujenga nyumba, kanisa na shule. Kwa kufanya kazi pamoja na Washilluki aliweza kujifunza lugha yao. Washilluki hawakujibu Injili kama Wamisionari walivyotegemea. Wakahama.

Baada ya kukaa Tonga miaka minane ilibidi Yosefu ahame huko Lulu katika Sudan ya Kusini. Huko nyumbani kwa mapadri na masista, kanisa, shule zilikwisha jengwa, kwa hiyo Bruda Yosefu akajitoa kuwatunza wagonjwa. Huko Tonga alijifunza kidogo mambo ya utabibu. Wagonjwa wakaja kwa uwingi. Bruda akawakaribisha na kuwahudumia kwa dawa, lakini zaidi kwa tabasamu na upole wake. Aliwatembelea nyumbani hata watu walianza kushangaa kwamba wanatembelewa na kuponywa bila malipo.

Bruda Yosefu alikuwa msaidizi tu wa Wamisionari. Ndugu wengine wa Shirika wakawaomba Wakuu wa Shirika ili Yosefu apokelewe katika Shirika. Wakakubali. Ndipo akarudi Italia na kuanza novisiati. Siku ya Krismasi 1921 aliweka nadhiri yake. Mwaka uliofuata akarudi Lul na kuendelea na kazi yake.

Pamoja na Padri Beduschi alitumwa kufungua misioni huko Detwok. Wakaanza kujenga vibanda na wakati ule kuhusiana na watu. Matumaini yalikuwa makubwa. Lakini mwaka 1925 madoa yakaonekana mikononi mwa Bruda Yosefu. Wenzao walikisia ni ukoma na wakamtuma Kairo ili apimwe. Kweli akadhibitiwa kwamba ilikuwa ugonjwa wa ukoma. Akatumwa huko Gesira pembezoni mwa mji Kairo. Akakaa upweke huko miaka mitatu kama kutengwa. Akafanya kazi bustanini na kusali. Mwaka 1928 alipelekwa Wau katika kambi ya wenye ukoma. Huko alibaki mpaka alipofariki mwaka 1932.

Siku moja Bruda Gatti alimpasha habari kwamba Bruda Corneo alikuwa mgonjwa sana kwa malaria na homa nyeusi. “Madaktari wanasema kwamba mwujiza tu unaweza kumwokoa”. Bruda Yosefu akakaa kimya kwa muda, baadaye alimwambia Bruda Gatti: “Kesho asubuhi Bruda Corneo atakuwa mzima”. Bruda Gatti akaondoka na Bruda Yosefu akaenda kusali kanisani. Akamwambia Mungu: “Bwana, mimi ni mwenye ukoma. Sifai kitu, siwezi kutenda kitu. Ni mzigo kwa jumuiya. Bruda Corneo yeye ni kijana, ana nguvu sana. Aishi!” Jioni ya siku ile Bruda Yosefu akajisikia vibaya. Mapadri walipashwa habari na kumpeleka misioni. Kesho yake asubuhi, kama saa 2.00 alipokea mpako wa wagonjwa. Akawaambia ndugu zake: “Msiniombee ili niwe mzima. Nilimtolea Mungu maisha yangu kwa ajili ya Bruda Corneo.” Akafariki siku ile, tarehe 4 Desemba 1932. Akiwa na umri wa miaka hamsini na miwili.

Mchakato wa kumtangaza kuwa Mtakatifu ulifungua Jimbo la Wau, tareha 25 Machi 2015.

Bruda Yosefu, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

**Desemba 5**

Sisi Wakatoliki tunamkumbuka Mt. **Krispina** wa Thagare, mfiadini, huko Thebaste Aljeria.[460] Alikuwa mwanamke mwema sana. Akakataa kuitolea sadaka miungu wa uongo, kwa hiyo, alihukumiwa kukatwa kichwa, Makaizari Dioklesiani na Maksimiani walipotawala, wakati wa Gavana Anolino. Sifa zake zilitangazwa na Mt. Augustino. Pia huko Thagare, Aljeria, Wanakumbuka Wat. **Julio**, **Potamia**, **Krispini**, **Feliksi**, **Grato** na **wengine saba**, wote wafiadini.[461] Pia kumbukumbu ya Mt. **Grato**, Askofu wa Kartago, tofauti ya Shahidi Grato, 350.[462]

Huko Misri, kumbukumbu ya **Mt. Sabas**, abate katika Palestina, aliyeenda Aleksandria pamoja na mtawa mwengine.

Huko Aljeria na shirika la OdM kumbukumbu ya Mtakatifu **Williamu Saggiano**, Mtawa, aliyeenda Aljeria kuwakomboa watumwa na hatimaye akachomwa mtoto na waislamu kwa ajili ya imani yake.

Huko Bulawayo, Zimbabwe, Wakatoliki wanawakumbuka **Adolfo Schmitt**, Askofu wa Bulawayo, **Possenti Weggarten**, Padri na **Maria Francis van den Berg**, Sista, waliouawa na askari mmoja wa ZANU (*Zimbabwe African National Union*), mwaka 1976.

Huko Gulu, Uganda, Wakatoliki wanawakumbuka Mashahidi wa upendo, **Dk. Mathayo Lukwiya na wenzake**, walifariki kwa ugonjwa wa ebola, mwaka 2000.[463]

Huko Kinshasa, Jamhuri ya ki-demokrasia ya Kongo, Wakatoliki wanamkumbuka **Nikola Eklou Komla,** Mseminari wa Shirika la Majesuiti, kutoka nchi ya Togo, aliyeuawa mwaka 2010.

Huko Misri, Wakoptiki wanawakumbuka Mt. **Poemen**, mtawa;[464] Wat. **Marko**, **Sankta**, **Primasio**, **Sabas**, **Muko** na **Paulo**, wafiadini. Wat.

---

[460] *Martyrologium Romanum,* ed. 2005.
[461] *Roman Martyrology,* ed. 1956. Pamoja nao: Gregori
[462] Dictionary of Saints
[463] Rejea Fr. Neno Contra,, Louis Kalonji, *African Lay Martyrs*, New People Media Centre, 2009, uk 113-115.
[464] *Coptic Synaxarium: 9 Kiahk*. Tazama tarehe 27 Agosti Wakatoliki wanaoadhimisha sikukuu yake.

**Karioni** (Cyrion) na mwana wake **Zakaria**, wakaa pweke huko Shete, Misri.
Huko Ethiopia, Wakristo wanamkumbuka Mt. **Iyasus Mo'a**.[465]
Huko Afrika ya Kusini, Waanglikana (*Church of South Africa*) wanamkumbuka **Petro Masiza**, Padri Mwanglikana Mwafrika wa kwanza, 1907.

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake. Amina.

## Mt. Krispina, mfiadini, 304

Mt Augustino anatuambia kwamba shahidi huyu alikuwa mwanamke wa ukoo bora, tena tajiri, mwenye ndoa na watoto wengi. Ingawa alikuwa na mwili mororo alivikwa na ushupavu wa kiume. Akitamani mbingu kuliko dunia, Mungu kuliko malimwengu, na kuyadharau majonzi ya watoto wake, alifurahi kuitwa kumkiri Yesu Kristo jukwani mbele ya watu wote. Hatuna habari nyingi kuhusu yeye, isipokuwa mashtaka ya mwisho ya hukumu yake. Alikuwa mwenyeji wa Thagare, katika Afrika ya Kaskazini. Akakamatwa kwa sababu ya imani yake na kupelekwa huko Thebesa, mbele ya Anulino, Liwali wa Afrika.
Hakimu huyu alimsihi kutoa sadaka kwa miungu wa uongo, kufuata amri ya Makaizari.
Krispina akamjibu: "Sijatoa sadaka na sitatoa sadaka kwa mungu yeyote isipokuwa kwa Mungu Baba, sadaka ya Bwana wetu Yesu Kristo, Mwanawe, aliyezaliwa na kuteswa kwa ajili yetu."
**Anulino**: "Acha ushirikina wako na inama mbele ya sanamu ya miungu ya Warumi".
**Krispina**: "Kila siku namwabudu Mungu mwenyezi. Nje ya Yeye sifahamu mungu mwingine".
**Anulino**: "Unakataa na kuonyesha madharau. Utajifunza kutambua nguvu za sheria".

---

[465] *The Ethiopian Rite Missal, Abba Emmanuel & Abba Brendan Cogavin, 2002, uk 205. Ethiopian Synaxarium: Hedar 26.*

**Krispina**: “Kwa vyovyote nitafurahi kuteswa kwa ajili ya imani yangu“.
**Anulino**: “Ni upuuzi gani kutoacha ushirikina na kutoiabudu miungu mitukufu!“
**Krispina**: “Kila siku namwabudu Mungu aliye hai na wa kweli. Yeye ndiye Bwana wangu, nje na Yeye simfahamu mungu mwingine.“
**Anulino**: “Ninakukumbusha amri kutoka kwa Kaizari lazima uitii“.
**Krispina**: “Nafuata sheria ya Bwana wangu Yesu Kristo“.
**Anulino**: “Nitatoa amri ya kukukata kichwa, ikiwa hutii amri ya Makaizari. Utazitii kwa nguvu. Afrika nzima imetoa sadaka. Unajua.“
**Krispina**: “Hawatabarikiwa wale wanaonilazimisha kuwatolea sadaka pepo. Nitamtolea sadaka tu kwa Mungu mmoja, Mwumba mbingu na nchi na yote yaliyopo.“
**Anulino**: “Kwa hiyo unaikataa miungu? Hata hivyo utalazimishwa kuitumikia ikiwa unataka kuishi na kuwa na dini.“
**Krispina**: “Hakuna dini inayoweza kuwalazimisha wanaoipinga.“
**Anulino**: “Dini inayokubaliwa ni kuinama kichwa katika hekalu tukufu na kuifukizia ubani miungu ya Warumi.“
**Krispina**: “Sijawahi kulifanya jambo hilo tangu nilipozaliwa. Sitaki kujifunza sasa wala kulitenda wakati ninapoishi.“
**Anulino**: “Fanya ikiwa unataka kuishi“.
**Krispina**: “Unachoniambia hakinitishi. Si kitu. Lakini Mungu aliye mbinguni, ikiwa nitakubali kumkufuru, atanipoteza na sitajitambua siku ya mwisho.“
**Anulino**: “Huwezi kukufuru ikiwa unatii amri tukufu“.
**Krispina**: “Miungu ipotelewe, ile ambayo haikuumba mbingu na dunia. Mimi ninamtolea sadaka Mungu wa milele, anayeishi milele milele, Yeye ambaye ni Mungu wa kweli, Mungu mwenye nguvu, aliyeumba bahari, majani mabichi, nchi. Wanadamu, aliyewaumba, wanaweza nini dhidi yangu?“
**Anulino**: “Heshimu dini ya Warumi, kama wanavyoiheshimu Makaizari wasioshindwa na sisi wenyewe“.
**Krispina**: “Nimekwisha kuambia, mateso yote unayonitayarishia, nitayavumilia, kuliko kupotea roho yangu kwa kuiabudu miungu ya mawe waliofanywa kwa mikono ya wanadamu.“

**Analino**: "Unakufuru, hufuati njia ya kweli kupata wokovu. Je, unaendelea kupotea?"
**Krispina**: "Mungu wangu anayeishi milele, ndiye yeye aliyenizaa, aliyeniokoa kwa njia ya maji ya ubatizo, ndiye yeye aliye pamoja nami kunisaidia. Atanifariji kwa namna yote, mimi mjakazi wake, ili nisimkufuru."
Basi Anulino akaamuru kwamba kichwa chake kinyolewe na aibishwe mbele ya watu wote katika hali hiyo ili watu wamdharau.
Krispina akasema: "Ikiwa miungu inachukizwa na maneno yangu, basi iseme yenyewe". Anulino, kwa hasira, akaamuru atendewe kama wenzake Maksima, Donatilla na Sekunda walivyotendewa kabla.
Akamjibu: "Mungu yu pamoja nami ili nisitende dhambi ya kumkufuru."
Liwali akaamuru kwamba maneno yote ya hukumu yasomwe na baadaye akatamka hukumu ya kifo. Krispina akaruka kwa furaha na kumshukuru Mungu. Akapelekwa mahali pa kifo chake na kukatwa kichwa, tarehe 5 Desemba 304.[466]
Mt. Krispina, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

## Mashahidi wa Upendo, Uganda, 2000

Mwanzoni mwa Oktoba 2000 katika hospitali ya Lacor, Gulu, Uganda Kaskazini, yowe kubwa ikisikika, Ajok Kristina, umri wa miaka 20, muuguzi mwanafunzi akafariki. Muda si muda nesi wa pili akafariki. Wote wawili walifariki kwa ugonjwa wa Ebola. Daktari Mathayo Lukwiya, mkurugenzi wa hospitali akawaeleza watumishi wote hali ilivyo. Akawaacha manesi na daktari kuondoka au kubaki. Kwa wale waliobaki akawauliza kama kwamba watawatunza wagonjwa walioambukizwa na Ebola. Akawaambia: "Sitaki kuhatarisha watu zaidi. Nitawaita kama ni lazima. Nitawashukuru kama mnaweza kunisaidia".
Grace Akullo akajitolea kuwatunza wagonjwa. Alikuwa na miaka 27, mama wa watoto wawili. Akahitimu kama nesi, mwaka 1999. Gresi akatumia muda mrefu kati ya wagonjwa. Siku moja akamwambia

[466] Butler's *lives of the Saints*, December, pp.85-86

kisirisiri Sista nesi: “Sijisikii vizuri“. Ilikuwa mwanzo wa kupigana na ugonjwa. Ingawa alipata dawa na matunzo yote, hali yake ikazidi kuwa mbaya sana baada ya saa. Akapata sakramenti ya mpako wa wagonjwa. Usiku wa tarehe 17 Oktoba, daktari Mathayo akamtembelea na kumwambia: “Gresi ulijitahidi kupigana na ugonjwa, kama sisi. Sasa weka maisha yako mikononi mwa Mungu na ukubali mapenzi yake, hata ikiwa hatuyaelewa. Tutawaangalia watoto wako“. Mgonjwa akamsikiliza macho yake yakifungwa. “Je, Gresi umenielewa?“ Kwa kichwa alimwonyesha kwamba alielewa. Grace akanong’oneza: “Aba, Baba“. Akafariki.

Daktari akaratibu kazi ya kuwasaidia wagonjwa kwa muda wa miezi miwili. Akawaambia manesi: “Nawaomba kuyafuata maagizo yote mliyopokea. Ni vita kubwa tunavyopiga. Hamjui jinsi mnavyokuwa wa maana kwangu. Nyuso zenu zimechapwa katika mawazo yangu na moyoni mwangu. Ninyi ni bora kwangu kuliko yote kwa wakati huu. Mimi, ikiwa ninaacha kazi hii sasa hivi, sitakuwa tena daktari.“

Vifo vikaendelea kuwepo: Adata Margaret, 42, mama wa watoto 10; Ajok Simon, nesi; Aol Monique, 22 nesi mwanafunzi; Ayello Daniel, 24 wauguzi mwanafunzi. Wakati wa mazishi ya Sista Pierina Asienzo, 45, Daktari alisema: “Wengine wanataka kuwa daktari ili kupata sifa binafsi, au kwa ajili ya kuyaokoa maisha ya watu. Mimi nimeamua. Nimechagua kuwa tayari kufariki kwa ajili ya wengine, kama ni lazima“.

Baada ya vifo vya Santina na Helema, watumishi walikataa kufanya kazi. Hali iliyo mbaya sana. Daktari Mathayo akamwambia nesi mzee: “Wewe na mimi tuna miaka mingi, na tunaweza kuelewa kwa nini tupo hapa, lakini hawa ni vijana. Huwezi kuelewa jinsi ninavyojisikia uzito wa wajibu wangu.“ Karibu mwisho wa mwezi wa Novemba akaanza kujisikia dhaifu. Jibu la maabara: Ebola! Sasa ilikuwa zamu yake kulazwa na kutunzwa. Alizungumza kwa shida, sauti yake ilikuwa dhaifu, uso wake ulionyesha maumivu makali. Akamwambia daktari Yotti: “Nipo tayari kwa yoyote, lakini Mungu akipenda, ningependa kuwa wa mwisho kufa kwa ugonjwa wa Ebola.“ Daktari Mathayo akafariki tarehe 5 Desemba 2000.

Watu wa Mungu mliofariki kwa kutoa maisha yenu kwa ajili ya wengine, mtuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

## Mt. Iyasus Mo’a, mtawa, 1294.

Iyasus Mo’a, maana yake ‘Yesu ameshinda‘, amezaliwa 1214, huko Dehana, Ethiopia. Alipokuwa na miaka 30, akasafiri na kufika monasteri ya Debre Damo, wakati Yohane (*Yohannis*) alipokuwa Abate. Akakubaliwa kuwa mtawa. Abate Yohane akampatia kazi ngumu za kutenda. Akakaa katika monasteri hiyo kwa miaka saba, baadaye alienda kuishi na Jumuiya ya wakaa pweke, huko Istqfanos, kisiwani mwa ziwa la Hayq la Amba Sel. Akawakusanya wakaa pweke wote ili kuishi pamoja na kwa kusudi hili alijenga monasteri moja yenye sheria na shule. Mmoja wa wanafunzi wake alikuwa Mt. Tekle Haymanot, aliyekaa katika monasteri hiyo miaka kumi.[467] Mmoja wa wafalme Zagwe akamfanya awe Abate wa monasteri hiyo.
Katika maisha yake, *Gadla Lyasus Mo’a*, yaliandikwa kwamba Yekuno Amlak aliwakimbilia Viongozi wa Amba Sel na kujificha katika kanisa kwa sababu ya unabii uliotolewa kwamba atakuwa mfalme. Mama yake aliposikia unabii huu akamleta katika Monasteri ya Istifanos, katika ziwa la Hyaq na kuwaomba watawa kumficha mwana wake ili asiuawe. Basi Iyasus Mo’a akamlinda mvulana na kumfundisha. Kwa kuwashukuru watawa Yekuno Amlak, baada ya kutawazwa kuwa Kaizari, akawajengea monasteri.
Mt. Iyasus Mo’a, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

[467] Tazama maisha ya Tekle Haymanot tarehe

**Desemba 6**

Sisi Wakatoliki tunawakumbuka siku ya leo Wat. **Dionisia** na mtoto wake **Majoriko**, (na dada yake **Dativa**) walifia dini huko Aljeria, wakati wa dhiki iliyosababishwa na Hunnerik, mfalme wa Waharabu (*Vandals*).[468] Wakati ule ule, katika dhiki ile, kumbukumbu ya **Emiliano**, mganga, **Tersio**, mtauwa, **Bonifasio** na **Leonsia**, na **wenzao watatu**, wote wafiadini.
Huko Kukusa, Afrika ya Kaskazini, kumbukumbu za Mt. **Rogato**, mfiadini, na **Viktoria**, mfiadini, 484 B.K.[469]
Huko Ethiopia, Wakatoliki wanamkumbuka **Gabra-Yohane**.[470]
Huko Guinea na Hispania, kumbukumbu ya Mhashamu **Tshikaba** (*Teresa Juliana de Sao Domingos*), Sista wa Shirika la Dominiko, 1748.
Huko Afrika ya Magharibi na Ufaransa, Wakatoliki wanawakumbuka Watumishi wa Mungu **Raoul** na mke wake **Magdalena Follereau** waliowahudumia wenye ukoma kwa upendo mkubwa.

Huko Misri, Wakoptiki wanawakumbuka Mt. **Viktori**, askofu; **Theofano**, Patriarka wa 60 wa Aleksandria, (953-956); Abba **Djooré** (Chourab), Shahidi.[471]
Huko Ethiopia, Wakristo wanawakumbuka Mt. **Yakobo** mwenye mwili uliokatwakatwa (*the mangled*); Wat. **Timotheo** wa Banhor na mke wake **Maura**, wafiadini; **'Al'are**, Abba **Takla Hawaryat** wa Gabrema.[472]

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake. Amina.

---

[468] *Martyrologium Romanum,* ed. 2005. Pamoja nao: Dativa, Leontia, Tersius, mtawa, Emilianus, mganga, Bonifasi na wengine watatu. Wote wafiadini, baada ya kuteswa vibaya sana.
[469] *Les petits Bollandistes*
[470] *The Ethiopian Rite Missal, Abba Emmanuel & Abba Brendan Cogavin, 2002, uk 205.*
[471] *Arabic-Jacobite Synaxarium*
[472] *Ethiopian Synaxarium: Hedar 27.*

## Wat. Dionisia na Majoriko, wafiadini, 484

Mwaka 484, Mfalme Hunerik akawahamisha Maaskofu Wakatoliki, na mara baadaye akawaamuru wale wanaokataa amri zake wateswe hata kufariki. Dionisia, mwanamke mzuri sana, lakini mzuri zaidi kwa sababu ya wivu wa Mungu na utauwa wake, akapigwa vikobo kiasi kwamba mwili wake wote ulikuwa majeraha na damu. Alipomwona Majoriko, mwana wake, akitetemeka kwa sababu ya mateso yake, akamwambia: "Mwanangu, kumbuka kwamba tulibatizwa kwa jina la Utatu Mtakatifu, katika Kanisa Katoliki, Mama yetu. Tusipoteze vazi letu la wokovu, hata Mfalme, akituona bila vazi la arusi, atawaamuru watumishi wake kututupa nje gizani." Kijana huyu alipoimarishwa na maneno yake, akateswa kwa ujasiri hadi kufariki. Mama yake akaukumbatia mwili wake, akamshukuru Mungu kwa sauti kubwa na kuzika mwili wake katika nyumba yake, ili aweze kuomba mara nyingi juu ya kaburi lake.

Dativa, dada yake Dionisia, Emiliano tabibu, aliyekuwa binamu yake, Leonsia, Tersio na Bonifasio, wakateswa kwa ukakamavu mateso makali kwa ajili ya imani. Pia huko Kukusa kulikuwa mashahidi wengi. Kati yao mwanamke mmoja Viktoria, aliinuliwa juu na moto ukawashwa chini yake. Yote yalifanyika wakati mume wake, aliyekana dini yake ya kikatoliki, alimshauri kwa maneno matamu, kumhurumia yeye na watoto wake, hasa mtoto wake mchanga, na kujiokoa kwa kutii amri ya Mfalme. Viktoria akaziba masikio yake na kuangalia upande mwingine ili aweze kuinua moyo wake kwa Mungu. Chakari walipoona mabega yake yaliteguka, mifupa mingi imevunjika, na kuona kwamba hapumui, walifikiri kwamba amefariki. Wakamtelemsha. Akarudi katika ufahamu wake. Baadaye akaeleza kwamba, bikira akamtokea na akamgusa viungo vyote vya mwili wake. Mara akapona.[473]

Wat. Dionisia, Majoriko na wenzenu, mtuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

## Mhashamu Tshikaba, 1748

[473] Rejea *Butler's Lives of the Saints*, December pp. 93-94



Tshikaba anajulikana huko Hispania kwa jina la Teresa Juliana de Sao Domingos. Wengine walizoea kumwita *El Nigrita*. Alizaliwa katika nchi ya Sierra Leone, Afrika Magharibi, manmo mwaka kama 1676. Nchi ya Sierra Leone ilitembelewa na Wamisionari kuanzia mwaka 1605. Mfalme Bai Farana akampokea vizuri Padri Balthassar Barrier na kubatizwa naye kwa jina la Filipo. Ukristo uliendelea hadi Mfalme Filipo II alipofariki, mwaka 1667. Mfalme mpya Naimbama akaacha imani. Wamisionari waliendelea kufika mara chache zaidi, hadi hawakufika tena. Lakini imani ikaendelea kuwepo kwa namna yake. Chembe iliyopanda ikakua ndani ya watu wachache, mmojawapo ndiye Tshikaba. Miezi michache kabla ya kufa kwake aliwasimulia masista wenzake habari zake.

Alikuwa binti wa mwisho wa Mfalme wa kabila la Gallinas, katika nchi ya Sierra Leone. Baba yake alikuwa mpagani. Kila asubuhi mapema aliabudu Jua na watu wake walimsindikiza kwa nyimbo na shangwe. Tshikaba, kinyume cha watu wengine, hakufanya hivyo. Alipenda kuzurura huko na huko, watumwa wa baba yake wakimwangalia kwa mbali. Akitembea kati ya mashamba, alikuwa anatafakari juu ya chanzo cha viumbe. “Nani alipamba mashamba haya kwa maua mazuri? Nani alijenga milima? Nani anamwagia maji miti ya porini? Siyo baba yangu, ambaye hajali viumbe hivi?” Alifikiri kwamba jua angani bila shaka limeumbwa na Mmoja. Ndiyo maana alitaka kumwabudu Muumbaji. Kuzungumza na baba yake kulimwacha kuhangaika. Daima alifurahi kutembea mashambani, na kuendelea kutafakari juu ya chanzo cha jua.

Pole pole hakutambua tu uwepo wa Mungu, bali alianza kusikia sauti yake. Mvumo wa maji ulimwambia: “Mfalme mkuu hataki uteswe na kiu”. Maua yalimwimbia sifa ya Mungu: ”Aliyetuumba ametutuma kwako kukupamba na kukufurahisha kwa harufu yetu.” Kwa hiyo katika sala alimwomba Mungu ajidhihirishe kwake.

Siku moja, jioni, tunasoma katika kitabu chake cha kumbukumbu (*diary*), aliona maono. Akainua macho yake na kuona, karibu ya chemchemi ya maji, mwanamke mweupe kama theluji, aliyebeba mtoto mwanamume mikononi mwake, akitabasamu. Akamwita kwa jina la Teresa na siyo Tshikaba.
Siku nyingine alitembea mashambani, lakini akapita njia nyingine. Akapotea na mwisho akafika mahali pa juu na kutoka pale aliweza kuona bahari. Pwani aliona kitu ambacho hakujua ni nini. Kumbe ilikuwa merikebu ya Wahispania. Tena peke yake, akaona kijana mmoja anayemkaribia na kumshika mkono wake na kumwongoza hadi merikebu. Wakapanda meli na akajikuta amezungukwa na watu wenye mshangao na upendo. Wakaondoka na kurudi Hispania. Tshikaba akajiona peke yake akipelekwa mbali na wazazi wake, ndugu zake na mahali alipolelewa. Akataka kujitupa baharini lakini mwanamke aliyemwona katika maono karibu ya chemchemi ya maji akamtokea tena, akasimama upande wake, akamzuia na akamfariji. Merikebu ikafika bandari ya Sevilla, mwisho wa safari yake.
Mmiliki wa merikebu na mke wake wakamtunza Tshikaba na kumfundisha mila, lugha na dini ya Wakristo. Akajifunza kwa haraka kwa sababu yale aliyofundishwa hayakuwa mambo mageni kwake, bali maelezo ya mambo yaliyopandwa ndani ya roho yake. Akabatizwa na kuitwa Teresa.
Walipotambua fadhila zake, wafadhili wake wakampeleka huko Madrid, mji mkuu wa Hispania, na kumpatia Mfalme Karolo II Teresa kama mtumwa wake. Yeye akipendezwa mno na uzuri wake hakutaka kumchukua kama mtumwa. Akamkabidhi kwa Pedro de Toledo y Leiva, mkuu wa Mancera. Mheshimiwa Pedro na familia yake wakaendelea kumfundisha dini. Lakini Shetani, adui wa mema yote, akawainua watumishi wote juu yake, wakamtesa kisirisiri, hata mmojawapo alimtisha kumwua. Teresa akavumilia mateso yote, akikimbilia kanisani na kukaa mbele ya Yesu msulubiwa. Yesu akamtokea mara kwa mara, akamfariji na kumshauri.
Wakati ule Mfalme wa Guinea Kusini akafika Hispania. Mfalme Karolo II akampasha habari kuhusu Teresa. Mara Mfalme akaenda kumwona na kumtambua. Akamweleza kwamba wazazi na ndugu zake walibatizwa kabla ya kufariki na wengi wa nchi yake walibatizwa.

Akamsihi kurudi katika nchi yake na kutawala pamoja naye. Lakini Teresa alimjibu: ”Hekima yako haihitaji msaada wangu. Kazi yangu ni kuwaombea watu wetu na kumtolea Mungu mateso yangu kwa ajili yao. Mapenzi ya Mungu ni kumaliza maisha yangu hapa kama mchumba wa Bwana wetu Yesu Kristo”.

Alipoonyesha hamu ya kuishi maisha ya utawa, Mheshimiwa Pedro akampeleka kwa konventi ya Mt. Maria Magdalena, wa Shirika la Dominiko, Salamanca. Huko katika konventi akashawishiwa kuhusu wito wake. Je, kweli Mungu anamwita kuishi maisha ya utawa? Je, si afadhali arudi katika nchi yake, awe Malkia na kuwaongoza watu wake kumjua Kristo, wabatizwe na kuwa Wakristo? Aliposhauriwa na kuimarishwa katika imani yake na mama mkuu, akabaki. Tarehe 29 Juni 1704 akaweka nadhiri zake, katika ibada iliyoongozwa na Askofu wa Salamanca. Baada ya ibada akaona katika maono Mt. Dominiko na viumbe vingi vya mbinguni vikimzunguka, akimbariki kwa ishara.

Akapewa kazi ya kuwahudumia wagonjwa. Sifa yake ya utakatifu ikaenea haraka katika nchi ya Salamanca. Watu wengi wakamfikia kutafuta shauri na uponyaji wa Mungu kwa njia ya mikono yake. Mwujiza wa ajabu ukatokea wakati wa vita katika nchi ya Hispania. Mji Salamanca uliposhambuliwa na mabomu na karibu kutekwa, kwa haraka Sista Teresa akaweka picha ya Mt. Visenti Ferrer dirishani na kuanza kusali. Mji ukaokolewa.

Sista Teresa akateswa na uvimbe gotini kwa miaka mingi, hadi mwaka 1748 ugonjwa wa kiharusi ulipoenea mwili wake mzima. Akafariki tarehe 6 Desemba 1748, baada ya kupokea sakramenti ya wagonjwa. Wakati wa kifo chake ngozi yake ikawa nyeupe kama theluji kwa muda mfupi na mwili wake ukatoa harufu nzuri sana. Akazikwa katika konventi ya Mt. Maria Magdalena, Salamanca, Hispania.[474]

Mhashamu Teresa Tshikaba, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

---

[474] Habari hizo zinatoka na kitabu kilichoandika na Dominic A. Nicoliello: *Our Ancestors in the faith*, ed Paulines Publications Africa, uk.80-91, 2d edition, 2001. Rejea pia kitabu cha Cebolla Luica Ordonez, *Juliana Sister Teresa of St. Dominic: The African Princess*.

Faleceu em  do mesmo ano após receber a  .

No momento de sua morte, outro milagre aconteceu.Sua pele ficou branca como a neve por alguns instantes e seu corpo exalava perfume.**Teresa Juliana de São Domingos** (  , Ocidental, às margens do  -  de  ,  ,  ), nascida **Tshikaba** , cognomizada *La Negrita* , foi uma religiosa dominicana, professora de catecismo e é  da  .

**Desemba 7**

Huko Aljeria, Wakatoliki wanamkumbuka Mt. **Severo** (*Servus*), mfiadini, huko Tuburbium Aljeria, 483. Wakati wa dhiki iliyosababishwa na Hunnerik, mfalme wa Waharabu (*Vandals*), akapigwa kwa muda mrefu na fimbo, akainuliwa juu na kuachwa ghafla aanguke juu ya mawe, akasuguliwa na mawe yenye ncha kali, na mwisho akafariki.
Huko Misri, Wakatoliki wanamkumbuka Mt. **Agato**, askari, mfiadini Aleksandria. Wakati wa dhiki iliyoanzishwa wa Kaizari Desio, akiwazuia watu kuidharau miili ya mashahidi, mkutano wakaanza kupiga kelele. Akakamatwa na kupelekwa mbele ya Hakimu. Alipokiri kwamba Yesu ndiye Kristo, basi akahukumiwa afe, [475] mnamo mwaka 384.
Huko Mahenge, Tanzania, Wakatoliki wanamkumbuka **Nikas Kipengele**, Askofu, aliyefariki mwaka 1971.

Wakoptiki wanawakumbuka Mt. **Abba Pijimi** (Bidshimi**,** au Bejimi), mtawa katika jangwa la Misri;[476] Mt. **Ptolemaeo**, mwana wa Nestorio wa Tentyris, mfiadini, wakati wa utawala wa Gavana Ariani.
Waorthodoksi wanawakumbuka **Mashahidi wa Afrika** walioteswa wakati wa dhiki ya Waharabu, mwaka 429 na baadaye.
Huko Ethiopia, Wakristo wanawakumbuka Mt. **Sarapamon**, askofu wa mji wa Nikiu (*Nakiyos* au *Lukyos*), mfiadini. Mt. Abba **Likani** (*Liqanos*), padre, wa monasteri ya Kuonasel, Ethiopia, mmoja wa Watakatifu tisa.[477]

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake. Amina.

.

---

[475] *Roman Martyrology,* ed. 1956. Habari za Servus zinapatikana katika kitabu cha Victor of Vita, *The Life of St. Eugene*.
[476] *Coptic Synaxarium: 11 Kiahk.*
[477] *The Ethiopian Rite Missal, Abba Emmanuel & Abba Brendan Cogavin, 2002, uk 206. Ethiopian Synaxarium: Hedar 28.*

## Mashahidi wa Afrika, 429



Mwaka 429, Waharabu (*Vandals*) themanini elfu walivuka bahari ya Kati, kutoka Hispania na kuingia Afrika ya Kaskazini. Kwa muda wa miaka kumi wakiua na kuvamia, walitawala maeneo yote ya ki-rumi katika Afrika ya Kaskazini. Waharabu hawa walikua wapagani walioongoka kuwa wafuasi wa Ario. Chini ya uongozi wa Mfalme wao Genserik walianza kudhuru Kanisa mahali popote walipolikuta. Wakristo Wakatoliki wengi, maelfu kwa maelfu, waliteswa ki-katili sana kwa kukiri imani yao, hasa makleri.

Leo Waorthodoksi wanawakumbuka waamini wao ambao Waharabu waliwachoma moto katika kanisa lao, wakiimba nyimbo na kumsifu Mungu hadi kufariki kwao. Waamini walipokusanyika ki-siri kuadhimisha ibada yao, askari waliwashambulia ghafla. Wachache walikimbia lakini mia tatu walifariki kwa kuteswa vibaya na kukatwa vichwa. Wakleri wawili walichomwa moto, na wakleri sitini walikatwa ulimi. Hata hivyo waliendelea kuhubiri kwa uwezo wa Mungu na kupinga uzushi wa Ario.

Genserik alipokufa mwaka 454, amani ikarudi lakini kwa muda mfupi. Waandamizi wake Hunerik (477-484) na Gonthamund (484-497) wakaendelea kuwadhuru Wakristo kwa ukatili kama zamani. Leo Waorthodoksi wanawakumbuka pia mashahidi mia tatu waliochagua kufa mjini Kartago kwa upanga, kuliko kukubali kubatizwa kwa ubatizo wa Ario.

Afrika ya Kaskazini ikawa chini ya utawala wa Waharabu kwa miaka mia, hadi Kaizari Justiniani akawafukuza tena katika vita yake miaka 523-525. Lakini Kanisa la Afrika, ambalo lilikuwa mwanga ulimwenguni, halikupata tena nguvu zake za zamani.

Mashahidi wa Afrika, mtuombee Injili ienezwe upya katika Afrika na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

## Mtakatifu Bejimi, Mwanakoriti

Mtakatifu huyu hafahamiki sana katika Kanisa Katoliki, lakini ni Mkaa pweke mmojawapo aliyeheshimika sana katika Kanisa la Wakoptiki. Abba Bejimi amezaliwa katika mji wa Fisha, Misri. Wazazi wake walikuwa wakristo. Alipokuwa anawachunga kondoo za baba yake shambani, Malaika wa Bwana akamtokea na kumwambia: "Je, ungependa kuwa mtawa pamoja nami, ili tutumie maisha yetu kumwabudu Mungu kuliko kuwatunza wanyama hao?  Siku tatu kuanzia leo, watawa watatu watakuja kunichukua kwenda monasteri yao, na ukitaka unaweza kuja tu!" Moyo wa kijana ukafurahi sana, kuishi maisha ya utawa ilikuwa hamu ya moyo wake. Kwa hiyo alimjibu rafiki yake mpya: "Ndiyo, tafadhali unichukue!" Siku tatu baadaye, watawa watatu walipopita mashambani na wakamwona Bejimi. Malaika akamwambia mkubwa wao: "Ni vyema kumchukua pamoja nanyi huyu nguzo ambaye atakuwa mwanga kwa ulimwengu, kwa sababu ni mpendwa mmojawapo wa Mungu. Atarudi mahali hapa siku za mwisho wake na Mungu atatenda kwa mikono yake miujiza mingi, hadi atakapomaliza safari yake duniani."

Alipotambua kwamba alikuwa Malaika wa Bwana aliyemfunulia maneno hayo, Mkubwa huyu akamkaribia kijana na kumwuliza: "Je, ungependa kujiunga nasi?  Lakini ninakuonya kwamba safari ni ndefu tena inachosha". Bejimi akawaambia: "Nitawasindikiza." Akijaa furaha akatembea pamoja nao hadi wakafika kwa Mlima Nitria, na huko akapumzika pamoja nao siku chache. Baadaye wakaendelea kutembea kwa njia ya jangwa la Shete umbali wa maili sabini. Njiani, watawa wakamfundisha Bejimi sheria na mila za utawa, na kwa njia ya mifano yao wakamfundisha unyenyekevu, sala, kufunga, kukesha, kufanya kazi ya mikono na kujifunza kwa moyo Maandiko Matakatifu. Bejimi akakua siku kwa siku katika maisha ya ki-roho, unyenyekevu na uvumilivu, akikaa katika hofu ya Mungu. Watawa wakafurahi kuona fadhila za Bejimi na matendo yake na upendo wake na kushiriki katika

sakramenti ya Kanisa. Alipoishi miaka saba katika utii na upendo wa kikristo kwa watawa hao watatu, wakamvisha na mavazi ya utawa.

Bejimi alikuwa mtu mzuri, umbo la kupendeza, na kwa sababu ya tabasamu na upole wake, wakamwita "Mwana wa amani". Akaishi kwa miaka kumi na tano kwa kuwatii kabisa watawa wazee watatu, hadi wakaaga dunia kuingia katika ufalme wa mbinguni. Wakati alipokaa na watawa hao, wakatabiri kwamba atakuwa siku moja Kiongozi mkuu kwa maisha ya ki-roho. Baada ya kufariki kwao, Bejimi akabaki miaka miwili mahali pale, na baadaye akakaa katika jangwa la Shete kwa miaka ishirini na minne. Sifa zake zikaenea katika nchi yote. Wengine miongoni mwa watawa na watu wakamfikia kupata baraka zake. Alipotambua kwamba alitumia muda mrefu sana kuongea na watu na kuwaongoza katika maisha ya ki-roho, akaanza kuogopa kujaa na kiburi na sifa za watu na kuchafua usafi wa moyo wake. Kwa hiyo, alianza kutafakari juu ya siku ya mwisho wa maisha yake, hukumu ya Mungu na akaanza kujilaumu akisema: "Nifanyeje ikiwa Mungu ataniita usiku wa leo? Je, nitasimamaje mbele yake na kutoa hesabu za matendo ya maisha yangu?" Basi, akasimama na kutembea katika jangwa la Shete kwa siku tatu, usiku na mchana. Hakuchukua kitu chochote isipokuwa kuti moja kama fimbo. Hakula kitu kwa siku hizo tatu. Mara pepo wakamtokea kama wanyama wakali, wakitaka kumrukia na kumla, lakini hawakuweza kumkaribia. Kwa hiyo, Mtakatifu Bejimi akawaambia: "Ikiwa Bwana wangu Yesu Kristo amenitupa kwenu, siyo lazima ninyi nyote muwe hapa, kwa sababu mmoja wenu angetosha kuniua, lakini kama Bwana hakuwapa mamlaka juu yangu, basi nendeni mbali nami". Aliposema maneno hayo, akafanya ishara ya msalaba na mara wakatoweka kama moshi.

Mtakatifu akaendelea kutembea jangwani. Akasali muda wote na akafurahi kwa sababu Mungu alikuwa anamsindikiza na kumwimarisha. Baada ya siku mbili, akafika katika bonde ndogo lililojaa na mitende na bwawa la maji. Akafurahi alipowaona wanyama wengi wakinywa maji kwa furaha. Akaendelea kutembea kwa maili ishirini hadi alipoona pango upande wa mlima mrefu. Hapa akakaa kwa miaka ishirini na minne, akiishi kwa majikanio, kusali na kuabudu, kwa upole na unyenyekevu wa moyo, akikumbuka daima maneno ya Bwana: "*Jitieni*

*nira yangu, mjifunze kwangu, kwa kuwa mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo, nanyi mtapata raha nafsini mwenu*“ Mt 11:29.
Kwa miaka mitatu ya kwanza kuishi pangoni, alikuwa anakunywa mara moja kila baada ya siku sita. Alikula tende chache zilizoanguka chini na kunywa maji ya chemchemi. Hakuweka akiba ya chakula wala maji katika pango lake. Kila siku alisali zaburi hamsini na kusoma vitabu vya Musa na Manabii. Alikuwa anasujudu mara mia nne asubuhi na usiku akipiga magoti na tena kusali zaburi hamsini, pamoja na kumsifu Mungu na kusali, kusoma vitabu vya Agano la Kale, na pia Injili na barua za Mitume.
Baada ya miaka mitatu nguo zake zilichakaa, akikumbuka mfano wa Paulo, mkaa pweke wa kwanza, akajifumia nguo ya makuti. Kwa miaka mitatu akapitia mashindano ya ki-roho, kwa hiyo Malaika wa Bwana akamtokea kwa mfano wa mwindaji na kumjalia chakula cha ki-mbinguni, sawa sawa kama malaika alimjalia Eliya Nabii.
Alipokaa jangwani kwa miaka ishirini na minne, Bwana Yesu Kristo, Malaika Mkuu Mikaeli na Mitume kumi na wawili wakamtokea Bejimi na jangwa likamulikwa na mwanga mkubwa. Bwana akamwambia Bejimi: “Amani kwako, mpendwa wangu! Kwa sababu ya upendo wako kwangu na mateso uliyoteswa kwa ajili yangu, kanisa moja litajengwa kwa heshima ya jina lako ... “ Baadaye akambariki na kumwambia: “Simama na rudi katika mji wako ulikotoka, na huko nitatenda miujiza kwa mikono yako, na waabudu miungu ya uongo wataongokea imani ya kweli. Kule utabaki miaka kumi, kabla ya kuaga dunia na kurudi kwangu katika ufalme wa mbinguni, milele na milele. “Bwana Yesu akampatia Bejimi amani yake na kumbariki, kisha akaondoka. Mikaeli akamweka Bejimi juu ya wingu lililompeleka kwa mlima mrefu, maili tatu karibu na nyumbani mwake. Huko Bejimi akakaa katika pango moja dogo na kuishi kwa majikanio na kusali. Alikuwa mfano mzuri kwa kila mmoja aliyemwona.
Siku chache baadaye, malaika wa Bwana akampeleka kwenye eneo la Pharan, nchi ya Palestina, kwa sababu ilikuwa imechafuka kwa uzushi mwingi. Bejimi kwa nguvu ya Roho Mtakatifu akashinda mafundisho potovu. Akapewa na Mungu karama ya miujiza, akiwaponya wagonjwa na kuwafukuza pepo. Abba Bejimi akakaa miaka mitano katika Pharan, akisali na kupiga vita vya ki-roho ili kuwarudisha kondoo waliopotewa.

Malaika wa Bwana akamchukua na kumrudisha katika pango karibu na nyumbani mwake. Akaishi tena miaka mitano, akiwaponya wagonjwa na kuwafariji wengi ili kurudia Imani ya kweli. Kwa hiyo, sifa zikaenea nchi nzima.

Iliandikwa kwamba Abba Shenuda, usiku mmoja, aliona maono. Akainua macho mbinguni na huko akakiona kiti cha enzi kizuri cha ajabu kilicho juu ya nguzo ya mwanga. Na juu ya kiti kulikuwa taji ya vito vyenye kumulika sana. Alipomwuliza malaika mmojawapo, "Kiti hiki cha enzi ni cha nani?" Malaika akamjibu: "Ni kwa ajili ya Abba Bejimi, mkaa pweke wa Fisha, katika jimbo la Maseal." Baada ya ufunuo huo, Abba Shenuda alitaka kumwona mtakatifu, kwa hiyo alitembea jangwani hadi akakutana naye. Abba Bejimi alijua kwa njia ya ki-roho kwamba Abba Shenuda ni nani, kwa hiyo wakakumbatiana kwa furaha. Walikesha usiku kucha wakimsifu Mungu na kusali pamoja, wakizungumza matendo makuu ya Mungu. Abba Shenuda alibaki pamoja na Mtakatifu Bejimi siku chache kabla ya kurudi katika monasteri yake.

Bwana akamfunulia Abba Bejimi saa ya kuaga dunia. Kwa hiyo akamwita mfuasi wake na kumpatia alama kutambua saa ya kuaga dunia hii. Ilikuwa saa 1.00 asubuhi, siku ya kwanza ya mwezi *Kiakh*, wakati Abba Bejimi akapata homa kali, lakini katika mateso yake, kundi la watakatifu wakafika kumtembelea. Siku ya kumi na moja ya mwezi wa *Kiakh*, Abba Bejimi akasalimia roho yake na mkutano mkubwa wa malaika wakampeleka kwa Bwana Yesu Kristo, aliyempenda sana. Alikuwa na umri wa miaka sabini alipofariki.

Kanisa likajengwa kwa jina la "Mababa Wakaa pweke" katika monasteri ya Mtakatifu Makari Mkuu. Katika patakatifu pake kuna ikon ya Abba Bejimi. Sikukuu yake ni tarehe 11 mwezi wa *Kiakh*, yaani tarehe 7 Desemba.[478]

Mtakatifu Bejimi, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

[478] Rejea kitabu cha Fr. Santaan PL Sourinay, *The Hermit Fathers*, uk. 185-190.

**Desemba 8**

Sisi Wakatoliki tunasherehekea sikukuu ya Bikira Maria, Mkingiwa dhambi ya asili. Pia tunamkuwabuka Mt. **Makari**, mfiadini, Aleksandria, Misri. Akachomwa moto, mnamo mwaka 250, wakati wa dhuluma ya Kaizari Desio; Pia kumbukumbu ya Mt. **Hydra**, mwanamke, Siere, Misri.[479]

Mt. **Patapios**, mwenye haki wa Theba, mkaa pweke, Theba, Misri. Alijaliwa karama ya kuponya. Baadaye alihamia Konstantinopoli na kufariki huko.[480]

Huko Afrika ya Kaskazini, kumbukumbu ya **Anthusa**, Shahidi kwa kucholmwa moto, karne la V.

Huko Ethiopia, Wakatoliki wanawakumbuka pia siku hiyo **Gabra-Masqal**, mwana wa Kaleb.[481]

Huko Malagasi, Wakatoliki wanamkumbuka Mtumishi wa Mungu **Henriko de Solages**, vika ya kitume, 1832.

Huko Ngongo Mbata, Jamhuri ya ki-demokrasia ya Kongo, Wakatoliki wanamkumbuka Mtu wa Mungu **Jorji de Geel**, Padri wa Shirika la Wakapuchini, aliyeuawa mwaka 1652.

Huko Tanzania, Wakatoliki wanamkumbuka Mtu wa Mungu **Lauriani** (Laurean) **Rugambwa**, Askofu wa Kwanza Mtanzania na Kardinali wa kwanza Mwafrika. Alikuwa Askofu Mkuu wa Dar es Salaam mwaka 1968 hadi 1992. Alifariki mwaka 1997.

Huko Jamhuri ya Afrika ya Kati, kumbukumbu ya **Yakobo Iyere** na **Yohane Klaudio Kilamong**, 40, mapadri wazalendo, waliouawa, mwaka 2002.

Huko Misri, Wakoptiki wanawakumbuka Mt. **Hedra**, askofu wa Aswan na Mt. **Yohane**.[482]

**Walei Mashahidi 300** na **Mapadri Mashahidi 62**, waliouawa na Waharabu (*Vandals*).

---

[479] Dictionary of Saints

[480] *Martyrologium Romanum,* ed. 2005. Rejea maisha ya Patapios, tarehe 21 Februari

[481] *The Ethiopian Rite Missal, Abba Emmanuel & Abba Brendan Cogavin, 2002, uk 206. Ethiopian Synaxarium: Hedar 29.*

[482] *Coptic Synaxarium: 12 Kiahk.*

Huko Ethiopia, Wakristo wanawakumbuka Mt. **Petro**, Patriarka, askofu wa 17 wa Aleksandria, Misri, mfiadini; Mt. **Klementi**, askofu wa Roma, (mfuasi wa Mtume Petro aliyembatiza huko Aleksandria, Misri); **Mashahidi wote** walioteswa chini ya utawala wa Kaizari Dioklesiani.

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake. Amina.

## Bikira Maria, Mkingiwa dhambi ya asili

Mwaka 1854, tarehe 8, mwezi wa Desemba,  wakati wa sikukuu ya Bikira Maria aliyekingiwa na dhambi ya asili, Baba Mtakatifu Pio IX, katika barua yake *'Ineffabilis Deus'*, alitangaza kwamba fundisho hilo ndilo imani kweli ya Kanisa Katoliki, ambayo sasa ilimbidii kila Mkataloki aisadiki. "Tunatangaza kwamba Bikira Maria, tangu kutungwa kwake, kwa neema na jaliwa la pekee kutoka na Mungu, na kwa mastahili ya Yesu Kristo, Mwokozi wa wanadamu, alikingiwa na doa yoyote ya dhambi ya asili…"
Miaka minne kisha kutangazwa Bikira Maria kukingiwa dhambi ya asili, mwaka 1858, msichana mmoja, jina lake Bernadeta, alieneza habari kwa ujasiri kwamba Bikira Maria alimtokea mara nyingi. Alimtokea huko Lurdi, Ufaransa, katika pango karibu ya mto Gave. Bikira Maria akajitambulisha, kwa lugha yake, ‘Maria, Mkingiwa dhambi ya asili‘.
Waorthodoksi na Wakoptiki hawana imani hiyo na hawasherekei sikukuu hiyo. Kwao wanakumbuka mtangazo wa malaika kwa Yoakimu na Anna [483] kwamba baada ya kukaa miaka mingi bila mtoto, Mungu amewahurumia. Malaika akawaambia: “Nabii za zamani zitatimizwa karibuni ndani yao. Watamzaa mtoto, atakayekuwa Sanduku la Agano Jipya, Ngazi Takatifu, Kijiti lilichowaka moto bila kuteketea, Hekalu hai ambamo Neno la Mungu atakaa.“ Ingawa kuzaliwa kwake Bikira Maria kutatokewa kwa tendo la ki-mwujiza la Mungu, Maria alitungwa kwa njia ya mume na mke kukutana, kadiri ya sheria ya ubinadamu, ulioanguka kwa dhambi la Adamu na kuwa chini ya dhambi na

[483] Rejea Waorthodoksi tarehe 9 Desemba, na Wakoptiki tarehe 31 July

uharibifu (Mwa 3:16). Kama chombo kiteule na Sakrario yenye thamani iliyotengenezwa na Mungu tangu kuweka misingi ya ulimwengu, kweli yeye ndiye binadamu mtakatifu sana na mkamilifu kuliko wanadamu wote, hata hivyo, hakukingwa na urithi na matokeo ya dhambi ya wazazi wetu wa kwanza. Mama wa Mungu alichaguliwa na kupendelewa kati ya wanawake wote, siyo kwa holela, bali kwa sababu Mungu alijua tangu zamani kwamba atalinda moyo kuwa safi, bila doa la dhambi, na kamilifu. Alipotungwa na kuzaliwa kama sisi sote, alichaguliwa kuwa Mama wa Mwana wa Mungu na Mama yetu sisi sote. Kwa hiyo katika upendo na huruma yake, anaweza kutuombea kwa Mwana wake, ili atuhurumia.
Waorthodoksi wanasema kwamba kadiri ya Mababu wa imani, tunarithi kutoka Adamu, siyo ushirikiano na dhambi ya asili, bali tunarithi matokeo yake, yaani kifo, uharibifu wa mwili na tamaa, pamoja na kuzaliana na kujamiana. Kwa hiyo, Waorthodoksi wanakiri kwamba Mama wa Mungu ni mrithi, kama sisi, wa matokeo yote ya dhambi ya Adamu, Kristo peke yake amekingwa na hayo. Hata hivyo, wakati huo, bikira Maria alikuwa safi na bila dhambi ya binafsi, kwa sababu alijikinga mwenyewe kwa anasa za ulimwengu na kutawala tamaa zake. Kwa hiari alifanya kazi pamoja na Mungu kwa kutimiza mapenzi yake: "*Tazama, mimi ni mjakazi wa Bwana; na iwe kwangu kama ulivyosema*" Lk 1:38.
Kutokana na maneno ya Baba Mtakatifu Pio IX, Wakatoliki tunaamini kwamba Maria aliokolewa pia na Yesu Kristo, Mwokozi wa watu wote, wakati wa kutungwa kwake. Jaliwa lake ni kwamba mastahili ya Yesu Kristo yalimfikia kabla ya Yesu kufa msalabani.
Bikira Maria, Mkingiwa dhambi ya asili, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

## Mtu wa Mungu Jorji wa Geel, 'Shahidi', 1652

Mtu huyu alikuwa mmojawapo wa watangulizi kupeleka Injili katika Afrika ya kati. Alizaliwa huko mji Geel, Uholanzi, tarehe 8 Agosti 1617. Wakati ule nchi yake ilikuwa chini ya utawala wa Wahispania. Baba yake aliitwa Melchiori Wimmems na mama yake Anna Tysmans. Akajifunza falsafa katika Chuo cha Louvain na teolojia katika Seminari ya Anvers. Ni katika kanisa kuu la Anvers alipopata daraja la ushemasi

tarehe 21 Septemba 1641 na kupadirishwa tarehe 15 Machi 1643. Kati ya tarehe hizo mbili, hamu ya kuwa mmisionari ilizaliwa moyoni mwake. Ndiyo maana, tarehe 11 Novemba 1642 akavalishwa mavazi ya wakapuchini na kupewa jina la Jorji wa Geel.

Tarehe 19 Machi 1648, Baba Mtakatifu Inosenti II aliwapokea mabalozi wa Mfalme Garcia II, mfalme wa Kongo, aliyeomba kutuma wamisionari. Tarehe 8 Juni, katika ofisi ya *Propagande Fidei*, hati ikasainiwa ili kuwatuma wamisionari wakapuchini kwenda Kongo. Kwa hiyo, mwezi wa Septemba, Jorji na wenzake wanne wakaanza safari zao wakifika bandari ya Cadix, Hispania, ili kupanda meli na kwenda Afrika. Njiani wakacheleweshwa. Mwanzoni mwa 1649 wapo bado Madrid, lakini tarehe 3 Aprili 1650 wakaondoka na kukaribia pwani ya Kongo, tarehe 13 Juni, baada ya kukumbwa na tufani na kuvumilia mashambulizi ya maharamia.

Wakapuchini wakafika Pinda, (kwa sasa Sao Antonio do Zaire) tarehe 29 Juni 1650. Wakakaa huko wakiwahudumia wagonjwa. Lakini hali ya hewa, ukosefu wa chakula, bila kuhesabu kushika sheria ya Shirika lao, kama kuvaa mavazi ya joto sana, kutembea peku na kufunga, vikawashinda. Padri Erasmo wa Furnes akafariki tarehe 1 Oktoba 1651. Basi Jorji, kwa kutembea wiki mbili, akaenda Sao Salvador, mji mkuu wa mfalme, ambapo hali ya hewa ilikuwa nzuri zaidi.

Wakati ule, ufalme wa Kongo ulianza kupoteza umuhimu wake. Misioni ya Luanda, Angola, ikapata kuwa muhimu kuliko Misioni ya Sao Salvador. Jorji alikuta jumuiya isiyo na uhai. Wanajumuiya waliteseka kwa njaa na hali ya hewa. Mawasiliano kati ya wamisionari na Mfalme Ndo Galassia I, aliyerudi kufuata dini ya jadi, yalikuwa mabaya. Basi pale pale Jorji alijitoa kuwahudumia wagonjwa, lakini hasa akajifunza kutokana na wenzake mila na lugha ya nchi, na namna ya kuinjilisha. Ndipo alianza kuandika kamusi ya kwanza Kilatini-Kihispania-kikongo.

Mwaka 1652 mawasiliano na Mfalme yakaanza kuwa mazuri zaidi, kwa hiyo kazi ya ki-misionari ilianza upya. Jorji akatumwa kwenda Matari, mkoa wa Nsundi, eneo ambalo limekwisha pokea Injili na Wakapuchini, lakini moyoni Wakristo walibaki wapagani. Tarehe 12 Februari akatembelea vijiji vya jirani na kurudi Matari tarehe 31 Machi. Tarehe 23 Mei, akaondoka tena kuelekea Inkisi, kwa njia ya Ngongo

Mbata. Akabaki miezi miwili katika eneo hilo, akitoa sakramenti ya Ekaristi kila siku, akibatiza, kuungamisha na kuwaongoa Waprotestanti wanane. Akarudi Matari kwa sikukuu ya Bikira Maria Kupalizwa mbinguni. Kutoka kule akaelekea kwenda Sao Salvador kukutana na Mkuu wa misioni ya Kongo, Padri Hiasinto (*Hyacinthe*) de Vetrella. Kufuatana na kazi yake njema, Padri Jorji akatumwa kukaa Ngongo Mbata.

Eneo la Mbata lilipokea Injili tangu mwanzo wa karne la XVI. Lakini kwa sababu wamisionari walikuwa hawakuweza kukaa, ukristo ukafifia hadi Jorji na mwenzake walipofika mwaka 1648. Mwezi wa Septemba 1652 aliamua kuzuru eneo. Akafika Ulolo, kijiji ambacho nusu ya wenyeji walibatizwa. Basi akaacha nguo za kanisa, na akaenda Matari kuchukua mizigo yake, akitamani kukaa Ngongo Mbata. Aliporudi Ulolo, mwisho wa Novemba, alishangaa kutambua kwamba Wakristo walishika mila ya ki-pagani. Kwa hasira alichoma hirizi zote na kuwakumbusha wajibu wao. Ndipo mganga asilia akampiga na rungu yake na kumwonyesha kwa wenyeji. Jorji akapigwa mawe na kuanguka. Watu wote wakakimbia. Lakini muda si muda, kwa hofu ya hukumu, wakamchukua akiwa amejeruhiwa vibaya na kumpeleka hadi Ngongo Mbata. Mwenzake akamtunza kadiri ya uwezo wake, akimpatia sakramenti. Jorji akafariki tarehe 8 Desemba 1652, akiwasamehe watesaji wake. Akazikwa katika shamba la wafu. Mfalme Ndo Ngalassi II alipopata habari akaamuru kijiji kiteketezwe na wakazi wauawe. Wamisionari wakaingilia kati, na amri haikutimizwa.

Mtu wa Mungu Jorji, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

## Mtumishi wa Mungu Henriko de Solages, 1832

Mtu huyu ni mfano wa Wamisionari wanaofariki kwa sababu ya wivu wao wa kueneza Injili, bila kufaulu.

Henri alizaliwa Ufaransa, tarehe 22 Agosti 1786. Baba yake alikuwa Hieronimo Lodi de Solages, afisa katika jeshi na mama yake Elizabeti Thompson, Mwingereza. Miaka miwili baada ya kuzaliwa alihamia Uingereza. Mwaka 1805 akarudi Ufaransa, akiwa na umri wa miaka 19. Akaingia seminari huko Paris. Akapadirishwa tarehe 17 Desemba 1814.

Alipokuwa seminari alisikia habari za misioni na kufa shahidi, ndipo hamu ya kwenda kuhubiri Habari Njema ya Kristo katika nchi za mbali ikazaliwa moyoni mwake.

Aliposubiri kutimiza hamu ya moyo wake akafanya kazi kwanza katika Parokia ya Mt. Benedikto, na baadaye akachaguliwa kuwa makamu wa askofu wa Pamiers. Mwaka 1829 akateuliwa kuwa Vika wa kitume wa Kisiwa cha La Réunion. Alipoondoka Ufaransa mwezi wa Septemba 1830 Henriko akafika Kisiwa cha La Réunion baada ya miezi mnne, akisindikizwa na Padri Dalmond. Kwa miezi 18 akalihudumia Kanisa, akikutana na vizuizi vingi kutokana na wakleri wa nchi hiyo. Hasa alijaribu kuinjilisha watumwa ambao walikosa mafundisho ya dini. Akachapisha katekisimu ndogo kwa ajili yao na kwa machotara wa Kisiwa. Lakini nchi ya La Réunion haikuwa nchi ya misioni ambayo alitamani. Macho yake yaliangalia Kisiwa kikubwa cha Malagasi. Kwa hiyo tarehe 13 Julai 1832 akapanda meli kuelekea Malagasi, akimwacha Padri Dalmond kuwa Makamu wa Prifekti wa Kanisa la La Réunion.

Kama alivyoeleza katika barua yake kwa Baba Mtakatifu Gregori XVI safari yake ililenga kutambua jinsi iwezekanavyo kuwaletea wenyeji Imani. Baada ya safari ngumu akafika Tamatave Jumanne, tarehe 17 Julai. Ndipo matatizo yakaanza. Kwa siku nzima alitafuta mahali pa kulala, na alihitaji siku kadhaa kupata nguvu zake zote baada ya safari. Tena hali ya hewa ilikuwa mbaya kwake. Akahusiana na Korola (*Coroller*), Gavana wa Tamatave, lakini ilimbidi asubiri wiki moja kabla ya kumwona. Korola akamshauri kumwandikia Malkia Ravalona I barua kabla ya kuamua kwenda Tananarivo, mji mkuu. Henriko hakujua kwamba Malkia, akishauriwa na Wamisionari Waprotestanti hakuwapenda Wafaransa wenye dini Katoliki. Akamwandikia akimweleza mpango wake kuanzisha shule kwa wasichana, ikiendeshwa na Masista wa Mt. Yosefu wa Cluny. Barua yake ya kwanza hakujibiwa. Vivyo hivyo kwa barua yake ya pili. Basi karibu mwisho wa mwezi Septemba 1832, kwa vyovyote, akaamua kwenda Tananarivo. Akafika Maromby, lakini wajumbe wa Korola wakamzuia kwenda mbele zaidi na kumlazimisha kurudi Tamatave. Akakataa. Akamwandikia tena barua Malkia na akaenda Andévoranto akisubiri jibu kutoka kwa Malkia. Akakaa kule, peke yake, bila chakula wala msaada wowote wa wenyeji wakiogopa bila shaka wajumbe wa Korola.

Akashikwa na malaria na kwa mwezi mmoja aliteswa na njaa, kiu na umaskini. Kabla ya kupata jibu kutoka Malkia alifariki akiwa peke yake katika kibanda chake, tarehe 8 Desemba 1832. Kesho yake vijana wawili wakaweka mwili wake katika magodoro mawili na kumzika. Kwa muda mrefu wenyeji walipaheshimu mahali alipozikwa kwake, hadi mchanga na mimea vilipofunika mahali kaburi halikuonekana tena. Wakati wa adhimisho la miaka 100 ya kufa kwake, Askofu Fourcadier, akaamua kutafuta kaburi lake. Tarehe 4 Januari masalia yalipatikana na yakazikwa Tananarivo.
Mtumishi Henri de Solages, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

## **Mtu wa Mungu Lauriani Kardinali Rugambwa, 1997**.

Lauriani Rugambwa, fahari ya Wahaya, alizaliwa Bukongo, Tanzania, tarehe 12 Julai, 1912. Akiwa na umri wa miaka 8 alibatizwa pamoja na wazazi wake Domisiano baba yake na Asteria mama yake. Akajifunza katika Seminari ndogo Rubya na baadaye katika Seminari Kuu ya Katigondo, Uganda, na kupadirishwa na Askofu Burcardo Huwiler, M.afr. tarehe 12 Desemba, 1943. Akafanya kazi ya Padri katika Parodia ya Rubya hadi mwaka 1949. Ndipo mwaka ule alienda Roma kufijunza Sheria ya Kanisa, katika Chuo cha kipapa cha Urbania. Tarehe 13 Desemba, 1951 akateuliwa kuwa Askofu wa cheo cha *Febiana* na kufanya kazi kama Vika wa kitume wa Kagera Kusini (*Lower Kagera*). Akapata daraja la Uaskofu tarehe 10 Februari, 1952, akiwa Askofu kijana kuliko maaskofu waafrika wenzake wote 25 katika Afrika nzima. Na tarehe 25 Machi , 1953, akateuliwa na Baba Mtakatifu Pio XII kuwa Askofu wa Rutabo na mwaka 1960, tarehe 28 Machi akainuliwa na Baba Mtakatifu Yohane XXIII kuwa Kardinali. Akawa Mwafrika wa kwanza kuwa Kardinali katika Afrika. Mwaka uliofuata Jimbo la Rutabo likaitwa Jimbo la Bukoba. Na mwaka 1968 akateuliwa kuwa Askofu Mkuu wa Dar es Salaam. Alibaki katika kiti hiki hadi alipostaafu tarehe 22 Julai 1992. Akafariki Dar es Salaam tarehe 8 Desemba 1997 akiwa na umri wa miaka 85. Katika barua yake ya rambirambi kwa Askofu Polycarp Pengo, Baba Mtakatifu Yohane Paulo

II akamwita “Lauriani Kardinali Rugambwa mfanyakazi wangu wa karibu.”

Kama Askofu alihudhuria na kushiriki ki-utendaji katika vikao vyote vya Mtaguso wa Vat. II. na mikutano ya Sekretariati ya Afrika nzima. Lakini mara nyingi alisifiwa kuwa mkimya na mtulivu, fadhila alizorithi kutokana na hali ya uchifu. Kama Askofu Mwafrica mmoja alisema: “Alikaa katika mikutano masaa kadhaa, kama machifu wa kabila lake, bila kusema neno. Hawa machifu hawakufunua mawazo yao kwa yeyote. Ndiyo sehemu ya uwezo wao.”

Alipokuwa Askofu Mkuu wa Dar es Salaam alianzisha shirika la Masista wadogo wa Mt. Fransisko.

Alikuwa mtu wa mahusiano akiumizwa na ubaguzi wowote. Mwaka 1966 Mwandishi wa Gazeti moja ya Vatikani alisimulia kwamba Rugambwa alipozuru Marekani aliumizwa na watu wenye ubaguzi wa rangi. Akakataliwa kukatwa nywele na kinyozi mmoja huko mji wa New York, “Hapa tunakata nywele tu za Watu weupe!” Mwandishi aliendelea kusema kwamba Rugambwa baadaye alimwombea Kinyozi huyu wa New York kila siku.[484]

Wakati wa ibada ya kumpokea kama Kardinali katika Tanzania, wengi kati ya Waseminari waliguswa moyoni wakiwaona wakleri wazungu, maaskofu na mapadri na masista wakimpigia magoti na kubusu pete yake. Rugambwa akasema katika hotuba yake: ”Kanisa Katoliki unatumia mvuto wake kuleta amani kati ya watu, kwa sababu daima linaona ndani yao siyo nafsi za kabila fulani au hali ya maisha tofauti, bali wanadamu walioumbwa na Mungu mmoja, Baba wa wote.” Wakati mwingine alisema: ”Kanisa siyo nyumba ya sanaa wala hifadhi ya nyaraka, bali mwalimu wa uhai”.

Mtu wa Mungu Rugambwa, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

---

[484] *L’osservatore Della Domenica*

**Desemba 9**

Huko Tunisia, Wakatoliki wanamkumbuka Mt. **Restituto**, askofu na mfiadini, Kartago. Wakati wa sikukuu yake Mt. Augustino aliwahubiria Wakristo na kumsifu sana.
Huko Afrika ya Kaskazini, Wakatoliki wanawakumbuka Wat. **Petro**, **Sukseso**, **Basiano**, **Primitivo** na **wengine ishirini**, wote wafiadini.[485]
Huko Ethiopia, Wakatoliki wanamkumbuka **Amda-Seyon I**, mfalme wa Ethiopia.[486] Pia kumbukumbu ya Mt. **Barsusio**, Mwumgama-dini.
Huko Kenya, Wakatoliki wanawakumbuka Watumishi wa Mungu, **Mariani Wachira, Yosefu Gacheru** na **Domeniko Nyota** Makatekista, wa Jimbo la Nyeri, waliouawa na MauMau, mwaka 1952.
Huko Burkina Faso, Wakatoliki wanamkumbuka Mtu wa Mungu **Alexanda Toé**, Padri wa Shirika la Wakamiliani.
Huko Nigeria, Wakatoliki wanamkumbuka Mtumishi wa Mungu **Gabrieli Gonsum Ganaka**, Askofu Mkuu wa Jos, aliyefariki tarehe 11 Novemba, mwaka 1999.[487]
Huko Tanzania, Wakatoliki wanamkumbuka **Mathayo Shija**, Askofu, aliyefariki mwaka 2015.

Huko Misri, Wakoptiki wanawakumbuka Wat. **Barsanufio**, mfiadini na **Abrasio**. Pia wanaadhimisha kumbukumbu ya **Kutabarukiwa Kanisa la Mt. Misaeli**, mwanakoriti.[488] Pia wanawakumbuka **Misaeli, Ghaleoni** na **Eliya** wa Mlima Samhood, wote wanakoriti; Mt. **Kristodulo**.[489]
Huko Ethiopia, Wakristo wanamkumbuka **Anania mnarani**. Waorthodoksi Tewahedo, Ethiopia, wanakumbuka kifo cha **Gabra Maskal**, Mfalme wa Ethiopia, Mworthodoksi, aliyefariki mwaka 1344 B.K.[490]
Waorthodoksi wanakumbuka siku ya **kutungwa Mtakatifu Maria**, Mama wa Mungu, katika tumbo la Anna.

---

[485] *Roman Martyrology,* ed. 1956. Miongoni mwao Abracius.
[486] *The Ethiopian Rite Missal, Abba Emmanuel & Abba Brendan Cogavin, 2002, uk 207.*
[487] Rejea maisha yake tarehe 11 Novemba
[488] *Coptic Synaxarium: 13 Kiahk.*
[489] *Arabic-Jacobite synaxarium*
[490] *Ethiopian Synaxarium: Hedar 30.*

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake. Amina.

## Watumishi wa Mungu Mariano Wachira, Gacheru Yosefu, Nyota Domeniko, Makatekista, 1952.

Tarehe 9 Desemba makatekista Mariano Wachira, Gacheru Yosefu na Nyota Domeniko waliitwa na chifu. Jioni walirudi nyumbani, lakini hawakuonekana tena. Baada ya kutafutwatafutwa, miili ya wawili ilionekana karibu na mto Gekira, siyo mbali na shule, mahali pale walipouawa. Walizikwa tarehe 14 Desemba. Kaburi la Mariano Wachira bado lipo wazi kwa sababu mwili wake haujapatikana. Wote watatu walikuwa Makatekista wenye bidii, Wazee wa Karothi na wanashirika wa ‘Kanisa/Shule‘. Askofu Cavallera, aliyeongoza ibada ya mazishi, aliwaambia waamini: “Kila mtu ana uhakika kwamba ni mashahidi“. Mazishi yao yalifanyika kwa shangwe, watu wa Gikondi na vijiji vya karibuni walifika kuhudhuria ibada wakiimba nyimbo za shangwe. Waliwaita mashujaa wao waliokuwa tayari kufa.

Gacheru Yosefu alikuwa baba wa watoto 9. Alikuwa na miaka 70 alipouawa. Mariano Wachira, (1896-1952), alipita wenzake wote wawili. Alikuwa katekista na mwalimu kwa miaka 35. Ni yeye aliyeanzisha shirika la kanisa/shule. Mtume kweli, alikuwa msitari wa kwanza katika kila kazi ya kueneza Ufalme wa Mungu. Hakuchoka kutafuta wakatekumeni wapya, kuwafundisha katekisimu, kuwatembelea wagonjwa na kuwasaidia Wakatoliki walioasi dini yao. Wakristo wote wa eneo hilo walimtazama kama Mwalimu na Baba yao. Alisimama imara mbele ya vitisho vya MauMau ambavyo vilimlenga muda mrefu. Alitaka jina lake liandikwe katika orodha ya mashahidi. Wakati wa mkutano wa makatekista, huko Karema, alijisikia moyoni mwake, kwamba atauawa. Wazo hilo lilimsukuma kusema: “Wakati umefika sisi kuwa mashahidi wa imani yetu na lazima tuwe tayari na mashujaa hata kumwaga damu yetu kwa ajili ya imani yetu. Najisikia kwamba nitauawa kwa ajili ya Yesu Kristo. Maadui wangu wataweza kuua mwili wangu, lakini roho yangu itaishi milele na milele.“

Tarehe 14 Desemba, Mariano angalipokea kwa mikono ya Vika wa ki-tume medali ya '*Pro Ecclesia et Pontifice*'. Mkristo Mkikuyu angestahili kupokea neema ya ushahidi, ndiye kweli Mariano![491]
Mariano na wenzako, mtuombee ili Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

## Mt. Misaeli, mwanakoriti

Misaeli ni mwanakoriti mwingine wa jangwa la Misri, ambaye hajulikani sana katika Kanisa Katoliki, lakini anaheshimiwa sana na Wakoptiki wa Misri.
Abba Isaka, Mkuu wa monasteri wa El-Kalamon alipoketi katika monasteri yake, kijana akamfikia. Abba Isaka akamfanyia ishara ya msalaba usoni mwake, kadiri ya desturi ya watawa na kumruhusu amkaribie. Kijana akamkaribia na kumsujudia akimwambia, "Baba yangu, Abba Isaka, uyapokee madhaifu yangu kwa ajili ya Bwana Yesu Kristo. Unisaidie kuokoa roho yangu na kunihesabu miongoni mwa watoto wako." Abba akashangaa kwa sababu alimwita kwa jina lake na akamwuliza: "Nani amekuambia jina langu?" Kijana akamjibu: "Neema inayokaa ndani mwako ilinipasha habari." Abate akamwomba Misaeli kukaa karibu naye na kumwambia, "Mungu Mwenyezi akufanye kuwa hekalu takatifu. Na sasa uniambie habari zako". Kijana akamjibu, "Jina langu ni Misaeli. Baba yangu alipenda malimwengu yaliyomzuia kumwabudu Mungu. Alihuzunika kwa sababu hakupata watoto. Siku moja alimkaribisha mtawa mzee mtakatifu na kumweleza huzuni yake kutopata mtoto atakayerithi mali yake. Mtawa akamwambia, "Utengeneze maisha yako mbele ya Bwana, Mpendwa wa wanadamu, na atakupatia mtoto". Akamwuliza mtawa, "Namna gani naweza kufanya hivyo?" Mtawa akamwambia, "Uishi maisha matakatifu na kushika sheria ya Kanisa. Usijitenge na Kanisa na uwe na padri unayemwendea ili akushauri kwa kila jambo. Ukiwa unafanya hivyo, wewe na mke wako, mtapata mnachotamani." Misaeli alimwambia: "Baba yangu alifanya kila alichoambiwa na mtawa mzee na maneno yake yakatimizwa. Mama yangu akajifungua na nikazaliwa."

---

[491] Rejea Fr. Neno Contra,, Louis Kalonji, *African Lay Martyrs*, New People Media Centre, 2009, uk. 34-35, 41.

“Nilipokuwa na umri wa miaka sita, wazazi wangu walifariki. Askofu alinitunza, akanielimisha na kutunza mali yangu. Nilipojifunza Maandiko Matakatifu nilitamani maisha ya utawa, ndiyo maana nimekuja hapa.“ Abate akapendezwa na maneno ya kijana. Akamkabidhi kwa mtawa mmoja wa maonasteri ili kumfundisha majikanio, kumwabudu Mungu wakati wa mashindano na yule Adui. Na ndipo wakamvisha mavazi ya utawa. Toka saa ile alianza kuishi maisha ya upweke, katika sala na majikanio.

Siku moja, mmoja wa watawa wa monasteri akamfikia Abba Misaeli. Akamkuta amesimama akisali. Alipogonga mlangoni, akamfungulia. Wakasali pamoja, wakabarikiana na wakikaa wakaanza kuzungumza namna ya kumshinda Adui. Mt. Misaeli akamwambia, “Shetani anakimbia mbali wakati sala zetu ni sala za kweli na zenye moyo safi“. Baada ya kumaliza mazungumzo yao wakamsifu Mungu na ndugu akaondoka. Muda si muda mtawa huyu akamrudia Abba Misaeli. Akamkuta akisali na kusema, “Bwana uniokoe, tazama upole wangu; unisafishe na uovu wangu, kwa sababu baba yangu na mama yangu wameniacha lakini Bwana amenipokea“. Ndugu alipomwona jinsi alivyo, na jinsi ngozi yake ilivyoshikamana na mifupa yake akalia na kusema, “Mwili wako unaonekana kama umeungua“. Mtakatifu akasema, “Namshukuru Mungu kwa sababu amenijalia macho yangu na masikio yangu ili niweze kusoma Maandiko Matakatifu na kusikia Neno la Mungu. Ananipa nguvu wakati ninaposimama kusali.“

Abate wa monasteri aliposikia habari za majikanio ya Misaeli akamtembelea. Mt. Misaeli akamwambia, “Baba yangu, baada ya siku tatu, watu wanaofanana na askari watakuja na kuuliza habari zangu. Usifiche. Usiogope wala usihuzunike kwa sababu ni mapenzi ya Mungu. Pia ujue kwamba njaa kubwa itatokea mwaka ujao. Nitakuja kuwaona wakati huo.“ Baada ya muda, watu wanaofanana na askari wakamchukua Mtakatifu na kuondoka naye. Abate akasikiliza Mtakatifu aliyomwambia. Akanunua ngano nyingi.

Kama alivyosema Misaeli njaa ikatokea. Gavana akaja kuchukua ngano yote atakayoweza kupata katika monasteri. Lakini askari wakatokea na kumzuia kutenda jambo hilo. Akarudi mikono mitupu. Abate akawakaribisha askari, akawashukuru na kuwatolea chakula. Wakamwambia: “Hatuhitaji chakula chochote“. Mmoja wao akaenda

mbele, akashika mkono wa Abate, akampeleka pembeni na kumwambia, “Mimi ni Misaeli, mwana wako. Watu hawa wanaofanana na askari ni wanakoriti waliofika mwaka jana na kunichukua. Sasa nakuomba uende kwa Abba Atanasi, askofu wa mji wangu nilipolelewa, umwambie habari zangu na kumwomba fedha ya baba yangu. Utajenga kanisa kwa heshima ya jina langu. Na baadaye umwite askofu aje kulitabaruku.“
Abate alifanya kama Misaeli alivyomwambia. Akamwendea askofu, akachukua dhahabu, fedha, vitabu vingi na kondoo mia tano. Tena, akapokea vitambaa, vito na vyombo vilivyokuwa mali ya Mtakatifu Misaeli. Abate akabomoa nyumba ya zamani ya Mtakatifu Misaeli, akanunua kiwanja karibu na nyumba na kujenga kanisa pale. Wakati Baba askofu alipoadhimisha kutabaruku kanisa, Misaeli na wanakoriti wakaja na kuhudhuria ibada. Misaeli akamwambia Abate Isaka, kwamba ataaga dunia hii mwaka kesho. Na mara wakatoweka.[492]
Mt. Misaeli, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

[492] *Coptic Synaxarium: 13 Kiahk.* .Rejea pia kitabu cha Padri Samaan El Souriany, *The Hermits of Egypt,* uk 165-172.

**Desemba 10**

Huko Roma, Wakatoliki wanamkumbuka Mt. **Melkiade**, Baba Mtakatifu aliyetoka Afrika ya Kaskazini.
Pia huko Misri, Wakatoliki wanawakumbuka Wat. **Mina** (*Menas*), **Hermogene**, **Eugrafo**, wafiadini, Aleksandria, Misri, walioteswa chini ya Kaizari Galerio Maksimiani, 235 B.K.[493]
Huko Elizabethville, Jamhuri ya ki-demokrasia ya Kongo, Wakatoliki wanamkumbuka **Fernando Gasgna**, Padri wa Shirika la Mt. Paulo, aliyeuawa mwaka 1961.
Huko Nairobi, Kenya, Wakatoliki wanamkumbuka **Yohane Njoroge Muhia**, Padri wa Jimbo, aliyeuawa mwaka 2018.

Wakoptiki wanawakumbuka Mt. **Kristodulo**, mtawa; Wat. **Simeoni wa Menouf**, Abba **Hori** na Abba **Mina** mzee, na **Amonio**, askofu wa Esna, wote wafiadini.[494] Pia kumbukumbu ya **Theodori**, askofu mkuu wa Aleksandria, mfiadini.
Waorthodoksi wanawakumbuka Wat. **Mina** (Menas)**, Hermogenes**, **Eugrafo**, mashahidi, 235.
Huko Ethiopia, Wakristo wanawakumbuka Mt. Abba **Yohane**, Patriarka, askofu wa 30 wa Aleksandria na Mt. **Atanasi**, Patriarka, askofu wa 73 (au 76) wa Aleksandria.[495]

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake. Amina.

## Wat. Mina, Hermogene na Eugrafo, wafiadini, 238.

Mina alizaliwa Athene, Ugiriki, lakini alipelekwa na Kaizari Maksimini, kufanya kazi huko Aleksandria, Misri, kutoka mwaka 235 hadi 238 B.K. Aliitwa Kallikelados, maana yake azungumzaye lugha ya umbuji, kwa sababu alikuwa mtu mwenye uwezo wa kuwashawishi


[493] *Roman Martyrology,* ed. 1956.
[494] *Coptic Synaxarium: 14 Kiahk.*
[495] *The Ethiopian Rite Missal, Abba Emmanuel & Abba Brendan Cogavin, 2002, uk 208.. Ethiopian Synaxarium: Tahisas 01.*

watu. Eugrafo alikuwa Katibu wake. Mina alitumwa na Kaizari kuyatatua matatizo kati ya watu, na kuwavunja Wakristo nguvu zao. Kinyume cha mapenzi ya Kaizari alifanya kazi hiyo akiwatia moyo Wakristo kubaki imara katika imani yao na jambo hilo halikumpendeza Kaizari Maksimini.

Hermogene, alikuwa eparki, aliyezaliwa na wazazi wasio Wakristo. Alikuwa anafanya kazi ya serikali katika Ikulu. Basi Kaizari Maksimini alimtuma Aleksandria kumshauri Mina kuacha ukristo wake. Yeye alipoona miujiza iliyotendeka na Mina kwa neema ya Mungu, akaongoka, akabatizwa. Kaizari Maksimini akakasirika na kwa amri yake Mina, Eugrafo na Hermogene wakauawa, mwaka 235, tarehe 10 mwezi wa Desemba.

Wat. Mina na wenzako, mtuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

## **Mt. Melkiade, Baba Mtakatifu**, **314**.



Melkiade alizaliwa Afrika. Siku ya kuzaliwa kwake inakumbukwa tarehe 11 Januari katika Martirolojia ya Kanisa la Roma. Akawa Baba Mtakatifu kwa muda wa miaka mitatu, miezi saba na siku kumi na mbili, wakati Kanisa lilipopata amani baada ya karne tatu za dhiki.

Wakati wa utawala wake, uzushi wa Wadonati ukaanza. Kwa sababu ya amani iliyokuwepo maaskofu wa Afrika wakakusanyika huko Kartago na kumchagua mwandamizi askofu Mensurio, aliyefariki wakati wa dhiki. Wakamchagua Shemasi Sesiliani kwa kauli moja. Feliksi, Askofu wa Aptonge, akamwekea mikono na kumkalisha katika kiti cha uaskofu. Akampatia pia orodha ya mali ya Kanisa, ambayo Mensurio aliyowakabidhi wazee wa Kanisa. Miongoni mwao, wengine walitamani kushika mali hiyo. Wakafanya njama na mashemasi wawili Botrio na Seleusio, walioshindania kiti cha uaskofu. Kwa pamoja wakawaita maaskofu wa Numidia, ambao hawakuweza kufika kwenye Mtaguso wa Kartago. Chini ya utawala wa Donati, askofu wa Cassis-Nigris, mji wa Numidia, wakamwondoa Sesiliani na

kumweka mahali pake msomaji Majorino, wakidai kwamba uchaguzi wa Sesiliani ulikuwa batili. Ndiyo chanzo cha uzushi wa Wadonati uliodumu muda mrefu.

Kaisari Konstantino alipoingia kwa shangwe huko Roma, baada ya kumshinda Maksensi, Wadonati wakamwendea na kumwomba akubali uzushi wao. Konstantino akawajibu kwamba Baba Mtakatifu Melkiade atatoa hukumu. Basi, tarehe 2 Oktoba 313, Baba Mtakatifu akaita Sinodi ndogo huko Latrani, maaskofu 19 kutoka Gallica, yaani Ufaransa na Italia walihudhuria. Askofu Donati akafika mwenyewe ili kujitetea. Taarifa za Mtaguso wa Kartago na za mkutano wa Wadonati zilichunguzwa. Mwishoni maaskofu wote wakakubaliana kwa kauli moja. Melkiade akamtangaza Sesiliani kuwa hakuwa na hatia na kuwa askofu halali wa Jimbo la Kartago. Akawasamehe maaskofu waliowekwa wakfu na Majorino, lakini Donati mwenyewe akatengwa na Kanisa. Huyu akaendelea kushindana na viongozi wa Kanisa na kuleta maumivu mengi kati ya Wakristo.

Baba Mtakatifu Melkiade alikuwa wa kwanza kuuona Msalaba wa Kristo kuwa ishara ya utukufu na dalili ya ushindi. Wakati wa utawala wake, Wakristo wakaanza kuheshimiwa na kulindwa. Kwa hiyo alipata nafasi kusimamia Kanisa katika misingi imara. Alijaribu kudai kwamba mali ya Kanisa iliyochukuliwa wakati wa dhiki irudishwe. Aliwatuma mashemasi kuwahudumia Wakristo mahali pa kuabudu. Alianzisha kujenga makanisa huko Roma na alikuwa wa kwanza kuingia katika Kanisa Kuu la Roma, Kanisa la Mt. Yohane wa Laterani. Kanisa hilo lilijengwa kwenye kasri la Laterani, lililokuwa zawadi ya Kaizari Konstantino kwa Askofu Mkuu wa Roma.

Akawa Baba Mtakatifu kwa miaka mitatu tu. Hata hivyo Mt. Augustino anamsifu kwa maneno haya: “Mtu mwema sana! Mwana kweli wa amani! Baba kweli wa Wakristo!“

Mt. Melkiade, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

**Desemba 11**

Huko Pulka, Nigeria, Wakatoliki wanawakumbuka **Makatekista wawili** na **watu kadhaa** waliouawa katika kambi la Minawao kwa kombora lililotumwa na Boko Haram.

Wakoptiki wanakumbuka **Tokeo la Bikira Maria** huko Warraq al-Hadar, Aleksandria, Misri.[496]
Huko Ethiopia, Wakristo wanamkumbuka Mt. Abba **Hori**, mtawa.[497] Pia kumbukumbu ya Mt. **Ansah** wa El-Kifti, shahidi.[498]
Waorthodoksi wanawakumbuka **Miraks wa Misri**, mnamo 640, **Akepsimas** na **Aithalas**, wote Mashahidi.

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake. Amina.

## Mt. Miraks wa Misri, 640

Miraks alizaliwa huko Tanis, Misri, katika familia ya kikristo. Alilelewa katika imani, lakini kwa nguvu ya pepo alikanyaga msalaba. Akamwendea Mtawala wa Misri na akishika upanga mkononi mwake akajitangaza kuwa Mwislamu.
Wazazi wake walisikitika sana na bila kukoma walimwombea mwana wao. Neema ya Mungu ikamwingia moyoni mwake. Akatubu kweli kweli na kurudi nyumbani. Wazazi wake wakamshauri kukiri dhambi yake na kuonyesha kutubu kwake hadharani. Mt. Miraks alikubali. Akaenda tena mbele ya Mtawala wa Misri na kutangaza kwamba amekuwa tena Mkristo. Mtawala akaamuru ateswe na mwishoni akakatwa kichwa. Mwili wake ukatupwa baharini.[499]
Mt. Miraks, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

---

[496] *Coptic Synaxarium: 15 Kiahk.*
[497] *The Ethiopian Rite Missal, Abba Emmanuel & Abba Brendan Cogavin, 2002, uk 208. Ethiopian Synaxarium: Tahisas 02.*
[498] *Arabic-Jacobite Synaxarium*
[499] OCA *Lives of the Saints of Africa*

## Matokeo ya Bikira Maria, Warraq al-Hadar, 2009



Inaaminika kwamba Bikira Maria aliwatokea watu wengi, huko Warraq al-Hadar, Aleksandria, Misri, asubuhi, saa 7.00 hadi saa 10.00 usiku, siku ya Ijumaa, tarehe 11 Desemba. Mtu wa kwanza kumwona alikuwa Mwislamu mmoja. Alikuwa amekaa katika duka lake la kahawa wakati alipoona mwanga mkubwa kutoka kanisa la ki-koptiki. Yeye na wenzake waliona kwamba mwanga ukachukua umbo la mwanamke. Maria alionekana juu ya makuba ya Kanisa akitembea kati ya minara pacha ya Kanisa. Watu wote wa jirani waliona tokeo hilo la Maria. Kwa njia ya simu ya mkononi waliwaita marafiki zao wakichukua picha na kuwatumia kwao.

Kanisa la Koptiki la Aleksandria lilithibitisha tokeo hilo. Habari kutoka uaskofuni inasema kwamba: "Bikira Maria alitokea kwa mwanga katika Kanisa linaloitwa kwa jina lake huko Warraq al-Hadar, Giza, siku ya Ijumaa, tarehe 11 Desemba 2009, saa 7 usiku. Bikira Maria alitokea kwa urefu wake katika joho la mwanga, juu ya kuba la katikati ya Kanisa, akivaa gauni jeupe na mkanda wa rangi ya bluu. Alivijwa kwa taji kichwani, na juu yake msalaba wa kuba ulionekana. Misalaba ya makuba na minara ya kanisa iling'aa sana kwa mwanga. Bikira Maria alitembea kati ya makuba akielekea juu ya kilele cha mlango wa kanisa kati ya minara pacha. Majirani wote walimuona. Tokeo lilidumu tangu saa 7.00 hadi saa 10.00 usiku, siku ya Ijumaa. Lilirekodiwa kwa kamera na simu za mikononi. Mkutano mkubwa wa watu kama 3.000, kutoka jirani na maeneo ya karibu, walikusanyika katika mtaa mbele ya kanisa ili kuona tokeo.

Tangu siku ya Ijumaa, mkutano mkubwa waliokusanyika karibu na kanisa wanaona, nyakati mbalimbali za usiku, njiwa wa mwanga wakiruka juu, na hata nyota, iliyotokea gafla, ikisafiri mita 200 toka upande mmoja hadi upande mwingine wa mbingu, na kutoweka.

Mkutano mkubwa uliokusanyika karibu na kanisa wanaendelea kumwimbia na kumsifu Bikira Maria.
Hiyo ni baraka kubwa kwa Kanisa na kwa watu wote wa nchi ya Misri. Baraka na maombezi yake yawe kwa watu wote.“[500]
Bikira Maria, mtakatifu sana, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

[500] Habari hiyo iliandikwa na Anba Theodosius, Askofu wa Giza.

**Desemba 12**

Sisi Wakatoliki tunawakumbuka Wat. **Epimaki** na **Aleksanda**, wafiadini, huko Aleksandria, Misri, 250. Sikukuu ya Epimaki iliadhimishwa pamoja na sikukuu ya Mt. Gordiani, mfiadini, tarehe 10 Mei. Pamoja nao Wat. **Ammonaria**, bikira, **Merkuria**, **Dionisia**, na **Ammonaria** mwingine. Amonaria, bikira, alishinda mateso mengi makali sana, wakati wa utawala wa Kaizari Decius na mwishoni alikatwa kichwa. Hakimu, akiogopa kuaibishwa tena na wanawake wengine, wakishinda kila aina ya mateso, akaamuru wakatwe vichwa mara.[501]
Huko Ethiopia, Wakatoliki wanamkumbuka Mwenyeheri **Samueli wa Ethiopia**, mtawa wa Shirika la Dominiko. Baada ya kukaa miaka 40 jangwani, kama mababu wa zamani huko Misri, akatumia muda wake kuangalia roho za watu, kwa amri ya Malaika wake mlinzi na kujenga monasteri ya shirika lake. Malaika walikuwepo alipofariki, na wakasindikiza roho yake mbinguni, karne la XIV.[502]
Watawa wa Shirika la Ki-fransisko wanawakumbuka **Yohane Mbatizaji wa Ponti** na **Petro wa Hispania**, mashahidi huko Tripoli, mwaka 1653.
Huko Mutongo, Jamhuri ya ki-demokrasia ya Kongo, Wakatoliki wanamkumbuka **Konrad Ndyanabo Boneza**, padri wa Jimbo la Goma, aliyeuawa mwaka 1994.

Huko Misri, Wakoptiki wanawakumbuka Wat. **Harouadji**, **Anania** na **Khouzi**, wafiadini. Pia wanaadhimisha kumbukumbu ya **Kutabarukiwa Kanisa la Mt. Yakobo *the Mangle***.[503] Na huko Panopolis, Misri, kumbukumbu za Wat. **Zakaria** na **Kassio**, wafiadini. Pia kumbukumbu ya Wat. **Eulogi** na **Arseni**, watawa wa mkoa wa Akhmin.[504]
Huko Minya, Misri, Wakoptiki wanawakumbuka **Imrad Kamal Sadiq** (49) na mwana wake **Daudi** (21) waliouawa mwaka 2018.

---

[501] *Martyrologium Romanum,* ed. 2005.
[502] *Les petits Bollandistes*
[503] *Coptic Synaxarium: 16 Kiahk.*
[504] *Arabic-Jacobite Synaxarium*

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake. Amina.

## Wat. Epimaki, Aleksanda na wenzao, Mashahidi, 250

Wakati wa dhiki iliyosababisha na Kaizari Desio, huko Aleksandria, Misri, mnamo mwaka 250, Wakristo wawili Epimaki na Aleksanda wakakamatwa. Bila kuficha wakakiri kwamba ni Wakristo. Basi wakafungwa kwa minyororo, wakatiwa gerezani na kubaki huko muda mrefu, wakivumilia mateso makali. Walipodumu katika kukiri imani yao, wakapigwa na marungu, ubavuni mwao ukachanwa na viopoo na mwishoni walichomwa moto hadi kufa.

Mt. Dionisi, askofu wa Aleksandria, alishuhudia baadhi ya mateso yao. Anatusimulia kwamba siku ile na mahali pale waliteswa pia wanawake wanne. Wa kwanza, Amonaria, bikira, aliyeishi maisha matakatifu, bila lawama yoyote, akavumilia mateso makali sana, bila kufungua kinywa chake, isipokuwa kutangaza kwamba hakuna ujanja wala uwezo utakaomshinda. Akashika ahadi yake, hadi mwisho akakatwa kichwa. Wa pili, Merkuria, alikuwa mwanamke wa kuheshimiwa sana kwa sababu ya umri wake na fadhila zake. Wa tatu, Dionisia, ingawa alikuwa mama wa watoto wengi, aliwakabidhi wote kwa furaha kwa Mungu, akichagua kumpenda Mungu kuliko kufuata mambo yote ya dunia. “*Upendo una nguvu kama mauti*.“ Wim 8:6. Wa nne alikuwa Amonaria mwingine.

Hakimu alipotahayarishwa kwa ujasiri na ushupavu wa mwanamke wa kwanza, na akiwaona wanawake wengine wenye sura ya ushujaa, aliamuru hawa wanawake wengine watatu kukatwa vichwa bila kuteswa.

Watakatifu Epimaki, Aleksanda na wenzenu, mtuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

## Wat. Eulogi na Arseni, watawa na mashahidi

Wakoptiki wanawakumbuka siku ya leo Eulogi na Arseni, Wakristo kutoka nchi ya Siria. Watakatifu hao walikaa katika monasteri ya

Deir-el-Hadid, katika mkoa wa Akhmim. Bwana Yesu alipowaita ili wafie dini wakamwendea Gavana na kukiri mbele yake kwamba hao ni Wakristo. Akawaambia: “Fukuzieni miungu ubani na ninyi mtapata mali na cheo cha juu“. Watakatifu hao, mashujaa katika imani, wakamjibu: “Sasa ni kwa mara ya tatu tunakaa mbele ya baraza. Tulimkiri Yesu kuwa Kristo. Tuliteswa vibaya lakini tulibaki katika imani yetu. Sisi tu Wasiria, tuliacha nchi yetu na kukimbilia nchi ya Misri, ili tusimkane Kristo. Fanya kama utakavyo.“ Gavana akakasirika, aliamuru wafungwe jiwe kubwa shingoni mwao na kuwaning’iniza kwenye Ngome vichwa chini na miguu juu. Baadaye wakafungwa jiwe miguuni mwao na kutupwa mtoni. Lakini kwa uweza wa Bwana Yesu, mawe yakaelea juu ya maji na watakatifu wakakaa juu yake. Wakafika wazima pwani. Gavana akakasirika sana na kuamuru kuwaning’iniza vichwa chini na kuwachinja kama kondoo.

Ndiyo maana Kristo akawajalia taji saba: Tatu kwa sababu mara tatu wameletwa barazani na walimkiri Yesu kuwa Kristo na kuteswa kwa ajili ya Jina lake; La nne kwa sababu ya mateso waliyovumilia huko katika Ngome; la tano kwa sababu ya matatizo waliyopata katika mto; La sita kwa sababu walichinjwa kama kondoo; Na la saba kwa sababu walikuwa wageni. Malaika wakazichukua roho zao katika ufalme wa mbinguni, karibu na Yesu Kristo, mkuu wa enzi.

Miujiza mingi ikafanyika kwa njia ya miili iliyowekwa katika kanisa lililojengwa kwa heshima yao. Mojawapo ilikuwa hivi: Palikuwa mchungaji aliyekaa juu ya mwinuko mdogo kaskazini ya monasteri. Alikuwa anaimba na kupiga filimbi kama wanavyofanya wachungaji. Ghafla akasikia mkono wa mtu uliomwinua na kumtupa katika mto, kwa sababu mto ulikuwa karibu. Mara mamba akatokea na kufungua kinywa ili kumumeza. Mchungaji alifikiri kwamba tatizo hilo limemtokea kwa sababu alikosa heshima kwa kanisa la watakatifu wawili. Akalia na kuwaomba watakatifu hawa wamsaidie. Mamba aliposikia jina la Bwana na majina ya watakatifu wawili akamwacha mchungaji na kuzama majini. Huyu akarudi pwani akitetemeka sana. Akamshukuru Mungu na kuapa kwamba kamwe hatapiga tena filimbi na kucheza bila heshima. Akaamuru kuacha desturi zake mbaya.

Siku moja mwanamume mmoja njiani akakutana na mwanamke aliyekuwa anaenda monasteri ya watakatifu wawili. Akamshika na

kumlaza chini ili amtendee kufuata shauku ya tamaa zake. Mara mbwamwitu wawili wakatokea na walitaka kumshambulia. Akalia kwa sauti kubwa: "Mungu wa mashahidi, uniokoe! Kwa mastahili ya mateso mliovumilia kwa jina la Yesu, watakatifu msiniache!" Akaapa kwamba kamwe hatagusa mwanamke ambaye si mke wake hadi mwisho wa maisha yake. Na mara mbwa mwitu wakatoroka kama kulikuwepo mtu nyuma aliyewafukuza. Mwanamume huyu akaingia kanisani, akakiri kosa lake, akamshukuru Mungu, akalisifu Jina lake na kubaki kanisani kuwa mtumishi wake, hadi mwisho wa maisha yake.

Wat. Eulogi na Arseni, mtuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

## Mapadri Yohane Mbatizaji na Petro, Mashahidi Tripoli, 1653

Padri Yohane alizaliwa Italia. Kama mtawa wa Mt. Fransisko alimwomba Mungu mara nyingi neema ya kueneza Injili kati ya Waislamu na kumfia Yesu. Siku moja Kiongozi alitafuta wamisionari kwenda Tripoli kuwahudumia watumwa Wakristo. Akajitokeza. Ingawa afya yake ilikuwa dhaifu na watawa wenzake walimshauri asiende, alikubaliwa. Huko Tripoli akapokelewa kwa furaha na mtawa mwenzake aliyemtangulia miaka kadhaa.

Upendo wake kwa watumwa na wivu katika sala zake, vikamvutia urafiki siyo kwa watumwa tu na hata ya Waislamu pia. Akapenda kufanya zaidi, yaani kuwahubiria Waislamu Injili ya Yesu, akiona jinsi Waislamu walivyokaa katika giza la udanganyifu. Kwa shauri la mwenzake akaenda Hispania kutafuta ruhusa ya pekee ya kiongozi wake. Alipofika Hispania hakumkuta kwa sababu kiongozi wake alikwisha enda Moroko. Basi Yohane Mbatizaji akapanda meli na kufika Aljeria. Kutoka mji Aljeria akaanza safari kwa miguu hadi Tripoli umbali wa kms 600. Alisafiri bila hofu ya hatari za njiani, wanyama wakali, mchanga wenye moto wa jangwa, dhuluma za wenyeji. Njiani akawahudumia watumwa Wakristo na kuwatia moyo.

Alipofika Tripoli akawakuta mapadri waliofungwa gerezani na kutiwa minyonyoro ya chuma, watawa wawili wenzake: Padri Luka wa Oriza na Marko wa Sisilia, pamoja na mapadri wawili wa jimbo. Kwa

maneno na ukarimu wake aliwatia moyo. Zaidi akampendekeza kwamba ashike nafasi ya Padri Luka ili aweze kurudi nyumbani mwake. Lakini huyu alikataakataa. Padri Yohane akaungama kwake kwa kulialia machozi mengi. Akaadhimisha misa mbele ya waamini wengi, na kukaa pamoja nao siku nzima, akiwahudumia. Usiku uliofuata akapiga magoti mbele ya picha ya Mwokozi na kutafakari hadi asubuhi. Akaungama tena dhambi zake na kuadhimisha misa. Kwa mara ya mwisho akawahutubia watumwa na akaondoka.

Gavana wa Tripoli, Osman Bassa, akamwamuru kuondoka katika mji huo kwa sababu mapadri walikuwa wa kutosha. Yohane akamwendea kumwomba ruhusa kwenda Malta. Gavana, ambaye alikuwa ameasi dini yake ya kikristo, akampokea kwa ukarimu na kukubali ombi lake. Lakini Yohane, akiwaka na wivu wa wokovu wa roho za watu, akamwambia kwamba hawezi kuondoka akiwa na uchungu, kwa sababu anamwacha katika utumwa wa Shetani. Akamsihi kwa nguvu kurudi katika dini yake. Maneno yake yakamchoma Gavana kiasi kwamba akatoroka asimsikilize tena. Padri Yohane akamfuata na kuendelea kumsihi atubu, aidharau mali ya dunia ili apate heri ya mbinguni. Ndipo wasaliti, walioguswa na maneno yake bila kutubu, wakamshika na kumwambia aondoke haraka. Mtume akakataa, akamwendea wakili wa Bassa na maafisa Waislamu, akiwasihi kuikana dini ya Mohammadi, kutanasari na kupokea ubatizo.

Wakristo wabaya waishio Tripoli na walio waovu kuliko Waislamu wakaanza kusaga meno na kupiga kelele: “Auawe, mtawa huyu anayehubiri kwa nguvu dhidi ya uislamu“. Ndipo Bassa akamwita Padri Yohane na akaamuru aletwe mbele ya Baraza lake. Wakati ule kiatu kimoja kikakatika. Wakamwambia kukichukua, lakini akajibu kwamba hakihitaji tena kwa sababu sasa anatembea njiani kwenda mbinguni. Alipofika mbele ya Gavana, walijaribu ayakane maneno yote aliyosema dhidi ya Muhammadi. Lakini mwungama dini akachukua nafasi kuwaambia kwamba bila kumwamini Yesu hakuna wokovu. Akazidisha: “Napenda zaidi kuingia katika uzima wa milele kuliko kuungua pamoja na nabii wa uongo katika miali ya moto wa milele.“

Akiwa na hasira, Gavana Bassa akaamuru kwamba auawe na mwili wake utupwe katika moto. Ndipo Waislamu wakamrukia, wakampigapiga na kumtemea mate. Wakamburuza nje ya mji Tripoli,

na baada ya kumchoma na mikuki mara mbili, akampigilia msimari kichwani. Shahidi akafariki akinyong'onya mara tatu: "Bwana, mikononi mwako naiweka roho yangu". Ilikuwa tarehe 12 Desemba, 1653.

Mwili wa Padri Yohane ukafungwa katika nguzo na kuwekwa kati ya kimbwi. Wakawasha moto lakini mvua ya ajabu ikawafukuza wote. Kesho yake wakawasha tena kimbwi, mwili wa Shahidi ukateketezwa na majivu yake kutupwa baharini. Usiku uliofuata, pale pale mwili wake ulipounguzwa, Padri Yohane akawatokea watu, kichwa chake kikizunguka na duara ya mwanga, mikono na macho yakielekea mbinguni na kinywani mwake msalaba wenye kung'aa sana. Waislamu kadhaa wakashuhudia tokeo hilo. Na Mwislamu yule aliyechukua viatu vyake aliona mahali alipoviokota mianga miwili ya ajabu. Miujiza mingi ikafanyika hasa kwa watumwa Wakristo waliokuwa wanamwomba Shahidi wao. Wakaimarishwa katika imani yao.

Pamoja na Padri Yohane tukumbuke pia Padri Petro wa Hispania aliyetumwa Afrika kuwahubiria Waislamu Injili, na wale wote walioteswa na kufariki mikononi mwa Waislamu, ambao majina yao yamepotea.[505]

Padri Yohane Mbatizaji na wengine mashahidi, mtuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

---

505 La Palmier Seraphique, XII, 176-183

**Desemba 13**

Huko Mauretania na Italia, Wakristo wanamkumbuka Mtakatifu **Antioko** wa Sulcis, Sardinia. Alipelekwa uhamishoni kwenye migodi ya kisiwa cha Sardinia na kuuawa huko kwa imani yake.[506]

Huko Misri Wakoptiki wanamkumbuka **Eliya**, mwanakoriti.[507]
Huko Ethiopia, Waorthodoksi Tewahedo, Ethiopia, wanawakumbuka Abba **'Os**, na **mabikira**, pamoja na **Yakobo**, **Zakaria**, **Simoni**, **Theodora** na **Theofana**.[508]
Waorthodoksi wanamkumbuka Mt. **Aresio**, mtawa, Misri.

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake. Amina.

## Mt. Eliya, mwanakoriti

Mt. Huyu anaitwa Eliya wa mlima wa Bichouaou, Djebel el-Labkhah. Wazazi wake walikuwa wa mji Ishkim, Mashariki mwa mto. Alipokuwa kijana akaanza kuwaza kuvuka mto na kwenda Mlima Chamah, Magharibi mwa mto. Akaingia katika monasteri moja na kuanza kujikania kiasi kwamba akisoma Maandiko Mtakatifu anayatimiza anayosoma. Akaanza kukariri vitabu thelathini na kurudia maneno hayo moyoni mwake. Alipokuwa anasoma asubuhi na mapema, kufuatana na desturi ya watawa, hakuacha kusoma maneno yale, hadi aliyakariri moyoni mwake. Ndipo alienda kufanya kazi ya mikono. Mara nyingi, alisema Mfuasi wake, alisali zaburi mia moja na hamsini akiinua mikono yake kuelekea mbinguni. Alikuwa anafunga na kufanya toba. Hasa alihimiza roho yake kutafakari heri nane za Injili ya Mathayo. Alizitamka zote mfululizo na kujenga maisha yake juu ya heri.
"*Heri walio maskini wa roho, maana ufalme wa mbinguni ni wao*" Mt 5:3. Heri hiyo aliitimiza kwa maneno na matendo yake.

---

506 Antioko waliweza kutokea Mauratiania (Aljeria siku hizi) au Kapadokia.
507 *Arabic-Jacobite Synaxarium*
508 *Ethiopian Synaxarium: Tahsas 04.*

Akapata furaha yake katika heri ya pili: "*Heri wenye huzuni, maana hao watafarijika*" Mt 5:4. Baba huyu, aliyekuwa malaika duniani, akinyosha mikono yake ili kusali, alikuwa analialia, akimwaga machozi yake kama mvua, hata wafuasi wake walikuwa wanashangaa. Kila wakati alipokuwa anasoma, akitamka jina la Bwana wetu Yesu Kristo, mara alisujudia hata nchini. Wafuasi wake wanasimulia kwamba hawakumwona akicheka wala kutabasamu. Bali daima aliwaambia: "Ndugu zangu, mniombee, labda Bwana ataniokoa na kunitoa kutoka gereza la ulimwengu huu unaopita". Katika huzuni na hofu yake ya siku atakapomkuta Mungu, mwili wake ulikuwa umeyeyuka na kufanana na maiti.
Akatafakari heri ya tatu: "*Heri wenye upole, maana hao watairithi nchi*". Mt 5:5. Mtu akimdharau, kumtukana na kusema maneno mabaya juu yake, Mtakatifu huyu alimpenda na kumwombea. Alikuwa kama kondoo au kama njiwa ya amani.
Kuhusu heri ya nne: "*Heri wenye njaa na kiu ya haki, maana hao watashibishwa*" Mt 5.6. Mtakatifu huyu alikuwa anafunga kila wakati hadi mwisho wa maisha yake. Mara kwa mara alifunga wiki nzima na akila, hali hadi kushiba. Siku moja alitamani siki na kabeji, basi akabaki miaka mitatu bila kuvigusa. Siku nyingine alitamani sana divai. Akachukua shayiri, akailowesha katika maji na kuiacha hadi rangi ikawa nyekundu na kunuka. Ndipo akasema: "Roho yangu, maskini, bila matumaini, yenye huzuni, ndiyo inayotamani!"
Vivyo hivyo alijishughulikisha na heri ya tano: "*Heri wenye rehema, maana hao watapata rehema*" Mt 5:7. Mtu akimwomba sadaka, katika upendo wake, angalimpatia hata mlango wa nyumba yake angaliweza kuling'oa. Mara nyingi mtu akimwomba amsaidie alitoa hata nguo aliyovaa na kumpatia. Aliwapa vitabu alivyosoma kwa sababu alivijua kwa moyo. Akipokea nafaka aliiwagawia maskini na wahitaji.
Baadaye akashughulikia heri ya sita: "*Heri wenye moyo safi, maana hao watamwona Mungu.*" Mt 5:8. Mtakatifu huyu alikuwa na moyo safi. Unyenyekevu na upendo wake ulikuwa kiasi kwamba, wakati alipokuwa anavunja kufunga kwake, mfuasi wake akifika, ni yeye alikuwa analowesha mkate, na kuuweka mbele yake – kwa sababu walipika mkate mara moja kwa mwaka – Vivyo hiyo kuhusu mboga na

mambo mengine. Ilikuwa ngumu kwa wafuasi wake kulikubali jambo hilo, lakini walifurahia moyo wake kwa njia hiyo.
Kuhusu heri ya saba: "*Heri wapatanishi, maana hao wataitwa wana wa Mungu*" Mt 5:9. Mtakatifu huyu alifanya kazi kwa nguvu zake zote kueneza amani kati ya wote. Akisikia kwamba wawili walikuwa wanabishana mara akatumia nguvu zake kuwapatanisha. Akimwona mtawa anazungumza juu ya mwingine alikuwa anashangaa na kusema: "Utulivu ni mzuri sana, lakini bora kumsifu Mungu. Maskini we! Kwa nini unazungumza kuhusu watu, tafuta wokovu wako, kwa sababu Shetani anapanda maovu. Tutamshinda kwa kutenda mema na unyenyekevu. Tukimbie kiburi, na hasa tupendane."
Alipofika heri ya nane: "*Heri wenye kuudhiwa kwa ajili ya haki, maana ufalme wa mbinguni ni wao*" Mt 5:10. Ndiyo heri aliyotenda hasa. Kila wakati alipokaa katika amani na utulivu, alikuwa anaondoka, kwa sababu hakutaka kujipumzisha, lakini daima alipenda amani. Alikuwa anaenda mlimani mwa Chamah na kukaa kati ya mifupa ya wafu iliyokuwa katika hali ya kuoza. Alijilazimisha kufunga, kukesha usiku, kukaa wima, kusujudu, kutesa mwili wake kwa hiari, n.k. Yote hayo yalikuwa mateso ya hiari ili atimize Neno la Bwana: "*Ufalme wa Mungu upatikana kwa nguvu, nao wenye nguvu wauteka*" Mt 11:12.
Abba Eliya alikuwa na wafuasi wawili, Abba Yohane na Abba Yousab. Kuhusu mfuasi wake Abba Yohane, hakuweza kukaa kati ya mifupa iliyokuwa katika hali ya kuoza na kunuka. Kila mara ilimbidi kutapika. Kwa hiyo aliepa kukaa karibu na Abba Eliya kwa sababu harufu ya waliokufa ilimsumbua sana. Mfuasi wake Yousab alipofariki, alikuwa na umri wa miaka thelathini na mitatu tu; Abba Eliya alilia sana na kusema: "Tayarisheni kaburi kubwa la kutosha kuiweka miili miwili", ili atakapofariki wamzike pamoja naye. Wote walihuzunika kwa sababu ya kutengana, lakini walifurahi kwa sababu ya utukufu wa ndugu yao Yousab aliopata karibu na Bwana Yesu Kristo.
Abba Eliya aliendelea kujitesa. Watu walimletea kijana mwenye pepo. Mtakatifu alipomtazama tu, mara pepo akatoka. Wagonjwa wakimfikia walipona mara walipomwona. Alipozeeka alimwomba Bwana amtulizie mateso ya kifo. Alitetemeka na machozi yake yalimwagika chini. Kwa hiyo mfuasi wake Abba Yohane alikuwa analia pamoja naye kwa maombolezo na kwa kuugua. Alipomsihi Bwana, basi Kristo, pamoja

na malaika wake, wakamfikia. Akasimama na kumsujudia mbele yake. Alipomwomba kuaga dunia hii akafunga kinywa na akafariki. Malaika wakaifunika roho yake kwa vitambaa vya utukufu.
Mt. Eliya, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

**Desemba 14**

Sisi Wakatoliki tunawakumbuka Wat. **Heroni**, **Arseni**, **Isidori** na kijana **Dioskoro**, mtoto wa miaka 12, wote wafiadini huko Aleksandria, Misri. Baada ya kuteswa kila aina ya mateso makali, hakimu akiona kwamba wanaendelea katika ujasiri wao, akaamua watupwe motoni. Wakafa mashahidi. Lakini, Dioskoro, baada ya kupigwa viboko, akaachiliwa huru, kwa faraja kubwa ya Wakristo.[509]

Huko Misri, Wakoptiki wanawakumbuka Wat. **Heraklas**, mfiadini na **Filemoni**, mkaa pweke, padre na mwungama dini.[510] Pia kumbukumbu za Wat. **Apolonio**, **Filemoni**, **Ariani** na **Theotiko**, wafiadini, Aleksandria, Misri, 287.
Huko Ethiopia, Wakristo wanawakumbuka **Eugenia**, mfiadini (na **Filipo**, baba wake Eugenia), mfiadini; Mt. **Viktori** wa mji wa Shaw (Wilaya ya Assiut), mfiadini. Wakatoliki wanamkumbuka pia Abba **Gabra-Nazrawi** wa Debra-Tsegada, mtangazaji wa Injili nchi ya Tigray. Waorthodoksi Tewahedo, Ethiopia, wanamkumbuka Mt. **Isidori**, mfiadini.[511]
Waorthodoksi wanawakumbuka Mt. **Hipasio** na **watawa wenzake** 36 wa Theba, Misri, wote mashahidi.

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake. Amina.

## Mt. Theotiko na wenzake, wafiadini, 287

Mashahidi hawa Theotiko, Filemoni, Apolonio, Ariani waliteswa kwa ajili ya imani yao huko Misri, katika mji wa Antinoe, wakati wa utawala wa Kaizari Dioklesiani (284-305). Ariani, hadi kuongoka

[509] *Martyrologium Romanum,* ed. 2005.
[510] *Coptic Synaxarium: 18 Kiahk.*
[511] *The Ethiopian Rite Missal, Abba Emmanuel & Abba Brendan Cogavin, 2002, uk 209. Ethiopian Synaxarium: Tahisas 05.* Katika *Roman Martirology*, Mt. Eugenia ana sikukuu yake tarehe 25 Desemba.

kumwamini Kristo, alikuwa mtesaji wa Wakristo, miongoni mwao Apolonio na Filemoni.
Apolonio aliogopa mateso, kwa hiyo alimwomba mpagani, mwenye muziki, kubadilishana nguo na kuitolea miungu ya uongo sadaka. Lakini, bila kutegemea, Filemoni akakiri mbele ya wapagani wote kwamba yeye ni Mkristo. Ndipo Apolonio akatubu na kumkiri Kristo. Baada ya kuteswa, wote wawili waliuawa. Mwili wa Filemoni ukafungwa juu ya mti wa mzeituni na ukapigwa kwa mishale. Mshale mmoja akampiga Ariani katika jicho lake na kuliharibu kabisa. Jicho lake likapona alipopaka udongo kutoka kaburi la Filemoni. Akatubu na kumkiri Yesu kuwa Kristo. Akabatizwa yeye na familia yake yote na walinzi wake. Kwa sababu ya upendo wa Kristo kwao, wakaenda kwa hiari kuteswa na wakahukumiwa kufa.[512] Theotiko alikuwa na umri zaidi kuliko walinzi wengine. Mashahidi Filemoni na Apollonio wamefariki tarehe 16 Machi, 286 na Theotiko na wenzake tarehe 4 Machi, 287.
Mt. Theotiko na wenzako, mtuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

## Mt. Viktori, mfiadini

Leo, Wakristo wa Ethiopia wanamkumbuka Mt. Viktori wa mji wa Shaw, mkoani mwa Assiut. Baba yake aliitwa Marmar na mama yake Martha. Walikuwa wenye haki mbele ya Mungu, lakini hawakupata mtoto, kwa hiyo waliomba bila kukoma na kuwasaidia maskini kwa sadaka. Siku moja Mungu akasikia ombi lao na mwanamke akapata mimba ya Viktori. Akajifungua mwezi wa Juni. Akamlelea katika hofu ya Mungu na imani. Alipokuwa na umri wa miaka ishirini, baba yake alimpeleka kwa Kaizari. Kaizari akamteua kuwa Hakimu badala ya baba yake mzee.
Baada ya siku chache amri ya Kaizari Dioklesiani ikatangazwa. Kaizari akaamuru Gavana wa Ansena kwamba kuwaua Wakristo wote wasioiabudu miungu wa uongo. Gavana akafika katika mji wa Shaw akiwatafuta Wakristo. Watu fulani wakampasha habari kwamba Viktori anamwabudu Kristo. Gavana akaamuru aletwe mbele yake. Gavana akajaribu kulazimisha Viktori kuiabudu miungu wa uongo. Alipokataa

[512] Rejea tarehe 4 Machi

basi Gavana akaamuru afungwe kwa minyororo na kutupwa gerezani. Alipokuwa akisali, Mikaeli, malaika wa Bwana, akamfikia na kumpeleka mbinguni. Mlinzi wa gereza alipokosa kumwona akahangaika sana. Baada ya siku tatu akampata tena na kumpeleka kwa Gavana na yeye akampeleka kwa Kaizari. Dioklesiani akajaribu kulazimisha kuiabudu miungu wa uongo. Aliposhindwa na kuchoka akamtuma kwa Gavana Eutychiano akamwambia: "Nimemtuma kwako. Akiitolea miungu sadaka, awe huru, kama sivyo usiogope kumwua".
Askari wakamfunga miguu na mikono yake na kumwingizia chuma kinywani mwake. Gavana akawaamuru kumweka katika meli mahali pa kuwekea mizigo. Alipokuwa pale malaika wa Bwana akashuka na kumweka huru. Baadaye wakamleta tena mbele ya Gavana. Mtakatifu akakaa kimya mbele yake, kama mbele ya Kaizari. Gavana akakasirika na kuamuru ateswe vibaya. Wakamfunga tena kwa minyororo na kumtupa gerezani. Alipokuwa gerezani Mkombozi akamtokea katika gari la nuru na kufunga agano naye. Tangu siku ile Mtakatifu akatenda maajabu na miujiza mingi na kuwaponya wagonjwa wote.
Gavana akakasirika sana aliposikia habari hizo. Akawaamuru askari wake kumleta mbele yake. Akamtenda vema na kumsihi aiabudu miungu. Lakini Mtakatifu akamshutumu na kuwalaani miungu ya uongo. Mara akaamuru afungwe kwa mkia wa farasi na kumkokota kwa siku moja. Baadaye wakamtupa katika tanuru la kupasha maji moto ya kuogea, ndipo akamaliza mashindano yake. Hawakuweza kuuondoa mwili wake kutoka tanuru, lakini Wakristo wakauchukua, wakampaka na manukato na kuuzinga sanda ya kitani safi. Wakajenga kanisa kwa heshima ya jina lake.[513]
Mt. Viktori, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

[513] *Ethiopian synaxarium*, tahisas 05

**Desemba 15**

Sisi Wakatoliki tunamkumbuka Mt. **Valeriani**, askofu wa Abbenza Afrika ya Kaskazini na mfiadini. Alipokuwa na umri wa miaka themanini, wakati wa dhiki iliyosababishwa na Genserik, Mfalme wa Waharabu (*Vandals*), aliamriwa mara nyingi kutoa vyombo vitakatifu vya Kanisa. Daima alikataa. Kwa hiyo amri ikatolewa apelekwe nje ya mji, na watu wote wasimpokee nyumbani au viwanjani mwao. Basi akabaki akikaa barabarani na mitaani hadi akafariki akiitetea dini ya kikatoliki.[514]

Huko Misri, kumbukumbu ya Mt. **Eusebio**, Askofu wa Vercelli, kuhamishwa Theba.

Huko Aljeria, kumbukumbu ya Wat. **Faustino**, **Lusio**, **Kandido**, **Cheliano**, **Marko**, **Januari** na **Fortunati**, wafiadini, Aljeria.[515]

Huko Uvira, Jamhuri ya ki-demokrasia ya Kongo, Wakatoliki wanamkumbuka **Beaudouin Ntemaya**, aliyeuawa na waasi, mwaka 2008.

Huko Misri, Wakoptiki wanamkumbuka Mt. **Yohane**, askofu wa El-Borollos. Ndiye yeye aliyekusanya maisha ya Watakatifu (*Synaxarium*).[516]

Huko Ethiopia, Wakristo wanamkumbuka Mt. Abba **Abrahamu Msiria**, Patriarka, askofu wa 61 wa Aleksandria.[517]

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake. Amina.

## Mt. Yohane, askofu wa El-Borollos

Wakoptiki wanamkumbuka siku ya leo Mt. Yohane wa El-Borollos. Alizaliwa katika familia yenye mali na ukoo wa makuhani. Wazazi

[514] *Martyrologium Romanum,* ed. 2005.

[515] *Roman Martyrology,* ed. 1956. Pamoja nao Makrosa.

[516] *Coptic Synaxarium: 19 Kiahk.*

[517] *The Ethiopian Rite Missal, Abba Emmanuel & Abba Brendan Cogavin, 2002, uk 210. Ethiopian Synaxarium: Tahisas 06.*

wake walikuwa watu wenye upendo, wakiwatolea maskini sadaka kwa moyo. Walipofariki, Yohane alirithi mali yao. Akawajengea wageni hosteli. Akawakusanya wagonjwa na kuwahudumia na kuwajalia kila kitu walichohitaji.
Siku moja mtawa akamtembelea na kuona matendo yake mema, akamsifu. Alisifu pia mbele yake utawa. Mtakatifu akavutwa na utawa na akautamani sana moyoni mwake. Baada ya mtawa kuondoka, Mtakatifu akawagawia maskini mali yake na akaenda jangwani mwa Shete. Akawa mtawa chini ya uongozi wa Abate Danieli.
Yohane akajulikana kwa ajili ya wivu kwa Mungu na kwa majikanio makubwa. Aliishi peke yake katika jengo la pembeni. Shetani na jeshi lake hawakufurahia matendo yake mema, siku moja wakamfikia na kumpiga vibaya. Yohane alikuwa mgonjwa kwa siku nyingi, lakini Bwana Yesu Kristo akamponya. Akapata tena nguvu zake na kumshinda Shetani.
Mungu akamwita awe askofu wa Borollos. Wakati ule kulikuwa na uzushi katika nchi yake. Akatumia muda wake na nguvu zake kuziondoa na kuwaongoa wazushi kwa imani ya kweli. Pia, mtawa kutoka mkoa wa Misri Kusini, akadai kwamba anaweza kuwaambia watu mambo ambayo Malaika Mkuu Mikaeli aliyomfunulia. Akawadanganya wengi kwa udanganyifu wake. Yohane akatambua kwamba matendo ya mtawa huyo yalikuwa kazi ya Shetani. Akaamuru kwamba mtawa apigwe hadi aungame madhambi yake na akamfukuza nje ya nchi.
Mwingine akadai kwamba nabii Habakuki alimfunulia mambo yaliyofichika. Kwa hiyo alifuatwa na wafuasi wengi. Yohane akamfukuza pia nje ya nchi baada ya kufunua udanganyifu wake. Pia akavichoma vitabu vingi vya mafundisho ya upotovu.
Palikuwa katika mji wake padri mmoja aliyefanya kazi ya unajimu na uchawi. Kazi hiyo ilizalisha fedha nyingi. Askofu akafunuliwa jambo hilo na Mungu na kuambiwa kumzuia kuadhimisha misa kwa sababu Mungu alisema: “Nitatakatifuzwa na wale wanaokaa karibu nami“. Siku moja askofu alipokuwa kanisani alimwambia padri: “Hutaadhimisha misa na hutaingia tena kanisani kwa sababu wewe ni najisi.“ Padri alimjibu: “Yote unayosema juu yangu ni uongo“. Akaadhimisha misa. Ulipofika wakati wa kugeuza mkate na divai watu

wawili wabaya na weusi wakaonekana. Mmoja akashika mkono wake wa kulia na mmoja mkono wake wa kushoto, na wote wakazama katika ardhi. Hofu ikawashika waamini wote. Padri mwingine akaingia na kumaliza ibada ya misa.

Kila wakati alipoenda kanisani kuadhimisha ibada takatifu, uso na mwili wake ulikuwa na rangi nyekundu sana, kama alitoka kwenye tanuru. Akiadhimisha sadaka ya misa machozi yake yalikuwa yanadondoka kama mvua, kwa sababu alikuwa anaviona viumbe vya ki-mbingu altareni. Mara tatu alipofanya ishara ya msalaba juu ya kikombe, wakati wa mageuzo, na kukishika kwa vidole vyake, alisikia kwamba kikombe kilikuwa na moto sana. Tena, zamani zake, Wakristo fulani walikuwa wanapokea Komunio mara ishirini kwa siku na walikuwa na kiburi sana. Mtakatifu akawakemea, lakini kwa sababu hawakumsikiliza na kurekebisha matendo yao, akawatenga na Kanisa na kuwazuia kushirikiana na jumuiya ya Wakristo. Walipokataa kutii alimwomba Mungu ili moto kutoka mbinguni ushuke na kuunguza kiongozi wao. Hofu ikawaangukia wengine, wote wakatubu.

Bwana alipoamua kumpumzisha na kazi yake, akawatuma kwake Mt. Antoni na Makari kumwambia kwamba siku ya kuaga dunia iko karibu. Akawaita waamini wake na kuwaachia wosia. Akafariki kwa amani.

Mt. Yohane wa El-Borollos, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

## **Mtu wa Mungu Baudouin Ntemeya, 2008**.

Alikuwa na umri wa miaka 52 Beaudouin alipouawa. Mwenyeji wa Goma, Kivu Kaskazini, alikuwa anafanya kazi ya ki-jamii huko Rutshuru, eneo lililotawaliwa na waasi. Alifanya kazi tangu miaka miwili, pamoja na ASVI, shirika kutoka Italia. Kazi yake ilikuwa kuwasaidia walimu na wanafunzi waliokuwa wanaishi katika eneo hilo.

Asubuhi ya tarehe 15 Desemba 2008, alitoka Rutshuru, kungali bado giza, pamoja na Deogratia, 57, dreva tangu mwaka 2003, katika shirika la ASVI.  Wote wawili walijua maeneo hayo, kwa sababu walizoea kuwaletea wenyeji msaada na matumaini. Lengo la safari yao lilikuwa kuhakikisha mashule mengapi yaliweza kufunguliwa baada ya mashindano kati ya Jeshi la Jamhuri ya ki-demokrasia ya Kongo na

Waasi. Walipokaribia mahali walipotaka kufika wakasimamishwa na askari wanne ambao walianza kupiga rizasi. Deogratia akajeruhiwa mkononi na tumboni, aliweza kuendesha gari kilomita moja zaidi hadi gari liliposimama. Baudouin, akajeruhiwa pia na risasi, akafariki kabla ya kufika hospitalini. Akaacha mke na watoto sita.[518]
Baudouin na mwenzako, mtuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

[518] Rejea Fr. Neno Contra,, Louis Kalonji, *African Lay Martyrs*, New People Media Centre, 2009, uk. 155.

**Desemba 16**

Sisi Wakatoliki tunawakumbuka **Mabikira wengi** waliofia dini, wakati wa dhiki iliyosababishwa na Hunnerik, Mfalme wa Waharabu (*Vandals*). Waliteswa vibaya kwa kufungwa mizigo mizito na kuchomwa kwa vyuma vya moto mwilini mwao,[519] mnamo mwaka 482.
Huko Aljeria, Wakatoliki wanawakumbuka Wat. **Tertula** na **Antonia**, Mashahidi, karne la III.[520]
Huko Ufaransa, Wakatoliki wanamkumbuka Mt. **Adjutori**, Padri mzaliwa Afrika, shahidi mwaka 403.
Katika Jamhuri ya ki-demokrasia ya Kongo, Wakatoliki wanawakumbuka:
Huko Elizabethville, **Albert Verhauwen** (*Didier*), Bruda wa Shirika la Wabenediktini, aliyeuawa mwaka 1961.
Huko Nkolo, **Maria Hendrika Gruyaert Godelieve**, sista wa Shirika la Wamisionari wa Moyo bila doa wa Maria (*Coeur immaculé de Marie*), aliyeuawa mwaka 1980.

Huko Misri, Wakopitiki wanamkumbuka Mt. **Zeno**, aliyeitwa Msiria, mwanakoriti. Pia kumbukumbu ya Abba **Eliasi** (Helias), askofu wa El-Mobaraq, monasteri ya Bikira Maria.[521]
Huko Ethiopia, Wakristo wanawakumbuka Mt. Abba **Danieli** wa Shete (Debra Sihat), monasteri ya Abba Makari; Mt. Abba **Mathayo** wa Asfoni, anayeitwa Maskini, Archimandrite wa Dabra ‘Aswan.[522]

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake. Amina.

## Mt. Mathayo wa Asfoni

---

519 *Martyrologium Romanum,* ed. 2005.
520 *Les Petits Bollandistes.* Rejea tarehe 4 Mei maisha yao.
521 *Arabic-Jacobite Synaxarium*
522 *The Ethiopian Rite Missal, Abba Emmanuel & Abba Brendan Cogavin, 2002, uk 210. Ethiopian Synaxarium: Tahisas 07.*

Wakristo wa Ethiopia wanamkumbuka leo Mt. Mathayo wa ‘Asfoni. Tangu ujana wake alilelewa katika hofu ya Mungu. Akawa mtawa na kuanza maisha yake ya ki-roho kwa kufunga na kusali. Akajenga kijumba chake jangwani. Akafanya kazi kwa mikono yake akitengeneza nyavu. Akiziuza, anagawia maskini fedha zake. Wafuasi wake Serapio na Abba Khadra wanasimulia yafuatayo:
Siku moja tulipokaa nje ya kijumba chake jangwani, tulisikia sauti, kama sauti ya mwanadamu akizungumza na rafiki yake ndani ya kijumba. Tulipoingia ndani hatukumwona mtu yeyote isipokuwa baba yetu, aliyekuwa peke yake. Tukamwambia: “Baba, sisi tulipokuwa nje tulisikia sauti ya mtu aliyezungumza nawe, lakini tulipoingia hatukumkuta mtu yeyote isipokuwa wewe“. Akatujibu kwa unyenyekevu na upole: “Watoto wangu, nayakumbuka madhambi yangu, na ninajihukumu, naikumbusha roho yangu adhabu zinazopita na mateso ya kifo kitakachoniangukia. Ole Mathayo maskini watakapovua mwili huu na kuuweka mbele ya kiti cha enzi ya Mungu aliye Hai, kati ya malaika na watakatifu wote wanaolinda usafi wa moyo, wanaouvaa kama kuvaa nguo!“ Kwa maneno hayo aliwasihi wafuasi wake na kuwakumbusha adhabu ya milele kwa wenye dhambi na thawabu ya milele kwa wenye haki. Ndipo akasali na kuendelea kupigana vita, kuhudumu katika monasteri aliyojenga kwa heshima ya jina la Mt. Pakomi na monasteri ya Dabra Bakalt.
Shetani na pepo wake walizoea kumtisha mchana na usiku. Akawaona uso kwa uso, wakikimbia mbele yake na kumfuata nyuma yake kila mahali alipoenda. Kila mmoja alibadilisha umbo lake, lakini baba yetu hakuwaogopa. Aliponyosha mkono wake na kufanya ishara ya msalaba walitoweka kama moshi katika upepo.
Siku moja alimwamuru Serapio mfuasi wake kuchukua kiriba cha maji na mkate kidogo kutoka monasteri na kupeleka kijumbani mwake na kusubiri pale hadi siku ifuatayo, wakati yeye aliendа kwenye shughuli fulani jangwani. Mfuasi wake alipofika kijumbani na kufungua mlango kuingia aliwaona wanyama wawili, wakubwa kuliko fisi, waliojilaza sakafuni, wakionekana wakali na kutisha. Akiogopa, alifunga mlango kwa nguvu. Na tazama baba yetu alikuja kutoka jangwani, na alipomwona mfuasi alicheka na kumwambia: “O Serapio, kwa nini hukuingia kijumbani na kunisubiri hadi nije?“ Na Serapio akamjibu: “O

baba yangu, niliwakuta ndani wanyama wawili wakali, na niliogopa na sikuingia.“ Mzee aliyekuwa mpole na safi kwa matendo na maneno alimjibu: “Unisadiki, mwanangu, kwa miaka kumi na miwili niliishi nao, niliwatumikia na mkate huu na maji niliyokuamuru kuvipeleka vilikuwa kwa ajili yao.“ Alipofungua mlango wanyama wawili wakamjia, wakalamba nyayo za miguu yake na kumhudumia kama rafiki. Mtakatifu akatia maji kutoka kiriba. Wakanywa na wakaondoka kwenda jangwani.

Abba Mathayo aliendelea kutenda miujiza hadi ripoti yake ikaenea kila mahali. Watu walizoea kumletea wagonjwa wenye kuteswa kwa kila aina ya magonjwa. Akawaponya wote kwa uweza wa Mungu uliofanya kazi ndani yake. Ifuatayo ni miujiza kadhaa aliyotenda.

Siku moja wakamletea mtu kiziwi ambaye amepagawa. Mara alipomwona Mtakatifu, pepo akapiga kelele kwa sauti kubwa na kumwangusha mtu nchini. Mtakatifu akampaka mafuta na kufanya ishara ya msalaba juu yake, kwa jina la Baba, Mwana na Roho Mtakatifu, Mungu mmoja. Na mara mtu huyu akawekwa huru. Akarudi katika ufahamu wake akifurahi sana. Walei kadhaa wakamfikia Mathayo na kumwalika kwa chakula. Mwishoni akawaaga kwa amani na kwa baraka. Walichukua sehemu ya ‘baraka‘ nyumbani mwao. Walipoweka baraka hiyo juu ya wagonjwa, waliponywa mara na kumsifu Mungu.

Siku nyingine wakamletea msichana mzuri sana aliyepagawa na pepo. Mara nyingi alichana nguo zake na hakuna mwanadamu aliyeweza kumkaribia. Wazazi wake walihangaika sana. Abba Mathayo akalia kwa sauti kubwa, akabariki mafuta yaliyokuwa katika taa, akampaka mafuta kwa jina la Kristo. Akapona.

Siku nyingine tena wakamletea mwanamke mbaya aliyeanguka katika dhambi kubwa sana. Alikuwa na mimba. Siku ya kujifungua ilipofika akapata shida kubwa, akiteswa usiku na mchana. Mtakatifu akamwambia: “Binti yangu, ungama dhambi yako kwangu na usimwambie Mungu uongo“ Akamwambia: “Nilizoea kulala na kaka wawili, bila kujua ni nani nilikuwa nalala naye. Nilipokuwa napata mimba, nilichukua dawa kuitoa na kumpatia mbwa“. Mtakatifu aliposikia hayo alimwomba Mungu na ardhi ikafungua kinywa chake na kummeza ili awe mfano kwa wengine.

Kwa kweli Mtakatifu huyu alitenda miujiza mingi! Ikiwa mmoja anataka kuiandika hawezi kufika mwisho. Siku moja alitembea jangwani, fisi akashika nguo yake kwa meno yake na kumwonyesha mtoto wake, ambaye alianguka katika shimo moja. Mtakatifu alipomwokoa kutoka shimoni, fisi akajikunja chini na kuanza kulamba nyayo za miguu yake. Akaondoka.

Siku ya kuaga dunia ilipokaribia, akaona maono. Ilionekana kwamba alialikwa kushiriki katika sikukuu ya Mababa Watakatifu, Abba Antoni, Abba Makari, Abba Pakomi, Abba Theodori, Abba Musa wa Ethiopia na Abba Sinoda. Wakamwambia: “Ni vizuri kufika kukaa pamoja nasi katika Yerusalemu ya mbinguni.“ Wakamchukua na kumbeba kwenye mlango wa Ukumbi mkubwa wenye bustani na viti ndani yake. Akasikia sauti ikisema: “Fungua mlango ili Mathayo aingie“. Akafariki na kupokea taji tatu.[523]

Mt. Mathayo, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

[523] *Ethiopian synaxarium, Tahisas* 07.

**Desemba 17**

Zamani huko Afrika ya Kaskazini (Kartago) Kumbukumbu ya Watakatifu, **Klementiani** na **Klementiana**, Shahidi.[524]
Huko Ethiopia, Wakatoliki wanamkumbuka Abba **Takla-Alfa**, abate wa Debra-Dima (Gojjam).
Huko Ivory Coast Wakatoliki wanamkumbuka Mtumishi wa Mungu **Valeria Ama Wandete** (Ouandete), mke wa Mtumishi wa Mungu Louis Wandete, 1948.[525]

Huko Misri, Wakoptiki wanamkumbuka Abba **Samueli**.[526]
Huko Ethiopia, Wakristo wanawakumbuka Mt. Abba **Hieroklis** (Yarokla), Patriarka, askofu wa 13 wa Aleksandria, Misri; Wat. **Barbara** na **Juliana**, wafiadini; Mt. Abba **Samueli**, Abate wa monasteri ya Kalamoun. Waorthodoksi Tewahedo wanawakumbuka Mt. Abba **Esi** na dada yake **Thekla**, wafiadini.[527]
Waorthodoksi wanamkumbuka Mt. **Danieli** Mwungama-dini wa Hispania na Misri, Karne la X.

Na mahali pengine ku  mbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake. Amina.

## Watumishi wa Mungu Aloisi Quandete, 1949, na mke wake Ama Valéria,  1948.

Quandete, maana yake ’Asiyejua baba yake‘ alizaliwa katika kabila la Djimini, karibu na Dabakala, Kaskazini/Mashariki nchi ya Ivory Coast, mnamo mwaka 1877. Alipokuwa na umri wa miaka 17 kijiji chake kilivamiwa na watu wa Samroy Toure. Mavuno yaliibiwa na wenyeji waliokimbia walikamatwa na kuuzwa kama watumwa sokoni mwa Bouaké. Mama yake alikamatwa lakini kijana aliweza kutoroka.

[524] Dictionary of Saints
[525] Rejea tarehe 2 Machi kumbukumbu ya mume wake Louis Wandete.
[526] *Arabic-Jacobite Synaxarium*
[527] *The Ethiopian Rite Missal, Abba Emmanuel & Abba Brendan Cogavin, 2002, uk 211. Ethiopian Synaxarium: Tahisas 08.*

Akatangatanga kwa miezi mingi katika nchi iliyoteswa na vita na njaa. Akatafuta ulinzi karibu na Jeshi la Wafaransa lililorudi nyuma. Watu wa Samroy walishambulia jeshi na kuwachukua wale waliokaa nyuma. Quandete akatoroka tena, lakini kwa miezi kadhaa aliishi bila tumaini kurudi katika nchi yake.



Wamisionari wa kwanza wa Shirika la African Missions (SMA) wakafika huko Grand-Bassam, mwaka 1895 na mwaka uliofuata walianzisha misioni mbalimbali Kusini ya Ivory Coast. Tarehe 15 Septemba 1896, Padri J.M. Bedel alifika Ivory Coast, na wiki mbili baadaye, pamoja na mapadri wawili, alienda katika Kituo cha Polisi kutafuta Wabambara 12 wangeweza kuwasindikiza ili kuanzisha misioni. Tangu siku ile maisha ya Aloisi Quandete na Padri Bedel yalisokotana, Padri akawa kama baba kwake na imani ya kikristo ikabadilisha maisha yake. Kwa miaka 30 wakafanya kazi kwa pamoja kueneza Injili. Basi kesho yake aliondoka kuelekea kwa Babou, pamoja na mapadri Hamard na Bedel. Walianzisha misioni, shule ya kilimo kwa yatima, shule ya msingi. Quandete alisaidia kujenga na kupanda shamba la kwanza la kahawa na kakao katika nchi.

Lakini hakubaki muda mrefu, mwaka 1899 homa ya manjano ikalipuka katika misioni ya Bassam. Quandete peke yake akawasaidia mapadri watatu waliofariki. Tena, kwa hatari ya maisha yake, tarehe 17 Mei 1899, alimsaidia Padri Pellet kuokoa sefu ya misioni yenye hati muhimu wakati nyumba zao ziliunguzwa kwa ajili ya usalama. Mara baadaye alirudi kwa Padri Bedel, huko Bonoua, na sikukuu ya Krismasi alibatizwa akapewa jina la Louis, yaani Aloisi (au Ludoviko).

Mwisho wa mwaka 1901, Padri Hamard, Mkuu wa SMA, akamchagua Padri Bedel kwenda kupeleleza maeneo ya Kaskazini ili waweze kuanzisha misioni. Padri Bedel akachagua kwenda pamoja naye Padri Fer na Aloisi Quandete. Wakaondoka tarehe 13 Januari 1902. Kwa Aloisi Quandete ilikuwa safari ya kurudi katika nchi yake ambapo ilitawaliwa sasa kwa Wafaransa tangu 1898. Wakafika Bouake tarehe 7 Februari. Padri Fer akabaki kule kusimamia ujenzi wa nyumba ndogo,

wakati Padri Bedel na Quandete waliendelea na safari zao. Wakazunguka huko na huko, wakizuru vijiji mbalimbali, kwa sasa katika Jimbo la Korhogo. Wakarudi Bouake siku ya Ijumaa Kuu, 28 Machi 1902 na kwa June 23 wakafika Bassam baada ya kutembea kms 1600.

Baada ya safari yake huko Kaskazini Aloisi akamwoa Maria Valeria Ama, tarehe 18 Agosti 1902, huko Dabou, mbele ya Padri J. Moury na Padri Hamard, Mkuu wa wamiisonari. Valérie Ama alikuwa mtumwa wa mfanyabiashara tajiri. Aliposikia kwamba bwana wake atamtolea sadaka wakati wa sikukuu fulani alifaulu kutoroka. Akaenda kwa mwanamke mzungu ambaye alimpeleka kwa masista huko Dabou. Kule akalelewa kikristo na kubatizwa. Inaonekana kwamba alizaliwa mnamo mwaka 1883. Aloisi alikuwa anafanya kazi kwa masista huko Dabou, kwa hiyo alipata nafasi kumfahamu vizuri.

Tangu ndoa yao Aloisi na Valeria walianza kuwa wamisionari kwa pamoja. Wakawasindikiza mapadri huko Kaskazini wakisimamia kazi nyingi za kitume. Wakakaa huko Guiembé, lakini miaka 2 baadaye, wakahama kukaa Korhogo, kijiji kilionekana kuwa muhimu zaidi kwa kazi ya kueneza Injili. Padri Bedel akaanzisha kijiji cha Wallonville, kwa ajili ya watumwa waliokombolewa. Aloisi na Valeria wakahamia Wallonville kuwasaidia waliopata uhuru wao na kuanzisha maisha mapya. Wakabaki huko hadi mwaka 1918. Vita vya Kwanza vya Dunia vilidhuru pia misioni katika nchi hiyo. Fr. Bedel akalazimishwa kujiunga na '*Senegaleese Shooters*' na kukaa huko Bouake, kms 230 mbali ya Korhogo. Akakabidhi usimamizi wa Jumuiya ya Waamini na kijiji cha Wallonville kwa Aloisi Quandete. Mwezi wa Aprili 1916, Aloisi na wakristo 20 wakaenda kwa miguu Bouake ili waweze kukomunika sikukuu ya Paska. Mwezi wa Juni 1916 Padri Bedel akahamishwa kwenda hospitalini mwa Jeshi, huko Ufaransa. Aliweza kurudi mwisho wa vita.

Aloisi alikuwa Katekista aliyefanya kazi bila kulipwa kwa sababu alitafuta riziki zake katika kazi nyingine. Alilima shamba lake, akawafuga nguruwe na mara kwa mara aliwinda. Alifanya kazi pia kama seremala, mwashi kwa ajili ya mahitaji ya familia yake na mahitaji ya watu wengine. Ili kuwa tayari kukabili hali yoyote alifuga ng'ombe. Akawa makini kutoelemea padri awaye yote.

Kama Katekista Aloisi akajadiliana na Wakristo mambo mengi kuhusu imani: namna ya kupumzika siku ya Jumapili, kutoshiriki katika tambiko bila kujitenga na ndugu, kuishi maisha ya ndoa ya kikristo kati ya wapagani, n.k. Tarehe 8 Februari 1928 Aloisi Quandete akapokea medali ya '*Bene Merenti*' kutoka Baba Mtakatifu Pio XI. Monsignore Diss, Prifekti wa kitume, wakati ule, akamsifu Aloisi akisema kwamba sasa anaweza kupumzika kwa sababu ya kazi aliyofanya, lakini hakufanya hivyo kwa sababu alijitoa kuwahudumia waamini hadi kufa kwake.

Valeria alikuwa mwanamke mwenye busara sana. Miongoni mwa wanawake wakristo alishika nafasi ya mshauri na kupanga. Akasaidia misioni katika mambo mengi. Kwa mfano, aliwapikia mapadri siku ya Ijumaa, siku ya kutokula nyama, kuvuna maembe na kuyauza kwa ajili ya faida ya misioni, n.k. Kila siku walihudhuria misa ikiwa padri alikuwepo, na jioni pamoja na Wakristo wengine walisali rozari.

Maisha yao hayakuwa tu furaha, walionja huzuni na uchungu. Aloisi na Valérie wakapata watoto watatu. Mwaka 1941, wakati wa Vita vya Pili vya Dunia, mwana wao wa pili Filipo alifariki, akiwa na umri wa miaka 35 tu. Na mwaka 1943 Padri Bedel alitoka Togo akiwa safarini kuja kukaa Korhogo wiki moja pamoja na familia ya Quandete. Lakini hakuweza kuja, alifariki njiani huko Abidjan, tarehe 14 Desemba 1943. Mwana wao wa kwanza Yohane Maria alitangulia pia kufariki kabla yao, tarehe 2 Machi, 1946.

Wakati wa Jubilee ya miaka 50 ya kueneza Injili, Oktoba 1945, Kanisa Katoliki nchini Ivory Coast likawaalika. Aloisi akasema: "Tulifanya kazi kwa nguvu bila kuona matokeo, lakini wakati nitakuwepo mbele ya Mungu, wakristo wengi watakuwepo huko Korhogo". Wakati Valeria alikaribia kufariki wenye ndoa walichukua nafasi ya kusameheana. Ndipo Aloisi akasema: "Nenda kwa amani, Valeria, mke wangu. Watoto wetu wametuacha na sasa ni zamu yako. Bwana atakupokea. Ikiwa utawaona watoto mbele ya Baba yetu aliye mbinguni, tafadhali njoo unichukue ili nipokee mimi kutoka Kristo thawabu aliyoniahidia". Valeria akafariki tarehe 18 Desemba 1948. Aloisi akafariki miezi michache baadaye, tarehe 2 Machi 1949.

Mwezi Aprili, 2005, Jimbo la Korhogo liliadhimisha jubilee ya miaka 100. Wakristo wakawakumbuka Aloisi na Valeria, pamoja na Padri

Bedel na kuwatolea heshimu kuu kwa kazi yote ya kitume waliyofanya. Wakati ule maelfu ya Wakristo waliishi imani yao ingawa vita vilikuwepo.[528]
Watumishi wa Mungu Aloisi na Valeria Quandete, mtuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

[528] Kwa habari zaidi rejea kitabu cha Padri Pierre Bouti, *Aux origines de l'Église de Korhogo, un couple: Louis Ouandété et Valérie Ama* [A Couple at the origin of the Church in Korhogo: Louis Ouandété and Valérie Ama], Korhogo: Conférence Épiscopale de Côte d'Ivoire, 1994.

**Desemba 18**

Sisi Wakatoliki tunawakumbuka Wat. **Namfamo**, **Miggini**, **Sanami** na **Lusita**, wafiadini.[529]

Huko Moroko, Wakatoliki wanawakumbuka Wat. **Kwinto**, **Simplisio**, na **wengine** walioteswa wakati wa Makaizari Desio na Valeriani, hadi kufa mashahidi; Wat. **Vikturio na wenzake 34**, wote wafiadini.[530]

Huko Ethiopia, kumbukumbu ya Mt. **Dekise**, Mwungama-dini.[531]

Huko Hanga, Tanzania, Wakatoliki wanamkumbuka **Plasido Nkalanga**, Askofu, aliyefariki mwaka 2015.

Huko Misri, Wakoptiki wanamkumbuka Mt. **Anastasi**, Patriarka, askofu wa 36 wa Aleksandria, Misri.[532] Pia kumbukumbu ya Mt. **Barnaba**, askofu wa Aidab.[533]

Waorthodoksi wa makanisa ya Mashariki wanamkumbuka Mt. **Samueli** Mwungama-dini, mwaka 693.[534]

Huko Ethiopia, Wakristo wanamkumbuka Mt. **Pamin** (Abba *Ba'Amin*), mwaminifu, aliyefia dini bila kumwaga damu yake.[535]

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake. Amina.

## Mt. Namfamo, Shahidi, na wenzake, mwisho wa karne la II.

Martirolojia ya Roma inaandika jina la Namfanio, ambalo limetafsiriwa kwa Namfanioni, lakini kadiri ya maandishi ya zamani yaliyopatikana

---

529 *Martyrologium Romanum,* ed. 2005. Zamani walikumbukwa tarehe 4 Julai

530 *Roman Martyrology,* ed. 1956. Baadhi yao: Viktori, Viktorino, Adjutor, Kwarto, Salvatori, Pompino, Moyesete, Artifas, Kresti, Bessa, Reduktula, Ampamoni na wengine thelathini,.

531 Dictionary of Saints

532 *Coptic Synaxarium: 22 Kiahk.*

533 *Arabic-Jacobite Synaxarium*

534 Rejea maisha yake tarehe 26 Desemba.

535 *The Ethiopian Rite Missal, Abba Emmanuel & Abba Brendan Cogavin, 2002, uk 211. The Ethiopian Rite Missal, Abba Emmanuel & Abba Brendan Cogavin, 2002, uk 211. Ethiopian Synaxarium: Tahisas 09.*

karibuni katika majengo ya ki-kristo huko Aljeria, jina lake ndilo Namfamo. Inaonekana kwamba alisifiwa sana kati ya Wakristo walioishi naye. Alipewa jina la *Archimartyr*, yaani Shahidi Mkuu. Kwa kweli alikuwa wa kwanza kumwaga damu kwa ajili ya Kristo, wakati wa dhiki wa Septimo Severo, mwishoni mwa karne la II. Ibada yake ilienea sana katika Afrika ya Kaskazini, hata Maksimo wa Madaurus, mwanasarufi mpagani, alilalamika kwa Mt. Augustino kuona kwamba jina lake la ki-shenzi linafuta majina yote ya miungu ya uongo. Mtakatifu Augustino akamjibu kwa busara, akimwambia kwamba hakuna sababu ya kulalamika kwa sababu jina lake ndilo jina la ki-puniki, na maana yake ni 'mbashiri mwema'. Mashahidi wenzake, Miggini, Lusita na Sanami walikuwa pia wa taifa la Puniki.

Mt. Namfamo na wenzake, mtuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

**Desemba 19**

Huko Moroko, Wakatoliki wanamkumbuka Mt. **Timotheo** (au *Timoleon*), shemasi, mfiadini. Baada ya kufungwa na kuteswa kwa ajili ya Kristo, alitupwa motoni na hivi kufa shahidi.
Huko Misri, Wakatoliki wanamkumbuka Mt. **Nemesio**, mfiadini.[536] Wakati wa dhiki iliyosababishwa na Kaizari Desio, Nemesio, Mmisri alishutumiwa kuwa mwizi. Akaachiliwa kwa kosa hilo. Lakini muda si muda akashtakiwa kuwa Mkristo na kupelekwa mbele ya Hakimu Emiliano. Aliteswa mara mbili zaidi kuliko wezi na kupigwa mijeledi. Baadaye alihukumiwa kuchomwa, pamoja na wezi na majambazi, lakini mwishoni, kama Yesu mwenyewe, alisulubiwa kati ya wahalifu wawili, mnamo mwaka 253.

Wakoptiki wanamkumbuka Mt. **Timotheo**, mwanakoriti.[537] Pia kumbukumbu za Wat. **Primo**, **Ares** na **Eliya**, wafiadini huko Askalon, Palestina, wakati waliposafiri kwenda Silisia.
Huko Ethiopia, Waorthodoksi Tewahedo, Ethiopia, wanawakumbuka Mt. Abba **Theofano**, Patriarka, askofu wa 6 wa Aleksandria, Misri; Abba **Tewashi**, towashi na mtawa;[538] Wat. **Gabrieli** na **Simeoni** na baba yao **Samueli,** waungama dini.
Waanglikana wa USA (*Episcopal Church*) wanamkumbuka **Lilian Trasher**, mmisionari katika nchi ya Misri, 1961.

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake. Amina.

## Mt. Timotheo, mwanakoriti

Mtakatifu huyu anaheshimiwa na Wakoptiki. Ni mtakatifu tofauti na Timotheo mfiadini Moroko. Pafnusi alipotembelea mwanakoriti Onufuri alikutana na mwanakoriti mwingine aliyeishi karibu naye, Aba Timotheo. Hatuna habari nyingi kuhusu mwanakoriti huyu, isipokuwa mambo Pafnusi aliyoandika.

---

[536] *Roman Martyrology,* ed. 1956.
[537] *Coptic Synaxarium: 23 Kiahk.*
[538] *Ethiopian Synaxarium: Tahisas 10.*

Baada ya kumzika Onufuri, Pafnusi alitembea jangwani siku tatu na kufika kwenye pango. Pafnusi anasimulia: “Ujasiri wangu ukarudi. Nikaingia lakini sikumkuta mtu yeyote. Nilifikiri ‘Ni mahali pa mtumishi wa Mungu. Atarudi karibuni.‘ Nikakaa mahali pale na kuanza kusali hadi jioni, nikikariri zaburi. Jua lilipoanza kutua nikatazama na kuona kwa umbali kidogo kundi la nyati na kati yao mtu. Aliponikaribia niliona kwamba alikuwa uchi, malaika zake zilikuwa nguo zake. Alipofika mahali nilipokaa akaogopa kweli, alifikiri kwamba mimi ni pepo. Akasimama na kuanza kusali, kwa sababu mara nyingi pepo walikuwa wanakuja kumshawishi, kama alivyonieleza baadaye. Nilimwendea na kumwambia: ‘Kwa nini kuogopa, ewe mtumishi wa Mungu? Tazama nyayo zangu, mimi ni mwanadamu. Uniguse na utatambua kwamba mimi ni nyama na damu‘. Akaniuliza: ‘Kwa nini ulifika mahali hapa?‘ Nikamjibu: ‘Nilifika hapa kwa sababu nilitaka kuwaona watumishi wa Mungu, na Mungu akanijalia niliyoomba.‘ Nikamwuliza: ‘Ulifikaje mahali hapa? Tangu lini unaishi hapa? Unakula nini? Kwa nini wewe ni uchi na huna nguo?‘

Akaanza kunieleza: ‘Nilikuwa mtawa. Niliishi kati ya watawa katika monasteri moja ya Theba. Wazo likanifikia moyoni. Simama, nenda na kuishi mahali peke yako. Ndipo utaishi maisha ya taamuli. Nilitaka kuwa mwanakoriti na kuwahudumia ndugu. Nilitaka kuwaonyesha ukarimu mkubwa kwa wageni, kupata riziki nyingi kwa kazi ya mikono yangu. Nikatekeleza yote. Nikaacha monasteri na kujenga kijumba faraghani. Watu wakaniajiri na nilichopata kwa kazi ya mikono yangu niliwagawia wageni.

Shetani akakasirika. Akanionea wivu kwa kazi niliyofanya kwa bidii na ya riziki nilizopata na kuwagawia wenye mahitaji. Pepo akamwingilia mwanamke aliyekuwa mtawa na kuniajiri kwa kazi fulani za mikono. Nilipokuwa namaliza kazi hiyo nilikuwa nampatia na yeye alikuwa ananiagiza kazi nyingine. Tulianza kufahamiana hadi kuwa rafiki. Tulizoea kuongea kwa uhuru na kushiriki mkate kwa pamoja. Uhusiano wetu ulituletea mauti. Tukaishi kwa pamoja kama mume na mke. Hali hiyo ilidumu miezi sita.

Nilipozingatia moyoni mwangu makosa yangu nikapata uchungu mkubwa. Nikalia na kulia. Nikiwa peke yangu nilifikiri moyoni mwangu: ‘Nikifa leo au kesho watatuadhibu kwa mateso makubwa,

kusaga meno, kutupwa gizani, kuungua kwa moto usiozimika na kutafunwa na funza ambao hafi. Simama, kimbilia mahali hapa, nenda jangwani.‘ Nilitamani kuacha dhambi. Nikasimama na kukimbia jangwani. Tangu siku ile sikuishi na mwanamke huyu.

Nilifika mahali ambapo chemchemi ya maji ilikuwepo, na mtende na pango moja. Mtende unazaa vicha kumi na viwili kwa mwaka, kila mwezi kicha kimoja. Sina nguo wala mkate. Nywele zangu zikakua na nguo zangu zikachanika. Ninajifunika na ndevu zangu. Na sasa ni miaka thelathini tangu nilipofika hapa.

Nikamwuliza: ’Ulipofika hapa uliteswa sana?’ Akanijibu: ‘Ndiyo niliteswa sana, kiasi kwamba mara kwa mara nilijitupa chini na kumlilia Mungu kwa sababu ya dhambi zangu. Na niliumwa mno kwa sababu ya udhaifu wa mwili wangu. Siku moja, karibu nami, nilimwona mtu mmoja aliyeng’aa sana. Akaniuliza: ‘Kiungo gani cha mwili wako kinakuuma?‘ Nguvu zangu ziliporudi kidogo nikamjibu: ‘Ini langu‘ na nilimwonyesha mahali ambapo niliumwa. Akanyosha mkono wake na kwa vidole vyake akapasua katikati ya ubavu wangu kama kwa kutumia kisu. Akatoa ini langu, akanionyesha jeraha lililokuwepo, akaliganga na kunirudishia ini langu mahali pake. Akachua kwa upole mwili wangu kwa mikono yake, akafunga nafasi wazi ubavuni mwangu na kuniambia: ‘Sasa umepona. Usitende dhambi tena, lisije likakupata jambo lililo baya zaidi. Bali tangu leo umtumikie Mungu daima.‘ Tangu siku ile mwili wangu ukawa mzima, maumivu yakaniacha, naishi hapa jangwani bila maumivu. Baada ya kupona akanifundisha namna gani niishi.‘

Mimi Pafnusi nilimsihi nikae pangoni nilipomwona kwanza. Akaniambia: ‘Nguvu zangu hazitoshi kushinda mashambulizi ya Adui.‘ Nilimwuliza jina lake. Akanijibu: ‘Timotheo, ndilo jina langu. Tafadhali ndugu mpendwa, unikumbuke katika sala zako, ili Bwana anipe nguvu, hadi mwisho wa maisha yangu, niendelee kushinda vita aliyoniita kupigana.‘ Nilijitupa miguuni mwake na kumwomba anikumbuke na kunibariki. Akanibariki.

Baadaye akasema: ‘Bwana anibariki. Aniweke huru na mitego ya Adui na kuniimarisha katika njia nyofu siku zote za maisha yangu, hadi kukaa pamoja na watakatifu wake.‘ Aliponibariki nguvu zangu zote zilinirudia kiasi kwamba sikujisikia kuwa na njaa au kiu.

Mtakatifu Timotheo, utuombee na Mungu utukuzwe daima na milele. Amina.

**Desemba 20**

Huko Misri, Wakatoliki wanawakumbuka Wat. **Amnoni**, **Zeno**, **Ptolemeo**, **Injeni** na **Theofilo**, askari na wafiadini, huko Aleksandria, Misri.[539] Pia kumbukumbu ya Mt. **Fulgosio,** Mwungama-dini.[540]
Huko Hispania na Tunisia Wakatliki wanamkumbuka Mtakatifu **Laurenti Compatny**, mtawa. Alienda Tunisia kukomboa watumwa, akafariki mwaka 1479.
Huko La Réunion, Wakatoliki wanamkumbuka Mwenyeheri **Jean-Bernard Rousseau** (Skubilioni), wa Shirika la Mabruda wa Shule za kikristo, 1867. Alifariki tarehe 13 Aprili, lakini huko La Réunion, sikukuu yake inaadhimishwa tarehe 20 Desemba, siku wenyeji wanasherehekea ukomeshaji wa utumwa.
Huko Tanzania, kumbukumbu ya Mhashamu **Antoni (Anthony) Banzi** askofu wa Tanga, aliyefariki mwaka 2020.

Wakoptiki wanakumbuka kuzaliwa kwake Mt. **Taklat-Haymanot**, Mwethiopia.[541]
Huko Ethiopia, Wakristo wanamkumbuka Mt. Abba **Bakimos**.[542]

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake. Amina.

## Askari  Amoni na wenzake, wafiadini, 250.

Askari Amon, Zeno, Ptolemi na Injeni, pamoja na Mkristo mwingine Theofilo, walisimama karibu na mahakama na kumwangalia Mkristo jinsi alivyoteswa. Akiwa karibu kumkana Yesu, wakamtia moyo kwa ishara zao. Mkutano wakapiga kelele na kuwashtaki kwa Hakimu. Wakajitokeza mbele na kukiri kwamba wao ndio Wakristo.

---

[539] *Roman Martyrology,* ed. 1956
[540] Dictionary of Saints
[541] *Coptic Synaxarium: 24 Kiahk.* Sikukuu yake inaadhimishwa tarehe 17 Agosti..
[542] *The Ethiopian Rite Missal, Abba Emmanuel & Abba Brendan Cogavin, 2002, uk 212. Ethiopian Synaxarium: Tahisas 11.*

Wakahukumiwa kukatwa vichwa. Hakimu alishangaa kuwaona jinsi walivyofurahi kwenda mahali pa kifo.
Katika dhiki ile Heroni, Ateri na Isidori, wamisri na Dioskoro, kijana wa miaka 15 walishtakiwa huko Aleksandria. Kwanza, Hakimu alimchukua kijana kwa mkono na kuanza kumshauri kwa maneno matamu; baadaye alimshambulia kwa mateso mbalimbali; lakini kijana huyu hakuyumbisha kwa maneno yake wala kutishwa na mateso yake. Wote, baada ya kuraruliwa na kutengwa viungo, walichomwa moto wakiwa wazima. Lakini Hakimu alimwachilia Dioskoro, kwa sababu ya ujana wake, akimwambia kwamba alimpatia nafasi ya kutubu kwa faida yake, na kuonyesha jinsi alivyopendezwa na uzuri wake.
Ninyi askari wafiadini, mtuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

## Mt. Laurenti Compony, 1479

Laurenti alizaliwa Hispania, huko El Puig, mwaka 1415. Alikuwa mtawa wa Kanisa Katoliki, *Order de Mercederi.* Mwaka 1452 alienda Tunisia kuwakomboa watumwa.
Wakati aliporudi, meli ilipatwa na dhoruba. Wengi baadhi ya watumwa waliokombolewa walikufa majini. Waliobaki wakarudishwa Tunisia na wakafanya watumwa tena pamoja na Laurenti. Baada ya miaka 15 akaachiliwa. Akarudi kwao na kufanywa mkuu wa shirka lake. Tangu kale anaheshimiwa kuwa Mtakatifu.

**Desemba 21**

Huko Ethiopia, kumbukumbu ya Mt. **Daruda**[543], Abate.
Huko Aljeria, Wakatoliki wanawakumbuka **Aloisi Richard**, **Gaspari Morat** na **Aleksi Pouplard**, Mapadri wa Shirika la Wamisionari wa Afrika (*White Fathers*), waliouawa na viongozi wao, huko Ghadamès, Aljeria, 1881.
Huko Kisangani, Jamhuri ya ki-demokrasia ya Kongo, Wakatoliki wanamkubuka **Roberti Besson**, Padri wa Shirika la Wamisionari wa Afrika (*White Fathers*), aliyeuawa mwaka 1995. Sababu ya uuaji haieleweki.
Huko Brazzaville, Kongo, Wakatoliki wanamkumbuka **Gui-Alfredi Nakavoua**, Mseminari wa jimbo, aliyeuawa mwaka 1998.

Huko Misri, Wakoptiki wanamkumbuka Mt.**Yohane Kama** (Khame), mtawa.[544]
Huko Ethiopia, Wakristo wanamkumbuka Mt. Abba **Samuel wa Waldebba**. Waorthodoksi Tewahedo wanawakumbuka Wat. Abba **Khadre** (Hydra) wa Dabra 'Aswan, na Mt. **John**, mwungama dini; **Eusis** (Ausis), mfiadini, na Abba **Antoni**.[545]
Waorthodoksi wanamkumbuka Mtu wa Mungu **mama Stavritsa**, mmisionari huko Kenya, 2000.

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake. Amina.

## Mapadri waliouawa Aljeria, 1881

Mapadri Richard, Morat na Pouplart, walioondoka R'damès, tarehe 18 Desemba 1881, wakitamani kufika Rh'at, huko Tchad, waliuawa na viongozi wao, siku mbili baadaye. Habari hiyo ilimfikia Karolo Kardinali Lavigerie tarehe 11 Januari 1882. Akahuzunika sana, kwa

[543] Dictionary of Saints
[544] *Coptic Synaxarium: 25 Kiahk.*
[545] *The Ethiopian Rite Missal, Abba Emmanuel & Abba Brendan Cogavin, 2002, uk 212. Ethiopian Synaxarium: Tahisas 12.*

sababu hakuamuru wala kuruhusu safari hiyo, akijua kwamba wakati wake haujawadia. Mwaka 1880, halmashauri ya Shirika ikaamua kuanzisha misioni ya Rh’at. Mapadri Richard, Royer na Pouplard wakateuliwa kwenda kukaa kule wakati nafasi ikipatikana. Walikuwa wanajitayarisha kuondoka mwaka 1881. Lakini ilipopatikana habari ya mauaji ya Kalani Flatters na askari wake, tarehe 16 Februari 1881, ikamlazimisha Kardinali kuwapasha habari wamisionari kusubiri. Wakatii, lakini macho yao yalielekea daima Kusini.

Padri Richard, tarehe 1 Julai 1881, bila kutambua vya kutosha uhasama wa wenyeji, akitegemea urafiki wake na kiongozi wake Chaambi wa Ouargla, akawaandikia wakubwa wake: “Uturuhusu kuanza safari yetu kwenda katikati ya Afrika, mahali ambapo roho nyingi za watu zinangoja kumjua yule ambaye ni Njia, Ukweli na Uzima.“ Padri Charbonnier, aliyekuwa Mkuu wakati ule, akamjibu tarehe 8 Septemba 1881, akawaruhusu, ikiwa wahakikishia vya kutosha kuhusu usalama uliopo.

Tarehe 18 Desemba 1881, mapadri Richard, Morat na Pouplard wakaondoka, wakisindikizwa na maombezi ya wamisionari waliobaki na waliowaonea wivu. Katika usiku wa kuamkia tarehe 21 mapadri waliuawa na viongozi wao Watouaregs.

Wamisionari waliobaki R’dames wakashikwa na ububmbuazi walipowaona viongozi watatu wakipiga hodi mlangoni mwao, tarehe 21 Desemba. Wakajaa na uchungu walipopata habari kwamba mapadri wenzao waliuawa na Watouaregs. “Kwa mvuto wa fedha, mtu mmoja alipatikana na akakubali kuwaua wamurabiti wa ki-kristo. Lakini msaliti Bou-Reddi akachukiwa na kulaaniwa na wote“ aliyoandika Padri Hacquard.

Baada ya kupata habari hiyo, misioni ya Sahara ikaachwa, na tarehe 5 Machi, 1882, wamisionari wa R’madès wakarudi Tripoli, wakisindikizwa na askari wa Pasha wa Tripoli. Mwaka 1893, tarehe 11 Januari, masalia machache ya wamisionari yaligunduliwa na mpelelezi Foureau na kukabidhiwa kwa mapadri huko Ouargla. Padri Richard alikuwa na umri wa miaka 35, Padri Morat miaka 28 na Padri Pouplard miaka 27.

Mapadri Richard, Morat na Pouplard, mtuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

**Desemba 22**

Sisi Wakatoliki tunawakumbuka Mt. **Karemoni**, **Iskirioni** na **mashahidi wengi**.[546]

Wakoptiki wanamkumbuka **Herakioni**, askofu na shahidi.[547]
Huko Ethiopia, Wakristo wanawakumbuka Mt. **Barsanufio** (*Basofreyos* au *Parsnuphis*), mfiadini wakati wa utawala wa Waislamu, Mt. **Apraksio** (*Abracius*). Waorthodoksi Tewahedo wanawakumbuka Mt. **Mikaeli**, mtawa wa Debra Kalmon, Abba **Makari**, aliyejilisha kwa kwale.[548]

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake. Amina.

## Mt. Karemoni na wenzake, Karne la III

Wakati dhiki, iliyosababishwa na Kaizari Desio, iliendelea kwa nguvu mnamo 250. Wakristo wengi, walioishi Misri, walilazimishwa kuondoka na kutembeatembea jangwani. Wengine waliliwa na wanyama wakali, wengine walikufa kwa njaa, baridi na magonjwa, na wengine waliuawa na Wabarberi na wezi. Wote walikufa mashahidi. Wakristo vijana waliuzwa kama watumwa.
Karemoni alikuwa askofu wa Nilopolis. Alikuwa mzee sana wakati dhiki ilipozidi kuwa mbaya. Yeye na mwenzake walienda kujificha katika milima ya Arabia. Hawakuonekana tena, wala miili yao kugunduliwa.
Pia tunamkumbuka Mt. Iskirioni, mfiadini huko Aleksandria. Alifanya kazi kwa afisa mmoja katika mji mmoja wa Misri, labda Aleksandria. Alilazimishwa na mkuu wake kuitolea sadaka miungu wa uongo. Akakataa kwa sababu amri hiyo ilipinga amri ya kwanza ya Mungu. Mkuu wake alikasirika na kuamua auawe. Iskirioni aliyadharau mateso

[546] *Martyrologium Romanum,* ed. 2005.
[547] *Arabic-Jacobite Synaxarium*
[548] *The Ethiopian Rite Missal, Abba Emmanuel & Abba Brendan Cogavin, 2002, uk 213. Ethiopian Synaxarium: Tahisas 13.*

yote aliyopata kwa kukataa kuitolea sadaka miungu wa uongo. Mwishoni alifariki utumbo wake ukitobolewa kwa kiguzo chenye ncha kali.
Mt. Karemoni na wenzake, mtuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

## Mt. Herakioni, karne la IV

Wakoptiki wanakumbuka leo Mt. Herakioni, askofu na shahidi. Tunapata maisha yake katika kitabu cha Watakatifu kilichoandikwa kwa lugha ya Kiarabu. Alipata daraja la uaskofu na Patriarka Theonas. Akawa askofu wa Abbou El-Hayyb, karibu na mji wa Aleksandria.
Herakioni alipopata habari kuhusu dhiki alimwendea Abba Petro, Patriarka wa Aleksandria, ‘shahidi wa mwisho‘, kujadiliana naye ili kujua la kufanya. Alipotoka nyumbani mwake, akakutana njiani na Waberbers. Wakamshika na kumlazimisha aende pamoja nao. Walimtesa kwa njaa, walimpiga vibaya na kumfunga kati ya ngamia. Usiku mmoja, akifungwa na kamba, akalia na kumsihi Mungu achukue roho yake, kwa sababu alikuwa katika uchungu na karibu kufariki. Malaika wa Bwana akamtokea na kumwambia: “Salamu! Kwa nini unahangaika kwa mapigo machache? Hadi sasa hawakukutesa juu ya gurudumu, hawakukutupia bakuli la mafuta ya moto, hawakukuweka juu ya kitanda cha chuma na kuwasha moto chini yake. Vumulia utapata ushindi.“ Waberbers wakaenda kuvamia njiani mji wa El-Behnesa.
Wakati ule Gavana Yohane wa familia ya Viktori, mwana wa Waziri Romano, alikuwa katika eneo hilo pamoja na wapandafarasi mia tano. Alipopata habari kwamba Waberbers walifika nchini akaenda kukutana nao pamoja na wapanda farasi mia mbili. Yohane akiona idadi yao, walikuwa askari 2000, akashuka kutoka farasi yake, akanyosha mikono yake kuelekea Mashariki, akaomba: “Bwana, ni wewe ulishinda falme ishirini na tisa kwa mikono ya Yoshua, mwana wa Nuni; ni wewe ulikuwepo pamoja na Samsoni mwenye nguvu kuwaharibu Wafilisti; ni wewe ambaye ulimpatia Daudi ushindi juu ya Goliathi. Mfalme wangu na Mwalimu wangu, Yesu Kristo, uwe pamoja nami leo, uokoe taifa lako na watu hawa wabaya. Utukufu una milele. Amina.“ Alipomaliza akapanda farasi yake na kulia kwa sauti kuu akiwaambia askari zake:

“Muwe hodari, Bwana yu pamoja nanyi anawapigania“. Na mara wakawaendea adui kwa nguvu ya Kristo. Waberbers walikuwa watu wa kutisha, wakivaa usoni mwao kitambaa cheusi. Walikuwa askari mashuhuri wakipanda ngamia. Yohane akawashinda na kuwaua, walibaki wachache. Baada ya kupumzika alitazama nyara zao. Wakaona kondoo, ng’ombe na wanyama wengi, mateka wengi, wanaume kwa wanawake. Wakamwona mtakatifu huyu Herakioni akivaa nguo zilizochakaa na joho. Alipigwa sana hata mwili wake ulikuwa vidonda vitupu. Mtumishi mmoja wa Yohane akafika mbele yake na kumsihi: “Nakuomba Jemadari wangu, Bwana wangu, unipatie mtawa huyu.“ Akakubali. Akamleta nyumbani mwake. Alipopona akamwuliza: “Baba yangu, uniambie wewe ni mtawa wa monasteri gani ili niweze kukurudisha kule na uendelee kuniombea“. Mtakatifu akamjibu: “Mwanangu, mimi nilikuwa askofu wa mji wa Abbou el-Hayyb. Sasa hakuna Mkristo anayeweza kujionyesha kwa sababu ya dhiki dhidi yao.“ Akabaki kwake akijikania, kwa kufunga na kukesha daima.mchana na usiku, lakini alikuwa mfungwa.
Habari ikamfikia Abba Theodosio, askofu wa Pemdjé, kwamba askofu alipatikana miongoni mwa mateka wa Waberbers, na kwamba alikuwa nyumbani mwa Mtumishi mmoja, akijikania, na Bwana anafanya miujiza mingi kwa mikono yake. Akawaza kumtembelea. Katika ndoto akamwona mtu mmoja ambaye alimwambia: “Harakisha kwenda kwa askofu Herakioni na pokea baraka zake kwa sababu hakika atashika nafasi yako“. Akaamka, akitetemeka na kujiuliza, “Kitatokea nini? Niache cheo changu kwa mwingine!“ Akamwendea askofu, akiwazawaza. Akamsalimia na kukaa karibu naye. Akamwuliza: “Baba, umekwisha sikia habari za mtu aliyeshushwa cheo chake kwa ajili ya mwingine?“ Ndipo Roho Mtakatifu akamjaza Herakioni: “Baba yangu, siyo kama unavyofikiri. Utafuata njia ya Yeremia, Nabii, aliyewaombea Waisraeli jangwani. Lazima uende jangwani na ujifiche kwa sababu ya dhiki dhidi ya Wakristo. Kuhusu mimi, siwezi kuondoka, utaniacha kuangalia jimbo lako.“ Askofu akafarijika. Akafika mara nyingi kumwona na kujifunza kutoka kwake. Ndipo amri ya Dioklesiani ikatangazwa: “Yeyote asiyeabudu miungu atauawa“. Askofu Theodosio akawakusanya waamini, akawaongoza kwa Abba Herakioni na

kuwakabidhi kwake. Akawaambia: “Tangu leo, huyu ndiye Mchungaji wenu. Amtiiye yeye anitii mimi“. Na mara akaenda jangwani.
Mtakatifu akabaki mateka kwa miaka kumi na miwili. Abba Paulo, mwana wa Mtumishi aliyemwokoa akamtembelea, akajifunza kutoka kwake na kumletea matunda. Walinzi walimruhusu aingie kwa kupata, kila mara, sarafu ya dhahabu. Abba Herakioni akampadirisha. Abba Paulo alikuwa anaadhimisha misa nyumbani mwake kwa kujificha kwa sababu hakuna mtu aliyeweza kuadhimisha misa kanisani. Sifa za mtakatifu zikaenea, miujiza mingi ilitendeka katika gereza lake. Gavana akamwita kwake. Alipomwona, katika hasira yake, akanyosha mkono wake na kwa kuchukua mkuki kwa askari mmoja aliyesimama karibu naye, akamchoma mtakatifu. Abba Herakioni akafariki mara. Gavana akaamuru kutupu mwili wake jalalani. Mwili wake ukakaa siku tano, hakuna mnyama wala ndege waliougusa, kwa sababu malaika wa Bwana aliulinda.
Mtakatifu akamtokea Abba Paulo na kumwambia: “Nimekupadirisha, baba yako amenipokea nyumbani mwake, kwa nini hunijali na kunisahau katika huzuni yangu? Mwili wangu unakaa juu ya takataka. Uuchukue, najua kwamba Bwana Yesu atakujazi.“ Basi Paulo akauchukua mwili wake na kuuficha katika kimoja cha vyumba vyake. Shetani akatangaza mjini kwamba Abba Paulo anaadhimisha misa kisirisiri na kwamba ni yeye aliyechukua mwili wa askofu na kumzika katika mojawapo wa vyumba. Waliposikia habari hizo, wenzake wakamwambia: “Uvae joho la askofu na tembea mjini.“ Gavana akasikia. Akatuma askari ambao wakamshika na kumtia gerezani. Jemadari Yohane akamwendea Gavana na kuzungumza vizuri kuhusu Abba Paulo. Gavana akamwachilia huru Abba Paulo.
Mt. Herakioni, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

**Desemba 23**

Huko Misri, Wakatoliki wanawakumbuka Mt. **Hellaniko**, askofu na **Begeo**, padre. Huko Abyssinia, kumbukumbu ya Mt. **Abashadi** (*Shade*), Padri na Shahidi.[549] Huko Ethiopia, Wakatoliki wanamkumbuka **Kristodoulo** wa Aleksandria.
Huko Luozi, Jamhuri ya ki-demokrasia ya Kongo, Wakatoliki wanamkumbuka **Emilio Charlier**, padri wa Shirika la Mkombozi, aliyeuawa mwaka 1974.

Wakoptiki wanamkumbuka Mt. Anba **Bisadi** (akijulikana pia kwa majina ya *Psote*, *Abashadi*, *Abassadius*, *Amba Sada*, *Beshada*), askofu na mfiadini,[550] mnamo 300.
Huko Ethiopia, Wakristo wanamkumbuka Mt. **Simon**, wa mji wa Manuf, Upper Misri, mfiadini wakati wa Waislamu. Waorthodoksi Tewahedo wanawakumbuka Mt. Abba **Gabra Krestos**, Patriarka, askofu wa 66 wa Aleksandria, Misri; Mt. Abba **Behur** na Abba **Minas** mzee, wafiadini, Mt. Abba **Amonio**, askofu wa mji wa 'Asna ('Esna), mfiadini.[551]

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake. Amina.

## Mt. Abashadi, Askofu na Shahidi, 300.

Kwa Wakoptiki Abashadi alikuwa Padri na pia Askofu wa 'Ebsay'. Tunasoma katika kitabu chao cha Watakatifu kwamba Kaizari Dioklesiani aliposikia kwamba Abba Abashadi na Abba Ghellaniko walipokuwa wanaimarisha Wakristo katika imani yao na kuwazuia kufanya ibada kwa miungu ya uongo akawaita mbele yake. Abba Abashadi akamwomba mjumbe wa Kaizari kumpatia nafasi usiku mmoja. Akaenda kanisani, akawaita Waamini wake na kuadhimisha

[549] *Les petits Bollandistes*
[550] *Coptic Synaxarium: 27 Kiahk.*
[551] *The Ethiopian Rite Missal, Abba Emmanuel & Abba Brendan Cogavin, 2002, uk 213. Ethiopian Synaxarium: Tahisas 14.*

ibada. Akawapa komunio. Akawasihi kuwa imara katika imani. Akawaaga na kutii mapenzi ya Bwana.

Akaenda pamoja na mjumbe wa Kaizari kwa Ariani, Gavana wa Ansena. Ariani alipoona jinsi uso wake ulivyong'aa na heshima yake kuu, alimhurumia na kumwambia: "Wewe ni mtu wa heshima sana. Afadhali ujihurumie na kutii amri ya Kaizari." Abba Abashadi akamjibu: "Siwezi kubadilisha ufalme wa mbinguni kwa ufalme wa dunia hii".

Baada ya majadiliano marefu, Gavana akaamuru Abba Abashadi kuteswa na kutupwa katika maji ya moto. Mungu akamlinda na kumwinua mzima, bila maumivu yoyote. Gavana akaamuru akatwe kichwa. Ndipo Abashadi akapata taji la ushahidi.

Mt. Abashadi, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

**Desemba 24**

Sisi Wakatoliki tunawakumbuka, pamoja na Yosefu, **Watakatifu wote wa Agano la Kale** walioishi kabla ya kuzaliwa Yesu Kristo na waliousubiri kwa imani ujio wake.[552]

Huko Libya, Wakatoliki wanawakumbuka Wat. **Lusiano**, **Metrobio, Paulo, Zenobio, Theotimo** na **Druso**, wafiadini, huko Tripoli, Libya.[553]

Huko Ethiopia, Wakatoliki wanamkumbuka **Abuna Eustasio.**[554]

Huko Heiban, Sudan ya Kusini, Wakristo wanawakumbuka **watu 6.000** waliuawa na Waarabu wa Kaskazini, mwaka 1992.[555]

Katika Jamhuri ya ki-demokrasia ya Kongo, wakatoliki wanawakumbuka:

Huko Nyakariba, **Emmanueli Nsengiyumva Mpoberabanzi**, padri na **Karolo Kanyamanza Ndagijimana**, shemasi, wote wawili wa Jimbo la Goma, na **mamia ya Wakimbizi Wahutu** waliouawa na Banyamulenge, mwaka 1996.

Huko Busuringi, Wakatoliki wanawakumbuka **Baudouin Busunyu** na **Yohane Ntirivamunda**, mapadri kutoka Rwanda, pamoja na **Magdalena Karitasi**, **Virginia Mukantwali** na **Bampire Basillusa**, masista wa Shirika la watumishi wa Maria bila dhambi, waliouawa mwaka 1996.

Huko Kameroun, Wakatoliki wanamkumbuka **Fransisko-Ksaveri Mekong**, aliyeuawa mwaka 2008. Pia wanamkumbuka **Antoni Probst**, Bruda wa Shirika la wamisionari wa Mt. Klaret, aliyeuawa.

Huko Misri, Wakoptiki wanawakumbuka mashahidi **wanaume mia moja na hamsini** na **wanawake ishirini na wanne**, wote kutoka Ansena.[556]

---

[552] *Martyrologium Romanum,* ed. 2001.
[553] *Roman Martyrology,* ed. 1956
[554] Rejea maisha yake tarehe 28 Septemba
[555] Rejea Fr. Neno Contra,, Louis Kalonji, *African Lay Martyrs*, New People Media Centre, 2009, uk. 187-190.
[556] *Coptic Synaxarium: 28 Kiahk.*

Waorthodoksi wanamkumbuka Mt. **Eugenia**, bikira na shahidi, mnamo 190, pamoja na baba yake **Filipo**, mama yake **Klaudia**, na matowashi wawili **Proto** na **Hiasinto**, na **Basila**.
Huko Ethiopia, Waorthodoksi Tewahedo, Ethiopia, wanawakumbuka Mt. **Yemsah**, mfiadini, Wat. **Herwag**, **Anania**, **Kazi** wa mji wa Akhmin, **Sansaradin** na **Awganyos** (Eugenius) wa mji wa Gawer. Pia wanamkumbuka Mt. **Miriam**, dada wa Musa.[557]
Waanglikana wanamkumbuka **Yohanna Tia**, mchungaji aliyeuawa na askari, mwaka 1966.

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake. Amina.

## Yusufu Babu Mtakatifu wa A.K.




Wakristo wa makanisa mbalimbali wanawaheshimu kama watakatifu. Mababu wa imani wa A.K. tangu Ibrahimu hadi Yoshua, walioishi Misri muda mfupi au muda mrefu: Ibrahimu, Sarah, Isaka, Yakobo, Yusufu, Musa, Haruni, Yoshua na Kalebu. Pengine wanakumbukwa katika Kalenda ya Kanisa, kama Musa na Haruni. Leo tumkumbuke kwa namna ya pekee Yusufu bin Yakobo. Maisha yake ni mfano wa maisha ya Yesu Kristo, Mwokozi wetu.
Mungu akamwonyesha katika ndoto mbili jinsi atakavyokuwa baadaye. Ni mwito wa pekee. Yusufu hakuelewa atakuwa nani, atafanya kazi gani, lakini ndugu zake na wazazi wake wameelewa kwamba atatawala juu yao. "*Ni ndoto gani hii uliyoiota? Je, mimi na mama yako na ndugu zako tutakuja tukusujudie hata nchi?*" Mwa 37:10. Kwa hiyo ndugu zake wakamhusudu. Tena alipendwa na babaye kwa sababu alikuwa

---

[557] *The Ethiopian Rite Missal, Abba Emmanuel & Abba Brendan Cogavin, 2002, uk 214. Ethiopian Synaxarium: Tahisas 15.*

mtoto wa uzee wake, mtoto wa kwanza wa mke wake mpenzi Raheli. Kwa kweli baba yake akamwonyesha upendeleo. Akamtengenezea kanzu ndefu inayofanana na kanzu ya mtawala wa nchi, inayofika mpaka mikononi na miguuni. Ndoto hizo zote hazikutekelezwa kama Yusufu alivyofikiri. Bali kinyume cha ndoto akapata shida, karibu kuuawa. Ndugu zake wakamkamata, wakampiga, hata walitaka kumwua. Mwishoni akauzwa kwa vipande 20 vya fedha kwa Wamidiani. Nao Wamidiani wakamwuza kwa Potifa, mkuu wa askari huko Misri. Alipata maisha mazuri lakini bila uhuru. Kwa sababu Mungu alikuwa pamoja naye, basi akaibariki nyumba ya Potifa, [558] lakini hakumbariki Yusufu bali watu waliohudumiwa naye.

Yusufu alikuwa mtu mzuri kwa umbo. Mke wa Potifa akaanza kumpenda, na tamaa ilipowaka akatamani kulala naye: "*Lala nami*" Mwa 39:7. Yusufu, mtu mwenye usafi wa moyo, akamjibu: "*Hakuna mkuu katika nyumba hii kuliko mimi, wala hakunizuia kitu chochote ila wewe, kwa kuwa wewe u mkewe. Nifanyeje ubaya huu mkubwa nikamkose Mungu?*" Mwa 39:9. Kwa hiyo, mke wa Potifa alipoona kwamba hakuweza kumshawishi, akashtaki kwa uongo, akamsingizia. Potifa akaamini maneno ya mke wake, akamtia Yusufu gerezani. Lakini Bwana hakumwacha Yusufu. Kwa sababu Mungu alikuwa pamoja naye, akambariki mkuu wa gereza na wafungwa waliohudumiwa naye, lakini hakumbariki Yusufu. Akakaa huko kama miaka minane. [559] Kwa neema ya Mungu akajaliwa karama ya kufasiri ndoto. Ikawa gerezani walikuwepo Mkuu wa wanyweshaji wa Farao na mwokaji wake. Wote wawili waliota ndoto. Yusufu akawafasiri ndoto zao na ikatokea kama alivyosema. Mwokaji akatundikwa na Mkuu wa wanyweshaji akarudishwa katika kazi yake. Lakini Mkuu wa wanyweshaji akamsahau Yusufu. Akabaki gerezani miaka miwili zaidi.

Ikatokea pia kwamba Farao akaota ndoto na hakuna mtu katika nchi ya Misri aliyeweza kufasiri ndoto zake. Yusufu akaitwa na Farao. Alipofasiri ndoto zake, Farao akamshangilia na kumweka kuwa Mkuu wa pili katika Misri. Ndipo Mungu akatimiza mpango wake. Sasa kwa huduma za Yusufu, Mungu akawabariki watu wengi, taifa nzima la

---

[558] Mwa 39:5-6

[559] Mwa 39 :20-40 :4.

Misri, hata wengine waliofika kununua chakula, kati yao ndugu zake Yusufu. Kwa moyo mkuu akawasamehe ndugu zake wote, na kuwajulisha mpango wa ajabu wa Mungu, akawaambia ndugu zake: "*Siyo ninyi mlionipeleka huku bali ni Mungu*", Mwa. 45:8. Yusufu akatawala katika nchi ya Misri mpaka kifo chake. Akazikwa huko.
Maisha yake ni mfano wa maisha ya Yesu, pia ni mfano wa maisha ya watu wengi siku hizi. Kwa huduma zao Mungu anawabariki watu wengi, lakini wao wenyewe wanapita kwa mateso mengi. Anawatakasa ili wafanane zaidi na zaidi na Yesu Kristo.
Mt. Yusufu bin Yakobo, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

**Desemba 25**

## Sherehe ya Kuzalizwa kwake Bwana wetu Yesu Kristo.

Zilipita karne nyingi tangu Mungu alipoumba mbingu, dunia na mwanadamu kwa mfano na sura yake; Miaka mingi tangu gharika kuu Mungu alipoweka upinde wa mvua uwinguni uwe ishara ya agano lake na amani; Karne ishirini tangu Ibrahimu Baba yetu wa imani alipotoka Uru wa Wakaldayo; Karne kumi na tatu tangu Musa alipowaongoza Waisraeli kutoka nchi ya Misri; Mnamo mwaka 1000 wa kutawazwa Mfalme Daudi ... Miaka 776 baada ya Michezo ya kwanza ya Olimpiki; Mwaka 752 wa kuanzishwa mji wa Roma; Mwaka 42 wa utawala wa Kaizari Oktaviani Augusto, wakati ulimwengu mzima ulikuwa na amani, Yesu Kristo, Mungu wa milele na Mwana wa Baba wa milele, akitamani kutakatifuza ulimwengu kwa kuja kwake, akachukua mimba kwa uweza wa Roho Mtakatifu kwa Bikira Maria, na baada ya miezi tisa akazaliwa Bethlehemu ya Yuda, akawa mwanadamu.[560]

Huko Roma na Aleksandria Misri, Mt. **Eugenia**, Bikira na Shahidi, Karne la III.[561]

Huko Nigeria na Kenya, Wakatoliki wanamkumbuka Mtumishi wa Mungu **Yosefu** (Joseph) **Shanahan**, askofu, 1943.

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake. Amina.

## Mt. Eugenia, Bikira na Shahidi, Karne la III


Mt. Huyu aliishi miaka kumi tu huko Misri, lakini maisha yake yalikuwa maisha ya ajabu jinsi Mungu alivyomwongoza katika miaka hiyo aliyoishi Misri. Eugenia alizaliwa Roma, mwaka 183, baba yake, afisa mkuu katika serikali ya Roma, aliitwa Filipo na mama yake Klaudia. Wote walikuwa wapagani. Kaizari Kommodo alipomtuma Filipo kuwa gavana wa Misri, familia ikaishi Aleksandria, wakati Eugenia alikuwa na umri wa miaka 10. Filipo, licha ya kushughulikia nchi, hakuacha kushughulia malezi ya watoto wake watatu: binti yake

---

560 *Martyrologium Romanum,* ed. 2005.

561 *Les Petits Bollandistes*

Eugenia, na wadogo zake wawili Aviti na Sergio. Alimpenda sana Eugenia, ambaye tangu ujana wake alionyesha kuwa na akili nyingi na kumbukumbu kubwa hata kuweza kukumbuka daima yote aliyosoma au kusikia. Eugenia akiwa na miaka kumi na tano alipokuwa amemaliza kujifunza elimu ya Kigiriki na Kilatini, akaanza kujifunza falsafa. Siku kwa siku baba yake Filipo alifurahia tabia na uwezo wa binti yake. Na zaidi, Eugenia alipambwa na Mungu kwa uzuri wa umbo la mwili, na katika siri ya moyoni, hamu ya usafi wa moyo.



Wakati ulipofika, baba yake alimtafutia binti yake mchumba mmoja. Mwaka 199, Aquilio, mwana wa balozi Aquilino, akamwomba amwoe. Baba yake Filipo akamwambia binti yake jinsi ingekuwa vizuri aolewe na mtu wa ukoo bora. Eugenia akamjibu: "Siyo kuzaliwa kwake, bali mwenendo wake, unaomwongoza mtu kumchagua mume. Mtu haishi na wazazi wa mume wake, bali anaishi naye". Wengine wengi walimwomba aolewe nao, lakini Eugenia aliwakatalia wote, akisukumwa moyoni mwake kwa hamu asiyotambua kupenda ubikira. Siku moja akakutana na kitabu chenye barua za Mt. Paulo. Akaanza kusoma barua zote, na hamu ya kupata wokovu ikazaliwa moyoni mwake. Uso wake ukabadilika, hata wazazi wakatambua kwamba binti yao Eugenia anahangaika, lakini hakuweza kushirikisha siri yake. Akawaomba nafasi ya kupumzika mbali kidogo na nyumbani, akiwa na wazo kuacha nyumbani na kutorudi. Baba yake, bila kujua nia ya binti yake, alikubali. Akaondoka kwenda shambani mwa baba yake, pamoja na matowashi wawili waliolelewa pamoja naye, Proto na Hiasinto. Njiani akasikia nyimbo za kikristo: "Mungu ni mkuu, astahili sifa zetu zote, ni mkuu kuliko miungu wote. Miungu wote wa mataifa ni pepo, lakini Mungu wetu ameumba mbingu na nchi. Utukufu na uzuri vinatembea mbele yake. Utakatifu wote unakaa hekaluni mwake." Kwa maneno hayo: "Miungu wote ni pepo. Mungu wetu ameumba mbingu na nchi", Eugenia akaanza kulia machozi akitambua upuuzi wa elimu yote ya ki-binadamu.

Walipofika mashambani mwa baba yake, Eugenia akawachukua Proto na Hiasinto na kuanza kuwaeleza kinaganaga dini mpya ya kikristo. Kwa sababu ya upendo wake na ujasiri wake, wakakubali kumfuata katika dini ya ki-kristo.
Siku zikapita. Eugenia alianza kutafakari namna ya kuanza maisha yake mapya. Aliposikia kwamba, karibuni mwa mashamba ya baba yake kulikuwa na monasteri ya wanaume, chini ya uongozi wa Abate Theodori, akawaeleza matowashi mpango wake, kuvaa ki-ume, na kesho yake, wanaporudi Aleksandria asubuhi na mapema, kungali giza bado, kutelemka kwa siri kutoka kwenye gari, na kwenda monasterini, wakati gari linaendelea kufika Aleksandria. Ndivyo ilivyotokea. Mungu akabariki mpango wake.
Njiani kwenda monasteri, wakakuta mkutano mkubwa na Wakristo, walioandamana na Askofu wao Heleno. Baada ya misa, Eugenia na wenzake walipelekwa mbele ya Askofu. Huyu akiangaziwa na Mungu kuhusu jinsia ya Eugenia, ambaye alijitambulisha kwa jina la Eugenio, na mipango ya Mungu juu yake, alimruhusu kubaki na nguo za kiume na watumishi wake wawili, walinzi wa ubikira wake. Akapanga wote watatu wabatizwe na kupokelewa kwenye monasteri.
Baba yake Filipo alipoona gari lake limerudi tupu akahuzunika sana. Kwa mwaka mmoja alimtafuta binti yake, bure. Alipoambiwa na makuhani wa ki-pagani kwamba binti yake alipalizwa mbinguni na miungu, alitengeneza sanamu yake ya dhahabu na kuamua iheshimiwe kama mungu.
Eugenio akaanza kujifunza na kuishi maisha yake ya ki-kristo. Mwaka wa pili aliweza kukariri Maandiko yote, na kujipatia kila fadhila ya ki-kristo. Alipata amani moyoni mwake, hata watawa wote walikuwa wanamshuhudia kwamba yeye ndiye malaika. Alipita wote kwa utakatifu wake. Mungu akamjalia karama ya uponyaji. Kwa kuwatembelea tu wagonjwa kuliwaponya. Abate Theodori alipofariki, watawa, kwa sauti moja, wakamchagua Eugenio ashike nafasi yake. Eugenio akahangaika. Afanyeje? Yeye ni mwanamke, na kwa sheria hana ruhusa kuwaongoza wanaume. Akamwomba Mungu tena na tena. Ikaonekana kwamba ni Mungu anayemwita kushika kazi hiyo. Mwishoni akakubali, na watawa wote wakafurahi. Kwa hiyo tangu siku ile, alijitupa katika kazi ya kuwahudumia watawa wenzake ki-roho na

ki-mwili. Akawafundisha, siku kwa siku, akisema: “Kuna namna moja kumheshimu Mungu ni kutii amri zake“. Mchana na usiku alikuwa anaongea na Mungu katika sala zake. Mungu akazidi kumjalia kujibu sala zake. Sifa zake zikaenea mahali pengi.

Melanthia, mwanamke wa ukoo bora, tajiri katika mali ya dunia kuliko mali ya mbinguni, aliyeishi karibu na monasteri, akamwendea Eugenio na kumwomba amsaidie katika mateso yake. Eugenio akambariki kwa ishara ya msalaba na kumtia tone la mafuta. Mara akapona, akarudi kwa miguu nyumbani mwake. Kwa kumshukuru Melanthia akamtumia Eugenio vikombe vitatu vilivyojaa dhahabu. Eugenio alimrudishia akisema: “Tunayo mahitaji yetu, tena zaidi, tafadhali uwagawie maskini wanaohitaji kuliko sisi.“ Melanthia akahuzinika. Akamwendea yeye mwenyewe Eugenio na kujaribu akubali zawadi yake. Akiwa karibu naye akaanza kumpenda na kumtamani. Eugenio, bila kutambua hamu ya Melanthia, alimzidi kumhutubia kwa maneno ya Mungu. Siku moja alijifanya kwamba yeye ni mgonjwa na akamwita Eugenio afike kumtembelea. Eugenio alienda, ndipo Melanthia akamfunulia hamu yake ya kumtamani. Ndipo Eugenio akamwambia: “Hapana. Jina lako linashuhudia giza la roho yako. Uovu una mahali pakubwa moyoni mwako. Rudi nyuma, Melanthia, Hatutaacha usafi wa moyo. Hapana, hatutakubali kugusa ubikira wetu ... “

Melanthia akaaibishwa kwa maneno hayo. Akamwendea Gavana wa Aleksandria, Filipo, baba wa Eugenia, na kumwambia: “Nimekutana leo hii na mwanaume mbaya, Mkristo, anayejitambulisha kama daktari“. Na kwa maneno mengi mengine alimshtaki kwa Gavana Eugenio, kwa kumtupia jinai yake, “Mtawa kijana huyu akanijia usiku na kutaka kunibaka. Nilipopiga kelele watumwa na watumishi wangu walinijia kwa mbio, lakini mtawa akakimbia“. Filipo akakasirika. Akaamua kufunga watawa wote pamoja na Abate. Mkutano mkubwa ukakusanyika na kuwakemea, wakiwasindikiza hadi uwanja wa michezo, wakitegemea kufurahia vifo vyao. Gavana akawazuia. Walioshtaki wakatupwa gerezani hadi siku ya hukumu. Siku hiyo wakazi wote wa Aleksandria na vijiji vya karibu wakakusanyika. Filipo akaketi barazani, pamoja na wana wake wawili, Aviti na Sergio. Eugenio akaletwa mbele yao. “Uniambie, wewe Mkristo, mhalifu sugu kati ya wote, mafundisho ya Kristo yanawaruhusu kutenda mabaya na

kuwatega mama wetu ili kuwaangusha katika zinaa? Jibu." Eugenio, akiinama macho ili asitambulike na baba yake akamjibu: "Mungu, baba wa Yesu Kristo ninayemtumikia, anatufundisha kuishi katika usafi wa moyo. Ni rahisi kwangu kukuthibitishia kwamba Melanthia amenishtaki kwa uongo. Lakini siyo kazi yangu. Sheria yetu ni kurudisha mema kwa mabaya. Ukituahidi kwamba hutamhukumu mama huyu kwa hukumu unayotaka kutuhukumu, basi nitakuthibitishia kwamba amenishtaki kwa uongo." Gavana akamwahidia. Basi Eugenio aliendelea kusema: "Melanthia, wewe mbaya, Mungu anayeona yote, atakuadhibu."

Gavana Filipo akawasikiliza mashahidi upande wa Melanthia. Wote walimshtaki Eugenio. Eugenio akasema: "Wakati wa kukaa kimya umepita, sasa ni wakati wa kuonyesha ukweli". Aliposema hayo, akachana nguo yake na kuonyesha mbele ya baba yake kwamba yeye ni mwanamke. Akalia: "Wewe ni baba yangu! Klaudia ni mama yangu! Ndugu zangu ndio hao Aviti na Sergio. Mimi ni Eugenia binti yako!". Mkutano, baada ya kushangaa, ukaanza kupiga kelele kwa furaha. Baba akaambatana na binti yake kwa muda mrefu. Mama yake Klaudia akafika kwa upesi aliposikia habari hiyo. Na mara Filipo akaamua kuwafungulia watawa na kuwazika waliofariki. Wakati Eugenia alipoenda nyumbani mwa baba yake, moto kutoka mbinguni ukashuka juu ya nyumba ya Melanthia na kuteketeza yote.

Baba yake na mama yake na watu wote wa nyumbani mwao wakabatizwa. Wakazi wa Aleksandria walipoona imani ya Filipo, wakampatia daraja la uaskofu, akawa askofu wa Aleksandria. Akakaa katika kiti cha Mt. Marko miaka mingi na kuwafundisha Wakristo imani. Gavana mwingine, asiyeamini, akawatuma kisirisiri watu kumwua Filipo aliposali kanisani. Wakamwua. Akafiadini.

Baada ya kifo cha baba yake, mwaka 204, alipokuwa na miaka ishirini tu, Eugenia na matowashi Proto na Hiasinto wakarudi Roma. Askofu mkuu wa Roma aliposikia habari za Mt. Eugenia, akampokea na kumfanya abatisa wa nyumba ya masista aliyojenga. Akaishi miaka hamsini na mitatu kabla ya kufia dini kama baba yake. Proto na Hiasinto wakimtangulia kupata taji hiyo. Gavana wa Roma akamshika Mt. Eugenia, akamtesa kwa mbinu mbalimbali hadi akakata roho, na kufiadini kwa ajili ya Yesu Kristo Bwana wetu.

Wat. Eugenia na Filipo, mtuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

## **Mtumishi wa Mungu Yosefu Shanahan, Askofu, 1943**.

Yosefu alizaliwa tarehe 4 Juni 1871, huko Ireland. Siku tatu baadaye alibatizwa. Wazazi wake, Daniel Shanahan na Margaret Walsh walifunga ndoa tarehe 17 Juni 1864. Yosefu alikuwa mtoto wa tano. Akaanza shule ya msingi karibu na nyumba yake, na shule ya sekondari huko Gortnagoona. Akamaliza mafunzo yake akiwa na umri wa miaka 15.

Mwaka 1886 akaenda Ufaransa kuendelea na masomo yake katika seminari ya Shirika la Mapadri wa Roho Mtakatifu. Yosefu alibaki Ufaransa miaka 11, bila kurudi Ireland. Licha ya masomo ya kawaida alijifunza falsafa na kumaliza novisiati. Mwaka 1897 akarudi Ireland kuwa 'Kiranja' katika Rockwell College. Alipenda sana kucheza Rugby na akawa mchezaji maarufu.

Mwaka 1900, tarehe 22 Aprili akapadirishwa na akawahudumia wanafunzi wa Rockwell College kama Mshauri wao. Lakini mwaka 1902 akachaguliwa kwenda Nigeria ya Kusini kama Mmisionari. Miaka mitatu tu baadaye akateuliwa kuwa Vika wa ki-tume wa Nigeria Kusini. Na mwaka 1920, akachaguliwa kuwa askofu wa Nigeria Kusini. Tarehe 6 Juni akapata daraja la uaskofu huko Ireland.

Tarehe 7 Machi 1924, akaanzisha Shirika la Masista Wamisionari wa Rozari Takatifu. Wanawake saba, waliokuwa na hamu ya kueneza Injili, wakakusanyika pamoja, huko Killeshandra, Ireland. Chini ya uongozi wa Sista mmoja wa Shirika la Dominiko wakajifunza maisha ya kitawa. Wakaanza kumsaidia Askofu Shanahan katika kazi ya umisionari, hasa kuhusu kueneza Injili kati ya wanawake wa jimbo lake. Siku hizi ni Shirika kubwa la ki-mataifa wanaofanya kazi katika nchi mbalimbali.

Mwaka 1932 Askofu Shanahan akajizulu na akarudi Ireland baada ya miaka 30 ya umisionari katika Afrika. Akakaa Dublin, akiendelea kushughulikia kazi ya misioni kutoka nchi yake. Mwaka 1938, kujibu mwaliko wa Askofu Heffernan, akaenda Nairobi, Kenya kumsaidia kuwahudumia Wakristo. Akafariki asubuhi ya Sikukuu ya Krismasi, mwaka 1943. Akazikwa katika shamba la wafu la Mt. Augustino. Na

mwaka 1956 masalia yake yakapelekwa Nigeria na kuzikwa upya katika kanisa kuu la Onitsha, alilobariki yeye mwenyewe miaka 21 iliyopita. Mchakato wa kumtangaza Mtakatifu ulianza tarehe 15 Novemba 1997.

Mtumishi wa Mungu, askofu Shanahan, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

**Desemba 26**

Huko Sardi (siku hizi Ouzara Uturuki), kumbukumbu ya Mtakatifu **Eutimio**. Alikuwa mmonaki, halafu askofu mkuu wa mji huyo ambaye baada ya kudhulumiwa muda mrefu, aliuawa kwa sababu ya kututea heshima kwa picha takatifu kinyume cha serikali ya Dola la Roma Mashariki, 851. Anaheshmiwa na Wakatoliki, Waorthodoxi na Wakoptiki.

Waorthodoksi wanakumbuka kukimbia Familia Takatifu huko Misri.
Huko Misri, Wakoptiki wanawakumbuka Mt. **Yohane**, padre mkuu wa Shete,[562] na **Zakaria**, mfuasi wake. Pia kumbukumbu ya **Abadiu**, askofu na mfiadini, huko Antinoe, Misri. Pia kumbukumbu ya Mt. **Yohane**, Mchukia wanawake, Ethiopia.[563]
Katika Tanzania, Waamini wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) wanawakumbuka **Mashahidi wote** wafiadini.

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake. Amina.

## Mt. Yohane wa Shete, au Mt. Samueli Mwungama-dini, 693.

Inaonakana kwamba Yohane wa Shete na Samuuel Mwungama-dini ni Mtakatifu mmoja. Tunasoma katika maisha yake, yaliyoandikwa kwa lugha ya Kiarabu kwamba Samueli alizaliwa mwaka 597 katika mji wa Daklube, Misri. Alikuwa mtoto wa Padri mmoja aliyekataa mtaguso wa Kalsedoni, kwa jina Arselaos. Alitumia miaka yake ya ujana kuwa mfuasi wa Mt. Agato katika monasteri ya Mt. Makari Mkubwa, huko Shete. Misri. Akapadirishwa.
Wakati Yohane aliwekwa kuwa Mkuu wa monasteri ya Mt. Makari, jangwa nzima ilimulikwa na nuru yake na akawa baba wa Watakatifu wengi. Miongoni mwao tunaweza kuwahesabu Abba Gawarga na Abba

[562] *Coptic Synaxarium: 30 Kiahk.*
[563] Dcitionary of Saints

Abrahamu, nyota mbili mkubwa, na Abba Mina, askofu wa Tamai (*Tamuz*) na Abba Zakaria na wengine wengi.
Kwa sababu ya utakatifu na utauwa wake, alipowagawia waamini komunio, aliweza kutambua wale wenyedhambi na wale wenye haki. Mara nyingi alimwona Kristo na malaika wake wakizunguka altare. Siku moja alimwona mmojawapo wa mapadri mwenye sifa mbaya, akifika kanisani na pepo wakimzunguka. Padri alipofika mlangoni mwa kanisa, malaika wa Bwana alitoka kutoka patakatifu pamoja na upanga wa moto mkononi mwake na kufukuza pepo. Padri aliingia kanisani, akavaa mavazi ya ibada, akaadhimisha misa na kuwagawia waamini komunio. Alipomaliza, akavua mavazi ya ibada na kutoka nje, ndipo pepo wakamrudia. Ndiyo mambo Mt. Yohane aliyowaambia watawa, ili kuwaelimisha kwamba hakuna tofauti kati ya padri mwenye dhambi na padri mwenye haki akiadhimisha sakramenti. Kwa sababu ni kwa ajili ya waamini kwamba mkate na divai vinageuzwa kuwa Mwili na Damu ya Kristo. Aliwaambia mfano: “Kama picha ya Kaizari imechapishwa katika muhuri mmoja uliotengenezwa kwa chuma au kwa dhahabu, ni muhuri mmoja, vivyo hivyo upadirisho ni mmoja kwa mwenye dhambi na kwa mwenye haki. Bwana atamzawadia kila mmoja kadiri ya matendo yake.“
Sifa yake ilianza kuenea kwa sababu ya majikanio yake. Alikuwa anakula na kunywa mara moja kwa wiki. Wakati walipokuwa katika monasteri ya Mt. Makari, wajumbe wa Kaizari kutoka Konstantinopoli, walijaribu kuwathibitishia watawa wa jangwani kukiri imani ya Kalsedoni. Samueli akaona wivu, akashika barua kutoka Kaizari na kuichana akisema: “Yapotee mafundisho hayo na kila mtu anayeyasadiki. Alaaniwe yeyote anayebadilisha imani ya Ki-Orthodoksi ya mababu zetu“. Wajumbe wa Kaizari walikasirika, wakaamua Yohane apigwe, atundikwe kwa mikono na kumpiga usoni mwake kwa nguvu. Pigo moja limeng‘oa jicho lake. Yohane akapigwa na Siro, Patriarka wa Aleksandria, mfuasi wa imani ya Kalsedoni. Akamwamuru Yohane ahame kutoka Jangwa la Nitria. Yohane akahamia kwenye Mlima Kalamoun, mkoa wa Al Minya. Akajenga monasteri ambayo ina jina lake na hadi leo ipo.
Huko Kalamoun, Yohane aliteswa na watu wa Kabila la Waberberi, wanaoabudu Jua. Walimteka nyara, kupelekwa katika nchi yao na

kumfunga kwa muda. Waberberi waliposhindwa kumshauri Yohane kuabudu Jua wakamfunga kwa mnyororo mguu wake wa kushoto na mguu wa kulia wa msichana mmoja. Wakawatuma kuwahudumia ngamia, wakitegemea kwamba msichana atamshawishi Yohane kuliabudu Jua. Hata hivyo Yohane akabaki kushika imani yake. Hatimaye, baada ya kumponya mwana wa bwana wake, aliyekuwa mahututi, akafunguliwa na kuruhusiwa kurudi katika monasteri yake kwenye mlima Kalamoun.

Aliporudi akatabiri na kushuhudia uvamizi wa nchi ya Misri na Waislamu, mwaka 641. Katika maono alijulishwa siku ya kuaga dunia hii. Akawaita ndugu zake watawa na kuwasihi kushika amri za Bwana, kufuata nyayo za Mababa Watakatifu, kushiriki nao urithi wa ufalme wa mbinguni. Muda si muda, akawa mgonjwa na aliwaona kundi la Watakatifu wakifika kuchukua roho yake. Akaisalimia roho yake katika mikono ya Bwana. Ndugu zake watawa wakauchukua mwili wake kanisani na kwa sababu ya upendo wao mkubwa kwake na kuamini kwao kuhusu utakatifu wake, wakabaki na sehemu ya nguo zake za mazishi ambazo zikawa chemchemi ya uponyaji wa magonjwa mengi. Yohane aliishi miaka 90. Akafariki mwaka 693. Yohane anaheshimiwa kama mwungama-dini na siyo shahidi ingawa aliteswa sana kwa ajili ya Kristo.

Mt. Yohane, utuombee na Mungu atujalie wote kukiri imani mmoja na atukuzwe daima na milele. Amina.

**Desemba 27**

Huko Misri, Wakatoliki wa Kanisa mahalia la Aleksandria, Misri, wanamkumbuka Mt. **Maksimo**, askofu, aliyejulikana na kusifiwa sana kwa sababu ya kumkiri Yesu Kristo.[564] Toka mwaka 251 B.K. hadi mwaka 264 B.K. alisimamia Kanisa wakati Patriarka Dionisi alipohamishwa. Askofu Dionisi alipofariki alishika nafasi yake.
Katika Shirika la Wadominiko, kumbukumbu ya Mwenyeheri **Bonaventura Tolomei**. Akatembea kwa miguu, bila vyakula, makanisa ya kuhiji katika nchi ya Italia, Hispania, Palestina na hata Misri. Mahali popote alikuwa akiwaongoa wakosefu wengi kwa mahubiri yake.[565]
Huko Jamhuri ya kidemokrasia ya Kongo, kumbukumbu ya Mwenyeheri **Fransisko Spoto**, Padri, mfiadini, 1964.
Huko Aljeria, kumbukumbu ya Wenyeheri **Yohane Chevillard**, **Alano Dieulangard**, **Karolo Deckers** na **Kristiani Chesel,** mapadri wa Shirika la Wamisionari wa Afrika (*White Fathers*), waliouawa huko Tizi-Ouzou, 1994.

Wakoptiki wa Misri wanawakumbuka Wat. **Dioskoro** na **Skapio**, ndugu yake, wakaa pweke, walioishi Mlimani mwa Akhmim.[566] Pia kumbukumbu ya Abba **Makari I**, Patriarka wa 59 wa Aleksandria, 953.[567]
Huko Ethiopia, Wakristo wanamkumbuka Mt. **Frumensio** au Abba **Salama**, aliyeitwa mwonyeshaji wa mwanga.[568]
Waorthodoksi wanamkumbuka Mt. **Maksimo**, Patriarka wa Aleksandria, Misri, 282.

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake. Amina.

---

[564] *Roman Martyrology,* ed. 1956
[565] *Les petits Bollandistes*
[566] Padri Samaan El Soruay, *The Hermits of Egypt*
[567] *Arabic-jacobite Synaxarium*
[568] *The Ethiopian Rite Missal, Abba Emmanuel & Abba Brendan Cogavin, 2002, uk 215. Ethiopian Synaxarium: Tahisas 18.*

## Mwenyeheri Bonaventura Tolomei, 1348

Mtakatifu huyu alikanyaga bara la Afrika safari moja akitembea peku katika nchi ya Misri. Alizaliwa huko Sienna, Italia. Katika ujana wake alijulikana kwa utakatifu wake na neema Mungu aliyomjalia. Lakini baadaye, akiafikiana na rafiki wawili wenye tabia mbaya, aliishi miaka minne katika hali ya uasherati na kukufuru. Alipoongoka akaanza maisha ya toba ya hali ya juu, akitawala tamaa zake kwa njia ya majikanio na nidhamu, kuvaa mkanda wa chuma, n.k. hadi kifo chake. Akazuru kwa miguu peku, bila masurufu, nchi ya Italia, Hispania, Palestina na Misri, akihiji mahali patakatifu. Na mahali popote akawaongoa watu wengi kwa mahubiri yake. Aliporudi Sienna, akaambukizwa kwa ugonjwa wa tauni kwa kuwahudumia wagonjwa. Akafariki akipiga magoti, mikono na macho yake yakielekea mbinguni, mwaka 1348.

Alipozikwa kwa muda mfupi, maiti ya mtawa mmoja, aliyefariki karibuni ikawekwa karibu naye. Huyu akafufuka alipoguswa na maiti ya Mwenyeheri Bonaventura. Wote wakashangaa. Tukio hilo linatukumbusha mwujiza uliotokea baada ya kifo cha nabii Elisha.“*Elisha akafa, nao wakamzika. Basi vikosi vya Wamoabi wakaingia katika nchi mwanzo wa mwaka. Ikawa, walipokuwa wakimzika mtu, angalia, waliona kikosi; wakamtupa yule mtu kaburini mwa Elisha; mara yule maiti alipoigusa mifupa ya Elisha, alifufuka, akasimama kwa miguu.*“ 2 Fal 13:20-21. Kaburini mwa Mwenyeheri Bonaventura miujiza mingi ikatendeka.

Mwenyeheri Bonaventura, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

## Mwenyeheri Fransisko Spoto, padri na mfiadini, 1964

Fransisko alizaliwa katika familia ya kikristo kweli, tarehe 8 Julai 1924, huko Italia. Akabatizwa tarehe 24 Septemba wa mwaka ule na kupata kipa-imara tarehe 27 Novemba 1932. Alikuwa mvulana mwema, mtiifu kwa wazazi wake na mchamungu. Mwaka 1936 akaingia katika seminari ya Shirika wa Mwenyeheri James Cusmano. Tarehe 22 Julai

1951 akapadirishwa na Ernesto Kardinali Ruffini, akiwa na umri wa miaka 27.

Alitafuta kushughulikia zaidi wokovu wa watu kuliko mabishano ya ki-teolojia ya wakati wake. Aliwatunza wale aliowaita '*Minimum*', yaani wazee, watoto, wagonjwa, walioachwa na waliofungwa.

Mwaka 1959 akateuliwa kuwa Mkuu wa Shirika lake. Akaongoza shirika lake kwa busara, akionyesha fadhila ya utii kwa Baba Mtakatifu na kufanana zaidi na zaidi na Yesu Kristo, mchungaji mkuu. Akawahudumia wenzake kwa unyenyekevu na upendo, akiwatia moyo wakati mgumu waliopita, akiwasaidia ki-akili na ki-moyo. Daima aliwaunga mkono wale walioanzisha kazi njema.

Katika roho hiyo alianza safari kwenda Jamhuri ya ki-demokrasia ya Kongo, kuwatembelea watawa wenzake katika misioni ya Biringi, wakati wa vita ya waasi wa Patrisi Lumumba. Siku moja waasi wawili waliwasimamisha Wamisionari wanne waliojaribu kusafiri na kwenda mahali pengine. Watatu wakafaulu kutoroka, lakini Padri Spoto, alipokuwa mdhaifu, hakuweza. Wakaanza kumpigapiga, wakifikiri kwamba ndiye Mmisionari Mweupe yule aliyeeneza Injili katika eneo hili. Wakamwua tarehe 27 Desemba 1994. Akatangazwa kuwa Mwenyeheri kwa Baba Mtakatifu Benedikto XVI, tarehe 26 June 2006.

Siku ya leo tuwakumbuke pia mamia, Wamisionari na Mapadri wazalendo, waliouawa katika machafuko yaliyoletwa na Patrisi Lumumba na wengine.

Mwenyeheri Francesco Spoto na wote waliouawa, mtuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

## Wenyeheri Yohane Chevillard na wenzake, wafiadini, 1994.

Miaka thelathini baada ya kifo cha Padri Fransisko, mapadri wanne wa Shirika la Wamisionari wa Afrika (*White Fathers*) waliuawa huko Tizi-Ouzou, nchi ya Aljeria, kwa ajili ya imani yao, Yohane Chevillard (69), Alano Dieulangard (75), Karolo Deckers (70) na Kristiani Chessel (36). Wote walijua kwamba katika milima ya Kabylia waliishi katika hatari ya kuawa. Hata hivyo wote walikubali kubaki Aljeria kushuhudia kwamba Yesu Kristo yu hai kati yao.

Yohane alisema: “Najua kwamba naweza kufariki kwa kuuawa. Wito wetu ni kuishuhudia imani yetu kwa Kristo katika nchi ya Uislamu. Mambo mengine ‘Inch Allah‘“. Kwa mmojawapo wa dada zake aliyemwuliza kwa nini anarudi Aljeria, alimwambia: “Narudi Aljeria kushuhudia. Nyumbani ni kule, karibu na Wakabylia, marafiki wangu. Nikifariki nataka kuzikwa kule.“

Alano Dieulangard alikuwa mtu wa Mungu. Alizoea kusema tena na tena akitafakari maneno ya Mt. Yohane Mtume na Mwinjili: “Lazima tumpende Mungu, Baba yetu, usalama wetu na uhai wetu, na kuwapenda ndugu zetu katika Yesu Kristo“. Kabla ya kifo chake aliandika: “Tupo kama mitume katika mtumbwi ziwani, inatupasa kumwasha Bwana kwa vilio vyetu ... Yajayo yamo mikononi mwa Mungu.“

Karolo Deckers alijua kwamba huduma zake zilimhatarishia maisha yake: “Hii ndiyo wito wangu, nabaki ... Mama yetu wa Afrika ipo katika hatari ya tendo moja la kichaa. Katika jimbo tunafikiri kwamba kuwepo Kanisa ni muhimu, kwa ajili ya Kanisa lenyewe na kwa ajili ya nchi ya Aljeria.“

Mwanamke kijana, Mwaljeria, aliwaandikia wazazi wa Kristiani Chessel: “Mjue kwamba, katika siku zake za mwisho, Kristiani alikuwa amejaa furaha. Alikuwa ameanzisha mradi wa moyo wake wa kujenga maktaba kwa ajili ya vijana wa Tizi-Ouzou.“

Siku ya sikukuu ya Mt. Yohane, tarehe 27 Desemba 1994, huko Tizi-Ouzou, Yohane alikuwepo katika ofisi yake akiwapokea watu, kuwasikiliza na kuandika barua. Mnamo saa 6.00 mchana, alinyakuliwa na watu wanne wenye silaha. Akauawa katika ua wa Misioni, kwa kupigwa risasi, pamoja na rafiki wake Karolo Deckers aliyekuja kumsalimia, na wenzake wawili wa Parokia, Alano Dieulangard na Kristiani Chessel.

Tarehe 8/12/2018, Baba Mtakatifu Fransisko aliwatangazwa kuwa wenyeheri, pamoja na wengine, kwa jumla mashahidi 19.[569] Mashahidi hao ni mfano mzuri wa Kanisa la Aljeria la siku hizi: ndogo, maelfu tu wa Wakristo wanaoishi katika majimbo manne: Aljiers, Oran, Konstantine na Laghouat. Ni Kanisa lenye uhai kwa njia ya umaskini

[569] Rejea tarehe 8, 23 Mei/1 Agosti/3 Septemba/23 Oktoba/10 Novemba

wake, kwa sababu lilipotea uwezo na fahari yake. Siku kwa siku linaishi katika upendo na huduma. Kwa sababu limetakaswa na halina tamaa ya makuu, linaweza kuwa kiwanja cha majadiliano na Uislamu. Kanisa linatumaini kwamba sisi sote tutatambua kwamba watu wote ni waana na mabinti wa Mungu, kazi ya mikono yake. Mungu mmoja, upendo mmoja.

Wenyeheri Yohane na wenzako, mtuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

**Desemba 28**

Sisi Wakatoliki tunawakumbuka Mt. **Theonas,** askofu mwandamizi wa Mt. Petro, Patriarka mfiadini.[570]
Huko Afrika ya Kaskazini, Wakatoliki wanawakumbuka Wat. **Kastorio**, **Viktori** na **Rogasiano**, wafiadini.[571]
Huko Tanzania sisi Watoliki tunamkumbuka Mtu wa Mungu **Aloisi Munsch**, askofu wa kwanza wa Morogoro, 1942.
Huko Ouled-Djellal, Aljeria, Wakatoliki wanamkumbuka **Renati Husson**, Padri wa Shirika la Wamisionari wa Afrika (*White Fathers*), aliyeuawa kwa kupigwa risasi, 1959.
Huko Mbulu, Tanzania, Wakatoliki wanamkumbuka **Nikodemo Hhando**, Askofu, aliyefariki mwaka 1997.
Huko Afrika ya Kusini, Wakatoliki wanamkumbuka Mtumishi wa Mungu **Jorji** (George) **Hyams,** mlei mwanzilishi wa *Little Edeen Society* pamoja na mke wake **Domitila Rota,** Mtumishi wa Mungu.

Wakoptiki wanamkumbuka Mt. **Theonas**, Patriarka, askofu wa 16 wa Aleksandria, Misri. Pia wanawakumbuka Mt. **Kalimaki**, askofu wa Oseem, Misri;[572] Mt. **Sabela**, aliyejulikana kwa karama yake ya kufasiri ndoto; Wat. **Faustino** na **Theodesia**, wafiadini, 368. Pia kumbukumbu ya Abba **Yona**, mwanakoriti.[573]
Huko Ethiopia, Wakristo wanamkumbuka Mt. Abba **Yohane**, askofu wa mji wa Burlos (*Burles*), Misri.[574]

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake. Amina.

---

[570] *Martyrologium Romanum*, ed. 2001.
[571] *Roman Martyrology,* ed. 1956
[572] *Coptic Synaxarium: 2 Tubah.*
[573] *Arabic-jacobite Synaxarium*
[574] *The Ethiopian Rite Missal, Abba Emmanuel & Abba Brendan Cogavin, 2002, uk 216. Ethiopian Synaxarium: Tahisas 19.*

## Mt. Theonas, Patriarka, Askofu wa 16 wa Aleksandria, 300.

Hatuna habari nyingi kuhusu Mtakatifu huyu. Mwaka 282, Askofu Theonas aliteuliwa kuwa Patriarka wa 16 wa mji Aleksandria, akishika nafasi ya Askofu Maksimo.

Wakoptiki wanamheshimu Askofu huyu kama mtu mwenye haki, mpole, msomi mnyenyekevu, aliyependwa na wote. Kwa sababu ya utakatifu wake na elimu yake akawa mwanga na pambo la Kanisa, wakati Kanisa lilifurahia amani na mafanikio. Wakati huo Mt. Pierio alikuwa Padri na Katekista katika Kanisa hilo, Origene akiwa mwanafunzi wake.

Hadi wakati wake waamini walisali nyumbani mwao na katika mipango, kwa sababu ya hofu ya wapagani wasioamini. Askofu Theonas aliwaendea na kwa upole aliwaongoa wengi, wakamwamini Yesu Kristo na kubatizwa. Mwaka wa kwanza wa utawala wake akambatiza Petro, atakayeshika nafasi yake katika kiti cha Mt. Marko. Inasemekana kwamba alimpa Petro daraja la usomaji akiwa na umri wa miaka 5, ushemasi akiwa na miaka 12 na upadirisho akiwa na miaka 16. Aliweza kujenga Kanisa huko Aleksandria, lililotabarukiwa kwa heshima ya Bikira Maria, *Theotokos*, Mama wa Mungu.

Mt. Theonas aliwaandikia Wakristo barua kuwafundisha jinsi wanavyostahili kuishi katika Ikulu ya Kaisari. Barua hiyo ilipelekwa kwa Lusiano, mtunza mali wa Kaizari Dioclesiani.

Wakati wa utawala wake alikabili uzushi wa Sabellio huko Aleksandria, ambaye alifundisha kwamba Baba, Mwana na Roho ni nafsi mmoja. Askofu Theonas akamtenga na Kanisa na kuonyesha kwa maneno na maandiko kwamba amepotea.

Mt. Theonas alifariki mwaka 300, kwa amani. Akakaa katika kiti cha Mt. Marko kwa muda wa miaka 19. Akaandamana na Mt. Petro.

Mt. Theonas, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

## Mtu wa Mungu Aloisi Munsch, askofu, 1942

Aloisi Munsch alizaliwa Ufaransa, tarehe 6 Oktoba 1869. Akapadirishwa tarehe 28 Oktoba 1894, akiwa na umri wa miaka 25. Pamoja na wenzake 30 aliweka nadhiri zake tarehe 15 Agosti, 1895,

huko Ufaransa. Na mwaka ule ule, tarehe 12 Septemba, akapanda merikebu huko Marseilles kuelekea Zanzibar. Mhashamu de Courmont, askofu wa Vikariati ya kitume ya Zanzibar Kaskazini, akamtuma Morogoro, eneo la jimbo lake lililotawaliwa na Wajerumani, kwa ajili ya kuanzia kazi yake.

Mwaka 1900 alikuwepo misioni ya Ilonga. Muda si muda akawa mkuu wa misioni ya Ilonga na miaka 1902 hadi 1910 mkuu wa misioni ya Mhonda. Akaonekana kama mtu ambaye ana uwezo mkubwa wa kufanikiwa. Zaidi ya hayo alikuwa na kipaji cha kuhusiana na Maafisa Wajerumani kiasi kwamba alipata fadhila zao bila kusaliti manufaa ya Waafrika.

Mwaka 1910, Vikariati vya Zanzibar Kaskazini ikagawanywa katika vikariati mbili Zanzibar kati (au Bagamoyo) na Kilimanjaro. Padri Aloisi Munsch akateuliwa kuwa Vika wa kitume wa kwanza wa Zanzibar kati, yaani Bagamoyo. Akapata daraja la Uaskofu tarehe 5 Februari 1911 huko Zanzibar. Miaka ifuatayo alitumia nguvu zake zote kueneza Imani Katoliki katika Vikaria yake. Lakini, mwaka 1914, Vita vya Kwanza vya Dunia vilimzuia kuendelea na kazi yake. Mabruda wote Wajerumani wakalazimishwa kuondoka ili kujiunga na jeshi la Wajerumani. Na mwisho wa vita Wamisionari wote Wajerumani wa Afrika Mashariki wakafungwa.

Majeshi ya Waingereza, chini ya Jemadari Deventer kutoka Afrika ya Kusini wakatwaa nchi ya Tanganyika. Wakaanza kuharibu misioni ya kikatoliki. Askofu Munsch alipolalamika akafungwa na kupelekwa Mombasa ili arudi Ufaransa kwa nafasi ya kwanza. Kwa sababu haikuwepo merikebu ya kwenda Ulaya akarudi Kilimajaro wakati nchi ilifurahia amani. Lakini Mtawala wa Dar es Salaam ukamlazimisha kwenda misioni ya Mandera. Kati ya mapadri 6 na mabruda 13 Wajerumani wa Vikariati waliofungwa watano tu waliruhusiwa kurudi Afrika Mashariki.

Mwaka 1922 Askofu Munsch akajiuzulu kuwa Vika wa kitume. Akaandamwa na Askofu Henry Gogarty, lakini Askofu Munsch akabaki katika Vikariati ya Bagamoyo kwa miaka 20 zaidi, akifanya kazi kama padri wa Mandera na Mhonda.

Inasemekana kwamba Baba huyu alikuwa mtu wa sala na imani kubwa na mwenye upendo kwa watu wote. Kutokana na imani yake kila

alichoomba kwa Mungu alifanikiwa. Mwaka fulani, mwezi Juni-Julai kulikuwa na njaa kubwa. Vijana wake waliokuwa wanasoma Kigurunyembe, akiwemo mzee Paulo Kamili Danduka, walishuhudia muujiza mkubwa. Aliwaambia: "Watoto wangu hatuna chakula, hivyo tusalini ili Mungu atupe chakula, vinginevyo tutafunga shule." Walisali novena ya siku 9. Siku ya 10, aliwaita wanafunzi washuhudie, vyakula na vinginevyo vilivyojaa ghala: chakula, sukari, mafuta na maharagwe bila kuletwa na gari lolote. Hata mlango ulikuwa haufungiki.[575]

Akafariki Mhonda tarehe 28 Desemba 1942, akiwa amebaki Afrika miaka 47. Alizikwa Kigurunyembe ambako kulikuwa makao makuu ya maaskofu na mapadri. Kwa sasa ndiyo makao makuu ya Mama Mkuu wa Shirika la Masista wa Moyo safi wa Maria wa Morogoro Mgolole, na Chuo cha Ualimu. Inasemekana kwamba watu wenye imani wanachukua udongo kwenye kaburi lake kwa ajili ya kuwaombea kwa nia mbalimbali. Wanafanikiwa.

Mtu wa Mungu Askofu Munsch, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

---

[575] Simulizi toka kwa mzee Paulo Kamili Danduka, aliyeshuhudia mwuujiza huu, akiwa mmoja wa wanafunzi wake.

**Desemba 29**

Sisi Wakatoliki tunamkumbuka Mt. **Liboso**, askofu wa Vagensis, mfiadini.[576] Pamoja naye Mt. **Dominiko na wenzake 6,** wote wafiadini, Afrika ya Kaskazini.[577]
Huko Ethiopia, Wakatoliki wanamkumbuka **Malkia Theofania**.[578]
Huko Toumi, Kameroun, Wakatoliki wanamkumbuka **Gabrieli Soh**, aliyeuawa na askari, alipomlinda Padri mmoja, mwaka 1959.
Huko Burundi, Wakatoliki wanamkumbuka **Mikaeli Courtney**, Balozi wa Baba Mtakatifu, aliyeuawa mwaka 2003.

Waorthodoksi wanawakumbuka Mhashamu **Athenodori**, mfuasi wa Mt. Pakomi, Karne la IV na Mhashamu **Benyamini**, mtawa wa Nitria, Misri, 392.

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake. Amina.

## Gabrieli Soh, aliyeuawa, 1959

Gabrieli alizaliwa mwaka 1938, Kusini/Magharibi ya Bafoussan, mji mkuu wa mkoa wa Mifi, Kameroun. Ni maeneo ya milima milima. Wakulima wengi wanafanya kazi chini ya Chifu wao Fo. Wanalima kwa kufuata mwongozo wa ki-maadili na imani kwa Mungu aliyeumba na kushika mikononi mwake kila kitu.
Gabrieli alibatizwa katika kanisa la Toumi. Alikuwa mtoto mpenzi wa mama yake. Alikuwa anasema tena na tena "Gabrieli aliumbwa kwa jiwe kichwani mwake", maana yake alipewa na Mungu neema ya pekee. Alipokuwa kijana alijiunga na baba yake kufanya kazi shambani. Shuleni alikuwa mwanafunzi aliyejifunza kwa makini lakini pole pole. Alikuwa mwangalifu kutomwumiza mtu yeyote, hasa wadogo, kwa hiyo alipenda zaidi kuepuka kubishana na kuangaliwa kuwa mtu

[576] *Martyrologium Romanum*, ed. 2001.
[577] *Roman Martyrology,* ed. 1956. Pamoja na Dominiko: Viktori, Primiano, Saturnino, Kresensi, Sekundo na Honorati, Ethiopian Synaxarium inarudia habari za siku iliyotangulia.
[578] *The Ethiopian Rite Missal, Abba Emmanuel & Abba Brendan Cogavin, 2002, uk 216.*

mwoga, kuliko kuangaliwa kuwa mtu mbishi. Alijifunza kujitoa tangu ujana wake. Alipenda kuwa padri lakini hakuweza kujiunga na seminari, basi akajitoa kuhudumia Misioni. Kule akaishi kwa ajili ya wengine, kuwahudumia kwa njia nyingi: kutafuta maji, tembo (*palm wine*), n.k.

Miaka kabla ya Kameroun kupata uhuru, Chama cha mapinduzi U.P.C. (*Union for the Peoples of Cameroun*), kilitafuta kuruta askari wapya, lakini kimezama katika ugaidi. Wilaya ya Bassa ilikuwa imeteketezwa, mapadri walitekwa nyara, mamia ya Wakristo waliuawa kwa njia ya ukatili mbaya. Eneo lote lilikuwa limechomwa hadi karibu ya Bamendjou. Gabrieli aliendelea na huduma zake. Aliwasindikiza mapadri katika safari zao za kuwatembelea Wakristo, ingawa safari zao zilifanywa hatarini. Aliandaa kila kitu, kwa ajili ya misa, mlo, mafundisho, n.k.

Jumapili, tarehe 29 Desemba, mchana kama saa 9.00, askari wagaidi walionekana misioni. Mara wakamshika Padri Siyam, baadaye Padri Fondjo, Paroko. Wakawavamia, wakashika kanzu ya Padri Siyam ili kuichana. Gabrieli aliangalia kutoka dirishani mwa jiko. Hakuweza kuamini kwamba watu wangeweza kumshambulia padri. Akatoka jikoni kwa mbio, akasimama katikati ya kundi la askari waliomzunguka Padri. Akamshika askari ambaye alimlenga Padri kwa bunduki yake na kukamata mkono wake. Askari wote waliwasahau mapadri ili kumwangalia Gabrieli. Mmoja wao, akampiga kwa ubapa wa panga lake, na kumwambia “Ondoka kutoka hapa, nenda kwa watu wako“. Lakini Gabrieli aliendelea kumshika askari kwa nguvu na kusema: “Ikiwa nakufa kwa ajili ya mapadri hawa ni kama kwenda kulala.“ Wakamwambia tena “Ondoka, Ondoka!“ Gabrieli hakusema kitu, hakutetemeka. Alifikiria tu kumwokoa Padri kutoka hatari hizo. Ghafla mtu aliyekuwa karibu na askari mwenye bunduki akampiga Gabrieli kichwani kwa upanga kwa nguvu. Gabrieli akafa mara. Muda si muda kanisa na misioni vikabomolewa na wote wakakimbia.

Padri Fondjo aliandika: “Gabrieli hakuwa Mkristo peke yake kungama imani yake, wengine kwa uongozi wa Roho Mtakatifu walifanya hivyo. Huko Bangang, Aloisi Taiemene,[579] Katekista mkuu aliuawa pamoja na

[579] See Maisha yake tarehe 30 Machi.

wakristo kumi kwa sababu walikataa kubomoa kanisa lao. Yosefu Fotsin wa Doumelong aliuawa kwa sababu alikataa kuwaua watu wasio na hatia. Fontsa alipigwa risasi kwa sababu alikataa kuungana na kundi la wauaji. Vivyo hivyo Makanisa ya Ndongsamba na Bafoussam, yaliyoteswa sana wakati wa vita, na pia ya mkoa wote wa Bassa, yanaweza kuzidisha orodha ndefu ya wakristo, ambao kama Gabrieli Soth, walimshuhudia Kristo hadi kufa. Wanahitaji kutangazwa siku moja kuwa ‘Watakatifu‘.[580]

Gabrieli Soth na wote waliouawa kwa sababu ya imani yao huko Kameroun, mtuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

[580] Rejea Fr. Neno Contra,, Louis Kalonji, *African Lay Martyrs*, New People Media Centre, 2009, uk. 20-22.

**Desemba 30**

Huko Misri, Wakatoliki wanawakumbuka Wat. **Mansueti**, **Severo**, **Apiano**, **Donati**, **Honorio** na **wenzao**, wafiadini huko Aleksandria.[581]
Huko Msumbiji, Wakatoliki wanamkumbuka **Laurindo Magalhäes Bonde,** mlei, aliyeuawa mwaka 1989.
Na huko Uvira, Jamhuri ya ki-demokrasia ya Kongo, Wakatoliki wanamkumbuka **Rufino Ndama Ruzangiza Abunuasi**, mlei, aliyeuawa na waasi, 1998.
Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake. Amina.

## Mtu wa Mungu Rufino Ndama Ruzangiza Abunuasi, 1998

Rufino alizaliwa Kavinvira (Uvira) 1954, baba yake alikuwa Marselo Rukweka na mama yake Zaina Nakangeta. Alibatizwa, kupata kipaimara na kukomunika kwa mara ya kwanza huko Kioanga tarehe 6 mwezi wa Aprili, 1969. Baba yake alifariki alipokuwa darasa la II. Familia ikahamia Makobola, mahali pa kuzaliwa mama yake. Wagaidi Muletists walipofika wakahamia Kalundu, mahali ambapo Rufino aliweza kumaliza shule ya msingi. Akamwoa Safi Nakaberenge tarehe 11 Julai 1973. Wakapata watoto tisa.
Mwaka 1977 alijiunga na shule ya nesi huko hospitalini mwa Uvira. Wakati wa mlipuko wa kipindupindu huko Makobola, miaka ya 1977-1980, akawa, pamoja na Paroko wake, msitari wa kwanza kuwatunza wagonjwa. Mwaka 1980 akafuata kozi ya maabara huko Luvungi, na kati ya miaka 1992 na 1993 alichukua kozi kuwa msaidizi katika Shirika la Msalaba Mwekundu (*Red Cross*).
Wakati wa mabishano kati ya Mai-Mai na jeshi alibaki daima katika kijiji chake. Alikuwa akifundisha Neno la Mungu, kusimamia Jumuiya Ndogo Ndogo na kuangalia kigango cha Makobola. Siku moja alikamatwa nyumbani mwake na jeshi na kuuawa. Mwili wake ulizikwa na vijana, siku mbili baadaye, pale pale alipouawa.

[581] *Roman Martyrology,* ed. 1956

Padri mmoja aliyemfahamu anamshuhudia kwa maneno hayo: “Alikuwa Mkristo kweli. Alikuwa ananifurahisha kumsikiliza. Alikuwa na kipaji cha kuwakaribisha watu. Mwaka 1998, aliwatunza kwa zamu mapadri watatu waliokimbilia kujificha. Akawalisha, akawatunza hata ikiwa maisha yake yalikuwa hatarini. Nilistaajabia uvumilivu na hamu ya kuendeleza familia yake na Jumuiya yake ya kikristo.“ [582]

Mtu wa Mungu Rufino, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

[582] Rejea Fr. Neno Contra,, Louis Kalonji, *African Lay Martyrs*, New People Media Centre, 2009, uk. 48.

**Desemba 31**

Huko Kinshasa, Jamhuri ya ki-demokrasia ya Kongo, Wakatoliki wanawakumbuka **waamini 5** waliouawa na Polisi, wakati wa maandamano ya amani, mwaka 2017.

Huko Ethiopia, Wakristo, wanamkumbuka Mt. Abba **Anastasi**, Patriarka, askofu wa 36 wa Aleksandria, Misri, 315 B.K.[583]
Kumbukumbu ya Mt. **Ausgenio**, Shahidi.
Wakoptiki wanamkumbuka Mt. **Banikouros**, Jemadari, shahidi.[584]
Waorthodoksi wanamkumbuka Mt. **Melania kijana**, aliyesafiri na kukaa kwa muda katika bara la Afrika.
Huko Marekani, Waamini ya Kanisa la ki-askofu (*Espicopal Church*) la Marekani (USA) wanamkumbuka **Samueli Ajayi Crowther**, askofu wa kwanza mwanglikana katika Nigeria, 1891.

Na mahali pengine kumbukumbu ya Mashahidi, Waungama-dini na Mabikira wengi waliompendeza Mungu. Atukuzwe Mungu katika watakatifu wake. Amina.

## Mt. Melania kijana, 439



Waorthodoksi wanamheshimu Melania kijana kama mtakatifu sana. Melania alizaliwa Roma kati ya familia yenye moyo wa ibada. Wazazi wake, wenye ardhi na mali, walitumaini kwamba binti yao angeolewa na kupata watoto watakaorithi mali yao. Alipokuwa na umri wa miaka 14 tu aliolewa na kijana mwenzake Apiniano. Tokea mwanzo wa ndoa yake alimwomba mume wake kuishi kwa kujizuia kutumia ndoa au kufungua kifungo cha ndoa. Apiniano akamjibu: “Siwezi kukubali sasa

[583] *The Ethiopian Rite Missal, Abba Emmanuel & Abba Brendan Cogavin, 2002, uk 217. Ethiopian Synaxarium : Tahisas 22.*
[584] *Arabic-Jacobite Synaxrum*

hivi. Tutakapozaa watoto wawili kurithi mali yetu ndipo sisi wawili tutaacha ulimwengu“. Melania akamzalia mtoto wa kike ambaye wazazi wake walimtolea kwa Mungu. Melania kisirisiri alivaa shati la manyoya na kusali usiku kucha. Akapata mtoto wa pili. Wakambatiza lakini mara alifariki. Melania akadhoofika ki-mwili. Apiniano akiwa na wasiwasi kuhusu afya ya mke wake, alimwomba Mungu amponye na kuweka nadhiri kuishi kwa pamoja katika usafi kamili wa moyo. Alipopona Melania aliacha kuvaa nguo za umalidadi na mapambo ya vito. Mtoto wao wa kike akafariki.

Watakatifu wakaacha mji wa Roma na wakaanza maisha kwa ajili ya kumtumikia Mungu tu. Apiniano wakati ule alikuwa na umri wa miaka 24 na Melania 20. Wakaanza kuwatembelea wagonjwa, kuwakaribisha wageni, na kuwasaidia maskini. Wakawatembelea pia waliohamishwa au waliohukumiwa kufanya kazi katika migodi. Wakiuza mashamba yao ya Italia na Hispania, wakatoa msaada kujenga monasteri, hospitali, kuwasaidia yatima na wajane huko Mesopotamia, Siria, Misri, Finisia na Palestina.

Wakaacha nchi yao na kuanza safari kuelekea Afrika. Dhoruba ikawakuta – mpango wa Mungu Melania alisema – na kuwapeleka katika kisiwa kilichotekwa na washenzi. Hao walidai malipo kuwaacha huru wenyeji wa kisiwa. Watakatifu waliwakomboa, wakiokoa mji wao na wakazi wao. Walipoendelea safari zao wakafika pwani ya Afrika. Kwa baraka ya Askofu wakawasaidia wahitaji. Melania aliendelea kufunga na kuimarisha roho yake kusoma Neno la Mungu na kunakili vitabu vya Maandiko Matakatifu na kuwavigawia wenyeji.

Watakatifu walibaki miaka saba katika mji wa Kartago. Baadaye waliaamua kuhiji Yerusalemu. Walipopita mji wa Aleksandria wakakaribishwa na askofu Sirili pamoja na mzee wa Kanisa Nestorio, mwenye karama ya unabii na uponyaji. Yeye akawaambia wawe na ujasiri na uvumilivu wakitumaini ufalme wa mbinguni. Baada ya kuzuru Misri kwa muda mfupi, akiwatembelea baadhi ya watawa wa jangwani, wakaenda Yerusalemu. Huko Yerusalemu watakatifu wakawagawia maskini mali yao iliyobaki na kuishi katika umaskini na sala. Mt. Melania akajifungia katika kijumba mlimani mwa mizeituni. Mara chache aliweza kuonana na Apiniano. Miaka ilipopita alianzisha konventi na mabikira tisini waliishi chini ya utii wake. Katika konventi

alijenga kanisa ndogo na kuweka katika altare masalia ya Watakatifu wa Nabii Zakaria, Stefano Shahidi wa kwanza na Mashahidi arobaini wa Sebaste. Wakati ule Apiniano akafariki. Moyoni alikuwa na hamu ya kujenga monasteri ya wanaume katika mlima wa kupaa Bwana Yesu. Bwana akambariki alipomtumia mfadhili mmoja aliyempatia fedha zote zilizohitajika. Akajenga monasteri kwa muda wa mwaka mmoja.

Melania akatambua kwamba siku ya kuaga dunia inakaribia. Akawaita padri na mabikira wake. Wakasikiliza mafundisho yake kwa mara ya mwisho kwa huzuni na machozi. Baada ya kuomba sala zao na kuwasihi kubaki katika usafi kamili wa moyo akapokea komunio kwa furaha. Kwa amani akasalimisha roho yake kwa Bwana mnamo mwaka 429.[585]

Mt. Melania, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

## **Mauaji Kinshasa Kongo, 2017**.

Ubalozi wa Baba Mtakatifu huko Kinshasa, tarehe 3 Januari, 2018, ulitoa ripoti ya matokeo ya maandamano ya amani yaliyotayarishwa na CLC (*Catholic Laity organization*) kumwomba Rais Yosefu Kabila kutangaza rasmi kwamba hatagombea kuwa Rais kwa awamu ya tatu, kufuata Katiba ya nchi na mapatano yaliyokubuliwa tarehe 31 Desemba 2016. Uchaguzi ulipangwa tena, kwa mara ya tatu, tarehe 23 Desemba 2018. Kadiri ya ripoti, parokia 134 walizungukwa na polisi; Katika parokia mbili waamini walizuiliwa kuingia na kuhudhuria misa ya Jumapili; Katika parokia tano polisi waliingia wakati misa iliadhimishwa na wakazuia mapadri kuendelea kusoma misa; Katika Parokia 18, kingo za eneo la Parokia zimevunjwa na Polisi; Tena katika parokia zingine 10 mabomu ya machozi yalipigwa. Watu 5 waliuawa, mmoja katika kanisa la Mt. Dominiko, wawili katika kanisa la Familia Mtakatifu, na wengine wawili katika kanisa la Mt. Alfonsi. Mapadri 6 na seminari 1 wametiwa mbaroni.

Waliouawa, mtuombee amani katika Afrika na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

[585] OCA *Lives of the Saints of Africa*

# Watakatifu bila tarehe ya kuzaliwa mbinguni

## Mtumishi wa Mungu Eulalia 'Gabriel, karne la XIX



Mama Eulalia 'Ma Gabriel amezaliwa mnamo mwaka 1830 Methalaneng, Mokhotlong (Lesotho). Amebatizwa na Mwenyeheri Padri Gérard na kupokelewa katika Kanisa Katoliki. Ameolewa.
Alipenda sana kusali rozari, hasa wakati mgumu wa matatizo. Watu wa Phamong walizoea kumwita kwa jina la utani '*Mchawi Kongwe'* kwa sababu ya miujiza yake. Akiita jina la Yesu mara tatu, ndipo aliweza kufanya kitu chochote hata ni cha hatari. Siku moja kundi la watu wenye silaha walimchoma kwa mkuki na wakamwacha kufariki. Lakini aliokolewa na Bikira Maria na rozari yake.
Mara nyingi aliwaombea akina mama tasa na wengi waliweza kupata mimba baadaye kwa njia ya sala zake. Yeye na mume wake wakaponyoka kuliwa na Wa-Motlejoah, kabila la mbwawa, huko Mohale's Hoek. Siku moja, Mama Eulalia, aliweza kuvuka mto sengu uliofurika akiwa na wifi yake, kwa mshangao mkubwa wa wote waliowaangalia. Wakati fulani mvua ikinyesha, yeye na wenzake walibaki bila kulowana. Wakati mwingine mazao yaliharibika kabisa na mvua ya mawe, lakini mazao yake hayakuguswa. Na yote yalitokea kwa sababu ya kusali rozari kwa imani.
Mwaka 2002, Jimbo la Mohale lilifungua mchakato wa kumtangaza kuwa Mwenyeheri kwa kuomba Mungu kuthibitisha kwamba Eulalia 'Ma-Gabrieli Mokhosi aliishi maisha matakatifu katika ulimwengu huu. Ili atangazwe kuwa Mwenyeheri na kushika nafasi kati ya Watakatifu katika Kanisa Katoliki : "Mungu mwenyezi, chemchemi ya utakatifu wote, ulimjalia binti yako Eulalia 'Ma-Gabrieli Mokhosi vipaji vya imani thabiti, ibada na kujinyima. Utusaidie kufuata mfano wake kumpenda Yesu, hasa katika Ekaristi na kumpenda Maria, Malkia wa rozari. Harakisha atangazwe kuwa Mwenyeheri ili atupatie kwa maombezi yake neema (kutaja mahitaji) … Tunaomba hayo kwa Jina la Bwana Wetu Yesu Kristo. Amina."

Mtumishi wa Mungu Eulalia, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina

## Mtumishi wa Mungu Manueli, 1686

Mlei aliyezaliwa mwaka 1604 katika nchi ya Angola. Aliishi na kufariki Argentina. Machakato yalianzishwa na Jimbo Kuu la Mercedes-Lujan.
Mtumishi wa Mungu Manueli, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina

## Mtumishi wa Mungu Göbou Yaza, 1928

Kijana mlei aliyeishi katika nchi ya Guinea, jimbo la N'zerekoré. Alipokuwa bado mkatekumeni aliuawa kwa sababu ya imani yake, mwaka 1928.
Mtumishi wa Mungu Göbou Yaza, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

## Huko Kameroun

Wakristu wanawakumbuka Msgr **Yohane Kounou** na Padri **Materne Bikoa**, waloiuawa mwaka 1982.
Padri **Amougou**, Jimbo la Sangunelima, aliyeuawa mwaka 1992.
Padri **Yamb**, Padri wa Jimbo, aliyeuawa. Hatujui mwaka.
Padri **Mario Bortoletto** (1938–2009), Priest of the Diocese of Treviso; Fidei Donum Missionary in the Diocese of Ebolowa; Associate of the Pontifical Institute for Foreign Missions (Italy-Cameroon)

## Ethiopia

Mtu wa Mungu: Luis de azevedo. In 1588 aliingia katika Shirika la Majesuiti na mwaka 1605 askatumwa Ethiopia. Akaa huko miaka 29 kama missionari. Aliandika kitabu cha sarufi kwa lutha ya ki-Ethiopia. Akatafsiri Agano Jipya na kazi nyingi katika lugha hiyo. Alifariki katika nchi ya Ethiopia mwaka 1634.

## Nigeria
Vivian Uchechi Ogu (1995-2009), Child of the Diocese Mbaise ; Martyr (Nigeria)

## Misri
1. Girgis wa Asiut na wenzake 5,000, wafiadini. Waliouawa na serikali ya Kiislamu ya nchi yao huko Asiut, Misri, 1169. Girgis alikuwa monaki na baadaye askofu wa kikopti.

2. Wafiadini wa Kosheh. Ni Wakoptiti 21 waliouawa na Waislamu wenye itikadi kali kwa ajili ya imani yao ya kikristo katika mji huo wa Misri ya Kati miaka 1998-2000. Wanaheshimiwa kama watakatifu wafiadini.

3. Didimo kipofu. Alikuwa mwanatheolojia maarufu wa Aleksandira, ambapo aliongoza chuo cha katekesi kwa karibu miaka 50. Ingawa hakuweza kuona, alikuwa na kumbukumbu kali sana, hata akaweza kumudu fani zinazofaidika sana na matumizi ya macho. Aliandika vitabu vingi Ufafanuzi wa Zaburi zote, Injili ya Mathayo na Yohane, kitabu dhidi ya Waario na juu ya Roho Mtakatifu, pia Isaya, Hosea, Zekaria, Ayubu na mada nyingine nyingi. Bahati mbaya, kati ya maandishi ya ufafanuzi ya Didimo, yanayofikiriwa kuhusu vitabu vyote vya Biblia ya kikristo, vimetufikia vipande tu.
Akiwa mfuasi wa Origen alipinga mafundisho ya Ario na Wapneumatomaki.

Abdel Messih El-Makari, mmonaki padri wa Kikopti (1892-1963, Misri

Gabriel Abdel El-Metgaly, padri mfiadini wa Kikopti (1918-1978, Misri

Mwisho wa Juzuu la 3